# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARAMIWA

**UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!**

***Paulo Alifungwa,Injili Haikufungwa***
***Barua Toka Gerezani***
***(Wakolosai,Waefeso, Filemon Baadaye Wafilipi)***

Na Dr. Bob Utley,
Profesa mstaafu wa kanuni za ufasiri
(utafasili wa Biblia)

*Study Guide Commentary Series*
*New Testament, Vol. 8*

Copyright © 2013 Bible Lessons International. Haki zote zimehifaziwa. Nukuu au usambazaji wowote wa sehemu ya maandishi haya lazima utolewe pasipo malipo yoyote. Nukuu au usambazaji huo lazima pongezi zimwendee mwandaaji Dr. Bob Utley na ikijumuisha nukuu toka www.freebiblecommentary.org
Msingi wa Mandiko ya Kibiblia yaliyotumika katika fasihi hii yametoka katika toleo la: New American Standard Bible (lililoboreshwa, 1995) Copyright ©1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 by The Lockman Foundation, P. O. Box2279, La Habra, CA 90632-2279

# ORODHA YA YALIYOMO

Neno Toka kwa Mwandishi: Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ........ 6

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika ........ 8

Vifupisho Vilivyotumika Katika Fasihi Hii ........ 15

Fasiri:

Utangulizi wa Wakolosai ........ 16

Wakolosai 1 ........ 24

Wakolosai 2 ........ 55

Wakolosai 3 ........ 72

Wakolosai 4 ........ 90

Utangulizi wa Waefeso ........ 101

Waefeso 1 ........ 109

Waefeso 2 ........ 138

Waefeso 3 ........ 164

Waefeso 4 ........ 180

Waefeso 5 ........ 201

Waefeso 6 ........ 218

Utangulizi wa Filemoni ........ 234

Filemoni ........ 237

Utangulizi wa wafilipi ........ 247

Wafilipi 1 ........ 253

Wafilipi 2 ........ 276

Wafilipi 3 ........ 292

Wafilipi 4 ........ 306

Viambatisho:

Maelezo Mafupi ya Muundo wa Kisarufi Cha Kiyunani ........ 317

Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi ........ 326

Ufafanuzi/Farahasa ........ 330

Maelezo ya Kimaandiko ........ 339

# VIELELEZO VYA MADA MAALUM

Kutuma ( *Apostellō)* ........................................ 25
Masihi ........................................ 26
Watakatifu ........................................ 28
Imani, Amini Au Sadiki (Pistis [Nomino], *Pisteuō,* [Kitenzi] *Pistos [*Kivumishi] ........................................ 29
Baba ........................................ 30
Majina Ya Uungu ........................................ 31
Tumaini ........................................ 33
Matumizi Ya Paulo Ya *Kosmos* (Ulimwengu) ........................................ 34
Urithi Wa Waaminio ........................................ 37
Mwana Wa Mungu ........................................ 38
Fidia /Ukombozi ........................................ 40
Mzaliwa Wa Kwanza ........................................ 43
*Archē* ........................................ 43
Kanisa (*Ekklesia* ........................................ 44
Amani (Maana Tofauti) ........................................ 46
Mwili (*Sarx)* ........................................ 47
Pasipo Lawama, Pasipo na Hatia, Pasipo Kuhukumiwa, Wala Mawaa ........................................ 48
Yesu na Roho ........................................ 52
Moyo ........................................ 56
Vita Mbinguni ........................................ 64
Ujasiri (*Parrhēsia)* ........................................ 64
Yawapasa Wakristo Wahukumiane Wao Kwa Wao ........................................ 65
Teketeza, Angamiza, Haribu (*Phtheirō)* ........................................ 69
Uhuru Wa Mkristo Dhidi Ya Wajibu Wa Mkristo ........................................ 70
Mungu Anaelezwa Kama Mwanadamu (Lugha Za Kibinadamu) ........................................ 74
Maneno Ya Agano Jipya Kuhusiana na Kurudi Kwa Yesu ........................................ 75
Uovu na Wema Katika Agano Jipya ........................................ 77
Usemi Wa Mwanadamu ........................................ 79
Kufanya Upya (*Anakainōsis*) ........................................ 80
Ubaguzi Wa Kimbari ........................................ 81
Karimu/ Utiifu ........................................ 88

Sala ya Shukrani ..... 91
Maombi Ya Kusihi ..... 94
Matumizi Ya Neno “Mlango” Katika Agano Jipya ..... 96
Vyeo Vya Agano La Kale Vya Mteule Ajaye ..... 111
Utakaso ..... 112
Utatu ..... 114
Takatifu ..... 116
Kuamriwa Kabla (Calvinism) Dhidi Ya Utashi Huru Wa Mwanadamu(Arminiasm) ..... 119
Vitenzi Vya Nyakati Vya Kiyunani ..... 123
Utele (Perisseuō) ..... 125
Mapenzi (*Thelēma*) Ya Mungu ..... 126
Uchaguzi/Kuamriwa Kabla Na Uhitaji Wa Uwiano Wa Ulali Wa Kithiolojia ..... 128
Kweli” Katika Maandiko Ya Paulo ..... 129
Muhuri ..... 129
Hulka Ya Roho ..... 130
Matumizi ya Paulo ya Neno Ambatani*“Huper* ..... 133
Nyakati hizi na Nyakati Zijazo ..... 135
Uovu Binafsi ..... 141
Kutawala Katika Ufalme Wa Mungu ..... 144
Kusadiki, Amini, Imani Na Uaminifu Katika Agano La Kale (ןמא) ..... 146
Ushahidi wa Wokovu  Mtu wa Agano Jipya ..... 150
Kujisifu ..... 150
Agano ..... 153
Batili Na Utupu (*Katargeō*) ..... 155
Sheria ya Musa na Mkristo ..... 156
Unabii wa Agano Jipya ..... 159
Jiwe Kuu la Pembeni ..... 161
Adilisha ..... 163
Mpango Wa Mungu Juu Ya Ukombozi, “Siri” ..... 166
Mpango Wa YHWH wa Ukombozi wa Milele ..... 168
Dhiki Kuu ..... 172
Sifa ya Paulo, Maombi, na Utoaji Wa Shukrani Kwa Mungu ..... 175
Milele [Nahau Ya Kiyunani] ..... 176

Amina ........ 178
Kuitwa ........ 182
Uwepo wa Mungu Mmoja ........ 184
Mbingu ........ 187
Haki ........ 192
Utajiri ........ 196
Ufalme wa Mungu ........ 204
Unyenyekevu ........ 209
Wanawake Ndani ya Biblia ........ 210
Kichwa (*Kephalē*) ........ 214
Maonyo ya Paulo kwa Watumwa ........ 221
Kufanywa Imara ........ 224
Kusimama (*Histēmi*) ........ 225
Malaika Katika Maandiko Ya Paulo ........ 226
Pepo(Roho Wachafu) ........ 227
Maombi Yenye Ufanisi ........ 231
*Koinōnia* ........ 241
Ustahimilivu ........ 260
Mlinzi Wa Mfalme ........ 265
Wafu Wako Wapi? ........ 269
Ukiri ........ 282
Maneno ya Kiyunani kwa Ajili ya Majaribio na Vidokezo Vyake ........ 288
Mafarisayo ........ 295
Muundo ........ 302
*Maranatha* ........ 309
Kanisa (*Ekklesia)* ........ 314

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIHI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS[4]). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today’s English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoriki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving’ang’anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
June 27, 1 996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## I. DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

   Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

### 1. Mduara wa kwanza wa usomaji

a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
   1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
   2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
   3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.

c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
    1) Agano la kale
        a) Simulizi za waebrania
        b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
        c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
        d) Alama za siri za ki-sheria
    2) Agano jipya
        a) Simulizi (Injili, matendo)
        b) Hadithi za mafumbo (Injili)
        c) Barua/nyaraka
        d) Fasihi za mafunuo

## 2. Mduara wa pili wa usomaji

a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## 3. Mduara wa tatu wa usomaji.

a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
    1) Mwandishi
    2) Tarehe
    3) Wapokeaji
    4) Kusudu mahsusi la uandishi
    5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
    6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## 4. Mduara wa nne wa usomaji

a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
    1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
    2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
    3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia fahisi au muundo wa kisarufi
    1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
    2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
    3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
    1) Istilahi muhimu
    2) Istahili zisizo za kawaida
    3) Muundo muhimu wa kisarufi
    4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
    1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
        a) Vitabu vya thiolojia
        b) Biblia za marejeo
        c) Itifaki

2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana na uthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kile kile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
1) Soma biblia
2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
3) Tangulizi za biblia
4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18
   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi

b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
c. Habari za kisarufi
d. Usomaji wa neno
e. Njia muhimu zilizo sambamba

5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
   a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
   b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
   c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
   d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
   a. Tofauti za mswada
   b. Maana ya maneno mbadala
   c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
   d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

| | |
|---|---|
| AB | Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman |
| ABD | Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman |
| AKOT | Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens |
| ANET | Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard |
| BDB A | Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs |
| IDB | The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick |
| ISBE | International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr |
| JB | Jerusalem Bible |
| JPSOA | The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America) |
| KB | The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner |
| LAM | The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa |
| LXX | Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970 |
| MOF | A New Translation of the Bible by James Moffatt |
| MT | Masoretic Hebrew Text |
| NAB | New American Bible Text |
| NASB | New American Standard Bible |
| NEB | New English Bible |
| NET | NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition |
| NRSV | New Revised Standard Bible |
| NIDOTTE | New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren |
| NIV | New International Version |
| NJB | New Jerusalem Bible |
| OTPG | Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith |
| REB | Revised English Bible |
| RSV | Revised Standard Version |
| SEPT | The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970 |
| TEV | Today's English Version from United Bible Societies |
| YLT | Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young |
| ZPBE | Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney |

# UTANGULIZI WA WAKOLOSAI

## MAELEZO YA UTANGULIZI

A. Namshukuru Mungu kwa ajili ya wale waliokuwa na imani kinyume na mafundisho kule Kolosai; kwa sababu yao Paulo alilazimika kuwaandikia barua ya nguvu. Kumbuka kuwa kukielewa kitabu, tunalazimika kukihusianisha na muundo wake wa kihistoria. Nyaraka za Paulo ziliitwa "nyaraka za kimatukio"kwa sababu alikuwa akielezea matatizo ya kimahala yakiwa na ukweli wa injili ya wote. Imani iliyo kinyume na mafundisho kule Kolosai ilikuwa ni mchanganyiko usio wa kawaida wa falsafa ya Kiyunani (watu waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee) na dini ya Kiyahudi.

B. Mamlaka ya Yesu kuhusu ulimwengu mzima (au kuuweka kwa namna nyingine, Yesu kama muumbaji, mwokozi, na Bwana wa uumbaji wote na uhusishaji wa maisha ya Kikristo) ndio kiini cha dhamira (k.v. Kol. 1 :1 5-1 7). Theolojia ya kitabu hiki kumhusu Yesu haijazidi kiwango! Wakolosai wanaunda maelezo ya msingi kwa Waefeso. Paulo alitambua imani potofu ingalisambaa katika Asia ndogo. Wakolosai waliyashambulia mafundisho ya uongo wakati Waefeso waliendeleza kiini cha dhamira zake kwa kuandaa makanisa mengine kwa ajili ya imani potofu inayokuja. Msisistizo wa Wakolosai ulikuwa ni wa kithiolojia kumhusu Yesu wakati msisistizo wa Waefeso ulikuwa ni umoja wa vitu vyote katika Kristo, ambaye ndiye Bwana wa vitu vyote.

C. Paulo alikanusha ushikiliaji sana wa sheria, kwa wote Wayahudi na Wayunani, kwa maneno ya nguvu (Kol. 2:6-23). Ukichukulia waraka huu kama mfano, mmoja anaweza kushangaa jinsi Paulo angaliweza kuwaelezea wale wenye imani iliyo kinyume wa leo. Hakika angaliweza kukabiliana nao!

## MJI WENYEWE

A. Kiasili mji wa Kolosai ulikuwa ni sehemu ya ufalme wa Pergamo ndani ya Phrygia. Katika mwaka wa 33 K.K mji huo ulikabidhiwa kwa baraza la uongozi wa Rumi.

B. Mji wa Kolosai ulikuwa ni mji mkubwa wa kibishara kabla ya siku za Paulo (k.v. Heroditus' *Histories* VII:30 na Xenophon *Anabasis* 1 :2:6).
   1. Kwenye bonde ambalo Kolosai ilionekana palikuwa ni Mediteranian ya kale iliyooongoza duniani kwa uzalishaji wa sufi, hasa sufi nyeusi, na sufi zilizorembeshwa, zambarau na rangi nyekundu. Udongo uliotokana na volcano ulitengeneza uwanda mzuri wa kijani kibichi na maji yake ya kichokaa yalirembesha mchakato wake (Strabo,1 3:4:1 4).
   2. Shughuli za kivolcano (Strabo, 1 2:8:6) zilisababisha mji kuharibiwa mara kadhaa katika historia yake; mwishoni mwa kipindi cha mwaka 60 B.K (Tacitus) au 64 B.K (Eusebius).

C. Mji wa Kolosai ulikuwa maeneo ya juu ya Mto Lycus, kijito cha Mto Maeander uliotiririka kuelekea Efeso, mile 100 kwenye mwelekeo wa mto. Katika bonde hili moja palikuwepo na miji mingine midogo midogo mingi ambapo Epaphras alianzisha makanisa: Hierapolis (yapata mile 6) na Laodicea (yapata mile 10, k.v. Kol. 1 :2; 2:1 ; 4:1 3, 1 5-1 6) na Kolosai.

D. Baada ya Warumi kujenga njia yao kuu pande za Mashariki mwa Magharibi, *Via Ignatia*, iliyopitia Kolosai, kiwastani haikupunguza chochote (Strabo). Pia hili lilifanana na kile kilichotokea Petra kupitia eneo la Jordan kule Palestina.

E. Mji ulikaliwa na watu wa Mataifa (wakazi wa Phrygia na walowezi wa Kiyunani), lakini palikuwa na Wayahudi wengi pia. Yusufu anatuambia kuwa Antiochus III (223-1 87 K.K.) aliwasafirisha Wayahudi 2,000 toka Babel kwenda Kolosai. Takwimu zinaonyesha kuwa kufikia mwaka wa 76 B.K Wayahudi wa kiume 11,000 waliishi kwenye Wilaya ambayo Mji mkuu wake ulikuwa Kolosai.

## MWANDISHI

A. Palikuwa na watu wawili waliopeleka, Paulo na Timotheo(k.v Kol. 1:1). Ingawa, mwandishi mkuu alikuwa Paulo; lakini Timotheo alikuwa akipeleka salamu kama mtumishi mwenza wa Paulo na yumkini mwandishi wake (*amanuensus*).

B. Maelezo ya mwanzo hayapingi kuwa Paulo Mtume alikuwa mwandishi;

1. Marcion (aliyeingia Rumi mwaka wa 1 40 B.K), mpinzani wa imani potofu ya Agano la Kale, alijumuishwa katika mkusanyo wa maandishi ya Pauline.
2. Aliorodheshwa na nyaraka za Paulo katika orodha ya sheria ya vitabu vya kanisa toka Rumi yapata mwaka 180-200 B.K)
3. Makasisi wengi wa kanisa la mwanzo walinukuliwa toka humo na kumtambua Paulo kama mwandishi
   a. Irenaeus (aliandika mwaka wa 177-190 B.K)
   b. Clement wa Iskandaria (aliishi mwaka wa 160-216 B.K)

## UHUSIANO WA FASIHI KATI YA WAKOLOSAI NA WAEFESO

A. Uhusiano wa kihistoria kati ya barua mbili toka gerezani unafuata maelezo haya
   1. Epaphras (Col. 1 :7; 4:1 2; Filemon 1 :23) aliongoka wakati wa kampeni ya Paulo akiwa kule Efeso (Acts 1 9).
      a. Epaphras aliendа na imani mpya alioipokea maeneo ya nyumbani kwao, bonde la Mto Lycus (k.v. Col. 4:1 2).
      b. Epaphras alianzisha makanisa matatu: Hierapolis, Laodicea (cf. Col. 4:1 3), na Kolosai.
      c. Epaphras alimwomba Paulo kwa ajili ya ushauli namna ya kukabiliana na Ukristo unaojitokeza, dini ya Kiyahudi, na fikra za Kiyunani, ambazo wale wenye imani potofu walikuwa wakizifundisha. Paulo alikuwa amefungwa jela (k.v. Kol. 4:3,1 8) huko Rumi (mwanzoni mwa miaka ya 60).
   2. Walimu wa uongo walitetea falsafa ya Kiyunani ya kuchunguza chanzo cha uhai na maarifa
      a. Roho na maada vilikuwa pamoja katika umilele
      b. Roho (mungu) alikuwa mwema
      c. maada (uumbaji) ilikuwa ovu
      d. Mlolongo wa *aeons* (ngazi za kimalaika), hasa katika uandishi wa Valentini, ukapata kuwepo kati ya Mungu mwema aliye juu na mungu mdogo aliyeumba maada
      e. Wokovu uliegemea juu ya maarifa ya siri yaliyowasaidia watu kuendelea kupitia ngazi ya kimalaika (*aeons*) hadi kwa Mungu mwema Mkuu.

B. Uhusiano wa kifasihi kati ya barua mbili za Paulo
   1. Paulo alisikia juu ya imani potofu ndani ya makanisa haya ambayo kibinafsi hakuwahi kuyazuru (k.v. Col. 1 :7-8).
   2. Paulo aliandika kwa kifupi barua ngumu iliyowalenga, sentensi za kihisia, zilizolenga walimu wa uongo. Dhamira kuu ilikuwa ni kuhusu mamlaka ya Yesu kuhusu ulimwengu mzima. Hili linajulikana kama barua ya Paulo kwa Wakolosai.
   3. Inavyoonekana, mara tu baada ya kuwaandikia Wakolosai, akiwa na muda mkononi mwake huko gerezani, akaanzisha mada nyingine tunayoifahamu kama waraka kwa Waefeso. Alitambua kuwa jaribio hili la kuunganisha fikra za Kiyunani na injili kwa kusudi la kutengeneza “umuhimu” wa Ukristo katika tamaduni za Kiyunani ungalisambaa kwenye makanisa yote mapya katika Asia ndogo. Waefeso wanatambulika kwa sentensi ndefu na uanzishwaji wa dhana ya kithiolojia (Kol. 1 :3-1 4, 1 5-23; 2:1 -1 0,14-18,19-22;3:1-1 2, 1 4-1 9; 4:1 1 -
      1 6; 6:1 3-20). Inawafanya Wakolosai kama alama ya kuanzia na kuwaondolea uhusianishaji wao wa kithiolojia. Dhamira yao kuu ni kuviunganisha vitu vyote kwa Kristo, ambacho ni kinyume na *aeons* (ngazi za kimalaika) ya watu waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee(Gnosticism).

C. Kuhusiana na muundo wa kifasihi na kithiolojia
   1. Msingi wa muundo
      a. Walikuwa na maelezo ya ufunguzi uliofanana
      b. Kila mmoja alikuwa na sehemu ya kimafundisho kimsingi yaliyoshughulika na Kristo
      c. Kila mmoja alikuwa na sehemu ya kiutendaji iliyosisitiza juu ya stadi ya maisha ya Kikristo yakitumia namna, maneno, na vifungu vya aina moja
      d. Wote walikuwa na mistari ya kufungia ya kweli inayofanana. Katika Kiyunani walishirikiana maneno 29 kwa pamoja; Wakolosai waliongeza maneno mawili tu ya nyongeza (“aliye mtumwa wa kwenu”). Linganisha Waefeso 6:21-22 na Wakolosai 4:7-9

2. Maneno yanayofanana au vifungu vifupi
   Efe. 1 :1 c na Kol. 1 :2a "mwaminifu"
   Efe.1 :4 na Kol. 1 :22 "mtakatifu na asiyekuwa na lawama"
   Efe. 1 :7 na Kol. 1 :1 4 "ukombozi…msamaha"
   Efe. 1 :1 0 na Kol. 1 :20 "vitu vyote….mbingu…nchi"
   Efe. 1 :1 5 na Kol. 1 :3-4 "tuliposikia….upendo mlionao kwa watakatifu wote"
   Efe. 1 :1 8 na Kol. 1 :27 "utajiri wa utukufu"
   Efe. 1 :27 na Kol. 1 :1 8 "tuliposikia…..kanisa"
   Efe. 2:1 na Kol. 1 :1 3 "mlikuwa wafu"
   Efe. 2:1 6 na Kol. 1 :20 "kuvipatanisha…..msalaba"
   Efe. 3:2 na Kol. 1 :25 "mhudumu"
   Efe. 3:3 na Kol. 1 :26,27 "siri"
   Efe. 4:3 na Kol. 3:1 4 "umoja"
   Efe. 4:1 5 na Kol. 2:1 9 "kichwa" na "hukua"
   Efe. 4:24 na Kol. 3:1 0, 1 2, 14 "mkivaa….."
   Efe. 4:31 na Kol. 3:8 "hasira" "ghadhabu" "uovu" "matusi"
   Efe. 5:3 na Kol. 3:5 "uasherati" "uchafu" "uchoyo"
   Efe. 5:5 na Kol.3:5 "uchafu" (tama mbaya)
   Efe. 5:6 na Kol. 3:6 "ghadhabu ya Mungu"
   Efe. 5:1 6 na Kol. 4:5 "mkiukomboa wakati"
3. Vifungu sahihi au sentensi
   Efe. 1 :1 a na Kol 1 :1 a
   Efe. 1 :1 b na Kol. 1 :2a
   Efe. 1 :2a and Col. 1 :2b
   Eph. 1 :1 3 na Kol. 1 :5
   Efe. 2:1 na Kol. 2:1 3
   Efe. 2:5b na Kol. 2:1 3c
   Efe. 4:1 b na Kol. 1 :1 0a
   Efe. 6:21 ,22 na Kol. 4:7-9 (maneno 29 mfululizo isipokuwa "kai syndoulos" katika Wakolosai)
4. Vifungu vinavyfanana au sentensi
   Efe. 1 :21 na Kol. 1 :1 6
   Efe. 2:1 na Kol. 1 :1 3
   Efe. 2:1 6 na Kol. 1 :20
   Efe. 3:7a na Kol. 1 :23d, 25a
   Efe. 3:8 na Kol. 1 :27
   Efe. 4:2 na Kol. 3:1 2
   Efe. 4:29 na Kol. 3:8; 4:6
   Efe. 5:1 5 na Kol. 4:5
   Efe. 5:1 9,20 na Kol. 3:1 6
5. Dhana ya maneno sawa kithiolojia
   Efe. 1 :3 na Kol. 1 :3
   Efe. 2:1 ,1 2 na Kol.1 :21
   Efe. 2:1 5 na Kol. 2:14
   Efe. 4:1 na Kol 1 :10 maombi ya shukrani
   Efe. 4:1 5 na Kol. 2:19 kutenganishwa na Mungu
   Eph. 4:1 9 and Kol. 3:5 kuenenda kunakostahili
   Efe.4:22,31 na Kol. 3:8 mwili wa Kristo ukuwao kuelekea makuzi toka kichwani
   Efe.4:32 na Kol. 3:1 2-13 uchafu wa kujamiiana "jitengeni " na dhambi
   Efe. 5:4 na Kol. 3:8 aina ya Ukristo kati ya mtu na mwingine
   Efe. 5:1 8 na Kol. 3:16 hotuba za Kikristo kujazwa na roho=neno la Kristo
   Efe. 5:20 na Kol. 3:17 utoaji shukrani kwa Mungu kwa ajili ya vitu vyote wanawake wawajibike kwa

waume zao
Efe. 5:22 na Kol. 3:18   waume wawapende wake zao watoto wawaheshimu wazazi wao
Efe. 5:25 na Kol. 3:19   baba msiwachokoze watoto watumwa wawatii bwana zao
Efe. 6:1 na Kol. 3:20    mabwana na watumwa
Efe. 6:4 na Kol. 3:21    hitaji la Paulo kwa ajili ya maombi
Efe. 6:5 na Kol. 3:22
Efe. 6:9 na Kol. 4:1
Efe. 6:1 8 na Kol. 4:2-4

Maneno na vifungu vilivyotumika kote katika Wakolosai na Waefeso ambavyo havipatikani kwingine katika fasihi ya Pauline

a. "ukamilifu" (ambalo lilikuwa ni neno la ujuzi wa kipekee kwa ngazi za kimalaika)
   Eph. 1 :23  "ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika yote
   Eph. 3:1 9  "mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu"
   Eph. 4:1 3  "utimilifu wa Kristo"
   Col. 1 :19  "utimilifu wote ukae"
   Col. 2:9    "katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu"
b. Kristo kama "kichwa" cha kanisa
   Efe. 4:1 5; 5:23 na Kol. 1 :1 8; 2:1 9
c. "kuwafarakanisha"
   Eph. 2:1 2; 4:1 8 and Col. 1 :21
d. "wakiukomboa wakati"
   Efe. 5:1 6 na Kol. 4:5
e. "shina"
   Efe. 3:1 7 na Kol. 1 :5
f. "kulisikia neno la kweli, injili"
   Efe. 1 :1 3 na Kol. 1 :5
g. "wakichukuliana"
   Efe. 4:2 na Kol. 3:13
h. Utumiaji wa maneno na vifungu kusiko kwa kawaida ("wekwa pamoja," "toa")
   Efe. 4:1 6 na Kol. 2:1

D. Muhtasari
   1. zaidi ya theluthi moja ya maneno katika Wakolosai yapo pia katika Waefeso. Imekwisha kadiriwa kuwa mistari 75 kati ya 155 katika Waefeso inafanana na Wakolosai. Yote yanadai uandishi wa Paulo akiwa gerezani.
   2. Wote waliokolewa na rafiki wa Paulo Tychicus
   3. Wate walipelekwa sehemu moja(Asia Ndogo)
   4. Wote walishughulika na mada ile ile ya kithiolojia kumhusu Yesu
   5. Wote walisisitiza Kristo kama kichwa cha kanisa
   6. Wote walitia moyo juu ya kuishi maisha ya Kikristo

E. Hoja kuu juu ya utofauti wake
   1. Kanisa mara zote linabaki kuwa la mahala hapo katika Kolosai lakini la wote katika Efeso. Hii yawezakuwa ni kwa sababu ya asili ya kidunia ya Waefeso.
   2. Imani potofu, ambayo ni sura maarufu ya Wakolosai, moja kwa moja vinakosekana katika Waefeso. Ingawa, herufi zote zinatumia uainishaji wa maneno yenye ujuzi wa kipekee ("hekima," "maarifa," "utimilifu," "siri," "mamlaka na nguvu," na "uwakili").
   3. Ujio wa mara ya pili ni wa haraka katika Wakolosai lakini kwa Waefeso umecheleweshwa. Kanisa lilikuwa, na linaendelea, kuitwa kuutumikia ulimwengu ulioanguka (Kol. 2:7; 3:21 ; 4:1 3).
   4. Kiuainishaji maneno mengi yametumika kivingine. Moja ya mfano ni neno "siri." Katika Wakolosai siri ni Kristo (Kol. 1 :26-27; 2:2; 4:3), lakini katika Waefeso (Kol. 1 :9; 5:32) ni uficho wa Mungu kipindi cha Nyuma, lakini sasa kimefunuliwa, mpango wa umoja wa watu wa mataifa na Wayahudi.

5. Waefeso wana vidokezo vingi vya agano la kale (Efe. 1 :22 -- Ps. 8; Efe. 2:1 7-- Isa. 57:1 9) (Efe. 2:20 -- Zab. 1 1 8:22) (Efe. 4:8 -- Zab. 68:1 8) (Efe. 4:26 -- Zab. 4:4) Efe. 5:1 5 -- Isa. 26:19, 51 :1 7, 52:1 , 60:1 ) (Efe. 5:31 -- Mwa. 2:24) (Efe. 6:2-3 -- Kut. 20:1 2) (Efe. 6:1 4 -- Isa. 1 1 :5, 59:1 7) (Efe. 6:1 5 -- Isa. 52:7) lakini kuna mmoja pekee au wawili katika Kolosai, Kol. 2:3 -- Isa. 1 1 :2, na yumkini Kol. 2:22 -- Isa. 29:1 3.

F. Ingawa zinafanana katika maneno, vifungu na mara nyingi katika maelezo, herufi pia inajumuisha dhana ya kipekee:
1. Baraka ya neema ya imani ya mafundisho ya Utatu, Efe. 2:1-1-3:1-3
2. Njia ya neema, Efe. 2:1-10
3. Muunganiko wa Wayahudi na Wayunani katika upya wa mwili mmoja, Efe. 2:11-3:13
4. Umoja na ukirimiwaji wa mwili wa Kristo, Efe. 4:1-16
5. "Kristo na kanisa" kama ufuataji wa mtindo wa mme na mke, Efe. 5:22-23
6. Njia ya vita ya kiroho, Efe. 6:10-18
7. Njia ya ufuatiliaji wa thiolojia kumhusu Yesu
8. Ibada za kidini za mwanadamu na sheria, Kol. 2:16-23
9. Dhamira ya umuhimu kuhusu ulimwengu mzima katika Kristo huko Kolosai dhidi ya dhamira ya umoja wa vitu vyote katika Kristo huko Efeso

G. Katika hitimisho, inaonekana ni vizuri kufuata A. T. Robertson na F. F. Bruce katika kudai kwamba Paulo aliandika barua zote katika hali ya kuwa karibu na kujenga fikra za Wakolosai kwenye uwasilishwaji wake wa kweli wa jiwe la chepeo, Efeso.

## TAREHE

A. Tarehe ya Wakolosai inahusianishwa na ile ya kuwekwa kwa Paulo gerezani (Efeso, Filipi, Kaisaria au Rumi). Kufungwa kwake kule Rumi kunafaa zaidi katika kweli ile ya Matendo.

B. Mara Rumi ilipofikiliwa kuwa sehemu ya kifungo, swali liliibuka wakati upi? Kitabu cha Matendo kinaweka kumbu kumbu kuwa Paulo iliwekwa gerezani kwenye mwanzoni mwa miaka ya 60. Ingawa, aliachiliwa na kuandika barua ya kichungaji (1 & 2 Timotheo na Tito) na baadaye alikamatwa tena na kuuwawa kabla ya tarehe 9/6, mwaka wa 68 B.K (tarehe mtawala Nero alipojiua), yumkini katika mwaka wa 67 B.K

C. Utabiri mzuri wa kisomi kwa ajili ya kuandika juu ya Wakolosai (Waefeso na Filemoni) ndio kifungo cha kwanza cha Paulo, mwanzoni mwa miaka ya 60. (waraka wa mwisho wa Paulo akiwa gerezani ulikuwa ni wa Wafilipi, yumkini uliandikwa katikati ya mwaka wa 60)

D. Tychicus, akiwa na Onesmo, yumkini alichukua barua ya Wakolosai, Waefeso na Filemon na kuzipeleka huko Asia Ndogo. Baadaye, yumkini baada ya miaka mingi, Epafrodito, alipopona katika ugonjwa wake alichukua barua ya Wafilipi na kuirudisha kwenye kanisa la nyumbani kwao.

E. Inawezekana utaratibu wa kupanga miaka na matukio ya uandishi wa Paulo unafuatisha ule wa F. F. Bruce na Murry Harris ikiwa na mjongeo mdogo

| | KITABU | TAREHE | MAHALI | UHUSIANO NA MATENDO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wagalatia | 48 | Antiokia,Syria | Mdo. 14:28, 15:2 |
| 2. | 1 Wathesolanike | 50 | Korintho | Mdo. 18:5 |
| 3. | 2 Wathesolanike | 50 | Korintho | |
| 4. | 1 Wakorintho | 55 | Efeso | Mdo. 19:20 |
| 5. | 2 Wakorintho | 56 | Makedonia | Mdo. 20:2 |
| 6. | Warumi | 57 | Korintho | Mdo. 20:3 |
| 7. | 7-10 nyaraka za gerezani | | | |
| | Wakolosai | mwanzoni mwa Mwaka wa 60 | Rumi | |
| | Filemoni | mwanzoni mwa Mwaka wa 60 | Rumi | |
| | Waefeso | mwanzoni mwa Mwaka wa 60 | Rumi | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wafilipi | mwishoni mwa Mwaka wa 62-63 | Rumi | Mdo. 28:30-31 |
| 11-13 Safari ya Nne Ya umisionari | | Efeso? | |
| 1 Timotheo | 63 au baadaye | Makedonia | |
| Tito | 63 lakini kabla | | |
| 2 Timotheo | 64 B.K 68) | Rumi | |

## WAPOKEAJI NA MAHALI

A. Kanisa kiuhalisia lilianzishwa na Epafrasi (k.v Kol. 1 :7,8; 2:1 ; 4:1 2-1 3), ambaye yumkini aliokolewa na Paulo huko Efeso (k.v Kol. 1:7-8 na linganisha na Kol. 2:1). Kiwastani liliundwa na watu wa mataifa (k.v Kol. 1:21; 3:7). Epafras alimfikia Paulo akiwa gerezani kumwelezea tatizo la walimu wa uongo wanaofundisha mchanganyiko wa Ukristo na falsafa za Kiyunani zinazojulikana kama ujuzi wa kipekee (Kol. 2:8) na ushikiliaji wa sheria za Kiyahudi (k.v. viashilia vya Kiyahudi, Kol. 2:11, 16, 17; 3:11; kuwaabudu malaika, Kol. 1:16; 2:15, 18 na kunyima mambo ya anasa Kol. 2:20-23). Kulikuwepo na jumuiya kubwa ya Wayahudi huko Kolosai ambao mwishiwe wakaja kuwa Wayunani. Asili ya tatizo linasimama likimhusu mtu na kazi ya Kristo. Wale waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee walikana kuwa Yesu alikuwa mtu kamili lakini wakathibitisha kuwa alikuwa na Uungu kamili kwa sababu ya upinzani wa ndani wa pande mbili kati ya umbo na roho. Wangaliweza kuthibitisha Uungu wake lakini wakakana ubinadamu wake. Pia waliweza kukana fahari ya kiuandishi. Kwa wao palikuwepo na ngazi nyingi za kimalaika (*aeons*) kati ya mungu mwema mkuu na mwanadamu; Yesu, japokuwa Yeye ni mkuu, alikuwa mmoja wa miungu. Pia walionekana kuwa wenye uwezo mkubwa wa kufikiri (k.v. Kol. 3:11,14,16,17) na kusisitiza maarifa ya siri maalumu yasiojumuishwa (k.v Kol. 2:15,18,19) kama njia kumwelekea Mungu badala ya upatanisho wa Yesu, dhabihu kwa ajili yaw engine na mwitikio wa toba ya imani ya mwanadamu  kwa ajili ya msamaha wa bure

B. Kwa sababu ya mazingira haya ya kisaikolojia na kithiolojia, kitabu cha Wakolosai kinasisitiza
   1. Upekee wa ubinadamu wa Kristo na kazi yake aliyoitimiliza ya wokovu.
   2. Umiliki wa kiulimwengu mzima, utawala na umuhimu wa Yesu wa Nazareti-kuzaliwa kwake, mafundisho yake, maisha yake, kifo chake, ufufuo wake na kupaa kwake! Yeye ni Bwana wa yote!

## KUSUDI

Kusudi la Paulo lilikuwa ni kukanusha imani potofu ya Wakolosai. Kulitimiliza kusudi hili, alimwinua Kristo kama

1. Taswira kamili ya Mungu (Kol. 1 :1 5) muumbaji (Kol. 1 :1 6)
2. Mwezeshaji wa vitu vyote aliyewahi kuishi kabla (Kol. 1:17)
3. Kichwa cha kanisa (Kol. 1:18)
4. Wa kwanza kufufuka (Kol. 1:18)
5. Utimilifu wa Uungu katika hali ya kiumbo (Kol. 1:19, 2:9)
6. Msuluhishi kati ya Mungu na mwanadamu (Kol. 1:20-22)

Hiyo basi, moja kwa moja Kristo alikuwa anatosha. Paulo alitumia cheo cha “Kristo” mara 25 katika kitabu hiki kidogo! Waamini “waliishapewa utimilifu katika Kristo” (Kol. 2:10). Imani potofu ya Kikolosai kiujumla ilikuwa ya kithiolojia isiotoshereza kutoa wokovu wa kiroho. Ilikuwa falsafa tupu na danganyifu (Kol. 2:8), ikikosa uwezo wa kuzuia asili ya dhambi ya kale (Kol. 2:23)

Dhamira ya kujirudia katika Wakolosai ni utosherevu mzima wa Kristo kama ilivyopingana na utupu wa falsafa ya mwanadamu. Utosherevu huu unaelezewa katika mamlaka ya Yesu kuhusu ulimwengu mzima. Yeye ni mmiliki, muumbaji na mwenye mamlaka juu ya vitu vyote, vinavyoonekana na visivyoonekana (k.v Kol. 1:15-18)

## MAELEZO YA MUHTASARI

A. Ufunguzi wa kidesturi wa Pauline
   1. Utambulisho wa mpelekaji, Kol. 1:1
   2. Utambulisho wa wapokeaji, Kol. 1:2a

3. Salamu, Kol. 1:2b

B. Mamlaka ya juu kabisa ya Kristo (mada 1-10 zimechukuliwa toka NKJV aya zenye maelezo ya muhtasari)
   1. Imani katika Kristo Kol. 1:3-8
   2. Ufahari wa Kristo, Kol. 1:9-18
   3. Upatanisho katika Kristo Kol. 1:19-23
   4. Huduma ya kujidhabihu ya Kristo, Kol. 1:24-29
   5. Sio falsafa, lakini Kristo, Kol. 2:1-10
   6. Sio ushikiaji wa sheria, lakini Kristo, Kol. 2:11-23
   7. Sio kuwa wa kimwili, lakini Kristo, Kol. 3:1-11
   8. Kumvaa Kristo, Kol. 3:12-17
   9. Mruhusu Kristo atawale nyumba yako, Kol. 3:19-4:1
   10. Mruhusu Kristo ayatawale maisha yako ya kila siku, Kol. 4:2-6

C. Wapeleka habari wa Paulo, Kol. 4:7-9

D. Marafiki wa Paulo wanapeleka salamu zao, Kol. 4:10-14

E. Paulo anatuma salamu, Kol. 4:15-17

## HALI YA KUWA NA UJUZI WA KIPEKEE

A. Kiwastani maarifa yetu juu ya imani potofu huja toka kwenye maandiko yenye ujuzi ya karne ya pili. Ingawa, mawazo ya mwanzo yalikuwepo katika karne ya kwanza (Magombo ya Bahari ya Chumvi).

B. Tatizo kule Kolosai lilikuwa ni Ukristo wa kichotara, ujuzi wa mwanzo, na ushikiliaji ya sheria wa dini ya Kiyahudi.

C. Baadhi wanaelezea itikadi ya Valentino na ujuzi wa Cerinthia wa karne ya pili:
   1. Maada na roho vilikuwa katika hali ya umilele (pande mbili za metafizikia). Maada ni ovu, roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni roho, hawezi moja kwa moja kuhusianishwa na utengenezaji wa vitu viovu.
   2. Kuna utokeaji (*aeons* au kwa ngazi ya kimalaika) kati ya Mungu na vitu. Wa mwisho au wa chini alikuwa ni YHWH wa agano la kale aliyeutengeneza ulimwengu (*kosmos*).
   3. Yesu alitokea kama YHWH lakini akiwa juu katika vipimo, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka katika sehemu ya juu lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika hakuubadili Uungu (k.v Yoh.1:14). Kwa vile vitu ni viovu, Yesu asingalikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa wa ki-Ungu. Alijitokeza kama mwanadamu, lakini kiukweli alikuwa roho (k.v 1 Yoh. 1:1-3; 4:1-6).
   4. Wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, ambayo tu yanajulikana na watu fulani wa kundi. Maarifa (neno la siri) lilihitajika kupitia ulimwengu wa kimbingu. Ushikiriaji sana wa sheria wa Kiyahudi pia ulihitajika kumfikia Mungu.

D. Walimu wa uongo wenye ujuzi walitetea miundo miwili iliyo kinyume kimaadili:
   1. Kwa baadhi, stadi ya maisha haikuhusiana na wokovu. Kwa wao, wokovu na mambo ya kiroho yalielezewa ndani ya maarifa ya kisiri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*aeons*).
   2. Kwa wengine, stadi ya maisha ilikuwa ni muhimu kwenye wokovu. Katika kitabu hiki, walimu wa uongo walisisitiza maisha ya kujinyima raha kama ushahidi wa kweli wa ukuaji wa kiroho (k.v Kol. 2:16-23).

E. Baadhi ya nukuu nzuri yakinifu:
   *The Gnostic Religion* by Hans Jonas, published by Beacon Press
   *The Gnostic Scriptures* by Bentley Layton, Anchor Bible Reference Library
   *The Dictionary ofNewTestament Background*, IVP, "Gnosticism" kur. 41 4-41 7

## KUSOMA MZUNGUKO WA KWANZA (toka "Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia"-"- A Guide to Good Bible Reading)

Huu ni mwongozo wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mtoa maoni.

Kwahiyo, soma Biblia nzima kwa mara moja. Taja mada kuu ya kitabu kizima kwa maneno yako mwenyewe

1. Mada ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi (namna ya uwasiilishaji)

## KUSOMA MZUNGUKO WA PILI (toka "Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia"- A Guide to Good Bible Reading)

Huu ni mwongozo wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mtoa maoni.

Kwahiyo, soma Biblia nzima kwa mara ya pili kwa mara moja. Ainisha mada kuu na zieleze kwa sentensi moja.

1. Mada ya kipengele cha kwanza cha maandiko
2. Mada ya kipengele cha pili cha maandiko
3. Mada ya kipengele cha tatu cha maandiko
4. Mada ya kipengele cha nne cha maandiko
5. Nakadhalika

# WAKOLOSAI 1

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Salamu | Salamu | Salamu | Salamu | Anwani |
| 1:1-2 | 1:1-2 | 1:1-2 | 1:1-2 | 1:1-2 |
| | 1:2a | 1:2a | 1:2a | |
| | 1:2b | 1:2b | 1:2b | |
| Paulo anamshukuru | Imani yao katika | Shukrani na | Maombi ya | Shukrani na |
| Mungu kwa ajili ya | Kristo | Maombezi | Shukrani | Maombi |
| wakolosai | | | | |
| 1:3-8 | 1:3-8 | 1:3-8 | 1:3-8 | 1:3-8 |
| Mtu na kazi ya | Ukuu wa Kabla wa | | | |
| Kristo | Kristo | | | |
| 1:9-20 | 1:9-18 | 1:9-14 | 1:9-14 | 1:9-12 |
| | | | | 1:13-14 |
| | | Mamlaka ya juu | Mtu na Kazi ya | Kristo ni kichwa |
| | | Ya Kristo | Kristo | cha uumbaji wote |
| | Kupatanishwa | 1:15-20 | 1:15-20 | 1:15-20 |
| | Katika Kristo | | | |
| | 1:19-23 | | | |
| | | | | Wakolosai wana |
| | | | | Ubia katika |
| | | | | wokovu |
| 1:21-23 | | 1:21-23 | 1:21-23 | 1:21-23 |
| Huduma ya Paulo | Ibada ya kidhabihu | shauku ya Paulo | Kazi ya Paulo | shughuli za Paulo |
| Kwa Kanisa | kwa ajili ya Kristo | kwa Wakolosai | kama Mtumwa | katika huduma |
| | | | Wa Kanisa | ya mataifa |
| | | (1:24-2:7) | (1:24-2:5) | |
| 1:24-2:5 | 1:24-29 | 1:24-2:5 | 1:24-2:3 | 1:24-29 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanywa na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani (Bief Definitions of Greek), Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi (Textual Criticism), Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko (Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza

2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 1:1-2**
***1*** **Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timotheo, ndugu yetu,** ***2*** **kwa ndugu watakatifu, waaminifu katika Kristo, walioko Kolosai. Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu.**

**1:1 "Paulo"** Sauli wa Tarso kwa mara ya kwanza anaitwa Paulo katika Matendo ya Mitume 13:9. Inawezekana kwamba Wayahudi wengi "wa uhamishoni/walio nje ya nchi yao" (Wayahudi wanaoishi nje ya Palestina) walikuwa na jina la Kiebrania na jina la Kiyunani. Kama ndivyo, kwahiyo wazazi wa Sauli walimpa jina hili lakini kwanini, "Paulo" kwa ghafla anatokea katika Matendo ya Mitume 13? Yawezekana

1. Wengine walianza kwa kumuita jina hili
2. Alianza kujiita mwenyewe kwa neno "mdogo" au aliye wa chini"

Jina la Kiyunani *Paulos* lilimaanisha "mdogo." Baadhi ya nadharia zimekua kutokana na asili ya jina la Kiyunani.

1. Karne ya pili iliweka desturi kuwa Paulo alikuwa mfupi, mnene, mwenye kipara, mwenye matege, mwenye nyusi nyingi kama kichaka, na mwenye macho yanayotokeza njema na yawezekana ndio asili ya jina lake, akitoa katika vitabu visivyo vya kikanoni kutoka katika Thesalonika iliyoitwa *Paul and Thekla*
2. Katika mapito yake ambapo Paulo alijiita mwenyewe "mdogo kati ya watakatifu" kwasababu aliliudhi kanisa kama ilivyo katika Matendo ya Mitume 9:1-2 (rejea 1 Wakorintho 15:9; Waefeso 3:8; 1 Tim 1:15) Wengine wameona huu "udogo" kama wenye asili ya cheo cha kujichagulia mwenyewe. Hata hivyo, katika kitabu kama Wagalatia, ambapo anahimiza uhuru wake na hali ya kuwa sawa na kumi na wawili wa Yerusalemu, hii inaweza isiwe hivyo. (rejea 2 Wakorintho 11:5; 12:11; 15:10)

▣ **"Mtume"** Hii ilitoka katika neno la Kiyunani "kutuma" (*apostellō*). Yesu alichagua wanaume kumi na wawili kuwa nae kwa maana maalumu ya kuwaita "Mitume" (Rejea Luka 6:13). Neno hili mara nyingi lilitumika kwa Yesu akitumwa kutoka kwa baba ( rejea Mathayo 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48; Yohana 4:34; 5:24, 30, 36, 37, 38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8,18,21,23,25; 20:21). Katika vyanzo vya Kiyunani, mtume alikuwa mtu aliyetumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, sawa na "balozi" (rejea 2 Wakorintho 5:20).

**MADA MAALUMU: UPELEKWA (** ***APOSTELLŌ*****)**

Hili ni neno la kiyunanila kawaida kwa "upelekwa" (yaani *apostellō*). Neno hili lina matumizi kadha ya kithiolojia:

1. Katika kiyunani cha sasa na kwa Wayahudi waliokuwa na elimu na viongozi wa dini, neno hili hutumiwa kama moja inayoitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, kitu kama kiingereza chetu "Balozi". (kama vile. 2 Kor. 5:20).

2. Injili daima zinatumia kitenzi hiki kwa Yesu kutumwa na baba yake, katika Yohana, linasikika zaidi kama Masihi (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48 na hasa Yohana 5:36, 38; 6:29, 57; 7:26; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8, 18, 21,23 25; 20:21 (Yote "*apostellō*" na KISAWE CHAKE *pempō* inayotumika katika mst. 21). Inatumika kwa Yesu kutuma waumini (kama vile. Yn 17:18; 20:2121 [Yote "*apostellō* na KISAWE CHAKE ni "*pempō*" katika Yohana 20:21]).

3. Agano Jipya lilituma jina "Mtume" kwa wanafunzi

    a. Mitume kumi na wawili wa mwanzo kama mzunguko wa kwanza kati ya wanafunzi wake.

(Marko 6:30; Luka 6;13; Matendo 1:2; 26)

b. Kundi maalumu la msaada la Mitume na watumishi wenzie.

1) Barnabasi (kama vile. Matendo 14:4, 14)
2) Andronicus na Junias (KJV, Junia , kama vile. Rum. 16:7)
3) Appollo (kama vile. 1 Kor. 4:6-9)
4) Yakobondugu wa Bwana (kama vile. Gal. 1:19)
5) Silvanus na Timotheo (kama vile. 1The. 2:6)
6) Bila shaka Tito (kama vile. 2 Kor. 8:23)
7) Bila shaka Epafrodito (kama vile. Efe. 2:25)

c. Zawadi inayoendelea katika kanisa (kama vile. 1 Kor. 12:28-29; Efe 4:11)

4. Paulo anatumia cheo hiki kwa ajili yake katika barua zake nyingi kama njia ya kuonesha mamlaka yake aliyopewa na Mungu kama mwakilishi wa Kristo. (kama vile. Rum. 1:1 1 Kor. 1:1; Gal. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; Tim. 1:1 2Tim. 1:1; Tito 1:1).

5. Tatizo tunalokumbana nalo kama waamini wa leo ni kwamba Agano Jipya halitafasiri hii zawadi inayoendelea inahusu nini au vipi inabainishwa kwa waamini. Bila shaka mtu apaswa kutofautisha kati kumi nambaili ya awali (# 3b) na matumizi ya baadaye (# 3b). Tazama Mada Maalumu: Msukumo na Mada Maalumu: Mwangaza. Kama mitume wa leo hawakusukumwa kuandika maandiko mengi matakatifu (yaani, kitabu cha Wayunani kanoni kimefungwa, kama vile. Yuda mst. 3; tazama. Mada Maalumu: kanuni ya kanisa) kisha kipi wanafanya tofauti na Manabii wa Agano Jipya na Wainjilisti (kama vile. Efe. 4:11) hapa kuna uwezekano wa mambo.

a. Waanzilishi wa kanisa la wamisionari huanza katika maeneo yasiyo ya uinjilisti (kutumika kama vile katika *Doache*)

b. Viongozi wa Wachungaji katika eneo Fulani au madhehebu.

c. ?

Napenda # 1.

▣**"Kristo"** Hili lilikuwa ni neno la Kiyunani sawa na lile la Kiebrania "Masihi" lililomaanisha "aliyepakwa mafuta." Lilihusisha"aliyeitwa na kuwezeshwa na Mungu kwa ajili ya jukumu fulani." Katika Agano la Kale makundi matatu ya vikundi vya viongozi: makuhani, wafalme, na manabii, walipakwa mafuta. Yesu alitimiza ofisi hizi zote za kupakwa mafuta (rejea Waebrania 1:2-3).

**MADA MAALUMU: MASIHI**

Ugumu katika kutafasiri neno hili ni kwa sababu ya matumizi tofauti kuhusiana na neno lenyewe "Masihi" au "aliyetiwa mafuta" (BDB 603, KB 645). Neno lilitumika katika kumwekea mtu mafuta maalumu kuonyesha wito wa Mungu na kumkabidhi majukumu ya uongozi.

1. Lilitumika kwa wafalme wa Kiyahudi (mf. 1 Sam. 2:10; 12:3; 24:6, 10;2 Sam. 19:21; 23;1; Zab. 89:51; 132:10, 17; Wim. 4:20; Hab. 3:13; "Malkia mtiwa mafuta" katika Dan. 9:25)
2. Lilitumika kwa makuhani wa Kiyahudi (yaani, "makuhani walitiwa mafuta," Kut. 29:7; mf. Law. 4:3, 5, 16; 6:15; 7:36; 8:12; bila shaka Zab. 84:9-10; na 133:2)
3. Lilitumika kwa makasisi, na Manabii (kama vile. Mwa. 26:7; 1 Nya. 16:22; Zab. 105:15, iliyomaanisha watu wa Agano kwa pamoja; yumkini Hab. 3:13)
4. Lilitumika kwa manabii (kama vile. 1 Fal. 19:16; yumkini 1 Nya. 29:22)
5. Lilitumika juu ya Koreshi (kama vile. Isa. 45 :1)
6. # 1 na # 2 umeunganishwa katika Zab. 110 na Zekaria 4.

7. Lilitumika kwa ujio maalumu wa Mungu, Ufalme wa Daudi kuleta enzi mpya ya haki
    a. uzao wa Yuda (kama vile. Gen. 49:10)
    b. nyumba ya Yesse (kama vile.2 Sam 7)
    c. utawala wa ulimwengu (kama vile. Zaburi 2; Isa. 9:6; 11:1-5; Mik. 5:1- 4 na kuendelea)
    d. Huduma kwa wahitaji (kama vile Isa. 61:1-3)

Mimi binafsi nimevutiwa na utambulisho wa neno "aliyetiwa mafuta" na Yesu wa Nazareti (kama vile.Yn. 1:41; 4:25) kwa sababu

1. kutambulishwa kwa ufalme wa milele katika Danieli 2 kipindi cha utawala wa nne
2. kutambulishwa kwa "mwana Adamu" katika Dan. 7:13 akipewa ufalme wa milele
3. maneno ya ukombozi wa Dan. 9:24, ambayo yanaashiria mwisho wa historia ya ulimwengu ulioanguka
4. matumizi ya Yesu ya kitabu cha Danieli katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14)

Lazima kukiri kuwa hii ni mada nadra katika Agano la Kale, bila shaka Dan. 9:25. Lazima pia ifahamike kuwa Yesu haingii sana katika maelezo ya jumla kuhusu Masihi katika Agano la Kale

1. hakuwa kiongozi katika Israeli
2. hakutiwa mafuta rasmi na kuhani
3. sio kama mwokozi wa Israeli
4. sio tu "mwana wa Adamu" lakini kwa mshangao "Mwana wa Mungu"

▣**"Yesu"** hili neno la Kiebrania lilimaanisha "YHWH anaokoa," "YHWH ni wokovu," "YHWH analeta wokovu." Ni sawa na jina la Agano la Kale "Yoshua." "Yesu" lilitoka katika neno la Kiebrania kwa ajili ya wokovu, "hosea," ikikamilishwa na jina la kiagano kwa Mungu, "YHWH" (angalia Mada Maalumu: Majina kwa ajili ya Uungu katika Wakolosai 1:3). Lilikuwa nii jina lililotolewa na Mungu kupitia malaika wa Bwana (kama vile Mathayo 1:21).

▣**"kwa mapenzi ya Mungu"** Tungo za Utangulizi huu inatumika katika 1 Wakorintho 1:1; 2 Kor. 1:1; Waefeso 1:1 na 2 Timotheo 1:1. Paulo alishawishika kwamba Mungu alimchagua yeye kuwa Mtume. Maana hii ya wito ilianza alipobadilishwa akiwa njiani kwenda Damaskasi (kama vile Mdo 9:1-22; 23:3-16; 26:9-18). Ufunguzi huu wa tungo unaweka msisitizo katika uelewa wa Paulo katika mamlaka aliyopewa itokayo kwa Mungu. Angalia Mada Maalumu: Mapenzi ya Mungu katika Waefeso 1:9.

▣**"Timotheo ndugu yetu"** Jina la Timotheo lilimaanaisha "aliyeheshimiwa na Mungu" au "amheshimuye Mungu." Alikuwa na mama Myahudi (kama vile Mdo 16:1; 2 Timotheo 1:5) na baba Myunani (Mdo 16:1). Alibadilishwa katika safari ya kwanza ya Paulo ya kimishionari ya kwenda Derbe/Listra (kama vile Mdo 16:1). Paulo alimualika yeye kujiunga na kikundi chake cha umishionari katika safari yake ya pili, yawezekana kuziba nafasi ya Yohana Marko (rejea Mdo 15:36-41). Paulo alimtahiri yeye ili aweze kusaidia kazi yake kati ya Wayahudi (rejea Mdo 16:3). Alikuwa mwakilishi wa Paulo mwaminifu, mwanafunzi na mkabilianaji wa ghasia (kama vile Mdo 16:1-17:14; 18:5-19:22; 20:4; Rum. 16:21; 1 Kor. 4:17; 16:10; 2 Kor. 1:1, 19; Fil 1:2; 2:19; Gal. 1:1; Filemoni. Kol. 1:4; na I na 2 Timotheo).
Anatajwa na Paulo katika barua kadhaa (kama vile2 Kor. 1:1; Fil. 1:1; 1 Wathesalonike 1:1; 2 Wathesalonike 1:1 na Filemon). Hii haimaanishi kufanya kazi kwa pamoja pekee, lakini uwepo wa Timotheo na salamu. Timotheo anaweza kuwa alifanya kazi kama mwandishi wa Paulo kama walivyofanya wakina Sila na Tikiko.

**1:2"Watakatifu"** "watakatifu" (*hagioi*) kithiolojia inafanana na neno la Agano la Kale "takatifu" (*kadosh*), ambayo inajumuisha "kuweka kando kwa ajili ya huduma ya Mungu" (kama vile 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Warumi 1:1; Waefeso 1:1; Wafilipi 1:1). Lina wingi katika Agano Jipya isipokuwa wakati mmoja katika Wafilipi 4:21; hata hapo inatumika kama andiko la jumla. Kuokolewa ni kuwa sehemu ya jumuiya ya imani, familia ya waaminio, inayomaanisha kutumikia (kama vile 1 Kor 12:7).
Watu wa Mungu ni watakatifu kwasababu ya shutumu ya haki ya Yesu (kama vile Warumi 4 na 2 Wakorintho 5:21). Ni mapenzi ya Mungu kwamba waishi maisha matakatifu (kama vile Kol. 1:22; 3:12; Waefeso 1:4; 2:10; 4:1; 5:27; 1 Petro 1:16). Waamini wana vyote, kutangazwa watakatifu (kutakaswa kinafasi) na kuitwa katika maisha ya utauwa (kutakaswa kunakoendelea). Angalia Mada Maalumu: Utakaso katika Waefeso 1:1

**MADA MAALUMU: WATAKATIFU**

Huu ni usawa wa Kiyunani wa neno la Kiebrania *kadosh* (NOUN, BDB 871; VERB, BDB 872, KB 1066-1067; tazama Mada Maalum: Takatifu), lililo na maana ya msingi ya kumweka mtu katia usawa, kitu fulani, au baadhi ya sehemu tofauti na matumizi ya YHWH yaliyojitenga. Hili linadokeza dhana ya Kiingereza ya "wekwa wakfu." Israeli lilikuwa "taifa takatifu" la YHWH (kama vile 1 Pet. 2:9, ambayo inanukuu Kut. 19:6). YHWH anaweka mbali na ubinadamu kwa kutumia asili Yake (milele, Utatakatifu usioumbwa) na sifa Yake (ukamilifu wa maadili). Yeye ni kipimo ambapo vitu vyote vinapimwa na kuhukumiwa. Yeye yu kila mahali, Mtakatifu, Mtakatifu wa Watakatifu.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa ushirika, lakini anguko (Mwanzo 3) lilisababisha kikwazo cha mahusiano na maadili kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi. Mungu alichagua kuurejesha ufahamu Wake wa uumbaji; hivyo, Anawaita watu Wake kuwa "watakatifu" (kama vile Law. 11:44; 19:2; 20:7,26; 21:8). Kwa imani uhusianao wa YHWH na watu Wake ukawa mtakatifu kwa nafasi zao za kiagano ndani Yake, lakini pia wanaitwa kuishi maisha matakatifu (tazama Mada Maalum: Utakaso, kama vile Mt. 5:48; Efe. 4:1,17; 5:2-3,15; 1 Pet. 1:15).

Huku kuishi kitakatifu kunawezekana kwa sababu waamini wamekubaliwa kwa utimilifu na kusamehewa kupitia (1) Maisha ya Yesu na (2) kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya fikra na mioyo yao. Hili linahimarisha hali ya ukinzani kwa waamini:

1. kuwa watakatifu kwa sababu ya haki ya Kristo iliyowekwa ndani yao (kama vile Warumi 4)
2. walioitwa kuishi kitakatifu kwa sababu ya uwepo wa Roho (tazama Mada Maalum: Utakaso)

Vaamini ni "watakatifu" (*hagioi*) kwa sababu ya

1. mapenzi ya yule Aliye Mtakatifu (Baba, kama vile Yohana 6:29,40; 1 Pet. 1:15-16)
2. kazi ya Mwana aliye Mtakatifu (Yesu, kama vile 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 1:18-21)
3. uwepo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani (kama vile Rum. 8:9-11,27)

Mara nyingi katabu cha Agano Jipya kinawarejelea watakatifu kama WINGI (isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lajkini muktadha unalifanya neno hili kuwa WINGI). Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia, mwili, ujenzi! Imani ya kibiblia huanza na mapokezi binafsi, bali suala la ndani ya ushirika wa pamoja. Kila mmoja wetu amekirimiwa kama vile 1 Kor. 12:11) kwa ajili ya afaya, ukuaji, na manufaa ya Mwili wa Kristo—kanisa (kama vikle 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili kutumika! Utakatifu ni sifa ya familia!

Hili linakuwa adimu kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 9:13,32,41; 26:10; Rum. 1:7; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2) na njia ya kuonyesha huduma kwa wengine (kama vile Rum. 12:13; 16:2; Efe. 1:15; Kol. 1:4; 1 Tim. 5:10; Ebr. 6:10). Paulo alichukua wakati wa kipekee wa kujitoa kwa makanisa Mataifa kwa watu wahitaji waliokuwa ndani ya Kanisa Mama ndani ya Yerusalemu (kama vile Rum. 15:25-26; 1 Kor. 16:1; 2 Kor. 8:4; 9:1).

▣**"Ndugu waaminifu"** Katika kitabu kilichoandikwa kukabiliana na kikundi cha mafundisho cha walimu wa uongo, sifa hii ni muhimu! Paulo aliamini kwamba kanisa lilikuwa limebaki aminifu kwa Injili ya Yesu Kristo, aliyopewa Paulo, ikakabidhiwa kwa Epaphra, wakapewa wao!
Maneno, "imani," "kusadiki," na kuamini vyote vina asili ya mzizi mmoja katika Kiyunani *pistis(*nomino) na *pisteuō (*kitenzi). Msingi wa msisitizo wa kwanzaupo katika uaminifu wa Mungu, sio ari au udhati wa mwitikio wa kibinadamu. Waaminio lazima kupokea na kuamini tabia ya kuaminika Kwake na ahadi za ke za milele. Ufunguo upo katika nia ya imani ya mwamini, na sio kiwango cha hiyo imani yake (kama vile Mathayo 17:20; Luka 17:6). Ukristo ni mwititio wa kwanza wa kuanzisha toba/mgeuko unaofuatiwa na mtindo wa maisha wa uaminifu. Imani ya kibiblia ni mfululizo uchaguzi wa toba wa mwanadamu, imani, utii na ustahimilivu. Uaminifuy wa Mungu

unazalishwa na watoto Wake. Taswira ya Mungu (kama vile Mwanzo 1:26-27) inarejeshwa na ushirika wa karibu sasa unawezekana!

**MADA MAALUMU: Imani, amini au Sadiki (Pistis [nomino], *Pisteuō,* [kitenzi] *Pistos [*kivumishi]**

A. Hili ni aina ya neno muhimu katika Biblia (kama vile. Ebr. 11:1,6). Lilikuwa ni somo la Yesu katika mahubiri ya awali (kama vile. Mk 1:15). Kiwastani kuna mahitaji mapya mawili ya agano: toba na imani (Mk 1:15; Mdo. 3:16, 19; 20:21)

B. Asili na historia yake ya maneno haya
   1. Neno "imani" katika Agano la Kale lilimaanisha mtiifu, mwaminifu au mwaminifu wa kutumainiwa na yalikuwa ni maelezo ya asili ya Mungu na si yetu.
   2. Linatokana na neno la Kiebrania (*emun, emunah*, BDB 53, yaani., Hab. 2:4), ambalo mwanzo kabisa lilimaanisha "kuwa na uhakika au imara." Kuitumikia imani ni
      a. Kumkaribisha mtu (yaani., imani binafsi, sadiki, kama vile. E.1.hapo chini)
      b. Kuamini imani kuhusu mtu (yaani., maandiko, kama vile. E.5.hapo chini)
      c. Kuishi maisha kama ya mtu huyo (yaani., mfano wa Kristo)

C. Matumizi yake katika Agano la Kale
   Lazima isisitiziwe kuwa imani ya Ibrahim ilikuwa si kwa ajili ya Masiha ajaye, lakini ni kwa ahadi ya Mungu ya kwamba atapata mototo na uzao (kama vile Mwa. 12:2-5; 17:4-8; Rum. 4:1-5). Ibrahim aliikubali ahadi hii kwa kumwamini Mungu (angalia Mada Maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika Agano la Kale) na neno lake. Bado anamashaka na kuhusika juu ya ahadi hii, ambayo ilimchukua miaka kumi na mitano kutimizwa. Imani yake isiyo kamili, hata hivyo, alikubaliwa na Mungu. Mungu anapenda kufanya kazi na mwanadamu mwenye mapungufu anayejongea kwake na katika ahadi zake kwa imani, hata kama kwa kipimo cha chembe ya haradari (kama vile. Mt. 17:20) au imani mchanganyiko (kama vile. Mark 9:22-24)

D. Matumizi yake katika Agano Jipya
   Neno "kuamini" linatoka katika neno la Kiyunani *pisteuō* au nomino *pistis,* ambayo yanatafasiliwa kwa Kiingereza "kuamini" "amini" au "imani." Kwa mfano, nomino haijitokezi katika injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna uwalakini katika uhalisia wa uwajibikaji wa kundi kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha. Mifano mwingine wa matumizi ya kubabiya ya neno hili "kuamini" ni katika Yohana 8:31-59 na Matendo 8:13, 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi ya uwajibikaji wa awali. Lazima ifuatishwe na mchakato wa uwanafunzi (cf. Mt. 13:20-23, 31-32; 28:19-20)

E. Matumizi yake ikiwa na vivumishi
   1. *eis* inamaanisha "ndani ya." Muundo huu wa kipekee unasisitizia waumini kuweka imani zao kwa Yesu
      a) ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
      b) ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45,48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
      c) ndani yangu (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
      d) ndani ya mwanaye (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
      e) ndani ya Yesu (Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
      f) ndani ya nuru (Yohana 12:36)
      g) ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
   2. *ev* inamaanisha "katika" kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mark 1:15; Mdo 5:14
   3. *epi* ikimaanisha "katika" au "juu ya" kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
   4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
   5. *hoti* likimaanisha "kuamini kwamba," inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
      a) Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
      b) Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
      c) Yesu katika Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)

d) Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
e) Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
f) Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
g) Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
h) Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30
i) Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
j) Tutaishi naye (Rum. 6:8)
k) Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

▣**”katika Kristo”** Hii ni tungo ya kisarufi iitwayo kihusishi cha mahali (ya tufe). Hii ilikuwa ni njia aipendayo zaidi Paulo ya kuwaelezea Wakristo. Kama Waaminio tunaishi na kutembea na kuwa tulivyo katika Yeye (kama vile Mdo 17:28)! Yeye ndiye asili na chanzo cha baraka zetu zote za rohoni. Paulo anatumia tungo hii mara 64 (“ndani ya Kristo,” “katika Yeye,” “katika pendo lake”). Angalia maelezo kamili katika Waefeso 1:4

▣**”Neema iwe kwenu na amani”** Salamu ya kawaida katika barua za Kiyunani ilikuwa neno “salamu” (*charein*, kama vile Mdo 15:23; 23:36; Yakobo 1:1). Kitabia Paulo aliibadilisha hii kuwa na mfanano sawa lakini neno la Kikristo, neema, (*charis*). Wengi walidhania kwamba Paulo alikuwa kwa namna fulani akiunganisha salamu ya Kiyunani na salamu ya kiebrania, amani (*shalom*). Ingawa hii ni nadharia inayovutia, inawezekana kusoma sana katika aina hii tungo ya utangulizi wa Paulo (kama vile (Warumi 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2; Wafilipi 1:2; na Filemoni 3). “Neema lilikuwa neno maalumu lililoeleza tabia ya Mungu ya Upendo na Rehema. Wanadamu wako sawa na Mungu kwasababu ya Yeye alivyo, si kwasababu ya wao walivyo. Ni wema, fadhili, upendo, msamaha, kutokuwa mwingi wa hasira, kujaa katika rehema na huruma inatyotengeneza tumaini pekee juu ya mwanadamu aliyeanguka (kama vile Kutoka 34:6-7; Nehemia 9:17; Zaburi 103:8-14; Yoeli 2:13; Mika. 6:18-20)! Ukristo umeweka mizizi katika sifa ya Mungu asiyebadilika (kama vile Malaki 3:6; Yakobo 1:17), kazi iliyomalizika ya Yesu Kristo (kama vile Marko 10:45; 2 Kor 5:21) na huduma ya Roho (kama vile Yohana 14:25-26; 16:7-15).“amani” ni matokeo ya uelewa wa tabia ya Mungu na ahadi ya Injili (kama vile Yohana 14:27; 16:33). Amani ni furaha ya ndani na uthabiti kutoka katika nje na mazingira, mafundisho ya uongo yavurugayo au dhiki (kama vile Wafilipi 4:7; Wakolosai 3:15).

▣**”Mungu wa Baba Yetu”** Usomaji huu unapatikana katika maandiko ya kale ya Kiyunani B, D, K, L Vulgate ya kale, Peshitta na Coptic na maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Origen na Chrysostom. Maandiko א, A, C, G inaongeza “na bwana wetu Yesu Kristo.” Tungo inawasilisha katika Wakolosai 1:3, ilikuwa ni tungo ya kawaida ya Paulo katika kufungua maombi (kama vile Warumi 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2; Gal. 1:3; Wafilipi 1:2; Wafilipi 1:2; 2 Wathesalonike 1:2; 1 Timotheo 1:2; 2 Timotheo 1:2 na Tito 1:4). UBS[4] inatoa usomaji mfupi kwa alama “A” (hakika).
“Baba” haitumika kwa namna ya kizazi cha kuzaa kwa njia za kujamiiana au mfulululizo wa mpangilio, bali familia yenye uhusiano wa karibu sana. Mungu alichagua maneno ya familia kujifunua mwenyewe kwa uanadamu (kama vile Hosea 2-3, ambapo Mungu anaoneshwa kama mwenye mapenzi, mpenzi mwaminifu, na sura ya 11 ambapo anaoneshwa kama baba na mama).
Uungu wa ufunuo sio kianzilishi au chanzo cha usababishi wa falsafa ya Kiyunani, lakini Baba wa Kristo Yesu. Biblia sio falsafa yenye mantiki/akili za kibinadamu bali imejifungamanisha yenyewe na Uungu, ufunuo ambao hauwezi kugundulikana kwa namna ya uchambuzi wa kibinadamu.

**MADA MAALUMU: BABA**

Agano la Kale linaanzisha neno mbadala la ndani la Mungu kama Baba. (tazama Mada Maalum: Ubaba wa Mungu):

1. Taifa la Israel daima linaelezwa kama “mwana” wa YHWH (kama vile. Hos. 11:1; Mal. 3:17)
2. Hata mwanzoni kabisa mwa kitabu cha Kumbukumbu la torati mfanano wa Mungu kama Baba umetumika (1:31)

3. Katika kumbukumbu la torati 32 Israeri inaitwa “Mwana wake” na Mungu anaitwa “Baba yako”
4. Ufananisho huu unatajwa katika Zab. 103:13 na kuendelea katika Zab. 68:5 (baba wa yatima)
5. Lilikuwa la kawaida katika manabii (kama vile. Isa. 1:2; 63:8; Israeli kama mwana, Mungu kama Baba, 63:16; 64:8; Yer. 3:4, 19; 31:9).

Yesu alizungumza Kiaramu, ikimaanisha kuwa kuna sehemu nyingi ambapo “Baba” anaonekana, ni *Pater* yule wa Kiyunani, na linaweza kuwa linaakisi neno *Abba* la Kiaramu (kama vile. Marko 14:36). Neno hili la kawaida “Baba” au “Papa” linaonyesha ukaribu uliopo wa Yesu na Baba. Udhihilisho wake huu kwa wafuasi wake pia kunahamasisha ukaribu wetu na Baba. Neno “Baba” lilitumika kidogo sana katika Agano la Kale kwa YHWH, lakini Yesu analitumia daima na kwa kulieneza. Ni uthibitisho mkubwa wa uhusiano mpya wa Waamini na Mungu kupitia kwa Kristo (kama vile. Mathayo 6:9)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 1:3-8**

**[3] Twamshukuru Mungu, Baba yake Bwana wetu Yesu Kristo, siku zote tukiwaombea; [4] tangu tuliposikia habari za imani yenu katika Kristo Yesu, na upendo mlio nao kwa watakatifu wote; [5] kwa sababu ya tumaini mlilowekewa akiba mbinguni; ambalo habari zake mlizisikia zamani kwa neno la kweli ya Injili; [6] iliyofika kwenu, kama ilivyo katika ulimwengu wote, na kuzaa matunda na kukua, kama inavyokua kwenu pia, tangu siku mlipoisikia mkaifahamu sana neema ya Mungu katika kweli; [7] kama mlivyofundishwa na Epafra, mjoli wetu mpenzi, aliye mhudumu mwaminifu wa Kristo kwa ajili yenu; *8* naye alitueleza upendo wenu katika Roho.**

**1:3-8** Mistari ya 3-8 ni sentensi moja katika Kiyunani ambayo humaanisha ni ombi moja la shukrani lililohimiliwa kwa ajili ya imani ya Kanisa katika Kristo. Maombi ya ufunguzi ya shukrani kwa ajili ya wapokeaji ilikuwa ni jambo la kawaida katika barua za Kiyunani. Katika Barua hii Paulo ana maombi ya ufunguzi ya aina mbili (yaani Wakolosai 1:3-8 na Wakolosai 1:9-14).

**1:3”asante”** “Asante” ni maudhui yanayojirudiarudia katika barua hii (kama vile Wakolosai 1:12; 2:7; 3:15; 4:2), kama “furaha” iko katika barua kwa Wafilipi. Kumbuka kwamba Paulo alikuwa amefungwa Rumi na kanisa la Wakolosai lilikuwa lilkipitia nyakati ngumu. Angalia Mada Maalumu: Shukrani katika Wakolosai 4:2.

▣**”Baba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo”** Angalia Utatu katika Wakolosai 1:3 na 8. Angalia Mada Maalumu katika Waefeso 1:3.

▣**”Bwana”** Neno “bwana” (*kurious*) linaweza kutumika katika namna ya jumla au katika namna ya kithiolojia. Linaweza kumaanisha “mheshimiwa” “mkuu” (kama vile Yohana 4:11,15,19,49; 5:7; 12:21; 20:15), “Mheshimiwa,” “mmiliki,” “mume,” au “mwanadamu kamili mwenye Mungu” (mfano Yohana 4:1; 6:34,68; 11:2,3,12,21,27,34,39). Mfano mzuri wa matumizi yote mawili katika muktadha mmoja ni Yohana 9:36 na 9:38.
Matumizi ya Agano la Kale ya neno hili (*adon*) lilitoka kutokana na hali ya waalimu wa injili kototaka kutamka jina la kiagano la Mungu, YHWH, kutoka katika kitenzi cha kiebrania “kuwa/kufanyika” (kama vile Kutoka 3:14). Walikuwa na hofu ya kuvunja sheria iliyosema “Usilitamke bure Jina la Bwana Mungu wako” (kama vile Kutoka 20:7, Kumbukumbu la Torati 5:11) walifikiri kama wasipolitamka, watakuwa hawajalitaja bure jina la Mungu. Hivyo walitafuta mbadala wake kwa neno la kiebrania Adon, ambalo lilikuwa na maana inayofanana na neno la Kiyunani, *Kurious* (Bwana)
Waandishi wa Agano Jipya walilitumia neno hili kufunua Uungu wa Kristo. Tungo “Yesu ni Bwana” ilikuwa ni ukiri kwa umma wa imani na kanuni ya ubatizo wa kanisa la mwanzo (kama vile Warumi 10:9-13; 1 Wakorintho 12:3; Wafilipi 2:11).

**MADA MAALUMU: MAJINA YA UUNGU**

Huu ulikuwa ni usemi wa kawaida wa Agano Jipya kwa uwepo binafsi na nguvu itendayo kazi ya utatu wa Mungu katika kanisa.Haikuwa kanuni ya miujiza, bali rufaa kwa tabia ya Mungu. Daima, usemi huu unamhusu Yesu

kama Bwana (kama vile Flp.2:11)

1. Weredi wa imani ya mtu katikaYesu wakati wa ubatizo (kama vile Rum 10:9-13; Mdo. 2:38; 8:12,16; 10:48; 19:5; 22:16; 1 Kor 1:13; 15; Yak. 2:7)
2. katika upungaji pepo, (kama vile Mt. 7:22; Mk. 9:38; Luka 9:49; 10:17; Mdo. 19:13)
3. katika uponyaji (kama vile Mdo 3:6,16; 4:10; 9:34; Yak. 5:14)
4. katika tendo la huduma (kama vile Mt. 10:42; 18:5; Luka 9:48)
5. katika muda wa kutekeleza nidhamu kanisani (kama vile Mt. 18:15-20)
6. wakati wa kuhubiria watu wa Mataifa (kama vile Luka 24:47; Mdo 9:15; 15:17; Rum.1:5)
7. katika maombi (kama vile Yn.14:13-14; 15:2,16; 16:23; 1 Kor 1:2)
8. kama njia ya kurejea Ukristo (kama vile Mdo 26:9; 1Kor 1:10; 2 Tim 2:19; Yak. 2:7; 1 Pet. 4:14)

Chohote tukifanyacho kama wahudumu, wasaidizi, waponyaji, watoa mapepo, n.k, tunafanya hivyo kwa tabia yake, nguvu Zake, upaji Wake - katika jina Lake

▣**"siku zote nikiwaombea"** "siku zote" inaweza kufanana kisarufi na "kuomba"(NASB, NKJV, NJB) au "asante" (NRSV,TEV). Maombi na shukrani haviwezi kutenganishwa kwa kuunganishwa katika thiolojia ya Paulo na utendaji kazi wake. Paulo aliwaombea (kama vile Wakolosai 1:9; Waefeso 1:16) na aliwataka kwamba wamuombee (kama vile Wakolosai 4:3; Waefeso 6:18; 1 Wathesalonike 5:25). Angalia Mada Maalum: Maombi ya Maombezi katika Wakolosai 4:3. Paulo analitaja hili tena katika Wakolosai 1:9. Inaonekana kuwa ni aina mbili za maombi yanayowekwa pamoja.

**1:4" tangu tuliposikia"** Kiwakilishi cha wingi kilirejerea Paulo na timu yake ya Umisheni. Walikuwa wamesikia kuhusu matatizo ya walimu wa uongo na imani ya waaminio wa Epafra (kama vile Wakolosai 1:7, 8) aliyeanzisha kanisa lake.

**1:4-5"imani…..upendo…tumaini"** Hii ilikuwa ni seti ya vitu vitatu ya thiolojia ya Paulo aliyoipenda sana (kama vile Warumi 5:2-5; 1 Kor. 13:13; Gal. 5:5-6; 1 Wathesalonike 1:3; 5:8). Inaelezea ujasiri ambao waaminio wanao kote kwa wakati huu (imani) na katika utimilifu wa siku zijazo (tumaini). Ujasiri huu unatakiwa kuuishi kila siku na katika upendo wa kila mara.

**1:4"imani yenu"** Neno hili (*pistis*) linaweza likawa linaashiria vitu vya aina yake vya aina tatu

1. Historia yake ya nyuma ya Agano la Kale ilimaanisha "uaminifu" au "inayoaminika" kwahiyo, ilitumika na waamini kuishi maisha ya utauwa.
2. Ilitumika na waamini kukubali au kupokea karama za bure za Mungu za msamaha ndani ya Kristo.
3. Ilitumika katika namna ya jumla ya mafundisho ya Mkristo au kweli kumuhusu Yesu (yaani "imani," kama vile Mdo 6:7 na Yuda 1:3, 20).

Katika baadhi ya vifungu vya habari ni ngumu kubaini alimaanisha nini. Angalia Mada Maalumu: Imani, Amini, Sadiki katika Wakolosai 1:2.

▣**"katika ya Kristo Yesu"** Kauli ya kawaida Paulo aliyoitumia kwa ajili ya imani ilikuwa "ndani" (*eis*) ya Kristo, iliyomzungumzia kama kielelezo cha imani ya mtu, lakini hapa kauli ni "ndani" (*en*) iliyomaanisha Yesu kama tufe la kuwepo kwake (kama vile Wakolosai 1:2; Mdo 17:28)

▣**"upendo mlionao kwa watakatifu wote"** Imani kwa Mungu inaelezwa katika upendo kuelekea wengine, hasa wale wa nyumba ya imani (kama vile Wagalatia 6:10). Matumizi ya neno "wote" ni muhimu katika mazingira yaliyovurugwa na hali ya kujitenga kwa kujiona bora kwa walimu wa uongo. Waaminio lazima wawe na uwezo wa kutofautisha kati ya walio watakatifu na wale wasio! Kwa "watakatifu" angalia Mada Maalum katika Wakolosai 1:2.

**1:5 "tumaini"** Paulo alitumia neno hili katika baadhi ya namna mbalimbali ila zinazofanana. Mara nyingi ilihusianishwa na kukamilishwa kwa imani ya waaminio. Hii inaweza kuelezewa kama utukufu, uzima wa milele, kilele cha wokovu, Kuja Mara ya Pili, n.k. kukamilishwa ni hakika, lakini kipengele cha muda ni cha baadaye na

kisichojulikana. Tumaini mara nyingi ilihusianishwa na "imani" na "upendo" (kama vile Warumi 5:2-5; 1 Kor. 13:13; Wagalatia 5:5-6; Waefeso 4:2-5; 1 Wathesalonike1:3; 5:8).

**MADA MAALUMU: TUMAINI**

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano., 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

▣**"mliloliweka akiba mbinguni"** Hii ilikuwa ni sitiari kwa ulinzi wa ki-Ungu wa tumaini la waaminio (kama vile 2 Timotheo 4:8; 1 Petro 1:4).
Walimu wa uongo wasingeweza kuadhiri kutimilizwa kwa wokovu wa waamini (tumaini).

▣**"mlizisikia zamani"** Hii ni Kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usio timilifu ya neno ambatani, "kusikia" na "kabla." Hii ilihusu mahubiri ya injili ya Epafra, ambayo Wakolosai walikuwa kibinafsi tayari wameitikia kwa imani. Waamini lazima wasikie, waitikie, watii na kustahimili.

▣**"kwa neno la kweli ya Injili"** Tungo hii inaweza ikaeleweka katika njia kadhaa

1. Kwa hati rasmi walisikia kweli kwa njia ya injili
2. Kwa muda walikuwa walishasikia injili
3. Kwa mrejeo sawa kama njia ya kutambua injili kama neno la ukweli

Angalia namna katika Wakolosai 1:6 injili inatabia kama "neema ya Mungu katika kweli." Angalia Mada Maalum: Kweli katika maandiko ya Paulo katika Waefeso 1:13.

**1:6" katika ulimwengu wote"** Hii inajulikana kama ulimwengu kati ya wagiriki na Warumi. Hii ilikuwa ni kutia chumvi kwa kawaida ya Agano Jipya, ambalo kwa sababu ya Mathayo 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo 1:8, ilikuwa ni dhahiri.
Neno la Kiyunani (*kosmos*) lilikuwa na matumizi kadhaa. Lingemaanisha

1. Sayari hii ya mwili inayoshikika
2. Wanadamu waishio katika uso wa sayari hii
3. Falsafa, miundo ya kiserikali, taasisi za kielimu na mifumo ya dini ya mwanadamu aliyeanguka inayowaruhusu kufanya kazi kama wao kutoka kwa Mungu

**MADA MAALUMU:MATUMIZI YA PAULO YA *KOSMOS* (ULIMWENGU)**
Paulo analitumia neno *kosmos* kwa njia tofauti tofauti.

1. Mpangilio wa vitu vyote vilivyoumbwa (kama vile Rum. 1:20; Efe. 1:4; 1 Kor. 3:22; 8:4,5)
2. Sayari hii (kama vile 2 Kor. 1:12; Efe. 1:10; Kol. 1:20; 1 Tim. 1:15; 3:16; 6:7)
3. Wanadamu (kama vile Rum. 3:6,19; 11:15; 1 Kor. 1:27-28; 4:9,13; 2 Kor. 5:19; Kol. 1:6)
4. Kuwa pamoja na kutenda kwa wanadamu mbali na Mungu (kama vile 1 Kor. 1:20-21; 2:12; 3:19; 11:32; Gal. 4:3; Efe. 2:2,12; Flp. 2:15; kol. 2:8,20-23). Inafanana na matumizi ya Yohana (yaani., 1 Yohana 2:15-17)
5. Muundo wa ulimwengu wa sasa (kama vile 1 Kor. 7:29-31; Gal. 6:14; inafanana na Flp. 3:4-9, mahali ambapo Paulo anaelezea muundo wa Kiyahudi)

Kwa baadhi ya namna huu mwngiliano na ni vigumu kuainisha kila matumizi. Neno hili, kama yalivyo mengi katika mawazo ya Paulo, yaweza elezewa kwa mazingira ya haraka na sio maelezo yaliyotengenezwa awali. Misamiati ya Paulo ilikuwa ni myepesi (cf. *James Stewart's A Man in Christ*). Hakuwa anajaribu kutengeneza msamiati wa kithiolojia, lakini akimtangaza Kristo.

▣**"mara zote mkizaa matunda na kukua"** Hizi zote ni kauli endelevu za wakati uliopo. Ya kwanza ni irabu ya kati na ya pili irabu tendwa lakini katika muktadha huu hakuna utofauti wa kithiolojia inayohusishwa, lakini haitoi vkielelezo uwiano wa agano wa binadamu na matendo ya ki-Ungu. Kuzaa matunda ni ishara ya uongofu (kama vile Kol. 1:10; Mt 13:1-23; Yoh. 15:16; Gal. 5:22-23; Yak 2:14-26).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kuelewa"** |
| **NKJV** | **"kujua"** |
| **NRSV** | **"kufahamu"** |
| **TEV** | **"kuja kujua"** |
| **NJB** | **"kutambua** |

Hii ni ya kina ya sura ya kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu ya neno la Kiyunani *epignōskō* inayohusisha neno "kwa ukamilifu na kujua kunakotokana na uzoefu wa mtu." Wakolosai walipokea injili ambayo ni vyote mtu na kweli (kuunganisha maana ya "kujua" kutoka Kiebrania na Kiyunani). Huu ulikuwa ni mwitikio wa Paulo kwa uongo wa wapotoshaji uliokuwa na msisitizo wa maarifa ya kibinadamu (kama vile Wakolosai 1:9, 10)
▣**"neema ya Mungu katika kweli"** Hii inamaanisha injili ya Yesu Kristo, ambayo mwishowe na kuelezea kwa ukamilifu asili na tabia ya Uungu kwenye mbio za mwanadamu. Kilele cha tumaini cha waaminio kiki katika tabia ya Mungu isiyobadilika ya rehema (yaani Malaki 3:6)
Neno la Kiyunani "neema" (*charis*) lilikuwa katika Kiyunani cha lugha ya Koine (200 K.K – 200 B.K) na maandiko ya Agano la Kale la Kiyunani (250-100 K.K) katika namna mbalimbali kadhaa ziburudishazo, zenye kupendeza, neema, suala la uthibitisho, faida, tendo la kibali au kukidhiwa. Katika Agano Jipya kimsingi ilianza kutumika kwa wasiostahili, upendo usio na vigezo na rehema ya utatu wa Mungu ambayo inatoa haki na kurejesha ushirika kwa anguko la mwanadamu (kama vile Waefeso 4:4-7). Msisitizo siku zote ilikuwa katika kustahili kwa mtoaji (Mungu). Yote yaliyotakiwa Mungu alitoa! Yote ambayo mtu aweza kufanya yanaweza kukidhiwa (kama vile Waefeso 2:8-9)!
Kwa "kweli" angalia Mada Maalum: "Kweli" ndani ya Maandiko ya Paulo katika Waeeso 1:13.

1:7"Epafra" (kama vile Wakolosai 4:12-13; Filemon 23). Alikuwa mwanzilishi wa makanisa matatu (Kolosai, Hierapolis, na Laodikia) katika bonde la mto Lycus, na uwakilishi wa Paulo (Wakolosai 1:7). Yawezekana aligeuzwa wakati wa Paulo alipokaa katika Efeso (kama vile 19:10). Jina lake lilikuwa ufupisho wa Epafrodito ambalo lilikuwa kwa asili likifanana na mungu mke Afrodito. Mtu mwingine kwa jina hili hili anatajwa katika Wafilipi 2:25; 4:18. Hata hivyo, alikuwa akitokea sehemu nyingine tofauti kijiografia.

**NASB** **"mtumwa mwaminifu wa Kristo kwa niaba yetu"**

| | |
|---|---|
| **NKJV, NRSV** | **"mhudumu mwaminifu wa Kristo kwa niaba yenu"** |
| **TEV** | **"mtendakazi mwaminifu wa Kristo kwa niaba yetu"** |
| **NJB** | **"msaidizi mwaminifu kwa ajili yetu kama mtumwa wa Kristo"** |

Maandiko ya kale ya Kiyunani yanatofautiana katika viwakilishi. Mengine yana "yetu" na mengine yana "yenu." "yetu" inaonekana kimaandiko kuwa bora kwasababu inapatikana katika maandiko ya kale ya Kiyunani $P^{46}$, א*, A, B, D*, F, and G. Lakini wanataaluma wa United Bible Society walijisikia "yenu" kuwa halisi kwasababu ya sehemu yake katika kanisa la kwanza la mababa na Tafsiri za kwanza za Kilatini, Kiaramaiki na tafsiri za Kikoptiki (kama vile Bruce M. Metzger, *A Textual Commentary on the Greek New Testament,* kurasa za 619-620).

**1:8 "upendo wenu katika Roho"** Hii kwa mshangao, ni rejea pekee ya Roho Mtakatifu katika barua ingawa Yupo, na kiukweli anaelezewa katika Wakolosai 1:9 na "kukaa ndani" katika Wakolosai 3:16. Kuelezewa waziwazi kwa Roho kuna sababisha upendo labda

1. Waaminio wengine
2. Paulo na timu yake ya umisheni
3. Epafra
4. Vyote hapo juu na hata waliopotea

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 1:9-14**
**[9] Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; [10] mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; [11] mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha; [12] mkimshukuru Baba, aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru. [13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; [14] ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;**

**1:9-20** hii ni moja ya sentensi katika Kiyunani. Wakolosai 1:9-12 ni maombi ya Paulo kwa waaminio. Wakolosai 1:13-14 inafunua kitu ambacho Baba amefanya kwa waaminio kupitia mwana. Mstari wa 15-18 yawezekana ni nukuu kutoka katika tenzi za wakristo wa kwanza au kauli ya kukiri ikihusianishwa na huduma ya mwana (yaani tenzi zingine ziwezekanazo, kama vile Wafilipi 2:6-11, 1 Timotheo 3:16, 2 Timotheo 11-12). Hii ni moja ya ukiri wa elimu ya Kikristo katika maandiko ya Paulo (linganisha na Wafilipi 2:6-11).

**1:9" tuliposikia habri zake"** Paulo hakuanzisha kanisa, wala hakujua washirika wake yeye binafsi. Alisikia habari ya imani yao na upendo kutoka katika mwanzilishi wake, Epafra (kama vile Wakolosai 1:7-8).

▣**"hatuachi kufanya maombi na dua"** Wingi wake unamaanisha kwa (1) Paulo mwenyewe (yaani wingi wa kihariri) au (2) Paulo na timu yake ya umisheni. Viongozi wanatakiwa mara kwa mara kug'ag'ania kundi lao kwa Bwana.
Angalia Mada Maalum: Maombi ya Maombezi katika Wakolosai 4:3

▣**"ili kwamba mjazwe"** Kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu. Waamini hawawezi kujijaza wenyewe, lakini lazima waruhusu na kushirikiana na Roho (Waefeso 5:18)
"kujazwa" ni kitenzi kikuu cha Wakolosai 1:9-12. Ni moja ya mahitaji mawili ambayo Paulo aliyaomba kwa baba kwa niaba ya makanisa ya Kolosai. Lingine ni kuenenda kwao kunakostahili (Wakolosai 1:10). Chunguza utaona anaunganisha maarifa ya Mungu na mtindo wa maisha ya ki-Mungu (kama vile Waefeso 4:1, 17; 5:2, 15). Imani bila matendo imekufa (kama vile Yakobo 2:14-26).

▣**"maarifa ya mapenzi yake"** Ujazo wa maarifa haya (*epignōskō*, yaani maarifa yatokanayo na ujuzi wa mtu, tazama mstari wa 6) ni injili. Injili ni (1) mwili wa kweliwa kuaminiwa; (2) mtu wa kupokea; na (3) maisha kama ya

kwamba ya kuishi. Mapenzi ya Mungu ni kwamba mtu mmoja mmoja kwa binafsi aitikie kwa Kristo (kama vile Yohana 6:29, 40) aliye lengo la wote “hekima ya kiroho na ufahamu”
Mstari huu ni tamthiliya katika thiolojia ya walimu wa uongo. Hii inathibitishwa na (1) matumizi ya Paulo ya “kujazwa (*plerōma*), moja ya maneno yaliyopendwa na wenye ujuzi kwa *aeons* kati ya mungu mkuu na viwango vya kimalaika na (2) msisitizo wao kwenye maarifa ya siri (Wakolosai 2:3). Kwa Paulo, ukamilifu wote na maarifa yalikuwa ndani ya Kristo aliyekuwa hekima ya Mungu (*Sophia*, kama vile Wakolosai 1:28; 2:3,23; 3:16; 4:5; Waefeso 1:8,17; 3:10) na kukutana kwa kweli zote (*sunesis*, kama vile Wakolosai 2:2)
Chunguza kwamba kuna marudio ya kufunganishwa kwa sehemu tatu: “maarifa,” “hekima,” na “uelewa.” Hii inaaksi msisitizo wa walimu wa uongo katika siri ya ukweli (kama vile Wakolosai 2:3). Kristo ni kweli ya Mungu (kama vile Yohana 14:6)!

**1:10 “kuenenda kwa namna inavyostahili”** Hii ni kauli tendaji isiyo na kikomo ya wakati uliopita usio timilifu. Inatolewa maana na hali ya kuendelea ya nne (kama vile Wakolosai 1:10-12) ambazo zinaeleza kuenenda kunakostahili (Kol. 2:6; 3:7; 4:5; Efe. 2:10; 4:1,17; 5:2,15; 1 The. 2:12; 4:1). Mapenzi ya Mungu ni kwamba watoto Wake waaksi tabia yake kila siku.

▣**”kuzaa matunda katika kila kazi njema”** kwa “kuzaa matunda” angalia kidokezo kamili katika Kol **1:6**. Hii ni moja ya kauli nne endelevu ya wakati uliopo (kama vile Kol 1:10-12) ambayo inaeleza maisha stahili
Mapenzi ya Mungu ni kuwa waaminio tuishi maisha ya utauwa. Mageuzi ya kimaadili ya waaminio ni ushahidi kwamba taswira ya Mungu imerejeshwa! Inatumika kama daraja kuelekea katika uinjilisti. Inaaksi tabia za familia mpya za waaminio na inaonyesha Baba yetu wa Kweli ni nani – Mungu.
Wokovu wa Kibiblia ni karama ya bure ambayo lazima iwe na matokeo katika maisha mapya na tofauti (Waefeso 2:8-9, 10).
▣**”kuongezeka katika maarifa ya Mungu”** Hii ni kauli ya pili endelevu ya wakati uliopo. Hii ni neno ambatani kali kwa maarifa ya mtu mwenye ujuzi (*epignōskō,* kama vile Kol. 1:9,10; 3:10; Efe 1:17; 4:13*).* Waamini wanaendelea kumeza maana ya injili na kuendelea kuishi yote yanayomaanishwa ndani.

**1:11” mkiwezeshwa kwa uwezo wote”** Hii ni kauli ya tatu endelevu ya wakati uliopo yenye maana “kwa nguvu zote zinazowezeshwa.” Kama wokovu, maisha ya Mkristo ni karama ya juu ya Mungu, ambayo haiachi kusaidiwa, kujitoa kunakohitaji bidii na nguvu nyingi za kibinadamu (kama vile Wagalatia 3:1-3). Waaminio lazima wazae matunda kwa Roho kwa ufanisi, maisha ya utauwa (kama vile Waefeso 5:18). Neno hili mara zote hutumika kwa nguvu zipitazo uwezo wa kawaida. (kama vile Waefeso 1:19; Wafilipi 4:13).

▣**”kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake”** Tungo hii inafunua namna waamini wanaweza “kuwezeshwa kwa nguvu zote.” Lazima wazae matunda ya Roho wa Mungu, na nguvu na Utukufu ni wake!

▣**”na saburi ya kila namna na uvumilivu”** Unaweza kushangaa kama haya yangeweza kutumika kimbadala. Kulikuwa na utofautiano kidogo. Saburi (*hupomonē*) ilimaanisha uvumilivu na ustahimilivu, wakati uvumilivu (*makrothumia*) ilimaanisha hali ya ustahimilivu wa kuvumilia mabaya au mateso. Yalikuwa vyote maonyo madogo ya mara kwa mara kutoka kwa Paulo (kama vile 2 Kor 6:4, 6; 2 Timotheo 3:10). Waaminio wanauwezo juu yao tu katika nguvu za Mungu. Maneno haya mara kwa mara yalitumika kufunua namna Mungu anavyoshughulika na kuwajali wanadamu walioanguka (kama vile Warumi 2:4; 9:22; 1 Kor 6:6) na namna wanadamu waliokombolewa wanavyotakiwa kutendeana wao kwa wao (kama vile Wagalatia 5:22-23; Waefeso 4:2; Wakolosai 3:12).

▣**”kwa furaha”** Hii inaweza kufanana kisarufi na Wakolosai 1:11 (NKJV) au Wakolosai 1:12 (NASB, NRSV, TEV, NJB)

**1:12” mkimshukuru”** Hii ni ni kauli endelevu ya wakati uliopo ya mwisho kati ya nne za Wakolosai 1:10-12 ambazo zinafunua kuenenda kunakostahili kama shukrani endelevu. Shukrani ni tabia ya maisha yaliyojaa Roho (kama vile Wakolosai 3:17; Waefeso 5:20; 1 Wathesalonike 5:18).

▣**"kwa Baba"** Wakristo wanatakiwa kukumbushwa mara kwa mara kwamba shabaha ya Agano Jipya katika huduma ya Mwana haitakiwi kupunguza sifa zao kwa Mungu Baba. YEYE ndiye ambaye tabia na neema zinadhihirishwa katika Yesu. Alikuwa ni mtumaji na muidhinishaji wa Mwana (kama vile Waefeso 1:3-14 na 15-23) Kuna kutofautiana katika Maandiko kadhaa ya Kiyunani ya Tungo hii. Hata hivyo usomaji huu unasaidiwa na maandiko ya kale ya Kiyunani P[61], A, C, D, K, na P kama vile tafsiri ya Latin Vulgate. USB[4] inatoa alama ya "B" (mkaribiano wa hakika). Kutofautiana huku kama ambavyo ni kweli mara nyingi, haiathiri namna, kweli au kuaminiwa kwa andiko. Waandishi wa kwanza walijaribu kufanya maandiko waliyoyanakili kuwa wazi. Angalia kiambatanisho cha pili.

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"kupewa sifa"** |
| **NRSV** | **"kuwezeshwa"** |
| **TEV** | **"imefanywa kutosha"** |
| **NJB** | **"imefanya muweze"** |

Neno hili limetumika hapa na katika 2 Wakorintho 3:5-6 (kivumishi kimetumika katika 2 Wakorintho 16; 3:5 na 2 Timotheo 2:2). Mungu ametustahilisha sisi (1) kwa kututangaza kuwa wenye haki katika Kristo (kustahilishwa na kutakaswa kinafasi) na (2) kwa kuendeleza kule kufanana na Kristo ndani yetu (kutakaswa kunakoendelea). Angalia Mada Maalum: Utakaso katika Waefeso 1:1

▣**"ndani yetu"** Maandiko ya Kale ya Kiyunani yanagawanywa kwa usawa kati ya neno "ndani yetu" (NASB, NKJV) na neno"yenu" (NRSV, TEV, NJB). USB4 inatoa alama ya "B" (mkaribiano unaofanana). Neno"yenu" linaweza kuwa liliandikwa hapa na mnakili ili kufananisha Wakolosai 1:13.

▣**"kushiriki karika urithi"** urithi ni neno halisia la "vingi." Katika Agano la Kale Mungu alimuahidi Ibrahimu nchi na mbegu (kama vile Mwanzo 12:12). Agano la Kale linaweka shabaha kwenye ardhi; Agano Jipya linaweka katika mbegu. Katika Agano la Kale, ardhi ya Wapelestina ilitolewa kama urithi wa kikabila kwa watoto wote wa Yakobo (kama vile Yoshua 12-19) isipokuwa Walawi kwasababu walimtumikia Mungu katika nafasi ya pekee (kama vile Hesabu 18:24). Katika namna watu wote wa Agano la Kale wa Mungu walikuwa makuhani (Kutoka 19:4-6) walikuwa ni ufalme wa ukuhani kuleta ulimwengu mzima kwa Mungu. Watu wote wa Mungu wa Agano JIpya wanazungumziwa katika neno la Agano la Kale makuhani (1 Petro 2:5, 9; Ufunuo 1:6). Kama walawi walikuwa na Mungu kama urithi wao, hata sasa ndivyo ilivyo kwa waamini wa Agano Jipya wote. (kama vile Mdo 20:32; Warumi 8:17; Wagalatia 4:7).

**MADA MAALUM: URITHI WA WAAMINIO**

Katika Agano la Kale kila kabila isipokuwa la Walawi lilipokea urithi wa ardhi (kama vile Yoshua 14-22). Walawi, kama kabila la kikuhani, wahudumu wa hekaluni, na waalimu wa kanisa la mahali, walionekana kuwa na YHWH Mwenyewe kama mrithi wao (kama vile. Zab. 16:5; 73:23-26; 119:57; 142:5; Wimb. 3:24). Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi walichukua haki na upendeleo wa Walawi na kuitumia kwa waamini. Hii ilikuwa ni njia yao ya kudai kuwa wafuasi wa Yesu walikuwa watu wa Mungu na kwamba sasa waamini wote wameitwa kutumika kama makuhani mbele za Mungu (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), kama Agano la Kale linavyo watetea Waisrael wote(kama vile Kut. 19:4-6). Msisitizo wa Agano Jipya sio juu ya mtu binafsi kama kuhani aliye na upendeleo Fulani, bali ni katika kweli kwamba waamini wote ni makuhani, wakihitaji ushirika wa mwenendo wa kitumishi (kama vile 1 Kor. 12:7). Watu wa Mungu wa Agano Jipya wamekwisha pewa majukumu ya Agano la Kale ya kueneza injili ulimwenguni (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5b; Mt. 28:18-20; Lk 24:46-47; Mdo 1:8; angalia Mda Maalum: Mpango wa YHWH wa ukombozi wa Milele).

Hii ni dhana ya Yesu kama mmiliki wa uumbaji kwa sababu alikuwa ni wakala wa Baba kipindi cha uumbaji (kama vile. Yn 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2-3). Sisi ni warithi wenza kwa vile Yeye ni mrithi (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7; Kol. 3:24). Maandiko yanazungumza kuhusu kurithi kwa waamini (kama vile Mdo 20:32; 26:18; Efe. 1:4; Kol. 1:12; 3:24) vitu vingi kwa sababu ya mahusiano yao ya kifamilia na Yesu ambaye ndiye mrithi wa vitu vyote (kama vile Ebr. 1:2). Kwa hiyo, wao pia ni warithi wenza (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7) wa

1. Ufalme (kama vile Mt. 25:34, 1 Kor. 6:9-10; 15:50; Efe. 5:5)

2. Maisha ya milele (kama vile Mt. 19:29; Ebr. 9:15)
3. Ahadi za Mungu (kama vile Ebr. 6:12)
4. Ulinzi wa Mungu wa ahadi zake (kama vile 1 Pet. 1:4-5)

▣**"ya watakatifu"** angalia Mada Maalumu katika mstari wa 2.

▣**"katika nuru"** Hii ilikuwa ni aidha (1) kauli ya kimaadili (kama vile Yoh. 3:19) au (2) kauli kuhusu kufanana na Kristo ikipingana na ya kipepo (Waefeso 6:12; Mdo 26:18).

**1:13-14** Mistari hii inafanya kazi kama mpito kuelekea katika ungamo zuri la imani la elimu ya Kristo ya Wakolosai 1:15-20. Inafunua kile ambacho Mungu baba amefanya kwa ajili ya waamini kupitia Mwanawe

**1:13"Naye aliyuokoa"** Kiwakilishi kinamaanisha Baba. Hii ni kauli ya kati elekezi (yenye ushahidi) ya wakati uliopita usio timilifu inatumika katika namna ya kuokoa (NRSV, TEV, NJB).

▣**"kutoka katika nguvu za giza"** Kiuhalisia hii "mamlaka (*exousia*) ya giza" (kama vile Wakolosai 1:12; Luka 22:53). NJB ina "nguvu za giza zitawalazo." Nuru na giza zilitumika mara kwa mara katika dini ya kiyahudi na magombo ya bahari ya chumvi kuwakilisha dola mbili za ulimwengu wa kiroho wa wema na ubaya (kama vile Yoh 3:19-21).. Paulo anatumia neno hili mara kadhaa katika Wakolosai (kama vile Wakolosai 1:13, 16; 2:10, 15).

▣**"akatuhamisha"** hii kuihalisia "kutengeneza makao" au "kutaftia eneo lingine." Vitenzi hivi vyote viwili katika mstari huu ni wakati uliopita usio timilifu. Hivi ni vitu Mungu amekwisha timiza kwa ajili ya waamini.

▣**"ufalme"** Yesu alitumia dhana kama ukweli wa sasa uliopo kwa kutumia utimilifu wa baadaye ujao. Muktadha unaotiwa msisitizo kwa nini waamini tayari wanamiliki katika Kristo (kama vile Waefeso 2:5-6)! Angalia Mada Maalum: Ufalme wa Mungu katika Waefeso 5:5.
Paulo hakutumia tungo ile ile ya Yesu "ufalme wa Mungu" mara nyingi, yawezekana kwa sababu Mataifa wasingeweza kuelewa hii dhana ya Kiyahudi.

▣**"wa Mwana wa Pendo lake"** Mungu Baba alitoa cheo hiki kwa Yesu wakati wa Ubatizo wake na kugeuzwa sura (kama vile Mathayo 3:17, 17:5). Yesu ni mwana wa pekee (*monogenēs,* kama vile Yoh 1:18, 3:16, 18; 1 Yoh 4:9). Waamini ni wana kupitia Yeye!

**MADA MAALUM: MWANA WA MUNGU**

Hii ni moja kati ya nyadhifa kubwa alizopewa Yesu katika Agano Jipya. Ni wazi kabisa ina kidokezo cha Uungu. Inamjumuisha Yesu kama "Mwana" au "Mwana wangu," pia Mungu anaelezewa kama "Baba" (angalia Mada Maalumu: Ubaba wa Mungu). Linatokea mara 124 katika Agano Jipya. Hata usanifu wa Yesu mwenyewe kama "Mwana wa Adamu" ina kidokezo cha Uungu toka Dan. 7:13-14

Katika Agano la Kale usanifu wa neno "Mwana" ingalirejea kwenye makundi maalumu manne (angalia Mada Maalumu: "Wana wa…….")

A. Malaika (mara nyingi iko katika hali ya WINGI, kama vile Mwa. 6:2; Ay. 1:6; 2:1)
B. Mfalme wa Israel (kama vile2 Sam. 7:14; Zab. 2:7; 89:26-27)
C. Taifa la Israel kwa pamoja (kama vile Kut. 4:22-23; Kumb. 14:1; Hos. 11:1; Mal. 2:10)
D. Waamuzi wa Israel (kama vile Zab. 82:6)

Ni utumiaji wa mara ya pili ambao unahusianishwa na Yesu. kwa njia hii "Mwana wa Daudi" na "Mwana wa Mungu" semi zote zinahusianishwa na 2 Samwel 17; Zaburi 2 na 89. Katika Agano la Kale neno "Mwana wa Mungu" kamwe halitumiki hasa kwa Masihi, isipokuwa kama ni mfalme wa siku za kiama kama mmoja wa "wapakwa mafuta" wa Israel. Hata hivyo, katika magombo ya bahari ya chumvi wadhifa unaohusiana na Masihi ni wa kawaida (angalia nukuu maalumu katika *Dictionary of Jesus and the Gospels*, uk. 770). Pia "Mwana wa Mungu"

ni wadhifa wa Kimasihi katika miingiliano miwili ya kazi za mafunuo ya Kiyahudi (kama vile II Esdras 7:28; 13:32,37,52; 14:9 na I Enoch 105:2)

Mazingira ya nyuma ya Agano Jipya kama inavyorejerea kwa Yesu kwa uzuri imefupishwa kwa namna mbali mbali.

1. Uwepo wake kabla (kama vile Yohana 1:15-30; 8:56-59; 16:28; 17:5; 2 Kor. 8:9; Flp. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8)
2. Kuzaliwa kwake kwa njia ya pekee (kama vile Isa. 7:14; Mt. 1:23; Luk. 1:31-35)
3. Ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17; Mk 1:11; Luk. 3:22. Sauti ya Mungu toka mbinguni ikiunganisha ufalme wa kifahali wa Zaburi 2 na mtumishi mwenye mateso wa Isaya
4. Majaribu ya shetani (kama vile Mt. 4:1-11; Mk 1:12,13; Luk 4:1-13. Anajaribiwa kuuwekea mashaka uwana wake au kutimiliza kusudi lake kwa njia tofauti na ile ya msalaba.
5. Uthibitisho wake na wale wakiri wasiokubalika
    a. Mapepo (kama vile Mk 1:23-25; Luk 4:31-37,41; Mk 3:11-12; 5:7; angalia Mada Maalumu: Pepo [roho wachafu])
    b. Wasioamini (kama vile Mt. 27:43; Mk 14:61; Yohana 19:7)
6. Uthibitisho wake kupitia wanafunzi wake
    a. Mt. 14:33; 16:16
    b. Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
7. Uthibitisho wake mwenyewe
    a. Mt. 11:25-27
    b. Yohana 10:36
8. Utumiaji wake wa stiari ya kawaida ya Mungu kama Baba
    a. Utumiaji wake wa neno *abba* kwa ajili ya Mungu
        1) Mk 14:36
        2) Rum 8:15
        3) Gal 4:6
    b. Utumiaji wake wa sasa wa jina Baba (*patēr*) kuelezea uhusiano wake na Uungu.

Kwa ufupi, wadhifa wa neno "Mwana wa Mungu" una maana kubwa ya kithiolojia kwa wale waliolifahamu Agano la Kale na ahadi zake, lakini waandishi wa Agano Jipya waliogopeshwa kuhusu utumiaji wao na watu wa mataifa kwa sababu ya mazingira ya nyuma ya wapagani ya "miungu" ikiwachukulia wanawake na matokea ya watoto kuwa "majitu."

**1:14** "ambaye ndani yake tunao" Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo. Katika Kristo waamini wanazo na wanaendelea kuwa na Baraka za familia za Mungu.

▣**"ukombozi"** Hii inawezekana ikawa ni maelezo kuelekea maneno ya Agano la Kale (*paduh*, "kuweka huru au kukomboa" na "*gaal*, " kuweka huru kupiti awakala wa ndugu [*go'el*]) Yesu alitununua kutoka utumwani (kama vile Isaya 53:11-12; Marko 10:45; Waefeso 1:7). Ukombozi ni uhalisia wa sasa (kama vile Waefeso 1:7) na kutimilizwa kwa baadaye (kama vile Waefeso 4:30).

### MADA MAALUM: FIDIA /UKOMBOZI

I. AGANO LA KALE

A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
    1. Ga'al (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno go'el unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki

ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).

2. Neno Padah (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
   a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
   b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
   c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)

B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
   a. Kimaumbile
   b. Kijamii
   c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
   a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
   b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya ga'al mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., go'el, BDB 145).
4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
   a. Baba
   b. Mme
   c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

I. AGANO JIPYA

A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
1. Agorazō (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisis ni wa Kristo.
2. Exagorazō (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laanae" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
3. Luō, "kuweka huru"
   a. Lutron, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
   b. Lutroō, "kuwekwa huru"
      1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
      2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
      3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
   c. Lutrōsis, "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
      1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
      2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
      3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
4. Apolytrōsis
   a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
      1) Luka 21:28

2) Warumi 8:23
3) Waefeso 1:14; 4:30
4) Waebrania 9:15
b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
1) Warumi 3:24
2) 1 Wakorintho 1:30
3) Waefeso 1:7
4) Wakolosai 1:14

5. Antilytron (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).

B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.

1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!
6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

▣**"msamaha wa dhambi"** Kulikuwa na baadhi ya maneno ya Kiyunani kwa "msamaha." Hii moja *(aphesis*) ilimaanisha "kutuma," ambalo ilikuwa ni maelezo kwa ibada ya siku ya Kiagano (kama vile Mambo ya Walawi 16). Mbuzi wa kafara alisimama kuchukua dhambi za watu. Tunajifunza kutoka kwa Irenaeus's *Heresies*, 1:21:2 kwamba baadhi ya walimu wenye ujuzi walitenganisha ukombozi na kuondolewa dhambi kwa muda na sababu ya makuzi. Paulo yumkini alikuwa anazungumzia uongo huu. Toleo la Bilblia la King James linaongeza tungo "kwa njia ya damu Yake," ambayo baadaye waandishi waliongeza kutokana na usambamba katika Waefeso 1:7

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 1:15-20**
***15*** **naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.** ***16*** **Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake.** ***17*** **Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.** ***18*** **Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.** ***19*** **Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae;** ***20*** **na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni.**

**1:15-20** habari hii ya kupendeza ya kishairi inaweza ikaaksi tenzi na tamko la kiimani la kanisa la kwanza. Inashughulika na (1) u-Bwana wa Yesu juu ya ulimwengu wote na (2) matendo yake ya ukombozi. Hali hiyohiyo ya kipengele cha upili inaonekana katika Waebrania 1:2-3. Ina aksi maneno kadhaa wa Wenye Ujuzi, "mzaliwa wa kwanza," "ukamilifu," na dhana kama viwango vya malaika (yaani *aeons*) ya Wakolosai 1:16, na ubinadamu wa ukweli wa Yesu na kifo katika Wakolosai 1:20.
Angalia neno "yote" linatumika mara saba (kama vile Wakolosai 1:15, 16) [mara mbili], 17 [mara mbili], 18, 20). Hudum ya Yesu ni jumuishi, vyote, vinavyotakikana, vinatoka kwake.

1. Kwa yeye vitu vyote viliumbwa
2. Vitu vyote vimeumbwa kupitia yeye
3. Yeye yupo kabla ya vitu vyote
4. Katika yeye vitu vyote vinawekwa pamoja
5. Yeye atakuja na kuwa sehemu ya kwanza katika kila kitu
6. Ukamilifu wote unakaa ndani yake
7. Kupitia yeye kupatanisha vitu vyote kwa yeye (kiwakilishi "kwa yeye" yawezekana kinahusiana na Baba)

Chunguza namna ambavyo mara kwa mara kiwakilishi "katika yeye" kinawasilishwa na pendekezo tofauti.

1. "katika Yeye," Wakolosai 1:16, 17, 19
2. "kupitia Yeye," Wakolosai 1:16, 20
3. "ndani yake," Wakolosai 1:16, 20 (chunguza hiki kitu kilivyo vile vile katika Waefeso 1:3-14)

**1:15"Yeye ni sura ya Mungu asiyeonekana"** Neno hilo hilo (*eikōn)* linatumika na Yesu katika Wakolosai 3:10 na 2 Wakorintho 4:4. Maelezo ya kithiolojia yanayofanana yanatokea katika Yoh. 1:18; 14:9; Wafilipi 2:6; Waebrania 1:3 kifungu cha habari kina neno la kiyunani lenye nguvu zaidi (character, ambayo inamaanisha uwakilishi sawa kabisa, kama vile Mwanzo 1:26-27; 5:1; 9:6; 1 Wakorintho 11:7; Yakobo 3:9). Kumuona Yesu ni kumuona Mungu! Mungu asiyeonekana ameonekana! Uungu umekuwa mwanadamu (kama vile Yohana 14:9).
Huduma ya Yesu ilikuwa ni kurejesha sura ya Mungu katika ubinadamu. Kwa namna moja Edeni ilikuwa imekwisha rejeshwa kupitia Yesu, Adamu wa pili ( kama vile Warumi 5:12-21; 1 Wakorintho 15:20-28; Wafilipi 2:6). Inawezekana pia kwamba mbingu itakuwa Edeni iliyorejeshwa;

1. Biblia inaanza na Mungu, mwanadamu na wanyama (kama vile Mwanzao 1-2) na inaishia na Mungu na mwanadamu katika mazingira ya bustani (pamoja na wanyama kwa kuusisha, kama vile Ufunuo 21-22)
2. Unabii wa Isaya 11:6-9 inafunua watoto na wanyama pamoja katika zama mpya
3. Yerusalemu mpya inashuka chini kwenye dunia iliyoumbwa upya (kama vile 2 Petro 3:10-13; Ufunuo 21:2)

◙**"mzaliwa wa kwanza wa uumbaji wote"** Hii ilikuwa ni sitiari ya Agano la Kale kwa upekee wa Yesu na nafasi ya kuinuliwa kwake

1. Walimu walisema kuwa ilimaanisha kuwepo kwake hapo kale kila mahali wakati wote
2. Katika Agano la Kale ilitumika kwa ajili ya mtoto wa kiume mkubwa kama mrithi na msimamizi wa familia
3. Katika zaburi 89:27 ilitumika kwa namna ya ki-Masihi
4. Katika Mithali 8:22 ilimaanisha hekima kama uumbaji wa kwanza wa Mungu na wakala wa uumbaji. Katika uchaguzi wa muktadha #1 na #2 zilizounganishwa zinaonekana kuwa bora zaidi

Tungo hii haitakiwi kueleweka kama Yesu kuwa mzaliwa wa kwanza wa uumbaji (#4). Hii ingekuwa imeangukia katika mikono ya walimu wajuzi waliofundisha kuwa Yesu alikuwa katika kiwango cha juu kabisa kinachokaribiana na mungu mkuu. Lazima itafsiriwe katika mazingira yake ya Kiyahudi ya Agano la Kale. Yesu mwana wa Mungu wa pekee (kama vile Yoh 1:18; 3:16, 18: 1 Yohana 4:9), na bado Yesu siku zote alikuwa Mungu (kama vile Wakolosai 1:17; Yohana 1:1; 5:18; 10:30; 14:9; 20:28). Alikuwa mwanadamu kwa muda katika Bethlehemu, ili kwamba wanadamu wafahamu na kumuelewa Mungu (Yohana 1:14, 18).

**MADA MAALUM: MZALIWA WA KWANZA**

Neno hili "mzaliwa wa kwanza" (prōtotokos) limetumika katika Biblia kwa maana tofauti mbali mbali.

1. Mazingira yake ya nyuma yanrejelea kwa
   a. Mzaliwa wa kwanza anamhusu YHWH YHWH (BDB 114, KB 131, kama vile. Kut. 13:2,12; 22:29;

34:19; Hes. 3:13)
   b. Ukaribu uliokuwepo kabla wa mzaliwa wa kwanza wa kiume katika familia (kama vile. Kumb. 21:17; Zab. 89:27; Lk 2:7; Rum. 8:29; Ebr. 11:28)
2. Matumizi yake katika Kol. 1:15 yanazungumza juu ya Yesu kama mzaliwa wa kwanza wa uumbaji ambacho kinawezekana katika kidokezo cha Agano la Kale Mit. 8:22-31, au wakala wa Mungu wa uumbaji (kama vile. Yn 1:3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:15-16; Ebr. 1:2)
3. Matumizi yake katika Kol. 1:15,18; 1 Kor. 15:20,23; Uf. 1:5 inarejelea kwa Yesu kama mzaliwa wa kwanza toka katika wafu
4. Ni wasifu wa Agano la Kale uliotumika kwa Masihi (kama vile. Zab. 89:27; Ebr. 1:6; 12:23); ni wasifu unaojumuisha dhana mbali mbali za Yesu kama kitovu na mmiliki wa mambo yote.

**1:16 "kupitia yeye vitu vyote viliumbwa"** Yesu alikuwa wakala wa Mungu wa uumbaji, kwa vyote vinavyoonekana na visivyonekanavyote, anga la ulimwengu na mbingu (kama vile Yohana 1:3, 10; Warumi 11:36; 1 Kor, 8:6; Waebrania 1:2; 2:10). Hii ilikanusha mawazo ya walimu wajuzi walio kinyume na uhusiano kati ya roho (Mungu) na maada. Ilikuwa ni Yesu aliyezungumza ulimwengu uwepo na ukawepo (kuishi/kuwepo/kuwa hai). Ilikuwa ni Yesu aliyemuumba Adam na akaweka pumzi ya uhai ndani yake (rejea Mwanzo 20.
kitenzi "aliumba kinatumika mara mbili katika wakolosai 1:16. Ya kwanza ni kauli tendwa elekezi ya wakati iliopo na ya pili ni katika mwisho wa mstari (katika Kiyunani) ni Kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo. Msukumo ni kwamba Yesu ni wakala wa uumbaji lakini Baba ni msababishi wa kwanza. Uumbaji ulikuwa ndani (*en*) ya Yesu, kupitia (*dia*) Yesu na kwa (*eis*) Yesu!

▣**"enzi au usultani au watawala au mamlaka"** katika baadhi ya muktadha maneno haya yanaweza yakamaanisha viongozi wa kitawala wa serikali (kama vile Warumi 13), lakini katika muktadha wa wakolosai zinamaanisha viwango vya kimalaika vya walimu wa uongo (*aeons*, kamam vile Warumi 8:38; 1 Wakorintho 15:24; Waefeso 1:21; 3:10; 6:12; Wakolosai 1:16; 2:10, 15; 1 Petro 3:22). Wa kale waliona ulimwengu si tu katika namna ya kusababishwa kwa mwili na uhusiano wenye ufanisi, lakini kama dola ya kiroho pia. Haiwezekani uwe na muono wa kibiblia alafu ukatae dola ya kiroho. Angallia Mada Maalum: Malaika katika Maandiko ya Paulo.

***MADA MAALUMU: ARCHĒ***

Neno la Kiyunani *archē* linamaanisha "mwanzo" au "asili" ya kitu.
1. mwanzo wa mpangilio ulioumbwa (kama vile. Yohana 1:1; Ebr. 1:10)
2. mwanzoni mwa injili (kama vile. Mk. 1:1; Flp. 4:15; 2 The. 2:13; Ebr. 2:3; 1 Yohana 1:1)
3. mwanzo wa jicho la kwanza la ushahidi (kama vile. Luka 1:2)
4. mwanzo wa dhambi (miujiza, kama vile. Yohana 2:11)
5. mwanzo wa mafundisho (kama vile. Ebr. 5:12)
6. mwanzo wa udhihirisho uliojikita katika kweli ya injili (kama vile. Ebr. 3:14)
7. mwanzo, Kol. 1:18; Ufu. 3:14

Ilikuja kutumika juu ya "utawala" au "mamlaka"
1. juu ya wanadamu rasmi watawalao
   a. Luka 12:11
   b. Luka 20:20
   c. Warumi 13:3; Tito 3:1
2. juu ya mpangilio wa mamlaka
   a. Warumi 8:38
   b. 1 Kor. 15:24
   c. Efe. 1:21; 3:10; 6:12
   d. Kol. 1:16; 2:10,15
   e. Yuda 1:6

▣**"na kwa Yeye"** Yesu si tu kwamba alikuwa wakala wa Mungu Baba katika uumbaji lakini lego la uumbaji pia (kama vile Warumi 11:36; Waebrania 2:10).

▣**1:17"Yeye alikuwako kabla ya vitu vyote"** "hakukuwahi kutokea muda ambao Yesu hakuwa! Yesu ni uwepo wa kabla wa uungu (kama vile Yohana 1:1-2; 8:58; 17:5, 24; 2 Wakorintho 8:9; Wafilipi 2:6-7; Wakolosai 1:17; Waebrania 10:5-7)! Chunguza matumizi ya "Yeye" (*autos*) katika Wakolosai 1:17 na 18, "Yeye, Yeye mwenyewe, ziko mwanzo wa kila kitu" na "Yeye, Yeye mwenyewe ni kichwa cha mwili"!

**NASB, NRSV**
**NJB** **"Katika Yeye vitu vyote vinaungana"**
**NKJV** **"katika Yeye vitu vyote vinaishi"**
**TEV** **"katika umoja pamoja naye vitu vyote vinakaa mahali pake"**

Hii ni Kauli tendaji elekezi ya wakai timilifu ya "*syn*" ambatani "kusimama pamoja na" (*sunistēmi)* ambalo inamaanisha "kuendelea," "kustahimili," au "kuwepo"
Hili ni fundisho la kukidhiwa kiungu (angalia Waebrania 1:3) na ni la kibinafsi! "vitu vyote" humaanisha vitu vya kiroho na kimwili vilivyoumbwa. Yesu ndiye muidhinishaji na pia muumbaji wa vitu vyote. Katika Agano la Kale kazi hizi zilifunua kazi ya *Elohim* (Mungu).

**1:18"Yeye ndiye aliyekichwa cha mwili, kanisa"** Kama Yesu alikuwepo kabla na alikuwa mahali pote katika uumbaji; hivyo Yupo katika kanisa. Hii inamaanisha kanisa la ulimwenguni (kama vile Waefeso 1:22-23; 4:15; 5:23; Wakolosai 1:18; 2:9). Waamini wote kwa pamoja kama mtu mmoja mmoja (kama vile 1 Wakorintho 6:19) na kwa pamoja (kama vile 1 Wakorintho 3:16) ni mwili wa Kristo (yaani hekalu jipya). Paulo mara nyingi alizungumza juu ya kanisa kama mwili wa Kristo (kama vile 1 Wakorintho 12:12-27), lakini ni katika Waefeso tu na Waokolosai ambapo Yesu anaposemwa kama "kichwa" cha mwili. Kwa kusema ukweli Yeye ndiye kichwa cha vitu vyote, hata usultani na nguvu (kama vile Waefeso 1:22).

### MADA MAALUM: KANISA (*EKKLESIA*)

Neno hili la Kiyunana, *ekklesia*, linatokana na maneno mawili, "nje ya"na "kuitwa." Neno hili linatumika kidunia (yaani., jamii iliyoitwa kwenye kikao, k.v Mdo. 19:32,39,41) na kwa sababu ya utumiaji wa maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno hili kwa ajili ya "kusanyiko" la Israel (*Qahal,* BDB 874, KB 1078, k.v. Hes. 16:3; 20:4; Kumb. 31:30),na matumizi ya kidini. kanisa la mwanzo walijiona wao kama mwendelezo wa Agano la Kale la watu wa Mungu. Walikuwa Waisrael wapya (k.v. Rum. 2:28-29; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), utimilizo wa kusudi la Mungu kidunia (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH
Neno lililotumika kwa maana nyingi katika injili na matendo.

1. Mikusanyiko ya kidunia , Mdo. 19:32,39,41
2. Watu wa Mungu ulimwenguni katika Kristo, Mt. 16:18 na Waefeso
3. Kusanyiko la waumini wa mahali katika Kristo, Mt. 18:17; Mdo. 5:11 (katika aya hii, ni kanisa huko Yerusalem); Mdo. 13:1; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; Filemoni uk. 2
4. Watu wa Israel kwa ujumla, Mdo. 7:38, katika hotuba ya Stephano
5. Watu wa Mungu kwenye Miji, Mdo. 8:3; Gal. 1:2 (Yuda au Palestina)

Kanisa ni watu waliokusanyika, na sio jengo. Hapakuwepo na majengo ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Katika Yakobo (moja ya kitabu cha mwanzoni kabisa cha Wakristo) kanisa lilitajwa kwa neno "*synagōgē*" (kusanyiko). Neno kanisa limetokea tu kwa Yakobo (k.v. Yakobo 2:2; 5:14).

▣**"Yeye ndiye mwanzo"** ukiangalia kwa haraka haraka inaonekana kama maelezo mengine kuhusu uumbaji (kama vile Mwanzo 1:1), lakini muktadha umebadilika kwa kanisa. Katika mazingira haya neno "mwanzo" yawezekana inahusiana na asili au chanzo kwa namna ya Kiyunani. Yesu ndiye kichwa au chanzo cha maisha ya watu wapya wa Mungu, Wayahudi na Wayunani, watumwa na waliohuru, wake kwa waume (kama vile Wakolosai 3:11; Wagalatia

3:28) Yeye ni Adamu mpya (kama vile Warumi 5:12-21). Kichwa cha kabila mpya, wakristo (kama vile Waefeso 2:11-3:13)

▣**"mzaliwa wa kwanza kutoka katika wafu**" maana ya kifungu cha habari cha agano jipya kuhusu ufufuo ni 1 wakorintho 15. Yesu ni aliyekuwako

▣**"ili kwamba Yeye mwenyewe aweze kuwa nafasi ya kwanza katika kila kitu"** kauli hii ya hitimisho ni sawa na ile ya Waefeso 1:22-23. Baba amemfanya mwana Mkuu sana na aliyepo mahali pote katika kila kitu (kama vile 1 Wakorintho 15:27-28).
**1:19** Hii inaanza na "kwa" (*hoti,* kishazi cha kusudi). Inataja Mapenzi ya Mungu kwa Masihi ambayo ni (1) ukamilifu wa uungu ukifunuliwa katika Yeye (kama vile Wakolosai 1:19) na (2) upatanisho wa vitu vyote kupitia yeye (kam vile Wakolosai 1:20).

**NASB "Kwa maana ukamilifu wote unakaa ndani yake"**
**NKJV "kwamba ndani yake ukamilifu wote ukakae"**
**NRSV "kwamba ndani yake ukamilifu wote wa Mungu….unakaa"**
**TEV "kwamba mwana katika yeye kuna asili yote kamili ya Mungu"**
**NJB "ukamilifu wote upatikane katika yeye"**

Huu ni mchezo wa maneno "ukamilifu"(*plerōma*), ambalo lilitumika na walimu wa uongo kufunua viwango vya kimalaika kati ya mungu mkuu na maada ya dhambi (kama vile Kol 2:9; Waefeso 1:23; 3:19; 4:13). Hii ilikuwa ni kauli ya kushtusha kumfunua fundi seremala kutoka Nazareth ambaye aliuawa kwa uhaini! Kumuona Yesu ni kumuona Mungu!
**1:20** "na kupitia yeye kupatanisha" Neno (kama vile Wakolosai 1:22) ilimaanisha "kubadilisha kutoka katika uadui kwenda katika amani" haswa kati ya watu wawili. Dhambi imesababisha utengano kati ya muumbaji na muumbwaji. Mungu alifanya kazi ndani ya Kristo kurejeshwa kwa ushirika (kama vile Warumi 5:18-19). Hii ni neno la jozi ambatani (*apokatallassō)* kwa ajili ya msisitizo wa kithiolojia (Paulo alitumia neno hilohilo katika Waefeso 2:16 na mzizi huo huo katika Wakorintho 5:18-20.

▣**"katika vitu vyote"** Hii inamaanisha waumbwaji wote, visivyoonekana na vinavyoonekana (kama vile Warumi 8:18; 1 Kor 15:27-28; Waefeso 1:22-23).

▣**"kwa yeye mwenyewe"** Hii inawezekana kithiolojia inamaanisha Baba au Mwana. Muktadha ni mwongozo tu. Hapa Baba anaonekana bora.

▣**"akiisha kutengeneza amani kupitia damu ya msalaba Wake"** Hii ilimaanisha dhabihu ya kifo (kama vile Warumi 5:9; Waefeso 1:7; 2:13, 16). Upatanisho haukufanyika isipokuwa kwa gharama kubwa! Msisitizo ulikuwa yawezekana katika ubinadamu wake (damu) na pia agano la upatanisho wa kulia makosa (dhabihu, kama vile Isaya 53: 2 Kor 5:21). Walimu wa uongo wangekuwa wamekiri uungu wao lakini walikataa ubinadamu wake na kifo.

**MADA MAALUM: AMANI (maana tofauti)**
Hili neno la asili la Kiyunani lilimaanisha "kuunganisha pamoja kile kilichokuwa kimevunjika" (kama vile Yohana 14:27; 16:33; Flp. 4:7). Zipo njia tatu ambazo Agano Jipya huzungumzia amani:
1. Kama kuhusu mtazamo wa amani yetu na Mungu kupitia kristo (kama vile. Kol. 1:20)
2. Kama dhahania ya mtazamo wa kupatanishwa na Mungu (kama vile. Yohana 14:27; 16:33; Flp. 4:7)
3. Kwamba Mungu ameunganishwa katika mwili mmoja mpya kwa njia ya Kristo, wote Wayahudi waaminio na Mataifa (kama vile Efe. 2:14-17; Kol. 3:15).

Newman na Nida, *A Translator's Handbook on Paul's Letter to the Romans*, p. 92, kina hoja nzuri kuhusu "amani."

"Katika Agano la Kale na katika Agano Jipya neno "amani" lina maana pana. Kimsingi unaelezea hali nzuri ya maisha ya mtu; uliasiliwa miongoni mwa Wayahudi kama kanuni ya salamu. Mtajo huu ulikuwa maana ya kina kiasi kwamba ungeweza kutumika na Wayahudi kama maelezo ya Wokovu wa kimasihi. Kwasababu ya ukweli huu ulikuwa na maana ya kina kiasi kwamba ungeweza kutumika na Wayahudi kama maelezo ya wokovu wa kimasihi. Kwasababu ya ukweli huu kuna nyakati inatumika karibu sawa na mtajo peleka "ili kuwa na uhusiano sahihi na Mungu" (uk. 92).

▣**"msalaba Wake"** Kumbukumbu la Torati 21:23 ilielezea kwamba yoyote aangikwaye juu ya mti amelaaniwa na Mungu (kama vile Wafilipi 2:8). Kwa asili hii ilimaanisha umma kususia mara baada ya kifo badala ya kutoa maziko. Hata hivyo kwa siku za Yesu,walimu walifasiri hilo kama kusulubishwa. Yesu alichukua laana ya kibinadamu yenye dhambi, laana ya Agano la Kale juu yake (kama vile Wakolosai 2:14; Wagalatia 3:13; Wafilipi 2:8).
▣**"kwa vitu vya duniani au vitu vya mbinguni"** tungo hii ina elekezwa kwa tabaini za uongo kati ya "roho" (mbingu) na "maada" (dunia, Wakolosai 1:16).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 1:21-23**
**[21] Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa; [22] katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama; [23] mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu; ambayo mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake.**

**1:21 "ninyi"** Hii inamaanisha waamini wa Mataifa. Chunguza namna ya uumbaji wa uhusika wa maisha ya kale katika upagani unafuata katika mstari.
▣**"ulitenganishwa na mambo ya kale"** Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea ya neno nadra ambatani kwa mgeni au asiye mwenyeji inayofunua uhusiano wa kabla wa kimataifa kwa Mungu. Maelezo ya kithiolojia ya maelezo haya inapatikana katika Waefeso 2:1, 3, 11-22. Maelezo ya kimaadili ni katika Waefeso 4:18-19. Inawezekana kwamba neno hili linatumika na watumwa katika maana ya kuhamishwa kwenda katika mmiliki mwingine." Ikiwa hivyo, 1:13 ni usuli.

▣**"uadui katika ufahamu"** mwanadamu aliyeanguka ana mpangilio wa ufahamu wa kujitegemea (kama vile Warumi 1:28; 8:7; Yakobo 4:4; 1 Yohana 2:15-16). Mungu sio mwanadamu inakuwa kipimo cha vitu vyote (ubinadamu usiomwabudu Mungu).

**NASB "kujishughulisha katika matendo mabaya"**
**NKJV "kwa kazi ya ubaya"**
**NRSV "kufanya matendo mabaya"**
**TEV "kwa vitu viovu ulivyofanya"**
**NJB "tabia yako ovu"**

Walimu wanaeleza kwamba kama mtu afikirivyo, hivyo anakuwa. Muyo muovu/ufahamu inapelekea kuaksi kwenyewe katika matendo maovu kuelekea Mungu and wanadamu wengine (kama vile Wagalatia 5:19-21; 2 Timotheo 3:2-5; Tito 3:3).

**1:22 "tayari amekwisha wapatanisha ninyi"** "kupatanishwa ni kitenzi kikuu cha Wakolosai 1:21-23. Angalia maelezo katika Wakolosai 1:20. Ni mabadiliko ya namna gani yametokea kwa sababu ya matendo ya Mungu katika Kristo kuelekea mataifa walioanguka, waliotengwa (kama vile Wakolosai 1:20)!
Ahadi ya Mungu kuwakomboa wanadamu katika Mwanzo 3:15 imetimilizwa. Ahadi hii ilitimilizwa kabisa kama kitendo cha Mungu. Mwanadamu aliyeanguka alishindwa kurudi kwa muumbaji (kama vile Isaya 53:6, ikinukuliwa katika 1 Petro 2:25; na Warumi 3:9-18 kwa mfululizo wa nukuu za Agano la Kale). Ni upendo wa namna gani huu

uliofuata ubinadamu wenye dhambi, wenye ukaidi kupitia muda na muda akamtoa Mwanawe wa Pekee kufa kwa niaba yetu!

▣**"katika mwili wake wa kibinadamu kupitia kifo"** Hii inawezekana ikawa na uhusiano na kukataliwa kwa ubinadamu wa Yesu na walimu wa uongo (kama vile Wakolosai 1:20). Yesu alikuwa Mungu kamili na binadamu kamili (kama vile 1 Yohana 4:1-6. Alikuwa na mwili unaoonekana (kama vile Wakolosai 2:11). Alikuwa kweli mmoja wetu.

**MADA MAALUM: MWILI (*sarx)***

Neno hili limetumiwa mara kwa mara na Paulo kwa Wagalatia na makuzi yake kithiolojia katika Warumi. Wasomi wana tofautiana juu ya namna gani dokezo la maana ya maneno haya ibainishwe. Kuna uhakika wa baadhi ya mipishano katika maana. Lifuatalo ni jaribio tu la kunukuu uwanja mpana wa maana ya neno.

A. mwili wa binadamu, Yohana 1:14; Rum. 2:28; 1 Kor. 5:5; 7:28; 2 Kor. 4:11; 7:5; 12:7; Gal. 1:16; 2:16,20; 4:13; Flp. 1:22; Col. 1:22,24; 2:5; 1 Tim. 3:16
B. kushuka kibinadamu, Yohana 3:6; Rum. 1:3; 4:1; 9:3,5,8; 11:14; 1 Kor. 10:18; Gal. 4:23,29
C. mwanadamu, Rum. 3:20; 7:5; 8:7-8; 1 Kor. 1:29; 2 Kor. 10:3; Gal. 2:16; 5:24
D. kuzungumza kibinadamu, Yohana 8:15; 1 Kor. 1:26; 2 Kor. 1:12; 5:16; 10:2; Gal. 6:12
E. udhaifu wa kibinadamu, Rum. 6:19; 7:18; 8:5-6,9; 2 Cor. 10:4; Gal. 3:3; 5:13,16,19-21; Kol. 2:18
F. ghasia ya wanadamu kumwelekea Mungu, inayohusiana na matokeo ya Anguko, Rum. 7:14; 13:14; 1 Kor. 3:1,3; Efe. 2:3; Kol. 2:18; 1 Petr. 2:11; 1 Yohana 2:16

Inasisitizwa ya kwamba "mwili" hautazamwi kama uovu katika Agano Jipya, ni katika fikira za Kiyunani. Kwa wanafalsafa wa Kiyunani "mwili" ulikuwa chanzo cha matatizo ya wanadamu; kifo kilimweka huru mtu kutoka kwenye matakwa yake. Lakini katika Agano Jipya, "mwili" ni uwanja wa mgogoro wa mapambano ya kiroho (kama vile. Efe. 6:10-18), tena usio na upande. Mwingine anaweza kutumia umbile lake la mwili kwa mazuri au mabaya.

▣ **"ili kuwapeleka ninyi mbele Yake"** Hii inaeza kumaanisha (1) siku za wokovu; (2) muda kifo wa waaminio; au (3) Siku ya Hukumu/Kuja kwa Mara ya pili (kama Wakolosai 1:28; Waefeso 5;27).

▣**"takatifu na isiyo na mawaa na ipitayo laumu"** Vivumishi hivi vitatu vinatumika kama kisawe. Hii inafunua usafi wa waaminio katika Kristo (kama vile Wafilipi 1:15). Si tu kwamba wamesamehewa wamebadilishwa kabisa! Hii ni sawa na msisitizo wa Waefeso 1:4; 4:1; 5;27. Lengo la kustahilishwa sio tu kwamba twende mbinguni tunapokufa, bali utakatifu wa sasa (kama vile Mambo ya Walawi 19:2; Mathayo 5:48)!
Utakaso ni uhalisia wa sasa kwa waaminio kama karama ya Kristo (kama vile Matendo ya Mitume 26:18; 1 Kor 1:2, 30; 6:11; Waebrania 10:10, 14). Huku ni kuishi maisha ya mwendelezo wa kufanana na Kristo (kama vile Efe 1:4; 2:10; 2 Tim. 2:12; Yak 1:4; 2 Pet. 3:14 la lengo la siku za mwisho (kama vile 2 Kor. 11:2; Efe 5:27; 1 Thes 3:13; 5:23; 1 Yoh 3:2).

**MADA MAALUM: PASIPO LAWAMA, PASIPO HATIA, PASIPO KUHUKUMIWA, WALA MAWAA**

A. Maelezo ya ufunguzi
   1. Hii dhana kithiolojia inaelezea asili ya mwanadamu (yaani., Mwanzo 1, bustani ya Edeni)
   2. Dhambi na uasi umekwisha haribu mazingira haya ya ushirika kamili (yaani., Mwanzo 3)
   3. Wanadamu (wa kiume na wa kike) wanatamani urejesho wa ushirika na Mungu kwa sababu wameumbwa kwa sura na mfano wake Mungu (yaani., Mwa. 1:26-27)
   4. Mungu ameshughulika na dhambi ya mwanadamu kwa njia kadhaa kwa kutumia
      a. Watu wa Mungu (yaani., Abraham, Musa, Isaya)
      b. mtindo wa utoaji dhabihu (yaani., Walawi 1-7)

c. Mifano ya ki-Mungu (yaani., Nuhu, Ayubu)

5. Hatimaye Mungu anamtoa Masihi
    a. Kama ufunuo kamili wake mwenyewe (kama vile Yn 1:1-14; Kol. 1:13-17; Ebr. 1:2-3)
    b. Kama dhabihu kamili kwa ajili ya dhambi (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)
6. Wakristo waliumbwa pasipo lawama
    a. Rasmi kupitia haki ya Kristo iliyowekwa ndani yetu (kama vile. Rum. 4:3,6,8,11,22,23,24; Yakobo 2:23)
    b. Kwa mwendelezo wa kazi ya Roho (Yn 16:8-1)
    c. Lengo la Ukristo ni kufanana kama Kristo (kama vile. Rum. 8:28-30; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3; 5:23; 2 The. 2:13; Tito 2:14; 1 Pet. 1:15), ambao katika ukweli, ni urejesho wa taswira ya Mungu iliyopotea katika anguko la Adamu na Hawa.
7. Mbinguni ndio urejesho wa ushirika kamili wa Bustani ya Edeni. Mbinguni ndiko Yerusalem Mpya inayotegemewa kuja nje ya uwepo wa Mungu (kama vile Ufu.21:2) kwenye ardhi iliyotakaswa (kama vile 2 Pet. 3:10). Biblia ilianza na kuishia kwenye maudhui yale yale ya:
    a. Ushirika binafsi wa ndani na Mungu
    b. Ndani ya muundo wa bustani (Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)
    c. Kwa maelezo ya kinabii, uwepo na urafiki wa wanyama (kama vile Isa. 11:6-9)

B. Agano la Kale
1. Kuna maneno mengi ya Kiebrania ya aina tofauti ambayo yanachukua dhana nzima ya utimilifu, pasipo lawama, pasipo hatia ambayo yangalikuwa vigumu kuyataja na kuonyesha namna yahusianavyo
2. Maneno makuu yanayochukua dhana nzima ya utimilifu, kutokuwa na kosa, au kutokuwa na hatia (kutokana na Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kur. 94-99) ni:
    a. *shalom* (BDB1022, KB 1532)
    b. *thamam* (BDB1070, KB 1743)
    c. *calah* (BDB478, KB 476)
3. Tafasiri ya maandiko ya Kiyunani (yaani., Biblia ya kanisa la mwanzo) inazitafasiri dhana hizi za Kiebrania kwa maneno ya lugha ya kawaida ya Koine yaliyotumika katika Agano Jipya (angalia hapa chini)
4. Dhana muhimu imejikita kwenye mtindo wa utoaji dhabihu
    a. *amōmos* (BDB 1071, cf. Kut. 29:1; Law. 1:3,10; 3:1,6; Hes. 6:14)
    b. *amiantos* and *aspilus* pia yana vidokezo vya kimadhehebu

C. Agano Jipya
1. Dhana ya kisheria
    a. Kidokezo cha sheria cha kimadhehebu ya Kiebrania kimetafasiriwa kwa neno *amōmos* (BDB 1071, kama vile Efe 5:27; Flp. 2:15; 1 Pet. 1:19)
    b. Vidokezo vya sheria za Kiyunani (kama vile. 1 Kor. 1:8; Kol. 1:22)
2. Kristo yule asiye na dhambi, lawama, hatia (*amōmos*, kama vile. Ebr. 9:14; 1 Pet. 1:19)
3. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kumfuata Yeye (*amōmos*, kama vile. Efe. 1:4; 5:27; Flp. 2:15; Kol. 1:22; 2 Pet. 3:14; Yuda 1:24; Ufu. 14:5)
4. Dhana hii pia inatumiwa na viongozi wa kanisa
    a. *anegklētos*, "pasipo mashitaka" (kama vile. 1 Tim. 3:10; Tit. 1:6-7)
    b. *anepilemptos*, "zaidi ya shutuma" au "hapana nafsi ya lawama" (kama vile. 1 Tim. 3:2; 5:7; 6:14; Tit 2:8)
5. Dhana ya "kutokuwa najisi" (*amiantos*) imetumika kwa
    a. Kwa Kristo mwenyewe (kama vile. Ebr. 7:26)
    b. Urithi wa Wakristo (kama vile. 1 Pet. 1:4)
6. Dhana ya "ujumla" au "kusikika" (*holoklēria*) (kama vile. Mdo. 3:16; 1 The. 5:23; Yakobo 1:4)
7. Dhana ya kuwa "pasipo kosa," "kutokuwa na hatia" linaelezewa kwa *amemptos* (kama vile. Lk 1:6; Fil. 2:15; 3:6; 1 The. 2:10; 3:13; 5:23)
8. Dhana ya "kutokuwa kwenye lamama" linaelezewa kwa *amōmētos* (kama vile. 2 Pet. 3:14)

9. Dhana ya “kuwa safi,” “pasipo doa” mara nyingi zimetumika katika sura zenye moja ya maneno ya hapo juu (kama vile. 1 Tim. 6:14; Yakobo 1:27; 1 Pet. 1:19; 2 Pet. 3:14)

D. Idadi ya maneno katika Kiebrania na Kiyunani yanayoelezea dhana hii yanaonyesha umuhimu wake. Mungu ametupatia mahitaji yetu kupitia Kristo na sasa anatuita kuwa kama Yeye.

Waamini kihali, kihukumu wametangazwa kuwa “sawa” “wenye haki” “wasio na lawama” kwa kazi ya Kristo. Sasa waamini wanatakiwa kumiliki nafasi yao. “Tembeeni katika nuru kama Yeye alivyo nuruni” (kama vile. 1 Yn 1:7). “tembeeni kwa thamani ya mwito wenu" (kama vile. Efe. 4:1,17; 5:2,15). Yesu ameirejesha taswira ya Mungu. Ushirika wa ndani sasa ni dhahiri, lakini kumbukeni Mungu anahitaji watu wanaoaksi tabia yake, kama Mwana wake alivyofanya, kwa ulimwengu uliopotea (yaani., mataifa). Hatukuitiwa chochote bali utakatifu (kama vile. Mt. 5:20,48; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:13-16). Utakatifu wa Mungu, sio tu kisheria, bali namna uishivyo!

**1:23”kama kweli mkiendelea katika imani”** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti ambayo inasadikiwa kuwa kweli kutokana na namna mwandishi anavyoona au kwa makusudi yake ya kiundishi. Paulo alidhania muendelezo wao ambao ulikuwa ni ushahidi wa kugeuka kwake kama vile 1 Yoh 2:19; Ufu. 2:7, 11, 17, 26; 3:5,12,21). Angalia Mada Maalum: Ustahimilivu katika Wafilipi 1:9)
Imani (isiyo na kibainishi) inamaanisha aidha (1) kutumaini binafsi katika Yesu, au (2) uaminifu kwa Kristo; au (3) mafundisho ya Kikristo (kama vile Mdo. 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 6:10; Yud. 1:3,20) pia katika nyaraka za kichungaji). Makuzi ya Kikristo yanajumuisha (1) imani binafsi; (2) mtindo wa maisha ya utauwa; na (3) usahihi wa kimafundisho. Katika muktadha wa mafundisho ya uongo, kila kimoja cha haya ni muhimu!

▣**”uanzishwaji ulio imara”** Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea (yenye mfumo wa kitenzi kama “kutengwa” katika Wakolosai 1:21). “wamekuwa na wanaendelea kuthibitishwa (kuhusishwa kwa Mungu).” Hii ilikuwa ni ujenzi wa sitiari kwa ajili ya msingi ulio hakika (kama vile Wakolosai 2:7; Mathayo 7:25; Waefeso 3:17). Inawezekana ikawa ni mchezo wa sehemu ya kijiografia ya Kolosai katika eneo la matetemeko.

**NASB “na kutoondolewa mbali kutoka”**
**NKJV “na hawaondolewi mbali”**
**NRSV “bila kuhamisha kutoka”**
**TEV “na haipaswi mjiruhusu wenyewe kutikiswa”**
**NJB “msiruhusu nyie wenyewe kusogezwa”**

Neno lilitumika hapa tu katika Agano Jipya. Ni muelezeo hasi wa kauli chanya ya awali. Inaweza kuwa irabu sauti tendewa (Mungu anatutunza, kama vile NASB, NKJV) au irabu sauti ya kati (waamini lazima wafanyie kazi kwa bidii, kama vile NRSV, TEV, NJB).

▣**”tumaini la injili”** Paulo anatumia neno hili katika namna kadhaa tofauti lakini zinazofanana. Mara kwa mara inahusishwa na kutimilizwa kwa imani ya waaminio. Angalia mada maalum:Tumaini katika Wakolosai 1:5. Hii inaweza ikaelezewa kama “utukufu,” kilele cha wokovu,” “Kuja kwa Mara ya Pili,” n.k kutimilizwa ni hakika, lakini muda haujulikani.

▣**”iliyotangazwa katika uumbaji wote chini ya mbingu”** “uumbaji wote” ni utiaji chumvi kwa dola ya Warumi (kama vile Wakolosai 1:6).
Mtindo huu wa kisarufi ni kauli tendwa ya wakati uliopita usio timilifu. Hata hivyo, hii haikidhi muktadha. Lazima ni katika namna ya kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. <u>Lazima</u> ikumbukwe kwamba mtindo wa kisarufi ni nyenyekevu kwa muktadha wa kifasihi kama ilivyo maana za maneno. Muktadha, sio mtindo wa kisarufi au maana za kimsamiati, siku zote huwa ni kipaumbele!

▣**"mhudumu"** Hili lilikuwa ni neno la jumla la "mtumwa" au "mhudumu" (*diakonos*, kama vile Wakolosai 1:7, 23, 25; 4:7; Waefeso 3:7; 6:21). Yesu alilitumia neno hili kwake yeye mwenyewe katika Marko 10:45. Hii ikawa ni cheo kwa watumishi na mashemasi wa makanisa (kama vile Wafilipi 1:1).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 1:24-2:5**
***24*** **Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake;** ***25*** **ambalo nimefanywa mhudumu wake, sawasawa na uwakili wa Mungu, niliopewa kwa faida yenu, nilitimize neno la Mungu;** ***26*** **siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake;** ***27*** **ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu** ***28*** **ambaye sisi tunamhubiri habari zake tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo.** ***29*** **Nami najitaabisha kwa neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu.** ***1*** **Maana nataka ninyi mjue jinsi ilivyo kuu juhudi yangu niliyo nayo kwa ajili yenu, na kwa ajili ya wale wa Laodikia, na wale wasioniona uso wangu katika mwili;** ***2*** **ili wafarijiwe mioyo yao, wakiunganishwa katika upendo, wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua kabisa siri ya Mungu, yaani, Kristo;** ***3*** **ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika.** ***4*** **Nasema neno hili, mtu asije akawadanganya kwa maneno ya kuwashawishi.** ***5*** **Maana nijapokuwa sipo kwa mwili, lakini nipo pamoja nanyi kwa roho, nikifurahi na kuuona utaratibu wenu na uthabiti wa imani yenu katika Kristo.**

**1:24"nafurahi katika mateso yangu"** Paulo alioma kufungwa kwake kama faida kwa kanisa (kama vile Wafilipi 2:17 na 2 Wakorintho 1:5. Paulo aliyaona maisha yake kama dhabihu kwa Mungu kwa niaba ya kanisa. Hii ni sehemu ya habari njema ambayo hatuitaki (kama vile Mathayo 5:10-12; Warumi 5:3; 8:17; 2 Kor 4:7-11 6:3-10; Fil. 1:29, 2:17; 2 Tim.3:12; Waebrania 5:8; 1 Pet. 1:7-8; 4:12-16)! Kama Yesu alivyoteseka kwa ajili ya wengine, pia lazima wafuasi wake (kama vile 2 Kor. 5:14-15; Wagalatia 2:20; 1 Yoh 3:16). Ni Roho tu awezaye kubadilisha dhiki kwenda katika furaha!

▣**"katika mwili wangu"** Angalia Mada Maalum katika Wakolosai 1:22

▣**"katika kujaza kile kinachopungua katika dhiki za Kristo"** Hiki kitenzi ambatani cha upili cha huzuni (*anti*, *ana*, *plēroō*) kinapatikana hapa tu katika Agano JIpya. Mapendekezo kwa nguvu yanakiri "kwa niaba ya" au "na kujaza kabisa." Hii ni sentensi ngumu sana kuitafsiri. Baadhi ya nadharia kuhusu maana za mstari ni;

1. Upatanisho kati ya Mungu na wanadamu wa Kristo haukuwa unatosheleza bila kanisa, yaani hali ya kustahili ya Wakatoliki wa Rumi kuhusu watakatifu.
2. Waaminio kama kanisa wanashirikishana mateso ya Kristo, (sio kwa kuwakilishwa), lakini kwa kufanya mapenzi ya Baba katika ulimwengu ulioanguka (kama vile Mathayo 5:10-12; Marko 10:39; Yohana 16:1 na kuendelea; 2 Wakorintho 4:10; Wagalatia 2:20; Wafilipi 3:10)
3. Kristo anateseka na waaminio (kama vile Mdo 9:4-5; 2 Kor 1:5; Isaya 63:9)
4. Mateso yanahitajika kwa ajili ya kukua (kama vile Waebrania 5:8)
5. Lazima tutimize "maumivu ya kuzaliwa" kwa kizazi kipya (kama vile Marko 13:8)
6. Paulo alikuwa anakataa kukamata tungo za walimu wa uongo

Neno hili kwa "mateso" halikuwahi kutumika katika Agano jipya kwa kifo cha Yesu msalabani. Muktadha wa Wakolosai 1:13-18 kabisa kabisa linafuta #1! Napenda #5 zaidi!

▣**"kanisa"***Ekklesia* ilitoka katika maneno mawili ya Kiyunani, "nje ya" na "kuita." Inatumika katika Kiyunani cha lugha ya Koine kufunua aina yoyote ya mkusanyiko, kama mkutano wa mjini (kama vile Mdo 19:32). Kanisa lilichagua neno hili kwasababu lilitumika katika tafsiri ya Agano la Kale (tafsiri ya Kiyunani ya vitabu vitano vya Musa iliyoandikwa mapema kama 250 K.K kutoka katika Mkataba ya Alexandria, Misri). Neno hili lilitafsiri neno la kiebrania *qahal* lililokuwa likitumika katika tungo "kusanyiko la Israel" (kama vile Hesabu 20:4). Waandishi wa Agano Jipya lilieleza kwamba walikuwa walioitwa kwa mpango wa Mungu" ambao wangekuwa watu wa Mungu

katika siku zao. Hawakuona msingi wa kuvunja kati ya watu wa Mungu wa Agano la Kale na wao, watu wa Mungu wa Agano jipya. Waamini lazima waeleze kwamba kanisa la Yesu Kristo, sio walimu wa Kiyahudi wa kisasa ndio urithi wao wa kweli wa maandiko ya Aagano la Kale. Katika Waefeso, barua ya wengi, neno "kanisa mara nyingi lina maana ya kiulimwengu, lakini katika Wakolosai lina maana ya sehemu ndogo. Kanisa ni vyote kumaanisha watu wote wa Mungu na mtu mmoja mmoja na likimaanisha kusanyiko la nyumbani la waamini. Katika andiko hili Paulo kwa uwazi anamaanisha sehemu ya jumla ya kanisa. Mada maalumu: Kanisa katika Wakolosai 1:18

**1:25"nalifanywa Mhudumu"** Paulo anamaanisha kwa wito wake wa Kitume wa kuhubiri kwa Mataifa (kama vile Mdo 9:15; 22:21; 26:17; Warumi 1:5; 11:13; 15:16; Gal. 1:16; 2:7; Efe. 3:1-2, 8; 1 Tim. 2:7; 2 Tim. 4:17). Hata hivyo, Paulo alichukulia wito wake na karama kama mtumishi, mtumwa, wakili! Katika Biblia uongozi ni utumishi.

▣**"kulingana na uwakili kutoka kwa Mungu"** Waaminio wote ni mawakili au walioaminiwa kwa injili (kama vile 1 Kor. 4:1-5; Efe. 3:2,9; Tito 1:7; 1 Pet. 4:10). Paulo anatumia neno hili katika namna baadhi ya kadhaa.

1. Agizo la Kitume la kuhubiri Injili (kama vile 1 Kor. 9:17; Efe. 3:2; Kol. 1:25)
2. Mpango wa milele wa ukombozi (kama vile Efe. 1:10, 3:9; 1 Kor 4:1)
3. Mafunzo katika mpango wa ukombozi na mtindo wa maisha unaofuatana nao (kama vile 1 Tim 1:4)

**NASB "kwamba niweze kwa ukamilifu kufanya kazi ya kulihubiri neno la Mungu"**
**NKJV "kutimiza neno la Mungu"**
**NRSV "kulifanya neno la Mungu lijulinane kwa ukamilifu**
**TEV "kwa ukamilifu tukiitangaza ujumbe wake"**
**NJB "kwamba kuumaliza ujumbe wa Mungu"**

Hii ni sawa na mzizi wa neno "kujaza (*plēroō)* linalotumika katika Wakolosai 1:24. Kufungwa kwa Paulo na kuhubiri kulikuwa ni kutimiza kusudi la Mungu kwa Mataifa (kama vile Mdo 9:15-16; 22:21; 26:17; Warumi 11:13; 15:16; Gal. 1:16; 2:7; Efe. 3:2,8; 1 Tim. 2:7; 2 Tim. 4:17).

**1:26 "siri"** Angalia Mada Maalum katika Waefeso 3:3

▣**"yaliyokuwa yamefichwa toka zamani na vizazi"** Hii ni kauli tendwa timilifu ya hali ya kuendelea, ilikuwa na iliendelea kufichwa na Mungu (kuhusishwa) zamani. Siri hii iliwekwa siri kutoka (1) mataifa, (2) wayahudi, na (3) malaika (kama vile 1 Petro 1:12). Manabii walikuwa na kaufahamu kadogo sana juu yake, lakini hawakuwahi kujua kweli yote (kama vile Waebrania 1:1) tungo "zama na vizazi"ilitumika na wajuzi kumaanisha viwango vya malaika (*aeons*).

▣**"lakini sasa imedhihirishwaa kwa watakatifu Wake"** Hii ni Kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu wa kitenzi kinachomaanisha "kufunua vizuri," au "kuleta katika nuru" (kama vile Wakolosai 1:27; Warumi 3:21; 16:26). Kile kilichokuwa kimefichwa kimefunuliwa kwa ukamilifu. Injili inaelekea na iko wazi kwa wote, si waliochaguliwa wachache! Angalia Mada Maalum: Watakatifu katika Wakolosai 1:2.

▣**"utajiri wa utukufu"** Paulo mara kwa mara anatumia neno "utajiri" kufunua faida za injili (kama vile Kol. 1:27; 2:2; Efe. 1:7,18; 2:7; 3:8,16; Fil. 4:19)

▣**"Kristo ndani yenu"** inawezekana kisarufi kwamba hii inawezakuwa ilifasiriwa "Kristo kati yenu," ambayo ingemaanisha siri ya injili na sio Kristo akaaye ndani yetu. Hicho Kiyunani kinachopendekezwa, *en,* ni fasiri "kati" katika tungo iliyotangulia, "kati ya Mataifa." Hii inaonekana kukidhi vizuri muktadha.Kuna kuelea kati ya kazi ya Mwana na Roho. G. Campbell Morgan anasema jina bora kwa ajili ya Roho ni "Yesu mwingine." Ufuatao ni mlinganisho wa muhtasari wa kazi na vyeo vya Mwana na Roho.

**MADA MAALUM: YESU NA ROHO**

Kuna bubujiko kati ya kazi ya Roho na Mwana. G. Campbell Morgan alisema jina zuri la Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine" (hata hivyo, tofauti yao, utu wa milele). Ufuatao ni mlinganisho wa mhutasari wa kazi na wadhifa wa Mwana na Roho.

1. Roho aitwaye "Roho wa Yesu" au maelezo yanayofanana (kama vile Rum. 8:9; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11).
2. Wote wanaitwa kwa maneno sawa
   a. "kweli"
      1) Yesu (Yohana 14:6)
      2) Roho (Yohana 14:17; 16:13)
   b. "mwombezi"
      1) Yesu (1 Yohana 2:1)
      2) Roho (Yohana 14:16,26; 15:26; 16:7)
   c. "Mtakatifu"
      1) Yesu (Marko 1:24; Luka 1:35; Matendo 3:14; 4:27,30)
      2) Roho (Luka 1:35)
3. Wote hukaa ndani ya waamini
   a. Yesu (Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17;Kol. 1:27)
   b. Roho (Yohana 14:16-17; Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
   c. Baba (Yohana 14:23; 2 Kor. 6:16)
4. Kazi ya Roho ni kutoa ushuhuda juu ya Yesu(kama vile Yohana 15:29; 16:13-15)

**1:27 "utajiri wa utukufu wa siri hii kati ya mataifa"** Paulo ametumia "utajiri" mara kadhaa kufunua matendo ya neema ya Mungu na kukidhiwa kwa mwanadamu aliyeanguka (kama vile Kol. 1:27; 2:2; Warumi 2:4; 9:23;11:33; 2 Kor. 8:2; Efe. 1:7,18; 2:7; 3:16).

Mungu siku zote alikuwa na mpango wa kuunganisha Wayahudi na Mataifa katika wokovu (kama vile Waefeso 2:11-3:13). Mwanzo wa mpango wa ukombozi unaweza kuonekana katika

1. Ahadi ya Mungu katika Mwanzo 3:15, ambayo inahusisha watoto wote wa Adam
2. Wito wa Mungu kwa Ibrahimu ambayo angebariki watu wote (kama vile Mwanzo 12:3)
3. Wito wa Mungu wa ufalme wa Kikuhani kuwafikia ulimwenguni (kama vile Kutoka 19:5)
4. Hata hekalu la Sulemani ulikuwa na maana kwa Mataifa kutubu na kuamini na kuwa sehemu (kama vile 1 Wafalme 8:43, 60)
5. Rejea baadhi katika manabii (haswa Isaya) kwa utawala wa ulimwengu wa kimungu na mwaliko wa wanadamu wote

▣**"tumaini la utukufu"** Hii inamaanisha Siku ya Ufufuo wakati watakatifu watakapopokea miili ya utukufu wao mpya (kama vile 1Yohana 3:2). Uchaguzi, kustahilishwa, na utakaso utasababisha kutukuzwa (kama vile Warumi 8:29-30) angalia kidokezo kamili katika "utukufu" katika Waefeso 1:6

**1:28 "tunamtangaza yeye"** Ukristo kimsingi sio thiolojia sahihi, maadili ya kati, au utaratibu wa kidini, lakini uhusiano binafsi na Yesu. Mara unapothibitishwa, vipengele vingine vinakuwa na sehemu yake sahihi (kama vile 2 Timotheo 3:15, 16-17).

▣**"tukionya"** neno hili linatumika katika "mafunzo ya watoto" katika Tafsiri ya Agano la Kale (kama vile Ayubu 5:17). Katika Agano Jipya linatumika katika kuwaonya waamini wao kwa wao (kama vile Mdo 20:31; Warumi 15:14). Mara nyingi inabebwa na kidokezo chanya cha kuonya kuhusu tabia zisizopendeza za Wakristo (kama vile Wathesalonike 5:14; 2 Wathesalonike 3:15).

▣**"katika kila mtu"**tungo hii inatumika mara tatu katika mstari huu kwa msisitizo. Mjumuisho wake ni tofauti sana

kutoka katika kutojichanganya kwa walimu wa uongo. Injili ni kwa binadamu wote (kama vile Yohana 3:16; 1 Timotheo 2:4; 2 Petro 3:9).

▣**"kwa hekima yote"** Hekima ya Mungu ni tofauti kutoka katika kujitenga na usiri wa walimu wa uongo wayaitayo maarifa.

▣**"kwamba tupate kumleta kila mtu"** lengo la Mungu kwa kanisa ni kwamba kila mwamini akue katika Kristo (kama vile Kol. 4:12; Efe. 4:13; 1 Kor. 2:6; 14:20; Fil. 3:15). Hakuna vikundi maalum, vyeo, karama, maarifa, au upendeleo katika mwili wa Kristo, ni watumwa tu!

**NASB "iliyokamilika"**
**NKJV, NJB "kamilifu"**
**NRSV, TEV "iliyokua"**

Hili ni neno la Kiyunani *telos* (pia likitumika katika fasihi za wenye ujuzi katika karne ya pili), ambayo ilimaanisha "kuwezeshwa kwa ukamilifu kwa kazi uliyopewa" (kama vile Waefeso 4:12). Ilitumika katika

1. Mbavu zilizovunjika zikiponywa na kuwa za maana na kutumika tena
2. Nyavu za kuvulia zikishonwa na hivyo kuweza kuvua samaki
3. Meli zikifungwa na kamba na kuelekezwa katika safari baharini
4. Kuku waliokuwa wakubwa vya kutosha kuweza kupelekwa sokoni. Haimaanishi hali ya kutokuwa na dhambi, lakini ukuaji wenye tija ya kutenda kazi.

**1:29"najitaabisha, nikijitahidi"** maneno mawili yenye nguvu yaliyo sawa yanatumika kwa pamoja katika 1 Timotheo 4:10 kufunua huduma ya Paulo.

▣**"nikijishughulisha"** Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) endelevu ya wakati uliopo. Hii ni aidha neno la kimichezo (kama vile 1 Kor. 9:25; 1 Tim. 6:12; 2 Tim. 4:7) au neno la kijeshi (kama vile Kol. 2:1; Yoh 18:36). Tunapata neno la Kiingereza "mateso makali" (kuumia kwa maumivu makali moyoni) kutoka katika mzizi wa Kiyunani huu. Kazi ya kanisa si rahisi!

▣**"nguvu Zake ambazo kwa nguvu zinatenda kazi ndani yangu"** Hii ni Kauli endelevu ya kati ya wakati uliopo. Ni nguvu ya Mungu na sio ya waamini "inayotia nguvu" huduma zote (kama vile 1 Cor. 2; Eph. 1:19; 3:7, 20; Phil. 3:21; 1 Tim. 1:12) nomino hii na hali ya kuendelea ni mtindo wa mzizi mmoja wa Kiyunani unaomaanisha, "Nguvu yake inanitia nguvu mimi."

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mtoa maoni. Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Paulo anatumia utangulizi wa kawaida wa kati katika barua zake? Ni kwa namna gani ufunguzi huu ni tofauti?
2. Nani alianzisha kanisa hili? Nini kilikuwa dhumuni au ni ya Paulo kuandika barua hii?
3. Orodhesha sababau za Paulo kuwashukuru watakatifu hawa.
4. Orodhesha sehemu tatu za vipengele vya mapenzi ya Mungu (1:9)
5. Orodhesha vipengele vi nne vya maombi ya Pulo kama zinavyohusiana na "maisha yanayostahili" (1:10-12).
6. Orodhesha vitu ambavyo Paulo anavisema kuhusu Yesu (1:15-19; 2:9-10.
7. Kwanini Paulo anasisitiza kifo cha Yesu kwa nguvu sana?
8. Je mtu anaweza kuanguka kutoka katika hali ya neema (1:23; 2:16-23)?
9. Mstari wa 1:24 unamaanisha nini?
10. Toa maana ya siri?

# WAKOLOSAI 2

| MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS4** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Huduma ya Paulo kwa kanisa<br><br>(1:24-2:5) | Sio falsafa, lakini ni Kristo | Shauku ya Paulo kwa Wakolosai<br><br>(1:24-2:7) | Mwenendo wa Paulo kama Mtumishi wa kanisa<br>(1:24-2:3) | uhusika wa Paulo kwenye imani ya Wakolosai |
| | 2:1-10 | | | 2:1-3 |
| | | | 2:4-5 | 2:4-5 |
| Utimilifu wa maisha Katika Kristo katika | | | Utimilifu wa maisha katika Kristo | Ishi kutokana na imani ya kweli |
| | | | | Kristo, sio kutokana Na mafundisho ya Uongo |
| 2:6-15 | | Onyo kutokana na Mafundisho ya uongo | 2:6-7 | 2:6-7 |
| | | 2:8-15 | 2:8-10 | 2:8 |
| | | | | Kristo pekee ndiye Mkuu wa kweli wa Mwanadamu na Malaika |
| | | | | 2:9-10 |
| | Sio ushikiliaji wa sheria lakini Kristo | | | |
| | 2:11-23 | | 2:11-15 | 2:11-13 |
| | | | | 2:14-15 |
| | | | | Dhidi ya kujitenga Kwa uongo na |
| starehe | | | | |
| | | | | Kunakosimamia juu Ya kanuni za Ulimwengu huu |
| 2:16-19 | | 2:16-19 | 2:16-19 | 2:16-19 |
| Maisha mapya Katika Kristo<br>(2:20-3:17) | | | kufa na kuishi na Kristo | |
| 2:20-3:4 | | 2:20-23 | 2:20-3:4 | 2:20-23 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Kugawanya katika aya hakuna uvuvio, isipokuwa ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 2:1-5**
**1 Maana nataka ninyi mjue jinsi ilivyo kuu juhudi yangu niliyo nayo kwa ajili yenu, na kwa ajili ya wale wa Laodikia, na wale wasioniona uso wangu katika mwili; 2 ili wafarijiwe mioyo yao, wakiunganishwa katika upendo, wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua kabisa siri ya Mungu, yaani, Kristo; 3 ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika. 4 Nasema neno hili, mtu asije akawadanganya kwa maneno ya kuwashawishi. 5 Maana nijapokuwa sipo kwa mwili, lakini nipo pamoja nanyi kwa roho, nikifurahi na kuuona utaratibu wenu na uthabiti wa imani yenu katika Kristo.**

**2:1 "jinsi ilivyo kuu juhudi"** "Juhudi" ni neno la kiriadha au vita (k.v. Kol. 1 :29; 4:1 2). Hapa linatumika kama (1 ) sitiari kwa maombi ya kusihi au (2) kazi ya Paulo kwa niaba ya watu wa mataifa.

◙**"Laodekia"** Huu ni mji uliokuwa karibu, yapata mile 10 mbali na mji wa Kolosai, katika bonde lile lile (k.v. Kol. 4:1 3, 1 5,1 6; Ufu. 3:1 4). Inavyoonekana Epaphras alianzisha kanisa katika kila mji uliokuwepo katika bonde la Mto Lycus yaani Kolosai, Laodekia, na Hierapolis (k.v. Kol. 4:1 3). Barua hii ilitakiwa kusomwa kwa kila mmoja.

◙**"na wale wasioniona uso wangu katika mwili"** Paulo hakulianzisha kanisa hili hata yale mawili yaliyoko kwenye bonde la Mto Lycus. Lilianzishwa na Epaphras (k.v Kol.1:7). Na bado Paulo aliteseka kwa maombi kwa ajili yao. Paulo alilipenda kanisa na makanisa yote!

**2:2 "ili wafarijiwe mioyo yao"**Hiki ni kishazinia kikiwa na kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Linatoka kwenye mzizi ule ule kama wa neno "*paracletos,*" ambalo linatumika kwa Roho Mtakatifu katika Yohana 1 4:1 6,26; 1 5:26; 1 6:7 na Yesu katika 1 Yohana 2:1. Maana yake ya msingi ni "kuitwa kwa hitaji la msaada na kutiwa moyo."Ilikuwa ni sitiari toka kwenye muundo wa kisheria wa Kirumi; dhana ya mwanasheria wa utetezi ulitokana na neno hili.

**MADA MAALUM: MOYO**

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani na Agano Jipya kuashiria neno la Kiebrania lēb (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile. Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*,, 2nd ed. kur. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile. Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)

a. Mungu anatujua mioyo (kama vile. Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani,uwezo wa kufikiri, kama vile. Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)
4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa,kama vile.Matendo 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile. Mt. 5:28; Matendo 2:26,37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
1. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani,Kristo katika mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejerea mtu (kama vile. Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.
a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
e. Ezek. 36:26, "moyo mpya" dhidi ya "moyo wa jiwe" (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

◙**"wakiunganishwa"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya muunganiko wa neno *syn*. Ilitukimika katika tafsiri ya Kiyunani ya agano la kale kwa ajili ya kutoa"maelekezo"(k.v. Isa. 40:1 3; 1Kor. 2:1 6). Katika maandishi ya Paulo ilitumika kama sitiari ya mwili kukua kuelekea katika ukomavu (k.v. Kol. 2:1 9; Efe. 4:1 6). Makuzi haya na umoja yanawezekana (irabu tendwa) tu katika Kristo, katika Roho na katika upendo. Umoja ulikuwa wa muhimu sana kwenye hali ya upotofu wa kiimani (k.v Efe. 4:1-6).

**NASB "utajiri wote"**
**NKJV,NRSV "ufahari wote"**
**TEV "wingi wa utajiri"**
**NJB "wao ni mafahari"**

Mara nyingi Paulo alitumia neno hili"utajiri" kuelezea upendo wa Mungu ulioko katika Kristo (k.v. Rum. 2:4, 9:23; *1 1 :1 2, 33; Efe. 1 :7, 1 8; 2:7; 3:8, 1 6; Fil. 4:1 9; Col. 1 :27; 2:2). Waumini ni matajiri kiroho (k.v. Yakobo 1 :9) kwa* sababu ya utajiri wa Mungu na ukarimu ulioko katika Kristo (k.v. 2 Kor. 8:9; 9:1 5). Hapa "utajiri ("hazina zote,"k.v. Kol. 2:3) ni uelewa wa waumini juu ya injili, zuio la muda na ufikiri kuhusu karama ya ufunuo!

◙**"wapate kufahamu kwa uhakika"** Paulo anaendelea kutumia maneno na dhana iliyotumiwa na walimu wa uongo wenye kudai kuwa na ujuzi wa pekee. Katika kifungu hiki, neno"uhakika"ni muunganiko wa neno *plērōma,* ambayo ni mapotoe yaliyotumika kurejerea kwenye ngazi za kimalaika. Neno "ufahamu" (*sunesis*) pia ni muunganiko wa neno *syn.*linahusianishwa na neno plērōma katika Kol. 1 :9. Asili yake ya neno ni ujio wa pamoja wa mtiririko wa fikra. Hawa walimu wa uongo walikuwa wakijaribu kuufanya Ukristo upate kueleweka, uwe wa muhimu na uweze kutumika katika jamii za Kiyunani na tamaduni zao. Msukumo wa aina moja uliwavuta wale wenye imani potofu kuilazimisha injili kuwa katika fikra za muundo wa kileo.

◙ **"maarifa ya kweli"** tena hili lazima litazamwe dhidi ya msisitizo wa walimu wa ungo wanaorudi nyuma na kudai kuwa na "siri" ya maarifa ya ndani kuhusiana na wokovu. Kwa Paulo, "maarifa ya kweli" (*epignōskō*) yanapatikana tu kwenye injili ya Yesu, ambaye ndio "fumbo la Mungu."

**NASB,NKJV**
**NRSV "fumbo"**
**TEV "siri ya kweli"**

**NJB "sababu iliyofichika kwa ajili ya haya yote"**

Mungu analo kusudi la pamoja kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (k.v. Efe. 2:1 1 -3:1 3) kwamba hata awe kitangulizi cha anguko (k.v. Mwanzo 3). Dokezo la mpango huu limefunuliwa katika Agano la Kale (k.v. Mwa. 3:1 5; 1 2:3; Kut. 1 9:5-6 na vifungu vya wote katika manabii). Hata hivyo, agenda hii nzima bado haikuwa wazi mpaka kwenye ufunuo wa injili ya Yesu Kristo (k.v. 1 Kor. 2:1 -8). Kwa ujio wa Yesu na Roho palianza kuwa dhahiri. Paulo alitumia neno "siri"kuelezea mpango wa pamoja wa ukombozi (k.v. 1 Kor. 4:2; Efe. 6:1 9; Kol. 4:3; 1Tim. 3:9). Angalia mada maalumu katika Efe. 3:3.

◙ **"moyo"** Tazama mada maalumu: Moyo katika Kol. 2:1 .

**NASB "*yaani,* Kristo"**
**NKJV "yaani, Kristo mwenyewe"**
**NRSV "wote Baba na Kristo"**
**TEV "ambaye ni Kristo mwenyewe"**

kuna tofauti nyingi juu ya machapisho ya Kiyunani. Usimamiaji wa maneno kisarufi usio wa kawaida wa P46, "wa Mungu, wa Kristo," unaelezea vizuri asili ya tofauti zingine zote (k.v. Appendix Two, II. B. 1 -6). Siri ya Mungu ni Kristo-maisha yake, mafundisho, kifo, ufufuko, kupalizwa na ujio wa pili! Siri ya umilele wa Baba, mpango wa pamoja wa ukombozi ulianzishwa na Mwana mwenye mwili wa kibinadamu. Tazama mada maalum:Siri katika Maandiko ya Paulo katika Efe. 3:3

**2:3 "katika Yeye kumefichwa hazina zote za hekima na maarifa"** Mstari huu unakanusha msisistizo wa walimu wa uongo na kukuza ubinadamu wa Kristo. Siri ya Mungu (ufunuo) ni mtu. Mpango wa Mungu ni mtu (k.v. NASB, NKJV, NRSV, TEV), na wokovu wa Mungu ni mtu, na sio maarifa ya mwanadamu au bidii. Inawezekana kisarufi kuwa kifungu hiki cha ufunguzi ni tasa ("katika hilo") na sio jinsia ya kiume ("katika yeye") na kwa hiyo, rejea kwenye siri (k.v NJB).

**2:4 "mtu asije akawadanganya katika maneno ya kuwashawishi"** Hiki kishazinia kikiwa na kauli ya kati (shahidi) tegemezi ya wakati uliopo. Kitenzi hiki kilitumika katika namna mbili: (1 ) kupotosha au kudanganya mtu (k.v Yakobo 1:22) na (2) kufikiria vibaya, kulaghai, au potosha. Udanganyifu huu ulifanyika kwa namna ya ushawishi, hoja zenye kubadilika, na/ au hotuba yenye kushawishi. Walimu wa uongo mara zote wana mantiki, wanavutia, wanashawishi (wako tofauti na Paulo k.v 1 Kor. 2:1-5).

**2:5 "ingawa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo na kusudi la kifasihi la mwandishi. Inaonyesha dhahili Paulo hakuwa nao katika hali ya kiuhalisia, lakini aliwaombea na kuwaza juu yao.

◙ **"hakuwa nao kimwili"** kikawaida "hakuwa nao katika hali ya kimwili."Tazama mada maalum: Mwili (*sarx*) katika Kol. 1 :22.

◙ **"nipo pamoja nanyi kwa roho"** Moyo wa Paulo na maombi muda wote vilikuwa pamoja mahali pa ufalme wa Mungu palipotengwa, padogo na penye mateso! Hapa neno "roho"linarejelea juu ya mwanadamu wa kweli pekee. Maelezo haya ya pamoja yanatumika katika 1 Kor. 5:3.

**NASB "utaratibu wenu......uthabiti"**
**NKJV "utaratibu mzuri.......uthabiti"**
**NRSV "uadilifu.....uimara"**
**TEV "mkithibitiana kwa kusimama pamoja"**
**NJB "ikiwekwa vizuri.....thabiti"**

Haya ni (1) maneno ya kijeshi kwa ajili ya mfumo na uthabiti (k.v. Efe. 6:1 0-1 7) au (2) maneno ya ujenzi kwa ajili ya msingi wenye uhakika, imara (k.v. 2 Tim. 2:1 4-1 9; 1 Petr. 5:9). Maneno haya yanaelezea imani ya waamini wa Kikolosai hata katikati ya mashambulizi na mkanganyiko wa walimu wa uongo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 2:6-7**
**6 Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; 7wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani.**

**2:6 "kama mlivyompokea Kristo"** Kitenzi kilichotumika hapa (*paralambanō*, kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu) ina vidokezo viwili.

1. Ukaribishaji wa mtu (k.v. Mat. 1 :20; Yoh. 1 :1 1 ; 1 4:3
2. Upokeaji wa "desturi"(k.v. 1 Kor. 1 1 :23; 1 5:1 ,3; Gal. 1 :9,1 2; Fil. 4:9; 1 Thes. 2:1 3; 4:1 ; 2Thes. 3:6)

Wakolosai walisikia maudhui ya injili kupitia mahubiri ya Epaphres; baadaye kibinafsi wakamkaribisha mtu wa injili (Yohana 1 :1 2). Imani ya Kibiblia ni agano. Mungu akaweka agenda na kufanya mawasiliano kwanza (k.v. Yoh. 6:44,65), lakini kibinafsi lazima uitikie kwa toba, imani, utii, na ustahimilivu (Kol. 2:6)! Ujumbe wa walimu wa uongo ulibadili thiolojia kote kwenye maudhui na mtu wa injili.

◙ **"Kristo Yesu"** "Yesu ni Bwan"ulikuwa ni ukiri wa wazi wa imani kwenye ubatizo (k.v. Rum. 1 0:9-1 3; 1 Kor. 1 2:3; 2 Kor. 4:5; Fil. 2:1 1 ). Ulikuwa ni uthibitisho wa kuwa Yesu wa Nazareti ni Masihi yule wa agano la kale na mwenye umbo la Uungu (k.v. Fil. 2:6-1 1 ).

◙ **"*enendeni* hivyo hivyo katika Yeye"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Ukristo sio kanuni ya imani ya kithiolojia tu; pia ni imani ya mtindo wa maisha ("enenda" k.v. Kol. 1 :1 0; Efe. 4:1 ,1 7; 5:2,1 5). Wokovu sio kitu cha waumini wanachokimiliki bali ni mtu yule anayewamiliki! Hapa Paulo anaangazia juu ya sura binafsi ya imani ya Mkristo kama inavyofanya injili ya Yohana (k.v. Yoh. 1 :1 2; 3:1 6; 6:40; 1 1 :25-26).

**2:7** Mstari huu una kauli nne endelevu (zilizotumika kama zenye kushurutisha) ambazo zinaelezea mwenendo unaostahili (k.v. Kol. 2:6):

1. **"wenye shina"** Hii ni kauli tendwa timilifu ambayo ni hali ya kuwa imetimilizwa iliyotolewa na Mungu. Haya maelezo ya sitiari ya elimu ya kilimo yalikuwa ya kipekee kwa Wakolosai na Waefeso (k.v. Kol.3:1 7).
2. **"wenye kujengwa katika Yeye"** Hii ni kauli tendwa ya wakati uliopo ambayo ni ya hali endelevu iliyotolewa na Mungu. Mara nyingi Paulo alitumia hii sitiari ya kiujenzi kuwaelezea watu wa Mungu (k.v. 1 Kor. 3:5; Efe. 2:20, 22). Yaweza kurejelea kwa watakatifu kama hekalu (kibinafsi, 1 Kor. 6:1 9 na kiushirika, 1 Kor. 3:1 6).
3. **"mmefanywa imara kwa imani"** Hii kauli tendwa ya wakati uliopo nyingine yenye hali ya kuendele iliyotolewa na Mungu. Nomino ("uthibitisho") inapatikana katika Fil. 1:7; na Ebr.6:16. Kitenzi kinadokeza "kuthibitisha" (k.v. 1 Kor. 1 :6,8; 2 Kor. 1 :21 ), "kuimarisha," na "kuhakikisha"mara nyingi kwa hoja (k.v. Rum. 1 5:8, 1 Kor. 1 :8). Kifungu hiki"kwa imani yako" kinaweza eleweka kama (1 )imani ya kudhahania, ukiamini katika Kristo au (2)imani isio na upendeleo, mafundisho kuhusu Kristo (k.v. Yuda 3, 20).
4. **"mkizidi kutoa shukrani"** Hii ni kauli tendaji ya wakati uliopo yenye hali ya kuendelea iliyotolewa na Mungu. Maisha ya Mkristo ni maisha ya shukrani kwa Mungu kwa neema yake katika Kristo. Hili linaelezewa katika hali ya utii wa furaha na ustahimilivu! Kuifahamu injili ni kufurahia katika furaha isiyoelezeka (k.v. Kol. 1 :1 2) na kuishi maisha yanayostahili (k.v. Kol. 1 :1 0-1 1 ) ukiwa na shukrani (k.v. Kol. 3:1 7). Tazama Mada Maalum: Sheheni (*Perisseuō*) katika Efe. 1 :8.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 2:8-15**
**8Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo.9Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. 10Na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka. 11Katika yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa kuuvua mwili wa**

**nyama, kwa tohara ya Kristo. [12] Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu.[13]Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote; [14]akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani; [15]akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.**

**2:8-15** Hii ni sentensi ndefu, mtu anaendeleza uwasilishaji katika Kiyunani.

**2:8**
**NASB, NRSV**
**TEV "angalieni"**
**NKJV "angalia"**
**NJB "hakikisheni"**

Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Wakristo lazima waendelee kulinda uhuru wao katika Kristo toka kwa walimu wa uongo wakati wakitoa kwa nduguze waliodhaifu (k.v. Rum. 1 4:1 -1 5:1 3; 1 Kor. 8; 1 0:23-33).Mara nyingi ni vigumu kuongea tofauti kati ya makundi haya mawili. Walimu wa uongo wanapotosha ukweli, wakati ndugu walio dhaifu wanatetea upendeleo.

◙ **"mtu asiwafanye mateka"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo hasi. Neno hili la Kiyunani la nguvu limetumika tu mahali hapa katika agano jipya, likimaanisha(1) kuteka (2) kushawishi (2 Tim. 3:6), au (3) kuchukua kama mtumwa. Walimu wa uongo mara zote wanataka kudhibiti!

◙**"kutokana na elimu yake"** Hii sio hukumu ya mwanadamu juu ya kufikiri kimantiki. Wanadamu wameumbwa kwa sura ya Mungu na lazima wamwabudu Yeye na viumbe vyao vyote, ukijumuisha na fikra zao (Kumb. 6:5; Mat. 22:32; Mark 1 2:29-30; Luk. 1 0:27). Huku ni kukataliwa kwa thiolojia/elimu ya kimtazamo ya walimu wa uongo (k.v. Kol. 2:23; 1 Kor. 1 :26-2:8; Efe. 4:1 3; 5:6; 1 Tim. 6:20).

◙**"madanganyo matupu"** Neno hili laweza kutafasiliwa "danganya, udanganyifu, au kulaghai" (k.v. Mt. 1 3:22; Efe. 4:22; 2 Thes. 2:1 0; Ebr. 3:1 3). Walimu wa uongo ni waaminifu, lakini wamedanganyika!

◙ **"kutokana na"** Hili ni neno la Kiyunani *kata*. Limerudiwa mara tatu kuelezea “elimu na madanganyo matupu”

1. **"kwa desturi za watu"** Wingi wa udini wa mwanadamu ni wa kiutamaduni, na sio Kibiblia (k.v. Isa. 29:1 3; Kol. 2:23). Mara nyingi tunapitia juu ya yale tuliopokea bila kuangalia Biblia kwa ajili yetu!
2. **"sio kutokana na Kristo"**Linatokana na fikra za mwanadamu, uzoefu, au mtizamo.
3. **"kanuni za msingi"** Mara nyingi maneno yanaanza kawaida, kwa maana halisia ya mwendelezo wa kisitiari. Neno hili (*stoicheia*) kiasili linarejea kitu kilichoko kwenye safu, mlolongo. Kinakua ndani ya vidokezo vingi:
   a. Msingi wa ujenzi wa dunia (hewa, maji, ardhi, na moto, k.v. 2 Petr. 3:1 0, 1 2).
   b. Mafundisho ya msingi ya somo (k.v. Ebr. 5:1 2; 6:1 kwa dini ya Kiyahudi).
   c. Nguvu ya kimalaika mbali na miili ya mbinguni (k.v. I Enoch 52:8-9; kasisi wa kanisa la mwanzo; Kol. 2:8, 20; 1 Kor. 1 5:24) au ngazi ya kimalaika (*aeons*) ya walimu wa uongo wenye ujuzi (k.v. Kol. 2:1 0, 1 5; Efe. 3:1 0).
   d. Malaika wenye uadui na wanadamu walijaribu kuzuia utoaji wa sheria kwa Musa (k.v. Mdo. 7:38; Ebr.2:2)
   e. Yumkini miundo isiokuwa ya kibinadmu kwa ulimwengu wetu ulioanguka ulioruhusu mwanadmu aliyeanguka kuonekana huru toka kwa Mungu (elimu, serikali, madawa, dini, n.k. (k.v. Gal. 4:3, 8-9 na Hendrik Berkhof's *Christ and the Powers* by Herald Press, uk. 32).

◙ **"wala si kwa njia ya Kristo"** Huu ulikuwa utumiaji mwingine wa neno *kata*. Tatizo ya elimu ya kidunia ni

kwamba inaelezea ukweli kwa kiwango kuliko ufunuo wa Mungu, injili ya Yesu Kristo. Ni uvumbuzi wa kibinadamu, na sio ufunuo wa ki-Ungu.

**2:9 "katika Yeye"** Kifungu hiki kipo katika nafasi ya msisitizo. "katika Yeye"kilikuwa ni kifungu muhimu katika thiolojia ya Paulo ("kwake Yeye" Kol. 2:3; " katika Kristo" Kol. 2:5; "katika Yeye" Kol. 2:6,9,1 0,1 1 ; "pamoja na Yeye" Kol. 2:1 2, 1 3). Tambua, pia, Efe.1 :3,4,7,9,1 0,1 2,1 3,1 4). Paulo anarudia tena thiolojia inayomhusu Kristo kama alivyofanya katika Kol. 1 :1 5-20. Hili ni suala muhimu na suala muhimu ni Mtu!

◙ **"utimilifu wote wa Mungu"** Dhana hii ya pande mbili kuhusu asili ya Kristo iliwakanusha walimu wa uongo, (k.v. Kol. 1 :1 5-20). Walikubali kuwa alikuwa Mungu kamili, lakini wakapinga kuwa hakuwa mwanadmu kamili (k.v. 1 Yoh. 1 na 4:1 -3). Neno "utimilifu" *(plērōma)* lilikuwa ni neno la ujuzi wa kipekee kwa ngazi ya kimalaika (*aeons*) kati ya mungu mwema mkuu na maada ovu (k.v. Yoh. 1 :1 6, Kol. 1 :1 9, Efe. 1 :23, 3:1 9; 4:1 3). Neno hili la kudhahania kwa "uungu"(*theotās*) limetumika mahali hapa tu katika agano jipya. Yesu ni ufunuo kamili wa Mungu, sio kwa ngazi ya kimalaika (*aeons*) au maarifa ya siri ya walimu wa uongo. Yawezekana kuwa hii ilikuwa moja ya maneno muhimu ya walimu wenye ujuzi. Mara nyingi Paulo analitumia istilahi kumwelezea Kristo.

◙ **"unakaa"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo. Baadhi ya walimu wa uongo wenye ujuzi waliamini kuwa "roho ya Kristo"ilimwijiia Yesu kwa muda muafaka . mstari huu unadai kuwa asili mbili za Yesu zilikuwa ni muungano wa moja kwa moja.

◙**"kwa jinsi ya kimwili"** Huu ndio ulikuwa ukweli kwamba waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee wasingaliweza kuthibitisha kwa sababu ya pande mbili za Kiyunani kati ya mungu mwema na maada zilizo ovu. Ni la muhimu katika maisha ya Kikristo (k.v. 1 Yoh. 4:1 -3).

**2:10 "nanyi mmetimilika"** Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea ya neno *plerōma* (k.v. Kol. 2:9; Yoh.1 :1 6; Efe. 3:1 9). Wakiristo wamekuwa na wanaendelea kujazwa na Yeye na kwa ajili yake! Yesu ametufanya kuwa kamili!

◙**"aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka"** Hii inarejelea kwa mtazamo wa walimu wenye ujuzi wa uongo juu ya wokovu. Kwao wokovu ulijumuishwa katika maarifa ya siri (neno la siri au jina la siri) yaliyowaruhusu kupita ulimwengu wa kimalaika kati ya maada(dunia) na roho wa Mungu (Mungu, k.v. Kol. 1 :1 6; 2:1 5; Efe.1 :22-23; 3:1 0; 6:1 2). Paulo anadai kuwa wokovu u kwake Kristo. Yeye ndiye kichwa cha ulimwengu wote wa kimalaika/ mapepo (k.v. Rum. 8:38-39)! Tazama Mada Maalum: Malaika katika maandiko ya Paulo Efe. 6:1 2. George Ladd's *A Theology ofthe NewTestament*, ana aya inayofurahisha kuhusu istilahi za Paulo:

> "Usomaji wa lugha ambayo Paulo anaitumia kudhihilisha hizi roho za kimalaika unashauli kuwa Paulo kwa makusudi alitumia istilahi isio dhahiri na zinazotofautiana. Hili linaonekana hasa katika mabadiliko yake kati ya miundo ya hali ya umoja na uwingi kwa maneno kadhaa. Ni vigumu kiufanisi kuweka pamoja istilahi hizi katika maelezo ya utaratibu mzuri wa viumbe vya kimalaika, wala kwa uzuri kuwa kwa maneno tofauti Paulo anakusudia kudhihilisha aina tofauti au ngazi za malaika. Yumkini Paulo alikuwa anakabiliana na maoni yanayoelezea utaratibu tofauti wa malaika, na alikusudia kwa lugha yake tosherevu yenye kunyumbulika, ambayo kiwastani ingeitwa ya kiishara, kudai kuwa nguvu zote za giza, ki vyovyote zitakavyokuwa iwe kibinadamu au sio kibinadamu, zimeletwa katika usaidizi kwa kifo na kumwinua Kristo na hatimaye kuangamizwa kupitia utawala wake wa kimasihi"(uk.402). kwa ajili ya "mamlaka"tazama Mada Maalum katika Kol. 1:16

**2:11 "mmetahiriwa kwa tohara"** Paulo anatumia alama za agano la kale (k.v. Mwa. 1 2:8-1 4) katika maana ya kiroho (k.v. Kumb. 1 0:1 6; 30:6; Yer. 4:4; Rum. 2:28-29; Fil. 3:3). Hii yawezakuwa ni lugha ya kitamathali au zaidi walimu wa uongo wenye tabia za kiuyahudi. Kuna mengi yasiotambulika na kujulikana kuhusu makundi ya upotoshaji ya agano jipya. Kwa namna fulani walimu hawa wa uongo ni muunganikano wa wale wenye ujuzi wa Kiyunani na washikiliaji sheria wa dini ya Kiyahudi (k.v. Kol. 2:1 1 ,1 6,1 8). Mtoa maoni mwepesi anadai kuwa walifanana na wale watu wa Esene (jamii ya kule kwenye magombo ya bahari ya chumvi ambako kulikuwa na kundi la utenganishaji la madhehebu ya Kiyahudi la karne ya kwanza lililoishi jangwani).

◙**"tohara isiyofanyika kwa mkono"** Huu ni utumiaji wa kiistiari wa tohara kama alama za agano katika agano la kale. Tohara "mpya" ni roho mpya na uhusiano mpya na Mungu kupitia Kristo (k.v.Rum. 2:28-29; Fil. 3:3). Hata katika agano la kale wakati agano jipya linajadiliwa (k.v. Yer. 31 :31 -34 na Ezek.36:22-38), tohara hata haikuweza tamkwa, ilisisitizwa kwa kiasi kidogo.

◙ **"kwa kuuvua mwili wa nyama"** Hii inarejea juu ya asili ya kale ya anguko, na sio mwili wa asili (k.v.Rum. 6:6; 7:24; Gal. 5:24; Kol. 3:5).

**2:12 "tukizikwa naye katika ubatizo"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita ya muunganiko wa neno *syn* yenye kumaanisha "kuzikwa pamoja."Hii ni sitiari ya ubatizo ya mfanano wa uzikaji kwenye mazishi (cf. Rom. 6:4). Kama waumini wanavyogawana maumivu ya Yesu, kifo na mazishi, pia watagawana ufufuko wake na utukufu (k.v Kol. 2:1 2b; Rum. 8:1 7; Efe. 2:5-6). Kwa ubatizo wa Paulo ilikuwa njia ya kudai mauti katika maisha ya kale (mtu wa kale) na uhuru wa maisha mapya (kiumbe kipya, k.v 2 Kor.5:17; Gal. 6:15) ya kumtumikia Mungu (k.v. Rum. 6:2-1 4; 1 Petr. 2:24).

◙ **"pia mlifufuliwa pamoja naye"** muunganiko huu ukiwa na neno *syn* unafanana na ule"mkiwa mmezikwa pamoja" (k.v.Kol. 2:1 3; 3:1 ; Rum. 6:4-5; Efe. 2:6). Mazishi ya waamini na ufufuo vinaunganishwa kama pande mbili za tukio kamili. "Walizikwa pamoja" na "kufufuka pamoja"katika Efe. 2:5-6, pia, utumiaji wenye muunganiko wa neno syn unaomaanisha "kuwa na ushikirishaji wa pamoja."

◙ **"aliyemfufua katika wafu"** Yesu ni tunda la kwanza la ufufuo (k.v. 1 Kor. 1 5:20,23). Roho iliyomfufua vile vile itawafufua waamini (k.v. Rum. 8:1 0-1 1 , 23). Kifungu hiki ni chenye fursa nzuri ya kuonyesha kuwa Agano Jipya mara nyingi ndio sababu ya kazi ya ukombozi kwa watu watatu wa Uungu.

1. Mungu Baba akamwinua Yesu (k.v. Mdo 2:24; 3:1 5; 4:1 0; 5:30; 1 0:40; 1 3:30,33,34,37; 1 7:31 ; Rum.6:4,9)
2. Mungu Mwana akajiinua mwenyewe (k.v. Yoh. 2:1 9-22; 1 0:1 7-1 8)
3. Mungu Roho akamwinua Yesu (k.v. Rum. 8:1 1 )

Msisitizo huu wa ki-Utatu unaweza onekana katika Kol. 2:9-1 0.

**2:13 "mlipokuwa wafu"** Hii ni kauli endelevu ya wakati uliopo yenye maana "mkiisha kufa."hii inaaksi matokeo ya anguko la kifo cha kiroho (k.v. Mwa. 3; Rum. 5:1 2-21 ; Efe. 2:1 -3). Watu wa mataifa walikuwa wadhambi waliotolewa toka kwa watu wa agano (k.v. Efe. 2:1 1 -1 2). Biblia inazungumzia juu ya hatua tatu za mauti.

1. Kifo cha kiroho (k.v. Mwanzo 3; Isa. 59:2; Rum. 7:1 0-1 1 ; Efe. 2:1 ; Yakobo 1 :1 5)
2. Kifo cha asili,(k.v Mwanzo 5)
3. Kifo cha milele, "mauti ya pili,""ziwa la moto" (k.v. Ufu. 2:1 1 ; 20:6,1 4; 21 :8)

◙ **"kutokutahiriwa kwa mwili wenu"** Ilikuwa ni njia ya kuwarejelea watu wa mataifa (k.v. Col. 2:1 1 ).

◙**"Yeye"** Hii inamrejea Baba. Kama ndivyo, kiwakilishi nomino kupitia Kol. 2:15 inamrejerea Baba.

◙ **"aliwafanya muishi pamoja na Yeye,"**Kuna muunganiko aina tatu wa neno *syn* katika Kol. 2:1 2-1 3 (kuzikwa pamoja, Kol.2:1 2; fufuliwa pamoja, Kol. 2:1 2; na kuwafanya hai, Kol. 2:1 3) kinachoonyesha kile ambacho kimekwisha tokea kwa waamini kiroho (wakati uliopita usiotimilifu). Hili linafanana na Efe. 2:5-6. Katika Waefeso Mungu alitenda kwa niaba ya Yesu katika Efe. 1 :20 na Yesu alitenda kwa niaba ya waumini katika Efe. 2:5-6.

◙ **"akisha kutusamehe makosa yote"** Hii ni kauli ya kati (shahidi) yenye hali ya kuendelea. "Mmesamehewa" linatokana na mzizi ule ule wa neno "neema" (k.v. Rum. 5:1 5, 1 6; 6:23; 2 Cor. 1 :1 1 ; Col. 3:1 3; Efe.4:32). Tambua Mungu anasamehe bure dhambi "zote" kupitia Kristo (isipokuwa wasioamini)!

**2:14**
**NASB "akiisha kuifuta ile hati ya mashitaka"**
**NKJV "mkiisha kufutiwa hitaji la mashitaka yenu"**
**NRSV "mkifutiwa kumbukumbu zenu"**
**TEV "mkiisha kufutiwa kumbukumbu za mashitaka yenu"**
**NJB "akiisha kuzifuta kumbukumbu za mashitaka yetu katika sheria"**

Hii lugha ya mafumbo yumkini inahusiana kwa namna fulani kwa walimu wa uongo. Inarejea kwenye agano la Musa (k.v. Efe. 2:1 5, ambayo ingaliweza kuainishwa kama “tenda na uishi”-“tenda dhambi na ufe” (k.v. Kumb. 27:26; Ezek. 1 8:4). Paulo kwa uwazi anafundisha juu ya utendaji dhambi wa mwanadamu (k.v. Rum. 3:9,1 9,23; 1 1 :32; Gal. 3:22). Kwa hiyo, agano la kale limekuwa hukumu ya kifo kwa wanadamu wote! Neno "hati" lilitumika kwa ajili ya (1 ) a signed IOU, (2)ukiri uliotiwa mkono, na (3)shitaka la kisheria. Agano la kale lilikuwa laana! Neno hili la Kiyunani lilitokana na neno la kiingereza “mwandiko binafsi.”

◙ **"akaiondoa isiwepo tena"** Hii ni kauli timilifu tendaji elekezi . kitenzi hiki cha aina moja kinatumika katika Yoh.1 :29 na 1 Yoh. 3:5 kurejerea uondoshaji wa dhambi.Yesu aliishi kwa hali ya chini na kutimiliza mahitaji ya agano la Musa. Alitenda kile ambacho hali ya dhambi, mwanadamu aliyeanguka asingeliweza kufanya. Kifo chake kilikuwa, hatimaye, sio kwa minajili ya dhambi ya kibinadamu, lakini akajakuwa dhabihu kamili (k.v Walawi 1-7) kwa dhambi. Akawa “laana”(k.v. Kumb. 21 :23) kwamba mwanadamu aweze kukombolewa toka kwenye laana ya sheri (k.v. Gal. 3:1 3)!

◙ **"wakimgongomelea msalabani"** Hii inarejelea kwenye moja ya (1 )ubao wa matangazo (2) gharama iliyowekwa juu ya mtu aliyesurubiwa. Msalaba (kifo cha Yesu) kiliukabiri uhasama wa sheria (sheria ya Agano la Kale, k.v. 2 Kor. 5:21 ).

**2:15**
**NASB, NKJV**
**NRSV "kuzivua enzi"**
**TEV "kuweka huru"**
**NJB "kuzivua"**

Hili ni neno adimu, kauli ya kati (shahidi) ya hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu. Msingi wa asili yake ya neno ulikuwa ni kuzivua nguo. Inaonekana kumaanisha “kuziweka mbali.”inarejerea kuichukua silaha toka kwa maaskari waliyokufa (cf. Arndt and Gingrich, *A Greek-English Lexicon ofthe NewTestament and OtherEarly Christian Literature*, uk. 82. Katika muktadha huu unahusiana ya maangamizi ya Uungu (Baba na Mwana) ya nguvu za ulimwengu wa kiroho ambazo zilikuwa na uadui na mwanadamu. Ushindi wa mwamini ni wa Mungu kupitia Kristo na kwa Roho. Kama kitenzi hiki adimu kinachotafsiliwa kama irabu ya kati hatimaye toleo ya Biblia ya TEV inaelezea fikra za “kujiweka huru mwenyewe toka kwenye nguvu ya watawala wa kiroho.”kama itatafasiliwa kama irabu tendaji hatimaye “inawavua enzi watawala” (k.v toleo la Biblia ya NASB)

◙ **"watawala na wenye mamlaka"** maneno haya yalitumiwa na wenye ujuzi (walimu wa uongo) kwa ngazi ya kimalaika (*aeons*, k.v. Col. 2:1 0; Efe. 1 :21 , 3:1 0; 6:1 1 -1 2; Rum. 8:38-39; 1 Kor. 1 5:24). Tazama Mada Maalum katika Kol. 1 :1 6 na Efe. 6:1 2.

**NASB "akifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akishangilia katika msalaba huo"**
**NKJV "akizifanya kichekesho kwa ujasiri, akishangilia juu yake "**
**NRSV "akizifanya mfano kwa ujasiri, akishangilia katika msalaba huo"**
**TEV "akizifanya kichekesho kwa ujasiri kwa kuziongoza kama mateka katika ushindi wake."**
**NJB "akazifanyia gwaride kwa ujasiri, nyuma yake akiushangilia msalaba"**

Usuri wa kihistoria kwa hili ulikuwa ni wa gwaride la ushangiliaji ndani ya Rumi kwa ajili ya ushindi wa mkuu wa

majeshi (k.v. 2 Kor. 2:1 4). Watumwa walipitishwa mbele yake wakiwa wamefungwa minyororo. Kwa kifo chake pale msalabani na ufufuko Yesu akayashinda (1) laana ya sheria na (2) uhasama wa nguvu za kimalaika. Kama ilivyo dhahili toka kwa watafasiri wa leo kwamba kiwakilishi nomino mwishoni mwa mstari kinaweza eleweka kwa namna mbili: (1) kwa ajili ya Kristo au (2) kwa ajili ya msalaba. Haina upande na wengi wa watafasiri wanahusianisha na ushindi wa Kristo dhidi ya namna ya kujidhabihu kwake kwa kifo.

**MADA MAALUM: VITA MBINGUNI**

Pamekuwapo na mjadala mrefu kuhusu tarehe ya makabiliano haya. Yesu anaonekana akitaja vita hii katika Luka 10:18 na Yohana 12:31. Lakini kwa kujaribu kuweka utaratibu wa mtiririko mzuri wa tarehe kuhusu tukio ni vigumu kabisa:

1. kabla ya Mwanzo 1:1 (kabla ya uumbaji)
2. katikati ya Mwanzo 1:1 na 1:2 (nadhari ya nafasi)
3. katika Agano la Kale baada ya Ayubu 1-2 (Shetani mbinguni)
4. katika Agano la Kale kabla 1 Fal. 22:21 (Shetani katika baraza la mbinguni)
5. katika Agano la Kale baada ya Zakaria 3 (Shetani mbinguni )
6. katika Agano la Kale baada ya Isa. 14:12; Ezek. 28:15 na II Enoch 29:4-5 (Wafalme waanzilishi walilaumiwa)
7. katika Agano Jipya baada ya majaribu ya Yesu (kama vile. Mathayo 4)
8. katika Agano Jipya wakati wa ujmbe wa sabini (niliona shetani akianguka toka mbinguni, kama vile. Luka 10:18)
9. katika Agano Jipya baada ya ushindi wa Yesu kuingia katika Yerusalem (mtawala wa ulimwengu huu anatupwa, kama vile.Yohana 12:31)
10. katika Agano Jipya baada ya ufufuo na kupaa mbinguni (kama vile. Efe. 4:8; Kol. 2:15)
11. wakati wa saa ya mwisho (kama vile. Ufu. 12:7, bila shaka kama tunapaswa kuiona tu kama vita ya milele kati ya Mungu na mwenyeji wa maovu)

kiurahisi tunapaswa kuvitazama kama vita vya ndani kati ya Mungu na wamiliki wa uovu; mtafaruku huu unakwenda kutimilizwa katika kushindwa kwa yule joka na wafuasi wake. Katika ufunuo 20 wameondolewa na kutengwa! Angalia Mada Maalumu:Kuanguka kwa Shetani na Malaika zake (Uf. 12:4)

◙**"akizifanya kuwa mkogo"** Tazama Mada Maalum hapo chini, aya ya pili.

**MADA MAALUM: UJASIRI (*PARRHĒSIA)***

Neno hili la Kiyunani ni muungno wa maneno "yote" (*pan*) na "" (*rhēsis*). Uhuru huu au ujasiri katika usemi mara nyingi una maana nyingine ya ushujaa katikati ya upinzani au ukataliwaji (kama vile Yohana 7:13; 1 The. 2:2).

Katika maandiko ya Yohana (limetumika mara 13) mara nyingi huonesha tangazo la wazi wazi (kama vile Yohana 18:20, pia katika maandiko ya Paulo, Kol. 2:15). Hata hivyo, wakati mwingine kwa maana ya kawaida ni "kwa uwazi" (kama vile Yohana 10:24; 11:14; 16:25,29).

Katika Matendo Mitume wanazungumzia ujumbe unaomhusu Yesu katika namna ile ile (kwa ujasiri) kama Yesu alivyozungumza kumhusu Baba na mipango na ahadi Zake (kama vile Matendo 2:29; 4:13,29,31; 9:27-28; 13:46; 14:3; 18:26; 19:8; 26:26; 28:31). Pia Paulo ilihitaji msaada wa maombi ambapo kwa ujasiri angeliweza kuihubiri injili (kama vile Efe. 6:19; 1 The. 2:2) na kuiishi injili (kama vile Flp. 1:20).

Tumaini la Paulo la mambo yahusuyo kifo, hukumu na pepo katika Kristo lilimpa ujasiri na kijiamini katika kuihubiri injili katika zama hizi za sasa za uovu (kama vile 2 Kor. 3:11-12). Pia alikuwa na iamani kwamba wafuasi wa Kristo wangefanya kazi kwa namna ya kufaa sana (kama vile 2 Kor. 7:4).

Kuna kipengele kimoja zaidi cha neno hili. Kitabu cha Waebrania kinatumia neno hili katika maana ya kipekee ya ujasiri wa mwamini, kumwendea Mungu na kuzungumza Naye (kama vile Heb. 3:6; 4:16; 10:19,35). Waamini wanakubaliwa na kwa ukamilifu na kukaribishwa katika ukaribu na Baba kupitia Mwana (kama vile 2 Kor. 5:21)!
Katika Agano Jipyali linatumika katika njia kadhaa.

1. imani, ujasiri, au moyo wa kujiamini inahusiana na
   a. wanaume (kama vile Matendo 2:29; 4:13,31; 2 Kor. 3:12; Efe. 6:19)

b. Mungu (kama vile 1 Yohana 2:28; 3:21; 4:12; 5:14; Ebr. 3:6; 4:16; 10:19)
2. kuzungumza wazi, dhahiri, au bila na utata (kama vile Marko 8:32; Yohana 7:4,13; 10:24; 11:14; 16:25; Matendo 28:31)
3. kwa kuzunza hadharani (kama vile Yohana 7:26; 11:54; 18:20)
4. muundo uhusianao (*parrhēsiazomai*) unatumika kuhubiri kwa ujasiri katikati ya mazingira magumu (kama vile Matendo 18:26; 19:8; Efe. 6:20; 1 The. 2:2)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 2:16-23**
**16 Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; 17mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo. 18Mtu asiwanyang'anye thawabu yenu, kwa kunyenyekea kwa mapenzi yake mwenyewe tu, na kuabudu malaika, akijitia katika maono yake na kujivuna bure, kwa akili zake za kimwili; 19 wala hakishiki Kichwa, ambacho kwa yeye mwili wote ukiruzukiwa na kuungamanishwa kwa viungo na mishipa, hukua kwa maongeo yatokayo kwa Mungu. 20 Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani, 21 Msishike, msionje, msiguse; 22 (mambo hayo yote huharibika wakati wa kutumiwa); hali mkifuata maagizo na mafundisho ya wanadamu? 23 Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika namna ya ibada mliyojitungia wenyewe, na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzizuia tamaa za mwili.**

**2:16-23** Mistari ya 1 6-23 ni yenye laana nzito ya ushikiliaji wa sheria za kidini katika maandiko ya Paulo. Wakati Paulo alipokuwa akishughulika na waamini “dhaifu”alikuwa mtu mpole (k.v. Rum. 1 4:1 -1 5:1 3; 1 Kor. 8-1 0), lakini wakati alipokuwa akiwahutubia wale washika sheria za dini waliojihesabia haki (yaani., walimu wa uongo) hakuafikiana nao. Hili la kujihesabia haki lilikuwa ni lile lililoleta laana toka kwa Yesu juu ya mafarisayo na waandishi. Paulo alitambua vizuri utendaji wa kibobezi wa dini. Alikabiliana na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (k.v Matendo 9) na kubadilisha kila kitu!
Palikuwepo na aina mbili za hawa waalimu wa uongo wenye ujuzi (1) wale waliodai wokovu ni kupitia maarifa ya siri na, kwa hiyo, haijalishi ni namna gani utaishi (upingaji wa kuwepo masharti/sheria) na (2) wokovu kupitia maarifa ya siri pamoja na muundo wa maisha wenye masharti (washika sheria).

**2:16**
**NASB "na mtu asitende mhukumiavyo"**
**NKJV "basi, mtu asiwahukumu ninyi"**
**NRSV "pasiwepo na mtu wa kuwahukumu"**
**TEV "pasiwepo mtu wa kuwafanyia maamuzi"**
**NJB "usiruhusu mtu akakushutumu"**

Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi, ikimaanisha kuzuia kitendo kilichoko kwenye mchakato. Hii inarejelea kwa (1) maada ya chakula (k.v 1 Tim. 4:3); (2) siku maalum (k.v. Rum. 1 4:5; Gal. 4:1 0); au (3) ibada ya hawa waliyeko ngazi ya kimalaika (k.v. Kol. 2:8,20).Kuna mfanano uliowazi kati ya Kol. 2:1 6 ("tenda kama hakimu wako") na Kol. 2:1 8 (tenda kama “mwamuzi"). Uwe mwangalifu juu ya ushikiliaji sana wa sheria za kidini ikiwa ni za Kiyahudi, Kiyunani, au za kisasa.

**MADA MAALUM: YAWAPASA WAKRISTO WAHUKUMIANE WAO KWA WAO**
Hukumu ni hakika (kama vile Mt. 12:36; Ebr. 9:27; 10:27; 2 Pet. 2:4,9; 3:7).
A. Yeye anayehukumu ni
1. Mungu (kama vile Rum. 2:2-3; 14:10,12; 1 Pet. 1:17; 2:23; Ufu. 20:11-15)
2. Kristo (kama vile Yohana 9:39; Mt. 16:27; 25:31-46; Mdo. 10:42; 17:31; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1)
3. Baba kupitia Mwana (kama vile Yohana 5:22-27; Mdo. 17:31; Rum. 2:16)

Hukumu sio somo zuri, lakini ni maudhui ya sasa katika Biblia. Imejikita katika misingi au miamba za kweli kibiblia.

1. Huu ni ulimwengu wa kimaadili ulioumbwa na Mungu mwadilifu (tunavuna tunachopanda, kama vile Gal. 6:7).
2. Uanadamu umeanguka; tumeasi.
3. Huu si ulimwengu ambao Mungu alikusudia uwepo.
4. Uumbwaji wote unaojielewa (malaika na wanadamu) tutatoa hesabu kwa muumbaji wao kwa zawadi ya uzima. Sisi ni mawakili.
5. Milele itaamuliwa kwa kudumu na matendo yetu na chaguzi tulizozifanya katika haya maisha.

B. Je Wakristo wahukumiane wao kwa wao? Jambo hili lazima lishughulikiwe katika namna mbili.

1. waamini wanaonywa wasije wakahukumiana wao kwa wao (kama vile Mt. 7:1-5; Luka 6:37,42; Rum. 2:1-11; Yakobo 4:11-12)
2. waamini waanaonywa kuwatathmini viongozi wao (kama vile Mt. 7:6,15-16; 1 Kor. 14:29; 1 The. 5:21; 1 Tim. 3:1-13; na 1 Yohana 4:1-6)

Baadhi ya vigezo kwa ajili ya tathmini sahihi inaweza kusaidia

1. tathmini lazima iwe kwa kusudi la kukiri (kama vile 1 Yohana 4:1 – "jaribu" ikiwa na mtizamo wa kuthibitisha; angalia Mada Maalum: Kujaribiwa [*peirazō* na *dokimazō*])
2. tathmini lazima ifanyike katika upole na unyenyekevu (kama vile Gal. 6:1)
3. tathmini lazima iweke shabaha kwenye upendeleo wa mambo ya kibinafsi (kama vile Rum. 14:1-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33)
4. tathmini lazima itambue wale viongozi walio na "sio weza kuvumilia kukosolewa" kutoka ndani ya kanisa au katika jamii (kama vile 1 Timotheo 3).

**2:17**
**NASB, NRSV "bali mwili ni wa Kristo"**
**NKJV "bali mwili ni wa Kristo"**
**TEV "kweli ni Kristo"**
**NJB "kweli ni mwili wa Kristo"**

Kuna tofauti kati ya “kivuri” (*skia*, Kol. 2:1 7a) "mwili" (*sōma*, hasa. "mwili," Kol. 2:1 7b).Ibada za kidini, moyo wa ibada, na siku maalum za kuabudu sio mbaya kwao isipokuwa litokee suala la ndani. Kristo, na sio utendaji wa kibinadamu katika eneo lolote, ni kitovu cha injili. Paulo aliona ibada za kidini na hitaji la utendaji wa kidini la walimu wa uongo kama kivuri cha uhalisia wa kiroho. Swali la kiufasiri ni nini maana ya “mwili wa Kristo”? nadharia mbili ni: (1) Filo wa Iskanderia na Yusufu wanatafasiri “mwili” kwa maana ya “mali” (NASB, NKJV) au "ukweli" (TEV), "kweli halisi ya kiroho katika Kristo" au (2) kweli ya kiroho imedhihilishwa katika kanisa ambao ni mwili wa Kristo (NJB, k.v. Rum. 1 2:4-5; 1 Kor. 1 0:1 7; 1 2:1 2,27).Mwandishi wa Kiebrania nae anatumia neno”kivuri” (*skia*, Kol. 2:1 7a) kulinganisha agano la Musa na agano jipya katika Kristo (k.v. Ebr. 8:5; 1 0:1).

**2:18**
**NASB "mtu asiwanyang’anganye thawabu yenu"**
**NKJV "mtu asiwanyang’anye ile thawabu yenu"**
**NRSV "mtu asiwaondolee haki yenu"**
**TEV "usiruhusu kulaumiwa na mtu yeyote"**
**NJB "usidanganywe juu ya thawabu yenu na yeyote"**

Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi, ikimaanisha kuzuia kitendo kilichoko kwenye mchakato. Neno hili limetumika hapa tu kwenye agano jipya. Hii ni moja ya sitiari ya riadha ya Paulo kwa maisha ya Kikristo (k.v. 1 Kor. 9:24,27; Gal. 2:2; Fil. 3:1 4; 2 Tim. 4:7). Waamini hawapaswi kuruhusu tendo la ushikiriaji sana wa sheria yawe kama mwamuzi wa kuwaondolea uhuru wao toka kwa Kristo (k.v. Rum. 1 4:1 -1 5:1 3; 1

Wakorintho 1 0-1 2. Tafasiri ya William ya Agano Jipya inaukamata ule msukumo wa riadha, ukitafasiri hili “asiwanyang’anye kama mwamuzi.””Thawabu”ni uhuru wa kweli katika Kristo (k.v. Gal. 2:4; 5:1 ,1 3; 1 Petr. 2:1 6)! Uhuru wa kumtumikia Mungu, na sio wewe mwenyewe. Uhuru kutokana na hofu ya nyuma na mila, uhuru toka kwa, na sio uhuru kwa (Warumi 6)!

**NASB "kunyenyekea kwa mapenzi yake mwenyewe"**
**NKJV "akichukuliana na kunyenyekea kusikofaa"**
**NRSV "akisisitiza kunyenyekea"**
**TEV "sisitiza juu ya kunyenyekea kusikofaa"**
**NJB "achaguaye kuwanyenyekea malaika"**

Kifungu hiki kithiolojia kinahusiana na Kol. 2:23. Katika ulimwengu wa kale wa Wagiriki-Warumi kujinyima starehe kulionekana kama ni moyo wa ibada.hii ilikuwa ni sehemu ya ushushaji thamani wa ujuzi wa kimwili. Kwao wao, na kwa Wayunani walitafakari kwa ujumla kuwa, mwili ulikuwa mwovu. Kwa hiyo, kuukana mwili ilikuwa ni alama ya u-kiroho. Mtazamo huu ungali hai katika kanisa! Neno la Kiyunani, lililotafasiriwa na toleo la NASB kama “kujinyenyekesha”inamaanisha “kujishusha chini””kutojivuna””kunyenyekea”na sio neno lenye kinyume katika agano jipya. Paulo alililitumia kwa maana chanya katika Mdo. 20:1 9; Efe. 4:2; Fil. 2:3; Kol.3:1 2. Ni nia ambayo inaweza geuzwa kuwa uongo wa kiroho!

◙ **"kuabudu malaika"** Dhahili hili linarejelea kwa ngazi ya wale wenye ujuzi wa kimalaika (k.v. Kol. 2:8,1 0,1 5). Pia yawezekana kuwa hili lilihusiana na hofu ya kithiolojia ya Kiyahudi na ule ulimwengu wa kimalaika. Mwenendo wa “enzi mpya” katika siku zetu za leo yaonekena kwenda katika mwelekeo huo. Malaika ni “roho za kitumishi”kwa mwanadamu aliyekombolewa (k.v. Ebr. 2:1 4).

◙**"akijitia"** Neno hili lilitumika kuanzisha makanisa ya siri (k.v. Moulton and Milligan,*The Vocabulary ofthe Greek NewTestament,* kur. 206). Linarejea kwa kile kinachoitwa ufunuo wa siri au maneno ya siri ya wale wenye ujuzi wa kipekee waliofikiri kuwa wameuleta wokovu kupitia anga za kimalaika ili kwamba ziufikie uwepo wa mungu mtakatifu, aliye mkuu.

◙ **"maono aliyoyaona"** Hii yawezekana linarejelea kwa madai ya walimu wa uongo ya mafunuo maalum. Toleo la King James linaongeza hasi, kuufanya mstari umaanishe kile ambacho hakikuonekana lakini likidai kukiona. Hili, ingawa, ni nyongeza ya kiuandishi ya baadaye kwenye machapisho 2א na D2. Machapisho ya kale ya Kiyunani P46, א*, A, B, na D* hayana ukinyume. Toleo la UBS4 linaipa daraja "B" (takribani ni yenye uhakika).

◙ **"na kujivuna bure"** Hii ni kauli tendwa yenye hali ya kuendele ya wakati uliopo. Kikawaida inamaanisha “kujivuna bure.”Paulo analitumia neno hili mara nyingi katika nyaraka zake za mwanzo kwa Wakorintho (k.v. 1 Kor. 4:6,1 8,1 9; 5:2; 8:1 ; 1 3:4). Wakala asieelezeka wa irabu tendwa alikuwa ni mawazo yao yaliyoanguka. Wasioamini na walimu wa uongo mara nyingi ni watiifu na wenye kuonyesha shauku.

◙**"kwa akili zake kimwili"** kwa Paulo kuna mwainisho wa dhahiri kati ya kuufikiria ulimwengu ulioanguka na Wakristo. Waamini wamekwisha pokea mawazo ya Kristo ambayo yako katika mgongano na mtazamo wa dunia unaoiendesha na unaotenda mbali na Mungu (k.v. Kol. 1 :21 ; Rum. 7:22-23; 8:5-7; 1 1 :34; 1 Kor. 2:1 6;Efe. 2:3;4:1 7-23). Tazama Mada Maalum: Mwili (*saxy*) katika Kol. 1:22

Hawa washika sheria za kidini lazima wakataliwe kwa sababu tatu.

1. Mtizamo wao ni kivuri tupu cha ukweli (Kol. 2:1 7)
2. maono yao ni ya uongo kwa sababu wanataarifiwa na mawazo ya kimwili (Kol. 2:1 8)
3. wameacha kusimama imara kwa Kristo (Kol. 2:1 9)

Walimu wa uongo waliozishika sheria bado wako nasi hata leo! Uwe mwangalifu! Uwe na taarifa!

**2:19** Paulo anashinikiza tena kweli kuu ya hitaji la mwanadamu aliyeanguka kwa ajili ya uhusiano na Kristo

(binafsi) na pia na mwili wake, ambalo ni kanisa (ushirika, k.v. Kol. 2:8; Efe.4:1 6). Tunahitaji wokovu toka kwenye dhambi na hekima toka kwa Mungu kwa namna ipasavyo kuishi. Yesu anatoa yote!

**NASB, NKJV**
**NRSV** **“wala hakishiki kichwa"**
**TEV** **"wala hakishiki kichwa kwa Kristo"**
**NJB** **"hakihusiani na kichwa"**

Hii ni kauli kanushi tendaji endelevu ya wakati uliopo. Kidokezo ni kuwa muda fulani walimu wa uongo hawakushikika kwa Kristo. Hili laweza eleweka kwa namna tofauti

1. walikuwa kama mbegu mbili katika mfano wa mpanzi (k.v. Mat. 1 3:20-23) kuwa iliotesha mimea lakini ikashindwa kutoa matunda
2. walikuwa kama “waumini”wa Yohana 8:31-59 waliokwenda kinyume na Yesu
3. kama washirika wa kanisa walioondoka katika 1 Yoh. 2:18-19
4. walikuwa kama waumini katika kanisa la Efeso waliouacha “upendo wa awali”(k.v. Ufu. 2:4)

◙ **"kichwa"** mara zote Paulo anatumia mshabihiano wa watu wa Mungu kama mwili (k.v. Rum. 1 2:4; 1 Kor. 1 0:1 7;1 2:1 2,1 4,20; Efe. 4:4,1 6; Col. 3:1 5), lakini inapatikana tu kwa Waefeso (1 :22; 4:1 5; 5:23) na Wakolosai (1 :1 8; 2:1 9) kuwa kwa dhahili Kristo anatambuliwa kama”kichwa” (tazama Mada Maalum: Kichwa katika Efe.5:23). Mstari mzima unaongelea Kristo kama mwanzilishi wa msingi, kiongozi, na mwezeshaji wa kanisa

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 2:20-3:4**
**20 na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni. 21 Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa; 22 katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama; 23 mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu; ambayo mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake. 3-1 Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. 2Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. 3Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. 4Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu.**

**2:20 "kama"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza ambayo inasadikiwa kuwa kweli kutokana na mtizamo wa mwandishi au kusudi lake la kifasihi. Waumini wanaungana na Kristo na wanatakiwa kujitenga toka kwenye nguvu na maumbo ya muundo wa ulimwengu huu ulioanguka.

◙ **"ikiwa mlikufa”**Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Kifo hiki kinaashiriwa katika ubatizo (k.v. Kol. 2:1 2; Rum. 6:4), na ni taswira ya kifo cha muumini kwa maisha ya kale na ufufuo wa maisha mapya ya Mungu aishie milele. Ubatizo kama ilivyo tohara, ni alama ya nje ya kweli ya undani wa kiroho (cf. Col. 2:1 1, 1 3). Kifo cha mara kwa mara kwenye lengo binafsi na upendeleo binafsi ni agizo lenye kufaa kwenye huduma (k.v. Rum.6:7; 2 Kor. 5:1 4-1 5; 1 Yoh. 3:1 6). Hata hivyo, huu sio upitishaji wa sheria, lakini ni uhuru toka kwenye uonevu wa anguko binafsi! Kifo cha kiroho cha mara kwa mara cha mtu huleta maisha ya kweli!

◙**"pamoja na Kristo"** Haya ni matumizi mengine ya kihusishi *syn,* ikimaanisha kukiwa na ushiriki wa pamoja. Miundo hii mitatu ya kisarufi: (1 )muunganiko wa neno *syn*; (2) njeo ya wakati uliopita usiotimilifu wa Kol. 2:1 1 ,1 2,1 3,1 5,20; na (3) sentensi yenye masharti daraja la kwanza ya Kol. 2:20 inaonyesha kile mwamini yule tayari yuko katika Kristo!

**NASB "kwenye kanuni za msingi za kidunia"**
**NKJV "toka kanuni za msingi za dunia"**
**NRSV "kwenye roho za kimsingi za ulimwengu"**
**TEV "toka roho zitawalazo za ulimwengu"**
**NJB "toka kanuni za ulimwengu huu"**

Neno hili (*stoicheia*) inaelezewa kama

1. kanuni za kimsingi (k.v. Ebr. 5:1 2. 6:1 )
2. dhana ya msingi ya ulimwengu, kama vile dunia, upepo, maji au fire (k.v. 2 Pet. 3:1 0, 1 2)
3. roho za asili, (k.v. Gal. 4:3, 8-9; Col. 2:8; Efe. 6:1 0-1 2)
4. miili ya kimbingu (k.v. *Enoch* 52:9-1 0 na makasisi wa kanisa la mwanzo waliodhani kurejerea mazingira ya kisayari, k.v. Baur, Arnt, Ginrich, Danker's *A Greek-English Lexicon ofthe NewTestament*, kur. 776)

Msingi wa asili ya neno ulikuwa"kitu fulani kilichoko katika mtiririko"au "safu."tazama maelezo kwenye Kol. 2:8. Paulo aliyatazama maisha kama bidii ya kiroho (k.v. Efe. 2:2-3; 6:1 0-1 8). Wanadamu walisongwa kwa uovu kutokana na mazingira yaliyowazunguka (asili ya anguko, k.v. Mwanza 3), kwa muundo wa ulimwengu ulioanguka (k.v. Mwanzo 3) na kwa uovu binafsi (Shetani, ya kimapepo na *stoicheia*). James Stewart's, *A Man in Christ*, ina hoja za kufurahisha:

> "dhambi sio kitu kile mwanadamu alitenda: kilikuwa kitu ambacho kilichukua nafasi juu yake, namna ile mtu alikuwa, kitu kilichombadilisha yeye toka kuwa adui wa wazi wa Mungu aliyempenda. Inaleta adhabu ya nje: kile mtu apandacho, ndicho atakachovuna. Lakini zaidi inaogofya kuliko zile zenye matokeo ya ndani. Iliitesa dhamiri: ikayaleta mapenzi ndani ya ufukara wa kitumwa: kizuri kile ningalikuwa nacho, sinacho, lakini uovu ule sikupashwa kuwa nao, ndio niutendao. Uliharibu ushirika na Mungu: watu wakafarakanishwa, pasipo Mungu katika dunia. Ikafanya mioyo kuwa migumu na kuipofusha hukumu, na kuipotosha maana ya uadilifu: Mungu akawapa zaidi fikra potofu. Ikayaharibu maisha yenyewe: 'mshahara wa dhambi ni mauti.'Hilo ni kadirio la kitume la dhambi ya kiwango cha juu. Na kupitia hayo yote, hata pale dhambi inapodhaniwa kuwa nguvu itokayo nje inayosubiri kuchukua nafsi ya asili ya mwanadamu katika udhaifu wake, hataruhusu kutokuwepo na uwazi kwenye uwajibikaji binafsi. Mamlaka na nguvu vyaweza kuwa katika usubiliaji, lakini mwishoni mwa kimbilio la mtu ni chaguo, jukumu la mtu, na kumwangamiza mtu" (kur. 1 06-1 07).Kwa ajili ya "dunia." tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya neno Kosmos katika Kolo. 1:6.

◙**"tamko"** Neno hili lina mzizi ule ule kama wa Kol. 2:1 4. Kristo hakuwafungua waamini toka kwenye sheria za Musa ili kushikamana tena katika sheria za wale waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee au hitaji lolote la mamlaka ya kibinadamu. Waamini walio huru wako kwa Kristo! Maumivu ya washika sheria waliokusudia vyema!

**2:21 "msishike, msionje, msiguse"** Mtiririko huu hauna vitenzi na viungo, vinavyofanya kuwa la msisitizo! Ungeweza kuwa ni msemo wa walimu wa uongo. Hii ni mifano ya sheria ya kidini ya mwanadamu ambazo hazileti haki ya kweli. Mwanadamu siku zote ana hali ya kujinyima anasa, tabia ya kujihalalishia (k.v. Isa. 29:1 3; Mat. 1 5:1 0-1 2; Mark 7:1 9; Rum. 1 4:1 7,21 ), lakini ni utupu wa dini wa bidii ya mtu mwenyewe, utukufu wa mtu mwenyewe na utosherevu wa mtu mwenyewe (k.v. Kol. 2:22-23).

**2:22 "(mambo hayo yote huharibika wakati wa kutumiwa)"** Katika Mat. 1 5:7-20 na Mark 7:6-23 Yesu analijadili aina ile ile ya suala linalohusiana na sheria za chakula za Walawi 11.

◙**"huharibika"** Tazama Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: TEKETEZA, ANGAMIZA, HARIBU (*PHTHEIRŌ*)**

Maana ya msingi ya neno hili *phtheirō* ni kuangamiza, kuharibu, kuchafua, au kuvuruga. Linaweza tumika kwa:

1. maangamizi ya kifedha (yawezekana 2 Kor. 7:2)
2. uharibifu wa kimwili (kama vile 1 Kor. 3:17a)
3. upotoshaji wa kimaadili (kama vile Rum. 1:23; 8:21; 1 Kor. 15:33,42,50; Gal. 6:8; Ufu. 19:2)

4. Utongozaji wa kingono (kama vile 2 Kor. 11:3)
5. uharibifu wa milele (kama vile 2 Pet. 2:12,19)
6. tamaduni za wanadamu zipoteazo (kama vile Kol. 2:22)

Mara nyingi neno hili limetumika katika muktadha uleule kama unavyokanusha pinzani yake (kama vile Rum. 1:23; 1 Kor. 9:25; 15:50,53). Angalia mvutano wa usambamba kati ya miili yetu ya duniani na miili yetu ya kimbingu isiyoharibika.

1. iharibikayo dhidi ya isiyoharibika, 1 Kor. 15:42,50
2. kukosa heshima dhidi ya utukufu, 1 Kor. 15:43
3. udhaifu dhidi ya nguvu, 1 Kor. 15:43
4. mwili wa asili dhidi ya mwili wa kiroho, 1 Kor. 15:44
5. adamu wa kwanza dhidi ya Adamu wa mwisho, 1 Kor. 15:45
6. taswira ya duniani dhidi ya taswira ya kimbingu, 1 Kor. 15:49

**2:23 "Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika namna ya ibada mliyojitungia wenyewe, na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali"** Hii ilikuwa moja ya lawama ya Yesu juu ya waandishi na mafarisayo (k.v. Isa. 29:1 3). Paulo anaelezea utendaji wa walimu wa uongo kwa maneno matatu:

1. **NASB " namna ya ibada mliyojitungia wenyewe "**
   **NKJV " namna ya ibada mliyojiamuria wenyewe "**
   **NRSV " namna ya uungu mliyojitungia wenyewe "**
   **TEV "namna mlivyolazimika kuwaabudu malaika"**
   **NJB "namna ya upaliliaji wa mapenzi yenu"**

2. Neno hili linatumika hapa tu katika Agano Jipya. Lawezakuwa limebuniwa na Paulo au Wakristo wa awali. Toleo la NASB linaonekena kuipata asili ya neno, “ibada mliojitungia wenyewe.”Toleo la TEV linadhani kuwa inaaksi Kol.2:1 8.

3. **NASB " katika kunyenyekea "**
   **NKJV, TEV "kunyenyekea kusikopasa"**
   **NRSV "kunyenyekea"**
   **NJB (weka pamoja neno la pili na la tatu)**

   Neno kama lile la Kiyunani linatumika katika Kol. 2:1 8. Kikawaida linamaanisha “unyenyekevu”lakini mazingira yanapendelea tafasiri ya toleo la NKJV na TEV.

4. **NASB, NRSV,**
   **TEV "katika kuutawala mwili kwa ukali"**
   **NKJV "kuutelekeza mwili"**
   **NJB "unyenyekevu usioujali mwili"**

   Hili linaaksi mtizamo wa wale watu wa dini wenye kujinyima starehe kwamba kukana hitaji la mtu kimwili kulionyesha au kulifanya huruma ya kidini. Mifano ni (1 ) kukataa chakula cha mwili; (2) useja; (3) kukosa nguo kipindi cha majira ya baridi, n.k. hili lilifuata mtizamo wa Kiyunani kwamba (mwili) ulikuwa mwovu.

## MADA MAALUM:UHURU WA MKRISTO DHIDI YA WAJIBU WA MKRISTO

**A.** Warumi 14:1-15:13 inajaribu kuweka usawa wa mfano wa Uhuruj wa Mristo na uwajibikaji. Sehemu ya fasihi inaanzia toka Rum. 14:1-15:13.

**B.** Tatizo ambalo lililoikumba sura hii bila shaka ni mvutano kati ya Watu wa Mataifa na waamini wa Kiyahudi ndani ya kanisa la Rumi. Kabla ya uongokaji Wayahudi walielekea kuwa wanasheria na wapagani waliendelea kutenda yaliyo maovu. Kumbuka, hili lihubiriwa kwa wafuasi waaminifu wa Yesus. Sura hii haiwahubirii

waamini walio wa mwili. Shauku kuu sana inawekwa kwa makundi yote mawili. Kuna hatari ndani ya uzidisho wa pande zote mbili. Mjadala huu sio kibali cha kutafuta makosa ya kisheria kuushagilia uhuru.

**C.** Waamini wanapaswa kujhadhari si kuifanya theolojia yao au maadili yao kuwa kipimo kwa waamini wote (kama vile 2 Kor. 10:12). Waamini wanapaswa kuenenda katika nuru walionayo lakini waelewe kwamba theolojia yao sio theolojia ya Munguinayojiendesha yenyewe. Waamini bado wanaathiriwa na dhambi. Yatupsa kutia moyo, sihi, na kufundishana kutoka katika Maandiko, sababu, na uzoefu, lakini katika upendo. Kadri mtu anavyoendelakujua ndivyo anavyoziodi kutokujua (kama vile 1 Kor. 13:12)!

**D.** Mtazamo na nia ya mtu mbele za Mungu jawabu kamili katika kuyatathimini matendo ya Mkristo wa kiume/kike. Wakristo watasisama mbele za Kristo kwa ajili ya kuukumiwa kuhusu namna walivyochukuliana (kama vile Matendo ya Mitume 15:10,12 na 2 Kr. 5:10).

**E.** Martin Luther anasema, "Mtu wa Kristo kwa kiasi kikubwa ni Bwana aliye huru kwa wote, asiye wajibika kwa mtu; mtu wa Kristo kwa kiasi kikubwa ni mtumishi aliyejitoa kwa wote, amejitoa kwa vyote." Kweli ya Kibiblia maranyingi inawasilishwa katika utimilifu wa ukinzani wa kimvutano (tazama Mada Maalum: Ukinzani kagtika Maandiko).

**F.** Ni vigumu lakini suala muhimu ni kushughulikia sehemu ya maandiko yote ya Warumi 14:1-15:13 na pia katika 1 Wakorintho 8-10 na Wakolosai 2:8-23.

**G.** Hata hivyo, inahitajika kueleza kwamba haliya wingi miongoni mwa waamini watiiifu si kitu kibaya. Kila mwamni anazonguvu na udhaifu. Kila mtu yampasa kuenenda katika nuru aliyo nayo, mara nyingi ni kuwa wazi kwa Roho na Bible kwa ajili ya kuwa na nuru zaidi. Katika kipindi hiki cha kuona kupitia kioo cha giza (1 Kor. 13:8-13) yampasa mtu kuenenda katika upendo (Matendo ya Mitume 15:15), na amani (Matendo ya Mitume 15:17,19) kwa ajii ya maadili ya pande zote mbili.

Tofauti zetu kama waamini ni mlango wa Mungu ulio wazi kwa ajili ya waamini tofauti tofauti wasioamini kuupata msamaha na urejesho ndani ya Kristo. Wingi wa Wakfristo, ndani ya mipaka ya Kibiblia, ni kitu kizuri kw aajili ya uinjilisti!

A. Hizi sifa "mwenye nguvu" na"mnyonge" ambazo Paulo anazitoa kwa makundi haya zinawaletea upendeleo kwetu. Hili ni yumkini si kusudi la Paulo. Makundi yote yalikuwa ya waamini watiifu. Hatujaribu kuwanyoosha Wakristio wengine kwa ajili yetu! Tunamkubali kila mmoja wetu katika Kristo!

B. Majadiliano yote yanaweza kuelezwa kama
   1. kukubaliana kila mmoja wetu kwakuwa Mungu anatukubali katika Kristo (Matendo ya Mitume 15:14:1,3; 15:7)
   2. tusuhukumiane sisi kwa sisi kwa kuwa Kristo ndiye Bwana na Hakimu wetu pekee (kama vile Matendo ya Mitume 14:3-12)
   3. upendo ni muhimu sana kuliko uhuru wa mtu bianafsi (kama vile Matendo ya Mitume 14:13-23)
   4. ufuate mfano wa Kristo na zitoe haki zako kwa ajili ya uadilifu wa wengine nay ale mema (kama vile Matendo ya Mitume 15:1-13

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Elezea mafundisho ya walimu wa uongo. Kwa nini walikuwa watu hatari
2. Nani au nini “kanuni za kimsingi” (*stoicheia,* k.v 2:8,1 5)?
3. Je Yesu ni Mungu au mtu? Kwa nini hili ni la muhimu?
4. Ni kwa namna gani Yesu anahusiana na nguvu za kimalaika
5. Kwa nini ushikiliaji mno wa sheria kuhusu kujinyima starehe ni kwa hatari (k.v. Kol. 2:1 6-23)?
6. Orodhesha maneno yenye mshiko ya watu waliojifikiri kuwa ni wenye ujuzi wa kipeke

# WAKOROSAI 3

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maisha Mapya katika Kristo<br><br>(2:20:-3:4) | Si Kimwili bali Kristo | Maisha ya Kweli ya Kristo<br><br>(2:20-3:4) | Kufa na Kuishi Maisha ya Kristo Kristo | Kuyatoa Maisha katika Umoja na |
| | 3:1-11 | 3:1-4 | Maisha ya Kale na Mapya | 3:1-4<br><br>Kanuni ya Jumla Mwenendo wa Mkristo |
| 3:5-11 | | 3:5-11 | 3:5-7<br>3:8-11 | 3:5-11 |
| | Sifa ya Mtu Mpya | | | |
| 3:12-17 | 3:12-17 | 3:12-17 | 3:12-17 | 3:12-17 |
| Wajibu wa Kijamii wa Maisha Mapya<br><br>(3:22-4:1) | Nyumba ya Mkristo | Wajibu wa Mkristo<br><br>(3:18-4:6) | Mahusiano Binafsi katika Maisha Mapya | Maisha ya Nyumbani na Unyumba |
| 3:18-19 | 3:18-4:1 | 3:18-19 | 3:18 | 3:18-21 |
| | | | 3:19 | |
| 3:20-21 | | 3:4:1 | 3:20 | |
| | | | 3:20 | |
| 3:22-4:1 | | | 3:22-4:1 | 3:22-4:1 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka **"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo, linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kol. 3:1-4 ni msingi wa kitheolojia kwa mwenendo wa Kikristo na maisha. Waamini lazima waishi ndani ya maisha yao mapya ya kila siku katika Kristo. Wanazikwa pamoja na kufufuliwa pamoja na Kristo (kama vile Kol. 2:12-13; Rum.6:3-11). Maisha yake hububujika kupitia kwao.

B. Paulo anaorodhesha yale mambo yanayotakiwa kuondolewa (weka kando, Kol. 3:8-9) na yale ya kushirikisha (ya kuonesha, Kol. 3:10) ambayo yanaunda usawa wa onyo kwa wale wanaomcha Mungu. Paulo mara nyingi alitengeneza orodha ya dhambi (kama vile. 1 Kor. 6:9-10; Gal. 5:19-21; Efe. 5:3-5) na maadili (kama vile Gal. 5:22-23; Efe. 5:18-20; Fpl. 1:4-7; 1 Thes. 5:12-22). Katika njia mbali mbali orodha hizi zinafanana na wale wenye maadili ya Kiyunani ya siku za Paulo. Lakini nia na utaratibu ulikuwa Kristo/ Roho, si juhudi binafisi. Tazama Mada Maalum katika Kol. 3:5.

C. Wito wa nguvu wa Paulo wa kuungana kwa sababu ya ule umoja wa Tatu, kwa uzuri kabisa umeelezwa kinagaubaga katika Efe. 4:1-10, unafananishwa katika Kol. 3:12-17. Pia, dai la Paulo la nguvu kwa kila mwamini linalopaswa kukamilishwa na Roho (kama vile Efe. 5:18) linafananishwa katika Kol. 3:16. Huu ufanano si ufanano wa neno, bali ni ufanano wa muhtasari. Kumbuka kwamba Wakolosai na Waefeso zimejikita takribani juu ya usahihi wa muhtasari huo huo.

D. Maonyo ya Paulo kukuhusu familia (Kol. 3:18-14:1) yanaonyesha namna maisha mapya ya mwamini katika Kristo yanavyoleta matokeo katika kila eneo la maisha. Imani ya Kibiblia ni imani inayoovunja asili ya zamani (asili iklyoanguka). Ushahidi wa badiliko ni kwamba hatuishi tena kwa ajili yake, bali kwa ajili ya wegine (kama vile 1 Yohana 3:16). Huu unayafuatisha maisha ya Yesu. Haya maelekezo mapya na ya ujumla ni ushahidi kwamba tumekwisha kombolewa!

Sura ya 3 (3:18-4:1) ni moja ya andiko lililounganishwa (kama vile Efe. 5:22-6:9).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBOFRESHWA) : WAKOLOSAI 3:1-4 ( Mgawanyo kamili wa aya unahusisha 2:20-3:4)**
**3:1 Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu.** 2 **Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.** 3 **Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.** 4 **Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu.**

**3:1"Basi"** Hili linaunganisha sehenmu ya kimafundisho (yaani, sura 1-2) 3-4). Hiki ndicho kipimo cha muundo wa kimaandishi katika maandishi ya Paulo (kama vile Rum. 12:1; Efe. 4:1; Flp. 4:1).

◙**"mkiwa"** Hii NI SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU ambayo inadhaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi ama kwa sababu zake za kiuandishi. Waamini wamefufuliwa pamoja na Kristo.

◙**"mmefufuliwa pamoja na Kristo "** Hili neno ambatani *syn* , "kufufufliwa pamoja " (kama vile Kol. 2:12,13; Rum. 6:3-11; Efe. 2:5-6). Sasa waamini wana maisha ya ufufuo, hivyo yawapasa kuishi kama huo ufufuo! Mistari 1-4 ni misingi ya kitheolojia kwa maadili ya Mkristo na maisha.

**◙"yatafuteni yaliyo juu "** Kwa vyo vyote hiki n**i** KITENZI TENDAJI ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPO AMA KITENZI TENDAJI CHENYE MASHARTI CHA WAKATI ULIOPO. Hivyo, hili ni onyo la kwendelea na yale mawazo na mambo ya kiroho (kama vile Kol. 3:2; Flp. 2:1-2;4:8).Mistari ya 1 na 2 ina ufanano. Bila shaka zote ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO. Waamini wanakuwa vile wanavyofikiria. Haya macho na masikio ni milango kwa ile nafsi. Badhi ya Wataalamu wanafikiri kwamba huu muktadha ni ile tofauti kati ya wale walio ndani ya Kristo (elekezi) na namna tunavyopaswa kuwa ndani ya Kristo (yenye masharti). Mara nyingi Paulo hatumii sifa hii ya kisarufi.

**◙"Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu"** Hiki ni kifungu cha lugha za kibinadamu (Zab. 110:1), ambacho kwa uchache Paulo hukitumia, kwa mamlaka ya Kristo na sehemu ya heshima (Luka 22:69; Matendo 7:55; Rum. 8:34; Efe.1:20;Ebr. 1:3; 8:1; 10:12; 12:2; 1 Pet. 3:22). Kwa kumweleza Kristo kama aliyekaa mkono wa kuume wa Baba pia ni njia ya kuirejelea ile huduma endelevu ya kule kusihi kwa watakatifu (kama vle Rum. 8:34; Ebr. 7:25; 9:24; 1Yohana 2:1). Hii ni ya kistiari kwa ajili ya kile chumba cha kiti cha enzi cha yule mfalme wa mashariki ya kati. Natumaini utakapoingia mbinguni unatarajia kumuona "yule mzee, yule mwanamme mdogo katika kiti kikubwa chenye njiwa aliyekuwa akiwazungukam!" Biblia humtumia mwanadamu, neno la kimwili kueleza umilele, la kiroho, Mungu mtakatifu. Maneno yote yaliyotumika kumweleza Yeye ni stiari, ushabihiano, ama ukanushi; yako kweli lakini si kwa ukamilifu.

I. **MADA MAALUM: MUNGU ANAELEZWA KAMA MWANADAMU (Lugha za kibinadamu)**

Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)

A. Viungo vya mwili
1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22

B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6

C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19

D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
1. Baba
   a. Wa Israel- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
   b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
   c. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17

2. Mzazi – Hosea 11:1-4
3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha
   A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!
   B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)
   C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)
   D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).

III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible,* ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika The International Standard Bible Encyclopaedia, kurasa za. 152-154

**3:2 "Yafikirini yaliyo juu"** Huu ni ufanano na Kol. 3:1 na kwa vyo vyote ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo ama kauli tendaji yenye masharti ya wakati uliopo. Bila shaka hii ni kauli shurutishi. Ukristo ni vyote maarifa na tendo (kama vile 1 Pet. 1:13-21)! Huu mstari una ufanano na Kol. 3:1.

◙**"siyo yaliyo katika nchi"** Hiki kifungu kinatoa ufafanuzi wa ule utofauti wa ile tofauti aliyoikusudia Paulo; waamini wanapaswa kufikiri na kuishi katika Roho, si katika mwili (kama vile Rum. 8:1-17). Hawa wana uchaguzi na yawapasa kuweka mpangilio wa vipaumbele vya maisha yao. Kuokolewa si jambo linalojiendesha lenyewe katika maisha ya kuishi ki- Mungu, bali inabidi. Paulo anatumia ile tofauti ya uwili, lakini si kati ya roho dhidi ya yale Mafunuo ya Uongo; kiasi, utofauti wake uko kati ya hili neno (umri) dhidi ya Ufalme wa Mungu (enzi mpya). Waamini ni raia wa falme mbili. Haya maarifa (mawazo ya ulimwengu) huleta tumaini, ushujaa na amani kati kati katikati ya majaribu ya maisha (mafundisho ya uongo, mateso, kifungo, dhiki, nk.).

**3:3"mlikufa"** Hii ni stiari nyingine iliyojikita juu ya ubatizo yenye kuelezea msimamo mpya wa mwamini katika Kristo (kama vile Rum. 6:1-11; Kol. 2:11-12). Waamini wanaifia dhambi na kuishi kwa Mungu! Hawa waliaswa kuutambua msimamo wao mpya katika Kristo (kama vile Kol. 3:5; Efe. 2:5-6) na kumfuatisha Yeye (kama vile 2Kor. 5:14-15; Gal.2:20; Efe. 5:1-2; 1 Yohana 3:16).

◙**"umefichwa"** HII NI KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA TIMIFU. Waamini wamekufa (katika Kristo) na wamekuwa na wanaendelea kufichwa katika Mungu. Zile dini za siri za kile kipindi kati ya Wagiriki na Warumi zilitumia neno hili kurejelea juu ya ule uanzishaji wa utaratibu wa jando. Dhana hii ya maficho ingeweza kuhusiana na (1) ulinzi ama (2) utukufu kamili wa mwamini ulioshirikishwa na Kristo si ule ambao bado unaonekana kwa ulimwengu (k.v Kolo. 3:4

**3:4 "Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu"** Hii inaaksi ile dhana ya kitheolojia ya "kuutoa uhai" (kama vile Gal. 2:20; Flpl. 1:21).

◙**"atakapofunuliwa"** Hii inarejelea ule Ujio wa mara ya Pili (kama vile 1 Yohana 3:2).

◙**" ninyi mtafunuliwa pamoja naye"** Waamini walikufa pamoja na Kristo, tulifufuliwa pamoja na Kristo, na tutakuwa sehemu ya kurudi Kwake kwa Utukufu (kama vile 1 The. 4:13-18). Kule "kufichwa" (Kol. 3:3) kutafunuliwa (Kol. 3:4). Tazama maelezo juu ya "utukufu" katika Efe. 1:6 na Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: MANENO YA AGANO JIPYA KUHUSIANA NA KURUDI KWA YESU**

Msisitizo wa matukio ya siku za mwisho ya siku maalum ya kuja ambayo wanadamu watakutana na Yesu (kama Mwokozi na Mtoa hukumu) yanatolewa maelekezo yake kadhaa.

1. "siku ya Bwana wetu Yesu Kristo" (kama vile 1 Kor. 1:8)
2. "siku ya Bwana" (kama vile 1 Kor. 5:5; 1 The. 5:2; 2 The. 2:2)
3. "siku ya Bwana Yesu" (kama vile 2 Kor. 1:14; MS א ina ". . .Bwana Yesu" katika 1 Kor. 5:5)
4. "siku ya Yesu Kristo" (kama vile Fil. 1:6)
5. "siku ya Kristo" (kama vile Fil. 1:10; 2:16)
6. "Siku Yake (Mwana wa Adamu)" (kama vile Luka 17:24)
7. "siku ambayo mwana wa Adamu atadhihirishwa" (kama vile Luka 17:30)
8. "ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo" (kama vile 1 Kor. 1:7)
9. "wakati Bwana Yesu atakapodhihirishwa kutoka mbinguni" (kama vile 2 The. 1:7)
10. "katika uwepo wa Bwana Yesu wakati wa kuja kwake" (kama vile 1 The. 2:19)

Kuna angalau njia nne ambazo waandishi wa Agano Jipya wanamaanisha kurudi kwa Yesu.

1. *epiphaneia*, ambayo inamaanisha mg'ao wa kumetameta ambako kithiolojia (japo sio kiasili) kunafanana na "utukufu." Katika 2 Tim. 1:10; Tito 2:11 na 3:4 inamaanisha kuja kwa Yesu kwa mara ya kwanza (yaani kuzaliwa) na kuja kwake mara ya Pili. Inatumika katika 2 The. 2:8 ambayo inajumuisha maneno yote matatu ya kuja kwa mara ya Pili: 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 4:1,8; Tito 2:13.
2. *parousia*, ambayo inamaanisha uwepo na kwa asili ikimaanisha utembeleo wa kifalme. Linatumika sana neno hili (kama vile Mt. 24:3,27,37,39; 1 Kor. 15:23; 1 The. 2:19; 3:13; 4:15; 5:23; 2 The. 2:1,8; Yakobo 5:7,8; 2 Petro. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28).
3. *apokalupsis* (au *apocalypsis*), ambayo inamaanisha kufunuliwa kwa kusudi la kufunuliwa. Ni jina la kitabu cha mwisho katika Agano Jipya (kama vile Luka 17:30; 1 Kor. 1:7; 2 The. 1:7; 1 Petro 1:7; 4:13).
4. *phaneroō*, ambalo linamaanisha kuleta mwanga au kwa ufasaha kufunua au kudhihirisha. Neno linatumika mara nyingi katika Agano Jipya kwa vipengele vingi vya ufunuo wa Mungu. Ni kama *epiphaneia*, Linaweza kurejerea kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo (kama vile 1 Petro 1:20; 1 Yohana 1:2; 3:5,8; 4:9) na kuja kwake mara ya Pili (kama vile Mt. 24:30; Kol. 3:4; 1 Petro 5:4; 1 Yohana 2:28; 3:2).
5. Neno lililozoeleka la "kuja," *erchomai*, pia linatumika mara kwa mara kwa kurudi kwa Kristo (kama vile Mt. 16:27-28; 23:39; 24:30; 25:31; Mdo. 1:10-11; 1 Kor. 11:26; Ufu. 1:7,8).
6. Pia linatumika pamoja na tungo "siku ya Bwana" (kama vile 1 The. 5:2), ambalo ni cheo cha siku ya Mungu ama Uungu kwa Agano la Kale (ufufuo) na hukumu.

Agano Jipya lote limeandikwa ndani ya mtazamo wa kiulimwengu wa Agano la Kale ambalo linaelezea

1. uovu wa sasa, kizazi cha uasi
2. kizazi kijacho cha haki/utauwa
3. kizazi kitakacholetwa na wakala wa roho kupitia kazi ya Masihi (Mpakwa Mafuta)

Dhanio za kithiolojia za ufunuo unaoendelea unatakiwa kwasababu ya waandishi wa Agano Jipya kidogo wamerekebisha mategemeo ya Israeli. Badala ya kuja kijeshi na kiuzalendo (Israeli) kwa Masihi, kuna kuja mara mbili. Kuja kwa kwanza ni kuzaliwa kwa uungu na kutungiwa mimba na kuzaliwa kwa Yesu wa Nazareth. Alikuja ila sio kijeshi, sio kwa ajili ya hukumu "mtumwa atesekaye" wa Isaya 53; pia mwendesha farasi (si farasi wa vita au farasi wa kifalme), wa Zekaria 9:9. Kuja kwa mara ya kwanza kunaanzishwa na kizazi cha Kimasihi, ufalme wa Mungu duniani (angalia Mada Maalum: Ufalme wa Mungu). Kwa namna moja, lakini, katika nyingine kuna kuwa bado mbali sana. Ni mvutano huu wa kuja mara mbili kwa kimasihi (angalia Mada Maalum: Masihi) ambao, katika namna, ni kupandana kwa vizazi vya kiyahudi (angalia Mada Maalum: Kizazi hiki na kizazi kijacho) ambacho kilikuwa hakionekani au kwa sehemu hakiko katika hali ya kuonekana kutoka katika Agano la Kale. Kiukweli huku kuja kwa mara mbili kunaweka mkazo katika kujidhatiti kwa YHWH kukomboa binadamu wote (kama vile. Mwanzo 3:15; 12:3; Kutoka 19:5 na kuhubiri kwa manabii, hasa Isaya na Yona).

Kanisa halisubiri kutimilizwa kwa unabii wa Agano la Kale kwasababu nabii nyingi zinamaanisha kuja kwa mara ya kwanza (kama vile *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa 165-166). Kile waaminio

wanachokibashiri ni kuja kwa utukufu wa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana aliyefufuka, kutimilizwa kwa kizazi kipya cha haki duniani kama ilivyo mbinguni kwa kihistoria kunakotarajiwa (kama vile Mt. 6:10). Uwasilishwaji wa Agano la Kale si kwamba haukuwa wa kweli bali haukuwa umekamilika (angalia Mada Maalum: Kwa nini Ahadi za Kiagano za Agano la Kale zinaonekana kuwa Tofauti na Ahadi za Agano Jipya?). Atakuja tena kama manabii walivyotabiri katika nguvu na mamlaka ya YHWH.

Cheo "Kuja kwa Mara ya pili" si neno la Kibiblia, lakini dhana ni ya kimtazamo wa ulimwengu na muundo wa Agano Jipya lote zima. Mungu atayaweka mambo yote sawa kwa sawa. Ushirika kati ya Mungu na mwanadamu ulifanya sura yake irejeshwe. Uovu utahukumiwa na kuondolewa. Kusudi la Mungu halitakuja kuondolewa wala kufeli!

Kanisa la kwanza liliabudu siku zote Sabato na siku ya kwanza ya wiki (yaani Jumapili, siku ya ufufuo). Sinagogi lilizungumzia kukua kwa uamsho wa Wakristo kwa kuwataka waumini wao kumkataa Yesu kama Masihi (yaani Mapokeo kumi na nane). Kwa wakati huu (yaani mwaka 70 B.K. ) Wakristo walikutana siku ya Jumapili.

**ANDIKO LA NASB (LILOLOBORESHWA) : WAKOLOSAI 3:5-11**

**5 Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu; 6 kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. 7 Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. 8 Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. 9 Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; 10 mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba. 11 Hapo hapana Myunani wala Myahudi, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala mwungwana, bali Kristo ni yote, na katika yote.**

**3:5**
**NASB "vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi"**
**NKJV "vifisheni viungo vyenu vilivyoko katika nchi"**
**NRSV "yawapasa kuzifisha zile shauku za kidunia katika kazi iliyo**
**TEV "iliyo ndani mwenu**
**NJB "ueni chochote ndani mwenu ambacho ni cha kidunia"**

Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ambayo inadokeza umuhimu kama vile. Kol. 3:8,12). Hii inaanza na sehemu ambayo inasistiza lile hitaji kwa waamini kuuvua mara moja uovu wao wenyewe na kwa wote (Kol. 3:5-11). Paulo mara nyingi anatumia neno kuvika kama stiari ya maisha ya kiroho (kama vile Rum. 6:6,11; 8:13; Efe. 4:22,24,25,31, bila shaka hili linatoka Zakaria 3). Waamini ni kwa ajili yao wenyewe, kutenda dhambi, na kuwa wa ulimwengu. Sehemu ya mwisho inasistiza kwamba yawapasa Wakristo kuifuatisha ile mienendo inayomfanana Kristo (Kol. 3:10-17).Paulo mara nyingi anazibainisha dhambi za maisha ya kale na yule mwanamme mzee katika orodha ambazo katika njia hizi zilifanana na wanamaadili wa Kiyunani (kama wale wenye kustahimili mateso) wa zile siku zake.

**MADA MAALUM: UOVU NA WEMA KATIKA AGANO JIPYA**

Orodha zote za mabaya na mema ni ya kawaida katika Agano Jipya. Mara nyingi yanaaksi orodha za sheria za Kiyahudi na kitamaduni. Orodha ya tabia kinzani ya Agano Jipya zinaweza onekana katika:

| | Maovu | Mema |
|---|---|---|
| 1. Paulo | Rum. 1:28-32 | --- |
| | Rum. 13:13 | Rum. 12:9-21 |
| | 1 Kor. 5:9-11 | --- |
| | 1 Kor. 6:10 | 1 Kor. 6:6-9 |
| | 2 Kor. 12:20 | 2 Kor. 6:4-10 |

| | | |
|---|---|---|
| | Gal. 5:19-21 | Gal. 5:22-23 |
| | Efe. 4:25-32 | --- |
| | Efe. 5:3-5 | --- |
| | --- | Flp. 4:8-9 |
| | Kol. 3:5,8 | Kol. 3:12-14 |
| | 1 Tim. 1:9-10 | --- |
| | 1 Tim. 6:4-5 | --- |
| | 2 Tim. 2:22a, 23 | 2 Tim. 2:22b,24 |
| | Tito 1:7, 3:3 | Tit 1:8-9; 3:1-2 |
| 2. Yakobo | Yak. 3:15-16 | Yak. 3:17-18 |
| 3. Petro | 1 Pet. 4:3 | 1 Pet. 4:7-11 |
| | 2 Pet. 1:9 | 2 Pet. 1:5-8 |
| 4. Yohana | Uf. 21:8; 22:15 | --- |

◙ "**uasherati, uchafu**" Hili ni neno la kwanza la Kiyunani (*porneia*) kiuhalisia lilimaanisha "kahaba," lakini lilikuja kutumika kwa habari ya zinaa katika ujumla (kama vile 1 Kor. 6:9). Tunalipata neno la Kiiingereza neno la pili "uchafu" (*akatharsia*) lililokuwa pia neno la jumla kwa habari ya zinaa, japo kwa uhalisia lilitumika katika Agano la Kale katika maana ya kutokuwa msafi kiibada au kutokuwa msafi kimaadili. Paulo aliikusudia ile maana ya pili.

◙"**tamaa mbaya, mawazo mabaya**" Haya maneno mawili pia yanatumika kwa pamoja katika 1 The. 4:5 na kutafsriwa "tamaa mbaya." Neno la kwanza, "tamaa" (*pathos*), linatumika Neno la pili, "mawazo mabaya" (*epithumia*), pia linatumika katika maana mbili tofauti sana, mawazo yenye nguvu kwa kitu fulani (1)kilicho chema ama (2)kiovu. Muktadha lazima utambulishe ni kipengele kipi cha eneo la neno la kimaana linalomaanishwa na mwandishi.Hii orodha ya dhambi za zinaa inaweza kuhusianishwa na wale waalimu wa uongo. Mafunuo ya walimu wa uongo yalikuwa ya aina mbili: (1)wale walioishi maisha ya unyenyekevu yasio ya anasa na (2) wengine walioutazama mwili kama usiopasa maisha ya kiroho na kudekeza tama za mwili . Mara nyingi unyanyasaji wa kijinsia na kifedha unaeleza juu ya wale walimu wa uongo.

◙" **kutamani**" Neno hili mara nyingi linatumika kwa maana ya kuwa na shauku ya vitu, lakini katika dhana ya unyanyasaji wa kijinsia, hili linaweza kuwa linamaanisha zaidi ya shauku ya zinaa kwa gharama yo yote! Baadhi wanawaona wengine tu kama vyombo binafsi, uridhisho wa kujamiiana.

◙"**ndiyo ibada ya sanamu**" Chochote kinachotawala, endesha, ama kudai kuinyenyekea sanamu ambayo huchukuwanafasi ya Mungu. Kwa wengine, shauku ya zinaa huwa mtazamo wa maisha yao, mawazo, na mipango.

**3:6** "**huja ghadhabu ya Mungu**" Katika njia nyingi hili linafanana na mjadala wa Paulo katika Rum. 1:18-2:16. Ghadhabu ya Mungu ilitazamwa katika sura kati ya mbili katika Biblia: (1) dhambi iliyoleta matokeo katika adhabu ya papo kwa papo, katika maisha haya (mtiririkol) na (2) Mungu atawahukumu wanadamu wote kwa siku moja (matukio ya siku za mwisho). Kuna tofauti ya machapisho ya Kiyunani katika hoja hii. Andiko refu zaidi, ambalo linahusisha ile nahau ya Kimaana "juu ya wana wa ukaidi," liiko katika herufi kubwa MSS ,אA, C, D, F, G, H, K, L, na P. Hili limeondolewa katika MSS P46 na B. Usomaji mrefu unapatikana katika kila machapisho ya Efe. 5:6 ambayo inaweza kuwa chanzo cha hili ongezeko (tazama Bruce M Metzger, *A Textual Commentary On the Greek NT*, uk. 824).

**3:7 "Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani** " Ule usuli wa waamini wa Kolosai ulikuwa wa upagani (kama vile Rum. 6:19; 1 Kor. 6:11; Tito 3). Hawa waamini walitumia kufikiri na kuziishi aina hizi za dhambi.

**3:8 " Lakini sasa** Tambua tofauti (mwanamme mzee dhidi ya mwanadamu mpya).

◙ "**yawekeni mbali**" Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ambayo inadokeza umuhimu. Waamini lazima wawe tofauti. Paulo alitumia neno vika kama stiari ya chaguzi za maisha ya mtu. Waamini wanasistizwa kuyavua maisha ya kale na kuyatupilia kando kama vazi (kama vile Kol. 3:8,9; Efe. 4:22,25,31; Yakobo 1:21; 1 Pet. 2:1). Hawa yawapasa kumvaa Kristo (kama vile Kol. 3:10,12,14; Efe. 4:24: Rum. 13:14; Gal. 3:27). Hawa waamini walikuwa wakiongozwa na kutawaliwa na tamaa zao mbaya, lakini sasa, kupitia Kristo, wanaweza kugeuka kutoka katika hizo (kama vile Rum. 5-6).

◙" **hasira**" Neno hili linamaanisha kuendelea, kulikopita kiasi, hasira iwakayo (kama vile 2 Kor. 12:20; Gal. 5:20; Efe.4:31).

◙ "**ghadhabu**" Neno hili linamaanisha kuwaka hasira ghafla ama mlipuko wa hasira kali (kama vile 2 Kor. 12:20; Gal. 5:20; Efe. 4:31).

◙ "**uovu**" Neno hili linamaanisha "fikra potofu" (kama vile Rum. 1:29; 1 Kor. 5:8; Efe. 4:31). Hili linamaanisha ile shauku ya kuwajeruhi wengine.

◙" **matukano, na matusi** "Watu wanasikiliza; usemi wetu unaaksi kwa uhalisia vile tulivyo (kama vile Mt. 12:34-35; 15:11,18; Marko 7:20; Efe. 4:29; 5:4; Yakobo 2:3-12).

**MADA MAALUM : USEMI WA MWANADAMU**

I. MAWAZO YA UFUNGUZI TOKA MITHALI
   A. Lugha ni sehemu ya taswira ya Mungu kwa mwanadamu (yaani., uumbaji umezungumzwa katika kuweko na Mungu kuzungumza kwenye uumbaji wake wa mwanadamu). Ni sehemu muhimu ya hulka bayana.
   B. Kauli ya mwanadamu inatuwezesha kuwasiliana na wengine jinsi tunavyofikiria kuhusu maisha. Kwa hiyo, inadhihilisha jinsi tulivyo (Mith. 18:2; 4:23, 20-27). Kauli ni ladha chachu ya mtu (Mith. 23:7)
   C. Sisi ni viumbe jamii. Tunawajibika na ukubalifu na uthibitisho. Tunavihitaji kutoka kwa Mungu na kutoka wanadamu wenzetu. Maneno yana nguvu ya kuyakabili mahitaji haya katika hali chanya (Mith. 17:10) na hasi (Mith. 12:18).
   D. Kuna nguvu ya ajabu katika kauli ya mwanadamu (Mith. 18:20-21-nguvu ya kubariki na kuponya (Mith. 10:11,21) na nguvu ya kulaani na kuangamiza (Mith. 11:9)
   E. Tunavuna kiile tulichopanda katika eneo hili (Mith. 12:14)

II. KANUNI TOKA KWENYE MITHALI
   A. Kauli za mwanadamu zilizo kinyume na zenye uharibifu
      1. Maneno ya mtu mwovu (1:11-19; 10:6; 11:9,11; 12:2-6)
      2. Maneno ya mwasherati (5:2-5; 6:24-35; 7:5 na kuendelea; 9:13-18; 22:14)
      3. Maneno ya mtu mwongo (6:12-15,19; 10:18; 12:17-19,22; 14:5,25; 17:4; 19:5,9,28; 21:28; 24:28; 25:18; 26:23-28)
      4. Maneno ya mtu mjinga (10:10,14; 14:3; 15:14; 18:6-8)
      5. Maneno ya mtu mwenye kushuhudia uongo (6:19; 12:17; 19:5,9,28; 21:28; 24:28; 25:18)
      6. Maneno ya msengenyaji (6:14,19; 11:13; 16:27-28; 20:19; 25:23; 26:20)
      7. Maneno ya mlopokaji (6:1-5; 12:18; 20:25; 29:20)
      8. Maneno ya msingizaji (29:5)
      9. Mtu mwenye maneno mengi (10:14,19,23; 11:13; 13:3,16; 14:23; 15:2; 17:27-28; 18:2; 21:23; 29:20)
      10. Maneno ya upotoshaji (17:20; 19:1)
   B. Kauli ya mwanadamu iliyo dhahili, yenye kuponya na kujenga
      1. Maneno ya mwenye haki (10:11,20-21,31-32; 12:14; 13:2; 15:23; 16:13; 18:20)
      2. Maneno ya utambuzi (10:13; 11:12)
      3. Maneno ya maarifa (15:1,4,7,8; 20:15)

4. Maneno yenye kuponya (15:4)
5. Maneno yenye jibu la upole (15:1,4,18,23; 16:1; 25:15)
6. Maneno yenye jibula kufurahisha (12:25; 15:26,30; 16:24)
7. Maneno ya kisheria (22:17-21)

III. SEHEMU YA AGANO LA KALE INAYOENDELEA KATIKA AGANO JIPYA

A. Kauli ya mwanadamu inatuwezesha kuwasiliana na wengine jinsi tunavyofikiria kuhusu maisha. Kwa hiyo, inadhihilisha jinsi tulivyo (Mt. 12:33-37; 15:1-20; Mk 7:2-23).
B. Sisi ni viumbe jamii. Tunawajibika na ukubalifu na uthibitisho. Tunavihitaji kutoka kwa Mungu na kutoka wanadamu wenzetu. Maneno yana nguvu ya kuyakabili mahitaji haya katika hali chanya (2 Tim. 3:15-17) na hasi (Yak. 2:2-12).
C. Kuna nguvu ya ajabu katika kauli ya mwanadamu ;nguvu ya kubariki (Efe. 4:29) na nguvu ya kulaani (Yakobo 3:9). Tunawajibika kwa kile tutakayoyasema (Mat. 12:36-37; Yak. 3:2-12)
D. Tutahukumiwa kutokana na maneno yetu (Mt. 12:33-37; Lk. 6:39-45) vile vile na matendo yetu (Mt. 25:31-46). Tunavuna kile tupandacho (Gal. 6:7)

**3:9 " Msiambiane uongo**" Hii ni kauli ya kati ya wakati uliopo (shahidi) yenye masharti yenye kiambata hasi ambayo inamaanisha kustisha tendo lililo katika mchakato. Sentensi ya Kiyunani inaendelea kutoka Kol. 3:9 hadi Kol. 3:11. Usemi wa Mkristo lazima uwe wa kweli, uaminifu, wa kurekebisha, na uzungumzwe katika upendo (kama vile Efe. 4:15).

**3:10 "mkivaa utu mpya, unaofanywa upya"** Hiki ni kitenzi cha kauli tendwa endelevu cha wakati uliopo yenye wakala aliyetumika akiwa Mungu ama Roho. Maisha ya Mkristo ni vyote hali (Efe. 2:5,8) na ule mchakato wa maendeleo (1 Kor. 1:18). Lengo lake ni lile lenye Kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:29; Gal. 4:19; Efe. 1:4), kurejeshwa katika ile sura ya Mungu. Huku "kufanya upya" (kama vile 2 Kor. 4:16 na ile nomino katika Rum. 12:2na Tito 3:5) ni kazi ya Mungu ambayo kila mwamini anapaswa kuifuata, na wanapaswa kushirikiana na Mungu ili kuikamilisha ndani mwao (kama ule "ujazo" wa Roho, pia kitenzi tendewa endelevu cha wakati uliopo katika Efe.5:18).

## MADA MAALUM: KUFANYA UPYA (*ANAKAINŌSIS*)

Neno hili la Kiyunani katika muonekano wake tofauti (*anakainoō, anakainizō*) lina maana mbili za msingi

1. "Kukifanya kitu kuwa kipya na cha tofauti (yaani., bora)"-Rum. 12:2; Kol.3:10
2. "Kufanya badiliko toka kwenye hali ya nyuma iliyokuwa ikipendelewa"-2 Kor. 4:16; Ebr. 6:4-6

(limechukuliwa toka kwa Louw and Nida's *Greek-English Lexicon,* juzuu. 1, kur. 157, 594)
Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, anasema kuwa neno hili (yaani., *anakkainōsis*) haliwezi kupatikana katika fasihi za Kiyunani mapema zaidi kuliko Paulo. Huenda Paulo amelitunga neno hili mwenyewe (uk. 34).

Frank Stagg, *New Testament Theology,* ana hoja ya kufurahisha.

"kuzaliwa upya na kufanywa upya kunamhusu Mungu mwenyewe. *Anakainōsis*, neno kwa ajili ya "kufanywa upya," ni nomino ya kitendo, na linatumika katika Agano Jipya, likiwa na miundo wa kitenzi, ikielezea hali ya mwendelezo wa kufanyika upya, kama ilivyo katika Warumi 12:2, ' ….' na 2 Wakorintho 4:16, '….' Wakolosai 3:10 inamwelezea 'mtu mpya' kama 'yule aliyefanywa upya kwa mpangilio kutokana na taswira ya yule aliye muumba.' Kwa maana hiyo ni 'mtu mpya,' 'maisha mapya' 'kuzaliwa upya' au 'kufanywa upya' hata hivyo usanifishwaji, unaangaliwa kwenye kitendo cha awali na kitendo endelevu cha Mungu kama mtoaji na mwezeshaji wa maisha ya milele" (uk. 118).

◙" **ufahamu sawasawa**" Hili kifasihi ni neno "katika maarifa kamili" (*epignōsin*). Katika utofautisho na maarifa ya

uongo ya wanamafunuo wa uongo.

**3:11** Mstari huu unaeleza ukweli ule ule kama ilivyo Rum. 3:22,29; 10:12; 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28 na Efe. 2:11-22. Vikwazo vyote vya mwanadamu na zile tofauti zinaondolewa kwa injili. Hili haliondoi tofauti zote za kibiblia, kwa mfano, ule uhusiano kati ya wanaume na wanawake (kama vile Efe. 5:21-31) ama tajiri na maskini (kama vile Yakobo 1:9-10), bali linaondoa mambo yote yasiyo ya usawa!

◙**"mgeni wala mshenzi"** Hili lilirejelea yale Mataifa yenye kushikiria utamaduni na yale yasiyoshikilia utamaduni. Lile neno lenye kuigiza sauti "mshenzi" ki uhalisia lilirejelea ile njia ambayo watu wa Dora ya Ugiriki ya Kirumi walioyasikia makabila ya Ulaya yakizungumza ambalo wao walilirejelea kama "bar bar bar." jamii ya Ugiriki ya Kirumi ilichukulia Wageni kama wasiostaarabika na taifa kamili la kishenzi.

**MADA MAALUM : UBAGUZI WA KIMBARI**

I. Utangulizi
   - A. Tabia hii ya kujikuza ni ya watu wote kwa wanadamu walioanguka katika jamii huu ni ubinafsi wa mwanadamu ili kujilinda kwa wengine ubaguzi wa mataifa kwa namna mbalimbali, na kauli ya sasa wakati utaifa (au ukabila) ni mtindo wa kizamani.
   - B. Utaifa ulianzia Babeli (Mwanzo 11) na mwanzoni ulihusishwa na wana watatu wa Nuhu ambapo neno hili mataifa lilitokana kwalo (kama vile Mwanzo 1-3; Matendo 17:24-26).
   - C. Ubaguzi wa mataifa ni mojawapo ya aina nyingi za uonevu
     1. Kutukuza elimu
     2. Ujivuni wa wa kijamii na kiuchumi
     3. Uhalalisho wa haki binafsi ya kidini
     4. Msimamo usiobadilika wa kuingiza dini katika siasa

II. Matini ya Biblia
   - A. Agano la Kale
     1. Mwa. 1:27 -mwanadamu kiume walifanywa kwa taswira na mfano wa Mungu vinavyomfanya awe wa pekee inaonesha pia uthamani wa mtu na hadhi/ utu (kama vile Yohana 3:18)
     2. Mwanzo 1:11-25- inaandika fungu, "… baada ya jinsi yao…" mara kumi. Hii imetumika kusaidia utenganisho wa mataifa. Hata hivyo ni wazi kutokana na mazingira hii inamaanisha wanyama na mimea na sio kwa watu.
     3. Mwa. 9:18-27- Hii imetumika kusaidia utawala wa mataifa. Ikumbukwe kwamba Mungu hakulaani kanani. Nuhu babu yake alimlaani kwasababu ya baba yake dhambi ya Ham) baada ya kuzinduka kutoka kwenye ulevi wa pombe. Biblia haioneshi kuwa Mungu alithibitisha kiapo/laana. Hata kama alifanya hivyo haiwaathiri watu weusi.
     4. Hes. 12:1- Musa anaoa mwanamke mweusi
     5. Yoshua 9:23- Hii imetumika kuhakiki kuwa taifa moja litatumikia lingine. Hata hivyo katika uhalisia wa Gibeonite ni wa asili moja na Wayahudi.
     6. Ezra 9-10 na Nehemia 13- Hivi vimetumika kwa maana ya mataifa, lakini kiuhalisia inaonesha kuwa ndoa zilikuwa zimekataziwa, sio kwa sababu ya mataifa (walitoka kwa kaka mmoja Nuhu Mwanzo 10) lakini kwa misingi ya kidini.
   - B. Agano Jipya
     1. Injili
        - a. Yesu alitumia hali hii ya chuki kati ya Wasamaria na Wayahudi katika mifano kadhaa ambayo ilionesha kuwa ubaguzi wa kimataifa haufai.
          1) Fumbo la Msamaria mwema (Luka 10:25-37)
          2) Mwanamke kisimani (Yohana 4)
          3) Mgonjwa wa ukoma aliyeshukuru (Luka 17:11-19)
        - b. Injili ni kwa watu wote

1) Yohana 3:18
2) Luka 24:46-47
3) Waebrania 2:9
4) Ufunuo 14:6

c. Ufalme utawajumuisha wanadamu wote
1) Luka 13:29
2) Ufunuo 5

2. Matendo
a. Matendo 10 ni habari kamili kuhusu upendo wa Mungu kwa ulimwengu wote na ujumbe wa injili kwa walimwengu wote.
b. Petro alishambuliwa kwa vitendo vyake katika Matendo 11 na tatizo lake halikutatuliwa hadi baraza la Yerusalemu katika matendo 15 lilipokutana na kupata ufumbuzi.

Mvutano kati ya Wayahudi wa Karne ya kwanza na wapagani ulikuwa umezidi.

1. Paulo
a. Hakuna Vipingamizi/vizuizi katika Kristo.
1) Gal. 3:26-28
2) Efe. 2:11- 22
3) Kor. 3:11
b. Mungu haitii watu
1) Rum. 2:11
2) Efe. 6:9
2. Petro na Yakobo
a. Mungu hatii watu (1 Petro 1:17)
b. Kwasababu Mungu haoneshi upendeleo, vivyo hivyo watu wake Yakobo 2:1
3. Yohana
a. Mojawapo ya maelezo marefu kuhusu uwajibikaji wa waamini yanaonekana katika 1 Yohana 4:20.

I. Hitimisho

A. Ubaguzi au kwa maana hiyo, uonevu wa aina yoyote haufai kabisa kwa watoto wa Mungu. Hapa kuna nukuu kutoka kwa Henlee Barnette aliyezungumza katika mkutano/kikao Glorieta New Mexico katika kamisheni ya maisha ya mkristo mwaka 1964. “Ubaguzi ni imani dhidi ya dini kwa sababu si wa kibiblia wala Kikristo wala wa kisayansi”.
B. Suala hili linawapa Wakristo fursa ya kuonesha upendo wao wa Kikristo msamaha na uelewa kuhusu ulimwengu uliopotea kuja kwa Kristo.
C. “Nifanye nini” (Sehemu hii inatolewa katika kamisheni ya maisha ya Mkristo iitwayo “mahusiano ya mataifa”)

KATIKA KIWANGO CHA MTU”

- Kubali kuwajibika binafsi katika kutatua matatizo yanayohusiana na taifa.
- Kupitia maombi, kusoma biblia na kushirikiana na mataifa mengine na kupambana na maisha ya uonevu wa mataifa mengine.
- Elezea msimamo wako kuhusu ushindani uliopo, hasa pale waliochochea ushindani wa chuki hawakupingwa

KATIKA MAISHA YA FAMILIA”

- Tambua umuhimu wa athari ya familia katika kueneza tabia kwa mataifa mengine.

- Jaribu kuendeleza tabia za Kikristo kwa kuzungumza juu ya kile ambacho watoto na wazazi wanasikia kuhusu maswala ya mataifa nje ya nyumbani kwao.
- Wazazi wanapaswa kuwa waangalifu kwa kuonesha mifano ya mienendo ya Kikristo kwa kuhusiana na watu wa mataifa mengine
- Tafuta fursa kufanya urafiki wa kifamilia kwa watu wa mataifa yote.

NDANI YA KANISA LAKO"

- Kwa mahubiri na mafundisho ya ukweli wa Biblia kuhusiana na mataifa, mkutano unaweza kuhamasisha kuonesha mfano kwa jamii nzima.
- Uwe na uhakika kuwa, ibada, ushirikiano na huduma kupitia kanisani viko wazi kwa wote hata vile ambavyo makanisa ya Agano Jipya yalivyoona kutokuwepo kwa vizuizi vya kimataifa (Efe. 2:11-22 Wagalatia 3:26-29)

KATIKA MAISHA YA KILA SIKU"

- Saidia kuondoa ubaguzi wa kimataifa wa aina zote katika ulimwengu wa kazi.
- Fanya kazi kupitia katika taasisi za kijamii za aina zote ili kupata haki sawa na fursa ukikumbuka kuwa ni tatizo la kimataifa linalotakiwa kushambuliwa, na sio watu, lengo ni kukuza uelewa na sio kuunda machungu.
- Ikionekana inaunda kamati maalumu za wananchi walengwa kwa lengo la kufungua njia za mawasiliano katika jamii kwa ajili ya kuwaelimisha wote katika mambo na vitendo maalumu katika kuboresha mahusiano ya mataifa.
- Saidia vyombo vya sheria na watunga sheria katika kupitisha sheria, kukuza haki za kimataifa na kupinga wale karibu haki kwa faida za kisasa.
- Pendekeza mtumiaji wa maarifa wa sheria kuitumia bila upendeleo.
- Epusha vurugu na hali ya kuheshimu sheria ili kufanya uwezekano wa mambo wa mambo kwenda sana kama raia Mkristo hakkikisha kuwa mfumo wa kisheria haitumiki kama vyombo vya kuwawezesha wanaojenga ubaguzi.
- Onesha mfano wa roho na fikra za Kristo kwa mahusiano yote ya wanadamu

◙" **Kristo ni yote, na katika yote**" Yesu ni usawa wenye uwanja mpana. Katika yeye tofauti zote za wanadamu zinaondolewa katika upendo wa Mungu! Wote wanaweza kuja, wote wanakaribishwa, wote wamekuwa familia (kama vile. Gal. 3:28). Wokovu katika Kristo ni kulipindua lile Anguko (kama vile Kol. 3:10, "sura") na ule Mnara wa Babeli (kama vile Mwanzo 10-11, mgawanyo wa watu
.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOROSAI 3:12-17**
**12 Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, 13 mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. 14 Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu. 15 Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani. 16 Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi zarohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. 17 Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.**

**3:12** "**mkichukuliana, na kusameheana**" Haya maneno yalitumika kuielezea Israeli (yaani, Kut. 19:5-6; Kumb. 4:37; 7:7,8; 10:15), lakini sasa yanalielezea kanisa (kama vile Gal. 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Tazama Mada Maalum: Takatifu katika Efe. 1:4. Tambua kwamba lengo la watu wa Mungu ni utakatifu kupiatia uchaguzi (kama vile Efe. 1:4), si kusimama kwa upendeleo. Israeli ilichaguliwa kama chombo kuwafikia wanadamu wote waliofanywa

katika sura ya Mungu. Israeli ilikosa mamlaka yake ya kiinjili (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5). Kwa udhihirisho kanisa limepewa kazi hii (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:46-47; Matendo 1:8). Waamini wanaitwa kuwa watakatifu na kuwa mashahidi. Tazama Tambuzi za Ndani kwa Waefeso 1:1-23, C. Pia tambua kwamba uchaguzi hauwezi kutengwa na jukumu la waamini la utendaji. Ukuu wa Mungu na yale mapenzi ya mwanadamu vinaungana katika dhana hii ya "agano." Mungu huanzisha na kupangilia hali, lakini wanadamu yawapasa kuitikia na kuendelea kuitikia!

◙ "**jivikeni** " Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uluiopita usio timilifu ambayo inadokeza umuhimu. Yawezekana kuwa ilikuwa ni istilahi ya kiubatizo (kama vile Gal. 3:27). Huu muktadha, unaoanza na "kuvua" (Kol.3:8-10), hufanana na Gal. 5:19-21 ("matendo ya mwili") na 5:22-
25 ("lile tunda la Roho"). Maisha ya milele yana muonekano wa sifa!

**NASB "moyo wa huruma"**
**NKJV "upole"**
**NRSV, TEV "huruma"**
**NJB "moyo wa huruma ya dhati"**

Kifasihi hii ni "hali ya kuonea huruma" (kama vile 2 Kor. 6:12; Flp. 1:8; 2:1; Filemoni 7,12,20). Watu wa kale waliamini kuwa makazi ya hisia yako katika eneo la ndani (fumbatio).

◙ "**moyo wa rehema**" Huu lazima uwe mwitikio wa Mkristo kwa wengine (kama vile Rum. 2:4; 9:23; 11:22; 2 Kor. 6:6; Gal.5:22; Efe. 4:32; Kol. 3:12; Tito3:4).

◙"**utu wema**" Hii ndiyo sifa pekee ya Mkristo (kama vile Efe. 4:2; Flp. 2:3). Wale wenye uvumilivu walitazamia unyenyekevu (upole) kama udhaifu na hawakuliweka hili katika orodha yao ya maadili. Ni watu wawili pekee katika Biblia walio wapole, Musa (kama vile Hes. 12:3) na Yesu (kama vile Mt. 11:29; Flp. 2:8). Hii sifa ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini (kama vile Mt. 18:4; 23:12; Yakobo 4:6,10; 1 Pet. 5:5,6). Neno hili linatumika katika maana hasi katika Kol. 2:18,23.

◙ " **unyenyekevu** " Kwa asili hili lilirejelea wanyama wafugwao (farasi, ngamia, punda) ambao nguvu zao zimeelekezwa kwa kusudi la bwana wao. Mungu hataki kutuharibu, bali kuzielekeza neema zake katika Utukufu Wake. Paulo mara nyingi anatumia stiari hii kwa maisha ya Mkristo (kama vile 1 Kor. 4:21; 2 Kor. 10:1; Gal.5:23; 6:1; Efe. 4:2; Kol. 3:12; 1 Tim. 6:11; 2 Tim. 2:25).

**3:13**
**NASB, NKJV "mkichukuliana"**
**NRSV, NJB "mkisaidiana"**
**TEV "mkivumiliana"**

◙"**uvumilivu** " Hii aya mara nyingi inatumika kwa uvumilivu wa Mungu na watu (kama vile Rum. 2:4; 9:22; Tito 3:2, 1 Pet. 3:20) ama uvumilivu wa Yesu (kama vile 1 Tim. 1:16; 2 Petro 3:15). Hii inatumika kuwasihi waamini katika kutendeana mambo (kama vile 1 Kor. 13:4; Gal. 5:22; Efe. 4:2; 2 Tim. 4:2). Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo (inayotumika kama shurutishi), ambayo inamaanisha hiari ya kutokulipiza kisasi (kama vile Efe. 4:2; Flp. 2:3-4).

◙"**kusameheana**" Hii ni njeo ya kati ya wakati iliyopo endelevu (yenye ushahidi). Hii inatokana na mzizi wa neno hilo hilo la Kiyunani kama neema, "kusamehe kwa uhuru." Moja ya alama ya waamini waliosamehewa ni kwamba wanawasamehe wengine (kama vile Mt. 5:7; 6:15;18:22-35; Marko 11:25; Luka 6:36-38; Efe. 4:32; Yakobo 2:13; 5:9). Msamaha kwa wengine si msingi wa msamaha, bali ni tunda.

◙"**mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake**" Hii ni sentensi yenye masharti daraja la tatu, ambayo ilimaanisha tendo la wakati ujao lisilo na shaka. Kutakuwa na kulaumiana! Wakristo watakuwa katika nafasi pamoja na Wakristo wengine, lakini msalaba wa Yesu lazima kulizuia hili (kama vile Rum. 14:1-15:13).

◙"**kama Bwana alivyowasamehe ninyi**" Huu ndiyo msingi kwa matendo ya mwamini kwa wengine (kama vile Efe. 4:32;Rum. 15:7).Kuna tofauti ya machapisho ya Kiyunani kati ya "Bwana," "Kristo," "Mungu" na "Mungu katika Kristo." "Bwana" zinazopatikana katika machapisho ya kale ya Kiyunani P46, A, B, D*, na bila shaka ni halisi.

**3:14**"**jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu**" Upendo, ambao uko katika umoja, ni alama ya tofauti ya Mkristo (kama vikle Efe. 4:2-3; 1 Kor, 13; Gal. 5:22).

**3:15**"**Na amani ya Kristo**" Hili neno kwa uhalisia "kufungunisha kwa pamoja kile kilicho katika" (kama vile Yohana 14:27; 16:33; Fpl. 4:7). Katika Agano Jipya kuna njia tatu zinazozungumzia amani.

1. kama shamilisho (mafundisho) ya amani yetu na Mungu kupitia Kristo (kma vile Kol. 1:20)
2. kama kiima (ki uzoeful) ya sisi kuwa sahihi na Mungu (kama vile Yohana 14:27; 16:33; Flp.
3. kama Mungu akiwaunganisha waamini wa Kiyahudi na watu wa Mataifa katika mwili mmoja kupitia Kristo ambayo ni siri ya Mungu (kama vile Efe. 2:14-17; Kol. 3:15)
   Tazma Mada Maalum: Amani katika Kol. 1:20.

◙"**ndiyo mliyoitiwa**" Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Katika kutofautisha na walimu wa uongo watendao kama mpatanishi katika Kol.2:18, Kristo ndiye mwamuzi wetu pekee, kiongozi, na msuluhishi

**2:18,** Kristo ni hukumu yetu pekee, mwongozo, na mpatanishi.

◙". . . **mioyoni**" Tazama Mada Maalum: Moyo katika Kol. 2:2.

◙" **mliyoitiwa**" Mara nyingi Mungu huuchukua uanzilishi wake katika wito, kuchagua, na kuwabembeleza Kwake waamini (kama vile Kol. 3:12; Yohana:44, 65; Efe. 1:4-5,11). Neno "kuita" (*kaleō*) linatumika katika maana mbali mbali ya kitheolojia.

1. wenye dhambi wanaitwa na Mungu katika wokovu kupitia Kristo
2. wenye dhambi wanaliitia jina la Bwana ili waweze kuokolewa (kama vile Rum. 10:9-13)
3. waamini wanaitwa kuishi maisha ya kumfanana Kristo (kama vile Efe. 4:1)
4. waamini wanaitwa kwa ajili ya kazi ya huduma (kama vile 1 Kor. 12:4-7) Tazama Mada Maalum katika Efe. 4:1.

◙"**katika mwili mmoja**" Hili linazungumzia juu ya umoja katikati ya hali ya kuwa tofauti (kama vile Kol. 1:18,24; Efe. 4:4-6)! Tambaua kwamba ule msistizo si wa uchaguzi binafsi, bali uchaguzi wa ushirika. Wokovu ni kushirikiana, si wa binafsi. Katika kupambana na matumizi mabaya ya madalaka katika Kanisa la Kirumi, wale Wapenzi wa Mageuzi walisististiza haki na majukumu ya mtu binafsi mbele za Mungu. Hata hivyo, uumbaji unakuwa usemi wa kibiblia zaidi. Biblia haifundishi "ukuhani wa mwamini," lakini "ukuhani wa waamini."Hili si fundisho linalosistiza uhuru wa mtu binafsi, bali (1) jukumu la maisha ya mwili kwa kila muumini (kama vile 1 Kor. 12:7) na (2) Agizo Kuu la Ukristo (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Matendo 1:8).

◙"**iweni watu wa shukrani**" Hii ilikuwa ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo, "kuendelea kuwa watu wa shukrani" Shukrani ni alama ya ukomavu wa Ukristo, ukubalifu wa maisha ya kujazwa yule Roho (kama vile Kol. 3:17; Efe. 5:20; 1 The. 5:18). Si ukubalifu kwa uamuzi (Uislam), lakini mtazamo wa kibiblia kwamba Mungu yu pamoja nasi na kwetu hata katikati ya magumu na mambo ya ulimwengu huu ulioanguka!

**3:16**"**Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu**" Hii ni kauli tendaji shututishi ya wakati ujao ya nafsi ya pili umoja. "neno la kristo " hii inaweza kurejelea (1) injili; (2) Uwepo wake binafsi; ama (3) yule Roho. Tambua kwamba huyu akaaye ndani si yule anayejiendesha mwenyewe (kwa vyo vyote ni wa binafsi ama

ushirika). Waamini yawapasa kushirikiana katika maisha ya Ukristo kama wanavyofanya katika wokovu. Kuna tofauti nyingine ya machapisho hapa ambayo ni sawa na ile iliyo katika Kol. 3:13 na 15. Wale Waandishi weledi elekea kuziunganisha semi za Paulo. Hiki kifungu "neno la Kristo," ni usemi pekee unaopatikana hapa tu katika Agano Jipya. Kwa hiyo, huu ulibadilishwa katika neno "neno la Mungu" (MSS A, C*) ama "neno la Bwana" (MS .)*א Kwa machapisho mazuri zaidi ya Kiyunani, P46, 2 ,אB, C2, D, F, G, na tafsriri za kale zilizo nyingi zina "neno la Kristo."Maelezo ya muhtasari wa Waefeso na Wakolosai yana fanana sana. Ule unaofananishwa na mstari huu katika Efe. ni 5:18! Maisha yenye kujazwa na yule Roho ni ya kumfanana Kristo kila siku ama kuliruhusu neno la Kristo na akili za Kristo kuongoza katika kila eneo, hasa mahusiano kati ya watu. Kuna utata katika mstari huu unaohusiana na kihusishi cha Kiyunani "ndani" (*en*). Pia hiki kinaweza kutafsiriwa kama"kati." Kihusishi "Ndani" kinaweza kuwa mtazamo binafsi, ambapo kihusishi "kati" ni mtazamo wa

ushirikiano (kama vile Kol. 1:27).

◙"**katika hekima yote**" Hii ni kejeli juu ya msistizo wa walimu wa uongo kuyahusu maisha ya mwanadamu. Neno la Kristo (maisha ya kujazwa na Roho Mtakatifu)ni hekima ya kweli. Hekima ni mtu (kama vile Mit. 8:22-31) na mtindo wa maisha, si kweli iliyojitenga ama kanuni.

◙"**zaburi**" Zile tafsri za NKJV na NASB zinamaanisha "mafundisho pamoja na nyimbo," lakini zile za NRSV na NJB zinamaanisha "walimu pamoja na nyimbo katika mioyo yao." Toleo la TEV linamaanisha kumwabudu Mungu kwa nyimbo. Mkanganyiko wa sasa kuhusiana na upendeleo wa kimuziki katika ibada unawezwa kuelezwa kwa mstari huu (na Efe.5:19) katika aina kadhaa na tofauti tofauti za muziki zinazoelezwa: (1)zaburi; (2) nyimbo za kumtukuza Mungu ; na (3) tenzi za rohoni. Japokuwa hatuwezi kuzitambua aina zote ni dhahiri kwamba kanisa la kale lilitumia miundo kadhaa na tofautitofauti ya muziki. Ufunguo ni moyo wa yule anayeabudu, si muundo wa muziki (kama Vile Kol.3:17).

**3:16-17** Kuna ufanano wa kitheolojia na kimuundo kati ya Efe. 5:18-21 na Kol. 3:16-17. Katika Waefeso kuna kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo, "kujazwa kivyovyote vile,"ambapo katika wakolosai kuna kauli tendaji shurutishi, "neno la kristo likae ndani mwenu." pia katika waefeso kauli shurutishi inafuatiwa na kauli tano endelevu za wakati uliopo ambazo zinaeleza maisha ya kujazwa yule.

(1) Kol. 3:19, mkifundishana katika zaburi, nyimbo za kumtukuza Mungu, na tenzi za rohoni kauli tendaji ya wakati uliopo)
(2) Kol. 3:19, mkiimba (kauli tendaji ya wakati uliopo)
(3) Kol. 3:19, kifarijiana (kauli tendaji ya wakati uliopo)
(4) (4) Kol. 3:20, mkitoa shukrani (kauli tendaji ya wakati uliopo)
(5) Kol. 3:21, iweni watii kwa kila mmoja wenu (kauli ya kati ya wakati uliopo)

Katika Wakolosai baadhi ya kauli za wakati uliopo endelevu pia zinatokea.

(1) Kol. 3:16, mkifundishana (kauli tendaji ya wakati uliopo)
(2) Kol. 3:16, mkionyana kwa zaburi, nyimbo, na tenzi za rohoni (kauli tendaji ya wakati uliopo)
(3) Kol. 3:16, mkiimba (kauli tendaji ya wakati uliopo)
(4) Kol. 3:17, mkitoa shukrani (kauli tendaji ya wakati uliopo)

**3:17 "Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo**" Hii ndiyo kweli kuu ya kiroho. Waamini lazima wahusianishe shauku na matendo yao yote kwa Mungu kupitia Kristo. Kila kipengele cha maisha yetu ni " katika jina la Bwana ." Waamini hawaishi maisha yao wenyewe (kama vile Kol. 3:23; Rum. 14:7-9; 1 Kor. 10:31; 2 Kor. 5:15; Efe. 6:7; 1 Pet. 4:11). Kweli ingeweza kupindua ule usasa, umagharibi, kanisa lenye mtazamo binafsi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAKOLOSAI 3:18-21**
**18 Ninyi wake, watiini waume zenu, kama ipendezavyo katika Bwana. 19 Ninyi waume, wapendeni wake zenu msiwe na uchungu nao. 20 Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote; maana jambo hili lapendeza katika Bwana. 21 Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa.**

**3:18** "**wake**, **watiini waume zenu**" Hiii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo. Neno la Kristo (yaani, maisha ya kujazwa na Roho, kama vile Efe. 5:18) likikaa ndani ya mwamini linaleta matokeo kila eneo la maisha! Ufanano ni Efe. 5:21-22; Tito 2:5; 1 Pet. 3:1, lakini kumbuka Wakolosai iliandikwa kwanza. Waefeso inaeleza kanuni ya ulimwengu ya utii kwa waamini wote katika Efe. 5:21 (kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo) na kuitumia nyumba ya Mkristo kama mfano wa makazi matatu fungamano ya zilivyo kazi za maisha ya "kujazwa na Roho " katika maisha ya kila siku: (1)waume - wake, 5:22-31; (2) wazazi-watoto, 6:1-4 na (3) mabwana-watumwa, 6:5-9. Mjadala huu unaonekana hasi kwetu kwa maisha ya sasa, bali katika siku zake ulikuwa na alama chanya. Yale makundi matatu ambayo yana mwongozo wa kiutamaduni wa moja kwa moja (waume, wazazi, na mabwana wa watumwa) ni wanaonywa kwa usawa kama wale waliokuwa hawana nguvu ya kiraia ama haki (wake, watoto, na watumwa). Haya mamlaka ya kibinafsi ni mfano wa kinyume cha Anguko. Ni tofauti gani anitegenezayo Kristo.
Tazama Mada Maalum: Utii (*hupotassō*) katika Efe. 5:21.

**3:18-19** Katika muktadha huu na ufanano wake, utii ulikuwa kati ya wawili waliooana, si wanaume na wanawake katika ujumla. Kanuni ya wanaume kuwa kichwa inaanza ndani ya Bibli nzima, kutoka Mwanzo 3 hadi mbele. Hata hivyo, kichwa cha mwanamme wa ki-Kristo kinabainishwa na, na kushurutishwa (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo) kuwa, ya kikafara, kujitoa, Upendo unaofanana na Kristo (Kama vile Efe. 5:25, 28-29). Kichwa katika Agano Jipya ni utumishi (kama vile Mt.20:25-27; 23:11) pamoja na Kristo kama mfano.

Katika siku zetu "utii" ni neno lililo kinyume, lenye kuvutia. Ki-uhalisia hili lilikuwa neno la kijeshi ambalo lilihusiana na utiifu uliojikita juu ya amri. Katika Agano Jipya, hata hivyo, hili mara nyingi lililotumika kwa mtazamo wa Yesu kuwaelekea wazazi wake wa kidunia (kama vile Luka 2:51) na Baba Yake wa mbinguni (kama vile 1 Kor. 15:28). Paulo alilipenda neno hili na alilitumia mara 23. Waefeso 5:21 inaonyesha hii ni kanuni ya ulimwengu ya kiroho iliyounganishwa na maisha ya kujazwa Roho. Utii unaenda tofauti na utamaduni wetu, ki-Magharibi, mtazamo wa mpangilio binafsi wa kififkra. Ubinafsi umekolea sana (kama vile Rum. 12:10; Gal. 5:13; Flp. 2:3; 1 Yohana 4:11)!
Tazama Mada Maalum: Utii katika Efe. 5:21.

◙"**kama ipendezavyo katika Bwana"** Ufanano wa ki- Waefeso una neno "kama kwa Bwana." Toleo la TEV linatafsiri hiki kifungu kama "kwa hili ndivyo mnavyopaswa kufanya kama Wakristo" (kama vile Kol. 3:20). Waamini yawapasa kuwachukulia katika upendo, kwa njia ya utii si kwa sababu ya kuwafaidisha wengine, bali kwa sababu wao ni Wakristo (kama vile Kol. 3:23-23). Roho humruhusu mwanadamu aliyeanguka kuiongoza tamaa yake mwenyewe kwenye tamaa za wengine, kama Yasu alivyofanya (kama vile 2 Kor. 5:14-15; 1 Yohana 3:16).

**3:19**
**NASB "msiwe na uchungu nao"**
**NKJV "msiwe na uchungu juu yao"**
**NRSV "msiwachukulie kwa ukali"**
**TEV "na msiwe wakali kwao"**
**NJB "na msiwashutumu"**

Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi, ambayo mara nyingi inamaanisha kustisha tendo lililo katika mchakato. "Ninyi, wenyewe, uzuieni uchungu." Kuna ufanano wa moja kwa moja wa kifungu hiki katika Waefeso 5, lakini Kol. 3:28-29 inaeleza kweli ile ile katika maana ya chanya. Katika dhana ya kibiblia ya "mwili mmoja" (kama vile Mwanzo 2) ndoa ambamo wanaume huwachukulia wake zao katika namna za upendo, wanajibariki wenyewe na kuwabariki wengine. Mtu kumpenda mke /mme wake ni , katika maana moja,kujipenda mwenyewe. Katika nyumba ya Mkristo mapenzi yetu kwa familia huyaaksi mapenzi yetu kwa Mungu na ni ushahidi wenye nguvu kwa ulimwengu uliochanganyikiwa na uliojeruhiwa.

**3:20 " watoto, watiini**" Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo, "endeleeni kuwa watii." Katika Efe. 6:1-4, hii mamlaka inapanuliwa kwa ajili ya kuhusiana na Kut. 20:12 na Kumb. 5:16, Mheshimu baba yako na mama yako." Katika muktadha huu, "maana jambo hili lapendeza katika Bwana" husianisha hili agizo kwa watoto wa ki-

Kristo.

Tambua kwamba watoto wanaagizwa kuwa watii, lakini wake wanaagizwa kujishusha. Katika mambo yote ni familia za ki-Kristo ambazo zinaagizwa. Jambo moja ambalo ni gumu kulisuluhisha kati ya hili na siku zetu ni "umri walionao watoto?" Katika utamaduni wa Kiyunani mvulana anawajibika kuitii Sheria na alioa katika umri wa miaka kumi na tatu, msichana katika umri wa miaka kumi na mbili. Katika utamaduni wa Kirumi mvulana alitambuliwa kama mwanamme katika umri wa miaka kumi na mine na katika utamaduni wa Kiyunani katika umri wa miaka kumi na minane.

**3:21"Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu**" Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambayo inamaanisha kustisha tendo lililo katika mchakato, "msiwachokoze watoto wenu." hili jukumu la kukubaliana ni dhahiri (kama vile efe. 6:4). Mara nyingi kumekuwa na kizuizi cha ki-kizazi. Wakristo (wote wazazi na watoto) lazima wayashughulikie mahusianao kwa namna tofauti kwa jinsi walivyojitoa kwa Kristo. Mjadala wa Paulo wa mahusiano sahihi ndani ya nyumba kwa ujumla ulikuwa tofauti kwa utamaduni na desturi za zile siku zake. Moja kwa moja Paulo alimweleza mtu pamoja na nguvu ya kitamaduni na mamlaka (waume, wazazi, na mabwana wa watumwa) na aliwaonya kuwapa furaha wale walio chini yao (wake, watoto, na watumishi wa numbani) kwa utu na upendo wa Kristo (zaidi kama Filemoni). Waamini ni watumishi wa Mungu, si wamiliki! Namna tunavyochukuliana inamaanisha kuonyesha zama mpya kwa ulimwengu uliopotea.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAKOLOSAI 3:22-4:1**

**[22] Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana. [23] Lo lote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, [24] mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo. [25] Maana adhulumuye atapata mapato ya udhalimu wake, wala hakuna upendeleo. [1] Ninyi akina bwana, wapeni watumwa wenu yaliyo haki na ya adili, mkijua ya kuwa ninyi nanyi mna Bwana mbinguni.**

**3:22** " **watumwa, watiini watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote**" hapatakiwi kuwa na ukatishaji wa ibara katika Kol. 3:22. Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo, "endeleni kuwa watii." Huu ni mfano wa tatu unaotoka ndani ya nyumba ya Mkristo (kama vile Efe. 6:5-9). Katika siku zetu hili linaweza kuhusiana (yaani, kutumika kwa) na waajiri wa ki-Kristo na waajiriwa. Katika Waefeso, na bila shaka pia katika Wakolosai, hili linarejelea kwa wote wale mabwana waliookolewa na wale waliopotea. Mimi binafsi siliamini hili "katika mambo yote"rejea juu ya uovu ama dhambi (kama vile Matendo 5:29). Huu ni usemi wa moja kwa moja unaoonya kuhusiana na utii, si leseni kwa waamini kushiriki katika mambo ambayo hayako katika Maandiko. Hili pia ni la kweli kwa wanawake (kama vile Kol. 3:18; Efe. 5:22). Tazama Mada Maalum: Onyo la Paulo kwa watumwa katika Efe.6:5.

◙"**kwa moyo"** Tazama Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM : KARIMU/ TIIFU

Neno hili (*haplotēs*) lina vidokezo viwili, “wema” au “uaminifu.” Ni sitiari iliyohusiana na maono. Katika Agano la Kale jicho lilitumika kama sitiari kwa ajili ya kusudi katika njia mbili.

1. Jicho baya (bahili, kama vile Kumb. 15:9 na Mith. 23:6; 28:22)
2. Jicho jema (wema, kama vile Mith. 22:9)

Yesu alifuatisha matumizi haya (kama vile Mt. 6:22-23; 20:15).

Paulo alilitumia neno hili kwa maana mbili.

1. "urahisi, uaminifu, usafi" (kama vile 2 Kor. 1:12; 11:3; Efe. 6:5; Kol. 3:22)
2. "ukarimu" (kama vile Rum. 12:8; 2 Kor. 8:2; 9:11,13)

**3:23** Kumtumikia Bwana ni shauku ya Wakristo wote katika shughuli zao (kama vile Kol. 3:17; Efe. 6:7; 1

Kor.10:31)! Waamini lazima wawe wa kila siku, waishi kwa ushuhuda wa nguvu ya ukombozi wa Mungu!

**3:24** Katika ulimwengu wa kale watumwa hawakuwa na haki ya urithi. Bali sasa, katika Kristo, wanazo! Mungu anakwenda kuwapa thawabu wale wanaompenda, wanaomsujudu, na kumtumikia (kama vile Kol. 3:23; Efe. 6:8).

**3:25** Hukumu ya ki-Ungu huleta upendeleo (kama vile Kumb. 10:17; Matendo 10:34; Rum. 2:11; Efe. 2:9; 6:9;1 Pet. 1:17). Kanuni hii inaelezwa kwa usahihi katika Gal. 6:7. Hata waamini watatoa hesabu kwa Mungu, si kwa ajili ya dhambi, bali kwa ajili ya utumishi (kama vile 2 Kor. 5:10). Dhambi ina matokeo katika wakati na ule umulele!

**4:1** Hili linaonyesha majukumu ya kiukubalifu (kama vile Kol. 3:19, 21). Si kama Waefeso, andiko hili linanena na wamiliki wa watumwa wa ki- Kristo (kama vile Filemoni). Tafsri ya NIV Study Bible (uk. 1817) inaongeza oni lenye kuvutia: " Sababu ya Paulo kuandika kuhusu watumwa na mabwana kuliko wake, waume, watoto, na akina baba inaweza kuwa ile ya mtumwa Onesimo (kama vile Kol. 4:9) inaenda pamoja na Tychicus kuuleta huu waraka wa Wakolosai kwa Filemoni, bwana wa Onesimo', ambaye pia aliishi huko Kolosai" Mstari huu kimuktadha lazima uendane na sura ya 3. Unahitimisha mfano wa jamaa za Paulo wa maisha yanayofanana na Kristo. Mada Maalum: Onyo la Paulo kwa Watumwa katika Efe. 6:5.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Kwa jinsi gani tulikufa na Kristo? Je! hili linamanisha nini katika maisha yetu ya kila siku?
2. Kwa nini mistari ya 11 na 17 ni muhimu sana katika imani ya Kristo?
3. Toa ufafanuzi wa neno "kutii." Je! hili linazungumzia uduni? Kwa nini ama kwa nini si vyo?
4. Kwa nini nyumba ya Mkristo imetumika kama mfano wa usawa wa unyenyekevu?

# WAKOLOSAI 4

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maonyo | Neema ya Mkristo | Wajibu wa Mkristo (3:18-4:6) | Maelekezo | Roho ya Kitume |
| 4:2-6 | 4:2-6 | 4:2-4<br>4:5-6 | 4:2-4<br>4:5-6 | 4:2-4<br>4:5-6 |
| Salamu za mwisho | Salamu za mwisho | Ufunguzi | Salamu za mwisho | Habari binafsi |
| 4:7-9 | 4:7-15 | 4:7-9 | 4:7-9 | 4:7-9 |
| | | | | Salamu na heri<br>Za mwisho |
| 4:10-27 | | 4:10-17 | 4:10-11<br>4:12-14 | 4:10-14 |
| | Kufunga kwa Maonyo<br>Baraka<br>4:16-18 | | 4:15-17 | 4:15-17 |
| 4:18 | | 4:18 | 4:18a<br>4:18b | 4:18 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka **"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo, linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 4:2-4**

**[2] Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani; [3] mkituombea na sisi pia, kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo, ambayo kwa ajili yake nimefungwa, [4] ili niidhihirishe, kama inipasavyo kunena.**

**4:2**
**NASB "jitoeni wenyewe katika kuomba"**
**NKJV "kuendelea kwa dhati katika kuomba"**
**NRSV "kuwa na bidii katika kuomba"**
**TEV "kuwa mstahimilivu katika kuomba"**
**NJB "muwe wastahimilivu katika maombi yenu"**

Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo, "endeleeni kujitoa wenyewe katika maombi." Maombi sio jambo la hiari. Maombi ni muhimu kwa ufanisi wa maisha ya Mkristo na huduma (kama vile Efe. 6:18-19; Rum. 12:2; Fil. 4:6; 1 The.5:17). Ikiwa Yesu, ndiye Mungu wa milele, alikuwa na tabia ya maombi ya wazi na maombi binafsi, je ni zaidi kiasi gani waamini wanahitaji kuomba kwa ajili ya injili, kwa ajili yao wenyewe na kuombeana wenyewe kwa wenyewe? Angalia Mada Maalum: Maombi yenye ufanisi katika Waefeso 6:19

**NASB, NRSV**
**TEV "Kuwa macho"**
**NKJV "kuwa macho"**
**NJB "kukaa macho"**

Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ikifanya kazi kama shurutishi. Maombi yanataka mipango, ustahimilivu na kuwa macho. Inahitaji kuwa mtindo wa maisha na sio tukio.

▣**"shukrani"** Angalia sehemu tatu za maombi katika Wakolosai 4:2. Pia kumbuka Paulo alikuwa amefungwa, na bado barua hii ilisisitiza "shukrani" (kama vile Kol. 1:3,12; 2:7; 3:15-17; 4:2). Ukweli wa Biblia (muono) unabadilisha namna unavyoyaangalia maisha (kama vile Warumi 8:31-39). Shukrani ina tabia ya kuja na roho mtakatifu (kama vile Efe 5:20; 1 The 5:18).

**MADA MAALUM: SALA YA SHUKRANI**

I. Utangulizi
    A. Huu ni mwenendo sahihi wa mwamini kumwelekea Mungu
        1. Hiki ndio chanzo cha sifa zetu kwa Mungu kupitia Kristo
            a. 2 Wakorintho 2:14
            b. 2 Wakorintho 9:15
            c. Wakolosai 3:17
        2. Hili ni kusudio sahihi kwa ajili ya huduma, 1 Kor. 1:4
        3. Hii ni dhamira endelevu ya mbinguni:
            a. Ufunuo 4:9
            b. Ufunuo 7:12
            c. Ufunuo 11:17
        4. Hii ndio dhamira endelevu ya waumini
            a. Wakolosai 2:7
            b. Wakolosai 3:17
            c. Wakolosai 4:2

II. Vikorokoro vya Biblia
    A. Agano la Kale
        1. Maneno mawili ya msingi
            a. *yadah* (BDB 392, KB 398), ikimaanisha sifa
            b. *todah* (BDB 392, KB 1695), ikimaanisha sala ya shukrani. Mara nyingi lilitumika kwenye utoaji wa dhabihu (kama vile 2 Nya. 29:31; 33:16)
        2. Daudi aliwachagua Walawi maalumu kwa ajili ya kumsifu na kumshukru Mungu. Hili liliendelezwa na Sulemani, Hezekia, na Nahemia.
            a. 1 Nyakati 16:4,7,41

b. 1 Nyakati 23:30
c. 1 Nyakati 25:3
d. 2 Nyakati 5:13
e. 2 Nyakati 7:6
f. 2 Nyakati 31:2
g. Nahemia 11:12
h. Nahemia 12:24,27,31,38,46

3. Kitabu cha Zaburi ni mkusanyiko wa sifa na shukrani za Waisrael.
   a. Shukrani kwa YHWH kwa ajili ya uaminifu wake kwenye agano
      1) Zaburi 107:8
      2) Zaburi 103:1 na kuendelea
      3) Zaburi 138:2
   b. Shukrani ilikuwa ni sehemu ya kimchakato ndani ya hekalu
      1) Zaburi 95:2
      2) Zaburi 100:4
   c. Shukrani ilisindikizwa na utoaji dhabihu
      1) Zaburi 26:7
      2) Zaburi 122:4
   d. Shukrani ilitolewa kwa ajili ya matendo ya YHWH
      1) Kuwakomboa toka mikononi mwa maadui
         a) Zaburi 7:17
         b) Zaburi 18:49
         c) Zaburi 28:7
         d) Zaburi 35:18
         e) Zaburi 44:8
         f) Zaburi 54:6
         g) Zaburi 79:13
         h) Zaburi 118:1,21,29
         i) Zaburi 138:1
      2) Ukombozi toka gerezani (isitiari), Zaburi 142:7
      3) Ukombozi toka katika mauti
         a) Zaburi 30:4,12
         b) Zaburi 86:12-13
         c) Isaya 38:18-19
      4) Aliwashusha chini waovu na kuwainua wenye haki
         a) Zaburi 52:9
         b) Zaburi 75:1
         c) Zaburi 92:1
         d) Zaburi 140:13
      5) Anasamehe
         a) Zaburi 30:4
         b) Isaya 12:1
      6) Hutoa kwa watu wake
         a) Zaburi 106:1 na kuendelea
         b) Zaburi 111:1
         c) Zaburi 136:1,26
         d) Zaburi 145:10
         e) Yeremia 33:11

B. Agano Jipya
   1. Neno kuu lililotumika kwa ajili ya shukrani na sala ya shukrani (baadhi ya nukuuu)
      a. *eucharisteō* (kama vile 1 Kor. 1:4,14; 10:30; 11:24; 14:17,18; Kol. 1:3,12; 3:17)

b. eucharistos (kama vile Kol. 3:15)
c. *eucharistia* (kama vile 1 Kor. 14:16; 2 Kor. 4:15; 9:11,12; Kol. 2:7; 4:2)
d. *charis* (kama vile 1 Kor. 15:57; 2 Kor. 2:14; 8:16; 9:15; 1 Pet. 2:19)

2. Mfano wa Yesu
   a. Alitoa shukrani kwa ajili ya chakula
      1) Luka 22:17,19 (1 Kor. 11:24)
      2) Yohana 6:11,23
   b. Alitoa shukrani kwa ajili ya maombi yaliyojibiwa, Yohana 11:41
3. Mifano mingine ya shukrani
   a. Kwa ajili ya zawadi ya Mungu ya Kristo, 2 Kor. 9:15
   b. Kwa ajili ya chakula
      1) Mdo. 27:35
      2) Warumi 14:6
      3) 1 Wakorintho 10:30; 11:24
      4) 1 Timotheo 4:3-4
   c. Kwa ajili ya uponyaji, Luka 17:16
   d. Kwa ajili ya amani, Mdo. 24:2-3
   e. Kwa ajili ya kukombolewa toka katika hatari
      1) Mdo. 27:35
      2) Mdo. 28:15
   f. Kwa ajili ya matukio yote, Wafilipi 4:6
   g. Kwa ajili ya wanadamu wote, hasa viongozi, 1 Timotheo 2:1-2
4. Sura nyingine za shukrani
   a. Ni mapenzi ya Mungu kwa waamini wote, 1 Wathesolanike 5:18
   b. Ni ushuhuda kwa ajili ya maisha yaliyojazwa na Roho, Waefeso 5:20
   c. Kutojali ni dhambi
      1) Luka 17:16-17
      2) Warumi 1:21
   d. Ni suluhisho kwa ajili ya dhambi, Waefeso 5:4
5. Shukrani za Paulo
   a. Baraka zake juu ya kanisa
      1) Kwa ajili ya kuitangaza injili
         a) Warumi 1:8
         b) wakolosai 1:3-4
         c) waefeso 1:15-16
         d) 1 wathesolanike 1:2
      2) Kwa ajili ya neema iliyotolewa
         a) 1 Wakorintho 1:4
         b) 2 Wakorintho 1:11; 4:15
      3) Kwa ajili ya kuipokea injili, 1 Wathesolanike 2:13
      4) Kwa ajili ya ushirika wa kuieneza injili, Wafilipi 1:3-5
      5) Kwa ajili ya ukuaji katika neema, 2 Wathesolanike 1:3
      6) Kwa ajili ya maarifa ya uchaguzi, 2 Wathesoalanike 2:13
      7) Kwa ajili ya Baraka za kiroho, Wakolosai 1:12; 3:15
      8) Kwa ajili ya wema katika utoaji, 2 Wakorintho 9:11-12
      9) Kwa ajili ya furaha kwa waamini wapya, 1 Wathesolanike 3:9
   b. Shukrani zake binafsi
      1) Kwa ajili ya kuwa muumini, Wakolosai 1:12
      2) Kwa ajili ya kukombolewa toka utumwa wa dhambi, Warumi 7:25; 2 Kor. 2:14
      3) Kwa ajili ya kazi ya utoaji dhabihu kwa ajili ya watu wengine, Warumi 16:4; 2 Kor. 8:16
      4) Kwa ajili ya baadhi ya matendo ambayo bado hayajatokea, 1 Wakorintho 1:14

5) Kwa ajili ya karama binafsi za kiroho, 1 Wakorintho 14:18
6) Kwa ajili ya ukuaji kiroho wa ndugu wengine, Filemoni 4-5
7) Kwa ajili ya nguvu ya huduma, 1 Timotheo 1:12

III. Hitimisho
A. Sala ya shukrani ni mwitikio wetu muhimu kwa Mungu mara tu tunapookolewa, haitolewi tu kwa ukubarifu wa maneno, bali kwa shukrani ya mfumo wa maisha
B. Sala ya shukrani katika vitu vyote ni lengo la maisha yaliyokomaa katika uangalizi wa Mungu (kama vile 1 The. 5:13-18)
C. Sala ya shukrani ni dhamira iliyopo ya maagano yote la kale na jipya. Je ni dhamira yako pia?

**4:3"Mkituombea na sisi pia"**Paulo alihitaji maombi ya maombezi. Katika Kol. 4:3, 4 (kama vile Efe 6:19-20), anawaombea vitu vitatu vinavyohusiana na kuhubiri kwake injili.

1. Mlango uliowazi kuhubiri (Mdo 14:27; 1 Kor. 16:9; 2 Kor. 2:12; Ufu. 3:8)
2. Uwezo wa kuelezea siri ya injili
3. Uwezo wa kuzungumza injili kwa usahihi.

**MADA MAALUM: MAOMBI YA KUSIHI**

I. Utangulizi
A. Maombi ni ya muhimu kwa sababu ya mfano wa Yesu
1. Maombi binafsi, Mk 1:35; Luka 3:21; 6:12; 9:29; 22:31-46
2. Kulisafisha Hekalu, Mt. 21:13; Mk 11:17; Luka 19:46
3. Maombi ya kuiga, Mt. 6:5-13; Luka 11:2-4
B. Maombi yanaweka kuamini kwetu kwenye hali ya kugusika kwa mtu, Mungu anayejali ambaye yupo , anayependa na kutenda kwa niaba yetu na kwa ajili ya wengine, kupitia maombi yetu.
C. Mungu binafsi amejizuia mwenyewe kutenda juu ya maombi ya watoto wake katika Nyanja nyingi (kama vile. Yakobo 4:2)
D. Kusudi kuu la maombi ni ushirika na muda wetu kwa Mngu wa Utatu.
E. Nafasi ya maombi ni mtu yeyote au kitu chochote kinachohusiana na waumini. Tunaweza kuomba,kuamini mara moja, au zaidi na zaidi tena kama fikra zinavyojirudia.
F. Maombi yanaweza kuhusisha ishara/dalili mbali mbali
1. Sifa na kuabudu kwa Mungu wa Utatu
2. Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya uwepo wake, ushirika, na upaji wake
3. Ukiri wetu wa utendaji dhambi, kwa hali zote za siku zilizopita na wakati sasa
4. Ombi la mahitaji yetu muhimu au hamu yetu
5. Usihi wetu pale tunapoyawasilisha mahitaji ya wengine mbele za Baba
G. Ombi la kusihi ni la ajabu. Mungu anawapenda wale tuwaombeao zaidi kuliko tufanyavyo, na bado maombi yetu yasifanye badiliko, uajibikaji, au hitaji lolote, sio tu kwetu binafsi, lakini hata kwao.

II. Taarifa za Kibiblia
A. Agano la Kale
1. Baadhi ya mifano ya maombi ya kusihi
a. Ibrahim aliomba maombi ya kuitetea Sodoma, Mwa. 18:22ff
b. Maombi ya Musa kwa ajili ya Israel
1) Kutoka 5:22-23
2) Kutoka 32:9-14,31-35
3) Kutoka 33:12-16
4) Kutoka 34:9
5) Kumbu. 9:18,25-29
c. Samweli akiiombea Israel
1) 1 Samweli 7:5-6,8-9

        2) 1 Samweli 12:16-23
        3) 1 Samweli 15:11
    d. Maombi ya Daudi kwa ajili ya watoto wake, 2 Samweli 12:16-18
2. Mungu anawatafuta waombeaji, Isaya 59:16
3. Dhambi ijulikanayo, usio ikiri, tabia usizozitubia zinaathiri maombi yetu
    a. Zaburi 66:18
    b. Mithali 28:9
    c. Isaya 59:1-2; 64:7

B. Agano Jipya
1. Huduma ya kusihi/kuombea ya Mwana na Roho
    a. Yesu
        1) Warumi 8:34
        2) Waebrania 7:25
        3) 1 Yohana 2:1
    b. Roho Mtakatifu, Warumi 8:26-27
2. Huduma ya Paulo ya kuombea kwa kusihi
    a. Akiomba kwa ajili ya Wayahudi
        1) Warumi 9:1ff
        2) Warumi 10:1
    b. Akiliombea kanisa
        1) Warumi 1:9
        2) Waefeso 1:16
        3) Wafilipi 1:3-4,9
        4) Wakolosai 1:3,9
        5) 1 Wathesolanike 1:2-3
        6) 2 Wathesolanike 1:11
        7) 2 Timotheo 1:3
        8) Filemon, uk. 4
    c. Paulo analiomba kanisa limwombee
        1) Warumi 15:30
        2) 2 Wakorinthp 1:11
        3) Waefeso 6:19
        4) Wakolosai 4:3
        5) 1 Wathesolanike 5:25
        6) 2 Wathesolanike 3:1
3. Huduma ya kanisa ya maombi ya kusihi
    a. Kuombeana wao kwa wao
        1) Waefeso 6:18
        2) 1 Timotheo 2:1
        3) Yakobo 5:16
    b. Maombi yaliyohitajiwa na makundi maalumu
        1) Adui zetu, Mat. 5:44
        2) Wakristo watembeaji, Waebrania 13:18
        3) Watawala, 1 Timotheo 2:2
        4) wagonjwa, Yakobo 5:13-16
        5) waliorudi nyuma, 1 Yohana 5:16

III. masharti kwa ajili ya maombi yaliyotakiwa kujibiwa

A. Mahusiano yetu kwa Yesu na Roho
1. Kutii ndani yake, Yohana 15:7
2. Katika jina lake , Yohana 14:13,14; 15:16; 16:23-24
3. Katika Roho, Waefeso 6:18; Jude 20

4. Kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, Mathayo 6:10; 1 Yohana 3:22; 5:14-15

B. Visababishi
   1. Kutotetereka, Mathayo 21:22; Yakobo 1:6-7
   2. Unyenyekevu na toba, Luka 18:9-14
   3. Kuomba vibaya, Yakobo 4:3
   4. Ubinafsi , Yakobo 4:2-3

C. Mitazamo mingine
   a. Usitahimilivu
   b. Luka 18:1-8
   c. Wakolosai 4:2
   1. Endelea kuomba
      a. Mathayo 7:7-8
      b. Luka 11:5-13
      c. Yakobo 1:5
   2. Kutoelewana nyumbani, 1 Petro 3:7
   3. Kuwa huru kutoka katika dhambi zijulikanazo
      a. Zaburi 66:18
      b. Mithali 28:9
      c. Isaya 59:1-2
      d. Isaya 64:7

IV. Hitimisho la kithiolojia
   A. Ni faida ipi, fursa ipi, shughuli na uwajibikaji upi
   B. Yesu ni mfano wetu. Roho ni mwongozo wetu. Baba anasubiri kwa hamu.
   C. Inaweza kukubadilisha wewe, familia yako, rafiki zako na hata dunia

▣**”**kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake” Angalia mada maalum inayofuata

**MADA MAALUM: MATUMIZI YA NENO “MLANGO” KATIKA AGANO JIPYA**

Agano Jipya linatumia neno “mlango” katika maana mbali mbali.

1. Maana iliyo wazi
   a. Ya nyumbani, Mt. 6:6; Mk 1:33; 2:2; 11:7, chumba cha juu, Yn 20:19,26
   b. Ya Hekalu, Mdo 3:2; 21:30
   c. Ya gereza, Mdo 5:19,23; 12:6; 16:26-27
   d. Ya kaburi, Mt. 27:60; 28:2; Mk 15:46; 16:3
   e. Ya zizi la kondoo, Yn 10:1,2
   f. Ya ua wa nje, Yn 18:16; Mdo 12:13
2. Ki-sitiari
   a. Ukaribu wa muda, Mt. 24:33; Mk 13:29; Mdo 5:9; Yak. 5:9
   b. Uzuiliwaji wa kuingia kwenye imani thabiti, Mt. 7:13-14; Lk 13:24; Uf. 3:20
   c. Fursa ya kuokoa roho zilizopotea, Mt. 25:10; Lk 13:25; Uf. 3:7
   d. Fursa ya kuiokoa imani, Mdo 14:27; Mdo. 3:7
   e. Fursa kwa ajili ya huduma, 1 Kor. 16:9; 2 Kor.2:12; Kol. 4:3; Uf. 3:8
   f. Ufunuo, Uf. 4:1; 19:11
   g. Wadhifa kwa ajili ya Yesu, Yn 10:7,9

▣**”siri ya Kristo”** Angalia kidokezo katika Kol 2:2 na Mada Maalum katika Efe 3:3.

▣”**ambayo kwa ajili yake nimefungwa”** Ikiwa taaluma ya sasa ni sahihi Paulo alifungwa Rumi katika mwanzo wa miaka ya 60 B.K. (kama vile Kol 4:18). Paulo hakuwa katika Rumi wala mbele ya Kaisari kwa bahati mbaya! Hii ilitabiriwa katika kuongoka kwake (kama vile Mdo 9:15-16; Fil. 1:13)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA); WAKOLOSAI 4: 5-6**
**[5] Enendeni kwa hekima mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati. [6] Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu.**

**4:5-6** Mistari hii miwili inahusiana na uinjilisti. Waaminio wanatakiwa kuishi kwa namna ambayo wasioamini (1) hatakwazwa, lakini (2) watavutwa. Kila mwamini lazima awe shahidi wa ulimi na shahidi wa mtindo wa maisha (kama vile 1 Petro 3:15)!

**4:5**
**NASB "Mwenende wenyewe kwa hekima"**
**NKJV "tembea katika hekima"**
**NRSV "Mwenendo wenu wenyewe uwe wa hekima"**
**TEV "muwe na hekima katika namna mnavyotenda"**
**NJB "Tendeni kwa hekima"**

Hii ni kauli shurutishi tendaji ya wakati uliopo, "siku zote mkienenda wenyewe kwa hekima." Waamini lazima wawe wainjilisti wa kukusudia. Uinjilisti ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kanisa (kama vile Mathayo 28:19-20) kila mwamini ni mhudumu wa kudumu wa muda wote wa injili (kama vile Efe. 4:11-12).

**NASB "mkiitumia fursa"**
**NKJV "mkiukomboa wakati"**
**NRSV "mkiufanya muda wenu wenye manufaa"**
**TEV "mkifanya matumizi mazuri ya kila fursa mliyonayo"**
**NJB "mkitumia vyema muda wenu wa sasa"**

Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo. Hili lilikuwa neno (*exagorazō)* lililotumika kufunua ukombozi (kama vile Wagalatia 3:13; 4:5) lilikuwa na kidokezo cha Agano la Kale cha kununua mtu kutoka utumwani, hata wakati mwingine wakala binafsi wa ndugu wa karibu (*go'el*). Ilitumika kisitiari kwa kutengeneza fursa nzuri ya kununua kitu kwa bei nzuri au katika muda mzuri (kama vile Efe 5:16).
Waamini lazima waishi kwa utauwa na watumie hekima ya ki-Mungu ili kwamba wakati fursa za kiroho na kiinjilisti zinapokuja waweze kupata faida ya kutosha ya fursa hizo.

**4:6 "Maneno yenu ………siku zote, yakikolea munyu"** Waaminio lazima waangalie maneno yao (kama vile Waefeso 4:29). Wanajulikana kwa kinywa chao (kama vile Mathayo 15:1-20; Marko 7:2-23) wanahukumiwa kwa maneno yao (kama vile Mathayo 12:33-37; Luka 6:39-45). Kauli zetu na maisha yetu yatatufungulia fursa kwa ajili ya kushuhudia! Kwa kukusudia si mbinu zinazotumika kufanya uinjilisti ambazo mtu atachagua kutumia zilizo za msingi hapa. Maombi na sio uwasilishaji uliokamilika ndiyo muhimu. Hekima ni msaada lakini Roho ndiye anayeamua na kuashiria! Angalia Mada Maalumu: Kauli za mwanadamu katika Kol. 3:10

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 4:7-9**
**[7] Tikiko, ndugu mpendwa, mtumishi mwaminifu, mjoli wangu katika Bwana, atawaarifu mambo yangu yote; [8]ambaye nimemtuma kwenu kwa sababu iyo hiyo, ili mjue mambo yetu, naye akawafariji mioyo yenu; [9] pamoja na Onesimo, ndugu mwaminifu, mpendwa, aliye mtu wa kwenu. Hao watawaarifu mambo yote ya hapa petu.**

**4:7-8 "Tikiko"** Paulo anamtaja Tikiko mara kadhaa (kama vile Mdo 20:4; Efe. 6:21; 2 Tim. 4:12 and Tito 3:12). Alikuwa muwasilishaji wa barua hii, na pia Waefeso na Filemoni. Paulo alimtuma aelezee hali yake kwa makanisa

ya Asia ndogo ili kwamba waweze kujua namna nzuri ya kumuombea na kufurahi pamoja naye (kama vile Kol 4:8 na utangulizi).

**4:8 “mioyo”** Angalia Mada Maalum katika Wakolosai 2:2.

**4:9 “Onesmo”** Onesmo alikuwa mtumwa aliyekimbia aliyegeuzwa kumjua Mungu akiwa gerezani. Paulo alimtuma yeye aende tena kwa wakubwa zake wa Wakristo, Filemoni, aliyeishi Kolosai na alijulikana kwa Paulo (kama vile Filemoni). Katika njia nyingi mvutano huu kati ya mtumwa na aliye huru ulikuwa ni jaribio/mtihani wa ufanisi kwa upendo wa dhati wa Mkristo wa Kweli.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 4:10-17**
**10 Aristarko, aliyefungwa pamoja nami, awasalimu; na Marko, mjomba wake Barnaba, ambaye mmepokea
maagizo kwa habari yake; akifika kwenu mkaribisheni. 11 Na Yesu aitwaye Yusto; hao ni watu wa tohara. Tena
hao peke yao ni watendaji wa kazi pamoja nami kwa ajili ya ufalme wa Mungu; nao walikuwa faraja kwangu.
12 Epafra, aliye mtu wa kwenu, mtumwa wa Yesu Kristo, awasalimu, akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu
katika maombi yake, ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu. 13
Maana namshuhudia kwamba ana juhudi nyingi kwa ajili yenu, na kwa ajili ya hao walioko Laodikia, na kwa
ajili ya hao walioko Hierapoli. 14 Luka, yule tabibu mpendwa, na Dema, wanawasalimu. 15 Wasalimuni ndugu
walioko Laodikia, na Nimfa, na kanisa lililo katika nyumba yake. 16 Waraka huu ukiisha kusomwa kwenu
fanyeni kwamba usomwe katika kanisa la Walaodikia pia; na ule wa Laodikia usomwe na ninyi. 17 Mwambieni
Arkipo, Iangalie sana huduma ile uliyopewa katika Bwana, ili uitimize.**

**4:10-14** Timotheo na watenda kazi wenzake sita walituma salamu zao binafsi kwa kanisa. Sita wa watenda kazi saba wanatajwa pia katika Filemoni. Tikiko yawezekana alikuwa muwasilishaji wa barua za Kolosai, Efeso na katika Filemoni. Kwenda Asia ndogo.

**4:10”Aristarko”** Mkristo wa Kiyahudi ambaye tunajua kidogo kuhusu yeye (kama vile Mdo 19:29; 20:4; 27:2).

▣**”mfungwa pamoja nami”** Hii kisitiari inamaanisha aidha huduma ya Mkristo au kiuhalisia kufungwa kwa ukweli ukweli (kama vile Warumi 16:7; Filemoni 23).

▣**”Marko, mjomba wake Barnaba”** katika nyumba ya Yohana Marko palikuwa sehemu ya Meza ya Bwana na Chumba cha juu wakati Yesu alipokuwa akiwatokea wanafunzi baada ya Ufufuo (Mdo 12:12). Alikuwa mwandishi wa injili ya Marko na rafiki na mwandishi wa Petro (kama vile 1 Petro 5:13). Alikuwa ni chanzo cha kutoelewana kukubwa kati ya Barnaba na Paulo baada ya safari yao ya kwanza ya kimishionari (Mdo 12:25; 13:5; 15:36-39).

▣**”akifika kwenu mkaribisheni”** Hii ni sentensi ya daraja la tatu lenye masharti. Paulo alikuwa amemkasirikia sana Yohana Marko kwa kumuacha katika timu ya safari yao ya kimishionari. Hata hivyo hatimaye walipatanishwa (kama vile 2 Timotheo 4:11)

**4:11” Na Yesu aitwaye Yusto”** Toleo la TEV lina “Yoshua.” “Yesu” na “Joshua” yanatokana yote kutoka katika maneno ya Kiebrania “YHWH” na “wokovu” na yana maana sawa katika Waebrania (kama vile Mathayo 1:21). Huyu Yusto anajulikana na Mungu, lakini sisi hatumfahamu.

▣**”ufalme wa Mungu”** Hii ni tungo muhimu katika vitabu vya injili (angalia Mada Maalumu katika Waefeso 5:5). Mahubiri ya kwanza na ya mwisho ya Yesu na mafumbo yake mengi yalihusu mada hii. Inamaanisha utawala wa Mungu katika mioyo ya watu sasa. Inashangaza kwamba Yohana anatumia tungo hii mara mbili tu (na haijawahi kutokea katika mafumbo ya Yesu). Katika Injili ya Yohana “uzima wa milele” ni neno na sitiari muhimu.
Tungo inahusiana na siku za mwisho wa nchi (zama za mwisho) msukumo wa mafundisho ya Yesu. Hii “tayari”, lakini bado haijawa ukinzani wa kithiolojia inayohusiana na dhana ya kiyahudi ya nyakati mbili, wakati wa sasa wa

kizazi cha uovu na nyakati ya kizazi cha haki kijacho ambacho kitawekwa wakfu na Masihi. Wayahudi walitegemea kuja kwa mara moja tu kwa kiongozi aliyepewa uweza wa kijeshi (kama Waamuzi katika Agano la Kale). Kuja kwa mara mbili kwa Yesu kunasababisha mpishano wa nyakati mbili. Ufalme wa Mungu umevunja katika historia ya mwanadamu kwa Bethlehemu. Hata hivyo, Yesu alikuja si kama mtawala wa kijeshi wa Ufunuo 19, lakini kama mtumwa mwenye mateso (kama vile Isaya 53) na kiongozi mnyenyekevu (kama vile Zakaria 9:9). Ufalme, hivyo unawekwa rasmi (kama vile Mt. 3:2; 4:17; 10:7; 11:12; 12:28; Mk 1:15; Lk 9:9,11; 11:20; 21:31-32), lakini sio kutimilizwa (kama vile Mt. 6:10; 16:28;26:64).
Waamini wanaishi katika uvutano kati ya nyakati mbili. Wana maisha ya ufufuo lakini bado wanakufa kimwili. Wanawekwa huru kutoka katika nguvu ya dhambi, na bado wanatenda dhambi. Wanaishi katika mvutano wa siku za mwisho ulio tayari na ule ambao haujakuwako bado!

▣**"kutoka katika tohara"** watu waliorodheshwa katika Kol 1:7 na utangulizi wote walikuwa waamini wa Kiyahudi (sawasawa na majina yao).

▣**"nao walidhibitisha kuwa na faraja kwangu"** Neno kiuhalisia linamaanisha "unafuu wa maumivu." Hili neno na Kiyunani ni chanzo cha dawa ya Kiingereza iitwayo "dawa ya kutuliza neva."

**4:12 "Epafra"** alikuwa mwanzilishi wa kanisa la Kolosai (kama vile Kol 1:7 na utangulizi).

▣**"akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu"** Hili ni neno lenye nguvu la kimichezo ambalo linakuja katika kingereza kama "kuugulia kwa maumivu makali." Epafra alikuwa mpambanaji wa maombi (kama vile Kol 4:13). Maombi yake kwa waamini ilikuwa kwamba (1) wasimame, (2) wakue, na (3) wawe na uhakika katika mapenzi ya Mungu.

**4:13"Laodikia na Hierapoli"** Hii ilikuwa miji mingine miwili (sambamba na Kolosai) ya bonde la Lycus ambayo Epafra alianzisha makanisa haya matatu.

**4:14"Luka"**Alikuwa Mtenda kazi wa karibu sana wa kimishionari wa Paulo na daktari. Alikuwa ni mtu wa Mataifa na mwandishi wa Injili ya Luka na Matendo ya Mitume.
▣**"Dema"** Baadaye alimuacha Paulo (kama vile 2 Timotheo 4:10)

**4:15"Nimfa"**Hili linawezekana likawa la kike ama la kiume. Chunguza kanisa la kwanza lilikuwa linakutana katika nyumba za watu binafsi (kama vile Warumi 16:5; 1 Kor. 16:19; Filemon 2).

**4:16"Waraka huu ukiisha kusomwa kwenu"** Barua zote za Paulo, sio tu Waefeso (barua ya wengi), ilikuwa ikipitishwa pitishwa kutoka kanisa mapaka kanisa na kusomwa sauti kwa kusanyiko lote. Kanisa liliamini kwamba Mitume walikuwa na neno lililovuviwa na la upekee wa aina yake kutoka kwa Mungu. Shauku yao ni kusikia barua zote za Paulo zikiandikwa na kwa makanisa mengine, na mazingira mengine, kuonesha namna Biblia inavyohusiana na kila mtu na kila kizazi.

▣**"fanyeni kwamba usomwe katika kanisa la Walaodikia"** barua hii yawezekana ilikuwa na "waefeso" ambayo ilikuwa ni barua ya wengi. Katika Kanoni ya Marcion, Waefeso iliitwa "barua kwa Walaodekia." Hakuna baba wa kanisa la kwanza anayenukuu kutoka katika barua ile inayojulikana kama barua kwa Walaodekia.

**4:17"Arkipo"** Akipo alikuwa mchungaji wa kanisa la nyumbani (Filemoni 2). Nafasi za uongozi wa kwanza zilikuwa ni kazi zinazofanywa na waamini wa nyumbani wenye karama na sio ajira/kazi ama ofisi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAKOLOSAI 4:18**
**18 Salamu yangu mimi Paulo, kwa mkono wangu mwenyewe. Kumbukeni kufungwa kwangu. Neema na iwe pamoja nanyi.**

**4:18"katika mkono wangu"** Hii ilikuwa ni njia ya Paulo ya kuwahakikishia udhati wa maandiko yake (kama vile 2 The. 2:2; 3:17). Hii pia inamaanisha kwamba mwandishi wa mara kwa mara aliye ajiriwa (Rum. 16:22), yawezekana kwasababu ya matatizo ya macho yake (kama vile Mdo 9:8-9,12,18; Gal. 4:15; 6:11), ambayo naamini lilikuwa ni "mwiba katika mwili" wake.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri.

Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.
Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha vipengele vitatu vya maombi Katika Wakolosai 4:2-3
2. Orodhesha vipengele vine vya maisha ya Mkristo katika Wakolosai 4:5-6
3. Jadili watu mmoja mmoja waliotajwa katika Wakolosai 4:7-14

# UTANGULIZI KWA WAEFESO

## MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Ukweli wa kitabu hiki umeleta mchango mkubwa katika maisha ya watakatifu

   1. Samuel Coliridge alikiita "tungo ya kiungu zaidi ya mwanadamu"
   2. John Calvin alikiita kitabu cha Biblia akipendacho zaidi
   3. John Knox aliomba kwamba asomewe mahubiri ya Calvin kutoka Waefeso wakati alipokuwa katika hali ya kufa kitandani pake.

B. Kitabu hiki kimekuwa kikiitwa "kito cha taji ya kifalme," au jiwe la chepeo, ya thiolojia ya Paulo. Maudhui makubwa yote aliyotaja Paulo katika Wagalatia, kukuzwa katika Warumi, na sasa zinaelezwa katika Waefeso katika namna nzuri ya ajabu ya aina ya muhtasari.

C. Kama Mungu alivyotumia Warumi kuchochea Mageuzi, atatumia Waefeso ili kuunganisha makanisa yaliyogawanyika na mataifa ya Kikristo. Umoja wa Waaminio na hali yao ya kawaida katika Kristo zaidi inatia kivuli tofauti zao.

## MWANDISHI

A. Paulo
   1. Kwa maelezo ikitajwa katika Waefeso 1:1, 3:1
   2. Urejereo wa kufungwa (yawezekana katika Rumi) katika Waefeso 3:1; 4:1; 6:20
   3. Ukaribiano wa desturi za kanisa lisilojulikana kwa hakika
      a. Clement wa Rumi, katika 95 B.K, aliandika barua kwa Wakorintho inayonukuu Waefeso 4:4-6
      b. Ignatius (30-107 B.K) ananukuu kutoka Waefeso 1:9; 2:19; 3:4-9
      c. Polycarp (65-155 B.K), Mwanafunzi wa Mtume Yohana, na Askofu wa Smirna anaelezea uandishi wa Paulo.
      d. Irenaeus (130-200 B.K) anaelezea uandishi wa Paulo
      e. Clement wa Alexandria (150-210 B.K) anaelezea uandishi wa Paulo
   4. Imeorodheshwa katika
      a. Orodha ya vitabu vilivyokubalika vya Marcion (aliyekuja Rumi katika miaka ya 140 B.K)
      b. Mgawanyiko wa Kimurato (180-200 B.K), orodha ya vitabu vya kikanoni kutoka Rumi na kukiweka katika maandiko ya Paulo.
   5. Kuhitimishwa kwa vitabu vyote Wakolosai na Waefeso kunakuwa na maneno 29 ambayo yanakaribiana sana kimfanano katika Kiyunani (kuna maneno ya ziada mawili katika Wakolosai.)

B. Mwandishi mwingine
   1. Erasmus alikuwa wa kwanza kutia wasiwasi uandishi wa Paulo akijikita katika
      a. Namna yake ya uandishi – sentensi ndefu ambazo hazina mfanano kabisa ya nyaraka zingine za Paulo
      b. Hakuna salamu binafsi
      c. Misamiati ya kipekee
   2. Uhakiki wa kitaaluma wa karne ya 18 walianza kukataa uandishi wa Paulo
      a. Mistari kadhaa inaonekana kutoka katika mwamini wa kizazi cha pili, Waefeso 2:20: 3:5
      b. Maneno ya kithiolojia yalitumika yakiwa na maana zinazotofautiana (mfano: "mystery" (maajabu/siri))
      c. Upekee wa aina ya uandishi ya mzunguko au barua za kawaida.

C. Majibu ya hoja za Erasmus
   1. Staili hii ni tofauti kwa sababu Paulo alikuwa na muda wa kufikiri alipokuwa akiandika Waefeso wakati akiwa gerezani.

2. Kukosekana kwa salamu binafsi inaelezwa kwa ukweli kwamba Waefeso ilikuwa barua ya wengi iliyotakiwa kutumwa katika eneo lenye makanisa mengi. Njia mbadala ya Warumi ilijumuisha Efeso na bonde la mto Lycus inaweza kuonekana katika Ufunuo 2-3. Paulo aliandika barua pacha, Wakolosai, kwa kikundi maalumu kilichojumuisha salamu binafsi kadhaa.
3. Hesabu ya maneno ya kipekee katika kitabu cha Waefeso ni sawasawa na hesabu ya maneno ya upekee (*hapax legomena*) katika kitabu cha Warumi. Kusudi, dhima, wapokeaji na eneo la tukio vinaeleza matumizi ya maneno mapya.
4. Paulo anazungumza juu ya "mitume na manabii" katika 1 Wakorintho 12:28, ambayo inafanana na Waefeso 2:20 na 3:5. Hakuna anayekana uandishi wa Paulo wa 1 Wakorintho.

## UHUSIANO WA KIFASIHI KATI YA WAKOLOSAI NA WAEFESO

A. Uhusiano wa kihistoria kati ya Wakolosai na Waefeso
   1. Epaphra (Wakolosai 1:7; 4:12; Filemoni 23) aligeuzwa wakati wa Kampeni ya Paulo kwa Waefeso (Mdo 19)
      a. Alichukua imani yake mpya aliyoipata kwenda nyumbani kwake, bonde la Mto Lycus
      b. Alianzisha makanisa matatu katika Hiarapolis, Laodikia na Kolosai.
      c. Epafra alimtafta Paulo kwa ajili ya ushauri juu ya namna gani ya kukabiliana na muunganiko maoni ya ulimwengu kwa wasomi. Paulo alikuwa gerezani katika Rumi ( mwanzoni mwa miaka ya 60)
   2. Walimu wa uongo walikuja na kuanza kuunganisha Injili kwa mafundisho ya Kiyunani inayohusu elimu ya viumbe
      a. Roho na maada yalikuwa yakiwa milele ya pamoja
      b. Roho (Mungu) alikuwa mzuri
      c. Maada (uumbaji) ulikuwa ni uovu
      d. Mfululizo wa *aeons* (viwango vya kimalaika) vilitokea kati ya Mungu mwema mkuu na mungu mdogo aliyetengeneza maada.
      e. Wokovu ulikuwa umejikita katika maarifa ya neno za siri yaliyosaidia watu kuendelea kupitia *aeons* (viwango vya malaika)

B. Uhusiano wa kifasihi kati ya nyaraka za Paulo
   1. Paulo alisikia juu ya majungu katika makanisa haya ambayo hakuwahi kuyatembelea binafsi kutoka kwa Epafra.
   2. Paulo aliandika barua kali kwa ufupi, zenye sentensi za kihisia, zikiwa zimelengwa kwa walimu wa uongo. Mada kuu ilikuwa u-Bwana wa Yesu juu ya ulimwengu mzima. Hii inajulikana kama barua ya Paulo kwa Wakolosai.
   3. Kwa uwazi, mara baada ya kuandika Wakolosai, na kwa muda katika mikono katika gereza,alikuza mada hizi hizi. Waefeso imejawa na tabia za kuwa na sentensi ndefu na kukuza dahna za kithiolojia (Waefeso 1:3-14, 15-23; 2:1-10, 14-18, 19-22; 3:1-12, 14-19; 4:11-16; 6:13-20). Inachukua Wakolosai kama mwanzo na kutoa kuhusika kithiolojia. Mada kuu ya Waefeso ni umoja katika Kristo ambacho ni ulinganifu wa dhana inayoanza ya ujuzi wa kipekee

C. Fasihi inayofanana na muundo wa kithiolojia
   1. Ufanano wa muundo wa msingi
      a. Vina ufunguzi unaofanana
      b. Vina vipengele vya kimafundisho vinavyojishughulisha kimsingi na Kristo
      c. Vina vipengele dhahiri vinavyotoa maonyo juu ya maisha ya Mkristo vikitumia aina, misamiati na tungo
      d. Vina mistari inayofunga sawasawa kwa mfanano uleule katika maneno 29 katika Kiyunani, yakiwa na maneno mawili to tofauti yaliyoongezeka katika Wakolosai.
   2. Ufanano wa maneno na tungo fupifupi

| | |
|---|---|
| Waefeso. 1:1c na Kol. 1:2a | "mwaminifu" |
| Waefeso1:4 na Kol. 1:22 | "mtakatifu na asiye na lawama" |
| Waefeso 1:7 and Kol. 1:14 | "wokovu….msamaha" |

| | |
|---|---|
| Waefeso 1:10 na Kol. 1:20 | “vitu vyote….mbingu….dunia” |
| Waefeso 1:15 na Kol. 1:3-4 | “kusikia…upendo kwa watakatifu wote” |
| Waefeso. 1:18 na Kol. 1:27 | “utajiri wa utukufu” |
| Waefeso 1:27 na Kol. 1:18 | “kichwa….kanisa” |
| Waefeso 2:1 na Kol. 1:13 | “mlikuwa mmekufa” |
| Waefeso 2:16 na Kol. 1:20 | “kupatanisha…msalaba” |
| Waefeso 3:2 na Kol. 1:25 | “uwakili” |
| Waefeso 3:3 na Kol. 1:26,27 | “siri/maajabu” |
| Waefeso 4:3 na Kol. 3:14 | “umoja” |
| Waefeso 4:15 na Kol. 2:19 | “kichwa” na “kukua” |
| Waefeso 4:24 na Kol. 3:10, 12,14 | “kuweka….” Hasira” “ghadhabu” “uongo” |
| Waefeso 4:31 na Kol. 3:8 | “uzushi” |
| Waefeso 5:3 na Kol. 3:5 | “uchafu” “tamaa” |
| Waefeso 5:5 na Kol.3:5 | “kuabudu sanamu” (tama) |
| Waefeso 5:6 na Kol. 3:6 | “ghadhabu ya Mungu” |
| Waefeso 5:16 na Kol. 4:5 | “kuutumia vizuri wakati” |

3. Tungo na sentensi zilezile
   Waefeso 1:1a na Kol 1:1a
   Waefeso 1:1b na Kol. 1:2a
   Waefeso 1:2a na Kol. 1:2b
   Waefeso 1:13 na Kol. 1:5
   Waefeso 2:1 na Kol. 2:13
   Waefeso. 2:5b na Kol. 2:13c
   Waefeso. 4:1b na Kol. 1:10a
   Waefeso 6:21, 22 na Kol. 4:7-9 (maneno yanayofuatana 29 kwa "kai syndoulos" katika Wakolosai)

4. Tungo na sentensi zinazofanana
   Waefeso 1:21 na Kol. 1:16
   Waefeso 2:1 na Kol. 1:13
   Waefeso 2:16 na Kol. 1:20
   Waefeso 3:7a na Kol. 1:23d, 25a
   Waefeso 3:8 na Kol. 1:27
   Waefeso 4:2 na Kol. 3:12
   Waefeso 4:29 na Kol. 3:8; 4:6
   Waefeso 5:15 na Kol. 4:5
   Waefeso 5:19,20 na Kol. 3:16

5. Mfanano unaokaribiana wa dhana za kithiolojia
   Waefeso 2:1,12 na Kol.1:21
   Waefeso 2:15 na Kol. 2:14

| | |
|---|---|
| Waefeso 4:1 na Kol 1:10 | sala ya shukurani |
| Waefeso 4:15 na Kol. | kujitenga na Mungu |
| 2:19 | uadui wa sheria |
| Waefeso 4:19 na Kol. 3:5 | kutembea kunakostahili |
| Waefeso 4:22,31 na Kol. | Mwili wa Kristo unaokua kuelekea makuzi kutoka |
| 3:8 | katika kichwa chake |
| Waefeso 4:32 na Kol. | Uchafu wa kujamiiana |
| 3:12-13 | “kuweka kando” dhambi |
| Waefeso 5:4 na Kol. 3:8 | Wakristo wakiwa wakitendeana wema |
| Waefeso 5:18 na Kol. | Kauli za Mkristo |

| | |
|---|---|
| 3:16 | kujazwa na Roho=neno la Kristo |
| Waefeso 5:20 na Kol. | shukrani kwa Mungu kwa mambo yote |
| 3:17 | wake wawatii waume zao |
| Waefeso 5:22 na Kol. | waume wapendeni wake zenu |
| 3:18 | watoto watiini wazazi wenu |
| Waefeso 5:25 na Kol. | wababa msiwachokoze watoto |
| 3:19 | watumwa watiini mabwana wenu |
| Waefeso 6:1 na Kol. 3:20 | mabwana na watumwa |
| Waefeso 6:4 na Kol. | Ombi la Paulo la Maombi |
| 3:21 | |
| Waefeso 6:5 na Kol. 3:22 | |
| Waefeso 6:9 na Kol. 4:1 | |
| Waefeso 6:18 na Kol. | |
| 4:2-4 | |

6. Maneno na tungo zilizotumika kote katika Wakolosai na Waefeso ambazo zote zinapatikana katika fasihi zingine za Paulo
    a. “ukamilifu” (ambalo lilikuwa neno la kiujuzi wa pekee kwa viwango vya kimalaika

    | | |
    |---|---|
    | | “Ukamilifu katika Yeye ajazaye yote katika yote” |
    | Waefeso 1:23 | “mkajazwe kwa ukamilifu wote wa Mungu” |
    | Waefeso 3:19 | |
    | Waefeso 4:13 | “mpaka ukamilifu wa Kristo” |
    | Wkolosai 1:19 | “kwa ukamilifu wote ukaao ndani Yake” |
    | Wakolosai 2:9 | “kwakuwa ndani yake ukamilifu wote wa uungu unakaa” |

    b. Kristo kama “Kichwa” cha kanisa
    Waefeso 4:15; 5:23 na Kol 1:18; 2:19
    c. “kutengwa”
    Waefeso 2:12; 4:18 na Kol 1:21
    d. “kuukomboa wakati”
    Waefeso 5:16 na Kol 4:5
    e. “Kuwekewa mizizi”
    Waefeso 3:17 na Kol 1:5
    f. “neno la kweli, injili”
    Waefeso 1:13 na Kol 1:5
    g. “Kuzaa”
    Waefeso 4:2 na Kol 3:13
    h. Tungo na maneno yasiyo ya kawaida (“yakiwekwa pamoja,” “kusambaziwa”)
    Waefeso 4:16 na Kol 2:19

D. Muhtasari
1. Zaidi ya robo ya maneno katika Wakolosai yapo katika Waefeso. Inakadiriwa kuwa asiimia 75 ya mistari 155 katika Waefeso inarandana katika Wakolosai. Zote zinadaiwa kuandikwa na Paulo wakati alipokuwa gerezani.
2. Vyote viliwasilishwa na rafiki wa Paulo aliyeitwa Tikiko
3. Vyote vilitumwa katika eneo moja (Asia ndogo)
4. Vyote vinashughulikia mada zimuhusuzo Kristo
5. Vyote vinasisitiza Kristo kama kichwa cha kanisa
6. Vyote vinahamasisha maisha mema ya Mkristo

E. Mambo makubwa yanayoweka kutofautiana
1. Kanisa lilikuwa la eneo dogo katika Wakolosai lakini la kiulimwengu kwa Waefeso. Hii inawezekana kutokana na asili ya mznguko wa barua ya Waefeso.

2. Porojo lilikuwa jambo kuwa na tabia kwa Wakolosai, halitajwi moja kwa moja katika Waefeso. Hata hivyo, barua zote zinatumia tabia za maneno ya kiujuzi ("hekima," "maarifa," "ukamilifu," "siri," "mamlaka na nguvu," na "uwakili."
3. Kuja Kwa Mara ya Pili kunakuja mara katika Wakolosai lakini kunachelewa katika Waefeso. Kanisa lilikuwa, na lipo, limeitwa kutumikia katika ulimwengu ulioanguka. (Waefeso 2:7; 3:21; 4:13).
4. Baadhi ya tabia za maneno ya Paulo yanatumika kiutofauti. Mfano mmojawapo ni neno "siri"(siri/ajabu). Katika Wakolosai siri ni Kristo (Kol 1:26-27; 2:2; 4:3), lakini katika Waefeso (Waefeso 1:9; 5:32) ni mpango wa Mungu uliokuwa umefichwa kabla lakini sasa mpango wa umoja wa Mataifa na Wayahudi.
5. Waefeso ina maelezo kadhaa ya Agano la kale (Waefeso 1:22 -- Ps. 8; Waefeso 2:17—Isaya 57:19) (Waefeso 2:20 -- Zaburi 118:22) (Waefeso 4:8 -- Zaburi 68:18) (Waefeso 4:26 -- Zaburi 4:4) Waefeso 5:15 -- Isaya 26:19, 51:17, 52:1, 60:1) (Waefeso 5:31 -- Mwanzo 2:24) (Waefeso 6:2-3 -- Kutoka 20:12) (Waefeso 6:14 -- Isaya 11:5, 59:17) (Waefeso 6:15 – Isaya 52:7) lakini liko moja au mawili katika Wakolosai, Kol. 2:3 -- Isaya 11:2, na yawezekana Kol. 2:22 -- Isaya 29:13.

F. Japo kuna mfanano mkubwa katika maneno, tungo na mara nyingi muhtasari, barua zinajumuisha ukweli wa pekee.
1. Baraka za utatu wa neema – Waefeso 1:3-14
2. Kupita kwa neema – Waefeso 2:1-10
3. Kupatanishwa kwa Wayahudi na Mataifa katika mwili mmoja mpya – Waefeso 2:11-3:13
4. Umoja na karama ya mwili wa Kristo – Waefeso 4:1-16
5. "Kristo na kanisa" ni utaratibu kwa "mume na mke" Waefeso 5:22-33
6. Kupita kwa vita vya kiroho – Waefeso 6:10-18
7. Kupita katika elimu ya Kristo – Wakolosai 1:13-18
8. Sheria, kanuni za kidini za binadamu – Wakolosai 2:16-23
9. Mada ya umuhimu Kristo kwa ulimwengu katika Wakolosai dhidi ya dhima ya umoja wa vitu vyote katika Kristo katika Waefeso

G. Kwa kuhitimisha inaonekana vyema zaidi kumfuata A. T. Robertson na F.F. Bruce katika kuelezea kwamba Paulo aliandika barua zote katika ukaribiano kwa kukuza mawazo ya Wakolosai kwenye jiwe la chapeo la uwasilishwaji wa kweli.

**TAREHE**

A. Tarehe za barua hii inaunganishwa kwa kifungo cha Paulo katika Efeso, Filipi, Kaisaria, au Rumi. Kifungo cha Kirumi kinalingana kabisa na kweli zilizo katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

B. Mara Rumi inadhaniwa kuwa ni sehemu ya vifungo, swali linaibuka, wakati gani? Paulo alikuwa jela katika mwanzo wa miaka ya 60, ambayo inatajwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume lakini aliachiliwa na akaandika barua za kichungaji (I & 2 Timotheo na Tito) na alikamatwa tena na kuuawa kabla ya June 9 B.K. ambayo ilikuwa ni tarehe ya kujiuwa ya Nero.

C. Makisio bora ya kisomi ya kuandikwa kwa Waefeso ni kufungwa kwa mara ya kwanza kwa Paulo katika Rumi katika miaka ya mwanzo ya 60.

D. Tikiko pamoja na Onesmo inawezekana alichukua barua za Wakolosai, Waefeso na Filemoni kuelekea Asia Ndogo.

E. Mtiririko unaowezekana wa maandishi ya Paulo kufuatia F. F. Bruce na Murry Harris ikiwa na marekebisho madogo

| | Kitabu | Tarehe | Mahali kilipoandikwa | Uhusiano na Matendo ya Mitume |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wagalatia | 48 | Antiokia | Mdo 14:28; 15:2 |
| 2 | 1 Wathesalonike | 50 | Korintho | Mdo 18:5 |
| 3 | 2 Wathesalonike | 50 | Korintho | |
| 4 | 1 Wakorintho | 55 | Efeso | Mdo 19:20 |
| 5 | 2 Wakorintho | 56 | Makedonia | Mdo 20:2 |
| 6 | Warumi | 57 | Korintho | Mdo 20:3 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7-10 Barua za gerezani | | | |
| Wakolosai | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Filemoni | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Waefeso | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Wafilipi | mwishoni mwa 62-63 | Rumi | Mdo 28:30-31 |
| 11-13 Safari ya Umishionari ya 4 | | Efeso(?) | |
| 1 Timotheo | 63(au baadaye, | Makedonia | |
| Tito | 63 lakini kabla | | |
| 2 Timotheo | 64 B.K 68) | Rumi | |

**WAPOKEAJI**

A. Maandiko mengi (Chester Beatty Papyri, $P^{46}$; Sinaiticus, א; Vaticanus, B; maandiko ya Kiyunani ya Origen, na maandiko ya Kiyunani ya Tertullain) yanaondoa "katika Efeso" katika Waefeso 1:1. Toleo la RSV na fasiri za Williams zinaondoa tungo.

B. Sarufi ya Kiyunani ya Waefeso 1:1 inaweza ikapokea jina la sehemu. Yawezekana barua ya wengi, jina la sehemu ya kanisa iliachwa wazi ili ijazwe wakati itakaposomwa kwa sauti kwa makanisa. Hii inaweza kuelezea tungo katika Wakolosai 4:15-16, “barua kutoka kwa walaodekia,” ambayo yawezekana ilikuwa katika kitabu cha Waefeso (Marcion aliita Waefeso kwa kichwa cha habari “barua kwa Walaodekia”).

C. Waefeso iliandikwa kimsingi kwa Mataifa, Waefeso 2:1; 4:17, ambao Paulo hakuwa amekutana nao kwa binafsi, Waefeso 1:15; 3:2. Kanisa katika bonde la mto Lycus (Laodikia, Hiapolis, na Kolosai) yalianzishwa, sio na Paulo lakini na Epafra (Wakolosai 1:7: 4:12: Filemoni 23).

**KUSUDI**

A. Maudhui ya kitabu hiki yanapatikana katika Waefeso 1:10 na 4:1-10, yanayosisitiza umoja wa vitu vyote katika Kristo. Kristo anarejesha taswira ya Mungu katika ubinadamu na katika ulimwengu (*kosmos*).

B. Sehemu ya mafundisho ya sura ya 1-3 inaweza ikawekwa kwa muhtasari kama:
Tabia ya Utatu wenye Neema na Utoaji kwa Mwanadamu mwenye Dhambi
   1. Asili ya Utatu ya Mungu (Waefeso 1:3-14)
   2. Tabia ya Mungu kuwa mwenye neema (Waefeso 2:1-10)
   3. Mpango wa milele wa mungu wa ukombozi (Waefeso 2:11-3:13)

C. Waefeso ni moja ya barua za Paulo za gerezani. Muhtasari wa Waefeso na Wakolosai unafanana. Wakolosai iliandikwa kukabiliana na porojo na uzushi wa Mwanzo wa wapotoshaji wenye ujuzi katika bonde la Mto Lycys katika Asia ndogo. Waefeso iliandikwa kama barua ya kawaida ya wengi kwenda katika eneo moja kuandaa makanisa mengine kwa ajili ya kuja kwa uzushi na porojo. Wakolosai ni barua inayotumia maneno machache, yenye ukali wa kuchoma wakati Waefeso ni upanuzi wa uwasilishaji wa kweli kwa kutumia sentensi ndefu sana;(Waefeso 1:3-14, 15-23; 2:9; 3:1-7, na kadhalika.

**MUHTASARI KWA KIFUPI**

A. Kitabu kwa asili kinagawa sehemu mbili (kama ilivyo katika maandiko mengi ya Paulo)
   1. Umoja katika Kristo, Sura 1-3 (Thiolojia)
   2. Umoja katika kanisa, sura 4-6 (kutendea kazi)

B. Muhtasari wa mada zinazopendekezwa
   1. Ufunguzi wa siku zote wa Paulo, Waefeso 1:1-2
   2. Mpango wa Baba kwa umoja wa vitu vyote katika Kristo, Waefeso 1:3-3:21
      a. Sifa za Paulo kwa baba, Waefeso 1:3-14
         (1) Kwa ajili ya upendo wa Baba kabla ya muda
         (2) Kwa ajili ya upendo wa Baba katika mwanawe kwa muda muafaka
         (3) Kwa upendo unaoendelea wa Baba kwa Roho kupitia muda
      b. Maombi ya Paulo kwa Baba kwa ajili ya kanisa,Waefeso 1:15-23
         (1) Kwa ajili ya kuuelewa  Ufunuo wa Baba katika Kristo

(2) Kwa ajili nguvu ya baba kufanya kazi kwa nguvu ndani ya Waamini
(3) Kwa ajili ya kuinuliwa kwa Baba wa Kristo juu ya vitu vyote

c. Uelewa wa Paulo wa mpango wa Baba kwa wanadamu wote, Waefeso 2:1-3:13
   (1) Hitaji la kibinadamu la kidhambi
   (2) Kukidhiwa kineema kwa Baba
   (3) Mwitikio wa kiagano unaohitajika kwa mwanadamu
   (4) Kudhihirishwa kamili kwa mpango wa Baba
d. Maombi ya Paulo kwa Baba kwa ajili ya Waaminio, Waefeso 3:14-21
   (1) Kupokea nguvu ya ndani (kwa Roho)
   (2) Kuelewa kwa ukamilifu Injili (sio katika kweli zinazopendekezwa tu) katika ujuzi na upendo
   (3) Kujazwa kwa ukamilifu wa Mungu (ambaye ni Kristo)
   (4) Vyote hivi kutoka kwa Mungu awezaye

3. Shauku ya Baba ya umoja wa watu Wake wapya, Waefeso 4:1-6:20
   a. Umoja wa Utatu wa Mungu unaakisiwa katika umoja wa watoto Wake, Waefeso 4:1-16
      (1) Umoja sio saresare, lakini mtindo wa maisha ya upendo
      (2) Uungu ni umoja wa utatu
      (3) Zawadi za kiroho ni njema kwa ajili ya mwili, sio heshima kwa ajili ya mtu mmoja mmoja binafsi
      (4) Umoja una hitaji huduma
      (5) Umoja upo chini ya mashambulizi ya kimalaika
      (6) Umoja upo katika Kristo
   b. Umoja wa Mkristo unatofautishwa na upagani ambao una ubinafsi, Waefeso 4:17-5:14
      (1) Weka kando matendo yote ya maisha ya kale
      (2) Tamanini kufanana na Kristo
   c. Namna za kutimiza na kuendeleza umoja, Waefeso 5:15-6:9
      (1) Kujazwa siku zote katika Roho
      (2) Kujazwa kwa Roho kunabainishwa
         (a) Njeo tano, Waefeso 5:19-21
         (b) Mifano mitatu ya nyumbani
            i. Waume – wake
            ii. Wazazi – watoto
            iii. Mabwana – watumwa
   d. Kuhangaikia umoja wa kufanana kama Kristo, Waefeso 6:10-20
      (1) Vita vya kiroho
      (2) Silaha za Mungu
      (3) Nguvu ya maombi
4. Maoni ya kufunga, Waefeso 6:21-24

## USULI WA KIFALSAFA NA KITHIOLOJIA WA WALIMU WA UONGO (GNOSTICISM)

A. Imani ya uongo ya kwanza na karne ya pili:
   1. Asili ya viumbe (milele) upili kati ya roho (Mungu) na maada (vitu vya mwilini).
   2. Roho alikuwa mwema, wakati maada ilikuwa ovu
   3. Mfululizo wa viwango vya malaika (*aeons*) kati ya Mungu mkuu mtakatifu na mungu mdogo aliyeumba maada ovu.
   4. Njia ya wokovu
      a. Maarifa ya neno la siri yanayoruhusu mtembeo kupitia tufe la kimalaika kutoka duniani kuelekea mbinguni.
      b. Cheche za ki-Ungu kwa wanadamu wote ingawa wote wasingeelewa au kupokea maarifa yaokoayo
      c. Maarifa yalikuja kwa ajili ya wana kikundi waliona elimu kwa ufunuo maalumu
   5. Maadili (aina mbili za kiujuzi)

a. Yasiyofanana kabisa na maisha ya kiroho (walio huru, wasiokubali mambo ya sheria)
b. Muhimu kwa ajili ya wokovu (wahalalishaji).

B. Ukinzani na historia, Ukristo wa kibiblia
1. Kutenganisha ubinadamu na Uungu wa Kristo(wenye ujuzi walisema asingeweza kuwa Mungu kwa ukamilifu na kuwa binadamu kwa ukamilifu)
2. Kuondoa uwakilisho wake wa kifo kama njia pekee ya wokovu
3. Kuweka mbadala wa neema ya bure ya kiungu badala ya maarifa ya kibinadamu

**MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (kutoka "A Guide To Good Reading" Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu chote cha Biblia kwa mara moja. Eleza dhamira kuu ya kitabu kizima kwa maneno yako mwenyewe (mzunguko wa usomaji #1)

1. Dhamira kuu ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi (aina ya fasihi aliyotumia katika kuwasilisha ujumbe wake).

**MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI** (**kutoka** "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia**")

Huu ni mwongozo kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu kizima cha Biblia kwa mara ya pili kwa mara moja. Weka kwa muhtasari masomo makuu (mzunguko wa Usomaji #2) na elezea somo kwa sentensi moja.

1. Somo la kipengele cha kwanza cha fasihi
2. Somo la kipengele ya pili cha fasihi
3. Somo la kipengele cha tatu cha fasihi
4. Somo la kipengele cha nne cha fasihi
5. Na nyinginezo.

# WAEFESO 1

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| salamu<br>1:1-2 | Salamu<br>1:1-2 | Salamu<br>1:1-2 | Salamu<br>1:1a<br>1:b<br>1:2 | Anwani na salamu<br>1:1-2 |
| Baraka za kiroho Katika Kristo<br>1:3-14 | Ukombozi katika Kristo<br>1:3-14 | shukrani na Baraka<br>1:3-6 | Baraka za rohoni katika Kristo<br>1:3-6<br>1:7-10<br>1:11-12<br>1:13-14 | Mpango wa Mungu wa wokovu<br>1:3-14 |
| Maombi ya Paulo<br>1:15-23 | Maombi ya Hekima Ya kiroho<br>1:15-23 | 1:15-23 | Maombi ya Paulo<br>1:15-23 | Ushindi na ukuu wa Kristo<br>1:15-23 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani (Brief Definitions of Greek Grammatical Structure), Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi (Textual Criticism), Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko (Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka **"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii Mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA WA WAEFESO 1:1-23

A. Tungo "katika Efeso" imeondolewa katika RSV, NJB na tafsiri za Williams kwasababu inakosa katika baadhi ya maandiko ya kwanza ya Kiyunani ($P^{46}$, א, na B). Kwa dhahiri kulikuwa na sehemu ya wazi ambapo jina la sehemu lilitakiwa kuingizwa. Ilikuwa ni barua ya watu wote kwa ajili ya makanisa yote ya Asia ndogo. Barua kwenda makanisa saba katika Ufunuo 2-3 inaonesha njia ya mkato ya Rumi ya kale.

B. Utatu ukisifiwa katika Waefeso 1:3-14 (na pia Waefeso 1:17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6)
   1. Baba katika umilele, Waefeso 1:3-6 (upendo wa Baba na kusudi katika Yeye)
   2. Mwana katika wakati, Waefeso 1:7-12 (Upendo wa Baba na kusudi katika Kristo)
   3. Roho katika siku za baadaye, Waefeso 1:13-14 (Upendo wa Baba na kusudi katika Roho)
   Mstari wa 3-14 unatengeneza ombi moja zuri la sifa kwa Mungu wa Utatu! Kila sehemu inahitimishwa na tungo "kwa sifa ya Utukufu Wake" (Waefeso 1:6, 12, 14). Japokuwa utatu wote unatajwa, ni Mungu Baba anayetiliwa mkazo (kama vile Waefeso 1:15:23)! Angalia Mada Maalumu: Utatu katika Waefeso 1:3.
C. Uchaguzi ni fundisho jema. Hata hivyo sio wito wa kubagua, bali wito wa kuwa mfereji, chombo au njia ya ukombozi wa wengine! Katika Agano la Kale, neno lilitumika kimsingi kwa ajili ya wokovu ambao ulikuwa ni jambo la huduma; Biblia haijawahi kupatanisha ukinzani unaoonekana kati ya ukuu wa Mungu na utashi huru wa binadamu lakini inakiri vitu vyote! Mfano mzuri wa mvutano wa Kibiblia ingekuwa Warumi 9 katika uchaguzi wa ukuu wa Mungu na Warumi 10 katika mwitikio wa muhimu wa kibinadamu (rejea Waefeso 10:9, 11-13).

Ufunguo wa mvutano huu wa kithiolojia unapatikana katika Waefeso 1:4. Yesu ni mwanadamu mteule wa Mungu na wote wateule watarajiwa katika Yeye (Karl Barth). Yesu ni "ndio" ya Mungu kwa uhitaji wa mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia inasaidia kuelezea jambo kwa kuelezea kwamba lengo lililoamriwa kabla sio katika mbingu, ila utakatifu (kufanana na Kristo). Mara nyingi tunavutwa kwa faida za injili na kususia majukumu! Wito wa Mungu (uchaguzi) ni kwa muda pia milele!

Mafundisho huja kwa uhusiano na kweli, sio kama moja, kweli zisizohusiana. Mfanano mzuri ungekuwa kundi la nyota dhidi ya nyota moja. Mungu anawasilisha ukweli katika mashariki, sio aina za fasihi za magharibi. Tunalazimika kuondoa mvutano unaosababishwa na safu za kilahaja (kweli zinazokinzana) za kweli za kimafundisho (Kutoka: Mungu avukaye mipaka dhidi ya Mungu kama Mungu mwenye asili ya kuwa kila mahali daima; usalama dhidi ya uvumilivu; Yesu kama sawa na Baba dhidi ya Yesu kama mnyenyekevu kwa Baba; uhuru wa Mkristo dhidi ya majukumu ya Mkristo kwa mwenza wa agano; n.k.).

Dhana ya kithiolojia ya "agano" inaunganisha Mungu Mkuu (ambaye siku zote anachukua hatua ya kuanzisha ajenda) kukiwa na mamlaka ya kuanzia na toba inayoendelea, mwitikio wa imani kutoka kwa mtu. Kuwa mwangalifu wa udhibitisho wa kimaandiko upande moja wa kweli kinzani na uchakavu wa lingine! Kuwa mwangalifu wa kutetea mafundisho yako pekee uyapendayo au mfumo wa thiolojia!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 1:1-2**
**1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko [Efeso] wanaomwamini Kristo Yesu. 2 Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.**

**1:1"Paulo"**Jina la Kiyunani Paulo lilimaanisha "mdogo." Baadhi ya nadharia zimekua kutokana na asili ya jina la Kiyunani.

1. Jina lililojulikana lilielezea umbile lake la mwili, karne ya pili iliweka desturi kuwa Paulo alikuwa mfupi, mnene, mwenye kipara, mwenye matege, mwenye nyusi nyingi kama kichaka, na mwenye macho yanayotokeza njema na yawezekana ndio asili ya jina lake, akitoa katika vitabu visivyo vya kikanoni kutoka katika Thesalonika iliyoitwa *Paul and Thekla*
2. Katika mapito yake ambapo Paulo alijiita mwenyewe "mdogo kati ya watakatifu" kwasababu aliliudhi kanisa kama ilivyo katika Matendo ya Mitume 9:1-2 (kama vile 1 Wakorintho 15:9; Waefeso 3:8; 1 Tim. 1:15)

3. Wengine wameona huu “udogo” kama wenye asili ya cheo cha kujichagulia mwenyewe. Hata hivyo, katika kitabu kama Wagalatia, ambapo anahimiza uhuru wake na hali ya kuwa sawa na kumi na wawili wa Yerusalemu, hii inaweza isiwe hivyo (rejea 2 Wakorintho 11:5; 12:11; 15:10)

Kimalezi, Wayahudi wengi waishio nje ya nchi (Wayahudi waishio nje ya Palestina) walipewa majina mawili mawili wakati wanazaliwa. Jina la kiebrania la Paulo alikuwa akiitwa Sauli na la Kiyunani ndio hilo la Paulo.

▣**”Mtume”** Hii ilitoka katika neno la Kiyunani “kutuma” (*apostellō*). Yesu alichagua wanaume kumi na wawili kuwa nae kwa maana maalumu ya kuwaita “Mitume” (Rejea Luka 6:13). Neno hili mara nyingi lilitumika kwa Yesu akitumwa kutoka kwa baba ( rejea Mathayo 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48; Yohana 4:34; 5:24, 30, 36, 37, 38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8,18,21,23,25; 20:21). Katika vyanzo vya Kiyunani, mtume alikuwa mtu aliyetumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, sawa na “balozi” (rejea 2 Wakorintho 5:20).

▣**”Kristo”** Hili lilikuwa ni neno la Kiyunani sawa na lile la Kiebrania “Masihi” lililomaanisha “aliyepakwa mafuta.” Lilihusisha” aliyeitwa na kuwezeshwa na Mungu kwa ajili ya jukumu fulani.” Katika Agano la Kale makundi matatu ya vikundi vya viongozi: makuhani, wafalme, na manabii, walipakwa mafuta. Yesu alitimiza ofisi hizi zote za kupakwa mafuta (rejea Waebrania 1:2-3).

**MADA MAALUMU: VYEO VYA AGANO LA KALE VYA MTEULE AJAYE**

A. Nabii – Kumb. 18:15,18

B. Mfalme
   1. kutoka kabila la Yuda, Mwa. 49:10; Ps. 60:7; 108:8
   2. kutoka nyumba ya Daudi, 2 Samueli 7 (kutoka kwa Yese, Isa. 11:1)
   3. kutoka maandiko mengine, 1 Sam. 2:10; Zab. 89:3-4; Isa. 9,11; Yer. 30:8-9; Eze. 37:21-22; Zek. 9:9-10

C. Mfalme /Kuhani
   1. Zaburi 110 (mfalme, mist. 1-3; kuhani, mst. 4)
   2. Zek. 4:14 (miti miwili ya mizeituni, wawili waliotiwa mafuta, Zerubabeli [uzao wa Daudi] na Yoshua [uzao wa Aaroni])

D. Aliyetiwa Mafuta (tazama Mada Maalum: Masihi)
   1. Mfalme wa Mungu, Zab. 2:2; 45:7
   2. Uwepo wa Roho, Isa. 11:2; 61:1
   3. Yule Ajaye, Dan. 9:26
   4. Viongozi watatu wa Gano la Kale walitiwa mafuta kama alama ya wito w a Mungu na nguvu: wafalme (kama vile Amu. 9:8,15; 1 Sam. 2:10; 9:16; 24:10; 2 Sam. 19:21; 23:1; Zab. 18:50), makuhani (kama vile Kut. 28:41; Law. 4:3; 6:22), na manabii (kama vile 1 Fal. 19:16)

E. Mwana wa Mfalme
   1. Zab. 2:7,12
   2. Mfalme wa Israeli kama alama ya utawala wa Mungukama vile 1 Samueli 8)

F. Mwana wa Mtu (Dan. 7:13;tazama Mada Maalum: Mwana wa Mungu)
   1. mwanadamu, Zab. 8:4; Eze. 2:1
   2. Uungu, Dan. 7:13

G. Nyadhifa Pekee za Wokovu
   1. Mtumishi ateswaye, Isa. 52:13-53:12
   2. Mchungaji ateswaye, Zek. 12-14
   3. Jiwe la kujikwaza, Zab. 118: Isa. 8:14-15; 28:16 (tazama Mada Maalum: Jiwe la Kujikwaa)
   4. Mwana wa Pekee, Isa. 7:14; 9:6-7; Mika 5:2
   5. Chipukizi, Isa. 4:2; 11:1-5; 53:2; Yer. 23:5-6; 33:15; Zek. 3:8; 6:12 (tazama Mada Maalum: Yesu Mnazarethi)

Kitabu cha Agano Jipya kinayachukua marejeo mbalimbali kuhusu usuluhisho pekee wa ukombozi wa Mungu na kuyabainisha na kuyakuza katika ufahamu wa Yesu kama Mungu Ajaye Aliyehaidiwa (m.f, Mt. 16:13-20; Yohana 11:25-27). Huu ujio wa Masihi wa mara mbili ni maana ambapo tofauti hizi zinatenda kazi na nyadhifa hizi

zinaunganishwa (tazama Mada Maalum: Zama hizi na Zama Zijazo).Kwa mjadala ulio mzuri wa tofauti katika Injili kati ya Mwana wa Adamu kama umbo la mamlaka dhidi ya Mtumishi ateswaye, tazama George E. Ladd, *A Theology of the New Testament*, uk. 149-158.

▣**"Yesu"** hili neno la Kiebrania/Kiaramaiki lililomaanisha "YHWH anaokoa," "YHWH ni wokovu," "YHWH analeta wokovu." Ni sawa na jina la Agano la Kale "Yoshua." "Yesu" lilitoka katika neno la Kiebrania kwa ajili ya wokovu, *hosea,* ikikamilishwa na jina la kiagano kwa Mungu, "YHWH" (angalia Mada Maalumu: Majina ya Uungu katika Wakolosai 1:3). Lilikuwa ni jina lililotolewa na Mungu kupitia malaika wa Bwana (kama vile Mathayo 1:21).

▣**"kwa mapenzi ya Mungu"** Tungo za Utangulizi huu inatumika katika 1 Wakorintho 1:1; 2 Kor. 1:1; Waefeso 1:1 na 2 Timotheo 1:1. Paulo alishawishika kwamba Mungu alimchagua yeye kuwa Mtume. Maana hii ya wito ilianza alipobadilishwa akiwa njiani kwenda Damaskasi (kama vile Mdo. 9:1-22; 23:3-16; 26:9-18). Ufunguzi huu wa tungo unaweka msisitizo katika uelewa wa Paulo katika mamlaka aliyopewa itokayo kwa Mungu. Angalia Mada Maalumu: Mapenzi ya Mungu katika Waefeso 1:9.

▣**"Kwa Watakatifu"** "watakatifu" (*hagioi*) kithiolojia inafanana na neno la Agano la Kale "takatifu" (*kadosh*), ambayo inajumuisha "kuweka kando kwa ajili ya huduma ya Mungu" (kama vile 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Warumi 1:1; Waefeso 1:1; Wafilipi 1:1). Lina wingi katika Agano Jipya isipokuwa wakati mmoja katika Wafilipi 4:21; hata hapo inatumika kama andiko la jumla. Kuokolewa ni kuwa sehemu ya jumuiya ya imani, familia ya waaminio, inayomaanisha kutumikia (kama vile 1 Kor 12:7).

Watu wa Mungu ni watakatifu kwasababu ya shutumu ya haki ya Yesu (kama vile Warumi 4 na 2 Wakorintho 5:21). Ni mapenzi ya Mungu kwamba waishi maisha matakatifu (kama vile Kol. 1:22; 3:12; Waefeso 1:4; 2:10; 4:1; 5:27; Kol. 1:22; 3:12; Mt. 5:48). Waamini wana vyote, kutangazwa watakatifu (kutakaswa kinafasi) na kuitwa katika maisha ya utauwa (kutakaswa kunakoendelea). Utakaso na kuhesabiwa haki lazimi vikiriwe kwa pamoja!

**MADA MAALUM: UTAKASO**

Kitabu cha Agano jipya kinadai kwamba wenye dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kumto mtu hatiani).

Lakini Agano Jipya pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, ni utakaso.

| **Mwitikio wa Awali** | **Ufanano na Kristo Endelevu** |
|---|---|
| Matendo 26:18 | Warumu 6:19 |
| Warumi 15:16 | 2 Kor. 7:1 |
| 1 Wakorintho 1:2-3; 6:11 | Waefeso 1:4; 2:10 |
| 2 Wathesalonike 2:13 | 1 Wathesalonike. 3:13; 4:3-4,7; 5:2 |
| Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12 | 1 Timotheo 2:15 |
| 2 Peter 1:2 | 2 Timotheo 2:21 |
| | 1 Petro 1:15-16 |
| | Waebrania 12:14 |

**NASB** "walioko Efeso"
**NKJV, NRSV** "walioko Efeso"
**TEV** "waishio katika Efeso"
**NJB** "---(imeondolewa)----"

Hili ni tatizo la kimaandiko katika jambo hili. Baadhi ya maandiko ya kale ya Kiyunani ($P^{46}$, א*, B*, pia na maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Origen na Tertullain) yameondoa "katika Efeso." Mpiga porojo wa kwanza Marcion aliita Waefeso "barua kwa Walaodikia." Tungo haitokei katika maandiko $א^2$, A, $B^2$, D, F, na G. Baadaye linatokea katika fasiri za Vulgate, Ki-Syriac, Ki-Coptic na Ki-Armenian.

Sarufi ya Kiyunani Efe.1:1 inaweza ikahifadhi jina la mahali. Hivyo, jina la sehemu yawezekana liliondolewa kwa makusudi kwasababu barua yake ilifanya kazi kama barua ya wengi. Kila kanisa likiweka jina lake mwenyewe inapokuwa ikisomwa kwa sauti mbele ya hadhara. Mapema sana mwandishi katika Efeso (kanisa kubwa katika eneo lile) likiachwa wazi.

▣**"wale walio waaminifu"** Maneno, "imani," "kusadiki," na kuamini vyote vina asili ya mzizi mmoja katika Kiyunani *pistis(*nomino) na *pisteuō (*kitenzi). Msingi wa msisitizo wa kwanza upo katika uaminifu wa Mungu, sio ari au udhati wa mwitikio wa kibinadamu. Waaminio lazima kupokea na kuamini tabia ya kuaminika Kwake na ahadi za ke za milele. Ufunguo upo katika nia ya imani ya mwamini, na sio kiwango cha hiyo imani yake (kama vile Mathayo 17:20; Luka 17:6). Ukristo ni mwititio wa kwanza wa kuanzisha toba/mgeuko unaofuatiwa na mtindo wa maisha ya uaminifu. Imani ya kibiblia ni mfululizo uchaguzi wa toba wa mwanadamu, imani, utii na ustahimilivu.
Angalia Mada Maalumu: Imani, Amini, Sadiki katika Kol 1:2

**1:2 "Neema na amani ziwe nanyi"** Salamu ya kawaida katika barua za Kiyunani ilikuwa neno "salamu" (*charein*, kama vile Mdo. 15:23; 23:36; Yakobo 1:1). Kitabia Paulo aliibadilisha hii kuwa na mfanano sawa lakini neno la Kikristo, neema, (*charis*). Wengi walidhania kwamba Paulo alikuwa kwa namna fulani akiunganisha salamu ya Kiyunani na salamu ya kiebrania, amani (*shalom*). Ingawa hii ni nadharia inayovutia, inawezekana kusoma sana katika aina hii tungo ya utangulizi wa Paulo (kama vile (Warumi 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2; Wafilipi 1:2; na Filemoni 3). "Neema" lilikuwa neno maalumu lililoeleza tabia ya Mungu ya Upendo na Rehema.

▣**"Baba"**Neno hili halitumiki katika namna ya kujamiiana kwa kimwili au mfuatano au mfululizo huu, lakini familia yenye ukaribu. Mungu alichagua maneno yanayohusiana na familia kujifunua mwenyewe kwa mwanadamu (mfalme; Hosea 2-3 kama mwenye upendo, mpenzi mwaminifu, Hosea 11 kama baba na mama mwenye upendo). Angalia Mada Maalum: Baba katika Kol 1:2.

▣**"Bwana"** Neno "Bwana" (*kurious*) inaweza kutumika katika namna ya jumla au katika namna ya kithiolojia. Inaweza kumaanisha "mheshimiwa" "mkuu" (kama vile Yohana 4:11,15,19,49; 5:7; 12:21; 20:15), "Mheshimiwa," "mmiliki," "mume," au "mwanadamu kamili mwenye Mungu" (mfano Yohana 4:1; 6:34,68; 11:2,3,12,21,27,34,39). Mfano mzuri wa matumizi yote mawili katika muktadha mmoja ni Yohana 9:36 na 9:38.
Matumizi ya Agano la Kale ya neno hili (*adon*) lilitoka kutokana na hali ya waalimu wa injili kutotaka kutamka bure jina la kiagano la Mungu, YHWH, kutoka katika kitenzi cha kiebrania "kuwa/kufanyika" (kama vile Kutoka 3:14). Walikuwa na hofu ya kuvunja sheria iliyosema "Usilitamke bure Jina la Bwana Mungu wako" (kama vile Kutoka 20:7, Kumbukumbu la Torati 5:11) walifikiri kama wasipolitamka, watakuwa hawajalitaja bure jina la Mungu. Hivyo walitafuta mbadala wake kwa neno la kiebrania adon, ambalo lilikuwa na maana inayofanana na neno la Kiyunani, *Kurious* (Bwana). Waandishi wa Agano Jipya walilitumia neno hili kufunua Uungu wa Kristo. Tungo "Yesu ni Bwana" ilikuwa ni ukiri kwa umma wa imani na kanuni ya ubatizo wa kanisa la mwanzo (kama vile Warumi 10:9-13; 1 Wakorintho 12:3; Wafilipi 2:11).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 1:3-14**
**3 Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo; 4 kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. 5 Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. 6 Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa. 7 Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake. 8 Naye**

**alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi; [9] akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na uradhi wake, alioukusudia katika yeye huyo. [10] Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo; [11] na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake. [12] Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sisi tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu. [13] Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.[14] Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.**

**1:3** Mstari wa 3-14 ni sentensi moja ndefu ya kiyunani, ambayo ina tabia ya kitabu chake hiki (Waefeso 1:3-14, 15-23; 2:1-10,14-18,19-22; 3:1-12,14-19; 4:11-16; 6:13-20)

▣**”Atukuzwe Mungu”** neno hili Kiyunani “atukuzwe” (*eulogō)* siku zote lilitumika kwa ajili ya kumtukuza Mungu. Ni neno tofauti na neno “kubarikiwa” (*makarios*) kwa heri (kama vile Mathayo 5:1-9, 10-11). Baba alituma Mwanawe wa kiume na Roho kuwaleta waamini katika ushirika na yeye mwenyewe na ushirika kati yetu. Paulo kwa dhahiri anafungua barua zake za shukrani kwa ajili ya wapokeaji (kama vile Waefeso 1:15-23), lakini hapa katika barua ya wazi, kwa upekee sana anaandika kwa Utatu wa Mungu.

▣**”aliyetubariki sisi…….katika Kristo”** Mungu mbarikiwa anabariki! Waaminio hupokea kila kitu kupitia Kristo. Mstari 3-14 ni sentensi moja katika Kiyunani, inayoonyesha kazi ya Utatu kabla ya muda, katika muda na baada ya muda. Hatahivyo uchochezi wa Baba unatukuzwa katika vipengele vitatu (kama vile Waefeso 1:3-6, 7-12 na 13-14).

**MADA MAALUM: UTATU**

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno “utatu,” kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

A. Injili
    1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
    2. Yohana 14:26
B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
C. Paulo
    1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
    2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
    3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
    4. Gal. 4:4-6
    5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
    6. 1 The. 1:2-5
    7. 2 The. 2:13
    8. Tit. 3:4-6
D. Petro – 1 Pet. 1:2
E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
    1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.

2. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7

A. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
   1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
   2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
   3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   4. Zakaria 3:1-2
B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
C. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
D. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea  (kama vile Yn.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho

**NASB, NKJV**
**NRSV** **"katika maeneo yote ya kimbingu"**
**TEV** **"katika ulimwengu wa kimbingu"**
**NJB** **"Baraka zote za rohoni za mbinguni"**

Kiashiria hiki cha mahali (tufe) hasi cha kivumishi chenye wingi "katika maeneo ya mbinguni" (*epouranious*) kilitumika tu katika Waefeso (kama vile Waefeso 1:20; 2:6; 3:10; 6:12). Kutoka katika muktadha wa matumizi yake yote, lazima imaanishe ulimwengu wa roho ambao waaminio wanaishi hapa na sasa, sio mbinguni.

**1:4"Alituchagua"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopita usio timilifu ambayo imejawa na tabia ya uchaguzi wa kimaamuzi ya somo. Hii inaweka shabaha katika uamuzi wa Baba kabla ya muda. Uamuzi wa Baba haupaswi kuanzia kueleweka katika namna ya kiislamu au uhitimishwaji wala sio kule kupitiliza kwa namna ya "Mungu alituchagua sisi dhidi ya Mungu hakuwachagua wengine," lakini katika namna ya kiagano. Mungu alihaidi kuokoa wanadamu walioanguka (kama vile Mwanzo 3:15). Mungu alimwita na kumchagua Ibrahimu kuchagua wanadamu wote (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5-6). Angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH. Mungu anawaita wote katika Kristo (kama vile Yohana 3:16; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4;14). Mungu mwenyewe aliwachagua watu wote ambao wangeweza kuweka imani yao kwa Kristo. Uchaguzi wa Waamini wa kutumaini katika Kristo unathibitisha, hakuashirii, uchaguzi wa Mungu kwao. Mungu siku zote ndiye anayechukua hatua ya kuanzisha katika wokovu (kama vile Yohana 6:44, 65). Andiko hili na Warumi 8:28-30; 9:1-33 ni maandiko makuu katika Agano Jipya kwa mafundisho ya kuamriwa kwanza iliyoweka msisitizo na Augustine na Calvin.

Mungu alichagua waamini sio tu kwa ajili ya wokovu (kufanywa haki) lakini pia utakaso (kama vile Kol. 1:12)! Hii inaweza kufanana na

1. Nafasi yetu katika Kristo (kama vile 2 Kor. 5:21)
2. Shauku ya Mungu ya kuzalisha tabia yake katika watoto wake (kama vile Waefeso 2:10; Warumi 8:28-29; Gal. 4:19; 1 The. 4:3)

Mapenzi ya Mungu kwa watoto wake ni vyote mbinguni siku moja na kufanana na Kristo sasa!
Viwakilishi katika kifungu hiki cha habari ni tata. Vingi kati ya hivi vinamrejerea Mungu Baba. Kifungu hiki chote cha habari kinazungumza juu ya upendo wake, kusudi na mpango wa kukomboa mwanadamu aliyeanguka. Hata hivyo katika muktadha huu ni wazi kwamba viwakilishi katika Waefeso 1:7, 9, 13 & 14 vinamuhusu Yesu.

▣**"katika yeye"** Hii ni dhana ya msingi. Baraka za Baba, neema na wokovu unatiririka tu kupitia Kristo (kama vile Yohana 10: 7-18; 14:6). Angalia kurudia rudia kwa mtindo huu wa kisarufi (kuwekwa mahali kwa tufe) katika Waefeso 1:3, katika yeye; Efe.1:7, "katika yeye"; Efe. 1:19, "katika yeye"; Efe. 1:10, "katika Kristo," "katika Yeye"; Efe.1:12, "katika Kristo" na Efe. 1:13, "katika yeye" (mara mbili). Hizi zinafanana na tungo"katika huyo mpendwa" ya Waefeso 1:6. Yesu ni "ndio" ya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Yesu ni mteule wa mwanadamu Mungu na wote ni wateule watarajiwa katika yeye (kama vile Yohana 3:16). Baraka zote za Mungu zinatiririka kupitia Kristo.

▣**"kabla ya misingi ya ulimwengu"** Tungo hii pia inatumika katika Mathayo 25:34; Yoh. 17:24; 1 Pet. 1:19-20 na Ufunuo. 13:8. Inaonesha vitendo vya ukombozi vya Utatu wa Mungu hata kabla ya Mwanzo 1:1. Angalia Mada Maalumu: Matumizi ya Paulo ya *Kosmos* katika Kol 1:6. Wanadamu tuna mipaka kwa namna ya muda; kila kitu kuhusu sisi kinakuwa kimepita ni cha zamani, sasa au kijacho lakini sio kwa Mungu. Historia kwake ni umilele wa wakati huu uliopo.

▣**"li tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake"** lengo la kuamriwa kabla ni utakatifu na sio upendeleo. Wito wa Mungu sio kwa waliochaguliwa wachache walio watoto wa Adamu lakini ni kwa wote! Ni wito wa kuwa vile Mungu alivyokusudia mwanadamu awe, kama yeye mwenyewe, yaani kufanana na Kristo (kama vile Warumi. 8:28-30; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 4:13; 1 The. 3:13; 4:3; 5:23; 2 The. 2:13; Tito 2:14; 1 Pet. 1:15); katika taswira yake (kama vile Mwazo 1:26-27). Kugeuza kuamriwa kabla katika misingi ya kithiolojia badala ya maisha ya utauwa ni janga. Mara nyingi mfumo wetu wa kithiolojia cha *priori* inazungumza zaidi na kwa nguvu zaidi ya maandiko ya kibiblia!
Neno "isiyo na shutuma" (*amōmos*) au "huru kutoka katika shutuma" linatumika kama

1. Yesu, (kama vile Ebr. 9:14; 1 Petro 1:19)
2. Zakaria na Elizabeth, (kama vile Luka 1:6)
3. Paulo (kama vile Wafilipi 3:6)
4. Wakristo wote wa ukweli (kama vile Wafilipi 2:15; 1 The. 3:13; 5:23)

Angalia Mada Maalum katika Kol. 1:22
Mapenzi ya Mungu yasiyoweza kuhairishwa au kukengeushwa kwa kila mwamini sio tu kwa ajili ya mbingu ya baadaye, lakini kufanana na Kristo sasa (kama vile Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Waamini wanatakiwa kuaksi tabia za Mungu kwa ulimwengu uliopotea kwa ajili ya uinjilishaji.

**MADA MAALUM: TAKATIFU**

I. Agano la Kale (likielezwa kwa zaidi kutoka Isaya)

A. Asili ya neno *kadosh* (BDB 872, KB 1072) halina uhakika, pengine ni Ki-kanaani (yaani, lugha Magharibi mwa Syria). Inawezekana kwamba sehemu ya mzizi wa neno (yaani, *kd*) unamaanisha "kugawanya."

Hiki ni chanzo cha ufafanuzi unaofahamika wa neno "tengwa (kutoka kwenye utamaduni wa ki- Kanaani, kama vile Kumb. 7:6; 14:2,21; 26:19) kwa matumizi ya Mungu."

B. Inahusiana na uwepo wa Mungu ndani ya vitu, mahali, wakati, na watu. Halitumiki katika kitabu cha Mwanzo, bali linakuwa la kawaida katika vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, na Hesabu.

C. Katika fasihi ya Kinabii (hasa Isaya na Hosea) hali ya kibinadamu ilikuwepo hapo awali, lakini haikuhimizwa kwa ajili ya kutenda kazi (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu). Inakuwa njia ya kueleza asili ya Mungu.(kama vile Isa. 6:3). Mungu ni Mtakatifu. Jina Lake linalowakilisha sifa yake ni takatifu. Watu wake ndio wanaopaswa kuifunua sifa Yake kwa ulimwengu unaohitaji utakatifu (ikiwa watalitii agano katika imani).

1. KIVUMISHI, BDB 872 שודק, "takatifu," "tukufu" linatumika juu ya

   a. Mungu, Isa. 5:16; 6:3 (mata tatu); tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu
   b. Jina Lake, Isa. 40:25; 49:7; 57:15
   c. kukaa Kwake ndani, Isa. 57:15
   d. Sabato, Isa. 58:13

2. KITENZI, BDB 872 שדק, "kutengwa mbali," "wekwa wakfu"

   a. sifa ya Mungu, Isa. 5:16; 29:23
   b. Mungu, Isa. 8:13; 65:5
   c. malaika wa Mungu, Isa. 13:3
   d. jina la Mungu, Isa. 29:23
   e. sherehe za kidini, Isa. 30:29
   f. wanadamu walioweka wakfu, Isa. 66:17

3. NOMINO, BDB 871 שדק, "utengwaji," "uwekwaji wakfu"

   a. uzao mtakatifu, Isa. 6:13
   b. mlima mtakatifu, Isa. 11:9; 27:13; 56:7; 57:13; 65:11,25; 66:20
   c. kutengwa, Isa. 23:18
   d. njia ya utakatifu, Isa. 35:8
   e. mahali patakatifu, Isa. 43:28; 62:9; 64:11
   f. mji mtakatifu, Isa. 48:2; 52:1
   g. aliye Mtakatifu, Isa. 49:7 (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu)
   h. mkono mtakatifu, Isa. 52:10
   i. siku takatifu, Isa. 58:13
   j. watu watakatifu, Isa. 62:12
   k. Roha Mtakatifu, 63:10,11
   l. Kiti cha enzi cha Mungu, Isa. 63:15
   m. sehemu takatifu, Isa. 63:18
   n. miji mitakatifu, Isa. 64:10

D. Huruma ya Mungu na upendo havitenganishwi kutoka katika dhana ya theojia ya maagano,haki, na sifa ya muhimu. Humu ndani pana mvutano wa Mungu dhidi ya utu ulioanguka, usio mtakatifu ,wenye kuasi. Kuna mada inayotia shauku sana kuhusiana na mahuhusiano kati ya Mungu kama "mwenye huruma" na Mungu kama "mtakatifu" katika kitabu cha Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kr. 112-113.

II. Agano Jipya

A. Waandishi wa Agano Jipya (isipokuwa Luka) walikuwa Waebrania wenye fikra pana, lakini waliandika katika lugha ya kawaida ya Koine. Kanisa la Agano Jipya lilitumia fasiri ya Kiyunani kufasiri kitabu cha

Agano la Kale. Ilikuwa ni tafasili ya Kiyunani ya Agano la Kale, sio fasihi ya Kiyunani cha daraja la juu, fikra, au dini, iliyodhibiti misamiati yao.

B. Yesu ni mtakatifu kwa kuwa Yeye ni wa Mungu na ni sawa na Mungu (kama vile Luka 1:35; 4:34; Matendo 3:14; 4:27,30; Ufu. 3:7). Yeye ni Mtakatifu na Mwenye Haki (kama vile Matendo 3:14; 22:14). Yesu ni mtakatifu kwa sababu hana dhambi (kama vile Yohana 8:46; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 1:19; 2:22; 1 Yohana 3:5).

C. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu (kama vile Yohana 17:11; 1 Pet. 1:156-16; Ufu. 4:8; 6:10), watoto Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Law. 11:44-45; 19:2; 20:7,26; Mt. 5:48; 1 Pet. 1:16). Kwa kuwa Yesu ni mtakatifu, wafuasi Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Wakristo wameokolewa ili kutumika katika ufanano wa Kristo (wenye utakatifu).

▣**"katika upendo"**kisarufi tungo hii ingeweza kwenda na aidha mstari wa 4 au mstari wa 5. Hata hivyo, wakati wa tungo hii inatumika katika maeneo mengine katika waefeso mara nyingi inarejerea upendo wa mwanadamu kwa Mungu (kama vile Efe. 3:17; 4:2, 15, 16).

**1:5**

**NASB "Aliamua kwanza katika sisi"**
**NKJV "alipo amua kabla ndani yetu"**
**NRSV "aliweka hatima yetu"**
**TEV "Mungu amekwisha tuchagua sisi tayari"**
**NJB "akituwekea alama hapo kwanza sisi kwa ajili yake**

Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu. Neno hili la Kiyunani ni ambatani ya "kabla" *(pro)* na kuweka "alama" (*horizō*). Inarejerea mpango wa ukombozi ulioamriwa na Mungu hapo kabla, angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH katika Waefeso 3:6, (kama vile Luka 22:22; Mdo 2:23, 4:28; 13:29; 17:31; Rum. 8:29-30). Angalia mpango wa Mungu ni jumuishi (kama vile Mdo. 13:48). Nadharia ya kimarekani ya ubinafsi imegeuza ujumuishi huu na msisitizo wa ushirika kwenda katika upendeleo wa baadhi, shabaha ya ubinafsi na u-mimi. Mungu alichagua watu ambao watamchagua yeye. Nadharia ya kumariwa kabla ni moja ya baadhi ya kweli zinazofanana na wokovu wa binadamu. Ni moja ya utaratibu wa kithiolojia au mfuatano wa kweli zianazofanana. Haikuwahi kukusudiwa kusisitizwa katika kusimama peke yake! Ukweli wa Kibiblia umetolewa katika mfululizo wa jozi zenye ukinzani na zilizojaa mvutano. Udhehebu umefanya kuondoa mvutano wa kibiblia kwa kusisitiza aina moja ya kweli Fulani tu (kwa mfano: kuamriwa kabla dhidi ya utashi binafsi wa mwanadamu: usalama wa mwamini dhidi ya ustahimilivu; dhambi ya asili dhidi ya hiari; hali ya kutokuwepo na dhambi dhidi ya kupungua kwa utendaji wa dhambi; tamko la utakaso wa mara moja dhidi ya utakaso endelevu; imani dhidi ya matendo; uhuru wa mkristo dhidi ya uwajibikaji wa mkristo; kubadilika dhidi ya kutobadilika).

**MADA MAALUM: Kuamriwa kabla (Calvinism) dhidi ya Utashi Huru wa Mwanadamu(Arminiasm)**

Tito 2:11 Ni mlinganyo wa vifungu vingine vya Agano Jipya kwenye uchaguzi. Nilifikiri inaweza kuwa ya msaada wa kitheolojia kusaidia kutoa maelezo yangu ya kiufafanuzi kutoka kwa Warumi 8:29 na sura ya 9, pamoja na Waefeso 1.

I. Warumi 8:29 – Paulo anatumia "naliwajua kabla" (*proginōskō*, "kujua kabla") maradufu, hapa na 11:2. Katika 11:2 inamaanisha upendo wa Agano la Mungu kwa Israeli kabla ya wakati kuanza. Kumbuka kwamba neno "kujua" kwa kiebrani linahusiana na uhusiano binafsi,wa ndani, sio kumwambia ukweli kuhusu mtu fulanii (kama vile. Mwanz. 4:1; Yer. 1:5). Hapa ilikuwa imejumuisha katika mlolongo wa matukio ya milele (kama vile. Waru. 8:29-30). Neno hili lilihusishwa na kuamuliwa kabla. Hata hiyo, ni lazima ieleweke kwamba maarifa ya Mungu ya mambo yajayo sio msingi wa uchaguzi kwa sababu ikiwa ni hivyo, basi uchaguzi utakua umeegemea katika mwitikio wa baadaye wa binadamu uliyeanguka, ambao utakua utendaji wa kibinadamu. Neno hili pia linapatikana katika Matendo 26:5; Pet 1. 1:2,20 na Pet 1. 3:17.

A. "aliowajua tagu asili" (*proginōskō*, "kujua kabla")

Maneno "aliowajua tangu asili" na "aliwachagua tangu asili"yote ni maneno ambatani pamoja na kihusishi "kabla" na, kwa hiyo inapaswa kutafsiriwa, "kujua kabla ," "kuweka mipaka kabla," au "alama kabla ." Vifungu ya uhakika juu ya kuamuliwa kabla katika Agano Jipya ni Warumi. 8:28-30; Waef. 1:13-14; na Warumi 9. Maandiko haya ni dhahiri kusisitiza kwamba Mungu ni Mfalme.Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu yote. Kuna mpango wa ki-Uungu uliowekwa tayari ili kufanywa kwa wakati. Hata hivyo, mpango huu sio wa kiholela wala kuchagua. Inategemea sio tu juu ya Ufalme wa Mungu na ujuzi wa asili, lakini kwa tabia yake isiyobadilika ya upendo, huruma, na neema isiyostahili. Tazama Mada Maalumu: YHWH's Mpango wa Ukombozi wa Milele.

Tunapaswa kua makini na ubinafsi wetu wa magharibi (Amerika) au moyo wetu wa uinjilisti wa kuulemba ukweli huu wa ajabu. Tunapaswa pia kulindwa dhidi ya kukingamizwa ndani ya historia, kitheolojia kati ya Augustine dhidi ya Pelegius au Calvinism dhidi ya Arminianism.

B. "imeamriwa kabla" (*proorizō*, "kuweka mipaka kabla")

Kuamriliwa kabla sio mafundisho yenye maana ya kupunguza upendo wa Mungu, neema, na huruma wala kuwatenga wengine kutoka kwenye injili. Ilikuwa na maana ya kuimalisha wanaoamini kwa kuunda maoni yao ya ulimwengu. Mungu ni kwa ajili ya binadamu wote (kama vile. Yohana 1:12; 3:16; Tim 1. 2:4; Petro 2. 3:9; Yohana 1. 2:2; 4:14).Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu vyote. Nani au nini kinachoweza kututenganisha na yeye (kama vile. Warumi. 8:31-39)? Mungu anaona historia yote mambo yaliyopita kama yapo sasa; binadamu ni kiumbealiyefungwa na muda. Mtazamo wetu na uwezo wa akili ni wenye mipaka/kikomo. Hakuna kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, Ni muundo wa Agano. Huu ni mfano mwingine uliotolewa katika mvutano wa lahaja. Mafundisho ya kibiblia yanatolewa kwa mtazamo tofauti. Mara nyingi huonekana fumbo la maneno. Ukweli ni mlinganyo kati ya jozi zilizo kinyume. Hatupaswi kuondoa mvutano kwa kuchukua moja ya ukweli. Hatupaswi kutenganisha ukweli wowote wa Kibiblia ndani ya chumba.

Ni muhimu kuongeza kwamba lengo la uchaguzi sio mbinguni tu wakati tunapokufa,lakini mapenzi ya Kristo sasa. (kama vile Warumi. 8:29-30; Wakorintho 2. 3:18; Gal. 4:19; Waefeso. 1:4; 2:10; 4:13; The. 1. 3:13; 4:3; 5:23; The 2. 2:13; Tito 2:14; Pet 1. 1:15). Tumechaguliwa kuwa "watakatifu wasio na lawama." Mungu huchagua kutubadili ili wengine waweze kuona badiliko na kuitikia kwa imani kwa Mungu katika Kristo. Majaaliwa sio pendeleo la kibinafsi, bali ni wajibu wa Agano. Huu ni ukweli mkuu wa kifungu hiki. Hili ni lengo la Ukristo. Utakatifu ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini. Uchaguzi wa Mungu ni mapenzi ya Kristo (kama vile. Waefeso 1:4),sio msimamo maalumu. Mfano wa Mungu ulotolewa kwa binadamu katika uumbaji (kama vile. Mwanzo. 1:26; 5:1,3; 9:6), ni kurejeshwa.

C. "kubali kugeuzwa kwa mfano wa mwanawe"—Lengo kuu la Mungu ni kurejesha picha iliyopotea kwenye anguko. Waamini wamewekwa mbele kwa mapenzi ya Kristo kama vile. Waefeso. 1:4).

II. Warumi 9

A. Warumi 9 ni mojawapo ya kifungu cha Agano Jipya juu ya Ufalme wa Mungu (mwingine kuwa Waef. 1:3-14), wakati sura ya 10 inasema kuwa uhuru wa binadamu ni dhahiri na hujirudia mara kwa mara (kama vile. "kila mtu" War. 9:4; "kila mtu" 9:11,13; "wote" 9:12 [maradufu]). Paulo kamwe hakujaribu kupatanisha mvutano huu wa kitheolojia. Wote ni wa ukweli! Mafundisho mengi ya Biblia yanawasilishwa kwa fumbo la maneno au jozi za lahaja. Mifumo mingi ya theolojia ni yenye mantiki na nusu ya ukweli . Augustinianism na Calvinism dhidi ya nusu-Pelegianism na Arminianism zina misingi ya ukweli na yenye makosa. Mvutano wa kibiblia kati ya mafundisho ni bora kwa maandishi ya ushahidi, yenye kutangazwa kama imani ya kanisa, ya kimantiki, ya mfumo wa kitheolojia ambayo inasisitiza Biblia kwenye mstari wa ramani iliyoelezea kabla.

B. Ukweli huo huo (unapatikana katika Warumi. 9:23) umeelezwa katika Warumi. 8:29-30 na Waefeso. 1:4,11. Sura hii ni maelezo yenye nguvu zaidi ya uweza wa Mungu katika Agano Jipya. Haiwezi kuwapo

na migogoro kwa vile Mungu ndiye muhusika wa jumla wa uumbaji na Ukommbozi. Ukweli huu mkubwa haupaswi kamwe kufutwa au kupunguzwa. Hata hiyo, ni lazima pawepo na mlinganyo na uchaguzi wa Mungu wa agano kama njia ya kuhusianisha na uumbaji wa mwanadamu, uliofanywa kwa mfano wake. Kama vile Mwanzo 15 isiyokuwa na masharti na haihusiani kabisa na majibu ya mwanadamu, lakini maagano mengine yenye masharti juu ya majibu ya binadamu (mf., Edeni, Nuhu, Musa, Daudi).Mungu ana mpango wa ukombozi kwa uumbaji wake;hakuna mwanadamu anayeweza kuathiri mpango huu. Mungu amechagua kuruhusu watu binafsi kushiriki katika mpango wake. Nafasi hii ya ushiriki ni mvutano wa kitheolojia kati ya Ufalme( Warumi 9) na mapenzi ya Kibinadamu (Warumi 10).

Sio sahii kuchagua msisitizo mmoja wa Biblia na kupuuza mwingine. Kuna mvutano kati ya mafundisho kwa sababu watu wa mashariki wanawasilisha kweli katika lahaja na jozi kujaza mvutano. Mafundisho lazima yafanyike katika mahusiano na mafundisho mengine. Ukweli ni kweli za Musa.

III. Waefeso 1

A. Uchaguzi ni mafundisho ya ajabu. Hata hivyo si wito kwa upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa ajili ya huduma; katika agano jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia haipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa Kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguzi wa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile. 10:11,13).

Umuhimu wa mvutano huu wa kitheolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni "ndiyo" ya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo).Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!

Mafundisho huja huja kutokana na kweli zingine, sio kama moja, lisilohusiana na ukweli. Mfuatano mzuri ungalikuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika namna ya kimashariki na sio kimagharibi. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho ( Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu aliye dhahili: usalama dhidi ya uvumilivu;Yesu aliye sawa na Mungu baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu; Uhuru wa kikristo dhidi ya wajibu wa kikristo kwa mwenzi wa agano, nakadharika).

Dhana ya kitheolojia ya "agano" inaunganisha Uweza wa Mungu (ambaye daima huchukua hatua kwa kuweka mswada) wenye mwanzo muhimu na mwendelezo wa mwitikio wa imani ya toba kutoka kwa mtu. Kuwa mwangalifu na uhakiki wa maandiko wa upande mmoja na kupuuza mwingine! Kuwa mwangalifu wa kuthibitisha mafundisho yako pendwa au mfumo wa theolojia.

B. "alivyotuchagua" katika Waef. 1:4 ni KAULI YA KATI ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ambayo inasisitiza somo. Hii inalenga katika uchaguzi wa Mungu kabla ya wakati. Chaguo la Mungu halipaswi kueleweka kwa maana ya kiislamu ya falsafa za maamuzi.Mungu aliahidi kuwakomboa wanadamu walioanguka (kama vile. Mwanzo. 3:15). Mungu alimwita na kumchagua Ibrahimu kuchagua wanadamu wote (kama vile. Mwanzo. 12:3; Kutoka. 19:5-6).

Mungu mwenyewe alichagua wanadamu wote ambao wangetenda imani katika kristo. Mungu daima huchukua maamuzi mwenyewe katika wokovu (kama vile. Yohana 6:44,65). Nakala hii na Warumi 9 ni msingi wa Kibiblia kwa mafundisho ya majaaliwa yaliyosisitizwa na Augustine na Calvin.Mungu alichagua wanaoamini si tu kwa wokovu (kuhesabiwa haki), lakini pia kwa utakaso (kama vile. Wakolosai 1: 10-12).

Hii inaweza kuhusiana na (1) nafasi yetu katika Kristo (kama vile. Wakorintho 2. 5:21) au (2) Nia ya Mungu kuzalisha tabia yake katika wana wake (kama vile. Waef. 2:10; Warumi. 8:28-29; Wagalatia. 4:19). Mapenzi ya Mungu kwa wana wake ni kuwaona wote mbinguni siku moja na kufanana na Kristo sasa!

"katika yeye" ni dhana muhimu ya Waef . 1:4. Baraka za Mungu, neema, na wokovu hupitia kwa njia ya kristo (kama vile. Yohana 14:6). Angalia kurudia rudia kwa umbo hili la kisarufi (ENEO LA MAHALI) katika

Waefeso. 1:3, "katika kristo"; 1:4, "katika yeye"; 1:7, "katika yeye"; 1:9, "katika yeye"; 1:10, "katika kristo," "katika yeye"; 1:12, "katika kristo" na 1:13, "katika yeye" (maradufu).Yesu ndiye mwanadamu aliyechaguliwa na wote wanawezekana kuchaguliwa ndani yake. Wote wa Mungu Baraka za Baba zinapatikana katika Kristo.

Maneno “kabla ya msingi wa Dunia” pia hutumiwa katika Mt. 25:34; Yohana 17:24; Pet 1. 1:19-20 na Ufu. 13:8. Inaonyesha nafsi tatu kwa moja ya shughuli ya ukombozi wa Mungu hata kabla ya Mwanzo. 1:1. Binadamu anakikomo kwa maana za wakati; kila kitu kwetu ni cha muda uliopita, wa sasa,na wa baadaye, lakini si kwa Mungu.

Lengo la kuamua kabla ni utakatifu sio pendeleo. Wito wa Mungu sio wa wachache waliochaguliwa wa wana wa adamu, bali kwa wote! Wito ulikuwa ni kile Mungu alichotaka mwanadamu kuwa kama yeye mwenyewe (kama vile. 1 Wathesalonike 5:23; 2 Wathesalonike 2:13);katika sura yake (kama vile. Mwanzo. 1:26-27). Ili kugeuza majaaliwa kuwa katika kanuni ya theolojia badala ya maisha takatifu kuwa janga. Mara nyingi theolojia yetu huzungumza kwa sauti zaidi kuliko maandiko ya Kibiblia.

Neno "wasio na lawama" (*amōmos*) au "bila lawama" linatumika

1. Yesu (kama vile. Waebrania. 9:14; Pet 1. 1:19)
2. Zekaria and Elisabeti (kama vile. Luka 1:6)
3. Paulo (kama vile. Wafilipi. 3:6)
4. wakristo wote wa kweli (kama vile. Wafiipi. 2:15; Wathesalonike 1. 3:13; 5:23)

Mapenzi ya Mungu yasiyowezekana kubadilika kwa kila Mkristo sio baadaye mbinguni tu, lakini ni mapenzi ya kristo sasa (kama vile. Warumi 8:29-30; Wagalatia 4:19; Pet 1. 1:2). Wanaoamini wanapaswa kuitazamisha tabia ya Mungu kwa ulimwengu uliopotea kwa dhumuni la Uinjilisti.

Kisarufi maneno “katika upendo” katika Tito 2:2 yanaweza kwenda pamoja na Tito 2:4 au 5. Hata hivyo wakati maneno haya yanatumika katika maeneo mengine katika Waefeso daima yanahusu upendo wa Kibinadamu kwa Mungu (kama vile. Waefeso. 3:17; 4:2,15,16).

C. Katika Waefeso. 1:5 neno "alitangulia kutuchagua" ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Neno hili la Kiyunani ni neno ambatani kwa “kabla” na “alama kabla.” Inahusu mpango wa ukombozi wa Mungu uliotanguliwa kabla (kama vile Luka 22:22; Matendo 2:23; 4:28; 17:31; Warumi 8:29-30). Majaaliwa ni moja ya ukweli kadhaa kuhusiana na wokovu wa mwanadamu. Ni sehemu ya kikolezo cha kitheolojia au mfululizo wa ukweli unaohusiana. Haikuwa na maana ya kusisitizwa katika kutengwa! Kweli ya Kibiblia imetolewa katika mfululizo wa mvutano wa anguko, jozi za fumbo la maneno. Ufuasi wa kimadhehebu umejaribu kuondoa mvutano wa kiibiblia kwa kusistiza kweli moja tu ya ukweli wa lahaja (majaaliwa dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu ; usalama wa mwamini dhidi ya uvumilivu wa watakatifu; dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari; kutokuwa na dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo; utakaso wa mara moja dhidi ya utakaso wa kuendelea;imani dhidi ya kazi; Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo; Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu wa asili).

Uchaguzi wa Mungu haukutegemea ujuzi wa mbele wa utendaji wa mwandamu, lakini kwa tabia yake ya neema (kama ile. Waef. 1:7,9,11). Alitamani kwamba wote (hapana mmoja kama mwenye mafunuo) angeokolewa (kama vile Ezek. 18:21-23,32; Yohana 3:16-17; Tim 1. 2:4; 4:10; Tito 2:11; Pet 2. 3:9; Yohana 1. 2:2; 4:14). Neema ya Mungu (tabia ya Mungu) ni muhimu kitheolojia kwa kifungu hiki (kama ile. Waef. 1:6a, 7c, 9b), kama huruma ya Mungu ni muhimu kwa kifungu kingine juu ya kuamuliwa kabla kwa mambo, Warumi 9-11.

Tumaini pekee la wanadamu walioanguka ni neema na huruma ya Mungu (kama vile. Isay. 53:6 na nyingine kadhaa za Agano la Kale zilizotajwa katika Warumi. 3:9-18). Ni muhimu sana kwa kutafsiri sura hizi za kwanza za kitheolojia ili kutambua kwamba Paulo anasisitiza mambo hayo ambayo hayahusiani kabisa na utendaji wa mwanadamu: kuamuliwa kabla kwa mambo (Waefeso 1), neema (Waefeso 2), na mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu (Ajabu, Waefeso 2:11- 3:13). Hii ilikuwa ni kusawazisha mkazo wa walimu wa uongo juu ya sifa ya binadamu na kiburi.

▣**”kufanywa wanawe”** hii ni stiari inayojulikana ya Paulo (kama vile Warumi 8:15, 23: 9:4; Wagalatia 4:5). Ni moja ya stiari kadhaa za Paulo anazozitumia kuonesha wokovu kwa msisitizo katika usalama. Ilikuwa ni ngumu na ghali

kumfanya mtoto wa mwingine awe wako katika mfumo wa sheria wa Kirumi, lakini mara ilikuwa ikishafanyika basi inakuwa ya kudumu na shurutishi kutii makubaliano. Baba wa Kirumi alikuwa na haki ya kisheria kukataa urithi wa watoto wake wa asili hata kuwauwa lakini si watoto ambao si wa asili ila amewafanya wawe wake. Hii inaaksi usalama wa waaminio katika Kristo.

**NASB** **"sawasawa na uradhi wa mapenzi yake"**
**NKJV, NRSV** **"sawasawa na tamaa njema ya napenzi yake"**
**TEV** **"Hii ilikuwa ni raha yake na kusudi lake"**
**NJB** **"hilo lilikuwa kusudi lake na nia yake njema"**

Uchaguzi wa Mungu haujajikita katika taarifa na maarifa aliyokuwa nayo hapo kabla kwa matendo ya mwanadamu lakini katika tabia yake njema ya neema (kama vile Waefeso 1:7,"kulingana na utajiri wa neema yake"; Waefeso 1:9, "sawasawa na Uradhi wa mapenzi yake"; Waefeso 1:11, "sawasawa kusudi lake"). Anatamani kwamba vyote (si kwa baadhi ya wajuzi au wanaoshikilia msimamo wa dhana ya kuamriwa kabla wa kisasa) wangeokolewa (Ezek. 18:21-23, 32; Yoh. 3:16-17; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yoh. 2:2; 4:11). Neema ya Mungu (tabia ya Mungu) ni ufunguo wa kithiolojia kwa kifungu hiki cha habari Efe. 1:6a; 7c; 9b), kama rehema za Mungu ni ufunguo wa kifungu kingine cha habari kwa kuamriwa kabla, Warumi 9-11.
Tumaini pekee kwa ubinadamu ulioanguka ni neema na rehema za Mungu (kama vile Mdo. 15:11; Rum. 3:24; 5:15; Efe. 2:5, 8) na tabia yake isiyobadilika (kama vile Zaburi 102:27; Mal. 3:6; Yak. 1:17; 1 Yoh. 1:5).

▣**"kwa njia ya Yesu Kristo Mwenyewe"** tungo hii inafunua upendo wa Baba, kama afanyavyo Yohana 3:16 (kama vile 2 Kor 13:14). Yesu ni mpango wa Mungu wa Baba wa kurejesha vitu vyote (yaani Masihi, kama vile Efe. 1:10; 1 Kor. 15:25-28; Kol. 1:15-23). Kuna njia moja tu na njia hiyo ni njia ya mtu (kama vile Yohana 14:6; Mdo. 4:12; 1 Tim. 2:5). Maudhui ya Waefeso ni umoja wa vitu vyote katika Kristo.

**1:6 "kwa sifa ya utukufu wa neema yake**" upendo aliouanzisha Baba katika Kristo Yesu unafunua umuhimu wake thabiti (kama vile Yohana 1:14, 18). Tungo hii inarudiwa mara tatu (kama vile Waefeso 1:6, 12, 14) na lafudhi ya kazi ya nafsi tatu za Utatu. Angalia Mada Maalum katika 1:3

1. Baba Mungu kabla ya muda, Efe. 3-6
2. Mungu mwana katika muda, Efe. 1:7-12
3. Mungu Roho kupitia muda, Efe. 1:13, 14

Hata hivyo katika sentensi yake ndefu ya Kiyunani kutoka Waefeso 1:3-14, ni Mungu anayesifiwa kwa kurudiwa rudiwa.

▣**"utukufu"** katika agano la Kale, neno linalojitokeza mara kwa mara la kiebrania kwa ajili ya utukufu ni *"kabod"* lilikuwa ni jina la kibiashara(ambalo linafanana na jozi za mizani), iliyomanisha "kuwa nzito." Kile kilichokuwa kizito kilikuwa na thamani au kilikuwa thamani ya asili. Dhana ya mng'ao iliongezwa kwa neno kuelezea ukuu wa Mungu (yaani shekinah, wingu la utukufu). Yeye pekee ni wa thamani na mwenye heshima. Yeye ana akili sana kwa ubinadamu ulioanguka (kama vile Mwanzo 16:13; 32:30; Kutoka 20:19; 33:20; Waamuzi 6:22-23; 13:22). Mungu anaweza akajulikana kwa uhakika kupitia Kristo (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15; Waebrania 1:3)
Neno "utukufu" kwa namna fulani ni tata

1. Linaweza kufanana na "haki ya Mungu"
2. Linaweza kurejerea kwa "utakatifu" au "ukamilifu" wa Mungu
3. Linaweza kurejerea taswira ya Mungu ambayo mwanadamu aliumbwa kwayo (kama vile Mwanzo 1:26-27; 5:1; 9:6) ambayo kwa baadaye iliharibika kupitia tamaa ya ukaidi ya kujitegemea (kama vile Mwanzo 3:1-22).

**NASB** **"ambayo ametuneemesha"**
**NKJV** **"ambayo ametufanya tukubaliwe"**
**NRSV** **"ambayo ametukirimia bure juu yetu sisi"**
**TEV** **"kwa karama ya bure aliyotupatia"**

**NJB “karama yake ya bure kwetu sisi”**

Neno la kiyunani “kupendelewa” (*charitoō*) lina mzizi sawa na "neema" (*charis*). Neema ya Baba, rehema na mtiririko wa upendo (kama vile Waefeso 1:8) kupitia mateso ya Masihi kwa mwanadamu aliyeanguka (kama vile Mwanzo 3:15; Isaya 53). Mtiririko wa upendo wa Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka kwasababu ya Yeye alivyo, na si jinsi tulivyo! Funguo hapa ni tabia ya Mungu na sio matendo ya binadamu!

▣**” katika huyo Mpendwa”** hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea. Yesu alikuwa na ndiye Mwana mpendwa na siku zote atakuwa hivyo. Wadhifa huu ulitumika katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani (LXX) kwa ajili ya Masihi. Iliwekwa mbadala na “Jeshurun” (Yerusalemu) katika Kumbukumbu la torati 32:15; 33:5, 26 na Isaya 44:2. Baba alitumia wadhifa huu kumuelezea Yesu katika Mathayo 3:17 (wakati wa ubatizo wa Yesu); Mathayo 12:18 (nukuu ya Agano la Kale yaani Isaya 42:1-3); na Mathayo 17:5 (wakati wa kugeuzwa kwa Yesu

**1:7“tunao”** kitenzi hiki kiko katika wakati uliopo wakati vitenzi vinavyozunguka vyote viko katika njeo ya wakati uliopita usio timilifu. Kwa sasa tuna miliki faida za vyote ambavyo Mungu amevitenda kupitia Yesu Kristo. Hata hivyo, angalia sentensi hiyohiyo ya Kiyunani (Waefeso 1:14) kwamba ukombozi ni wakati ujao. Wokovu unaanza na wito wa Mungu, kuomboleza kwa Roho Mtakatifu (kama vile Yohana 6:44, 65). Inatoa maamuzi ya imani/kutubu yakifuatiwa na maisha ya kusadiki, utii na ustahimilivu kwamba siku moja tutatimilizwa katika ukamilifu wa kufanana na Kristo (kama vile 1 Yoh 3:2). Wokovu ni uhusiano na pia matamko ya waziwazi, mtu na pia ujumbe.

**MADA MAALUM: VITENZI VYA NYAKATI VYA KIYUNANI**

Wokovu si zao, bali ni uhusiano na Mungu wa kila siku katika Kristo. Huu haukamilishwi wakati mtu anapomwamini Kristo; unaanza tu (mlango na kasha njia, kama vile Mt. 7:13-14)! Si sera ya bima ya moto, hata kibali cha kwenda mbinguni, bali maisha ya kuukulia ufanano wa Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15). Tunazo semi za kimithali humu Marekani ambazo zinanena kadri wenza wanavyozidi kuishi kuishi pamoja, ndivyo wanavyozidi kufanana. Hili ndilo kusudi la wokovu!

WOKOVU KAMA TENDO TIMILIFU (njeo)

- Matendo ya Mitume 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11 (unganisha njeo nay a wakati ujao)

WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (wakati timilifu)

- Waefeso 2:5,8

WOKOVU KAMA HALI ENDELEVU (wakati uliopo)

- 1 Wakorinhto 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

WOKOVU KAMA UTIMILIFU WA UJAO (wakati ujao katika njeo za vitenzi vya kiyunani au muktadha)

- Warumi 5:9,10; 10:9,13
- 1 Wakorintho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebrania 1:14; 9:28
- 1 Petro 1:5

Kwa hiyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani halisi (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13), lakini hili lazima linatolewa katika maisha ya imani (kama vile Rum. 8:29; Gal. 2:19-20; Efe. 1:4; 2:10), ambapo siku moja utataimizwa katika eneo hilo (kama vile 1 Yohana 3:2). Hii hali ya mwisho inaitwa kutukuza (kama vile Rum. 8:28-30). Hili linaweza kuelezwa kama

1. wokovu halisi – uthibitisho (kuokolewa kutoka adhabu ya dhambi)
2. wokovu endelevu – utakaso (kuokolewa kutoka nguvu yadhambi)

wokovu wa mwisho –kutukuza (kuokolewa katoka katika uwepowa dhambi)

▣**"ukombozi"** hii kwa dhahiri ni "kuokolewa kutoka" (kama vile Rum. 3:24; Kol. 1:14). Ni kisawe cha neno la Agano la Kale (*gaal*) "kununua kutoka" mara nyingine kunakuwa na usaidizi wa neno linalofanana (*go'el*). Neno hili lilitumika katika Agano la Kale kurejerea kununua tena watumwa na wafungwa wa kivita. Paulo anatumia maneno yanayofanana na Kiyunani mara nne katika Waefeso na wakolosai (kama vile Efeso 1:7, 14 and 4:30; Kol. 1:14). Inaaksi usaidizi binafsi ambao kwao Mungu huleta wokovu. Haiweki shabaha kwa nani au kwa kiwango gani cha malipo. Marko 10:45 inaelezea kwa uwazi kwamba Yesu alikuja kulipa fidia kwa mwanadamu aliyeanguka (kama vile 1 Petro 1:18-19). Wanadamu walikuwa watumwa kwa dhambi (kama vile Isaya 53:6; nukuu kadhaa za Agano la Kale katika Warumi 3:9-18; 1 Petro 2:24-25). Angalia Mada Maalum: Fidia/ukombozi katika Kol 1:14.

▣**"kupitia damu yake"** damu ni stiari kwa kifo (Mwanzo 9:4; Mambo ya Walawi 17:11). Hii inarejerea kifo cha dhabihu na mbadala cha Yesu. Alikufa kwa ajili yetu kwa dhambi yetu (kama vile Mwanzo 3:15; Isaya 53 Warumi 3:25; 5:9; 2 Kor. 5:21; Efe. 2:13; Kol. 1:20; Ebr. 9:22). Kwasababu ya uwepo wa walimu wa uongo (yaani Wajuzi) waliokataa ubinadamu wa Yesu, hii inawezekana ilikuwa njia ya kurejerea Yesu kama aliyekuwa mwanadamu kamili (damu, mwili, n.k)

▣**"msamaha"** Hii kwa dhairi ni "kutuma." Siku ya upatanisho kulikuwa na kafara mbili zilizohusika katika ibada ya mwaka za Walawi 16.

1. Moja ilikuwa inaachiwa, ikiwakilisha kuondolewa kwa dhambi ya Israeli (wakati Mungu anaposamehe, Mungu anasahau, kama vile Zaburi 103:12; Isaya 1:18; 38:17; 44:22; na Mika 7:18.
2. Ingine ilitolewa sadaka ikiashiria kwamba dhambi inagharimu maisha Yesu aliichukua dhambi ya mwanadamu kwa kufa kwa niaba yetu (kama vile 2 Kor. 5:21; Kol. 1:14) kwahiyo kuunganisha maana mbili.

▣**"makosa"** hili ni neno la Kiyunani kwa ajili ya dhambi (*paraptōma)* kidhahiri "kuanguka katika upande mmoja." Neno llijengwa kutumiwa kistiari juu ya tabia ya Mungu. Mungu ni kipimo ambacho wanadamu wote wana adhibiwa na kupotoshwa (kama vile Isaya 53:6; Rum. 3:9-23; 11:32; Gal. 3:22)

▣**"sawasawa na utajiri wa Neema yake"** msamaha wetu katika Kristo hauwezi kufanya kazi ili uupate (kama vile Waefeso 2:8-9; 2 Tim. 1:9; Tito 3:5). Neno "utajiri" linatumika mara nyingi katika barua za Paulo alipokuwa gerezani; "Waefeso 1:7; 2:7; "utajiri wa utukufu wake," Waefeso 1:18; 3:16; "tajiri katika rehema," waefeso 2:4 "utajiri katika Kristo," waefeso 3:8. Katika Kristo mwanadamu alikombolewa na kupewa utajiri wa sifa ya Mungu!

**1:8"alituzidishia"** Paulo anatumia neno hili (*perisseuō*) tena na tena (kama vile Rum. 5:15; 15:13; 1 Kor. 15:58; 2 Kor. 1:5; 8:2,7; 9:8; Efe. 1:8; Fil. 1:9; 4:12, 18; Kol. 2:7; 1 The. 4:1). Inaelezea namna ya Paulo ya kipimo kamili na zaidi cha neema ya Mungu na kukidhiwa katika Kristo. Upendo wa Mungu katika Kristo ni kama chemichemi inayotiririka au kisima cha Artesian.

**MADA MAALUM: UTELE (*perisseuō)***

Neno hili linatumiwa mara nyingi na Paulo. Hili linadokeza kile chenye kujaa hadi pomoni (yaani, maana chanya).

1. Kweli ya Mungu yenye kuzidisha utukufu wake, Rum. 3:7
2. Kipawa cha bure katika neema ile ya mwanadamu mmoja, Yesu Kristo, kilichozidi, Rum. 5:15
3. Waamini wazidi sana katika tumaini, Rum. 15:13
4. Waamini hawasifiwi mbele za Mungu kwa kula au kwa kutokula vyakula fulani, 1 Kor. 8:8 (kama vile Mko 7:15,17-23)
5. Waamini wazidi katika kulijenga kanisa, 1 Kor. 14:12
6. Waamini wazidi kutenda kazi ya Bwana, 1 Kor. 15:58
7. Waamini wanazidi kuyashiriki mateso ya Kristo na wanazidi katika kuipokea faraja ya Kristo, 2 Kor. 1:5
8. Huduma ya haki ina utukufu unaozidi, 2 Kor. 3:9
9. Shukrani ya waamini yapaswa kuzidi ili Mungu atukuzwe, 2 Kor. 4:15
10. Wingi wa furaha ya mwamini, 2 Kor. 8:2
11. Waamini wana wingi katika mambo yote (imani, usemi, elimu, na bidii yote, na upendo), pia katika neema kwa ajili ya kanisa la Yeresalemu, 2 Kor. 8:7
12. Wingi wa neema zote kwa waamini, 2 Kor. 9:8
13. Wingi wa shukrani za mwamini kwa Mungu, 2 Kor. 9:12
14. Utajiri wa neema ya Mungu unazidishwa kwa mwamini, Efe. 1:8
15. Pendo la waamini lizidi kuwa jingi sana, Efe. 1:9
16. Fahari ya waamini kuwa na Paulo katika Kristo, Flp. 1:26
17. Kuwa na wingi, Flp. 4:12,18
18. Waamini wakizidi katika shukrani, Kol. 2:7
19. Waamini wanaongezewa na kuzidishiwa katika upendo wao kwa wao, 1 The. 3:12
20. Kuzidi kuenenda katika kumpendeza Mungu, 1 The. 4:1
21. Kuzidi katika pendo na waaini wengine, 1 The. 4:10

Uelewa wa Paulo kuhusu neema ya Mungu katika Kristo ulikuwa "juu ya na zidi wastani," hivyo sana, unahitajika kwa waamini kuenenda katika juu ya na "zidisha wastani" neema na pendo katika maisha ya kila siku!

▣**"katika hekima yote na maarifa"** hii inarejerea karama ya Mungu ya uelewa (si maarifa ya siri wa wajuzi walimu wa uongo), ambayo alitoa ili kwamba mwanadamu apate uwezo wa kuelewa kile kinachomaanishwa na Injili (kama vile Waefeso 1:3, 4, 5, 6, 7, 9, 10 and 18-23; Luka 1:17; Kol. 1:9). Walimu wa uongo walisisitiza hekima za siri. Hekima ya Mungu ni Kristo. Anapatikana kwa wote!

**1:9"siri"** Paulo mara nyingi analitumia neno hili (kama vile Warumi 11:25 16:25; 1 Kor. 2:7; 4:1; Efe. 1:9; 3:3,4,9; 6:19; Kol. 1:26; 2:2; 4:3; 2 Tim. 1:9-10). Lina visawe kadhaa tofauti kwa ajili ya sehemu tofauti za mpango wa ukombozi wa Mungu. Katika Waefeso 2:11-3:13, inarejerea kuwaunganisha watu wote Wayahudi kwa Wayunani katika Kristo kwa Mungu. Hii ilikuwa mara nyingi mpango wa Mungu (kama vile Mwanzo 3:15; 12:1-3; Kutoka 19:4-6; Efe. 2:11-3:13). Hii ilikuwa kiashiria cha Mungu mmoja (mmoja na Mungu mmoja tu). Ukweli huu ulifichwa huko nyuma lakini kwasasa umefunuliwa kikamilifu katika Kristo. Angalia Mada maalum katika Waefeso 3:3

▣**"ya mapenzi yake"** angalia Mada Maalum inayofuata: Mapenzi ya Mungu

**MADA MAALUM: MAPENZI (*thelēma*) YA MUNGU**

"Mapenzi" ya Mungu yamejikita katika namna mbalimbali.

INJILI YA YOHANA

- Yesu alikuja kuyatenda mapenzi ya Baba yake (kama vile Yohana 4:34; 5:30; 6:38)
- Kuwafufua siku ya mwisho wale wote Baba aliowampa Mwana (kama vile Yohana 6:39)
- Kwamba wote waamini katika Mwana (kama vile Yn 6:29; 40)
- Maombi yaliyojibiwa kuhusiana na kuyatenda mapenzi ya Mungu (kama vileYn 9:31 na Yn 5:14)

VODOKEZO VYA INJILI

- Kuyatenda mapenzi ya Mungu ni jambo la muhimu (kama vile. Mt. 7:21)
- Kuyatenda mapenzi ya Mungu hutufanya kuwa kaka na dada pamoja na Yesu (kama vile Mt. 12:50; Marko 3:35)
- Sio mapenzi ya Mungu kwa yeyote kuangamia (kama vile Mt.18:14; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9)
- Kalvari ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Yesu (kama vile Mt. 26:42; Luka 22:42)

NYARAKA ZA PAULO

- ukomavu na huduma ya waamini wote (kama vile Rum. 12:1-2)
- waamini waliondolewa kutoka katika enzi hii ya maovu (kama vile Gal. 1:4)
- mapenzi ya mungu ulikuwa ni mpango wake wa ukombozi (kama vile Efe.1:5, 9,15)
- waamini wanapitia na kuishi maisha yaliyojazwa na Roho (kama vile Efe. 5:17-18)
- waamini wamejazwa na maarifa ya Mungu (kama vile Kol. 1:9)
- waamini wanafanywa kuwa imara na wakamilifu (Kol. 4:12)
- waamini wanatakaswa (cf. 1The. 4:3)
- waamini watoa shukrani katika vitu vyote (kama vile The.5:18)

NYARAKA ZA PETRO

- Waamini wanatenda haki (yaani, kunyenyekea kwenye mamlaka ya chini) na, kwa hiyo wanawanyamazisha watu wajinga, hivyo kuwapa fursa kwa kuijua injili/matendo mema (kama vile 1Pet. 2:15)
- Mateso ya waamini (kama vile 1 Pet. 3:17; 4:19)
- Waamini hawapaswi kuishi maisha ya ubinafsi (kama vile 1 Pet. 4:2)

NYARAKA ZA YOHANA

- waamini kuendelea kudumu milele (kama vile Yohana 2:17)
- waamini ni kielelezo kwa maombi yaliyojibiwa (kama vile 1 Yohana 5:14)

**1:10**
**NASB "utawala"**
**NKJV "mgao"**
**NRSV "mpango"**
**TEV "mpango huu"**
**NJB "kwa yeye kutenda kazi"**

Hii kwa dhahiri ni "uwakili wa nyumbani" (*oinokomia*). Paulo anatumia neno hili mara kadhaa katika sentensi mbalimbali katika namna tofauti.

1. Agizo la kitume ka kuihubili Injili (kama vile 1 Kor. 9:17; Efe. 3:2; Kol. 1:25)
2. Mpango wa milele wa ukombozi, "siri" (kama vile Efe. 1:9-10; 3:9, 1 Kor. 4:1)Mafunzo katika mpango wa ukombozi na mtindo wa maisha unaofanana nao (kama vile 1 Timotheo 1:4)
3. Mstari huu ni kivuli cha mbele cha maudhui makuu ya kitabu (umoja wa vitu vyote katika Kristo) ambayo tayari kimeshakuzwa kwa ukamilifu katika Waefeso 4:1-6.

▣**"ukamilifu wa nyakati"** tungo hii inatilia mkazo (kama ambavyo hufanya unabii wa mbele) kwamba Mungu yeye hushughulikia historia. Na kwa wakati sahihi Mungu alimtuma Kristo kwa wakati sahihi, Atakuja tena.

▣**"akijumlisha vitu vyote katika Kristo"** Katika Kiyunani cha Koine (lugha ya biashara katika ulimwengu wa Mediteranian katika ya 200 K.K mpaka 200 B.K, ilikuwa ni lugha ya watu wa kawaida) hili neno ambatani ni dhahiri "kuunganisha vitu kadhaa vingi chini ya kichwa kimoja." Hii ni rejea kwa umuhimu wa ulimwengu wa kazi ya Kristo

(kama inavyoonekana kwa uwazi katika 1 Wakorintho 15:24-28 na Kol. 1:17-22). Hii ni maudhui kuu katika kitabu cha Wakolosai. Kristo ni kichwa sio tu kwa mwili wake, kanisa bali kwa uumbaji *(kosmos).*

**1:11**
**NASB, NKJV,**
**NRSV "tumepata urithi"**
**TEV "Mungu alituchagua sisi kuwa watu wake"**
**NJB "tumepata urithi wetu'**

Hii kwa dhahiri "tulichaguliwa kama urithi," kauli tendwa elekezi ya wakati usio timilifu. Kwa asili katika Agano la Kale hii ilimaanisha Walawi tu (kabila la Walawi, watumishi wa hekaluni, walimu wa nyumbani wa sheria), ambao hawakurithi ardhi ya Nchi ya Ahadi (Hesabu 18:20; Kumb. 10:9; 12:12; 14:27,29). Walipokea Majiji kadhaa, Yoshua 20-21. Ilikuja kurejerea kweli ambayo Mungu mwenyewe ni urithi wa waaminio wote na ni wake Mungu (kama vile Zaburi 16:5; 73:26; 119:57; Maombolezo 3:24). Na pia ilikuja kuwa stiari kwa watu wa Mungu (kama vile Kumb. 4:20; 7:6; 9:26,29; 14:2; 2 Sam. 21:3; 1 Wafalme 8:51,53; 2 Wafalme 21:14; Zaburi 28:9; 33:12; 68:9; 78:62,71; 94:14; 106:5,40; Isaya 19:25; 47:6; 63:17; Yeremia 10:16; 51:19). Agano Jipya linachukua mbadala wa ahadi ya ardhi kwa ahadi ya kuwa sehemu ya familia ya Mungu. Waandishi wa Agano Jipya wanaweka kiulimwengu utofauti wa Wayahudi-Mataifa kwenda katika mfano wa waaminio na wasioamini. Hiyo kweli ni sawa kwa Mji wa Yerusalemu ambao unakuwa Mji Mpya wa Yerusalemu (kama vile Ufunuo 3:12; 21:2,10), hii ni stiari ya mbinguni na sio kioneshi cha kijiografia.

▣**"tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye"** hii kauli tendwa ya endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu inayoelezea ukweli kwamba uchaguzi ni sawasawa na neema ya Mungu na siokwa vigezo vya kibinadamu (kama vile Waefeso 2:8-9, ambayo ina kanusho; "ambayo si kwa ajili yetu;" "ni karama ya Mungu," na "haitokani na matendo, asije mtu akajivuna"). Msamiati huu huu unapatikana katika Warumi 8:28-29. Kusudi lililopo ni kufanana na Kristo. Angalia maelezo kamili kuhusu Kuamriwa kabla katika maarifa ya kimuktadha kwa 1:1-23, 3c na 1:4 na 1:5.

**MADA MAALUM: Uchaguzi/Kuamriwa kabla na uhitaji wa uwiano wa ulali wa kithiolojia**

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile.Warumi10:11,13).

Umuhimu wa huu muvatano wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!

Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu
2. . Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. DHAMBI YA ASILI DHIDI YA DHAMBI YA HIARI
4. KUTOTENDA DHAMBI DHIDI YA KUTENDA DHAMBI KIDOGO
5. UDHIHILISHO NA UTAKASO WA PAPO KWA PAPO DHIDI YA UTAKASO ENDELEVU
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye

10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhumu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kitheolojiaya "agano" inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu(k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maanddishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maeneo na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa theolojia!

**1:12"sisi"** hii inarejerea Wayahudi waaminio (kama vile Rum. 1:16).

▣**"utukufu"** angalia maelezo zaidi katika Waefeso 1:6

**1:13"ninyi"** hii inarejerea Mataifa waaminio (Waefeso 2:12)

▣**" huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu…….mmekwisha kumwamini"** Hizi kauli zote ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu. Wokovu ni vyote ujumbe wa kuamini na mtu wa kusadiki. Inahusisha vyote kukubali kiakili kwa uaminifu wa kibiblia (mtizamo wa kiulimwengu) na ukaribisho wa kibinafsi wa Yesu! Injili lazima ipokelewe kibinafsi (kama vile Yohana 1:12; 3:16, 18, 36; 6:40; 11:25-26; Rum. 10:9-13). Umuhimu wa injili unaweza kufanyiwa muhtasari ufuatao kama

1. Mtu wa kumkaribisha /kumpokea (uhusiano wa kibinafsi)
2. Kweli kuhusu mtu wa kumwamini (mtizamo wa kiulimwengu)
3. Maisha kama mtu wa kuishi (kufanana na Kristo)

**MADA MAALUM:"KWELI" KATIKA MAANDIKO YA PAULO**

Katika maana hii Yohana anaunganisha historia ya nyuma ya Waebrania na Wayunani ya neno alētheia yaani "ukweli" kama alivyofanya kwenye neno *logos* (kama vile 1:1-14). Waebrania (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika Agano la Kale) ikidokezwa hivyo ambavyo ni kweli, au uaminifu (mara nyingi linahusianishwa na maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno pisteuō). Katika Kiyunani lilihusianishwa na ukweli wa Pilato dhidi uongo; mambo ya kimbingu dhidi ya kidunia. Hili linakaa sawa kuhusiana na uwili wa Yohana. Mungu kwa uwazi ameridhihilisha hili (maana na asili ya neno alētheia ni kuweka wazi, kutokuficha, kudhihilisha wazi) Yeye mwenyewe katika Mwana. Hili limeelezewa katika njia tofauti.

1. Nomino, alētheia, kweli
   a. Yesu amejaa neema na kweli ya kutosha (kama vile Yohana 1:14,17 – maneno ya patano katika Agano la Kale)
   b. Yesu ndiye alikuwa mlengwa kwenye ushuhuda wa Yohana Mbatizaji (cf. Yohana 1:32-34; 18:37 – nabii wa mwisho wa Agano la Kale)
   c. Yesu anaongea ukweli (kama vile Yn 8:40,44,45,46 – ufunuo ni fumbo na kitu binafsi)
   d. Yesu ni njia, kweli, na uzima (kama vile Yohana 14:6)
   e. Yesu anawatakasa katika kweli (kama vileYohana 17:17)
   f. Yesu (neno Logos, 1:1-3) ni kweli (kama vile Yohana 17:17)
2. Kivumishi, *alēthēs*, kweli, uaminifu
   a. Ushuhuda wa Yesu (kama vile Yohana 5:31-32; 7:18; 8:13-14)
   b. Hukumu ya Yesu (kama vile Yohana 8:16)
3. Kivumishi, *alēthinus*, kweli
   a. Yesu ni nuru ya kweli (kama vile Yohana 1:9)
   b. Yesu ni mkate wa kweli (kama vile Yohana 6:32)
   c. Yesu ni mzabibu wa kweli (kama vile Yohana 15:1)
   d. Yesu ni shuhuda wa kweli (kama vile Yohana 19:35)
4. Kielezi, *alēthōs*, hakika
   a. Msamalia mwema anamshuhudia Yesu kama mwokozi wa ulimwengu (kama vile Yohana 4:42)

b. Yesu ni chakula na kinywaji cha kweli, kama chakula cha manna kilivyopingwa katika siku za Musa (kama vile Yohana 6:55)

Neno ukweli na unyumbulisho wake pia unaelezea ushuhuda mwingine wa Yesu, kwa neno *alēthēs*

a. Ushuhuda wa Yohana Mbatizaji ni wa kweli (kama vileYohana 10:41)
b. Ushuhuda wa Yohana (mwandishi wa Injili) ni wa kweli (kama vile Yohana 19:35; 21:24)
c. Yesu anaonekana kama nabii wa kweli (kama vileYohana 6:14; 7:40)

Kwa mazungumzo mazuri kuhusu ukweli katika Agano la Kale angalia George E. *Ladd's A Theology of the New Testament*, kur.263-269

▣**”na kutiwa muhuri katika yeye”** katika tamaduni za kipindi kati ya Wagiriki na Warumi kutia muhuri ilikuwa ni ishara ya usalama, ukweli na umiliki (kama vile Efe. 4:30; 2 Kor. 1:22; 5:5; Ufunuo 7:1-4). Kutiwa muhuri (kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu) ni usambamba wa kithiolojia wa ubatizo wa Roho wa waamini wapya katika Kristo (kama vile 1 Kor. 12:13; yawezekana Efe. 4:4-5).

**MADA MAALUM: MUHURI**

Muhuri au lakiri yawezakuwa ni njia ya kale ya kuonyesha

1. Ukweli (kama vile Yohana 3:33)
2. Umiliki (kama vile Yohana 6:27; 2 Tim. 2:19; Ufu.. 7:2-3; 9:4)
3. Ulinzi (kama vile Mwa. 4:15; Mt. 27:66; Rum. 4:11; 15:28; 2 Kor. 1:22; Efe. 1:13; 4:30; Ufu. 20:3)
4. Yawezakuwa pia ni dalili za ukweli wa ahadi ya Mungu (kama vile Rum. 4:11 and 1 Kor. 9:2)

Kusudi la muhuri huu katika Ufunuo 7:2-4; 9:4 ni kuwatambua watu wa Mungu ili kwamba ghathabu ya Mungu isiwadhuru. Muhuri wa shetani pia huwatambua walio wake, wale walio chombo cha ghathabu ya Mungu. Katika kitabu cha Ufunuo “dhiki kuu” (yaani., *thlipsis)* mara zote inarejerea wasio waumini wakiwatesa waumini, wakati ghathabu/hasira (yaani., *orgē* or *thumos*) mara zote huwa ni hukumu ya Mungu juu ya wale wasioamini ili kwamba wapate kutubu na kuirudia imani katika Kristo. Kusudi hili chanya la hukumu laweza kuonekana katika agano la laana/Baraka katika kitabu cha Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 27-28;30; Zaburi 1

▣**”na Roho yule wa ahadi”** kuja kwa Roho kulikuwa na ishara ya zama mpya (kama vile Yoeli 2:28; Yohana 14:26 na kuendelea). Alikuwa ni ahadi ya Baba (kama vile Yohana 14:16, 26; 15:26; Mdo. 1:4-5; 2:33). Roho akaaye ndani ya waamini ni hakika ya ufufuo wao (kama vile Warumi 8:9-11).

**1:14”atolewaye kama ahadi”** hii dhana ya ahadi inaonekana kwanza katika Agano la Kale

1. Ahadi ya kulipa deni(kama vile Mwanzo 38:17,18,20; Kumbukumbu la Torati 24:10-13)
2. Ahadi ya kutoa utoshelevu (kama vile 1 Samweli 17:18)
3. Ahadi binafsi (kama vile 2 Wafalme 18:23; Isaya 36:8).

Neno la Kiyunani linarejerea “malipo ya awali” au fedha kwa ajili ya kupata kibali (kama vile 2 Wakorintho 1: 22; 5:5) katika Kiyunani cha kisasa inatumika kama pete ya uchumba ambayo ni ahadi ya ndoa ijayo. Roho ni ahadi iliyotimizwa ya nyakati mpya ya haki. Hii ni sehemu ya “utayari” na “bado” uvutano wa Agano Jipya ambacho kuna mpishano wa nyakati mbili za Kiyahudi kwasababu ya kuja kwa Kristo (angalia mjadala mzuri katika *Howto Read the Bible for All Its Worth* na Fee and Stuart, ukurasa wa 129-134). Roho ni ahadi iliyotolewa sasa kwa ajili ya kutimilizwa kwa badaye.

**MADA MAALUM: HULKA YA ROHO**

Kwenye Agano la Kale “Roho wa Mungu” (yaani *ruach*) ilikuwa nguvu iliyotimiza kusudi la YHWH, lakini kuna kidokezo kwamba alikuwa mtu binafsi (yaani Mungu mmoja, tazama Mada Maalumu: U-Mungu mmoja). Hata hivyo kwenye Agano Jipya ukamilifu wa nafsi ya ubinadamu na utu wa Roho umefunuliwa:

1. Anaweza kufanyiwa kufuru (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Hufundisha (kama vile. Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Hushuhudia (kama vile Yohana 15:26)
4. Ana hukumu, anaongoza (kama vile Yohana 16:7-15)

5. Anaitwa “ambaye" (yaani, *hos*, kama vile Efe 1:14)
6. Anaweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anaweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)
8. Anaweza kupingwa (kama vile Matendo 7:51)
9. Anawatetea waaminio (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)
10. Humtukuza Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya utatu (hapa yapo matatu mioongoni mwa mengi, tazama Mada Maalumu: Utatu) pia anazungumza juu ya watu watatu.

1. Mt. 28:19
2. 2 Kor. 13:14
3. 1 Pet. 1:2

Ingawa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni sio na jinsi wakati linapohusika Roho, Agano Jipya kila mara hutumia KIVUMISHI KIONYESHI CHA JINSIA YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho anahusishwa na shughuli za binadamu.

1. Matendo 15:28
2. Rum. 8:26
3. 1 Kor. 12:11
4. Efe. 4:30

Mwanzoni kabisa mwa matendo, jukumu la roho lina sisitizwa (kama katika injili ya Yohana). Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali, sura mpya. Yesu kila wakati alikuwa na Roho. Ubatizo wake haukuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali mwanzo wa sura mpya. Roho ndio njia yenye nguvu ya makusudi ya Baba kwa sura yake (tazama Mada Maalumu:Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)!

▣**” ukombozi”** angalia ukumbusho katika Waefeso na Mada Maalum katika Kol. 1:14

▣**”watu wa milki ya Mungu”** haya yanaweza yakawa ni maelezo kwa Kutoka 19:5; Kumbukumbu la Torati 7:6; 14:2. Wayahudi walikuwa watu maalum wa thamani wa Mungu kwa kusudi la kuwafikia ulimwengu (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:6), sasa Wakala wake ni kanisa, mwili wa Kristo.

▣**”kwa sifa ya Utukufu wake”** angalia Waefeso 1:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 1:15-23**
**15 Kwa sababu hiyo mimi nami, tangu nilipopata habari za imani yenu katika Bwana Yesu, na pendo lenu kwa watakatifu wote, 16 siachi kutoa shukrani kwa ajili yenu; nikiwakumbuka katika sala zangu, 17 Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye; 18 macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; 19 na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; 20 aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; 21 juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; 22 akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo 23 ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.**

**1:15-23** haya ni maombi ya Paulo ya shukurani na maombezi juu ya wapokeaji (yaani makanisa ya Asia ndogo). Ni sentenzi moja ndefu ya Kiyunani kama ilivyo Waefeso 1:3-14 (yaani maombi ya Paulo ya sifa kwa Mungu baba kwa ajili ya karama yake ya neema ya Kristo na Roho). Sentensi hizi ndefu ni tabia ya staili ya uandishi ya Paulo kwa Waefeso tu (kama vile Waefeso 1:3-14, 15-23; 2:1-10, 14-18, 19-22; 3:1-12,14-19; 4:11-16; 6:13-20). Pia angalia maombi ya Paulo kwake yeye mwenyewe katika Waefeso 6:19-20! Paulo alikuwa mtu wa Maombi na sifa (yaani 3:20-21).

**1:15**
**NASB "imani….kati yenu"**
**NKJV, NRSV**
**TEV, NJB "imani yako"**

Waefeso kwa kuwa barua ya wengi inaonesha kuwa Paulo anarejerea makanisa kadhaa, na sio tu makanisa katika Efeso. Alikuwa amesikia matatizo ya makanisa katika bonde la Lycus (Laodikia, Hierapoli na Kolosai) kupitia Epafra (kama vile Kol. 1:6-8).
Neno "imani" linarejerea kwa
1. Imani ya kwanza ya mtu katika Kristo (kama vile Waefeso 1:19 "kuelekea sisi tulioamini"
2. Maisha yanayoendelea ya uaminifu ya wakristo (yaani namna ya Agano la Kale ya Kol. 1:9-10)
3. Mafundisho ya Wakristo "imani," ikiwa na kibainishi cha wazi, (kama vile Mdo. 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 6:10; Yuda 3, 20)

Hapa lina kibainishi na yawezekana mbadala wa #3 ni bora

▣**"upendo wako"** haya sio maandiko ya Kiyunani ya Kale P[46], א, A, au B, wala maandiko ya Kiyunani yaliyotumika kwa Origen, Jerome, au Augustine lakini inajitokeza katika usambamba wa Wakolosai (kama vile Waefeso 1:4) na Filemoni 1: 5. Ni wazi kuna nyongeza ya kimaandiko hapa katika Waefeso. Walijifanya kuweka kiwango cha tungo ya Paulo.

▣**"watakatifu"** angalia Mada Maalum: Watakatifu katika Kol. 1:2.

**1:16** mstari huu unafuua sehemu mbili za maisha ya Paulo ya Maombi; (1) shukrani na (2) ustahimilivu. Paulo kwa mwendelezo aliendelea kuwaombea makanisa yote ya Kristo (kama vile Warumi 1:9; 2 Kor. 11:28; Fil. 1:3-4; Kol. 1:3,9 ; 1 The. 1:2-3; 2 Tim. 1:3, Filemon 4).
Huu ni uwiano mzuri wa kithiolojia kati ya kumwamini Mungu na maisha maombezi. Tamko la injili na ukuaji wa makanisa ilikuwa ni mapenzi ya mungu. Bado Paulo alihisi kuna hitaji la kuendelea kuwaombea. Kwa namna fulani maombi ya waamini yanaachilia nguvu ya Mungu ya wakati muafaka na njia mpya. Mungu mwenye mamlaka yote alichagua mwenyewe kujiwekea mpaka yeye mwenyewe kwa maombi ya watu wake (kama vile Yakobo 4:2)! Maombi ya maombezi ni siri ya nguvu ya Mungu inayowaunganisha maombi ya hiari ya waaminio. Angalia Mada Maalum katika Shukrani katika Kol. 4:2. Angalia Mada Maalum:Maombi ya Maombezi katika Kol. 4:3.

**1:17**
**NASB, NRSV**
**NJB "Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya"**
**NKJV "Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya"**
**TEV "Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba mwenye utukufu, awape ninyi roho"**

Angalia msisitizo katika utatu unaoonekana katika fasiri ya TEV ya (1) Waefeso 1:3-14; (2) Waefeso 1:17; (3) Waefeso 2:18; (4) Waefeso 3:14-17 na (5) Waefeso 4:4-6. Angalia Mada Maalum: Utatu katika Waefeso 1:3.

▣**"Baba wa utukufu"** Huu ulikuwa ni wadhifa wa Agano la Kale la Mungu (kama vile Zaburi 24:7; 29;3; Mdo. 7:2). Kirekebishi kimilikishi (ya utukufu) pia inatumika na Yesu katika 1 Kor 2:8 na Yakobo 2:1. Maombi ya Paulo ni kwamba YHWH itatoa haya kwa waamini wapya ufahamu na uelewa kamili wa hekima iliyoko katika Yesu Kristo, sio hekima ya uongo ya kiakili ya walimu wa uongo. Hakuna hekima ya siri. Yesu ni hekima ya Mungu ambaye kwa ukamilifu anamfunua Yeye! Angalia ukumbusho kamili kuhusu "utukufu katika Waefeso 1:6.

▣**"awapeni ninyi roho"** neno "roho" (hakuna kibainishi cha wazi) lakini kinafanya kazi ya kusudi mara mbili ya kurejerea roho ya binadamu inayotiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Isaya 11:2 inafunua karama ya Mungu ya Roho kama "roho ya hekima," na "uelewa," "roho ya mashauriano," na "nguvu," "roho ya maarifa," na "hofu ya

Mungu." Katika Agano Jipya kuna mfululizo wa vifungu vya habari vinavyofunua nini ambacho Roho anazalisha katika maisha ya waamini.

1. "roho ya utakatifu," Warumi 1:4
2. "roho ya kufanya wana," Warumi 8:15
3. "roho ya upole," 1 Kor.4:21
4. "roho ya imani," 2 Kor.4:13
5. "roho ya hekima na ufunuo," Waefeso 1:17
6. "roho ya kweli," dhidi ya "roho ya ukosaji," 1 Yoh. 4:6

▣**"ya hekima na ufunuo katika kumjua Yeye"** viwakilishi katika aya vinarejerea Mungu baba kama vingi vyao vifanyavyo katika Waefeso 1:3-14. Hekima hii na ufunuo ilikuwa si kwa baadhi lakini kwa waamini wote (kama vile Waefeso 4:13). Hii ilitumika kukanusha uwezo wa akili na msisitizo wa kuweka kando kwa walimu wa uongo. Maarifa ya Injili yanatolewa na Mungu na yana shabaha ya Yesu (kama vile Kol. 1:9). Yeye ni kweli (kama vile Yohana 8:32; 14:6)!

**1:18-19** Maarifa ya Mungu kwa utoaji wa Baba katika Kristo unajumuisha sehemu tatu

1. Tumaini lililoamriwa la waaminio
2. Urithi wenye utukufu wa waaminio
3. Ufahamu wa nguvu ya Mungu ipitayo kawaida ya waamini unaodhihirishwa katika Kristo.

**1:18"macho ya mioyo yenu yatiwe nuru"** hii ni sitiari ya injili inayoleta ufahamu kwa mwanadamu aliyeanguka (Mdo. 26:18; 2 Kor. 4:4-6). Hii imekuwa ni mapenzi ya Mungu. Angalia Mada Maalum: Moyo katika Kol. 2:2

▣**"tumaini la mwito wake"** kwa ajili ya maelezo kamili kuhusu "tumaini" angalia Mada Maalum katika Kol. 1:5
Neno "wito" (*kaleō)* inatumika katika namna za kithiolojia za Agano la Kale

1. Wenye dhambi wanaitwa na Mungu kupitia Kristo kwa wokovu
2. Wito wa Mungu kwa jina la Bwana kuokolewa
3. Waaminio wanaitwa kuishi maisha ya kufanana na Kristo
4. Waaminio wanaitwa kwa kazi ya huduma

Mchocheo wa andiko hili ni #1. Kwa "wito" angalia Mada Maalum katika Waefeso 4:1

▣**"utajiri wa utukufu wake"** Paulo mama nyingi anazungumzia kweli za Injili kama "utajiri" kama vile Waefeso 1:7, 18; 2:4,7; 3:8,16). Angalia maelezo katika Waefeso 1:7

▣**"urithi"** angalia maelezo kamili katika Waefeso 1:11

**1:19**
**NASB "ukuu uzidio"**
**NKJV "ukuu upitao wote"**
**NRSV "ukuu unaopita kipimo"**
**TEV "ukuu wa namna gani"**
**NJB "ukuu wa namna gani upitao kiwango"**

Neno hili *huperballō* linatumika tu na Paulo katika Agano Jipya. Inaelezea hisia za furaha yao iliyopitiliza za vile ambavyo Mungu ametenda kupitia Kristo kwa ukaidi wa binadamu katika ukombozi (kama vile 2 Kor. 3:10; 9:14; Efe. 1:19; 2:7; 3:19).

**MADA MAALUM: MATUMIZI YA PAULO YA YA NENO AMBATANI*"HUPER"***

Paulo alikuwa na upendeleo binafsi kwa ajili ya kuyaumba maneno mapya kwa kutumia KIWAKILISHI cha Kiyunani *huper*, ambacho kimsingi kinamaanisha "juu ya" ama "kuu." Hiki kilipotumika pamoja na KIMILIKISHI

( CHA KUONDOA) kilimaanisha "badala ya" Pia kinaweza kumaanisha "karibia na" au "kuhusiana na" kama *peri* (kama vile 2 Kor. 8:23; 2 The. 2:18). Hiki kikitumika pamoja na HALI YA KUSHUTUMU kinamaanisha "kuzidisha wastani," "juu ya," au "zaidi ya" (kama vile A. T. Robertson, *A Grammar of the Greek New Testament in the Light of Historical Research*, kr. 625-633). Wakati Paulo alipotaka kutia mkazo alitumia KIWAKILISHI katika uambatani. Ifuatayo ni orodha ya matumizi maalum ya Paulo ya KIWAKILISHI hiki katika uambatani.

A. Hapax legomenon (kimetumika mara moja katia Agano Jipya pekee)
   1. *Huperakmos*, mmoja wa maisha kwanza yaliyopita, 1 Kor. 7:36
   2. *Huperauxanō*, kuongezeka sana, 2 The. 1:3
   3. *Huperbainō*, kupunja ama kukosa, 1 The. 4:6
   4. *Huperkeina*, mbele ya, 2 Kor. 10:16
   5. *Huperekteina*, kupita kadri, 2 Kor. 10:14
   6. *Huperentugchanō*, kuomba kwa kuugua, Rum. 8:26
   7. *Hupernikaō,* tunashinda tena zaidi ya kushinda, Rum. 8:37
   8. *Huperpleonazō*, kuwa katika hali ya kuzidi sana, 1 Tim. 1:14
   9. *Huperupsoō*, kuadhimisha mno, Flp. 2:9
   10. *Huperphroneō*, kunii yaliyo makuu, Rum. 12:3

B. Maneno yaliyotumika katika maandiko ya Paulo pekee.
   1. *Huperairomai*, kujivuna kwa mtu mwenyewe, 2 Kor. 12:7; 2 The. 2:4
   2. *Huperballontōs*, zaidi ya kipimo, kupita kiasi, 2 Kor. 11:2 (KIVUMISHI kiko hapa tu, lakini KITENZI ki katika 2 kor. 3:10; 9:14; Efe. 1:19; 2:7; 3:19)
   3. *Huperbolē*, kuzidi zaidi, kujilinda kuliko pitiliza, Rum. 7:13; 1 Kor. 12:31; 2 Kor. 1:8; 4:7,17; 12:7; Gal. 1:1
   4. *Huperekperissou*, zaidi ya vipimo vyote, Efe. 3:20; 1 The. 3:10; 5:13
   5. *Huperlian*, katika kiwango cha juu ama kuzidi wengine, 2 Kor. 11:5; 12:11
   6. *Huperochē*, maarufu, bora, 1 K. 2:1; 1 Tim. 2:2
   7. *Huperperisseuō*, kuzidi zaidi, Rum. 5:20 (KAULI YA KATI, to ninaujasiri mwingi, kupita kiasi, 2 Kor. 7:4)

C. Maneno yaliyotumiwa na Paulo na yaliyo haba katika waandishi wengine wa Agano Jipya
   1. *Huperanō*, juu sana, Efe. 1:21; 4:10; na Ebr. 9:5
   2. *Huperechō*, maarufu, bora, Rum. 13:1; Flp. 2:3; 3:8; 4:7; 1 Pet. 2:13
   3. *Huperēphanos*, kusingizia au majivuno, Rum. 1:30; 2 Tim. 3:2 na Luka 1:51; Yakobo 4:6; 1 Pet. 5:5.

Paulo alikuwa mtu wa hisia kali; wakati mambo au watu walipokuwa wema, walikuwa wazuri sana na walipokuwa wabaya walikuwa wabaya sana. KIWAKILISHI hiki kilimruhusu kueleza hisia zake zilizozidi kuihusu dhambi, mwenyewe, na Kristo na Injili.

▣**"kwetu sisi tunaoamini"** tungo hii inaonesha uongo wa fundisho la "imani ya kiulimwengu" ambayo inadai kwamba hatimaye watu wote wataokolewa. Fundisho hili mara nyingi linajikita katika uhakiki wa maandiko katika vifungu vyenye kujitenga kama Warumi 5:18. Mungu amechagua kuruhusu binadamu kushiriki (agano lenye masharti) katika wokovu wao wa kiroho na kuhiji. Wakristo lazima watubu na kuamini (kama vile Marko 1:15; Mdo 3:16,19; 20:21). Ujumuishaji wa Injili (kama vile Yohana 1:12; 3:16; 1 Tim. 2:4-6; Tito 2:11; 1 Petro 3:9) ilikuwa na mvutano kwa kujitenga kwa walimu wa uongo. Injili ni mwaliko wa kiulimwengu (kama vile 1 Tim. 2:4; Tito 2:11; 2 Petro 3:9) kwa wote watakaomwita kwa jina la Bwana (kama vile Rum. 10:9-13).

▣**"kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake"** hii inawezekana ikawa ni maelezo kwa Isaya 11:2 (kama vile Waefeso 1:17). Hii tungo inaundwa na maneno matatu (*energas*, *kratos*, and *ischus)* ambayo inaonesha nguvu ya Mungu. Neno la nne kwa ajili ya nguvu (*dunamis*) inatumika mapema katika mstari huu. Shabaha ya wokovu ni matendo makuu ya Mungu kupitia Kristo na sio matendo ya kibinadamu ya mtu mmoja mmoja au dhana za kiakili.
**1:20** tungo tatu zijazo zinafunua nini ambacho Baba kwa nguvu za uweza wake amefanya kwa Yesu

1. “Alimfufua katika wafu” Waefeso 1:20. Hii ilikuwa ni ishara ya sadaka yake kupokelewa (kama vile 1 Wakorintho 15).
2. “Alimkalisha katika Mkono Wake wa Kuume,” Waefeso 1:20. Hii ilikuwa ni sehemu ya kuinuliwa na kuweko katika mamlaka (kama vile Kol. 3:1). Hii iliwakilisha huduma ya maombezi ya Kristo inayoendelea (kama vile Rum. 8:34; Ebr. 7:25; 9:24; 1 Yohana 2:1 na ilikuwa ni kutimilizwa kwa unabii wa Agano la Kale, kama vile Zab. 110:1; Mdo. 7:56).
3. “Alimfanya kuwa juu kimalmala na kuwa kichwa cha kanisa,” Waefeso 1:22. Matumizi haya ya neno kanisa inarejerea upekee wa watu wapya wa Mungu ambao wanajumuisha wote wanaoamini, wote Wayahudi na Mataifa (kama vile Waefeso 2:11-3:13; Wagalatia 3:27-29).

Vitu ambavyo Baba amefanya kwa Kristo, Kristo amefanya kwa wafuasi wake (kama vile Waefeso 2:5-6). Maneno yote matatu katika Waefeso 2:5-6 ni ambatani pamoja na vioneshi *syn* vinavyomaanisha “ushirika wa pamoja na.”

▣**“katika ulimwengu wa roho”** Hiki kioneshi cha mahali (tufe) hasi cha kivumishi cha wingi (*epouranious*) kinatumika tu katika Waefeso (kama vile Waefeso 1:3, 20; 2:6; 3:10; 6:12). Kutoka katika muktadha wa matumizi yake yote lazima imaanishe ulimwengu wa roho ambamo waaminio wanaishi kwa sasa, na sio mbinguni.

**1:21 “juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu”** tungo hii inaweza kumaanisha vyeo au ngazi na mpangilio ya mguvu za kiroho au viwango vya kimalaika ambavyo ni katili kwa binadamu (kama vile waefeso 2:2 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:10,15; Rum. 8:38-39; 1 Kor. 15:24). Yesu yuko juu ya vyeo vyote vya kimalaika (kama vile Ebr. 1-2). Hii ilikanusha msisitizo katika vyeo vya kimalaika *(aeons)* vilivyokuwa vikisisitizwa sana na wajuzi wa walimu wa uongo. Vyeo hivi pia vinaweza vikaashiria miundo isiyo ya kibinafsi katika ulimwengu wetu ambayo inaruhusu wanadamu kufanya kazi mbali na Mungu. Mfano ni Falsafa, elimu, serikali, madawa, dini, n.k (kama vile Hendrik Berkhof's *Christ and the Powers*, Herald Press). Angalia Mada Maalum:Malaika katika Maandiko ya Paulo katika Waefeso 6:12. Zaidi, kwa “kuzidi sana” angalia Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya *Huper* ambatani katika Waefeso 1:19. Kwa ajili ya “Mamlaka” angalia Mada Maalum: *Archē* katika Kol. 1:16

▣**“na kila jina litajwalo”** hii inaweza kumaanisha siri za walimu wa uongo au majina yanayotumiwa kupita katika anga la kimalaika.walikuwa wakitumainia maarifa yao ya siri ya majina ya kimiujiza kuleta wokovu. Paulo anaelezea kuwa wokovu au ushirika pamoja na Mungu vinapatikana tu katika Jina la Yesu (Wafilipi 2:9-11). Katika Agano la Kale, jina la mtu liliwakilisha tabia yake. Tabia ya Baba inadhihirishwa kwa ukamilifu katika Mwana (kama vile Yoh. 14:8-14; 17:11).

▣**“wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia”** Wayahudi waliamini katika nyakati mbili, wakati wa sasa wa uovu na nyakati mpya ya haki ambayo ingekuja kupitia Masihi. Huu wakati mpya wa haki wa Roho ulikuja wakati wa Pentekoste! (kama vile Yoeli 2:28-32; Mathayo 12:32, Marko 10:30; Luka 16:8; 18:30; 20:34; 1 Tim. 6:17; 2 Tim. 4:10; Tito 2:12, Ebr. 6:5)

## MADA MAALUM: NYAKATI HIZI NA NYAKATI ZIJAZO

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kiliicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipya linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

| Yesu | Paulo | Webrania (Paulo) |
|---|---|---|
| Mt. 12:32; 13:22,39 | Warumi 12:2 | Ebr.1:2; 6:5; 11:3 |
| Marko 10:30 | 1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18 | |
| Luka 16:8; 18:30; 20:34-35 | 2 Kor. 4:4 | |
| | Wagalatia 1:4 | |
| | Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12 | |
| | 1 Timotheo 6:17 | |
| | 2 Timotheo 4:10 | |
| | Tito 2:12 | |

Katika theolojia ya Agano Jipya zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyekevu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale liilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipya wa uliopo tayari, lakini bado!

**1:22 "akavitia vitu vyote chini ya miguu yake"** "kuweka chini ya" ni neno la kijeshi katika mnyororo wa mamlaka (kama vile Zab. 110:1; 8:6). Baba amempa mwanawe nafasi ya kwanza katika kitu (kama vile Kol. 1:18-19). Katika nyakati za mwisho, Mwana atageuza vitu vyote kwa Baba (kama vile 1 Kor. 15:27-28). Unyenyekevu wa Yesu kwa Baba hauashirii kwa maana yoyote hali ya kutokuwa na usawa lakini hali ya mgawanyo wa mamlaka, wa kazi katika Utatu. Angalia maelezo kamili ya "kunyenyekea" katika Waefeso. 5:21.

▣**"akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote "** sitiari iliyopanuliwa ya Yesu kama kichwa cha mwili wake, kanisa inapatikana tu katika Waefeso na Wakolosai (kama vile Efe. 4:15; 5:23; Wakolosai 1:18-19; 2:19). Watu wa Kale wa ulimwengu wa Mediterania waliamini kichwa kinatoa uzima kwa mwili.

▣**"kanisa"** katika elimu ya kawaida ya Kiyunani, neno hili lilimaanisha kusanyiko (kama vile Mdo. 19:32). *Ekklesia* lilitumika katika Tafsiri ya Agano la Kale (LXX) kutafsiri neno la Kiebrania "kusanyiko (*qahal*) la Israeli" (kama vile Kutoka 16:3, 12:6; Mambo ya Walawi 4:13; Hesabu 20:4). Haya ni matumizi kadhaa ya kwanza ya neno hili katika Waefeso (kama vile Efe 1:22; 3:10, 21; 5:23,24,25,27,29,32). Vyote katika (Efe. 1:22-23) na katika Kol.1:24) Paulo analiita kanisa mwili wa Kanisa. Kanisa la kwanza lilijiona lenyewe kama watu wa Mungu waliotiliziwa haja zao kwa Kristo Yesu, Masihi kama kichwa chao. Moja ya uhusiano wa kifasihi kati ya Waefeso na Wakolosai ni kwamba katika Waefeso neno hili linaashiria kanisa la kiulimwengu (kama vile 1 Kor. 10:32; 12:28; 15:9; Gal. 1:13; Fil. 3:6), wakati katika Wakolosai mara nyingi inamaanisha kanisa la nyumbani. Hii inatupeleka kwa Waefeso kama barua ya wengi. Angalia Mada Maalum katika Kol. 1:18

**1:23**
**NASB, NKJV**
**NRSV** **"anayekamilika kwa vyote katika vyote"**

**TEV** **"ukamilisho wa yeye ambaye yeye mwenyewe anakamilisha vitu vyote kila mahali"**
**(tanbihi "..ambaye yeye mwenyewe anatukamilisha kwa kutujaza ukamilifu wa Mungu")**
**NJB** **"ukamilifu katika Yeye ndani yake anayetujaza vyote katika vyote"**

Kisarufi hii ni kauli ya kati ya wakati uliopo usio timilifu. Hizi ni baadhi ya fasiri zinazowezekana kuwa za tungo hii;

1. Kristo analijaza kanisa
2. Kanisa linamjaza Kristo (kama vile Kol. 1:24)
3. Kanisa linakuwa likijazwa kwa hesabu kamilifu ya waaminio (kipengele cha hesabu kama vile Warumi 11:25)

Hi misamiati ililenga kuvamia mfumo wa kithiolojia wa *aeons,* wa kutoka au vyeo vya kimalaika uliopokelewa wa wajuzi wa walimu wa uongo. Maneno "ukamilifu" na "kujazwa" ni mfumo wa maneno ya Kiyunani *plērōma,* ambayo baadaye katika Karne ya pili yalikuja kuwa kati ya kuu, takatifu, mungu wa kiroho na mungu mdogo aliyekuwa akipanga na kuachia mambo maovu. Angalia maelezo kuhusu nadharia ya walimu wa uongo katika Utangulizi wa Waefeso. Hii ni maana yenye nguvu ya kanisa. Amemaanisha kikamilifu kuaksi kichwa chake, Yesu. Kama Yesu alivyomfunua Baba, vivyo pia kanisa linatakiwa kumfunua Baba.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nani anayetukuzwa katika Waefeso 1:3-14?
2. Toa maana ya "Gnosticism." (Nadharia ya wajuzi)
3. Je uchaguzi ni kwa namna gani (Waefeso 1:4, 5, 11) inahusiana na mwitikio wa kibinadamu (Waefeso 1:13)?
4. Orodhesha mambo yaliyotokea kabla ya uumbaji (Waefeso 1:4; Mathayo 25:34; Yohana 17:24; 1 Petro 1:20; Ufunuo 13:8).
5. Je sisi ni urithi wa Mungu au Yeye ndiye urithi wetu (Waefeso 1:11)?
6. Ni kwa nani ambaye kauli hii inayojirudia rudia ya "kwa sifa na utukufu Wake" inamaanisha?
7. Ni kwa namna gani Waefeso 1:20 inafanana na Waefeso 2:5-6?
8. Nani anayeongelewa katika Waefeso 1:21 (malaika, mashetani, majengo ya ulimwengu ulioanguka)?
9. Elezea nyakati mbili za Kiyahudi.

# WAEFESO 2

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Toka kifo hadi Uzima | kwa neema kupitia imani | Faida za kuwa na Kristo | Toka kifo hadi uzima | Wokovu katika Kristo, zawadi ya bure |
| 2:1-10 | 2:1-10 | 2:1-10 | 2:1-3 | 2:1-6 |
| | | | 2:4-10 | |
| | | | | 2:7-10 |
| Mtu katika Kristo | Amesogezwa karibu Kwa damu yake | | Mtu katika Kristo | Upatanisho wa Wayahudi na wapagani na watu wengine na Mungu |
| 2:11-13 | 2:11-13 | 2:11-22 | 2:11-12 | 2:11-18 |
| | Kristo amani yetu | | 2:13-18 | |
| 2:14-22 | 2:14-22 | | | |
| | | | 2:19-22 | 2:19-22 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo, linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 2:1-22

A. Msisitizo wa wale wenye ujuzi wa kipekee na Wayahudi juu ya wanadamu waliobobea katika kazi wanashushwa hadhi kwa msisitizo wa Paulo juu ya
   1. Uchaguzi wa Mungu katika Efe. 1 :3-1 4
   2. Hekima ya Mungu, maarifa na ufunuo, Efe. 1 :1 5-23
   3. Neema iliyoanzishwa na Mungu katika Efe. 2:1 -1 0

4. Siri ya mpango wa Mungu uliofichika toka enzi (yaani., Myahudi na Mtu wa Mataifa sasa ni wamoja katika Kristo) katika Efe. 2:1 1 -3:1 3

   Paulo anasisitiza vitu vinne ambavyo mwanadamu hana sehemu ndani yake! Wokovu wote ni wa Mungu(k.v. Efe.1 :3-1 4; 2:4-7), lakini watu wenyewe lazima kwa binafsi waitikie (k.v Efe. 2:8-9) na kuishi katika nuru ya agano jipya (Efe. 2:1 0).

B. Kuna maadui watatu wa mwanadamu aliyeanguka wakielezewa kinagaubaga katika Efe. 2:2-3 (k.v. yakobo 4:1 ,4,7):
   1. Muundo wa ulimwengu ulioanguka, Efe. 2:2
   2. Mshitaki wetu wa kimalaika, shetani, Efe. 2:2
   3. Asili ya mwandamu aliyeanguka (asili ya ki-Adamu), Efe. 2:3

   Mstari 1 -3 unaonyesha kutokuwepo tumani na kutokuwepo msaada wa mwanadamu aliyeanguka mbali na kuwa katika uasi na Mungu (k.v. Rum. 1:1 8-2:1 6).

C. Kama Efe. 2:1 -3 inavyoelezea hali ya huruma ya mwanadamu, Efe. 2:4-6 inapingana na wingi wa pendo la mwanadamu na rehema kwa mwanadamu aliyeanguka. Dhambi ya mwanadamu ni mbaya, lakini upendo wa Mungu na rehema ni mkubwa (k.v. Rum.5:20)! Kile Mungu alikifanya kwa ajili ya Kristo (k.v. Efe. 1 :20), Kristo sasa amefanya kwa ajili ya waamini (k.v. Efe. 2:5-6).

D. Kuna mvutano wa kweli katika agano jipya kati ya neema ya bure ya Mungu na bidii ya mwanadamu. Mvutano huu waweza kuelezewa katika jozi za kimafumbo:
   1. Kauli elekezi (ya maelezo) na kauli shurutishi (yenye amri);
   2. Neema/kishamirisho cha imani (maudhui ya injili) na kiima (uzoefu wa injili wa mtu);
   3. Kuzishinda mbio (katika Kristo) na kukimbia mbio (kwa ajili ya Kristo).

   Mvutano huu wazi kabisa unaonekana katika Efe. 2:8-9, ambao unasisitiza neema, wakati Efe. 2:10 inasisitiza kazi njema. Sio suala la hiki/wala kile lakini ni vyote/ na pendekezo la kithiolojia. Hata hivyo, neema siku zote hutokea kwanza na ni msingi wa mtindo wa maisha wa mfanano wa Kristo. Mistari ya 8-10 ni muhtasari wa kidaraja juu wa fumbo la injili ya bure ya Wakristo, lakini inagharimu kila kitu! Imani na matendo (k.v. Yakobo 2:1 4-26)!

E. Mada mpya imeanzishwa katika Efe. 2:1 1 -3:1 3. Ni siri, iliyofichika toka mwanzo, kuwa Mungu anapenda ukombozi wa wanadamu wote, Myahudi (k.v. Ezek. 1 8:23,32) na mtu wa mataifa (k.v. 1 Tim. 2:4; Tito 2:1 1 ; 2 Pet. 3:9), kupitia imani binafsi katika kifo mbadala cha Masihi. Zawadi hii ya pamoja ya wokovu ilitabiriwa katika Mwa. 3:1 5 na 1 2:3. Kimsingi huu ni msamaha wa bure (k.v.Rum. 5:12-21) iliwashangaza Wayahudi na wasomi wa kidini (walimu wa uongo wenye ujuzi, wasaliti) na wote "watenda haki" wa kisasa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 2:1-10**

**[1]Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; [2]ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; [3]ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine. [4]Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; [5] hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. [6]Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; [7]ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu. [8]Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; [9]wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. [10]Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.**

**2:1** Huenda Efe. 2:1-7 au Efe. 2: -10 inaunda sentensi moja ya Kiyunani, ikiwa na kitenzi kikuu katika Efe. 2:5. Ni hoja moja endelevu. Uwasilishaji wa Paulo unajumuisha

1. Lisilo na tumaini, lisilo na msaada,na upotevu wa kiroho wa mwanadam, Efe. 2:1 -3
2. Neema ya Mungu isiyostahili, Efe. 2:4-7
3. Umuhimu wa mwitikio wa mwanadamu, imani na maisha, Efe. 2:8-1 0

◙ **"nanyi"** katika Wakolosai na Waefeso hiki kiwakilishi nomino cha wingi mara zote kinarejea kwa watu wa mataifa wanao amini (k.v. Efe. 1 :1 3;2:1 2).

◙ **"mlikuwa wafu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ikimaanisha "mlikuwa wafu."Hili linarejelea kwenye kifo cha kiroho (k.v. Efe. 2:5; Rum. 5:12-21; Kol. 2:13). Biblia inaongelea juu ya hatua tatu za mauti:

1. Mauti ya kiroho (k.v. Mwa. 2:17; Mwanzo 3; Isa. 59:2; Rum. 7:10-11 ; Yakobo 1:15)
2. Mauti ya mwili (k.v. Mwa. 2:16-17; 3:4-5; 5)
3. Mauti ya milele, yaitwayo "mauti ya pili" (k.v. Ufu. 2:11 ; 20:6,14; 21:8)

◙**"makosa"** Neno la Kiyunani (*paraptōma*) linamaanisha "kuangukia upande mmoja" (k.v. Efe. 1:7). Maneno yote ya Kiyunani kwa ajili ya neno "dhambi"yanahusiana na dhana ya Kiebrania ya kuchepuka kutoka katika haki ya kiwango cha Mungu. Neno "mwema""haki"na mengine yatokanayo katika Kiebrania yanatoka kwenye uundwaji wa sitiari ya futi kamba (angalia Mada Maalum katika Efe. 4:24). Mungu ni kipimo. Wanadamu wameondoka toka kwenye kipimo cha Mungu (k.v. Zab. 14:1-3; 5:9; 10:7; 36:1 ; 53:1-4; 140:3; Isa. 53:6; 59:7-8; Rum. 3:9-23; 1 Pet. 2:25).

◙ **"dhambi"** Hili neno la Kiyunani (*hamartia*) linamaanisha "kuikosa shabaha" (k.v. Efe. 4:26). Maneno mawili kwa ajili ya dhambi katika mstari wa kwanza yanatumika kama kisawe kuelezea mwanadamu aliyeanguka, mwenye hali ya kufarakanishwa ( k.v. Rum. 3:9,19,23;11 :32; Gal. 3:22).

**2:2 "ambazo mlienenda zamani"** "kuenenda" ni sitiari ya kibiblia kwa stadi ya maisha (k.v. Efe. 2:2,10; 4:1,1 7;5:2,8,15).

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJB** | **"kwa kuifuata kanuni ya dunia hii"** |
| **NRSV** | **"kufuatana na kanuni ya dunia hii"** |
| **TEV** | **"ikifuatisha njia mbaya za dunia hii"** |
| **NJB** | **"wakiishi kwa kanuni za dunia hii"** |

Huu muundo wa sasa wa ulimwengu ulioanguka (yaani.,., zama) unaufanya mwili kama adui (k.v. Gal. 1:4). Ni mwanadamu aliyeanguka ndiye anajaribu kuyapata mahitaji yake yote mbali na Mungu. Ni maandiko ya Yohana yanayoita "ulimwengu" (k.v. 1 Yoh. 2:2,15-17;3:1 ,13,17; 4:1-17; 5:4,5,19) au "Babeli" (k.v. Ufu. 14:8; 16:19; 17:5; 18:2,10,21 ). Katika istilahi zetu za kisasa inaitwa "elimu ya binadamu kumkana Mungu."Tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya Neno *Kosmos* katika Kol. 1 :6.

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"kwa kumfuata mfalme wa uweza wa anga"** |
| **NRSV** | **"kufuatia watawala wa uwezo wa anga"** |
| **TEV** | **"ukawatii watawala wa uweza wa kiroho"** |
| **NJB** | **"wakitii watawala wanaotawala anga"** |

Huyu ni adui wa pili wa mwanadamu aliyeanguka, mshitaki wetu Shetani. Mwanadamu anawajibika kujitoa kwa mjaribu binafsi wa kimalaika (k.v. Mwanzo 3, Ayubu 1-2, Zakaria 3). Inaitwa mtawala au mungu wa ulimwengu huu (k.v. Yohana 12:31 ; 14:30; 16:11 ; 2 Kor. 4:4; 1 Yoh. 5:19).katika Agano Jipya anga ni ulimwengu wa kimapepo. Anga la chini (*aēr)* lilionekana na Wayunani kuwa halikuwa safi na kwa hiyo lilimiliki pepo wachafu. Baadhi wanaona matumizi haya ya neno "anga"kama linavyorejelea kwenye asili isiyo muhimu ya ulimwengu wa kiroho. Dhana ya "kunyakuliwa kwa kanisa"linatokana na tafasiri ya Kilatini ya 1 The. 4:17, "alinaswa." Wakristo

watamwona Bwana katikati ya ufalme wa shetani, “katika anga”kuonyesha ameisha tupwa!

**MADA MAALUM: UOVU BINAFSI**

I. SOMO KUHUSU SHETANI NI GUMU SANA

A. Agano la Kale halibainishi adui mkubwa wa (Mungu), bali mtumishi wa YHWH ambaye anawapa wanadamu mbadala na kutuhumu huyu mwanadamu kwa kutokuwa na haki (A. B. Davidson, *A Theology of the OT,* kur. 300-306).

B. Dhana ya adui mkubwa wa Mungu ulianza wakati wa fasili kati ya Biblia (zisizo na taratibu za kikanisa) katika kipindi cha dini ya kiislamu iliyoanzishwa na Zoroaster huko Uajemi. Hii kwa namna nyingine, kwa kiwango kikubwa ilisababisha sheria ya dini ya Kiyahudi (yaani, waliokuwa wametengwa na kuishi nje ya Israel yaani Babiloni, na Persia).

C. Agano Jipya linaunda dharura ya Agano la Kale katika ugumu wa ajabu lakini makundi yaliyochaguliwa

kama mtu anaanza kusoma habari za uovu katika mtizamo wa thiolojia ya biblia (kila kitabu au mwandishi au michoro alisoma na kuandika kwa kifupi kwa kutenganisha) basi mawazo mbalimbali kuhusu uovu yangeibuliwa. hata hivyo, mtu ataanza kusoma kuhusu uovu lakini kwa njia isiyo ya kibiblia au nje zaidi ya biblia mfano dini za kiulimwengu au dini za mashariki, basi sehemu kubwa ya mambo mengi ya maendeleo ya agano jipya yalionyeshwa katika pande mbili za uajemi na tabia za uyunani na kiroma.

Kama mtu alidhaniwa kujitoa kwa uwezo wa kiungu neno la Mungu (lama nilivyo!),kwa hiyo mambo ya Agano Jipya lazima yaonekane kama ufunuo endelevu. Wakristo yawapasa wajilinde dhidi ya kuruhusu simulizi za Kiyahudi au fasihi za Kiingereza (yaani, Dante, Milton) kufafanua zaidi dhana hiyo bila shaka miujiza na maana tofauti tofauti katika eneo hili la wokovu. Mungu amechagua kutobainisha mambo yote ya uovu, asili yake (tazama Mada Maalumu: Lusifa),kusudi lake,lakini amebainisha kushindwa kwake!

II. SHETANI KATIKA AGANO LA KALE

Katika Agano la kale neno "Shetani" (BDB 966, KB 1317) au "mshitaki" linaonekana kuhusiana na makundi matatu tofauti.

A. Washtaki wa wanadamu (1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 5:4, 11:14,23,25; Zab. 109:6,20,29

B. Washtaki wa kimalaika (Hes. 22:22-23; Zak. 3:1)

1. Malaika wa Bwana – Hes. 22:22-23
2. Shetani – 1 Nya. 21:1; Ayubu 1-2; Zak. 3:1

C. Washtaki wa kimapepo (bila shaka shetani) (1 Fal. 22:21; Zak. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha kuingia agano jipya ibilisi wa Mwanzo 3 alijulikana ni shetani (kama vile.Kitabu cha Hekima 2:23-24; II Enoch 31:3), na hata baadaye ambapo anakuja kuwa chaguo la viongozi wa kidini wa Uyahudi (kama vile. Sot 9b na Sanh. 29a). "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 wanakuwa malaika wa uovu katika I Enoch 54:6. Wanakuwa waanzilishi wa uovu katika thiolojia ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi. Nalitaja hili sio kwa kuonyesha usahihi wake wa kithiolojia, bali kuonyesha maendeleo yake katika Agano Jipya, shuguli hizi za Agano la Kale zinachangia katika uovu wa malaika wa nuru (yaani shetani,)katika 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9.

Asili ya uovu wa yule aliyejigeuza kuwa malaika wa nuru ni mgumu au haiwezekani (kutegemea maoni yako) kuupima toka katika Agano la Kale. Sababu moja wapo ni ile imani ya nguvu juu ya uwepo wa Mungu mmoja tu. (kama vile. Kumb. 6:4-6; 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amos 3:6). Majeruhi wote walipelekea YHWH kuonyesha kwa vitendo alivyo wa pekee na mkuu (kama vile. Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Uwezekano wa vyanzo vya habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo shetani ni mojawapo wa wana wa Mungu "mwana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14; Ezekieli 28, ambapo ujivuni karibu na wafalme wa mashariki (Babiloni na Uturuki) wamekuwa wakielezea sifa au ujivuni wa shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganya mihemko kuhusu kuliendea suala hili. Ezekieli anatumia bustani ya Edeni kama neno mbadala sio tu kwa mfalme wa Uturuki kama shetani (kama vile. Ezek. 28:12-16), lakini pia kwa ufalme wa Misri kama mti wa maarifa wa mema na mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa kurasa 12-14, anaonekana kuelezea uasi wa malaika kupitia majivuno kama Mungu alivyotaka kubainisha kwetu jinsi alivyo hasa na asili ya shetani hii ni njia isiyo elezea moja kwa moja na mahali pa kuifanya (tazama Mada Mada Maalumu: Lusifa). Lazima tujilinde dhidi ya mwenendo wa Theolojia wa kuchukua sehemu ndogo ndogo, tata toka kwenye maeneo yenye maana mbalimbali ya waandishi, vitabu, na kuviunganisha kama vipande vipande vya fumbo la Kiungu.

III. SHETANI KATIKA AGANO JIPYA

Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII [kur.. 748-763] na XVI [kur. 770-776]) anasema mafundisho ya sheria za Kiyahudi yameathiriwa wazi kabisa na umiliki wa pande mbili za Uajemi na mtizamo wa kimapepo. viongozi hawa wa kidini sio vyanzo vizuri vya ukweli katika eneo. Yesu kimsingi anakwepa kutoka kwenye mafundisho ya sinagogi. Nafikiri kuwa dhana ya viongozi wa dini ya kiyahudi ya upatanisho wa kimalaika (kama vile.Matendo 7:53) na upinzani katika kutoa sheria za Musa kwenye mlima Sinai ilifungua mlango kwa dhana ya adui mkuu wa YHWH kadhalika na mwanadamu. Palikuwa na Mungu wawili wa pande mbili za Iran (ufuasi wa Zoroaster).

1. *Ahura Mazda,* baadaye akaitwa *Ohrmazd*, aliyekuwa mungu muumbaji, mungu mwema
2. *Angra Mainyu,*baadaye aliitwa *Ahriman*,roho aangamizaye, mungu mwovu,

Vita juu ya ukuu na dunia ikawa kama uwanja wa vita. Umiliki wa pande mbili ukajengeka ndani ya pande mbili za Kiyahudi zenye ukomo kati ya YHWH na shetani.

Hakika kuna mafunuo endelevu katika agano Jipya kama ilivyo kwenye uovu, lakini sio kama ilivyoelezewa kama walimu wa dini ya Kiyahudi wanavyodai. mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita vya mbinguni." Kuanguka kwa shetani (Mwovu) ni mantiki yenye umuhimu, lakini sehemu husika haikutolewa (Tazama Mada Maalumu: Kuanguka kwa shetani na malaika wake). Hata hivyo kile kilichotolewa kimefichika kwenye mafunuo tanzu (k.v. Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa shetani ameshindwa na kutupwa duniani, bado anatenda kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile. Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20).

Lazima tuthibiti kiu yetu katika eneo hili. Kuna nguvu binafsi ya majaribu na uovu lakini bado kuna Mungu mmoja tu na mwanadamu bado anawajibika kwa uchaguzi wake. kuna vita ya kiroho kabla na baada ya wokovu. Ushindi wawezakuja tu na kubakia ndani na kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umekwisha shindwa na utaondolewa (kama vile. Ufu. 20:10)!

**NASB, NKJV "katika wana wa kuasi"**
**NRSV "katikati ya wale walioasi"**
**TEV "watu waliomwasi Mungu"**
**NJB "katika hali ya uasi"**

Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuasi na tabia ya jumla (k.v. Efe. 5:6).

**2:3 "sisi sote nasi tulienda kati yao"** Katika Waefeso "sisi"inawarejelea waamini wa Kiyahudi, katika hali hii, ni Paulo na huduma yake. kifungu cha "hata wale waliobaki,"wanakifanya kuwa kifungu hiki kiwarejelee wale wote waliochaguliwa wa Agano la Kale, yaani Wayahudi. Kitenzi hiki ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Irabu sauti tendwa ingalisisitiza kuwa mwanadamu aliyeanguka alidhibitiwa na nguvu za roho wachafu wa nje, kama shetani au mapepo yaliyotajwa katika Efe. 2:2 na 3:10; 6:12.

**NASB, NKJV "katika tama za miili yetu"**
**NRSV " katika tamaa za miili yetu"**
**TEV "kutokana na tamaazetu za kiasili"**
**NJB "maisha ya tamaa"**

Hii ni hatua ya tatu ya mwanadamu aliyeanguka. Ingawa haikuorodheshwa katika muundo wa kisarufi unaofanana ("kutokana na. . .") ikiwa na wale maadui wawili walioko katika Efe. 2:2, ni ufanano wa kithiolojia. Anguko la mwanadamu, ubinafsi (k.v. Mwanzo 3) ni adui wake mkubwa (k.v. Gal. 5:1 9-21). Inageuza na kutenda kila kitu kwa kila mmoja kwa haja zake mwenyewe (k.v. Rum. 7:14-25).

Paulo alilitumia neno "mwili"kwa namna mbili tofauti. Mazingira tu ndio yanaweza kuamua utofauti. Katika Efe.2:11,15; 5:29,31; 6:5 na 12 inamaanisha "nafsi ya mwanadamu," na sio "asili ya mwanadamu aliyeanguka.
"tazama Mada Maalum: Mwili (*sarx*) katika Kol. 1:22.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"tuliyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia"** |
| **NKJV** | **"tukiyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia"** |
| **NRSV** | **"tukiyafuata mapenzi ya mwili na ya nia"** |
| **TEV** | **"na tukitenda kile kilichoyapendeza mapenzi ya miili yetu na fikra"** |
| **NJB** | **"tukitawaliwa na tama zetu za mwili na nia"** |

Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo inayosisitiza mwendelezo, tendo endelevu. Mwili wa mwanadamu na fikra haina uovu ndani yake zenyewe, lakini ni uwanja wa vita wa majaribu na dhambi (k.v.Efe. 4:17-19; Warumi 6 na 7).

◙ **"kwa asili"** Hili linarejelea anguko la mwanadamu, tabia za ki-Adamu (k.v. Mwanzo 3; Zab. 51:5; Ayubu 14:4; Rum. 5:12-21; 7:14-25). Inashangaza kuwa walimu wa dini ya Kiyahudi kwa pamoja hawasisitizi anguko la mwanadamu katika Mwanzo 3. Badala yake wanadai kuwa mwanadamu anayo makusudi mawili (*yetzers*), moja jema, lingine ovu. Mwanadamu anatawaliwa na chaguzi. Kuna msemo maarufu wa dini ya Kiyahudi unaosema "kila mtu ana mbwa mweupe na mweusi katika roho yake, yule anayemlisha sana ndiye anakuwa mnene."hata hivyo, Agano Jipya linawasilisha sababu mbali mbali za kithiolojia kwa dhambi ya mwanadamu (1 ) anguko la Adamu; (2) ujinga wa kujitakia; na (3) chaguzi za dhambi.

◙ **"watoto wa hasira"** "Watoto wa. . .", kama "wana wa. . .", ni kifungu cha nahau ya Kiebrania kwa tabia za mtu. Mungu anapinga utendaji dhambi na uasi katika uumbaji wake. Ghadhabu ya Mungu ni ya muda (kwa wakati mmoja) na ya matukio ya siku ya hukumu (siku ya mwisho).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"na hao wengine"** |
| **NKJV** | **"wametufanya tukae pamoja"** |
| **NRSV, TEV** | **"kama wengine"** |
| **NJB** | **"kama wengine wa dunia"** |

Hii inarejelea upotevu wa mwanadamu, kwa wote Wayahudi na watu wa mataifa (k.v. Rum. 1:18-3:21 ). Paulo analitumia neno "wengine"kuwarejea waliopotea (k.v. 1 The. 4:13; 5:6).

**2:4 "lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake aliyotupenda"** Kuna kitu cha kuvutia hapa kati ya mwanadamu aliyeanguka asiye na tumaini na asiye na masaada katika Efe. 2:1-3 na neema na rehema ya ajabu ya Mungu katika Efe. 2:4-7.
Ni ukweli jinsi gani huu! Rehema ya Mungu na upendo ni vigezo vya wokovu (k.v. Efe. 2:7). Kwa tabia za rehema zake (k.v. Kut. 34:6; Nah. 9:17; Zab. 86:15; 103:8; 145:8-9; Efe. 1:7,18; 2:7; 3:8,16;), sio utendaji wa mwanadamu, unaotoa njia ya haki (k.v. Rum 3:21-31 ). Tazama ukumbusho juu ya "mwingi" katika Efe. 1:7. Ni muhimu kuwa huu mstari unaohusu neema ya Mungu unajumuisha kauli endelevu za wakati uliopo na kauli tendaji elekezi za wakati uliopita usiotimilifu. Mungu alitupenda huko nyuma (k.v. Yohana 3:16; 1 Yohana 4:9-10)
na anaendelea kutupenda (k.v. 1 Yohana 4:7-8, 16)!

**2:5 "hata wakati tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu,"** Kifungu hiki kinafanana na kile cha Efe. 2:1a. Paulo anarudi kwenye fikra zake za awali baada ya zile fikra zake zilizokuwa kwenye mabano (k.v. Efe. 2:1-3) kuhusu upotevu wa mwanadamu. Katikati ya hitaji letu, Mungu akatenda kwa upendo (k.v. Rum. 5:6,8).

◙ **"alituhuisha pamoja na Kristo"** Kifungu hiki cha Kiingereza kinaaksi neno moja la Kiyunani (*suzōpoieō*). Hiki ni kitenzi kikuu cha sentensi (kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu) kinachoanzia katika Efe. 2:1 . Hii ni moja kati ya vitenzi vitatu ambatanishi vya wakati uliopita usiotimilifu vikiwa na kihusihi, *syn*, chenye kumaanisha "ushiriki wa pamoja na."Yesu alifufuliwa toka katika wafu katika Efe. 1:20 na waamini wamewahishwa kwenye maisha ya kiroho kupitia Yeye (k.v. Kol.2:13; 3:1 ). Waamini sasa wako hai na Kristo. Tuna maisha ya ufufuko sasa! Kifo, adui wetu wa mwisho, kimeisha shindwa (k.v. 1 Kor. 15).

◙ **2:5,8 "tumeokolewa kwa neema"** Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea yenye mafumbo, inayojirudia katika Efe. 2:8 kwa ajili ya msisitizo. Hii inamaanisha kuwa waamini waliokolewa huko nyuma, na wakala mwingine, wakiwa na matokeo yanayodumu; "wamekuwa na wanaendelea kuokolewa na Mungu."Muundo huu wa aina ile ile unajirudia katika Efe. 2:8 kwa ajili ya kusisitiza. Tazama Mada Maalum katika Efe. 1:7.
Hivi ni moja ya vifungu vya kibiblia vinavyounda msingi wa mafundisho juu ya ulinzi wa mwamini (k.v. Yohana 6:37, 39; 10:28; 17:2, 24; 18:9; Rum. 8:31 -39). Kama yalivyo maandiko mengine ya kibiblia, lazima yaoanishwe (yakiwa na mvutano) na kweli zingine na maandiko.

**2:6 "tumefufuliwa pamoja nae"** Hii ni ambatani ya pili ya wakati uliopita usiotimilifu ikiwa na *syn*. Waamini wamekwisha fufuliwa na Kristo. Waamini walizikwa na Kristo katika ubatizo (k.v. Kol. 2:1 2; Rum. 6:3-11 ) na kufufuliwa naye na Baba (k.v. Kol. 2:13; Rum. 6:4-5) aliyemfufua Yesu (alifufuliwa na Roho katika Rum.8:11 ). Huu ni unasaba wa ukombozi maalum. Waamini kiroho wanashiriki katika matukio muhimu ya uzoefu wa Yesu: kusulubiwa, kifo, kuzikwa, ufufuko, na kutawazwa! Waamini wanashiriki maisha yake na maumivu, pia nao watashiriki utukufu wake (k.v. Rum. 8:17)!

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"akatuketisha pamoja nae"** |
| **NKJB** | **"akatufanya tuketi nae pamoja"** |
| **TEV** | **"tutawale nae"** |
| **NJB** | **"akatupatia nafasi pamoja nae"** |

Hii ni ambatani ya tatu ya wakati uliopita usiotimilifu ikiwa na *syn*. Nafasi yetu katika Yeye ni moja ya wakati uliopo, vile vile na wakati ujao, ushindi (k.v. Rum. 8:37)! Dhana ya kuketishwa pamoja nae inamaana sisi ni watawala pamoja nae (k.v. Mt.19:28; Rum. 5:1 7; Kol. 3:1 ; 2 Tim. 2:12; Ufu. 2:26; 3:21 ).

## MADA MAALUM: KUTAWALA KATIKA UFALME WA MUNGU

Dhana ya kutawala tukiwa na Kristo ni sehemu ya namna kubwa ya kithiolojia inayitwa "ufalme wa Mungu." Huu ni mwito toka dhana ya Agano la Kale la Mungu Yeye kama Mfalme wa kweli wa Israel (kama vile 1 Sam.8:7). Kiishara anatawala (1 Sam. 8:7; 10:17-19) kupitia kizazi cha kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:10) na familia ya Yese (kama vile 2 Samwel 7).
Yesu ni ahadi ya utimilifu wa unabii wa Agano la kale kuhusiana na Masihi. Aliuanzisha Ufalme wa Mungu akiwa na mwili wa kibinadamu pale Bethlehemu. Ufalme wa Mungu ukaja kuwa ni nguzo kuu ya mafundisho ya Yesu. ufalme wa Mungu ukawa kamili ndani yake (kama vile Mt. 10:7; 11:12; 12:28; Mark 1:15; Lk 10:9,11; 11:20; 16:16; 17:20-21).
Hata hivyo, ufalme ulikuwa wa wakati ujao (matukio ya siku za mwisho). Ulikuwepo lakini ukawa haujatimilizwa (kama vile. Mt. 6:10; 8:11; 16:28; 22:1-14; 26:29; Lk 9:27; 11:2; 13:29; 14:10-24; 22:16,18). Kwa mara ya kwanza Yesu akaja kama mtumwa mwenye mateso (kama vile. Isa. 52:13-53:12); mwenye kunyenyekea (kama vile. Zak. 9:9), bali atarudi kama Mfalme wa Wafalme (kama vile. Mt. 2:2; 21:5; 27:11-14). Dhana ya "kutawala" kwa uhakika ni sehemu ya "Ufalme" wa thiolojia. Mungu amekwisha kuwapatia ufalme wafuasi wa Kristo (angalia Lk 12:32).
Dhana ya kutawala pamoja na Kristo ina mitizamo mbali mbali pamoja na maswali

1. Je sura zile zinazodai kuwa Mungu amewapa waamini "ufalme" kupitia Kristo zinarejea juu ya "kutawala" (kama vile Mt. 5:3,10; Lk 12:32)?
2. Je maneno ya Yesu kwa wanafunzi wa mwanzo kwenye karne ya kwanza katika mazingira ya Kiyahudi yanarejea kwa waamini wote (kama vile. Mt. 19:28; Lk 22:28-30)?
3. Je misisitizo ya Paulo juu ya kutawala katika maisha haya ya sasa yanakinzana au yanawiana na maandiko ya hapo juu (kama vile. Rum. 5:17; 1 Kor. 4:8)?
4. Ni kwa namna gani mateso na utawala vinahusiana (kama vile. Rum. 8:17; 2 Tim. 2:11-12; 1 Pet. 4:13; Uf. 1:9)?
5. Dhana ya kujirudia ya ufunuo unachangia pamoja utawala wa Yesu uliotukuzwa, lakini huo utawala wa
   a. Kidunia, Uf. 5:10
   b. Utawala wa miaka i000, Uf. 20:4-6
   c. Milele, Uf. 2:26; 3:21; 22:5 na Dan. 7:14,18,27

**NASN, NKJV**
**NRSV "katika ulimwengu wa roho"**
**TEV "katika ulimwengu wa roho"**
**NJB "katika ulimwengu"**

Hiki kivumishi cha uwingi cha uhusika tasa wa mahali, “katika ulimwengu wa roho,”kimetumika tu katika Waefeso (k.v. Efe. 1:20; 2:6; 3: 0; 6:12). Kutokana na mazingira ya utumiaji wake wote, lazima imaanishe ulimwengu wa kiroho katika waamini wanaoishi ndani yake sasa, na sio mbinguni.

**2:7 "katika zamani zinazokuja"** Wayahudi waliamini katika zama mbili, ulimwengu wa sasa wa uovu, (Gal. 1 :4) na ulimwengu wa haki unaokuja (tazama Mada Maalum katika Efe. 1:21). Huu ulimwengu mpya wa haki utazinduliwa na Masihi anayetarajiwa katika wingi wa nguvu ya Roho. Katika Efe. 1:21 neno" zama" liko katika hali ya umoja, lakini hapa liko katika wingi (k.v. 1 Kor 2:7; Ebr. 1:2; 11:3). Hii inamaanisha kuwa (1 ) kiwastani kuna zama mbili au (2) hali ya uwingi inatumika kusisitiza na kukuza zama inayokuja-nahau ya ya ki-ualimu ya dini ya Kiyahudi unayoita “wingi wa utukufu.”Matumizi haya ya uwingi wa maana ya ishara yanaweza kuonekana katika kifungu kile kinachorejelea “zama” zilizopita (k.v. Rum. 16:25; 1 Kor. 10:11 ; 2 Tim. 1:9; Tito 1:2).
Baadhi ya wasomi wanaamini hii kiuhalisia ilikuwa ni sitiari ya umilele kwa sababu ya namna kifungu kilivyotumika katika Kiyunani cha lugha ya Koine kiulimwengu na sehemu mbali mbali katika Agano Jipya (k.v. Lk 1:33, 55; Yohana 12:34; Rum. 9:5; Gal. 1:5;1 Tim. 1:17).

◙ **"audhihilishe"** Hii ni kauli ya kati tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Kwa uwazi mkubwa Mungu anadhihilisha tabia yake (k.v.Efe. 1:5-7). Neno hili linamaanisha “kuonyesha kwa uwazi” (k.v. Rum. 9:17,22). Rehema ya Mungu na kusudi katika Kristo zimedhihilishwa kwa uwazi kwa malaika kwa matendo yake mwanadamu aliyeanguka (k.v. Efe. 3:10; 1 Kor. 4:9).

◙ **"upitao kiasi"** *Huperballō*. Tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya neno ambatani *Huper* katika Efe. 1:1 9.

**2:8 " kwa neema"** Wokovu ni kwa “neema” ya Mungu ( k.v. Efe. 1:3-14). Tabia ya Mungu inadhihilishwa kupitia rehema zake (k.v. Efe. 2:4-6). Waamini ni kumbukumbu ya ushindi wa pendo lake. Neema imeelezewa vizuri kama upendo wa Mungu ambao haujahakikiwa, na kumilikiwa. Unatililika toka asili ya Mungu kupitia Kristo na pasipo kujali thamani yake au thamani ya yule aliyependwa.

◙ **"mmeokolewa"** Hii ni kauli timilifu tendwa endelevu yenye mafumbo ambayo ni rudio la Efe. 2:5 (tazama ukumbusho hapa). Msukumo wake ni kuwa “waamini wamekuwa na wanaendelea”kuokolewa na Mungu. Katika Agano la Kale neno “okoa” linazungumza juu ya “kukombolewa kimwili” (k.v. Yakobo 5:15). Katika Agano Jipya maana hii imechuliwa juu ya kipimo cha kiroho. Mungu anawaokoa waamini kutoka kwenye matokeo ya anguko na kuwapa maisha ya milele. Anarejesha taswira ya Mungu na kuwezesha ushirika pamoja nae tena. Tazama Mada Maalum katika Efe. 1:7

◙ **"kwa imani"** imani hupokea zawadi ya bure toka kwa Mungu (k.v. Rum. 3:22,25; 4:5; 9:30; Gal. 2:1 6; 3:24; 1Pet. 1 :5). Mwanadamu sharti aitikie kwa zawadi ya Mungu ya neema na msamaha katika Kristo (k.v. Yohana 1 :12; 3:1 6-17,36; 6:40; 11:25-26; Rum. 10:9-13). Mungu anashughulika na mwanadamu aliyeanguka kwa namna ya agano. Mara zote anachukua fursa (k.v. Yohana 6:44, 65) na kuweka agenda na mipaka (k.v. Marko 1 :15; Mdo. 3:16,1 9; 20:21 ). Anamruhusu mwanadamu aliyeanguka kushiriki kwenye wokovu wao kwa kuitikia kwa zawadi ya agano lake. Itikio lililoruhusiwa ni kwa yote ya awali na imani endelevu. Inajumuisha toba, utii, huduma, ibada, na ustahimilivu. Neno “imani”katika Agano la Kale ni mwendelezo wa ki-stiari wa mkao imara. Ilikuja kuonyesha kuwa kile ambacho ni cha uhakika, cha kutumainiwa, chenye kutegemewa, na aminifu. Hakuna kati ya hili linaelezea hata mwanadamu aliyekombolewa. Sio tumaini la mwanadamu, uaminifu, au tegemeo, lakini ni Mungu mwenyewe. Tunaamini katika ahadi ya tumaini lake, na sio tumaini letu! Utii wa agano unatiririka toka kwenye shukrani! Mtazamo mara zote umekuwa juu ya uaminifu wake, na sio imani ya waamini! Imani haiwezi kumwokoa

mtu. Ni neema tu inaokoa, lakini inapokelewa kwa imani. Mtazamo kamwe sio juu ya wingi wa imani (k.v. Mt. 1 7:20), lakini ni juu ya kitu (Yesu).

I. **MADA MAALUM: Kusadiki, Amini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale (ןמא)**

Maelezo ya awali

Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoelezewa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.

Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale

- A. Watu binafsi na jamii
- B. Ukabiliano binafsi na utii wa agano

Imani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani., usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezewa vizuri katika

- A. Ibrahim na uzao wake
- B. Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majaribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

II. Asili kuu iliyotumika

- A. ןמא (BDB 52, KB 63)
  - 1. KITENZI
    - a. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (i.e., 2 Fal. 10:1,5; Ester 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
    - b. Shina la neno ni *phal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
      - 1) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
      - 2) Kwa vitu, Isa. 22:23
      - 3) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
    - c. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini
      - 1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
      - 2) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)
      - 3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
      - 4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9
      - 5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
      - 6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12
  - 2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
  - 3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno "amina" katika agano la kale na agano jipya.
- B. תמא (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli
  - 1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
  - 2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
  - 3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16
- C. הנומא (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu
  - 1. Katika mikono, Kut. 17:12
  - 2. Katika muda, Isa. 33:6
  - 3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
  - 4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138

III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale

A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (cf. Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).

B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (ןמא).

1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.
2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pembeni kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
   a) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
   b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (cf. Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)

IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale

A. Petro anaunganisha
1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pembeni)
3. Zab. 118:22 – 1 Petr. 2:7 (jiwe lililokatariwa)

B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliielezea Israel kama “jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka
1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
2. Isa. 61:6; 66:21
3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

Na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (cf. 1Petr. 2:5,9)

V. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii

A. Utumiaji wake kwenye Agano Jpya

Neno “aaminiye" linatokana na neno la Kiyunani pisteuō ambalo pia laweza kutafasiliwa “ kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi
1. eis inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
   a. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
   b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
   c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
   d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
   e. ndani ya Yesu(Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
   f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
   g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. ev inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mark 1:15; Mdo 5:14
3. epi ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mat. 27:42; Mdo 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10

5. *hoti*, likimaanisha "kuamini kwamba," inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
   a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
   b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
   c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
   d. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
   e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
   f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
   g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
   h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
   i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye "Mimi ndiye" (Yohana 8:24; 13:19)
   j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
   k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1Thes. 4:14)

VI. Hitimisho

A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
   1. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
   2. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
   3. Utii
   4. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)

B. Imani ya Kibiblia ni
   1. Uhusiano binafsi (imani ya awali)
   2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imani katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
   3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

   Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (cf.Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba "urafiki wa karibu." Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za "kifamilia" (yaani., utakatifu, cf. Law. 19:2; Mat. 5:48; 1 Petr. 1:15-16). Anguko (cf. Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (cf. Ezek. 36:27-38), akitupatia "moyo mpya" na "roho mpya" inayotuwezesha kupitia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye!

   Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)

A. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipya), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipya katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, iliyoonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (cf. Efe. 2:8-9 na 10)

   Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

◙ **"na kwamba"** Hiki ni kiwakilishi kionyeshi cha Kiyunani *(touto),* ambacho ni hasi katika jinsia. Nomino za karibu, za neno "neema" na "imani," yote ni jinsia ya kike. Kwa hiyo, hili lazima lirejelee mchakato wote wa wokovu wetu katika kazi aliyoitimiliza Kristo. Kuna uwezekano mwingine unaoegemea juu ya ufanano wa muundo wa kisarufi katika Fil. 1:28. Kama hili ndo suala lenyewe hivyo basi fungu la kielezi linahusiana na imani, ambayo pia ni zawadi ya neema ya Mungu! Hapa kuna siri ya ukuu wa Mungu na utashi wa mwanadamu.

◙ **"hakitokani na nafsi zenu"** Hiki ni moja ya vifungu vitatu ambavyo wazi vinaonyesha kuwa wokovu hautokani na utendaji wa mwanadamu: (1) "sio kwa nafsi zetu wenyewe" Efe. 2:8; (2) "kipawa cha Mungu" Efe. 2:8;na (3) "sio kwa matendo" Efe. 2:9.

◙ **"bali ni kipawa cha Mungu"** Hiki ni kiini cha neema ya upendo kisichokuwa na mfungo (k.v. Rum. 3:24; 6:23). Fumbo la wokovu ni kama vyote zawadi ya bure na mwitikio wenye agano lenye mamlaka ambalo ni gumu kulishika. Pamoja na kwamba Bado yote ni kweli! Wokovu hakika ni wa bure, na bado unagharimu kila kitu. Mafundisho mengi ya kibiblia yanawasilishwa kama jozi ya mvutano wa kweli (ulinzi dhidi ya ustahimilivu, imani dhidi ya matendo, ukuu wa Mungu dhidi ya utashi wa mwanadamu, maamuzi ya kabla dhidi ya itikio la mwanadamu na kupita uwezo wa binadamu dhidi ya kuwepo kila mahali).

**MADA MAALUM: USHAHIDI WA WOKOVU WA MTU WA AGANO JIPYA**

Inasimamia juu ya Agano Jipya (kama vile Jer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38) katika Yesu:

1. Tabia ya Baba (kama vile Yn 3:16), kazi ya Mwana (kama vile 2 Kor. 5:21), na huduma ya Roho (kama vile Rum. 8:14-16),sio juu ya utendaji wa mwanadamu, sio malipo kutokana na utii, sio imani.
2. Ni karama (kama vile Rum. 3:24; 6:23; Efe. 2:5,8-9).
3. Ni maisha mapya, mtazamo mpya wa kidunia (kama vile Yakobo na 1 Yohana).
4. Ni maarifa (injili), ushirika (imani iliyoko ndani na pamoja na Kristo), na stadi ya maisha (mwongozo wa Roho unaomfanana Kristo) yote matatu, na sio moja kati ya hayo.
5. Angalia majaribu ya wokovu wa kweli katika tambuzi za kimuktadha kwenye 1 Yohana 2:3-27, C. kwenye mtandao.

**2:9 "sio kwa matendo,"** wokovu sio kwa kigezo (k.v. Rum. 3:20, 27-28; 9:11, 16; Gal. 2:16; Fil 3:9; 2 Tim. 1:9; Tito 3:5). Huu ni utofauti wa moja kwa moja kwa walimu wa uongo.

◙ **"asiwepo mtu wa kujivuna"** wokovu ni kwa neema ya Mungu, sio kwa bidii ya mtu, kwa hiyo hakuna nafasi ya mwanadamu kujitukuza (k.v. Rum. 3:27; 4:2). Ikiwa waamini watajisifu, na wajisifu katika Kristo (k.v. 1 Kor. 1:31, ambayo ni nukuu toka kwa Yer. 9:23-24).

**MADA MAALUM: KUJISIFU**

Haya maneno ya Kiyunani, kauchaomai, kauchēma, na kauchēsis, yametumiwa na Paulo mara therathini na tano na mara mbili tu katika kitabu vya Agano Jipya (yote katika kitabu cha Yakobo). Matumizi yake yaliyozidi yanapatikana katika 1 na 2 Wakorintho.

Kuna kweli kuu mbili zilizohusishwa kwenye majivuno.

A. Hapana mwili utakao jisifu/kujivuna mbele za Mungu (kama vile. 1 Kor. 1:29; Efe. 2:9)
B. Waamini wanapaswa kujisifu katika Bwana (kama vile. 1 Kor. 1:31; 2 Kor. 10:17, ambalo ni dokezo kwa Yer. 9:23-24)

Kwa hiyo, kuna majivuno yenye kustahili na yasiyo stahili (yaani., kiburi)

A. Majivuno yanayo stahili
    1. Katika tumaini la utukufu (kama vile Rum. 4:2)
    2. Katika Mungu kupitia mwanaye Yesu Kristo (kama vile Rum. 5:11)
    3. Katika msalaba wa Bwana Yesu Kristo (yaaani., dhamira kuu ya Paulo, kama vile 1 Kor. 1:17-18; Gal. 6:14)
    4. Paulo anajivuna katika
        a. Huduma yake isiyo na fidia (kama vile 1 Kor.9:15,16)
        b. Mamlaka yake kutoka kwa Kristo (kama vile. 2 Kor. 10:8,12)
        c. kutojisifu kwake katika kazi ya wengine (kama baadhi huko walivyokuwa, kama vile 2 Kor. 10:15)

d. urithi wa kijamii 2:Kor.(kama wengine walivyokuwa wakifanya huko Korintho , kama vile. 2 Kor. 11:17; 12:1,5,6)
e. Makanisa yake
1) Korintho (2 Kor. 7:4,14; 8:24; 9:2; 11:10)
2) Thessalonika (kama vile. 2 The. 1:4)
3) Kujiamini kwake katika faraja ya Mungu na ukombozi (kama vile. 2 Kor. 1:12)

B. Majivuno yasiyo stahili
1. Katika kuhusiana na urithi wa Kiyahudi (kama vile. Rum. 2:17-23; 3:27; Gal. 6:13)
2. Baadhi katika kanisa Korintho walikuwa wakijivuna
a. Katika Watu (kama vile. 1 Kor. 3:21)
b. Katika hekima (kama vile. 1 Kor. 4:7)
c. Katika uhuru (kama vile. 1 Kor. 5:6)
3. Walimu wa uongo walijaribu kujivuna ndani ya kanisa huko Korintho (kama vile. 2 Kor. 11:12)

**2:10 "maana tu kazi yake,"** neno la kiingereza kwa "ushairi"linatokana na neno hili la Kiyunani (*poiēma*). Neno hili limetumika mara mbili tu katika Agano Jipya, hapa na katika Rum. 1:20. Hii ni nafsi ya waamini katika neema. Kifumbo wao ni bidhaa kamili iliyoko katika mchakato!

◙ **"tuliumbwa katika Kristo Yesu"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu. Roho anawatengeneza waamini kupitia huduma ya Kristo kwa mapenzi ya Baba (k.v. Efe. 1:3-14). Tendo hili la uumbaji wa kiroho limeelezewa katika maneno yale yale yaliyotumika kwenye uumbaji wa awali katika Mwanzo (k.v. Mwa. 3:9; Kol. 1:16).

◙ **"tutende matendo mema"** mtindo wa maisha ya mwamini baada ya kumpata Kristo ni ushuhuda wa wokovu wao (k.v.Yakobo na 1 Yohana). Wanaokolewa kwa neema kupitia imani kuelekea matendo! Wameokolewa ili watumike! Imani bila matendo imekufa, kama ilivyo matendo bila imani (k.v. Mt. 7:21-23 na Yakobo 2:14-26). Wokovu ni lango na njia. Lengo la uchaguzi wa Baba ni kuwa waamini wawe "watakatifu na wasio na lawama" (k.v. Efe. 1:4). Mara nyingi Paulo alivamiwa kwa ajili ya injili yake ya bure kwa sababu ilionekana kutia moyo maisha yasiyokuwa na Mungu. Injili inaonekana kutounganikana na utendaji wa mwanadamu lazima iongoze kutukana. Injili ya Paulo ilkuwa ya bure katika neema ya Mungu, lakini pia ilihitaji mwitikio sahihi, sio tu katika toba ya awali, lakini katika mwendelezo wa toba, maisha ya ki-Mungu ni matokeo, sio kutokuwepo na sheria. Matendo mema sio chombo cha wokovu, lakini ni matokeo. Fumbo hili la wokovu huru wa moja kwa moja na mwitikio wa gharama ya kila kitu ni ngumu kuuwasilisha, lakini yote mawili lazima yashikiliwe katika mlingano wenye mvutano.

Ubinafsi wa ki-Amerika umeibadili injili. Wanadamu hawaokolewi kwa sababu Mungu anawapenda sana kibinafsi, lakini kwa sababu Mungu anampenda mwaanadamu aliyeanguka, mwanadamu akaumbwa kwa sura yake. Aliokoa na kuwabadili wale wabinafsi ili awafikie watu binafsi. Mtizamo wa ndani wa upendo kimsingi ni wa ushirika (k.v. Yohana 3:16), lakini unapokelewa kibinafsi (k.v. Yohana 1:12; Warumi 10:9-13; 1 Kor. 15:1).

◙**"ambao Mungu aliutengeneza tuenende nao"** Hili neno la nguvu (*pro* + *hetoimos,* "kuandaa kabla") inahusiana na dhana ya kithiolojia ya maamuzi ya kabla (k.v. Efe. 1:4-5, 11 ) na linatumika hapa tu na katika Rum. 9:23. Mungu alimuchagua mtu aweze kuaksi tabia yake. Kupitia Kristo, Baba amerejesha sura yake kwa mwanadamu aliyeanguka (k.v. Mwa. 1:26-27).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):WAEFESO 2:11-22**

**11 Kwa ajili ya hayo kumbukeni ya kwamba zamani ninyi, mlio watu wa Mataifa kwa jinsi ya mwili, mnaoitwa Wasiotahiriwa na wale wanaoitwa Waliotahiriwa, yaani, tohara ya mwilini iliyofanyika kwa mikono;**
**12kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani. 13Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa**

**mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. [14]Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. [15]Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani. [16]Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba. [17]Akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na amani kwao wale waliokuwa karibu. [18]Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja. [19]Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. [20]Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. [21]Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. [22]Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.**

**2:11 "kwa ajili ya hayo"** Hili laweza kurejelea kwa (1) Efe. 2:1-10, or (2) Efe. 1:3-2:10. Paulo mara nyingi anatumia neno hili kuanza sehemu mpya ya fasihi kwa kujenga juu ya kweli zilizo pamoja za sehemu za nyuma (k.v. Rum. 5:1 ; 8:1, 12:1 ). Hizi ni kweli ya tatu zilizo kubwa za sehemu ya kimafundisho ya Paulo (Efe. 1-3). Ya kwanza ilikuwa ni ule uchaguzi wa Mungu wa milele uliosimamia juu ya tabia Yake yenye rehema, ya pili ilikuwa ni kukosa tumaini kwa mwanadamu aliyeanguka, na kuokolewa kwa neema ya matendo Yake kupitia Kristo ambayo yatupasa kuipokea na kuishi nayo kwa imani. na ya tatu, mapenzi ya Mungu mara zote yamekuwa ndio wokovu wa mwanadamu aliyeanguka (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5), wote Wayahudi na watu wa mataifa (k.v. Efe.2:11 - 3:13). Si kwa akili za mwanadamu (yaani., wenye ujuzi wa pekee) wakaelewa kweli hizi zilizodhihilishwa.

◙ **"kumbukeni"** Hii kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hawa watu wa mataifa wanaamriwa kuendelea kukumbuka mfarakano wao wa nyuma na Mungu, Efe. 2:11 -12.

◙ **"kwamba zamani ninyi, mlikuwa watu wa mataifa kwa jinsi ya mwili"** Hili kikawaida ni neno "mataifa" (*ethnos*). Linarejelea watu wote wasio wa ukoo wa Yakobo. Katika Agano la Kale neno "mataifa" (*go'im*) lilikuwa ni neno la matusi lenye kuwarejelea wale wote wasio Wayahudi.

◙ **"mnaoitwa wasiotahiriwa'"** Hata katika Agano la Kale, utaratibu huu ulikuwa ni mwonekano wa nje wa imani ya ndani (k.v. Mambo ya Walawi.26:41-42; Kumb. 10:16; Yer. 4:4). "Wasaliti" wa ki-Galatia walidai kuwa haya yalikuwa bado ni mapenzi ya Mungu na yasiyo epukika kwa ajili ya wokovu (k.v. Mdo. 15:1 na kuendelea; Gal. 2:11 -12). Yumkini hili lilikuwa ni neno la dhihaka. Kueni waangalifu pasipo kuchanganya alama na ukweli wa kiroho kwa kile unachokisimamia (k.v. Mdo. 2:38 kwa ajili ya mfano mwingine)

**2:12**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"hamna Kristo"** |
| **NKJV, NRSV** | **"pasipo Kristo"** |
| **TEV** | **"mbali na Kristo"** |
| **NJB** | **"hamkumjua Kristo"** |

Kikawaida hili ni "juu ya misingi tofauti."Hivi vifungu vichache vinavyofuata, kama Efe. 2:1-3, vinaonyesha kukosa msaada na tumaini kwa watu wa mataifa pasipo Kristo
.

| | |
|---|---|
| **NASB, NJB** | **"mmetengwa"** |
| **NKJV,NRSV** | **"mmekuwa wageni"** |
| **TEV** | **"wageni"** |

Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea ikimaanisha "mmekuwa na mnaendelea kutengwa."katika Agano la Kale neno hili lilirejelea kwa wakazi wasio wazawa wenye haki finyu (wageni). Watu wa mataoifa wamekuwa na

wanaendelea kutengwa, wamefarakanishwa toka kwenye agano la YHWH.

◙ **"Jamii ya Israel"** Kiuhalisia hili linamaanisha "uraia" (*politeia*). Hili neno linatokana na neno la Kiingereza "siasa."linarejea kwa kizazi kilichochaguliwa cha Ibrahimu. Faida zake zimeelezewa katika Warumi 9:4-5.

◙**"maagano ya ahadi,"**Agano Jipya linaweza kurejea kwenye Agano la Kale kama agano moja au maagano mbali mbali. Mvutano huu wa kithiolojia unaweza kutazamwa kama agano moja la imani likielezewa katika (1 ) mahitaji yanayokinzana au (2) lililopewa kwa watu wengine. Mungu anawakabili watu wa Agano la Kale kwa njia tofauti. Neno lake kwa Adamu lilikuwa kuhusu mambo ya kwenye bustani ya Edeni, kwa Nuhu kuhusu Safina, kwa Ibrahim kuhusu mwanae na mahala pa kuishi, kwa Musa kuhusu kuwaongoza watu, n.k. Lakini kwa yote yanahusisha utii kwenye neno la Mungu! Baadhi ya makundi (wagawanyaji) wanatizamisha juu ya utofauti. Makundi mengine (wanaosisitiza ukuu wa Mungu) wanatizamisha juu ya kuunganisha dhana ya imani. Paulo mwenyewe anatizama juu ya agano la Ibrahim (k.v Warumi 4) kama muundo wa kielelezo cha uhusiano wote wa imani. Agano Jipya ni kama Agano la Kale katika hitaji lake la utii na imani binafsi katika ufunuo wa Mungu. Tofauti yake ni kwa namna mtu alivyo sawa na Mungu (k.v. Yer. 31:31 -34). Agano la Musa lilitizama juu ya utii wa mwanadamu na utendaji, wakati Agano Jipya linaangazia juu ya utii na utendaji wa Kristo. Hili Agano Jipya ni njia ya Mungu ya kuwaunganisha Wayahudi na watu wa mataifa kwa imani katika Kristo (k.v. Efe. 2:11-3:13). Agano Jipya, kama lilivyo lile la kale, yote hayana masharti (ahadi ya neema ya Mungu na msamaha) na yana masharti (mwitikio wa mwanadamu). Yanaaksi kwa pamoja ukuu wa Mungu (majaaliwa) na uchaguzi huru wa mwanadamu (imani, toba, utii, ustahimilivu).

## MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale berith (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni "kukata"ikimaanisha sadaka ya mnyama inayojumuishwa kwenye agano(kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji. Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadmu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abraham (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. Kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israeli toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Walawi 26, Kumbu kumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika "agano jipya" (kama vile. Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata

ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).
Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika wake mpya na waamini "agano jpya" (kama vile Mt. 26:28; Marko 14:24; Lk 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, lakini ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani., Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekena kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika Agano Jipya (angalia Mada Maalum: Uasi)

◙ **"mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani"** Kama kweli kuna Mungu muumbaji mmoja na Israel walikuwa watu wake waliochaguliwa, watu wa mataifa walitupiliwa mbali pasipo tumaini, wakipotelea kwenye ibada ya sanamu na kipagani (k.v. 1 The. 4:13 na Rum. 1:18-2:16).

**2:13 "lakini sasa"** Pana tofauti kati ya kutokuwepo na tumaini kwa watu wa mataifa kipindi cha nyuma, Efe. 2:11 –12, na tumaini lao kubwa katika injili, Efe. 2:13-22.

◙ **"ninyi mliokuwa mbali hapo mwanzo mmekuwa karibu"** Dhana hii mfanano inajirudia katika Efe.2:17, wakati Isa. 57:19 inanukuliwa. Katika Isaya andiko hili linarejelea kwa Wayahudi walioko uhamishoni lakini hapa katika Waefeso linarejelea kwa watu wa mataifa. Huu ni mfano mojawapo ya matumizi ya uainishaji ya Paulo ya vifungu vya Agano la Kale. Mitume wa Agano Jipya wamelijumuisha kwa wote tumaini la Agano la Kale. Kama ilivyo wakimbizi wa Kiyahudi walivyokuwa mbali na Mungu, vile vile nasi pia, watu wa mataifa wamefarakanishwa na Mungu.

◙ **"kwa damu ya Yesu."** Hili linarejelea juu ya uwakilishwaji, upatanisho mbadala wa Kristo (k.v. Efe.1:7; Rum. 3:25; 5:6-10; 2 Kor. 5:21 ; Kol. 1:20; Ebr. 9:14,28; 1 Pet. 1:19; Ufu. 1:5). Familia ya Mungu sio tena ya kitaifa, bali ni ya kiroho (k.v. Rum. 2:28-29; 4:1 6-25). Damu ya Kristo ilikuwa ni stiari ya kujitoa kisadaka (k.v. Walawi 1 -2) kwa kifo cha Masihi (k.v. TEV). Yohana mbatizaji alisema juu ya Yesu "tazama, Mwanakondoo wa Mungu aondoae dhambi za ulimwengu" (k.v. Yohana 1:29). Yesu alikuja kufa (k.v. Mwa. 3:15; Isa. 53; Marko 10:45). Pia ilikuwa ni njia ya kutetea ubinadamu wa Yesu, (k.v. Efe. 2:15) ambayo wale waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee waliikana.

**2:14** Mstari huu una kauli tatu. Ya kwanza ni kauli elekezi ya wakati uliopo. Yesu anaendelea kuwa na kutupatia amani yetu. Ya pili na ya tatu ni kauli tendaji ya hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu ("kuwafanya wote wamoja" na "kuondoa kiambaza"); yote ambayo ni muhimu yameisha kukamilishwa kuwaunganisha Wayahudi na watu wa mataifa kuwa kitu kimoja (ambalo ni kanisa).

Amani kati ya Wayahudi na watu wa mataifa inaangazia juu ya sehemu ya fasihi, Efe. 2:11-3:13. Hii ilikuwa ni siri ya injili iliyokuwa imefichwa katika zama zilizopita. Neno "amani "linarejelea

1. Amani kati ya Mungu na mwanadamu (k.v. Yohana 14:27; 16:33; Rum. 5:1 -1 1 ; Fil. 4:7,9)
2. Amani kati ya Wayahudi na watu wa mataifa, Efe. 2:14, 15, 17 (k.v. Gal. 3:28; Kol. 3:11 )

Tazama ukumbusho katika Efe. 2:15.

◙**"Yeye ndiye amani yetu,"** "Yeye ndiye" (*autos*) linasisitizwa (k.v. Efe. 2:15). Neno "amani"linamaanisha "kurejesha kile kilichokuwa kimevunjika"(upatanisho). Yesu Kristo anaitwa Mfalme wa Amani ( k.v. Isa. 9:6 na Zak. 6:12-13). Amani ya Mungu katika Kristo ina dhana mbali mbali. Tazama ukumbusho katika Efe. 2:15 na Mada

Maalum: Amani na Wakristo na amani katika Kol. 1:20.

**NASB "aliyetufanya wote kuwa kitu kimoja"**
**NKJV "aliyewafanya wote wamoja"**
**NRSV "aliyetufanya wote tuwe wamoja"**
**TEV "aliyewafanya Wayahudi na wamataifa kuwa watu wamoja"**
**NJB "aliyewafanya wawili kuwa wamoja"**

Waamini sio tena Wayahudi na watu wa mataifa, lakini wamekuwa Wakristo (k.v. Efe. 1:15; 2:15; 4:4; Gal. 3:28; Kol. 3:11). Hii ilikuwa ni siri ya Mungu iliyodhihilishwa katika Waefeso. Mara zote huu umekuwa ndio mpango wa Mungu (Mwa. 3:15). Mungu alimchagua Ibrahim ili kuchagua watu, kuchagua dunia (Mwa. 1 2:3; Kut. 19:5-6). Hii ni dhamira ya ambatani ya Agano la Kale na Agano Jipya. Tazama Mada Maalum: Ubaguzi wa kimbali katika Kol. 3:11 .

**NASB "kiambaza cha kati kilichotutenga,"**
**NKJV "kiambaza kinachotenganisha"**
**NRSV "kiambaza kinachotenganisha"**
**TEV "kiambaza kile kinachotenganisha"**
**NJB "kiambaza kilichotumika kuwatenganisha"**

Kiuhalisia huu ni "ukuta wa kati unaotenganisha."Hili lilikuwa ni neno adimu. Kimuktadha ni dhahili linarejelea kwenye sheria za Musa (k.v. mst.15). Baadhi ya watoa maoni wamedai kuwa lilikuwa ni dokezo la ukuta katika Hekalu la Herode kati ya uwanda wa watu wa mataifa na uwanda wa wanawake ambao uliwatenganisha kati ya Wayahudi na watu wa mataifa walioabudu. Maana ile ile ya kuondoa kiambaza inaonekana katika pazia la Hekalu lililopasuka toka juu mpaka chini wakati wa kifo cha Yesu (k.v. Mt. 27:51 ). Umoja sasa unawezekana. Umoja sasa ni mapenzi ya Mungu (k.v. Efe. 1:10; Efe. 4:1-10). Kwa wale wenye ujuzi hili neno linarejelea kwenye kiambaza kati ya mbingu na dunia ambalo laweza kudokezwa katika Efe.4:8-10.

**2:15**
**NASB "kuuondoa"**
**NKJV "akisha kuuondoa"**
**NRSV "ameuondoa"**
**TEV "kuuondoa"**
**NJB "kuuangamiza"**

Neno "kuuondoa"ni kipendeleo cha Paulo (k.v. Rum. 3:31; 6:6; Kol. 2:14). Kiuhalisia linamaanisha "kuwa batili na utupu"au "kutoleta madhala."Ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu. Yesu moja kwa moja ameondoa hukumu ya sheria ya kifo ya Agano la Kale (k.v. Efe. 2:16; Kol. 2:14; Ebr. 8:13).Hii haimaanishi kuwa Agano la Kale halikuvuviwa na ufunuo muhimu kwa muumini wa Agano Jipya (k.v. Mt. 5:17-19). Inamaanisha sheria sio kigezo cha wokovu (k.v. Mdo. 15; Warumi 4; Wagalatia 3; Waebrania). Agano Jipya (Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-36) linasimamia juu ya moyo mpya na roho mpya, na sio juu ya utendaji wa mwanadamu wenye utaratibu mpya wa kisheria. Sheria ilitenda kazi kwenye utakaso, na sio kwenye kupewa haki. Waamini wa Kiyahudi na waamini wa mataifa sasa wana msimamo mmoja mbele za Mungu-haki ya Kristo iliyoidhinishwa.

### MADA MAALUM: BATILI NA UTUPU (*KATARGEŌ*)

Hili neno (*katargeō*) lilikuwa ni moja ya maneno pendwa ya Paulo. Aliyatumia takribani mara ishirini na tano lakini lilikuwa na utofauti mpana.

A. Mzizi wa kiasili wa neno unatoka kwenye neno *argos* linalo maanisha
   1. Isio tendaji
   2. Isio na kazi

3. Isiotumika
4. Isiofaa
5. Isiofanya kazi

B. Neno ambani likiwa na *kata* lilitumika kuelezea
1. Isiofanya kazi
2. Isiofaa kabisa
3. Iliyo imebatilishwa
4. Lililofanyikia mbali
5. Ambalo lilikuwa halifanyi kazi kabisa

C. Limetumika mara moja tu katika Luka kuelezea lisilozaa matunda, kwa hiyo ni mti usiofaa(kama vile. Lk 13:7)

D. Paulo analitumia kwa maana ya kitamathari kwa njia mbili za msingi
1. Mungu anafanya vitu visivyotumuka ambavyo havina faida kwa mwanadamu
   a. Asili ya dhambi ya mwanadamu-Rum. 6:6
   b. Sheria za Musa ukilinganisha na ahadi ya Mungu ya "mbegu"-Rum. 4:14; 3:17;5:4,11; Efe. 2:15
   c. Nguvu za kiroho-1 Kor. 15:24
   d. "Mtu asiye wa sheria"-2 The. 2:8
   e. Mauti ya mwili– 1 Kor. 15:26; 2 Tim. 1:10 (Ebr. 2:14)
2. Mungu anaweka ktu kingine cha zamani (Agano, zama) kwa kipya
   a. Vitu vinavyohusiana na sheria za Musa – Rum. 3:3,31; 4:14; 2 Kor. 3:7,11,13,14
   b. Mshabihiano wa ndoa uliotumia sheria – Rum. 7:2,6
   c. Mambo ya zama hizi – 1 Kor. 13:8,10,11
   d. Mwili huu – 1 Kor. 6:13
   e. Viongozi wa zama hizi – 1 Kor. 1:28; 2:6

Neno hili linatafasiliwa kwa njia mbali mbali, lakini maana yake kuu ni kukifanya kitu kisichofaa, batili na utupu, kisichofanya kazi, kisicho na nguvu, lakini sio muhimu kuwa hakiishi, kilichoharibiwa au angamizwa

**NASB, NKJV "kwa mwili wake"**
**NRSV (2:14) "mwili"**
**TEV (2:14) "kwa mwili wake mwenyewe"**
**NJB (2:14) "kwa mwili wake"**

Hili linasisitiza juu ya ubinadamu wa Yesu (k.v. Kol. 1:22) kama ilivyo kwenye huduma ya kuwa mwanadamu (K.V. Efe. 4:8-10). Walimu wa uongo wenye ujuzi wangalikana yote kwa sababu ya asili ya uhai ya pande mbili kati ya roho, ambayo waliiona ni njema, na maada, walioiona kuwa ni ovu. Tazama utangulizi kwa Waefeso "usuli wa falsafa na thiolojia wa walimu wa uongo [hali ya kuwa na ujuzi wa kipekee];(k.v. Gal. 4:4; Kol. 1 :22).

◙ **"uadui"** ulinganifu wa kiumbo unaondoa "uadui" (k.v. Efe. 2:16) na "sheria za amri zilizojumuishwa kwenye tamko."agano la Kale linasema "tenda na uishi"lakini mwanadamu aliyeanguka akashindwa kuitenda sheria ya Musa. Mara moja ikavunjika, sheria za Agano la Kale zikawa laana (k.v. Gal. 3:10); "nafsi itendayo dhambi ndiyo itakayokufa" (k.v. Ezek. 18:4,20). Agano liliondoa uadui kwa kumpa mwanadamu moyo mpya, fikra mpya, roho mpya (k.v. Yer. 31:31 -34; Ezek. 36:26-27). Utendaji ukwa matokeo, na sio lengo. Wokovu ni zawadi, na sio thawabu kwa kazi iliyokwisha fanyika.

**NASB "ndiyo sheria ya amri zilizoko katika maagizo,"**
**NKJV "sheria ya amri zilizoko katika maagizo"**
**NRSV "sheria zenye amri na maagizo"**
**TEV "sheria ya Kiyahudi, ikiwa na amri na kanuni"**
**NJB "kanuni na maagizo ya sheria"**

Hii inarejelea juu ya namna ya wokovu uliofikiriwa kupatikana kwa namna ya utendaji wa sheria ya Musa (k.v.

Rum. 9:30-32; Gal. 2:15-21).

A. **MADA MAALUM: SHERIA YA MUSA NA MKRISTO**
   Sheria ni maandiko yaliyovuviwa na za milele (kama vile. Mt. 5:17-19).
B. Sheria kama njia ya wokovu ni batiri na zimeendelea kuwepo, bali mwanadamu anatakiwa kuziangalia kuwa bidii zake ni bure (kama vile. Mt. 5:20, 48; Rum. 7:7-12; Gal. 3:1na kuendelea; Yakobo 2:10).
C. Injili ya Kristo ndio njia pekee kumwendea Mungu (kama vile. Yn 14:6; Rum. 3:21; Gal. 2:15-21; Ebr. 8:12).
D. Agano la Kale bado ni la msaada kwa waamini kama yalivyo mapenzi ya Mungu katika jamii (hasa "Amri kumi"), lakini si kama njia ya wokovu (yaani., kazi yake katika utakaso na si katika kuhesabiwa haki). Madhehebu ya Israel (muundo wa dhabihu, siku takatifu, jamii na sheria za kidini) zimepitwa na wakati lakini bado zinasikika kupitia Agano la Kale. Masharti yaliyotolewa katika Mdo. 15:20 yanarejea tu kwa masuala ya ushirika, na sio kwenye wokovu.
E. Maandiko yaliyo muhimu kuhusu Agano la Kale na uhusiano wake kwa waamini wa Agano Jipya
   1. Baraza la Yerusalem la matendo 15
   2. Muhtasari wa kithiolojia wa ujumbe wa injili katika Wagalatia 3
   3. Ulinganifu wa Agano la Musa(Agano la Kale) na Agano Jipya la Yesu (Agano Jipya) ni kitabu cha Waebrania. Kinatumia aina tofauti kuelezea ubora wa Agano Jipya.
   4. Angalia Mada Maalum: Maoni ya Paulo kuhusu Sheria za Musa

◙**"ili afanye"** Kiwalishi nomino "ili afanye"ni cha msisitizo. Kusudi la Mungu la milele ni kuwaunganisha wanadamu katika wokovu (k.v. Mwa. 3:15) na ushirika ulikamilishwa moja kwa moja kupitia utendaji wa mtu ambaye ni Masihi, na sio sheria za Musa.

◙ **"mtu mpya mmoja,"** Neno hili la Kiyunani linamaanisha "mpya"katika aina, na sio muda. Watu wa Mungu sio Wayahudi, na sio watu wa mataifa, bali ni Wakristo! Kanisa ni mwili mpya, katika na kupitia kwa ajili ya Kristo (k.v. Rum. 11 :36; Kol.1:16; Ebr. 2:10).

◙ **"akafanya amani"** Hili ni neno pendwa kwa Paulo. Limetumika mara kumi na moja katika Warumi na mara saba katika Waefeso (k.v. Efe. 1:2; 2:1 4,1 5,1 7; 4:3; 6:1 5,23). Alilitumia kwa namna tatu:
1. Amani kati ya Mungu na mwanadamu, Kol. 1 :20
2. Amani dhahania na Mungu kupitia Kristo, Yohana 14:27; 16:33; Fil. 4:7
3. Amani kati ya watu, Efe. 2:11-3:13.

Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo. Kristo anaendelea kufanya amani kwa wana wa Adamu walioanguka ambao wataitika kwa toba na imani. Amani ya Kristo haijiendeshi yenyewe (kauli tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu ya Efe 2:16) bali inapatikana kwa wote (k.v. Rum. 5:12-21 ).

**2:16 "akawapatanisha"** Neno la Kiyunani linamaanisha kumsafirisha mtu toka hali moja kwenda nyingine. Inadokeza hali ya badiliko la nafasi kinzani (k.v. Rum. 5:10-11 ; Kol. 1:20,22; 2 Kor. 5:18,21 ). Katika maana ya upatanisho ni hali ya kuondoa laana ya Mwanzo 3. Mungu na,mwanadamu wamerejesha ushirika wa ndani hata katika maisha haya, katika muundo wa ulimwengu huu ulioanguka. Upatanisho huu na Mungu unaelezeka wenyewe katika ushirika mpya na wanadamu wengine na hatimaye na asili (Isa. 11:6-9; 65:25; Rum. 8:18-23; Ufu. 22:3). Uunganishaji tena wa Wayahudi na watu wa mataifa kupitia Kristo (k.v. Efe. 1:7) ni mfano mojawapo mzuri wa Mungu kuunganisha kazi katika ulimwengu wetu.

◙ **"katika mwili mmoja"** Hii stiari ya umoja imetumika katika Nyanja tofauti kwenye maandiko ya Paulo.
1. Mwili wa asili wa Kristo (k.v. Kol.1:22) au mwili wa Kristo, ambao ni kanisa (k.v. Kol.1:23; Efe. 4:1 2;5:23,30)
2. Ubinadamu wa wote Wayahudi na watu wa mataifa (k.v. Efe. 2:16)
3. Njia ya kurejelea umoja na tofauti ya karama za kiroho (k.v. 1 Kor. 12:12-13,27)

Kwa maana hiyo zote zinahusiana na #1 .

◙**"kwa njia ya msalaba"** Viongozi wa Kiyahudi walimaanisha msalaba wa Yesu kuwa laana (k.v. Kumb. 21:23). Mungu aliutumia kama njia ya ukombozi (k.v. Isaya 53). Yesu akawa "laana"kwa ajili yetu (k.v. Gal. 3:13)! Ikajakuwa ushindi wake (k.v. Kol. 2:14-15), ukiwapa waamini ushindi juu ya (1) laana ya Agano la Kale; (2) nguvu za uovu; na (3) uadui kati ya Wayahudi na watu wa mataifa.

**NASB "akiisha kuufisha huo uadui"**
**NKJV "mara akiufisha uadui"**
**NRSV "hivyo akiufisha ule uadui kwa huo"**
**TEV "Kristo aliuangamiza uadui"**
**NJB "katika mwili wake akauangamiza uadui"**

Tafasiri ya Kiingereza inaonyesha kuwa kifungu hiki kinaweza eleweka kwa namna mbili. Hii ni kwa sababu kiwakilishi nomino cha umoja chaweza kuwa uhusika wa wakati jinsia ya kike (TEV, NJB) au uhusika wa wakati ulio hasi (NASB, NRSV). Katika muktadha kinawezekana. Msisitizo wenye muktadha mpana ni juu ya kazi ya ukombozi iliyokwisha kukamilishwa.

**2:17** Hiki ni kidokezo kwa Isa. 57:19 au yumkini 52:7. Paulo, kwa kutumia ufafanuzi wa kiuanishaji, uliotumika kwenye maandiko ya Agano la Kale kwa Wayahudi waliokimbilia uhamishoni na watu wa mataifa. Hata walimu wa dini ya Kiyahudi, ukirudi nyuma kwa Isaya. 56:6, lilitumia kifungu hiki kuwarejea watu wa mataifa waliobadili itikadi.

**2:18** Kazi ya Utatu imeelezewa vizuri katika kitabu hiki (k.v. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 4:4-6). Ingawa neno "Utatu" sio neno la Kibiblia, dhana inabaki kuwa ndo yenyewe (k.v. Mt. 3:16-17; 28:19; Yohana 1 4:26; Mdo. 2:33-34,38-39; Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:9-10; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 1:21-22; 13:14; Gal. 4:4-6; Efe. 1:3-14; 2:18; 3:14-17; 4:4-6; 1 The. 1:2-5; 2 The. 2:13; Tito 3:4-6; 1 Pet. 1:2; Yuda 20-21 ). Tazama Mada Maalum katika Efe.1:3.

◙ **"sisi sote tumepata njia"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo ikimaanisha "tunaendelea kupata njia." Hii ni dhana ya Yesu binafsi kuwaleta waumini kwenye uwepo wa Mungu na kuwapa utambulisho binafsi (k.v. Rum. 5:2; pia inatumika kwa maana ya kujiamini katika Ebr. 4:16; 10:19,35).

◙**"katika roho mmoja"** Hii pia imesisitizwa katika Waefeso 4:4. Walimu wa uongo walikuwa wanasababisha utengano, lakini Roho akaleta umoja (sio kiulinganifu)!

**2:19** watu wa mataifa waliofarakanishwa (Efe. 2:11 -12) sasa wamejumuishwa kikamilifu. Hili linaelezewa vizuri kwa kutumia stiari nne za kawaida za kibiblia

1. wenyeji (mji)
2. Watakatifu (taifa takatifu lililowe kwa ajili ya Mungu)
3. Watumishi wa ndani wa Mungu (mmoja wa wanafamilia)
4. Ujenzi wa kiroho (hakalu, Efe. 2:20-22a)

◙ **"watakatifu"** Tazama Mada Maalum katika Kol. 1:2.

**2:20 "mmejengwa"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu. Msingi (k.v. Efe. 2:12) wa imani yetu umetimilizwa, na kujengwa kikamilifu juu ya Mungu wa Utatu. Habari njema ya Mungu ilitangazwa na Mitume na Manabii (k.v. Efe. 3:5).

◙**"juu ya misingi ya mitume na manabii"** Yesu aliweka msingi wa injili (k.v. 1 Kor.3:11 ). Yesu ni hekalu jipya (k.v. Yoh. 2:19-22). Agano la Kale linatoa unabii wa juu ya ujio wa ufalme wa Mungu, Roho wa Kristo-aliongoza maisha, kifo, na ufufuo ukakamilisha, na mitume wakaihubiri ile kweli. Swali pekee ni kuwa, ni yupi neno "nabii"linamrejelea? Ni manabii wale wa Agano la Kale au manabii wa Agano Jipya (k.v. Efe. 3:5;4:1 )? Agizo la

neno linadokeza manabii wa Agano Jipya (k.v. Efe. 2:3:5; 4:11), lakini kidokezo cha ki-Masihi cha Agano la Kale kwenye "jiwe kuu la pembeni" linadokeza juu ya unabii wa Agano la Kale. Sababu ya utofauti uliopo kati ya manabii wa Agano la Kale na Agano Jipya ni juu ya suala la ufunuo. Manabii wa Agano la Kale waliandika maandiko. Walikuwa ni vyombo vya Mungu vya ufunuo binafsi uliovuviwa. Hata hivyo, unabii ni karama endelevu katika Agano Jipya (1 Kor. 12:28; Efe. 4:11 ). Je uandishi wa maandiko bado unaendelea? Lazima pawepo na utofauti uliowekwa kati ya uvuvio? (mitume na manabii wa Agano la Kale) na nuru na ukarimiwaji wa karama za kiroho (waamini wa Agano Jipya waliokarimiwa).

**MADA MAALUM: UNABII WA AGANO JIPYA**

I. Sio sawa na Unabii wa Agano la Kale (BDB 611, KB 661; tazama Mada Maalumu:Unabii [Agano la Kale]), ambao una vidokezo vya upokeaji wa sheria za Kiyahudi na kunukuu mafunuo yaliyovuviwa toka kwa YHWH (kama vile Matendo 3:18, 21; Rum. 16:26). Ni manabii tu waliweza kuandika maandiko.
   A. Musa aliitwa nabii (kama vile kumb. 18:15-21)
   B. Vitabu vya historia (Yoshua – Wafalme [isipokuwa Ruthu]) waliitwa "manabii wa mwanzo" (kama vile Matendo. 3:24)
   C. Manabii wanachukua nafasi ya makuhani wakuu kama chanzo cha habari kutoka kwa Mungu. (kama vile Isaya –Malaki)
   D. Mgawanyo wa pili wa kanuni za kanisa la Kiebrania ni "Manabii" (kama vile Mt. 5:17; 22:40; Luka 16:16; 24:25, 27; Rum. 3:21).

II. Katika Agano Jipya dhana ya unabii imetumika katika njia kadhaa tofauti tofauti.
   A. Kuwarejea manabii wa Agano la Kale na jumbe zao zilizovuviwa (kama vile Mt. 2:23; 5:12 11:13; 13:14; Rum. 1:2).
   B. Kuurejea ujumbe kwa mtu mmoja badala ya kikundi kichoungana (yaani, manabii wa Agano la Kale kimsingi waliongelea juu ya Israeli).
   C. Kuwarejea wote wawili Yohana mbatizaji (kama vile Mt. 11:9; 14:5; 21:26 Luka 1:76) na Yesu kama mpiga mbiu wa ufalme wa Mungu (kama vile Mt. 13:57; 21:11, 46; Luka 4:24; 7:16; 13:33; 24:19). Yesu pia alidai kuwa mkuu kuliko manabii (kama vile Mt. 11:9; 12:41; Luka 7:26).
   D. Manabii wengine katika Agano Jipya
      1. Maisha ya awali ya Yesu kama ilivyoandikwa katika injili ya Luka (yaani., kumbu kumbu za Maria)
         a. Elizabethi (kama vile Luka 1:41-42)
         b. Zakaria (kama vile Luka 1:67-79)
         c. Simoni (kama vile Luka 2:25-35)
         d. Ana (kama vile Luka 2:36)
      2. Ubashiri wa kejeli (kama vile. Kayafa, Yohana 11:51)
         a. Inarejea juu ya mtu anayeitangaza injili (ikijumuishwa kwenye orodha ya kipawa cha utangazaji katika 1 Kor. 12:28-29; Efe. 14:11)
         b. Ikirejea juu ya vipawa vinavyoendelea kanisani (kama vile Mt. 23:34; Matendo 13:1; 15:32; Rum. 12:6; 1 Kor. 12:10, 28-29; 13:2; Efe. 4:11) wakati mwingine hii inaweza kumaanisha kwa wanawake (kama vile Luka 2:36; Matendo 2:17; 21:9; 1 Kor. 14:4-5).
         c. Ikirejea kwa sehemu mafunuo ya kitabu cha ufunuo (kama vile Ufu. 1:3; 22:7, 10, 18,19)

III. Manabii wa Agano Jipya

   A. Hawatoi ufunuo uliovuviwa kwa maana sawa kama manabii wa Agano la Kale waliofanya (yaani mafundisho ya Biblia). Usemi huu unawezekana kwa sababu ya Matumizi ya kifungu cha neno "Imani" (yaani., kwa maana ya injili iliyokamilika) iliyotumika katika Matendo 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; 6:10; Flp. 1:27; Yuda 3, 20.

   Dhana hii iko wazi kutokana na fungu kamili la maneno lililotumika katika Yuda 3, "imani ya mara moja pasipo kujirudia imekabidhiwa kwa watakatifu." Imani ya "jumla pasipo kujirudia" inarejerea kwenye ukweli, mafundisho, dhana, maoni ya dunia juu ya mafundisho ya ukristo.

Msisitizo huu unaotolewa mara moja tu ni msingi wa Kibiblia kwa ajili ya kuzuia uvuvio ulio wa kithiolojia wa maandiko ya Agano Jipya na pasipo kuruhusu maandiko mengine kufikirika kimafunuo (angalia Mada Maalumu: Uvuvio). Kuna maeneo mengi yenye utata, yasiojulikana katika agano jipya (Tazama Mada Maalumu: Fasihi za mashariki [mafumbo ya Kibiblia]), lakini waamini wanathibitisha kwa imani kuwa kila kitu "kinachohitajika" kwa ajili ya imani na utendaji inajumuishwa ikiwa na utosherevu wenye uwazi wa kutosha katika Agano Jipya. Dhana hii inaelezwa kama "ufunuo pembe tatu."

1. Mungu amejidhihirisha mwenyewe katika historia kwa muda muafaka (UFUNUO)
2. Amechagua baadhi ya waandishi wa kibinadamu kuweka kumbu kumbu na kuelezea matendo yake (UVUVIO).
3. Alimtoa Roho Wake ili kufungua mawazo na mioyo ya watu wapate kuyaelewa maandishi haya, si kwa ubora tu bali kwa utoshelevu wa wokovu na maisha ya Mkristo yenye kufaa (NURU, tazama Mada Maalumu: nuru). Hoja iliyopo hapa ni kuwa uvuvio umewekewa ukomo kwa waandishi wa neno la Mungu. Hakuna maandiko mengine, maono au mafunuo yenye mamlaka. Sheria za kanisa zimefungwa. Tuna ukweli wote tunaouhitaji ili kuitikia vizuri kwa Mungu. Ukweli huu unaonekana vizuri katika makubariano ya waandishi wa Kibiblia dhidi ya waumini watiifu wa ki-Mungu wasiokubali. Hakuna mwandishi au mnenaji wa kisasa aliye na kiwango cha uongozi wa ki-Uungu kama ambao waandishi wa neno la Mungu waliokuwa nacho.

B. Kwa namna nyingine manabii wa Agano Jipya ni sawa na wale wa Agano la Kale.

1. Utabiri wa matukio yajayo (kama vile Paulo, Matendo 27:22; Agabo, Matendo 11:27-28; 21:10-11; manabii wengine wasiotajwa Matendo 20:23).

1. Kutangaza hukumu (kama vile Paulo, Matendo 13:11; 28, 25-28)
2. Dalili za matendo ambayo dhahili yanaonyesha matukio (kama vile Agabo Matendo 21:11).

C. Mara zote wananena kweli ya injili, wakati mwingine kwa njia ya utabiri (kama vile Matendo 11:27-28; 20-23; 21:10-11) Lakini kimsingi huu sio mtazamo wenyewe. Unenaji wa unabii katika Wakorinto wa 1 kimsingi unaibainisha injili (kama vile 1 Kor. 14:24,39).

D. Ni Roho wa wakati ule ule akimaanisha kudhihirika wakati ule ule na utumiaji wa kiutendaji wa kweli ya Mungu kwa kila hali, tamaduni mpya au kipindi cha muda (kama vile 1 Kor. 14:3).

E. Walikuwa imara katika makanisa ya mwanzo ya Paulo (kama vile 1 Kor. 11:4-5; 12:28, 29;13:2, 8, 8,9; 14:1 3,4,5,6,22,24,29,31,32,37,39; Efe. 2:20; 3:5; 4:11; 1 The. 5:20) na wametajwa katika *Didache* (iliyoandikwa katika karne ya mwisho au karne ya pili tarehe haijulikani) na wakati wa mienendo ya Kikristo ya karne ya pili na tatu katika Afrika ya kaskazini.

IV. Je karama za Agano Jipya zimekoma?

A. Swali ni gumu kulijibu. Linasaidia kufafanua jambo kwa kuelezea kusudi la karama. Je wanamaanisha kuthibitisha mafundisho ya awali ya kuhubiri injili au ni njia endelevu ya kanisa kujihudumia lenyewe kwenye ulimwengu ulipotea?

B. Je mmoja aweza kuangalia kwenye historia ya kanisa kujibu maswali au Agano Jipya lenyewe? Hakuna kiashirio chochote kinachoonyesha katika Agano Jipya kuwa karama za rohoni zilikuwa za muda tu. Wale wote wanaojaribu kutumia 1 Kor 13:8-13 kuelezea habari hii wanatukanisha kusudi la mwandishi wa aya hii, ambayo inadokeza kuwa kila kitu kitatoweka isipokuwa upendo.

C. Nathubutu kusema kuwa tangu Agano Jipya, si historia ya kanisa, ndiyo yenye mamlaka,

waamini wanapaswa kuthibitisha kuwa karama zinaendelea. Hata hivyo ninaamini kuwa mila zinaathiri tafsiri za maandiko. Baadhi ya maandiko yalioko wazi hayatumiki tena (yaani busu takatifu, Baibui, makanisa kukutana nyumbani n.k). kama mila zinaathiri maandiko, hivyo kwa vipi zisiathiri historia ya kanisa?

D. Hili ni swali ambalo haliwezi kujibiwa. Baadhi ya waumini wanatetea kuwepo na"ukoma" na wengine watetea "kusiwepo na ukomo". Katika eneo hili,kama ilivyo kwa mambo mengi yaliyo fasiliwa, moyo wa mwamini unabaki kuwa ndo kiini. Agano jipya ni tata na la kitamaduni zaidi. Ugumu unaweza kuamua ni maandiko yapi yanaathiliwa na mila/historia na yapi yanaathiriwa kwa wakati wote na yapi kwa mila (cf. Fee na Stuart, *How to read the Bible for all its Worth,* kur. 14-19 na 69-77 hapa ndipo pale mjadala wa uhuru na kuwajibika, unaopatikana katika Warumi 14:1-15, 13 na Kor. 8-10 unapokuwa wenye umuhimu mkubwa. Namna tunavyojibu swali ni muhimu katika njia mbili.

1. Kila mwamini anapaswa kutembea katika imani yake kwa mwanga walio nao. Mungu anaona mioyo yetu na nia.
2. Kila mwamini yampasa aruhusu waamini wengine kutembea katika uelewa wa imani. Lazima pawepo na uvumilivu ndani ya mipaka ya kibiblia. Mungu anatutaka tupendane kama anavyotupenda.

E. Kwa kuhitimisha suala hili, Ukristo ni maisha ya imani na upendo, na sio tu thiolojia kamili. Uhusiano wetu na Yeye unaosababisha kuwepo na uhusiano na wengine ni muhimu zaidi kuliko habari au imani kamili.

◙ **"jiwe kuu la pembeni"** Hii ni sitiari ya ki-Masihi ya Agano la Kale (k.v. Isa. 28:16; Zab. 11 8:22; 1 Pet. 2:4-8). Katika Agano la Kale uthabiti wa Mungu, nguvu na ustahimilivu mara nyingi vinaonyeshwa katika "mwamba" kama"wadhifa (k.v. Kumb. 32:4, 15,18, 30; Zab. 18:2, 31, 46; 28:1 ; 31:3; 42:9; 71:3; 78:15). Sitiari ya Yesu kama jiwe.

1. Jiwe lililokataliwa - Zab. 118:22
2. Jiwe la kujengea - Zab. 118:22; Isa. 28:16
3. Jiwe la kujikwaa - Isa. 8:14-15
4. Jiwe la ushindi (ufalme - Dan. 2:45)
5. Yesu alitumia vifungu hivi kujielezea mwenyewe (k.v. Mt. 21:42; Marko 12:10; Lk. 20:17).Alikuwa ni kipengele muhimu cha ujengaji kilichoachwa katika taratibu za ibada na ushikaji wa sheria wa Agano la Kale (k.v. Isa. 8:14).

**MADA MAALUM: JIWE KUU LA PEMBENI**

I. Matumizi ya Agano la Kale
   A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu mkinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
   B. Alafu baadae lilikuzwa kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanza 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).
   C. Neno "jiwe" au "mwamba" lilikuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 KUTENGENEZA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).
   D. Hii ilikuzwa mpaka kuwa sitiari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).
      1. linalowekwa la kwanza, ambalo lililuwa linahakikisha usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia liliitwa" jiwe kuu la pembeni"
      2. Ingeweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama

vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), liliitwa "jiwe kifuniko," kutoka katika Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)

3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya njia ya kuingilia na kushikilia uzito wa jengo la kuta nzima.

II. Matumizi ya Agano Jipya

A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko 12:10-11; Luka 20:17)

B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiunganisha kukataliwa kwa YHWH na Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)

C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 kama urejereo kwa Kristo

D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.

III. Kauli za Kithiolojia

A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wangelitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliharibiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!

B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katik muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa binafsi na wa kiungu pamoja na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, kuelekezwa kwa uyahudi.

C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).

D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).

E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani the Alfa na Omega). Bado, pia jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na ardhi nyingine ya kati hapa!

**2:21-22** Wazo la pamoja la watu wa Mungu linaonekana katika Efe. 2:19 (mara mbili), 21 na 22 lilielezewa katika hali ya uwingi "watakatifu."Kuokolewa ni kuwa miongoni mwa familia, jengo, mwili, hekalu (k.v. Efe.1:23; 4:16; Kol. 2:19). Dhana ya kanisa kama hekalu imeelezewa katika 1 Kor. 3:16-17. Huu ni msisitizo juu ya asili ya ushirika wa kanisa. Dhana binafsi imeelezewa katika 1 Kor. 6:16. Yote ni kweli! Yesu ni hekalu jipya, k.v. Yohana 2:19-22. kitenzi katika Efe. 2:21-22 pia kina mtizamo wa ushirika. Kina neno ambatani *syn* linalomaanisha "ushirika wa pamoja."Zote ni kauli tendwa za wakati uliopo. Mungu anaendelea kujenga/kuongeza Kanisa Lake. Kuna tatizo la machapishi ya Kiyunani yanayohusiana na kifungu hiki "kanisa zima."Machapisho ya herufi kubwa ya kale א*, B, D, F na G hayana kibainishi, wakati אc, A, C, na P yanacho. Swali ni kuwa, Paulo alikuwa akirejelea juu ya jengo moja kubwa (NASB, NKJV, NRSV, NIV, TEV, REB) au majengo mengine madogo madogo (ASV, NJB, Phillips) yaliyoungana kwa namna Fulani? United Bible Society's chapisho la 4 la neno la Kiyunani linaipa alama "B" ambayo inaonyesha "kiwastani ina uhakika" kuwa inarejea kwenye jengo moja. Jengo hili moja bado halijaisha. Liko kwenye mchakato wa ukuaji. Stiari ya jengo inadokeza kwenye hekalu la kiroho (watu wa Mungu).

**MADA MAALUMU: ADILISHA**

Neno hili oikodomeō na muundo wa maneno yake mengine yanatumiwa mara kwa mara na Paulo. Kidhahiri lilimaanisha "kujenga nyumba" (kama vile Mt. 7:24), lakini lilikuja kutumika kisitiari kwa:

1. Mwili wa Kristo, kanisa, 1 Kor. 3:9; Efe. 2:21; 4:16

2. Kujenga
    a. ndugu wadhaifu, Rum. 15:1
    b. majirani, Rum. 15:2
    c. ninyi kwa ninyi, Efe. 4:29; 1 Wathesalonike 5:11
    d. watakatifu kwa ajili ya huduma, Efe. 4:11
3. tunajenga au kuonya kwa
    a. upendo, 1 Kor. 8:1; Efe. 4:16
    b. kuweka mipaka juu ya uhuru binafsi, 1 Kor. 10:23-24
    c. kukwepa kudhaniwa, 1 Tim. 1:4
    d. kuweka mipaka ya wazungumzaji katika huduma za kuabudu (waimbaji, walimu, manabii, wanenaji kwa lugha, na wakalimani), 1 Kor. 14:3-4,12
4. vitu vyote sharti vionywe
    a. mamlaka ya Paulo, 2 Kor. 10:8; 12:19; 13:10
    b. kauli za kimutahsari katika Rum. 14:19 na 1 Kor. 14:26

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Watu wote wamefarakanishwa na Mungu
2. Wanadamu wana sehemu muhimu katika wokovu wao?
3. Kwa nini muungano wa Wayahudi na watu wa mataifa ni wa muhimu?
4. Ni kwa namna gani Yesu aliifanya sheria kuwa “batili na utupu”?
5. Sheria ya Mungu ni ya milele? Ni kwa vipi wakristo wanahusiana na sheria ya Musa na Agano lote la Kale
6. Kwa nini Paulo anasisitiza stiari ya jengo katika Efe. 2:19-23?

# WAEFESO 3

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Huduma ya Paulo kwa Mataifa | Ile Siri Iliyofunuliwa | Ombi kwa ajili ya Hekima | Kazi ya Paulo kwa Mataifa | Paulo, Mtumishi wa Siri |
| 3:1-13 | 3:1-7 | 3:1-6 | 3:1-6 | 3:1-13 |
| | Kusudi la hiyo Siri | 3:7-13 | 3:7-13 | |
| | 3:8-13 | | | |
| Kuufahamu upendo wa Kristo | Ukubalifu wa ile Siri | | Upendo wa Kristo | Ombi la Paulo |
| 3:14-19 | 3:14-21 | 3:14-19 | 3:14-19 | 3:14-19 |
| 3:20-21 | | 3:20-21 | 3:20-21 | 3:20-21 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (**Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo, linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya tatu
8. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA 3:1-21

A. Kwa kuzingatia sababu zile za kitheolojia za barua ya Paulo ya kimzunguko inayojulikana kama ya Waefeso, ni dhahiri kwamba zile kweli kuu tatu za Paulo katika sehemu ya mafundisho zinahusiana na ujuzi wa walimu wa uongo. (Tazama Utangulizi.)
   1. Efe. 1 inamsifu Baba kwa ajili ya pendo lake la "kabla" lililodhihirishwa katika ule upatanisho mbadala wa Kristo na ule uwepo mwendelezo wa Roho.
   2. Efe. 2:1-10 hulifunua lile pendo la Baba lililo kuu na huruma kwa mwanadamu aliyeanguka, asiye na msaada.

3. Efe. 2:11-3:13 hufunua ule mpango wa milele wa Mungu kwa ajili ya kuwaweka pamoja wanadamu wote katika wokovu wa bure kupitia Kristo (kama vile Mwa. 3:15), Myahudi na Myunani, mwanamume na mwanamke, mtumwa na mtwana.

   Kwa hiyo, Efe. 2:11-3:13) hufunua ule mpango wa Mungu wa milele, kwa wote (tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi wa Milele); Efe. 2:1-10) hufunua ule moyo wa upendo wa Mungu na Efe. 1:3-14) hufunua kusudi la Mungu la milele, ufanano wa mwanadamu na Kristo. Mungu aliutambua kwa ukamilifu sana uasi wa mwanadamu na alitengeneza mipango kwa kushughulika na tatizo, hata kabla ya uumbaji (kama vile Efe. 1:4).

B. Efe. 2:11-22 na 3:2-13 zinaeleza bayana moja ya ufafaniuzi kadhaa wa siri za Mungu zinazopatikana katika maandiko ya Paulo. Myahudi na mtu wa Mataifa waliungana katika mwili mpya, ambao ni Kanisa la Yesu Kristo. Mada Maalum katika Efe. 3:3

C. Paulo anaanza na maombi ya sifa katika Efe. 3:1, lakini alikwepa kuizungumzia huduma yake kwa Mataifa na anaanza maombi yake katika mistari ya 14-21.

D. Lile ombi ambalo lilianza katika mstari 1 na kumalizikia katika Efe. 3:14-21 inaligawa ombi hili katika ibara tatu. (Tazama maelezo kamili katika Efe. 3:16-19)
   1. Waamini hupokea nguvu ya ndani, Efe. 3:16-17a
      a. kwa nguvu ya Roho
      b. kupitia Kristo aishie ndani
   2. Watakatifu wanaweza kuielewa kwa ukamilifu ile kweli ya injili na ile siri, Efe. 3:17b-19a
      a. kupokea kwa ajili ya kushikiria
      b. kujua kwa uzoefu
   3. Waamini wamejazwa kwa ukamilifu (*plērōma*) wa Mungu, Efe. 3:19b

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAEFESO 3:1-13**
**1Kwa sababu hiyo mimi Paulo ni mfungwa wake Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi Mataifa; 2ikiwa mmesikia habari ya uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu; 3 ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. 4 Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. 5Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho; 6 ya kwamba Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili; 7Injili hiyo ambayo nalifanywa mhudumu wake, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa kadiri ya utendaji wa uweza wake. 8 Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nalipewa neema hii ya kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika; 9na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote; 10 ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; 11 kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu. 12 Katika yeye tunao ujasiri na uwezo wa kukaribia katika tumaini kwa njia ya kumwamini. 13 Basi naomba msikate tamaa kwa sababu ya dhiki zangu kwa ajili yenu, zilizo utukufu kwenu.**

**3:1 "Kwa sababu hiyo"** Waefeso 3:2-13 ni mwendelezo wa kitheolojia wa Efe. 2:11-22. Paulo anakirudia kifungu hiki katika Efe. 3:14, pale anapoyaelekeza maombi yake kwa Mungu. (Baada ya maoni ya 2:2-13 kuhusu wito na huduma yake kwa Mataifa).

◙**"mfungwa wake Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi Mataifa"** Wakati Paulo alipoandika kitabu hiki alikuwa amefungwa huko Roma kwa sababu ya mgomo huko Yerusalemu (kama vile Mdo. 21:27-22:22). Mgomo ulitokea

pale Wayahudi walipomshtaki Paulo kwa kumchua Trophimo, yule Mtu wa Efeso aliyeongoka, katika Hekalu. Wayahudi walimfahamu yeye kama mtu wa Mataifa na walimtenda uovu (kama vile Efe. 2:14). Paulo aliusikia wito maalum kwa Mataifa (kama vile Efe. 3:2,8; Matendo 9:15; 22:21; 26:16,18; Rum. 11:13;15:16; Gal. 1:16; 2:9; 1 Tim. 2:7; 2 Tim. 4:17).

**3:2 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza ambayo inadhahaniwa kuwa ya kweli kutokana na matazamo wa mwandishi ama yale makusudi yake ya kiuandishi. Mistari ya 2-7 inaunda tungo moja katika Kiyunani. Hawa waamini wameisikia huduma na wito wa Paulo. Paulo hakuwa mwanzilishi wa makanisa yote katika Asia Ndogo.

◙**" uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu"** Paulo alijisikia kama mwenye kukabidhiwa injili (kama vile Efe. 3:9; 1 Kor. 4:1-2; 9:17; Gal. 2:7; Kol. 1:25; 1 The. 2:4; 1 Tim. 1:11; 1 Pet. 4:10). Neema ya Mungu alimjia Paulo kama kipawa, mist.7-8, na kama uwakili, Efe. 3:2. Huu ni mtazamo pacha wa agano la Mungu. Kama ilivyo kawaida, waamini wote wamekirimiwa kupitia yule Roho (kama vile 1 Kor. 12:7, 11; Efe. 4:7) na kutangaziwa uwakili wa lile Agizo Kuu (kama vile Mt. 28:19-20). Huu si Uchaguzi Mkuu! Huu ni vyote uinjilisti na ukomavu wa ufanano wa Kristo. Haiwezekani kuwa wakili mwema na mwenye imani pasipo kuitambaua kazi!

**3:3" kwa kufunuliwa"** Hili linaweza kurejelea juu ya

1. uzoefu wake akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:3-8; 22:6-11; 26:12-18)
2. Mafundisho ya Anania katika Dameski (kama vile Mdo. 9:10-19; 22:12-16)
3. maono yake katika Yerusalemu (kama vile Mdo. 22:17)
4. Kufundishwa kwa Paulo kupita Yesu aliyepaa na kutukuzwa huko Arabuni (kama vile Gal. 1:12, 17-18)

◙ **"siri hiyo"** Paulo alitumia neno "siri" mara ishirini kwa maana mbalimbali. Mara nyingi hili linahusiana na namna na sababu ya ule umoja wa kuamini kwa Wayahudi na Mataifa katika jumuiya mpya, kanisa (kama vile Efe. 2:11-3:13; Kol. 1:26-27).

**MADA MAALUM: MPANGO WA MUNGU JUU YA UKOMBOZI, "SIRI"**

Katika Agano la Kale

Neno la kiaramaiki (BDB 1112, KB 1980), raz, humaanisha "kuficha," "kufanya siri." Danielinatumika mara kadhaa katika Danieli (kama vile Danieli 2:18,19,27,28,29,30,47; 4:9). Inakuwa dhamira kuu katika maandishi ya nyakati za mwisho na inatajwa mara kadhaa katika magombo ya bahari ya chumvi. Mungu anafunua shauri lake lililofichika kwa manabii (kama vile Mwanzo 18:17; Yeremia 23:18; Danieli 9:22; Amosi 3:7).

Katika jamii ya magombo ya bahari ya chumvi ufunuo wa Mungu uliingiliwa kupitia (1) ujumbe wa manabii wa Agano la Kale (raz), lakini pia (2) ukalimani (pesher) wa "mwalimu wa haki." Taratibu za upande mbili za ufunuo na ukalimani wenye tabia za maandiko ya siku za mwisho.

II. Katika Injili nne "siri" inatumika katika maarifa ya kiroho yatokanayo na mafumbo ya Yesu.

1. Marko 4:11
2. Mathayo 13:11
3. Luka 8:10

III. Paulo analitunia katika njia kadhaa tofauti tofauti.

1. Kufanya mioyo ya Israeli kuwa ngumu kuruhusu Mataifa kujumuishwa. Huku kujumuishwa kwa mataifa kutafanya kazi kama mbinu kwa Wayahudi kumkubali Yesu kama Kristo wa unabii (kama vile Rum. 11:25-32).
2. Injili kuifanya ijulikane kwa mataifa kwa kuwaambia kwamba wanajumuishwa katika Kristo na kupitia

Kristo, (kama vile Rum. 16:25-27; Kol. 2:2).

3. Miili mipya ya waamini wakati wa kuja kwa mara ya pili (kama vile 1 Kor. 15:5-57; 1 The. 4:13-18).
4. Kuhitimishwa kwa mambo yote katika Kristo (kama vile Efe. 1:8-11).
5. Mataifa na Wayahudi kama warithi wenza (kama vile Efe. 2:11-3:13).
6. upendo wa kimahusiano ya karibu kati ya Kristo na kanisa unaoelezwa katika maneno ya kindoa (kama vile Efe. 5:22-33).
7. Mataifa yalijumuisha watu wa agano na kuishi kwa Roho wa Kristo ili kuweza kutengeneza makuzi ya kufanana na Kristo ya kwamba kurejesha taswira ya Mungu kwa mwanadamu (kama vile Mwanzo 1:26-27; 5:1; 6:5,11-13; 8:21; 9:6; Kol. 1:26-28).
8. Mwisho wa Mpinga Kristo (kama vile 2 The. 2:1-11).

IV. Tenzi za kanisa la kwanza au Katekisimu kuhusu siri za injili zinapatikana katika 1 Tim. 3:16.

V. Katika Ufunuo wa Yohna inatumika maana ya Yohana ya ishara za siku za mwisho.

**NASB "kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache "**
**NKJV "(kama nilivyoandika kabla katika maneno machache)"**
**NRSV "kama nilivyoandika juu ya hili katika maneno machache"**
**TEV "(kama nimeandika kwa ufupi juu ya jambo hili. . .)"**
**NJB "kama nilivyoeleza kwa ufupi sana"**

Yule mleta mabadiliko mkuu, John Calvin, alifikiri kuwa hii aya ilirejerea kile alichokiandika Pauo katika barua ya awali,lakini ingekuwa vizuri zaidi kuelewa kwa kurejelea sehemu ya awali ya Waefeso, bila shaka 2:11-22. Haya matumizi haya ya kawaida ya njeo ya wakati uliopita usio timilifu unaitwa waraka wa wakati uliopita usiotimilifu.

**3:4 "myasomapo"** Bila shaka hili linarejelea juu ya ule usomaji wa hadharani wa barua za Paulo katika makanisa (kama vile Kol. 4:16; 1 The. 5:27; Ufu.1:3). Kumbuka kwamba barua ya Waefeso ilikuwa ya kimzunguko.

**3:5**
**NASB "katika vizazi vingine"**
**NKJV "katika zama zingine"**
**NRSV "katika vizazi vilivyopita"**
**TEV "katika nyakati zilizopita"**
**NJB "katika kizazi kilichopita"**

Sasa Mungu anaufunua dhahiri mpango Wake wa zama za kale za ukombozi wa mwanadamu (kama vile 1 Kor. 2:6-9; Kol.1:26a), Myahudi na Myunani, tajiri na maskini, mtumwa na mtwana, mume na mke (kama vile 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28).

◙**"hawakujulishwa. . kama walivyofunuliwa"** Hivi vitenzi tendewa viwili, ambavyo vinaonyesha matendo ya Mungu katika ufunuo wa hii kweli kuu kabla ya wakati (1:3-6), katika wakati (1:7-12), na kupitia huo wakati (1:13 14).Waamini wa Agano Jipya wanafahamu zaidi kuhusu Mungu na mpango Wake na Masihi Wake kuliko mtu wa Agano la kale!

◙**"mitume wake watakatifu na manabii"** Kifungu hiki pia kinapatikana katika Efe. 2:20; 4:11. Hawa ni "watakatifu" kwa kuwa wametengwa kwa ajili ya kazi ama kusudi maalum. Hili linarejelea kwa wale manabii wa Agano Jipya (tazama Mada Maalum katika Efe.2:20, kama vile Efe 4:11; Matendo 11:27; 13:1; 15:32; 21:9,10; 1 Kor. 12:28; 14:1-40). Makundi yote, Mitume na manabii (pamoja na wainjilisti na wachungaji/walimu, kama vile Efe. 4:11), waliitangaza hii siri mpya ya injili iliyofunuliwa, ambapo Myahudi na Mtu wa Mataifa aaminiye wameunda mwili mpya, ambalo ni kanisa.

**3:6**
**NASB "Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi"**

**NKJV** **"yawapasa Mataifa kuwa warithi pamoja nasi, wa mwili mmoja, na washiriki wa ile ahadi yake"**
**NRSV** **"Mataifa wamekuwa warithi pamoja nasi, washirika wa mwili mmoja, na wenye kushiriki katika ahadi"**
**TEV** **"Mataifa wana sehemu pamoja na Myahudi katika Baraka za Mungu; ni washirika wa mwili mmoja, na wenye kushiriki katika ahadi.**
**NJB** **"watu wasiomjua Mungu sasa wanashiriki urithi ule ule, kwamba hawa ni mwili mmoja, na kwamba ahadi imehaidiwa kwao"**

Ni ufunuo namna gani wenye kushangaza wa zama kale ya siri za mpango wa Mungu wa ukombozi. Katika Kristo hakuna Myahudi tena wala Myunani (kama vile Rum. 2:28-29; 3:22; 10:12; 1 Kor. 12:13; Gal. 3:7-9, 28-29; Kol. 3:11). Neno hili hili, "warithi pamoja nasi," pia linatumika katika Rum. 8:17;Ebr. 11:9 na 1 Pet. 3:7. Hapa kuna uambatani wa aina tatu za neno *syn*: (1) "warithi pamoja nasi"; (2) "wa mwili mmoja"; na (3) "washiriki wa ile ahadi." Paulo mara nyingi anatumia huu uambatani wa aina tatu wa neno *syn* kuyaelezea maisha mapya ya mwamini katika Kristo. Hili linafanana sana na ule uambatani wa aina tatu pamoja na neno *syn* katika Efe. 2:5-6.

## MADA MAALUM: MPANGO WA YHWH WA UKOMBOZI WA MILELE

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Jer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31),wale wote walio umbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israel, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.
Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anauanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani., iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israel. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihilisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Abraham, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakfisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
    a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
    b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19

c. Mika 4:1-3
d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa “agano jipya” (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna “moyo mpya,” “mawazo mapya,” na “roho mpya.” Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimalisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani., ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni “fumbo la Mungu,” lililofichika lakini sasa limedhihilishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya linaangazia juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israel ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumai utapata wasaa wa kusoma Mada Maalum: kwa nini ahadi za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti toka ahadi za Agano Jipya. Waweza kupata katika mtandao www.freebiblecommentary.org.

**3:7** Aya hii ingewaza kurejelea ule ukombozi wa Paul'o wa awali, lakini katika muktadha huu inaonekana kurejelea kile kipawa maalum cha Mungu kwa umisheni wa kitume kwa Mataifa (kama vile Efe. 3:2; 6:20; Rum. 12:3; 15:15-16; 1 Kor. 3:10; 15:10; Gal. 2:9; kol. 1:25).

◙"**mhudumu**" Tunalipata neno la Kiingereza "shemasi" kutokana na kitenzi jumuishi cha Kiyunani kinachohusu mhudumu (*diakoneō*, kama vile Mt. 8:15 ama *diakonia*, kama vile Efe. 4:12).

◙ "**utendaji wa uweza wake**" Wokovu na huduma yenye nguvu ni vya Mungu, si Paulo (kama vile Efe. 1:19; Kol. 1:29).

**3:8-12** Hii ni moja ya tungo ya Kiyunani. Hizi tungo ndefu ndizo sifa za Waefeso.

**3:8 "mdogo wa watakatifu wote"** Kiuhalisia hii ni "ndogo zaidi," ambacho ni sifa ya juu linganishi (kama vile1 Kor. 15:9; 1 Tim. 1:15). Paulo alinyenyekeshwa na maisha yake ya awali ya haki ya kidini, na mateso ya shari. Pia alishangazwa na lile pendo la Mungu kwa huyu mtesi wa kanisa Lake. Tazama Mada Maalum: Watakatifu katika Kol. 1:2.

**NASB “siopimika"**
**NKJV "isiyochunguzika"**
**NRSV "isiyo na mwisho"**
**TEV, NJB "usiopimika"**

Lile neno la nguvu ya utajiri wa Mungu katika Kristo (kama vile Rum. 11:33 na tafsiri ya Maandiko ya kale ya Kiyunani ya Ayubu 5:9; 9:10). Mwanadamu hawezi kumjua Mungu, bali Mungu amechagua kujifunua Mwenyewe.

◙" **utajiri wake Kristo**" "utajiri" ni moja ya maneno aliyoyapenda Paulo (kama vile Efe 1:7, 18; 2:4,7; 3:8,16). Katika sura ya 1 alizungumzia ule utajiri wa Mungu Baba. Hapa Paulo anauhamishia kwa Mwana! Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi wanadokeza ule Uungu wa Yesu kwa kumhamishia majina na kazi ya YHWH (mfano tazama "Mungu Mwokozi wetu"na "Kristo Yesu Mwokozi wetu" katika Tito 1:3 na 1:4; 2:10 na 2:13; 3:4 na 3:6).

**3:9**
**NASB "kuwaangaza"**

**NKJV "kuwafanya watu wote waone"**
**NRSV "kumfanya kila mtu aone"**
**TEV "kuwaangazia watu wote waone"**
**NJB "kufafanua"**

Kiuhalisia hili neno ni "kuwaangazia"(Efe. 1:18; Mdo. 26:18; 2 Kor. 4:6; 1 Pet. 2:9). Ni Roho pekee awezaye kuleta ufunuo kwa moyo wenye giza (kama vile Yohana1:4-5; 6:44, 65). Tunalipata neno la Kiingereza "picha" kutokana na neno la Kiyunani.

**NASB "madaraka ya siri hiyo"**
**NKJV " ushirika wasiri hiyo"**
**NRSV "mpango wa siri hiyo"**
**TEV "mpango wa Mungu wa siri uliofichika unavyotekelezeka"**
**NJB "namna siri ilivyoachiliwa"**

Kiuhalisia huu ni "utumishi wa nyumbani (*oikonomia*)." Hili ni moja ya maneno aliyoyapendelea Paulo kuhusu mpango wa Mungu wa ukombozi wa milele katika Kristo kwa watoto wote wa Adamu (kama vile Efe. 1:10; 3:2,9; Kol. 1:25). Kuna tatizo la machapisho ya Kiyunani ya neno "uwakili" dhidi ya "ushirika." "Uwakili" unapatikana katika Uk.46, maandiko yote ya herufi kubwa, machapisho machache zaidi, matoleo yote ya kale, na zile nukuu za makasisi wa kanisa la kale, kwa hiyo, "uwakili" ni neno asilia. Tazama mjadala wa uhakiki wa tofauti za kiuandishi katika Kiambatisho cha Pili. Kwa neno "siri" tazama Mada Maalum katika Efe. 3:3.

◙"**Mungu aliyeviumba vitu vyote**" Hii inakanusha pande mbili za wale wenye ujuzi wa kipekee kati ya maada na roho (kama vile Efe.2:10). Katika ufanano wa ki-Kolosai, Yesu anatambuliwa kama wakili wa Mungu Baba katika uumbaji (kama vile Yohana 1:3, 10; Rum. 11:36; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:15-16; Efe. 1:2-3; 2:10).

**3:10**
**NASB, NKJV "hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingI"**
**NRSV "hekima ya Mungu iliyo katika utajiri wake mbalimbali"**
**TEV "hekima ya Mungu, katika muundo wake mbalimbali"**
**NJB "namna kulivyo kuitambua hekima ya Mungu"**

Hili neno ambatani lenye mkazo juu ya hekima ya Mungu "iliyochanganywa kwa namna mbali mbali". Katika 1 Pet. 1:6 hili linarejelea yale mateso yaliyofungamana na mwanadamu na katika 1 Pet. 4:10 hili linarejelea zile neema za Mungu fungamano. Hii kweli ya Mungu yenye sura nyingi inaweza kuonekana kwa ubora zaidi katika nyimbo za Paulo za kumsifu Mungu katika Rum. 11:33-36 na Efe. 3:18-21.

◙" **kanisa**" *Ekklesia* lilitumika katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani (LXX) kutafsri neno la Kiebrania "kusanyiko (*qahal*) la Israeli" (kama vile Kut. 12:6; 16:3; Hes. 20:4; Mambo ya Walawi. 4:13). Hii ni moja ya matumizi kadhaa ya hili neno katika Waefeso (kama vile Efe. 1:22; 3:10, 21; 5:23, 24, 25, 27, 29, 32). Paulo analiita kanisa mwili wa Kristo sehemu zote katika Efe. 1:22-23 na Wakolosai 1:24. Kanisa la mwanzo lilijiona kama watu wa Mungu wa kweli wa
Agano la Kale pamoja na Yesu Kristo Masihi kama Kichwa.

Moja ya uhusiano wa kimaandishi usio wa kawaida kati ya Waefeso na Wakolosai ni kwamba katika Waefeso hili neno kiulimwengu linalirejelea kanisa (kama vile Mt. 16:18; Gal. 1:13), ambapo katika Wakolosai mara nyingi hili lina rejelea lile kanisa la mahali (1 Kor. 10:32; 12:28; 15:9; Gal. 1:12; Flp. 3:6). Hoja hizi zinaihusu Waefeso kama barua ya mzunguko.
Tazama Mada Maalum katika Kol. 1:18.

◙"**ijulikane**" Malaika walichukua muda kuufahamu mpango wa Mungu (kama vile 1 Pet. 1:12). Mungu alilitumia pendo Lake kwa Kanisa kujifunua Mwenyewe kwa mwanadamu na kwa malaika (kama vile Efe. 2:7; 1 Kor. 4:9).

◙"**falme na mamlaka**" Hii aya inarejelea juu ya vile viwango vya malaika vya kiinjilisti, vilivyo vizuri na vibaya (kama vile Rum. 8:38-39; 1 Kor. 2:8; Efe. 1:21; 6:12; Kol. 1:16; 2:10, 15, 20). Hii ndiyo iliyokuwa sifa kuu ya kitheolojia ya wenye ujuzi. Kwao, huu ulikuwa uwakala wa maarifa ya siri ili kwamba mtu angeliweza kuvipitia viwango hivi vya kimalaika (*aeons*) kumfikia mungu mkuu, aliye mwema.
Orodha kamili ya maneno yaliyotumika katika Agano Jipya kwa ajili ya viwango hivi vya kimalaika inaweza kuonekana katika kitabu cha George E. Ladd's *A Theology of the NewTestament*, uk. 401. Hii mipangilio na madalaja ya viumbe vya kimalaika haitolei ufafanuzi na haikujadiliwa kwa undani sehemu yoyote katika Agano Jipya. Jihadhari na udadisi na mifumo ya kitheolojia ambayo inajaribu kueleza kwa uwazi lile jibu ambalo kitabu cha Agano Jipya kinaacha utata!

Mfano mzuri wa hili angalizo unahusiana na haya madalaja ya kimalaika. Katika baadhi ya vifungu, hivi si vya uovu, bila shaka miundo ya ulimwengu huu ulioanguka ambao unawasababisha wanadamu kuishi kinyume na Mungu. Kitabu kizuri kuhusu nadharia hii kingekuwa Hendrik Berkhoff's *Christ and the Powers*, Herald Press. Tazama Mada Maalum: Malaika katika Maandiko ya Paulo katika Efe. 6:12 na *Archē* katika Kol. 1:16.

◙ "**katika ulimwengu wa roho**" Hili eneo (lililozunguka) kivumishi cha wingi hasi (*epouranious*) "katika ulimwengu wa roho"linatumiwa tu katika Waefeso (kama vile Efe. 1:20; 2:6; 3:10; 6:12). Kutokana na muktadha wa matumizi yake yote, hili lazima limaanishe ule ufalme wa kiroho ambamo waamini wanaishi sasa, si mbingu.

**3:11** "**kusudi la milele**" Kiuhalisia hii "inahusu enzi" (kama vile Efe. 1:9-10). Hili neno linatumika katika Kiyunani cha Sasa kurejelea juu ya kupanga mpango. Mungu hashangazwi na mpango na Yeye hana mpango B (Luka 22:22; Matendo 2:23; 3:18; 4:28; tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH' wa Ukombozi wa Milele)!
Je! Mpango wa Mungu wa milele ulikuwa upi? Hili linaelezwa bayana katika Mwanzo 1-3. Mungu alimuumba mwanadamu kwa ushirika (kama vile.Mwanzo. 1:26-27; 3:8); ushirika huo ulivunjwa kwa uasi wa mwanadamu (kama vile Mwa. 3). Ule urejesho wa sura na ushirika na mwanadamu (Myahudi na mtu wa Mataifa) ndiyo kusudi la kazi ya Mungu katika Biblia. Lile lengo linatimia kupiti ile kazi ya Kristo (k.v. Mwa. 3:1 5) na huduma ya Roho (k.v. Yoh. 16:8-14)

**3:12**
**NASB, NKJV**
**NRSV "ujasiri"**
**TEV "matumaini"**
**NJB "ushujaa"**

Hili neno linatumika kwa uhuru wa kuongea, lakini linaweza kumaanisha ushupavu wa kumkabiri mtu katika mamlaka (kama vile Ebr. 4:16; 10:19,35; 1 Yohana 2:28; 3:21). Katika Kristo, waamini wana ujasiri!

**NASB "ujasiri na uwezo wa kukaribia"**
**NKJV "kukaribia kwa matumaini"**
**NRSV "matumaini"**
**TEV "kwa matumaini yote"**
**NJB "katika matumaini kamili"**

Hili neno linatumika katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani (LXX) kwa ajili ya utambulisho binafsi kwa ufalme. Hii dhana inasistizwa katika Efe. 2 na Rum. 5:2. Waamini wanamkaribia Baba kupitia Kristo pekee (kama vile 1 Pet. 3:18).
Yeye ndiye mpatanishi pekee (kama vile 1 Tim. 2:5). Katika Kristo, wamini wanayo matumaini ya kumkaribia! Haya Mageuzi yanayosistiza juu ya “ukuhani wa mwamini" yalikuwa ni mapambano dhidi ya mtazamo wa Kanisa

Katoriki wa kimamlaka. Hata hivyo, kibiblia, tazamio haliwezi kuwa juu ya "mwamini," bali juu ya "waamini." Ukristo wa Magharibi umechochea mtu kujitenga na ule mwili wa ushirika. Wakristo yawapasa kuwa makuhani katika ile maana ya kiinjili na kiushirika, si kwa nafasi ya upendeleo binafsi. Ni kweli kwamba wanadamu Wakajakuwa waamini binafsi, lakini Ukristo ni uzoefu wa ushirika.

◙"**kwa njia ya kumwamini**" Yesu ni mwongozo wa Mungu kwa Baraka zote za kiroho (kama vile Efe. 1:4, 7, 9, 10 (mara mbili), Efe. 1:12, 13 (mara mbili). Kiuhalisia huu ni "uaminifu kwake" (kama vile Gal. 2:16; 3:22). Ikiwa hiki ni kishamilisho milikishi, waamini wanaamini katika Kristo. Yeye ni wa Kuaminiwa! Ikiwa hiki ni kiima milikishi, kinarejelea ule "uaminifu" wa Kristo (maana Agano la Kale au neno). Uaminifu katika kuikamilisha sheria ya Agano la Kale (uhai Wake) na kujitoa Mwenyewe kama dhabihu kwa ajili ya dhambi (kifo Chake).

**3:13**"**naomba msikate tamaa** " Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopo, yenye kumaanisha "ninyi, wenyewe, msikate tamaa." Kisarufi, hii inaweza kurejelea kwa Paulo ama lile kanisa la Efeso. Watoa maoni wanakubali kwamba hii inarejelea kwa makanisa ambayo Paulo anayaelekeza katika ile barua ya mzunguko. Paulo anakitumia kifungu hiki mara nyingi (kama vile 2 Kor. 4:16; Gal. 6:9; 2 The. 3:13).

◙ " **dhiki zangu kwa ajili yenu**" Tazama Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: DHIKI KUU**

Kunahitajika kuwepo na utofauti wa kithiolojia kati ya matumizi ya Paulo ya neno **(*thlipsis*)** na Yohana

A. Matumizi ya Paulo (ambayo yanaaksi matumizi ya Yesu)
   1. Matatizo, mateso, uovu uliohusishwa kwenye ulimwengu ulioanguka
      a. Mt. 13:21
      b. Rum. 5:3
      c. 1 Kor. 7:28
      d. 2 Kor. 7:4
      e. Efe. 3:13
   2. Matatizo, mateso, uovu uliosababishwa na wasio amini
      a. Rum. 5:3; 8:35; 12:12
      b. 2 Kor. 1:4,8; 6:4; 7:4; 8:2,13
      c. Efe. 3:13
      d. Flp. 4:14
      e. 1 The. 1:6
      f. 2 The. 1:4
   3. Matatizo, mateso, uovu wa siku za mwisho
      a. Mt. 24:21,29
      b. Mark 13:19,24
      c. 2 The. 1:6-9

B. Matumizi ya Yohana
   1. Yohana analeta utofauti maalum kati ya *thlipsis* na *orgē* au *thumos* (ghadhabu) katika ufunuo. *Thlipsis* ni kile waaminio hukifanya kwa wale wasio amini na *orgē* na *thumos* ni kile Mungu hukifanya kwa wale wasio amini.
      a. *thlipsis* – Uf. 1:9; 2:9-10,22; 7:14
      b. *orgē* – Uf. 6:16-17; 11:18; 16:19; 19:15
      c. *thumos* – Uf. 12:12; 14:8,10,19; 15:1,7; 16:1; 18:3
   2. Yohana pia analitumia neno katika injili yake kuaksi matatizo yale waaminio hukabiliana nayo katika kila zama-Yohana 16:33

◙"**zilizo utukufu kwenu**" Kwa usahihi kabisa mateso ya Paulo (kama vile Efe. 3:1) yaliyo hayajafunuliwa. Bila shaka haya yanarejelea juu ya wokovu wa Paulo na kazi ya huduma katika Matendo 9:15-16 (kama vile Matendo 20:23). Paulo aliikamilisha huduma yake miongoni mwa Mataifa, hivyo, mateso yake yalifungua mlango kwa ajili ya

wokovu wao. Tazama maelezo kamili kuhusu "utukufu" katika Efe. 1:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAEFESO 3:14-19**
**[14] Kwa hiyo nampigia Baba magoti, [15] ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa, [16] awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. [17] Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; [18] ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; [19] na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.**

**3:14** " **Kwa hiyo**" Paulo analirudia lile kusudio lake la awali (kama vile Efe. 3:1, yaani, ombi lake): Tambua sehemu ya mafundisho yanayofungua kwa maombi mbele ya Mungu wa Utatu (kama vile Efe. 1:3-14) na kumalizia kwa maombi.

◙"**nampigia Baba magoti**" Kusimama, si kupiga magoti, ilikuwa sehemu ya kawaida kwa Maombi ya Kiyahudi. Hili linaonyesha mkazo wa Paulo (kama vile Mt. 6:5; Mark 11:25; Luka 18:11, 12; 22:41; Matendo 7:60; Flp. 2:10).

**3:14-15 "Baba. . . familia"** Hii ni kejeli juu ya jina la Kiyunani *pater* na *patria*. Tambua msistizo juu Baba, kama katika Efe. 1:3-14. Mungu Muumbaji ni kielelezo cha viumbe vyote viishivyo na umoja wao wa kijamii (yaani, makabila/mataifa).

**3:14-17 "Baba. . .Roho. . .Kristo"** Tambua kazi ya Utatu kama ilivyo katika Efe. 1:3-14. Ni kweli kwamba neno "Utatu" halitumiki katika kitabu cha Agano Jipya. Hata hivyo, kuna vifungu kadhaa ambapo zile nafsi tatu za Uungu zimetajwa katika muktadha usio wa namna moja (kama vile Mt. 3:16-17; 28:19; Yohana 14:26; Matendo 2:33-34,38-39; Rum. 1:4-5; 5:15; 8:9-10; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 1:21-22; 13:14; Gal. 4:4-6; Efe. 1:3-14, 17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6; 2 The. 2:13; Tito 3:4-6; 1 Pet. 1:2; Yuda 1:20-21). Tazama Mada Maalum: Utatu. Ile tafsiri ya KJV inaongeza "Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo," lakini kifungu hiki si cha yale machapisho ya kale ya Kiyunani $P^{46}$, א, A, B, C, ama yale maandishi ya Kiyunani yaliyotumiwa na Jerome na Augustine. Ile nyongeza inatokea katika machapisho ya herufi kubwa $א^{c}$, D, G, K, na lile andiko la Kiyunani lililotumiwa na Chrysostom. Ile dhana ya nafsi tatu za Uungu zenye asili ya Uungu mmoja (yaani, Mungu mmoja) ni vigumu kuielewa.Bado, ikiwa Yesu ni Mungu na Roho ni nafsi, kisha wale waiaminio Biblia wanalazimishwa kuukiri ule umoja wa Utatu. Tazama Mada Maalum: Utatu katika Efe. 1:3.

**3:15 "mbinguni na duniani"** Hili linawarejelea wale waamini walio hai na walio kufa (kama vile Flp. 2:10).

**3:16-19** Ombi lao linaweza kuelezwa kwa kutumia mionekano miwili ya kisarufi.

1. Vishazi nia vitatu (*hina*)
   a. Efe. 3:16, Mungu angeridhia (kauli tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu)
   b. Efe. 3:18, Mungu angewezesha kwa ukamilifu (kauli tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu)
   c. Efe. 3:19b, Mungu angekamilisha (kauli tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu)
2. Kauli nne za vitenzi jina tegemezi vya wakati uliopita usio timilifu
   a. Efe. 3:16, " kufanywa imara "
   b. Eph. 3:17, " Kristo akae mioyoni mwenu"
   c. Eph. 3:18, " ili mpate kufahamu"
   d. Eph. 3:19, "kuujua"

Hii aya inaaksi ombi la Paulo kwa waamini katika makanisa haya yote ambayo yaliimarika na kusimikwa kwa nguvu za Mungu kupitia matendo ya Kristo na nguvu ya Roho Mtakatifu izuiayo (1) walimu wa uongo na (2) mateso ya ulimwengu ulioanguka.

**3:16** "**kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake**" "Utajiri" ni moja ya maneno yaliyopendelewa na Paulo kueleza neema ya Mungu katika Kristo (kama vile Efe. 1:7,18; 2:4,7; 3:8,16). Asili ya Mungu ni ufunguzi wa nguvu za Mungu na utoaji.

◙ **"utu wa ndani**" Ukuaji wa kiroho ni wa milele, bali unachochewa na nguvu ya nje. Paulo mara nyingi anatumia tofauti kati ya utu wa ndani na utu wa nje. Yule mtu wa ndani ni kipengele cha kiroho, ambapo utu wa nje ni kipengele cha kimwili. Ule utu wa ndani tayari ni sehemu ya Zama Mpya, ufalme wa Mungu, bali ule utu wa nje unakufa na unapambana na zile zama za kale, ile asili ya kale iliyoanguka, na ule mfumo wa ulimwengu ulioanguka (kama vile Efe. 2:1-3).

**3:17** "**Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani**" Hiki ni kitenzi jina tendaji cha wakati uliopita usio timilifu chenye kulenga tendo maalum la imani. Kuna sintofahamu katika kitabu cha Agano Jipya kati ya ule ukaaji ndani wa Mwana na Roho. Kazi ya Roho (kamavile Yohana 14-16) ni

1. kulifunua hitaji la Kristo (yaani, dhambi ya mwanadamu)
2. kumfunua Kristo (yaani, injili)
3. kueleza juu ya Yesu
4. kubatiza katika Yesu (kama vile 1 Kor. 12:13)
5. Kumuumba Yesu ndani ya waainio (yaani, Ufanano na Kristo), tazama Mada Maalum: Moyo katika Kol. 2:2

Tazama Mada Maalum: Yesu na Roho katika Kol. 1:26.

◙"**mkiwa na shina**" Hii ni tungo tendwa ya wakati uliopita yenye hali ya kuendelea ambayo ingeweza kutafsiriwa "mmekuwa na mnaendelea kuwa shina kutokana na Mungu." Paulo anatumia hii stiari ya kilimo hapa pekee na katika Kol. 2:7. Hizi tungo mbili tendewa za wakati uliopita za hali ya kuendelea ni njia ya kuonyesha matumaini yake ndani ya waamini hawa na haya makanisa.

◙" **na msingi**" Hii ni tungo ya pili tendewa ya wakati uliopita yenye hali ya kuendelea. Hii ni stiari ya uundaji. Uchanganyaji ule ule wa stiari ya kilimo na uundaji unapatikkana katika Efe. 2:20-22 na 1 Kor. 3:9.

**3:18-19 " ili mpate. . . kufahamu "** Hizi zote ni kauli za vitenzi jina vya wakati uliopita usio timilifu (yaani, kuna kauli nne za wakati uliopita usio timilifu katika ombi hili, Efe. 3:16-19). Huu msistizo juu ya maarifa unakinzana na yale madai ya wasomi waliojitenga na Mafunuo ya walimu wa uongo. Hili linaweza kurejelea juu ya kufunuliwa kwa siri mpya ya Mungu, kuwaunganisha Wayahudi na watu wa Mataifa katika Kristo (kama vile Efe. 3:9).

**3:18**" **ili mpate**" Hiki ni kishazi nia cha pili. Paulo anaomba kwamba waamini wote waimalishwe na waweze Kuifahamu kwa ukamilifu ile injili (yaani, "kujua" na "kufahamu").

◙ "**pamoja na watakatifu wote**" Hili neno mara nyingi ni wingi, isipokuwa katika Fil. 4:21, ambalo pia ina ushirika wa andiko. Kuwa Mkristo ni kuwa jumuiya. Pia, tambau kwamba mapenzi ya Mungu ni ukomavu wa waamini wote (kama vile Efe.4:13). Tazama Mada Maalum: Watakatifu katika Kol. 1:2.

**3:19** "**upitao**" Upendo wa Kristo ni mkuu kuliko ufahamu wa mwanadamu! *Huperballō*. Tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya neno ambatani *Huper* katika Efe. 1:19. Hili neno linatumika katika Efe. 1:19; 2:7; na 3:19. Neno lingine ambatani la *huper* linatumika katika Efe. 3:20 (*huperekperissou*), ambalo pia linatumika katika 1 Thes. 3:10 na 5:13.

◙ "**kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu**" Hiki ni kishazi nia cha tatu katika ombi hili. Hiki hakirejelei juu ya Kristo ama Roho akaaye ndani, Efe. 3:17, bali ni kejeli juu ya mafundisho ya Mafunuo ya walimu wa uongo, ambao walisististiza ukamilifu (*plērōma*) kama ufahamu maalum ambao ulimwezesha mtu kupitia mizunguko yote ya kimalaika (*aeons*) hadi mbinguni. Kristo ndiyo "ukamilifu wa Mungu" wa kweli (kama vile Efe. 1:23; Kol. 2:9).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAEFESO 3:20-21**
**[20] Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; [21] naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina.**

**3:20** "**yeye awezaye**" Hii aya inaanza na moja ya sifa za ajabu za Paulo za nyimbo za kumtukuza Mungu ambazo zinafunga sehemu ya kimafundisho ya barua ya mzunguko. Hii sifa ya Mungu ishangazayo inatumika mara tatu katika kitabu cha Agano Jipya (kama vile Rum. 16:25; Yuda 24). Kila moja ya maandiko haya inajihusisha vipengele tofauti vya kazi ya Mungu.

**MADA MAALUM: SIFA, OMBI, NA UTOAJI WA SHUKRANI WA PAULO KWA MUNGU)**
Paulo alikuwa ni mtu wa sifa. Alilifahamu Agano la Klae. Kila moja ya ile migawanyo minne (yaani., kitabu) ya mwisho wa Zaburi zenye nyimbo wa kumsifu Mungu (kama vile. Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48). Watu wanao mjua Mungu humusifu na kumwinua mara zote.

1. Wakiwa wanaanza aya katika nyaraka zao
   a. Wakianza kwa Baraka au kwa salamu (kama vile. Rum. 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2)
   b. Wakianza kwa dua (*eulogētos*, kama vile. 2 Kor. 1:3-4; Efe. 1:3-14)
2. Wakiripuka kwa shangwe fupi za sifa
   a. Rum. 1:25; 9:5.
   b. 2 Kor. 11:31
3. Nyimbo za Sifa (zikiainishwa kwa utumiaji wa[1] *doxa* {yaani., utukufu} na [2] "Milele na Milele")
   a. Rum. 11:36; 16:25-27
   b. Efe. 3:20-21
   c. Flp. 4:20
   d. 1 Tim. 1:17
   e. 2 Tim. 4:18
4. Shukrani (yaani., *eucharisteō*)
   a. Ufunguzi wa barua (kama vile. Rum. 1:8; 1 Kor. 1:4; 2 Kor. 1:11; Efe. 1:16; Flp. 1:3; Kol. 1:3,12; 1 The. 1:2; 2 The. 1:3; Filemoni 1:4; 1 Tim. 1:12; 2 Tim. 1:3)
   b. Wito wa kutoa shukrani (kama vile Efe. 5:4,20; Flp. 4:6; Kol. 3:15,17; 4:2; 1 The. 5:18)
5. Wakiripuka kwa shangwe fupi za shukrani
   a. Rum. 6:17; 7:25
   b. 1 Kor. 15:57
   c. 2 Kor. 2:14; 8:16; 9:15
   d. 1 The. 2:13
   e. 2 The. 2:13
6. Wakihitimisha kwa dua
   a. Rum. 16:20,24
   b. 1 Kor. 16:23-24
   c. 2 Kor. 13:14
   d. Gal. 6:18
   e. Efe. 6:24

Paulo alimtambua Mungu wa Utatu kithiolojia na kiuzoefu. Katika uandishi wake alianza kwa maombi na sifa. Katikati ya uwasilishaji wake alilipuka kwa shangwe na shukrani. Katika hitimisho lake la waraka, siku zote alikumbuka kuomba, kusifu, na kumshukuru Mungu. Maandiko ya Paulo yana pumzi ya maombi, sifa na shukurani. Alimtambua Mungu, akajitambua mwenyewe, na kuitambua injili.

**NASB ,NKJV** **"mambo ya ajabu mno"**
**NRSV** **"yenye kushangaza zaidi"**

**TEV** **"mambo makuu zaidi"**
**NJB** **"yasiyona kipimo"**

Hii ni sifa ya maana ya vichochezi ambatani vya Pauline, "mambo ya ajabu mno" (kama vile 1 The. 3:10; 5:13). Tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya neno Ambatani *Huper* katika Efe. 1:19. Hii ni sarufi mbaya, lakini theolojia iliyo kuu!

◙" **kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu**," Huu ni urejeleo wa yule Kristo akaaye ndani kupitia Roho (kama vile Efe. 3:7, 16-17; Gal. 2:20; Kol. 1:27). Huyu Roho wa kudumu akaaye ndani ya kila mtu na kila mwamini ni tofauti na lile Agano La Kale na yule aliye Mpya, yaani, "moyo mpya," "fikra mpya," "roho mpya"(kama vile Eze. 36:26-27).

**3:21"atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu"** Hii sehemu iliyoinuliwa ya Bwana harusi ambaye ni Yesu na mwili, ambao ni kanisa, kanisa (kama vile Efe. 1:23), Damu Yake iletayo, watu waliojazwa na Roho! Hili neno "kanisa" linatokana na maneno mawili ya Kiyunani, "nje ya" na "kuita." Hili lilitumika katika tamaduni za Wagiriki-Warumi kwa ajili ya mikutano (kama vile Matendo 19:32). Katika maisha ya Kiyahudi hili neno lilitumika kutafsiri dhana muhimu za kitheolojia za "kusanyiko la Israeli" ama *qahal* (kama vile Kut. 12:6; 16:3; Law. 4:13; Hes. 14:5; 20:6; Kumb. 5:22; 9:10; 10:4; 18:16). Waamini wa kale walijiona kama watu sahihi "Watu wa Mungu" na wenye kuendelea mbele (kama vile Gal. 6:16; 1 Pet. 2:5-9; Ufu. 1:6).

◙" **milele na milele**" Tazama Mada Maalum ifuatayo.

### MADA MAALUM: MILELE *('olam*)

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, םלוע (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzuu. 3, uk. 345). Yametumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na maudhui). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

1. vitu vya kale
   a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
   b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
   c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
   d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
   e. mda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. mda/ wakati ujao future time
   a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
   b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
   c. uwepo endelevu
      1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
      2) mbinguni, Zab. 148:5
   d. uwepo wa Mungu
      1) Mwa. 21:33
      2) Kut. 15:18
      3) Kumb. 32:40
      4) Zab. 93:2
      5) Isa. 40:28
      6) Yer. 10:10
      7) Dan. 12:7
   e. Agano
      1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
      2) Kut. 31:16
      3) Ufu. 24:8
      4) Hes. 18:19

5) 2 Sam. 23:5
6) Zab. 105:10
7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
8) Yer. 32:40; 50:5

f. Agano maalumu na Daudi
1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
3) 2 Nya. 13:5
4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
5) Isa. 9:7; 55:3

g. Masihi wa Mungu
1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
2) Isa. 9:6

h. Sheria za Mungu
1) Kut. 29:28; 30:21
2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
3) Hes. 18:8,11,19
4) Zab. 119:89,160

i. Ahadi za Mungu
1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51
2) 1 Fal. 9:5
3) Zab. 18:50
4) Isa. 40:8

j. Uzao wa Abrahamu na nchi ya ahadi
1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
2) Kut. 32:13
3) 1 Nya. 16:17

k. Sikukuu za ahadi
1) Kut. 12:14,17,24
2) Ufu. 23:14,21,41
3) Hes. 10:8

l. umilele, kudumu milele
1) 1 Fal. 8:13
2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
3) Isa. 26:4; 45:17
4) Dan. 9:24

m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
2) kudumu katika uwepo Wake, Ps. 41:12; 61:4,7
3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
7) tukuza jina lake,Zab. 86:12; 145:2
8) baliki jina lake, Zab. 145:1

n. linatumiwa na Isaya kueleza enzi mpya
1) agano la milele, Isa. 24:5; 55:3; 61:8
2) YHWH kama mwamba wa milele, Isa. 26:4
3) furaha ya milele,Isa. 35:10; 51:11; 61:7
4) Mungu wa Milele, Isa. 40:28
5) Wokovu wa milele, Isa. 45:17

6) Wema wa milele, Isa. 54:8
7) Ishara ya milele, Isa. 55:13
8) Jina la milele, Isa. 56:5; 63:12,16
9) Nuru ya milele, Isa. 60:19,20

Matumizi yenye hali ya ukanushi kuhusiana na adhabu ya milele kwa waharifu inapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya kila wakati anatumia "moto" kuelezea hasira ya Mungu (kama vile. Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini katika Isa. 33:14 "ndipo anasema wa milele"

3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
   a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
   b. Zab. 90:2 (Mungu pekee)
   c. Zab. 103:17 (huruma zake)

Kumbuka,mktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani , Yeremia 7, tazama Mada Maalumu: Agano). Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la theolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka pia, Agano Jipya linajumuisha ahadi zote za Agano la kale (tazama Mada Maalumu: utabiri wa mambo yajayo ya Agano la Kale dhidi ya utabiri wa mambo yajayo ya Agano Jipya.).

◙"**Amina**" Tazama Mada Maalum ifuatayo.

**MADA MAALUM: AMINA**

I. AGANO LA KALE
   A. Neno "Amina" linatoka kwenye neno la Kiebrania lenye maana ya
      1. "ukweli" (emun, emunah, BDB53)
      2. "Uaminifu" (emun, emunah, BDB 53)
      3. "imani" au "uaminifu"
      4. "amini" (dmn, BDB 52)
   B. Asili yake ya neno inadokeza mkao wa mwili wa mtu ulivyo imara. Kinyume cha hili kinaonyesha mwili wa mtu Yule asio imara, unaoteleza (kama vile. Zab. 35:6; 40:2; 73:18; Yeremia 23:12) au kizuizi (kama vile. Zab. 73:2). Kutokana na utumiaji huu wa fasihi unatengeneza upanuzi wa kiisitiari wa imani, uaminifu, utiifu na wa kutegemewa (kama vile. Hab. 2:4)
   C. Utumiaji maalumu (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika agano la kale)
      1. Nguzo, 2 Fal. 18:16 (1 Tim. 3:15)
      2. Kuthibitika, Kut 17:12
      3. Uimalifu, Kut. 17:12
      4. Uthabiti, Isa. 33:6
      5. Ukweli, 1 Fal. 10:6; 17:24; 22:16; Pro. 12:22
      6. Thabiti, 2 Nya. 20:20; Isa. 7:9
      7. Stahili (sheria alizopewa Musa), Zab. 119:43,142,151,160
   D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yanatumika kwa ajili ya imani thabiti
      1. Bathach(BDB 105), imani
      2. Yra(BDB 431), hofu, heshima, abudu (kama vile. Mwa. 22:12)
   E. Kwa maana ya kuamini au uaminifu ulioanzishwa kwa matumizi ya liturujia ambao ulitumika kuthibitisha maelezo ya kweli ya mtu mwingine (kama vile. Hes. 5:22; Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Neh. 5:13; 8:6; Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48; Yer. 11:5; 28:6).
   F. Kiongozi cha kithiolojia kwenye neno hili sio uaminifu wa mwanadamu, bali ni wa Mungu mwenyewe (cf. Kut. 34:6; Kumb. 32:4; Zab. 108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni neema, uaminifu, kutii Agano la Mungu na ahadi zake. Wale wanaomfahamu Mungu wanahitajika kufanana naye (kama vile. Hab. 2:4). Biblia ni historian na kumbu kumbu ya Mungu kurejesha taswira yake (kama vile. Mwa. 1:26-27) kwa mwanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu. Hii ndio sababu ya kuumbwa kwetu.

I. AGANO JIPYA

A. Utumiaji wa neno “amina” kama hitimisho la kiliturujia kwa minajili ya kuthibitisha ukweli wa maelezo/taarifa ni la kawaida katika Agano Jipya (kama vile. 1 Kor. 14:16; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12).
B. Utumiaji wa neno kama kifungio cha maombi ni wa kawaida kwenye Agano Jipya (kama vile. Rum. 1:25; 9:5; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 6:18; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 2 Thess. 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2 Tim. 4:18).
C. Yesu ndiye yeye aliyelitumia hili neno (limezidishwa mara 25 katika Yohana, yaani., Yohana 1:51; 3:3,5,11; n.k.) kuyatambulisha maelezo muhimu (kama vile. Luka 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43).
D. Linatumika kama cheo kwa Yesu katika Ufu 3:14 ( pia angalia 2 Kor 1:20, yamkini jina la heshima la Mungu kutoka Isa. 65:16)
E. Dhana ya kusadiki au sadiki, au kuamini au amini inaelezewa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis*, ambalo linatafasiliwa katika Kiingereza kama “imani”,“sadiki”,“kuamini”(angalia mada maalumu: Sadiki, Kuamini au Imani).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani Paulo alijifunza theolojia yake?
2. Kwa nini Paulo alijita "mdogo kuliko watakatifu"?
3. Kwa nini siri ya Mungu imefichwa katka zama zilizopita?
4. Nini sababu ya kanisa kuuelekea utawala wa kimalaika?
5. Orodhesha mambo matatu ambayo Paulo alimwomba Mungu kuwaidhinisha waamini katika Efe. 3:16-19.
6. Je! Wakristo kuwa na yule akaaye ndani kunamaanisha nini?

# WAEFESO 4

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Umoja wa mwili | Tembeeni katika umoja | Hitaji la kuendeleza Umoja wa imani | Umoja wa mwili | Wito wa umoja |
| 4:1-8 | 4:1-6 | 4:1-16 | 4:1-6 | 4:1-6 |
| | Karama za Rohoni | | | |
| | 4:7-16 | | 4:7-16 | 4:7-16 |
| 4:9-16 | | | | |
| Maisha ya kale Na mapya | Mtu mpya | Hitaji la kutangaza upya njia za kipagani (4:17-5:20) | Maisha mapya katika Kristo | Maisha mapya katika Kristo |
| 4:17-24 | 4:17-24 | 4:17-24 | 4:17-19 | 4:17-24 |
| | | | 4:20-24 | |
| Kanuni za maisha Mapya | Usimuhuzunishe Roho | | | |
| 4:25-5:5 | 4:25-32 | 4:25-5:2 | 4:25-32 | 4:25-5:20 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji  Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA 4:1-32

A. Sura ya 4 inaanza na kipengere cha kiutendaji cha barua hii (yaani. "tembea," k.v. Efe. 4:1 , 17; 5:2,15). Mafundisho lazima yaathiri mtindo wa maisha! Ukweli ni wa kimahusiano! Wokovu sio bidhaa, sera ya

bima ya moto, au tiketi ya kwenda mbinguni, lakini ni toba endelevu/ uhusiano wa imani katika Kristo ambayo hutoa mfanano wa maisha ya Kristo.

B. Mistari ya 1-6 inaangazia juu ya dhamira ya kitabu kizima-umoja (k.v Efe. 1:10). Umoja wa waaminio unasimamia juu ya Mungu wa Utatu. Ushirika wa pamoja wa injili unakabiliana na hali ya kutowajumuisha walimu wa uwongo na Wayahudi. Sifa za kiroho zinazokupelekea kwenye umoja zimeelezewa katika mstari wa 2-3. Umoja ni wajibu wa kila mwamini. Umoja ndiyo ombi la (k.v. Yoh. 17:11, 21-22; vile vile angalia Efe. 4:23).

C. Umoja lazima utendwe kimakusudi na pasipo kukoma kwa sababu ya tofauti ya ukirimiwaji wa watu wa Mungu. Kila mwamini amekwisha pewa kipawa cha huduma thabiti ya wokovu (1 Kor. 12:7, 10). Ukweli kuwa waamini ni wahudumu wa Yesu waliokwisha kirimiwa, sio kile kipawa mahsusi mtu alichonacho, ni kigezo muhimu ndani ya kanisa. Waamini ni mwili mmoja na lazima watende kwa pamoja.

D. Makanisa ya kisasa ya kimagharibi kwa uhakika yanahitaji ukweli wa Efe.4:11-12. Viongozi wa kanisa ni vipawa vya mwili wa Kristo (kanisa), wamepewa kusaidia na kutia moyo mwili wote upate kutenda katika huduma. Huduma ni kazi ya waaminio. Hapana "Kasisi -Mlei" wa aina tofauti tofauti katika Agano Jipya. Kama wewe ni Mkristo, basi umeitwa, umekirimiwa, mhudumu wa moja kwa moja. Sio wote walioitwa kikazi, lakini wote wameitwa kutumika! Kazi ya viongozi wa kanisa (Efe. 4:11 ) ni kuwafunza watu wa Mungu kufanya kazi ya huduma, ambayo ni kuwahubiri waliopotea na kuwakomaza waliookolewa (Efe. 4:12; Mt. 28:19-20).

E. Waefeso 4:1 7-5:20 inaelezea dhambi ya upagani (k.v. Efe. 4:17) au mafundisho ya walimu wa uongo wenye ujuzi wasiopenda mambo ya sheria. Jinsi waamini wanapaswa kuishi ndilo jambo la muhimu! Pasipo matunda, hakuna mizizi (k.v. Mathayo 6;7:15-23)! Maisha ya milele ni tabia zinazochunguzika! Maisha yaliyo badilika na ubadilishaji wa maisha ni ushuhuda wa waamini kwa wokovu wao (k.v. Yakobo; 1 Yohana).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): WAEFESO 4:1-6**
**1 Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; 2 kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; 3 na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. 4 Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. 5 Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. 6 Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.**

**4:1 "mfungwa katika Bwana"** Kiuhalisia “katika Bwana.” Hii ni moja ya barua ya Paulo akiwa gerezani, yumkini aliiandika akiwa Rumi mwanzoni mwa miaka ya 60. Ni tofauti toka 3:1, ambayo ina kifungu “mfungwa wa Yesu Kristo.” Paulo aliwaona waaminio wamezingirwa na Kristo. Waliishi na kutembea na kuvipata wakiwa katika Yeye (k.v. Ayubu 1 2:1 0; Dan. 5:23; Mdo.1 7:28).

◙ **"mwenende kama inavyoustahili"** Hii barua inaanza na sehemu ya kiutendaji. Umoja unaendelezwa na matendo yenye kusudio la maisha yanayomfanana Kristo (k.v. Efe. 2:2, 10; 4:1,17; 5:2, 15; Kol. 1 :10; 2:6). Ukristo ni maamuzi ya awali yakifuatiwa na maisha ya uanafunzi (yaani., lango na njia, k.v. Mt. 7:13-14). Hili linafuatisha dhana ile ile kama usanifishaji wa mwanzo wa kanisa, “njia” (k.v. Mdo. 9:2; 1 9:9, 23; 22:4; 24:14, 22).
Neno “stahili”linaelezewa kwa uzuri katika 1 Yohana 2:6. Tambua kuwa tunapaswa kuenenda inavyostahilli kwa sababu ya mwito wetu, na sio kuupokea mwito. Hiki kipengere kinafuatisha Efe. 2:8-9, 10. Yatupasa kuyatenda matendo mema kwa sababu tumeokolewa kwa neema kwa njia ya imani. Matendo mema na kuenenda kunakostahili kunawezekana tu kwa sababu tumeokolewa na kujazwa na Roho Mtakatifu! Hayo ni matokeo, na sio namna (k.v. Efe.2:8-9).Wokovu ni lango ukifuatiwa na njia! Ni zawadi ya bure ikifuatiwa na maisha ya “kughalamiwa.”

◙ **"wito wenu mlioitiwa"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Mara zote wito hutoka kwa Mungu (k.v. Yohana 6:44, 65). Neno "wito" kiasili linahusiana na neno "kanisa" katika Efe. 3:21. Dhahili kuna dhihaka juu ya neno hili (k.v. Efe. 4:1 [mara mbili] na 4 [mara mbili]). Waamini wameitiwa utakatifu (k.v. Efe. 1:4). Huu ni mlingano wa kithiolojia wa kwenye mafundisho ya uchaguzi; mwanadamu lazima apokee ule wito wa awali wa Mungu (k.v. Efe. 1:1 3). Mungu mkuu amechagua kumpokea mwanadamu aliyeanguka kupitia Kristo na mwitikio wao wa imani ya toba (k.v. Marko 1:1 5; Mdo 3:16,19; 20:21 ). Wito mkuu na itikio linalostahili ni nguzo pacha za kithiolojia za maagano yote Jipya na la Kale, lakini nguzo ya tatu ni maisha ya utauwa. Mungu anawahitaji watu wale wanaoaksi tabia yake (yaani., aliye mtakatifu, k.v. 1 Pet.1 :13-25).

**MADA MAALUM: KUITWA**

Siku zote Mungu anachukua uwezo wa kuanzisha jambo katika mwito, uchaguzi, na akiwatafuta waumini waje kwake (kama vile. Yohana 6:44,65; 15:16; 1 Kor. 1:1-2; Efe. 1:4-5,11). Neno "kuitwa" limetumika kwa maana nyingi za kithiolojia.

A. Katika Agano la Kale "uitaji wa jina" mara nyingi ulikuwa katika mazingira ya kuabudu (kama vile. Mwa. 4:26; 12:8; 21:33; 26:25; Kut. 34:5).
B. Wenye dhambi wanaitwa kwenye wokovu kwa neema ya Mungu (yaani., Kut. 34:6-7) kupitia katika kazi aliyoimaliza Kristo na kwa kusadikishwa na Roho ((yaani., *klētos*, kama vile. Rum. 1:6-7; 9:24, ambayo kithiolojia inafanana na 1 Kor. 1:1-2 na 2 Tim. 1:9; 2 Petr. 1:10).
C. Wenye dhambi wanaliitia jina la Bwana ili waokolewe (yaani., *epikaleō*, kama vile. Mdo. 2:21; 22:16; Rum. 10:9-13). Maelezo haya ni nahahu ya Kiyahudi katika taratibu za kuabudu.
D. Waumini huliita jina lake nyakati za migogora na msongo wa mawazo (yaani., Mdo.7:59).
E. Waumini wameitwa kuishi maisha yanayomfanana Yesu i.e., *klēsis*, kama vile. 1 Kor. 1:26; 7:20; Efe. 4:1; Fil. 3:14; 2 The. 1:11; 2 Tim. 1:9).

Waumini wameitwa kwenye kazi ya huduma (kama vile. Mdo. 13:2; 1 Kor. 12:4-7; Efe. 4:1).

**4:2**
**NASB, NRSV "kwa unyenyekevu wote"**
**NKJV "hali ya chini"**
**TEV "kuwa mnyenyekevu"**
**NJB "pasipo ubinafsi"**

Neno hili linaanza na orodha ya wema wa Mkristo unaozalisha umoja. "unyenyekevu" kiupekee kabisa ni wema wa Mkristo ambao hapo awali haukujumuishwa katika orodha ya waadilifu wa Kiyunani wenye kutenda wema. wote (k.v. Hes. 12:3) na Yesu (k.v. Mt. 11 :29) wanaelezewa na neno hili. Paulo analitumia mara nyingi (k.v. Fil. 2:3; Kol. 2:18, 23;3:12).

◙**"upole"** Hii inarejelea "nguvu ya ndani"kama mnyama aliyefundishwa. Toleo la NKJV linalitafasiri kama"upole." Wanyama wa mwitu wamefunzwa kumtumikia mwanadamu. Waamini nao "wamefunzwa" kutumikiana wao kwa wao, na sio kushindana kati yao. Mtizamo ni ushirika, na sio ubinafsi. Mungu hahitaji kuwavunja waamini kiroho (k.v. Zaburi 139, aliwaumba wao), lakini akaziongoza nguvu zao kwa kusudi lake. Hii ni moja ya stiari pendwa ya Paulo kwa maisha ya Mkristo (k.v. 1 Kor. 4:21 ; 2 Kor. 10:1 ; Gal. 5:23; 6:1 ; Kol. 3:12; 1Tim. 6:11 ; 2 Tim. 2:25; Tit. 3:2).

◙ **"uvumilivu"** Hili ni neno lingine pendwa la Paulo (k.v. Rum. 2:4; 9:22; 2 Kor. 6:6; Gal. 5:22; Kol. 1:11 ;3:12; 1 Tim. 1:16; 2 Tim. 3:10; 4:2). Waamini wanavumiliana wao kwa wao kwa vile Mungu nae anawavumilia. Yote

upole na uvumilivu ni matunda ya Roho (k.v. Gal. 5:22-23).

◙**"mkichukuliana katika upendo"** Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo. "Mkichukuliana" ni neno lingine ambalo Paulo analitumia mara nyingi, mara kumi na mbili katika maandiko yake. Kwa vile Mungu ana uvumilivu wa msamaha kwa wasioamini (k.v. Rum. 2:4; 9:22) waamini wanapashwa kuendelea kushughulika na makosa na udhaifu (k.v. 1 Tim.1:6) ya waamini wengine katika hali ya fadhili. Waamini wanapashwa kuchukuliana na wengine ambao Kristo alikufa kwa ajili yao (k.v. Rum. 14:1-15:13; Gal. 5:22; Fil. 2:3; 4:5; Kol. 3:12-13). Huku kujitoa kibinafsi kunamfuatisha Kristo (k.v. 1Yohana 3:16), na ni kielelezo cha nyuma cha tabia ya anguko.

**4:3**
**NASB "mkijitahidi kuuhifadhi"**
**NKJV "mkijaribu kuuhifadhi"**
**NRSV "mkifanya kila bidii kuuendeleza"**
**TEV "mkifanya kila njia kuuhifadhi"**
**NJB "mkifanya kila liwezekanalo kuuhifadhi"**

Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Ikiwa na kauli tendaji isio na ukomo ya wakati uliopo. Toleo la Biblia ya NEB inalitafasiri kama "msiache kutia bidii." Umoja ni muundo unaojirudia wa barua nzima, zaidi kama Wafilipi. Umoja ni mapenzi ya Mungu kwa kanisa lake (k.v. Yohana 17:11 ,21 ,23), lakini lazima uwe wa kulazimisha, wa kuendelea, wa kimakusudu na utendeke kibinafsi!

◙ **"umoja"** Kumbuka, lengo ni umoja, na sio ufanano! Kifungu hiki kinasisitiza kuwa kitu kimoja ili kukanusha msisitizo wa wenye ujuzi juu ya (1) vyanzo vingi na (2) kutojumuishwa wasomi. Waamini lazima wamaanishe hitaji kwa ajili ya ustawi wa mwili wa Kristo (amabalo ni kanisa) na kuchukua uwajibikaji binafsi kwa uendeleaji wake! Huu ni ukweli unaohitajika katika siku za leo za haki binafsi na chaguo binafsi!

◙ **"kifungo cha amani"** Waamini wanawajibika kibinafsi kwa ajili ya ustawishaji wa umoja na nguvu ya mwili wa Kristo (ambalo ni kanisa, k.v. Kol. 3:14-15 and 1 Kor. 12:7). Hii inamaanisha wewe! Kujitoa kuliko hai katika mema yote kunaweza endeleza amani (k.v. Efe. 5:21 ). Angalia maelezo katika Efe. 2:15.

**4:4 "mwili mmoja"** Paulo anatumia hii stiari mara nyingi katika Waefeso (k.v. Efe. 2:16; 3:6; 4:4; pia Kol. 1:18). Hili linarejelewa kwa kanisa la wote kwa sababu ya asili ya mzunguko wa kitabu (yaani., kilipelekwa kwa makanisa mengi). Mara nyingi anapotumia neno"kanisa" katika Agano Jipya hurejelea kwa kusanyiko la mahala. Kanisa la wote linaelezewa katika Mt. 16:18 na Waefeso. Msisitizo uko juu ya umoja na kuwa kitu kimoja kwa watu wa Mungu na kanisa.

◙ **"Roho mmoja"** Hii inarejelea kwa Roho Mtakatifu. Pasipo Roho ni vigumu kumjua Mungu, kuja kwa Kristo, na kuishi maisha ya Kikristo katika umoja (k.v. Yohana 1 6:8-1 5). Angalia maelezo katika Efe. 3:1 7. Wale wenye ujuzi walidai kuwa "roho" au *aeons* (yaani., ngazi za kimalaika). Neno "Utatu" sio neno la kibiblia, lakini dhana ndio yenyewe. Inaelezewa katika vifungu mbali mbali(kama vile Mt; 3:1 6-1 7; 28:19; Yohana 14:26; Mdo. 2:33-34,38-39; Rum. 1:4-5;5:15; 8:9-10; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 1:21-22; 13:14; Gal. 4:4-6; Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6; 2 Ths. 2:13; Tito 3:4-6; 1 Pet. 1:2; Yuda 20-21 ). Kama yesu ni wa Uungu na roho ni nafsi, basi wanadai kuwepo Mungu mmoja wa dini ya Kiyahudi (k.v. Kumb. 6:4-6 lakini angalia Isa. 63:9-10) lazima watafsiri tena katika mwanga wa roho moja wa Uungu lakini katika nafsi tatu ziishizo, zinzotegemeana, udhihilisho binafsi. Kuna siri hapa lakini pia mafundisho ya wazi ya kibiblia! Angalia Mada Maalum Efe. 1:3.

◙ **"tumaini moja"** Paulo analitumia neno hili mara nyingi kwa namna mbali mbali lakini katika maana inayofanana. Mara nyingi linahusiana na utimilifu wa imani ya mwamini. Utimilifu unajulikana, lakini kipengere cha muda ni cha wakati ujao na usiojulikana. Angalia Mada Maalum: Tumaini katika Kol. 1:5.

**4:5 "Bwana mmoja"** Jina hili lina usuli wa agano la kale kwa ajili ya YHWH (K.V. Kut. 3:14, angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Kol. 1:3), na matumizi ya Agano Jipya likihisiana na Uungu (k.v. Rum. 10:9; 1 Kor. 12:3; Fil. 2:9-11). Kuna njia moja tu ya kuwa sawa na imani –Mungu katika Kristo (k.v. Yohana 1:9-18, 3:16; 10:7-18; 1 4:6; 20:31 ).

◙ **"imani moja"** Hili huenda linarejelea pia kwenye mafundisho (k.v. Gal. 1 :23; 3:23, 25; Fil. 1 :27; Yuda 3, 20), ambayo inatoshereza mazingira makubwa ya Waefeso na Wakolosai, au imani binafsi, ambayo inatosheleza vizuri huu muktadha (k.v.Gal. 2:1 6; 3:6-9).

◙**"ubatizo mmoja"** kwa sababu ya Uungu uliokwishwa kutajwa mapema katika muktadha huu, hii yumkini inaweza kurejelea ubatizo wa maji, ambao mwanzoni ndio ulikuwa ukiri wa imani ya kanisa (k.v. Mt. 28:19; Rum.1 0:9-13). Ilimaanisha kuzika maisha ya kale na kuanza maisha mapya katika Kristo (Rum. 6:4; Kol. 2:12). Hata hivyo, ingiweza kurejelea kwenye ubatizo wa Roho (k.v. Mdo. 2:38; 1 Kor. 12:13). Hata kama Roho ametajwa katika Efe. 4:4, haya matukio mawili ya mwanzo, la kwanza la ndani (ubatizo wa Roho) na lingine la nje (ubatizo wa maji), kiukaribu vimehusianishwa katika Agano Jipya.

**4:6 "Mungu mmoja naye Baba wa wote"** kwa kiasi Fulani inashangaza kumwita Mungu Baba (k.v. Mal. 2:10). Kwa maana moja muhimu watu wote wanahusika kwa Mungu. Wameumbwa naye, kwa mfano wake (k.v. Mwa. 1:26-27). Lakini katika muktadha huu, mtizamo sio juu ya uumbaji, bali ni uumbaji upya, ambao ni kuzaliwa mara ya pili, ukombozi kupitia juhudi za Mungu wa Utatu (k.v. Efe. 1:3-14). Watu wote hawako sawa mbele za Mungu kwa maana ya uumbaji, bali ni kwa toba binafsi na imani kwa kazi aliyoimaliza Kristo (k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16, 19; 20:21 ).

**MADA MAALUM: IMANI YA MUNGU MMOJA**

Mwanadamu siku zote amekuwa akihisi kuna zaidi ya ukweli kuliko huu unaoonekana (yaani kuathiriwa na vitu nje ya uwezo, kama vile dhoruba, kupatwa kwa jua na mwezi, kuanguka kwa vimondo, hali ya hewa, matukio, vifo, n.k.). Wataalamu wa sayansi ya binadamu wanatwambia kuwa wanakutana na vitu katika makaburi ya wanyama wa kale waliowahi kuishi ambavyo yumkini ni viashiria ya maisha yajayo, ambayo yanaweza kuonekana kama mwendelezo wa maisha ya baadaye.

Tamaduni ya kwanza kuandikwa ilikuwa ni ya wakati wa kiangazi (Tigris Kusini, Mito Yufrati), ilianza miaka ya 10,000 - 8,000 K.K. Waliandika mashairi kuelezea mawazo yao kwa Mungu na namna wanavyojamiiana. Tena, zaidi kama wanadamu pamoja na madhaifu yao yote. Tamaduni zao zilikuwepo katika namna za midomo zamani hata kabla hazijaandikwa.

Kulikuwa na kukua kwa kithiolojia kutoka
1. kuabudu wanyama mpaka
2. kuabudu miungu wengi mpaka
3. mungu mkuu (kuabudu miungu wawili)

Dhana ya "Mungu mmoja" (mmoja na mmoja tu binafsi Mungu mwenye maadili asiye na asili ya kike), si tu "mungu mkuu" ya miungu wengi au mungu mzuri kama miungu ye upili ya kiashuru (wafuasi wa Zoroaster), ni pekee kwa israeli (Ibraham na Ayubu, 2000 K.K.). ni mmoja tu wa pekee asiye patikana patikana katika Misri (Amenhotep IV, pia akijulikana kama Akhenaten, 1367-1350 au 1386-1361 K.K., aliyeabudu *Aten*, mungu jua, kama mungu pekee). Angalia J. Assmann, *The Mind of Egypt*, kurasa za 216-217.

Dhana hii inaelezea katika tungo kadhaa katika Agano la Kale
1. "hakuna kama YHWH wetu Elohim," Kutoka 8:10; 9:14; Kumbukumbu la Torati 33:26; 1 Wafalme 8:23
2. "Hakuna mwingine zaidi Yake," Kumbukumbu la Torati:30; 1 Kor. 8:4,6; 1 Tim. 2:5; Yakobo 2:19
3. "Hakuna kama wewe," 2 Samweli 7:22; Yeremia 10:6
4. "wewe pekee ndiwe Mungu," Zaburi 86:10; Isaya 37:16

5. "Kabla yangu hakukuwa na Mungu na baada yangu hatotokea," Isaya 43:10 adherence
6. "hakuna mwingine; zaidi yangu. . .hakuna mwingine," Isaya 45:5,6,22
7. "Yeye ni chanzo cha vitu vyote," Isaya 45:7 (kama vile Amosi 3:6)
8. "hakuna mwingine, hakuna Mungu mwingine," Isaya 45:14,18
9. "hakuna mwingine isipokuwa," Isaya 45:21
10. "hakuna kama mwingine;. . .hakuna kama mimi," Isaya 46:9

Lazima kukiri kuwa fundisho hili muhimu limefunuliwa katika maendeleo katika njia. Kauli ya mwanzo ingeweza kueleweka "utii kwa mungu mmoja kati ya wengi" au kuabudu mungu mmoja kwa kimatendo (kuna miungu mingine, yani Joshua 24:15; 1 Wafalme 18:21), lakini Mungu mmoja tu kwa ajili yetu (kama vile Kutoka 15:11; 20:2-5; Kumbukumbu la Torati 5:7; 6:4,14; 10:17; 32:12; 1 Wafalme 8:23; Zaburi 83:18; 86:8; 136:1-9).

Maandiko ya kwanza ambayo yalianza kuonesha umoja (Hali ya Kifalsafa ya Mungu mmoja) ni mapema (kama vile Kutoka 8:10; 9:14; 20:2-3; Kumbukumbu la Torati 4:35,39; 33:26). Madai yaliyokamili na yashinda nayo yanapatikana katika Isaya 43-46 (kama vile 43:10-11; 44:6,8; 45:7,14,18,22; 46:5,9).

Agano la Kale linapunguza miungu ya mataifa kama

1. Uumbaji wa kibinadamu – Kumbukumbu la Torati 4:28; 2 Wafalme 19:18; Zaburi 115:4-8; 135:15-18; Isaya 2:8; 17:8; 37:19; 40:19; 41:7,24,29; 44:10,12; 46:6-7; Yeremia 10:3-5; Ufunuo 9:10
2. mapepo – Kumbukumbu la Torati 32:17; Zaburi 106:37; Isaya 8:19; 19:3c; 1 Kor. 10:20; Ufunuo 9:20
3. ubatili, utupu – KumbuKumbu la Torati 32:21; 2 Wafalme 17:15; Zaburi 31:6; Isaya 2:18; 41:29; Yeremia 2:5; 10:8; 14:22; Yeremia 2:5; 8:19
4. hakuna miungu – Kumbukumbu la Torati 32:21; 2 Nyakati 13:9; Isaya 37:19; Yeremia 2:11; 5:7; 1 Kor. 8:4-5; 10:20; Ufunuo 9:20

Agano Jipya linaelezea katika Kumbukumbu la Torati 6:4 katika Warumi 3:30; 1 Kor. 8:4,6; Efe 4:6; 1 Tim. 2:5; na Yakobo 2:19. Yesu alinukuu kama amri ya kwanza katika Mt. 22:36-37; Marko 12:29-30; Luka 10:27. Agano la Kale pia kama Agano Jipya, linaelezea ukweli wa viumbe vingine vya kiroho (mapepo, malaika), lakini muumbaji mmoja tu/Mungu mkombozi (YHWH, Mwanzo 1:1).

hali ya kuwepo kwa Mungu mmoja kibiblia kunatabia zifuatazo

1. Mungu ni mmoja na wa pekee ((ontology) nadharia inayojishughulisha na asili ya uhai inadhaniwa, haijawekwa bayana)
2. Mungu ni wa binafsi (kama vile Mwanzo 1:26-27; 3:8)
3. Mungu ni mwadilifu (kama vile Mwanzo 34:6; Nehemia 9:17; Zaburi 103:8-10)
4. Mungu aliwaumba wanadamu katika sura yake (Mwanzo 1:26-27) kwa ajili ya ushirika (yaani #2). Ni Mungu mwenye wivu (kama vile Kutoka 20:5-6)

Kutoka katika Agano Jipya

1. Mungu ana milele tatu, udhihirisho wa nafsi (angalia Mada Maalum: Utatu)
2. Mungu kwa ukamilifu wake amefunuliwa kikamilifu ndani ya Yesu (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15-19; Ebr. 1:2-3)
3. Mpango wa milele wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka ni sadaka ya Mwanawe wa Pekee (Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; Fil. 2:6-11; Waebrania)

◙**"aliye juu ya yote na katika vyote na ndani ya vyote"** Agano Jipya linaukandamiza undani wa Baba (k.v. 1 Kor.3:23; 15:28). Mazingira haya ni moja ya mfano wa namna Biblia inavyoweka pamoja kazi za ukombozi wa nafsi tatu za Uungu. Hapa, Baba aishie ndani (k.v Yoh. 14:23) anasisitizwa. Katika Mathayo 28:20 na Kol. 1:27 Mwana aishie ndani anasisitizwa. Ni yule Roho, hata hivyo, kwa Yeye ambaye kazi zote amekabidhiwa (k.v. Yoh. 14:17; Rum. 8:9). Muktadha huu unaelezea kipaumbele cha Baba (k.v. Efe. 1:3-14; Rum. 11:36). Katika Kol. 1:16 istilahi ile ile inatumika juu ya Mwana. Kuna mashaka na upendeleo unaendelea kati ya nafsi za Utatu katika matendo yao yaliyoleta wokovu kwa mwanadamu. Neno "wote" (*pas*) limerudiwa mara nyingi kwa ajili ya msisitizo. Kisarufi, laweza kuwa liko kati, likirejelea uumbaji wote, au jinsi ya kike, likirejelea mwili wa Kristo (ambao ni kanisa) kote kiushirika na kibinafsi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 4:7-16**
**7 Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo. 8 Hivyo husema,**
**Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa. 9 Basi neno hilo, Alipaa, maana yake nini kama siyo**
**kusema kwamba yeye naye alishuka mpaka pande zilizo chini za nchi? 10 Naye aliyeshuka ndiye yeye aliyepaa**
**juu sana kupita mbingu zote, ili avijaze vitu vyote. 11 Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa**
**manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; 12 kwa kusudi la**
**kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; 13 hata na sisi sote**
**tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata**
**kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; 14 ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na**
**huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu.**
**15 Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo.**
**16 Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya**
**utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo**

**4:7 "lakini mmoja wetu alipewa neema"** tambua swichi toka dhana ya ushirika wa kanisa kwenda kwa dhana binafsi. Kila mwamini ana karama ya roho, aliyopewa na Roho wakati wa wokovu kwa lengo jema (k.v. 1 Kor. 1 2:7, 11). Agano Jipya linaziorodhesha hizi karama (k.v. 1 Kor. 12:1-13, 28-29; Rum. 12:3-8; Efe. 4:11) ni wakilishi, na sio za kuchosha. Hili linaweza kuonekana kutokana na ukweli kuwa uorodheshaji wa karama na utaratibu zilivyoorodheshwa unatofautiana. waamini mara zote huwa kinyume na tija kama

1. Watajivuna juu ya karama zao
2. Wakilinganisha karama moja na nyingine
3. Wataielezea kamili tabia ya kila karama

Agano Jipya haliko ndani ya maswala haya. Ukweli wa wahudumu wa familia walioitwa, na kukirimiwa, ufalme wa kikuhani ndilo suala lenyewe (k.v. 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Waamini wameitwa kutumika, na sio kunufaika!

◙ **"kwa kadri ya kipimo cha kipawa cha Kristo"** Yesu ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka. Tabia yake ("karama za rohoni," 1 Kor. 12) na huduma ("tunda la Roho," Gal. 5:22-23) vimegawanywa kati ya watu wake kuhakikisha uendelevu wa injili kupitia umoja wao na ushirika katika Roho.

**4:8** Hii ni nukuu toka zaburi 68:18, ambayo mwanzoni ilirejelea kwa YHWH. Kifungu "akawapa wanadamu vipawa" kinapatikana katika lugha moja ya kiarama cha Targum, toleo la Peshitta (Syriac), na tafasiri ya Kikaldayo, wakati , "akawapa wanadamu karama" ni maandiko ya Biblia ya Kiyahudi (andiko la Kiebrania) na tafsiri ya agano la kale (tafsiri ya Kiyuinani). Paulo alichukua tafsiri ya Agano la Kale ambayo inaaksi kusudi la kithiolojia. Mungu katika Kristo amewazawadia watu wake. Aliwazawadia kwa ajili ya huduma, na sio kunufaika kinafasi (k.v. Mt. 20:25-28; 23:1-12).

◙ **"aliteka mateka"** Wakolosai inayofanana na (k.v 2:15) inadokeza kuwa huu mstari unarejelea kwenye ushindi wa parade wa jeshi la Kirumi, pale vikosi vilivyoshindwa vilionyeshwa. Hapa inarejelea kwenye ushindi wa Kristo juu ya nguvu pinzani za kiroho za ulimwengu (yumkini zikihusiana na zile za wenye ujuzi wa kipekee *aeons*).

**4:9** Mstari unarejelea huenda (1) ile hali ya kuwa bianadamu (k.v. Flp. 2:6-11 ) au (2) kushuka kwa Yesu kule kuzimu(k.v. Mdo.2:31 ; Rum. 10:6-7; au yamkini 1 Pet. 3:1 8-20; 4:6; ambao uliaksiwa katika kanuni za imani za kanisa la mwanzo,"alishuka kuzimu").

**4:10 "kupita mbingu zote"** Huu ufanano unatofautiana na ule "sehemu ya chini ya dunia." Yesu aliacha mbingu ili awe mwanadamu. Alirudi mbinguni kama mwokozi aliyeshinda! Tambua wingi, "mbingu" (k.v. 2 Kor. 12:2). Walimu wa dini walibishana kama palikuwepo na mbingu tatu au saba. Hili linarejelea juu ya pale Mungu alipo au penye kiti cha enzi katika Ufunuo 4-5.

**MADA MAALUM: MBINGU NA MBINGU YA TATU**

Katika Agano la Kale neno "mbingu" mara nyingi iko kwenye hali ya wingi (yaani , shamayim, BDB 1029, KB 1559). Neno la Kiebrania hii inamaanisha "urefu." Mungu anaishi mahali pa juu. Dhana hii inaakisi utakatifu na uwezo mkuu wa Mungu.

Katika Mwa.1:1, wingi, "mbingu na dunia," vimetazamwa kama vitu vilivyoumbwa na Mungu (1) angani juu ya hii sayari au (2) njia ya kuitaja kweli yote (yaani, ya kiroho na ya kimwili). Kutokana na uelewa huu wa kimsingi maandiko mengine yalitajwa kama marejeo kwa viwango vya Kimbingu: "mbingu ya mbingu" (kama vile Zab. 68:33) au "mbingu na mbingu ya mbingu" (kama vile Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Neh. 9:6; Zab. 148:4). Wanasheria walidhani kwamba kungekuwa na

1. mbingu mbili (yaani, R. Yuda, Hagigah 12b)
2. mbingu ya tatu (Test. Lawi 2-3; Ascen. ya Isa. 6-7; Midrash Tehillim kwenye Zab. 114:1)
3. mbingu ya tano (III Baruch)
4. Mbingu ya saba (R. Simon b. Lakish; Ascen. ya Isa. 9:7)
5. mbingu ya kumi (II Enoch 20:3b; 22:1)

Hizi zote zilikuwa na maana ya kuonyesha utenganisho wa Mungu kutoka katika uumbaji uonekanao na /au mipaka Yake. Zaidi ya namba za kawaida za mbingu katika sheria za Kiyahudi zilikuwa saba. A. Cohen*, Everyman's Talmud* (uk. 30), anasema hii ilihusishwa na elimu sayari, lakini nafikiri inataja juu ya saba kama namba timilifu (yaani, siku za uumbaji na kuwakilisha pumziko la Mungu siku ya saba katika Mwanzo 2:2). Paulo, katika 2 Kor. 12:2, anataja mbingu "ya tatu" (Kiyunani ouranos)kama njia ya kuutambulisha upekee wa Mungu, uwepo wa ukuu. Paulo alikutana na Mungu binafsi

◙**"ili avijaze vitu vyote"** Yesu alikuja kutimiliza mpango wa Mungu wa milele kwa kuwaunganisha na kuwakomboa wanadamu wote vile vile pia uumbaji wa asili (k.v. Rum. 8:19-21 ). Neno hili "kujaza"(plēroō*,* k.v. Efe. 1:23; 3:19; 4:10; 5:18) lilikuwa neno maalum lililotumiwa na walimu wa uongo kuelezea ngazi za kimalaika (*aeons*). Wokovu hauko kwenye maarifa ya kibinadamu bali ni katika imani ya toba katika kazi ya Kristo aliyoikamilisha, maisha, mafundisho, mateso, ufufuo, kupalizwa, kutuombea na ahadi ya kurudi tena.

**4:11**
**NASB "alitoa"**
**NKJV "naye alitoa"**
**NRSV "alitoa karama"**
**TEV "yeye alitoa karama kwa watu,"**
**NJB "baadhi, walikuwa na karama"**

Yesu mwenyewe, au kiasi fulani Utatu (k.v. Efe. 4:4-6; 1 Kor. 12:4-6), huwapa vipawa vya rohoni watu wake. waamini wote ni wahudumu waliokirimiwa. Baadhi si viongozi, bali ni wahudumu. Tumeokolewa ili tutumike. Kuna karama mbali mbali za rohoni katika maandiko ya Paulo (k.v. 1 Kor. 12: 8-10, 28-30; Rum. 12:6-8; Efe. 4:11). Orodha hizi hazifanani. Hii inaonyesha kuwa orodha hizi hazichoshi, bali ni wakilishi. Kwa Paulo karama ni dhana kwenye huduma ya Yesu aliyotolewa mwilini mwake (ambalo ni kanisa) kuendeleza huduma yake. Agano jipya kamwe halitoi orodha yenye kuzielezea karama au mwongozo kwa waumini ili kutambua ni karama gani walizopewa. Mtizamo sio juu ya kuzitambua karama, bali ni juu ya dhana tofauti ya huduma. Moja ya mwongozo wa kiutendaji ya kuitambua karama ya mtu inapatikana katika kijitabu kidogo kiitwacho "kuyathibitisha mapenzi ya Mungu" kwa Paulo. Mwongozo ule ule wa kuyajua mapenzi ya Mungu unatumika kuitambua karama ya rohoni ya mtu.

◙ **"mitume"** Huu ni mwendelezo wa utumiaji wa neno mbali na "wale Tenashara" (k.v. Mdo. 1 4:4, 1 4, Barnaba; Rum. 1 6:7, Andronia and Yunis; 1 Kor. 4:6, 9; 12:28-29; 15:7, Apollo; Flp. 2:25, Epaphrodito; 1 The. 2:6, Silvano and Timotheo). Kazi yao kamili haijulikani, bali inajumuisha tamko la injili na uongozi wa kitumishi wa kanisa. Hata inawezekana kuwa Rum, 16:7 (KJV "Yunia") inarejelea kwa mtume jinsi ya kike!

◙ **"manabii"** Kazi mahsusi ya waamini waliokirimiwa pia haijulikani (k.v. Mdo. 11:28; 21:9-11 ; 15:32). Hawafanani na manabii wa Agano la Kale walioandika maandiko. Manabii wa Agano Jipya wanatumia maandiko kwa hali mpya na iliyo tofauti. Wanahusianishwa na mitume , wainjilist, wachungaji na waalimu kwa sababu wote waitangaza injili, lakini wakiwa na misisitizo tofauti. Angalia Mada Maalum katika Efe. 2:20.

◙**"wainjilisti"** Kwa mshangao, kwa ufahamu wa Mt. 28:19-20, karama hii imetajwa mara tatu katika Agano Jipya. Kazi zao katika kanisa la mwanzo, kama yalivyo mawili ya nyuma, hayajulikani (k.v. Mdo. 21:8; 2 Tim. 4:5),lakini tena kwa wazi yanahusiana na upigaji mbiu wa injili na uongozi wa kitumishi. Yawezekana kuwa hawa viongozi watatu wa mwanzo waliokirimiwa walikuwa ni watu wa kusafiri au huduma za kimkoa.

◙ **"wachungaji na waalimu"** Cheo cha "wazee" (*presbuteroi*), "askofu" (*episkopoi*), na "wachungaji" (*poimenas*) wote wanarejelea kwenye kazi moja na baadaye ofisi moja (k.v. Mdo. 20:17, 28; na Tito 1:5-7). Neno "mzee" lina usuli wa Agano la Kale, wakati "askofu" au "mwangalizi" walikuwa na usuli wa mji wa Kiyunani. syntaksi ya Kiyunani (yenye kiungo kimoja [*de*] na kibainishi kimoja [*tous*]) kikiungaisha hizi nyadhifa mbili pamoja kama kazi moja, mtu mmoja aliyekirimiwa ambaye hutangaza na kuielezea injili katika hali ya kawaida. Inafuarahisha kuwa katika Rum. 12:7 na 12:28 walimu wameorodheshwa kama karama tofauti na wachungaji ambao hawajatajwa kabisa (isipokuwa "kwa yule mtia moyo" katika Rum. 12:8). Kuna mengi sisi wa leo hatuyajui kuhusu kanisa jipya.

**4:12**
**NASB "kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke"**
**NKJV "kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu kwa kazi ya huduma"**
**NRSV "kuwakamilisha watakatifu kwa kazi ya huduma"**
**TEV "alilifanya hili kuwaandaa watu wa Mungu kwa kazi ya huduma ya Mkristo"**
**NJB "kwamba watakatifu kwa pamoja wafanye umoja katika kazi ya huduma"**

Viongozi ni zawadi ya Mungu aliyoitoa ili kuufundisha mwili wa Kristo kazi ya huduma! Kanisa linahitaji kuirudisha nguvu, kukirimiwa na uteuzi wa kibiblia wa washirika wote wa kanisa (kasisi-mlei, mzee-kijana, mwanaume-mwanamke, k.v. Yoel 2:28 iliyonukuliwa katika mahubiri ya Petro siku ya Pentecoste katika Matendo 2). Kila Mkristo ni mhudumu wa muda wote, aliyeitwa na Mungu, Mhudumu wa Mungu aliyekirimiwa. Neno "kukamilishwa" linamaanisha kusababisha kitu kiweze kutendeka kwa kusudi fulani. Linatumika kwa:
1. Mbavu zilizovunjika zinapona na kufanya kazi tena
2. Nyavu zilizochakaa zinakarabatiwa na kunasa samaki tena
3. Melikebu inatayarishwa kwa kamba na kuikabili safari
4. Kuku wakubwa walio tayari kupelekwa sokoni

Pia, tambua kusudi si lile tu baadhi ya waumini wamekua kwalo, lakini ni yote (k.v. Efe. 4:13). Kwa "watakatifu" angalia Mada Maalum katika Kol. 1 :2.

Karama zinatolewa kwa kila mwamini kwa ajili ya kusudi jema (k.v. 1 Kor. 12:7,11 ). Kila mwamini anaitiwa kwazo, amekirimiwa, ni muhudumu wa Kristo wa muda wote. Sio wote ni wahudumu wenye "wito," pamoja na kwamba wanahudumu. Kanisa la kisasa limeharibiwa na (1) hali ya kikasisi/kilei na (2) dhana ya wokovu kama bidhaa badala ya mchakato wa kitumishi wa kiushirika!!!

◙**"hata mwili wa Kristo ujengwe"** Paulo anachanganya stiari yake ya kiujenzi (k.v. Efe. 2:20-27) na stiari yake ya mwili (k.v. Efe. 1:23; 4:12; 5:30). Waamini wamekirimiwa kwa ajili ya faida iliyo njema, na sio kwa sifa binafsi (1 Kor. 12:7). Mtizamo sio kwa watu binafsi bali ni juu ya mwili (k.v. Efe. 4:4-6). Karama za rohoni ni taulo za watumishi, na sio vishikizo vya thamani! Waamini ni nyuki watembezi. Angalia Mada Maalum: Adilisha katika Efe. 2:21.

**4:13 "sisi sote tutakapoufikia"** Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu inayomaanisha dhana ya tahadhari. Kiuhalisia inamaanisha "kuifikia hatma."Kumbuka kuwa neno"wote"linazungumzia uwajibikaji wetu wa kishirika. Tambua dhana tatu za ukuaji zilizotajwa: (1) umoja wa imani; (2) maarifa ya Mwana wa Mungu; (3) ukomoavu wa mfanano wa Kristo. Pia, tambua kusudi sio hao baadhi ya waliokuwa, bali ni wote!

◙ **"maarifa"** Hili ni neno ambatani la Kiyunani *(epiginōskō),*ambalo linadokeza maarifa kamili ya kiuzoefu. Huu ulikuwa ni ukataaji wenye msisitizo wa wazi wa walimu wa uongo waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee juu ya maarifa ya siri, yasiyo jumuishi. Maarifa ya waamini ni kamili katika Kristo. Huu waweza kuwa ni mchezo juu ya dhana ya Kiebrania ya neno "tambua" kama ushirika binafsi (k.v. Mwa. 4:1; Yer. 1:5; Flp. 3:8,10) dhidi ya dhana ya Kiyunani ijulikanyo kama habari za kiutambuzi. Yote yanahitajika kwa ajili ya ukomavu wa Mkristo.

◙ **"mtu mkamilifu"** Hili liko kinyume na neno "watoto"kwenye mstari wa 14. Mzizi wa Kiyunani (*telos*) unamaanisha "kamili," "kukamilishwa,"na sio asiye na dhambi au mkamilifu (KJV).

**4:14 "ili tena tusiwe watoto wachanga"** Hili linadokeza kuwa wengi wa waamini wameokolewa lakini bado wachanga (k.v. 1 Kor. 3:1-3; Ebr. 5:11-14). Bado haileti maana ya umuhimu wa kunyenyekea na kujitoa kunakohitajika kuwa mhudumu wa kutumika. Waamini wanapaswa kufa wenyewe na kuwa hai tena kwa Mungu (k.v. Rum. 6:1-14; 2 Kor. 5:1 4-15; Gal. 2:20; 1 Yoh.3:16).

**NASB "kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu"**

**NKJV "kuchukuliwa huku na kule na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu"**
**NRSV "kuchukuliwa na kuendeshwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu"**
**TEV "kuchukuliwa na kuendeshwa na kila upepo wa elimu ya mafundisho ya watu wadanganyifu, wakiwapotosha watu kwa ujanja kwa tukizifuata njia za udanganyifu"**
**NJB "mkuchukuliwa kwa njia moja au nyingine na kila upepo wa elimu, kwa huruma ya ujanja wa hila ya watu, tukizifuata njia za udanganyifu"**

Kiwazi kabisa hili linarejelea kwa walimu wa uongo, ambao wanaonekana kuwa ni muunganikano wa wanafalsafa wa Kiyunani na washika sheria wa Kiyahudi. Kifungu hiki kinarejea kwa vyote uongo wa mwanadmu (walimu wa uongo) na uongo wa kimalaika (namna ya ujanja katika mpango wa udanganyifu). Mbali na hawa walimu wa uongo kuna shughuli za ngazi za malaika walioanguka (k.v.Efe. 6:10-12; 1 Kor. 10:20; Daniel 10). Watu wa Mungu wanapofushwa, wanatumiwa kiujanja na kudanganywa kwa sababu hawajakomaa katika Kristo. Kuna vita ya kiroho hata baada ya kubadilika. Lengo la Mkristo sio tu kwenda mbinguni wakifa bali ni kumfanana Kristo na kuhudumu sasa (k.v. Efe. 4:15; Rum. 8:28-30; Gal. 4:19)!

**4:15** waamini sio tu waseme ukweli, bali waishi na kuufundisha ukweli katika upendo (k.v. Ezra 7:10). Lengo ni umoja (Efe. 4:2-3)! Ni kwa vipi tofauti hii ilikuwepo toka kwenye mkanganyiko na upinzani wa walimu wa uongo.

**4:16** Paulo anatumia stiari ya mwili wa binadamu kusisitiza umoja katika hali ya upendo, katikati ya utofauti. Matengano yanafungua mlango kwa shetani, kwa malaika wake, na walimu wa uongo (k.v. Kol. 2:8). Angalia Mada Maalum: adilisha katika Efe.2:21 .

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 4:17-24**
**[17] Basi nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana, tangu sasa msienende kama Mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao; [18] ambao; akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; [19] ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani. [20]Bali ninyi, sivyo mlivyojifunza Kristo; [21]ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu, [22]mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; [23] na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; [24]mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.**

**4:17**
**NASB " Basi nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana"**
**NKJV " Basi nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana"**
**NRSV " Basi nathibitisha neno hili, tena nasisitiza katika Bwana"**
**TEV "katika jina la Bwana , tena, nasema hili na kuwaonyeni"**
**NJB "hasa, nawasihi kwa jina la Bwana"**
Madai haya ya uthibitisho mwenza na Kristo unaonyesha mamlaka ya kitume ya Paulo na maarifa ya Yesu ya kimafundisho.

◙ **"msienende"**Katika Efe. 4:1 7-1 9 kuna mlolongo wa tabia za maisha ya kipagani. Hawa waamini wapya wao wenyewe waliishi maisha kama haya (k.v. Efe. 4:28). Paulo anaorodhesha tabia ya mwanadamu aliyeanguka mara nyingi katika maandiko yake (k.v. Rum.1:29-31; 1 Kor. 5:11; 6:9; 2 Kor.12:20; Gal. 5:19-21 ; Efe. 4:19,31; 5:3-4; Kol. 3:5-9). Angalia Mada Maalum katika Kol. 3:5.
Namna ya kutengeneza utakatifu ulikuwa ugomvi mkubwa kati ya Paulo na Wayahudi wenye kushika sheria. Wote Paulo na wale wenye kufuata sheria za Kiyahudi walihitaji maisha ya haki katika uongokaji wao. Paulo alikiri dhambi za kipagani za nyuma za hawa waamini, lakini akaamini kuwa neema ya bure, Roho aishiye, na ukuaji wa maarifa ya injili ungalizaa kile ambacho washika sheria wasingeweza. Utendaji wa Agano la Kale umewekewa mbadala wa moyo mpya na fikra mpya za Agano Jipya (k.v. Yer. 31 :31 -34; Ezek. 36:22-32).

**NASB, NKJV**
**NRSV "katika ubatili wa nia zao,"**
**TEV "ambao fikra zao ni batili"**
**NJB "maisha ya ubatili"**

Neno hili linamaanisha “batili,” “tupu,”pasipo kusudi” (k.v. Rum. 1:21 ). Mistari ya 17-19 inarejerea kati ya (1 ) mtizamo wa walimu wa uongo au (2) maisha ya nyuma ya waamini katika upagani.

**4:18 "ambao akili zao zimetiwa giza"** Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea. Hali yao ya sasa ya upofu wa kiroho (kama ulivyo wetu) ni matokeo ya (1 ) majaribu ya nguvu ipitayo kiasi; (2) ushawishi wa imani potofu; na (3) uchaguzi binafsi

◙**"wamefarikishwa na uzima wa Mungu"** Hii ni kauli nyingine timilifu tendwa ya hali ya kuendelea. Hii inarejelea kwenye utengano toka Mungu wa Agano wa Agano la Kale na ahadi zake (k.v. Efe. 2:12).

◙ **"kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao"** Hii inarejea kwenye ujinga wa kujitakia (k.v. Warumi 1:18-3:20).

◙**"kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao"** Haya ni matokeo yanayodumu ya anguko (k.v. Mwa. 3; Yoh. 3:17-25). Angalia Mada Maalum: Moyo katika Kol. 2:2.

**4:19**
**NASB "wakisha kufa ganzi"**
**NKJV "wakiwa na fikra za nyuma"**
**NRSV "wakipoteza umakini wote"**
**TEV "wakipoteza mawazo yote ya aibu"**
**NJB "mawazo ya wema na mabaya yamepofushwa"**

Hii ni kauli nyingine timilifu tendaji ya hali ya kuendelea. Mwanadamu aliyeanguka amekuwa, na kubaki, asiye makini au kufanywa mgumu zaidi inavyofikiliwa, kwa yote ufunuo wa kiasili (k.v. Zab. 19:1-6; Rum. 1:1 8-2:16) na ufunuo maalum wa Biblia na ule wa Mwana, ambao ni neno lililoandikwa (k.v. Zab. 19:7-12) na neno liishilo (k.v.

Yoh. 1:1-14).

**NASB "wanajitia katika mambo ya ufisadi"**
**NKJV "wakijitia katika mambo ukware"**
**NRSV "wakajitia na mambo ya ukware"**
**TEV "wakijitia wenyewe katika uovu"**
**NJB "wakijitia wenyewe katika uasherati"**

Kiuhalisia inamaanisha "kufanya mambo ya aibu" (k.v. Rum. 1:24, 26, 28). Mwanadamu aliyeanguka amejitenga na vizuizi vyote, mambo ya jamii na mambo ya kiroho. Hawa walimu wa uongo hata waliweza kuwashangaza wapani wengine.

**NASB "kila namna ya uchafu kwa kutamani"**
**NKJV "kuondoa uchafu wote wenye tamaa"**
**NRSV "tama ya kutenda kila aina ya uchafu"**
**TEV "na kutenda uchafu wote pasipo kujizuia"**
**NJB "kukiwa na hamu ya kutenda aina zote za uchafu"**

Hii inamaanisha zaidi na zaidi kwangu mimi kwa gharama yeyote (k.v. Kol. 3:5). Mwanadamu aliyeanguka amepoteza maana ya ushirika mzuri. Wanadamu wanaishi kwa ajili yao wenyewe, kwa kitambo cha muda kidogo. Hii ndio sababu ya anguko la Mwanzo 3 linadhihilishwa wazi katika jamii ya kisasa ya watu wa Magharibi!

**4:20 "bali ninyi sivyo mlivyojifunza Kristo"** Huu ni utofauti wa Nguvu kati ya wahubiri wa Kristo na walimu wa uongo. Mstari wa 17 unadokeza utofauti huu kati ya maisha ya zamani ya kipagani na maisha mapya katika Kristo.

**4:21 "kama"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza ambayo ilifikiriwa kuwa kweli kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudi lake la kifasihi. Hawa waamini wamekwisha kuisikia ile kweli.

◙ **"Yesu"** Hili lilikuwa tumizi adimu la jina "Yesu"lenyewe, katika maandiko ya Paulo. Yawezakuwa linahusiana na mafundisho potofu kuhusu Yesu mwanadamu(yaani., ubinadamu wake) dhidi ya Yesu kama Roho (yaani., Uungu wake). Kwa fikra za wale waliodai kuwa wenye ujuzi wa pekee Yesu asingalikuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili kwa sababu "roho" (yaani., Mungu) ni mwema, lakini maada (yaani.,mwanadamu) ni mwovu. Wangelidai Uungu wake lakini wakaukana ubinadamu wake (k.v 1 Yoh. 4:1-6). Inafurahisha kuwa jamii za kisasa zimepindisha mafundisho haya potofu.

**4:22 "mvue"** kuna vishazi vitatu visivyo na ukomo vya wakati uliopita usiotimilifu katika Efe. 4:22,23 and 24. Kuvaa nguo inatumika kama stiari kuelezea tabia za kiroho (k.v. Ayu. 29:14; Zab. 109:29; na Isa. 61:10). Huu pia ulikuwa msisitizo juu ya hitaji la toba na matokeo ya maisha yaliyobadilika (k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:1 6,19; 20:21 ).

**NASB "mwenendo wa kwanza wa maisha"**
**NKJV "mwenendo wa kwanza"**
**NRSV "njia zako la kwanza za maisha"**
**TEV "yaliyokufanya uishi kama ulivyokuwa"**
**NJB "kuyatoa maisha yako ya mwanzo"**

Tafsiri ya toleo la KJV lina neno "maongezi" linalomaanisha "mtindo wa maisha" katika mwaka wa 1611 B.K kipindi ambacho tafsiri hii iliandikwa. Hili kwa wazi kabisa linaonyesha hitaji la tafasiri kufanywa upya! Hakuna tafsiri iliyovuviwa. Kazi zao ni kuiwasilisha injili toka kizazi kimoja hadi kingine. Ujumbe wa awali tu uliotolewa na Mungu ndio umevuviwa.

◙ **"utu wa zamani"** hii inarejelea kwenye tabia za mwanadamu aliyeanguka na upendeleo katika Adamu (k.v. Rum. 6:6; Kol. 3:9).Ni kipaumbele cha mtu, binafsi toka kwa Mungu, zaidi na zaidi kwangu mie kwa gharama yeyote!

**4:23 "mfanywe wapya katika roho za nia zenu,"** Hii ni kauli tendwa isio na ukomo ya wakati uliopo. Waamini yawapasa kuendelea kutengenezwa upya katika kufikiri kwa kumuruhusu Roho aweze kujenga fikra za Kristo akilini mwao (k.v. Rum. 12:2; Tito 3:5). Hii ni dhana ya "Agano Jipya" toka kwa Yer. 3 :31-34 (k.v. Ezek. 36:22-38).

**4:24 "vaeni"** Hii ni kauli ya kati yenye kitenzi jina cha wakati uliopita usio timilifu. Hii ni stiari ya uvaaji ambayo inasisitiza juu ya mwendelezo wa maamuzi ya kuwa katika Kristo (k.v. Rum. 13:14; Gal. 3:27; Kol. 3:8,10,12,14; James 1:21 ; 1 Pet. 2:1 ). Istilahi ya uvaaji juu ya Kristo ingeweza kuwa imeunganishwa kwenye utaratibu wa ubatizo katika kanisa la awali, pale waamini wapya walivaa nguo safi, nyeupe baada ya kubatizwa. Inadokeza uchaguzi wa hiari!

◙ **"utu upya"** Hii ni stiari ya maisha mapya katika Kristo. Petro anaiita "washirika wa tabia ya Uungu"katika 2 Pet. 1:4. Hii ni tofauti na ile asili ya kale ya Adamu aliye anguka ya Efe. 4:22.

◙ **"kwa namna ya Mungu"** Waamini yawapasa kuwa na tabia ya familia ya Mungu (k.v. Rum. 8:28-29; Gal. 4:19). Biblia inasisitiza nafasi yetu katika Kristo na pia hitaji letu kwa ajili ya kuendelea kumfanana Kristo. Wokovu ni wa bure, lakini ukomavu unagharimu kila kitu! Ukristo ni vyote kifo na uzima, hatua na mchakato, karama na zawadi! Fumbo hili ni gumu kwa watu wa kisasa kuweza kuchukua. Wanajaribu kusisitiza dhana moja au nyingine.

◙**"katika haki"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: HAKI**

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana.Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsia ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsia ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii anatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wawili halisi walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21). Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae . Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko,hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya aagano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

1. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, mahakama ya haki)
2. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kusingiziwa)

3. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu

4. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

1. Toba
2. Imani
3. Utii wa mtindo wa maisha
4. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, iliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo.Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa rabbi aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiyunani, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana).Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [ utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu wa Edeni. Biblia inaanza kati Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (cf. Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

1. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
    a. Warumi 3:26
    b. 2 Wathesalonike 1:5-6
    c. 2 Timotheo 4:8
    d. Ufunuo 16:5

2. Yesu ni haki
    a. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
    b. Mathayo 27:19
    c. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
3. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki. Mambo ya Walawi 19:2
    a. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
4. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
    a. Warumi 3:21-31
    b. Warumi 4
    c. Warumi 5:6-11
    d. Wagalatia 3:6-14
5. Iliyotolewa na Mungu
    a. Warumi 3:24; 6:23
    b. 1 Wakorintho 1:30
    c. Waefeso 2:8-9
6. Iliyopokelewa kwa imani
    a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
    b. 2 Wakorintho 5:7,21
7. kupitia matendo ya Mwana
    a. Warumi 5:21
    b. 2 Wakorintho 5:21
    c. Wafilipi 2:6-11
8. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
    a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
    c. Waefeso 1:4; 2:10
    d. 1 Timotheo 6:11
    e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
    f. 1 Yohana3:7
    g. 1 Petro 2:24
9. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
    a. Matendo 17:31
    b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

1. agizo la Mungu
2. zawadi ya Mungu
3. tendo la Kristo
4. maisha yapasayo kuyaishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana Naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na Barua Zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa na kipengele cha kuachiliwa. Calvin anasistiza asili ya ajabu ya

mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

1. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
2. injili ni ukweli (msistizo wa Augustine na Luther)
3. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.
Yatupasa kumkaribisha Yesu!
Yatupasa kuiamini injili!
Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 4:25-32**
**25Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake. 26 Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; 27 wala msimpe Ibilisi nafasi. 28 Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. 29 Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. 30 Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. 31 Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; 32tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.**

**4:25 "uvueni"** Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu ikitumika kama shurutishi. Inaendeleza stiari ya uvaaji (k.v. Efe. 4:24). Waamini wanatakiwa kufanya uamuzi wa awali ukifuatiwa na (yaani., kila siku, hata kila saa) maamuzi ya kuishi maisha matakatifu. Angalia Mada Maalum: Uovu na Wema katika Agano Jipya katika Kol. 3:5.

◙ **"uongo"** Hii inarejelea huenda kwenye

1. Kudanganya
2. "uongo" kwa wasio amini kama ulivyotumika katika 1 Yoh. 2:22
3. Ujumbe wa walimu wa uongo

◙**"mkaseme kweli kila mtu na jirani yake,"** Hii ni nukuu toka kwa Zakaria 8:16. Tambua Paulo ananukuu Agano la Kale kama utiaji moyo kwa waamini wapya (k.v. Efe. 4:26). Agano la Kale sio suluhisho la wokovu, bali bado ni ufunuo wa Mungu uliodhihilishwa na wenye mamlaka (k.v. Mat. 5:1 7-1 9). Bado Agano la Kale linatenda katika utakaso, sio tu katika kuhakifishwa. Angalia Mada Maalum: Ukweli katika Efe. 1:13.

◙ **"kwa maana tu viungo, kila moja kiungo cha mwenzake"** Neno"mwili" ni moja ya stiari ya Paulo kwa ajili ya kanisa (k.v. 1 Kor.12:12-30). Waamini wamekirimiwa kwa faida njema (k.v. 1 Kor. 12:7). Waamini wanaishi kwa ajili ya familia. Hawawezi kuishi kama watu binafsi waliojitenga.

**4:26 "Iweni na hasira, ila mstende dhambi"** Hii ni kauli ya kati (shahidi) shurutishi ya wakati uliopo. Hii ni nukuu toka Zab. 4:4. Kuna baadhi ya maeneo katika maisha pale hasira inafaa, lakini lazima iangaliwe kiumakini (yaani., wakati Yesu akilisafisha hekalu, k.v Yoh. 2:13-17).

Hii inaanzisha mlolongo wa kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi ambacho mara zote humaanisha kuzuia kitendo ambacho tayari kipo kwenye mchakato (k.v. Efe. 4:26, 27, 28, 29, and 30).

◙ **"jua lisichwe na uchungu wenu bado hujawatoka"** Hili lingeweza kuwa ni dokezo kwa Kumb.24:15. Siku kwa Wayahudi ilihesabiwa jua likizama (k.v. Mwa. 1:5). Hasira ni hisia yenye nguvu ambayo inapaswa kushughulikiwa kwa haraka. Hili ki-stiari laweza kurejelea kwenye muda au kiuhalisia kwenda kulala ambavyo inaweza kuisababisha hasira ikawa imepungua

**4:27**
**NASB "msimpe shetani nafasi"**
**NKJV "wala msitoe nafasi kwa shetani"**
**NRSV "msimpe chumba shetani"**
**TEV "usimpe shetani nafasi"**
**NJB "vinginevyo utampa shetani mwanya"**

Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi chenye kumaanisha kuzuia kitendo ambacho kipo kwenye mchakato. Hasira isiyo ya ki-Mungu ni mwanya wa mashambulizi ya kiroho; hata hasira ya ki-Mungu (k.v. Yoh. 2:13-17; Mt. 21 :12-13) lazima ishughulikiwe mapema (k.v. Efe. 6:10-18). Neno "shetani" ni neno ambatani la Kiyunani (*diabolos*) lenye kumaanisha "kurusha upande wa pili" (k.v. Mdo 1 3:10; Efe.4:27; 6:11 ; 1 Tim. 3:6,7; 2 Tim. 2:26). Ilikuwa ni namna ya ki-stiari ya kurejelea kwa shatani mshitaki wetu. Paulo anamrejelea shetani katika sura mbali mbali (k.v. Mdo. 26:18; Rum. 10:20; 1 Kor. 5:5; 7:5; 2 Kor. 2:11 ; 11 :14: 12:7; 1 Thes. 2:18; 2 Thes. 2:9; 1 Tim. 1 :20; 5:15). Inavyoonekana shetani alikuwa kiumbe cha kimalaika kilichomwasi Mungu (k.v. Mwa. 3; Ayu. 1 -2; Zak. 3). Ni vigumu kibiblia kuzungumuzia kuhusu shetani kwa sababu

1. Biblia haizungumzi waziwazi kuhusu mwanzo au kusudi la uovu
2. Maandiko ya Agano la Kale mara zote ni yale yanayoonekana kuhusiana na uasi wa shetani, kimahsusi yanaelekezwa kwenye laana za viongozi wa kidunia wenye majivuno (Mfalme wa Babel, Isaya 14 na Mfalme wa Tiro, Ezekiel 28) na sio shetani (angalia Mada Maalum: Uovu Binafsi katika Efe. 2:

Ni dhahiri toka sura mbali mbali za Agano Jipya kuwa kulikuwepo na msigishano katika ulimwengu wa roho (Mt. 4:10; 12:26; 16:23; Yoh. 13:27; 1 4:30; 16:11 ; Mdo. 5:3; 2 Kor. 4:4. Efe. 2:2; 1 Yoh. 5:19; Ufu. 2:9,13,24; 3:9; 12:9; 20:2,7). Wapi, lini, na kwa namna gani haya yote ni siri. Waamini huwa wana adui wa kimalaika (k.v. Efe. 2:2)! Uhusiano kati ya Mungu na shetani umejenga moja ya huduma ya msigishano. Shetani hakuumbwa kama mwovu. Kazi yake ya ushitaki katika Mwanzo 3, Ayubu 1 -2 na Zakaria 3 ilikuwa ndani ya mapenzi ya Mungu (k.v. A. B. Davidson's *An Old Testament Theology*, kur. 300-306, kwa ajili ya maendeleo ya uovu katika Biblia). Ilijaribu kutoa jaribio au utii wa binadamu na uaminifu. Lakini mwanadamu akashindwa!

**4:28 "mwibaji asiibe tena"** Maisha mapya katika Kristo ni kuwanufaisha na kulenga moja kwa moja mabadiliko ya matendo na tabia ya mtu. Hili badiliko ni moja ya ushuhuda wa wokovu wa mtu na ushahidi kwa wale wanaopotea.

◙ **"lazima atende kazi"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Dini ya Kiyahudi inashikilia kazi ya mikono katika mtizamo wa juu; hata sisi pia, kama ulivyofanyika Ukristo wa awali (k.v. 1 The. 4:11 ; 2 The. 3:10-12).

◙ **"apate kuwa na kitu cha kumugawia mhitaji"** Kazi si tu mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu, (yaani., Adamu alifanya kazi katika bustani kabla ya dhambi kuja), lakini ni njia ya kugawana na wale wenye uhitaji. Waamini ni waangalizi wa mali walizopewa na Mungu (k.v. Kumb. 8:11 -20), na sio wamiliki. Utoaji wetu ni kipimo cha kweli cha afya yetu ya kiroho (k.v. 2 Wakorintho 8-9).

**MADA MAALUM: UTAJIRI**

I. Mtazamo wa kitabu cha Agano la Kale kwa ujumla
   A. Mungu ndiye mmiliki wa vitu vyote
      1. Mwanzo 1-2

2. 1 Nyakati 29:11
3. Zaburi 24:1; 50:12; 89:11
4. Isaya 66:2

B. Wanadamu ni wasimamizi wa mali kwa ajili ya makusudi ya Mungu
1. Kumbukumbu 8:11-20
2. Mambo ya Walawi 19:9-18
3. Ayubu 31:16-33
4. Isaya 58:6-10

C. Wingi wa mali ni sehemu ya ibada
1. zaka za aina mbili
   a. Hesabu 18:21-29; Kumb. 12:6-7; 14:22-27
   b. Kumb. 14:28-29; 26:12-15
2. Mithali 3:9

D. Wingi wa mali huonekana kama zawadi kutoka kwa Mungu kwa ajiri ya agano la uaminifu
1. Kumbukumbu 27-28
2. Mithali 3:10; 8:20-21; 10:22; 15:6

E. Onyo dhidi ya mali katika kuwagharimikia wengine
1. Mithali 21:6
2. Yeremia 5:26-29
3. Hosea 12:6-8
4. Mika 6:9-12

F. Wingi wa mali sio dhambi kuwa nayo isipokuwa ikiwekwa kama kipaumbele
1. Zaburi 52:7; 62:10; 73:3-9
2. Mithali 11:28; 23:4-5; 27:24; 28:20-22
3. Ayubu 31:24-28

I. Mtazamo wa kipekee wa kitabu cha Mithali

A. Mali imewekwa katika nafasi ya juhudi ya mtu binafsi
1. uzembe na uvivu umelaaniwa – Mithali 6:6-11; 10:4-5,26; 12:24,27; 13:4; 15:19; 18:9; 19:15,24; 20:4, 13; 21:25; 22:13; 24:30-34; 26:13-16
2. kufanya kazi kwa bidii kumeungwa mkono – Mithali 12:11,14; 13:11

B. Umaskini dhidi ya mali umetumika kueleza juu ya haki dhidi ya unyonge – Mithali 10:1na kuendelea; 11:27-28; 13:7; 15:16-17; 28:6,19-20

C. Hekima (kumjua Mungu na nenp lake na kuishi katika maarifa haya) ni bora kuliko utajiri- Mithali 3:13-15; 8:9-11,18-21; 13:18

D. Maonyo na makaripio
1. Maonyo
   a. jihadhari na kudhamini deni la jirani yako (dhamana) –Mithali 6:1-5; 11:15; 17:18; 20:16; 22:26-27; 27:13
   b. jihadhari na kupata utajiri kwa njia ya uovu – Mithali 1:19; 10:2,15; 11:1; 13:11; 16:11; 20:10,23; 21:6; 22:16,22; 28:8
   c. jihadhari na mkopo – Mithali 22:7
   d. jihadhari na utajiri wa muda mfupi – Mithali 23:4-5
   e. mali hazifaidii kitu siku ya ghadhabu – Mithali 11:4
   f. utajiri una "marafiki" wengi– Mithali 14:20; 19:4
2. makaripio
   a. ukarimu huungwa mkono – Mithali 11:24-26; 14:31; 17:5; 19:17; 22:9,22-23; 23:10-11; 28:27
   b. afadhali haki kuliko utajiri – Mithali 16:8; 28:6,8,20-22
   c. maombi kwa ajili ya uhitaji, na sio utosherevu – Mithali 30:7-9
   d. kumpa mhitaji ni kumpa Mungu – Mithali 14:31

I. Mtazamo wa kitabu cha Agano Jipya

A. Yesu

1. mali hutengeneza jaribu pekee la imani ndani yetu wenyewewe rasilimali na zetu badala ya Mungu na rasilimali Zake
    a. Mathayo 6:24; 13:22; 19:23
    b. Marko 10:23-31
    c. Luka 12:15-21,33-34
    d. Ufunuo 3:17-19
2. Mungu atatupa mahitaji yetu ya kimwili
    a. Mathayo 6:19-34
    b. Luka 12:29-32
3. kupanda kunahusiana na kuvuna (kiroho pamoja na kimwili)
    a. Marko 4:24
    b. Luka 6:36-38
    c. Mathayo 6:14; 18:35
4. toba huithiri mali
    a. Luka 19:2-10
    b. Mambo ya Walawi 5:16
5. unyanyasaji wa kiuchumi umelaaniwa
    a. Mathayo 23:25
    b. Marko 12:38-40
6. Humu ya nyakati za mwisho inahusiana na matumizi yetu ya mali – Mathayo 25:31-46

B. Paulo
1. Maoni ya kiutendaji kama ule wa Mithali (kazi)
    a. Waefaso 4:28
    b. 1 Wathesalonike 4:11-12
    c. 2 Wathesalonike 3:8,11-12
    d. 1 Timotheo 5:8
2. Maoni ya kiroho kama yale ya Yesu (mambo ni ya muda mfupi, iweni na utoshevu)
    a. 1 Timotheo 6:6-10 (kuridhika)
    b. Wafilipi 4:11-12 (kuridhika)
    c. Waebrania 13:5 (kuridhika)
    d. 1 Timotheo 6:17-19 (ukarimu na kuamini Mungu, si utajiri)
    e. 1 Wakorintho 7:30-31 (kubadiklika badilika kwa mambo)

V. Hitimisho

A. Hakuna theolojia ya kimfumo iliyo ya kibiblia kuhusiana na mali.

B. Hakuna kifungu cheye uhakika kuhusiana na suala hili, hivyo, mitazamo ya kiundani lazima ikusanywe kutokana na vifungu mbalimbali. Jihadhari na kutokutumia maoni yako katika maandiko haya yaliyojitenga.

C. Kitabu cha Mithali, ambacho kiliandikwa na watu wenye hekima (busara), wana mtazamo tofauti kuliko aina nyingine za miundo ya kibiblia. Kitabu cha Mithali ni cha kiutendaji na kina tazamio binafsi. Hiki kina ulinganifu na lazima kiwe na ulinganifu na Maandiko mengine (kama vile Yer. 18:18)

D. Katika hizi siku tulizonazo tunahitaji kuchambua maoni na utendji wake kuhusiana na mali katika nuru ya Biblia. Vipaumbele vyetu vimepotea ikiwa ubepari au ukomonisti ni mwongozo wetu wa pekee. Ni kwa nini na ni kwa namna gani kufanikiwa kwa mtu ni maswali muhimu sana kuliko kuliko kile mtu alichojilimbikizia.

E. Kujilimbikizia mali lazima kuwe na ulinganifu na ibada ya kweli na utumishi unaostahili kama vile 2 Wkakorintho 8-9).

**4:29**

**NASB "neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu"**
**NKJV "na maneno yenye kupotosha yasitoke vinywani mwenu"**
**NRSV "mazungumzo yeyote yaliyo maovu yasitoke vinywani mwenu"**

**TEV "na maneno yenye kuumiza yasinenwe kwenu"**
**NJB "jilindeni na maneno yasiyo na staha"**

Neno hili kiuhalisia lilitumika kwa kitu kilichooza au kwa kazi ya uvunjaji wa jiwe (k.v. Mt. 7:17-18; 12:37; Lk 6:43). Lilikuja kutumika ki-stiari kwa kitu "kilichoharibika," "kilicho kiovu," "kilicho kichafu," "kisicho safi," au "kichafu." Katika mazingira haya inarejelea kwenye mafundisho ya maisha ya walimu wa uongo (k.v. Kol. 3:8). Haimanishi, katika muktadha huu, hairejelei kwenye mizaha, au matani yenye kuleta makwaruzano (k.v. Efe. 5:4; Kol. 4:6). Yesu alifundisha kuwa kile kikutokacho ndicho kilichoujaza moyo (k.v. Marko 7:15; 18-23). Angalia Mada Maalum: Maneno ya mtu katika Kol. 3:8.

◙ **"Bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji"** Ushahidi mmoja wa karama za rohoni zitolewazo na Mungu ni kuwa zinaujenga mwili wote (k.v. Rum. 14:13-23; 1 Kor. 14:4,5,12,17,26). Waamini lazima waishi, watoe, na wahudumu kwa faida ya mwili (ambalo ni kanisa, k.v 1 Kol.12:7), sio kwa ajili yao wenyewe (k.v. Efe. 4:3). Tena hali ya ushirika wa imani ya kibiblia imesisistizwa zaidi ya uhuru wa kibinafsi (k.v. Rum. 14:1 -15:13). Angalia Mada Maalum: Adilisha katika Efe. 2:21.

◙ **"ili liwape neema wanaosikia"** Katika muktadha hili haliwezi kumaanisha "neema,"kama ilivyo katika wokovu, lakini wema au upendeleo kwa waamini wengine, hasa waliojaribiwa na (1) walimu wa uongo (k.v. 2 Petr.2:1-21) au (2) uondoaji wa maisha ya nyuma ya mtu katika upagani (k.v. 2 Pet. 2:22).

**4:30 "wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi ambacho kinamaanisha kuzuia kitendo kilichoko katika mchakato. Hii inaelezea ukweli kuwa Roho ni nafsi hai. Pia inaonyesha kuwa vitendo vya mwamini vinasababisha maumivu kwa Roho Mtakatifu (k.v. 1 Thes. 5:1 9). Hili linaweza kuwa ni dokezo kwa Isa. 63:10. Lengo la Roho kwa waamini wote ni kufanana na Kristo (k.v. Efe. 1:4; 2:10; 4:13; Rum. 8:28-29; Gal. 4:19). Angalia Mada Maalum: Hulka ya Roho katika Efe. 1:14.

◙ **"ambaye kwa Yeye mlitiwa mhuri"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Huu upigaji muhuri unafanywa na Roho wakati wa kuokoka (k.v. Efe. 1:13-14; Ufu. 7:2-4). Uwekwaji muhuri ulikuwa ni alama ya kitamaduni ya umiliki, ulinzi, na uhalisia. Waamini ni mali ya Kristo! Angalia Mada Maalum: Muhuri katika Efe. 1:13

◙ **"hata siku ya ukombozi"** Hii inamaanisha ujio wa mara ya pili, siku ya ufufuo, au siku ya hukumu, ikihusiana na uhusiano wa mtu na Kristo. Angalia Mada Maalum: Fidia/ukombozi katika Kol. 1:14. Kwa maelezo mazuri juu ya mstari huu angalia Gordon Fee, *To What End Exegesis?* kur. 262-275.

**4:31 "uchungu wote"** Hii inarejelea hali komavu ya uchungu ikiwa na nafasi finyu ya mapatano.

◙ **"ghadhabu"** Neno (*thumos*) linarejelea kwa hasira ya haraka inayowaka au ghadhabu (k.v. 2 Kor. 12:20; Gal. 5:20; Kol. 3:8).

◙ **"hasira"** Neno (*orgē*) linarejelea hasira inayowaka taratibu (k.v. 2 Kor. 12:20; Gal. 5:20; Kol. 3:8).

◙ **"makelele"** Hii inarejelea kwenye kuangua kilio (k.v. Mt. 25:6; Mdo. 23:9). Katika muktadha huu ingeweza kurejelea kwenye vitisho vya nguvu au madai ya tabia mbaya ya walimu wa uongo au wafuasi wengine.

◙ **"matukano . . .na kila namna ya ubaya"** Hii pia inaweza kuaksi mbinu ya walimu wa uongo. Orodha hii inaonyesha matatizo yaliyo sababishwa na (1) walimu wa uongo au (2) tabia zile zilizo sababisha matengano. Hizi dhambi za aina moja zimeorodheshwa katika Kol.3:8.

◙ **"uondoke kwenu"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Waamini wanapaswa kuruhusu Roho kuwaondolea hizi tabia mbaya za kale, zilizo anguka, za asili ya ki-Adamu kwa wakati mmoja na jumla. Kama

wokovu unavyohusiana na chaguo muhimu binafsi, ndivyo hata maisha ya Mkristo.

**4:32 "tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane"**Hii inakinzana na Efe. 4:31. Ni kauli ya kati (shahidi) shurutishi ya wakati uliopo. Hizi ni amri chanya zinazoendelea (k.v. Kol.3:12-13) kuwa

1. Zimfurahisha Roho
2. Zijenga ushirika wa watakatifu
3. Ziwavutia wale waliopotea

◙ **"kama na Mungu katika Kristo alivyo wasamehe na ninyi"** Hii ni sababu ya msingi kwa matendo ya waamini, matendo ya Kristo dhidi yao (k.v. Mt. 6:12, 14-15; 18:21 -35; Fil. 2:1-11 ; 1 Yoh. 3:16).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha tabia za "maisha yenye thamani." Ni kwa namna gani unalinganisha na maisha yako?
2. Kwa nini umoja ni wa muhimu?
3. Kwa nini Paulo anweka msukumo katika mistari ya 4-6
4. Je kila Mkristo ana karama ya kiroho? Ni wakati gani wanaipokea? Nani anawapa? Kwa ajili ya kusudi lipi?
5. Nini lengo la kanisa?
6. Orodhesha matatizo ya mpagani
7. Orodhesha vitu vitatu vinavyompasa Mkristo kuvifanya (Efe. 4:22-24)
8. Orodhesha maovu manne ya Wakristo yaliyoorodheshwa katika Efe. 4:25-31

# WAEFESO 5

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Sheria za maisha Mapya | Enendeni kwa upendo | Ombi la kutangaza upya namna za kipagani | kuishi katika nuru | Maisha mapya katika Kristo |
| | | (4:17-5:20) | | (4:17-5:20) |
| 4:25-5:5 | | 4:25-5:2 | | 4:25-5:20 |
| | 5:1-7 | | 5:1-2 | |
| | | 5:3-5 | 5:3-5 | |
| Enendeni kama Wana wa nuru | Enendeni katika nuru | | | |
| 5:6-14 | | 5:6-14 | 5:6-14 | |
| | 5:8-14 | | | |
| | Enendeni kwa hekima | | | |
| 5:15-20 | 5:15-21 | 5:15-20 | 5:15-17<br>5:18-20 | |
| Wake na waume | Ndoa na kanisa | watumwa wa Kikristo | Wake na waume | Maadili ya kwenye Mji |
| 5:21-32 | | (5:21-6:9) | 5:21 | (5:21-6:9) |
| | 5:22-33 | 5:22-24 | 5:22-24 | 5:21-6:4 |
| | | 5:25-6:3 | 5:25-33 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji  Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu

4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA WAEFESO 5:1-6:9

A. Efe. 5:1-14 ni mwendelezo wa Efe. 4:17-32. Hii inashughulika na maisha ya Mkristo na inaeleza kile ambacho Wakristo wanapaswa kufanya na kile wasichopaswa kukifanya.
B. Efe. 5:3-5 unageuka toka kwenye upendo wa Kristo alioutoa wa mstari wa 2 hadi kwenye ubinafsi, upendo wa kidunia wa mwanadamu aliye anguka (kama vile Efe. 4:25-32).
C. Efe. 5:8-18 inawatofautisha walimu wa uongo na wale waamini wa kweli
   1. giza, Efe. 5:8 nuru, Efe. 5:8
   2. Matendo ya giza yasiyozaa matunda, Efe. 5:11 yale matunda ya nuru Efe. 5:9
   3. Fedheha . . .kwa siri, Efe. 5:12 inayaweka wazi, Efe. 5:11,13
   4. Watu wasio na hekima, Efe. 5:15 watu wenye hekima, Efe. 5:15
   5. Wajinga, Efe. 5:17 kuyafahamu mapenzi ya mwili, Efe. 5:17
   6. Msilewe kwa mvinyo, Efe. 5:18 mjazazwe Roho, Efe. 5:18
D. Hii kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo ya Efe. 5:18, "bali mjazwe Roho,"inatolewa ufafanuzi kwa kauli tano endelevu za wakati uliopo (kama vile Efe. 5:19-21). Hiki ni kifungu bora kabisa kinachohusu kujazwa Roho katika Agano Jipya.
E. Paulo anaeleza kwa mifano yale maisha ya kujazwa na Roho kwa kutumia nyumba ya Mkristo kama mfano. Yeye aliandika juu ya
   1. Waume na wake, Efe. 5:22-31
   2. Wazazi na watoto, Efe. 6:1-4
   3. Mabwana na watumwa wa majumbani, Efe. 6:5-9

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGUCHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILLILOBORESHWA) : WAEFESO 5:1-2**
**1 Hivyo mfuateni Mungu, kama watoto wanaopendwa; 2 mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato.**

**5:1" Hivyo mfuateni Mungu,"**Hii ni kauli ya kati (shahidi) shurutishi ya wakati uliopo. Hili neno la Kiingereza "kuiga" linatokana na huu mzizi wa Kiyunani. Katika Efe. 4:32 na 5:2 mwigilizaji wa Mungu anafafanuliwa kama yule ambaye (1) anayesamehe na (2) anayetembea katika upendo na kufadhiliana kama Yesu. Haya matendo huimarisha na kuuhifadhi umoja (kama vile Efe. 4:2-3).Waamini wajitahidi kuuhifadhi umoja wa mwili ulio mzuri, si haki binafsi, upendeleo, ama uhuru (kama vile Efe. 4:3).

◙**"kama watoto wanaopendwa"**Waaminiwaliitwa kwa jina lile lile muhimu la kitheolojia kama Yesu (kama vile Efe. 1:6). Waamini wanapendwa kwa sababu Yeye alipendwa. Wanapaswa kuaksi tabia ya familia ya Babawa wanaziaksi sifa za familia ya Baba Yesu na Roho huirejesha ile sura ya Mungu ndani ya wanadamu walio kosa katika anguko la Mwanzo 3.

**5:2"mkaenende"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo, ambayo ni sitiari ya kibiblia ya mtindo wa maisha (kama vile Efe. 4:1, 17;5:2,15). Ukristo ni maamuzi ya awali yakifuatiwa na maisha ya uanafunzi. Hii ni hoja ya wakati, tendo lipitalo ndani ya wakati, na hitimisho zaidi ya wakati! Tazama Mada Maalum: Vitenzi vya Kiyunani vya Wokovu katika Efe1:7.

◙**"kama Kristo naye alivyowapenda ninyi"** Machapisho ya kale ya Kiyunani yana tofauti kati ya "sisi" na "ninyi." "Sisi" iko katika $P^{46}$, $א^{a}$, D, G, na K; "ninyi" iko katika א, A, na B. "Ninyi" linafaa kati aandiko. Yesu ndiye mfano wetu (kama vile 1Yohana 4:11).

◙**"tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu"** Hii inarejelea juu ya upatanisho wa Kristo wa kujitoa kwa kifo mbadala (kama vile Isaya 53; Marko 10:45; Rum. 5:8; 8:32; 2 Kor. 5:21; Flp. 2:6-11; 1 The.5:9). Kile kihusishi cha Kiyunani cha neno *huper* chenye kimilikishi (cha hali ya kuondoa) hasa hasa ni kisawe cha kihusishi cha Kiyunani "*anti*" chenye maana ya "badala ya" Ushahidi wa machapisho ya Kiyunani wa neno "ninyi" badala ya "sisi" ndani ya kifungu hiki unatoshereza: "ninyi" katika $P^{46}$, $P^{49}$, א, A, D; "sisi" liko katika B pekee.

◙**"kuwa harufu ya manukato"** Hii ilikuwa sitiari ya kidhabihu ya Agano la Kale kwa wale wenye dhabihu kukubaliwa mbele za Mungu (kama vile Mwa. 8:21; Kut. 29:18; Law. 1:9, 13; Eze. 20:41; 2 Kor. 2:14; Fil. 4:18). Kadri dhabihu ilivyoteketezwa ndivyo ilivyotoa moshi ambao ulipaa hadi angani. Hii iliondolewa katika ulimwengu unaoonekana hadi ule usioonekana, kutoka katika ulimwengu wa mwili hadi katika ufalme wa Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAEFESO 5:3-5**
**3 Lakini uasherati usitajwe kwenu kamwe, wala uchafu wo wote wa kutamani, kama iwastahilivyo watakatifu; 4 wala aibu wala maneno ya upuzi wala ubishi; hayo hayapendezi; bali afadhali kushukuru. 5 Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu.**

**5:3 "uasherati"** Hili ni neno la Kiyunani (*porneia),* ambapo tunalipata neno la Kiingereza "picha za ngono."Katika Agano Jipya hili linazungumzia juu ya kwenda mbali na makubaliano ya mwongozo wa tendo la ndoa. Hili linaweza kurejelea

1. uasherati kama vile Mt. 21:31-32; Mko 7:21; Mdo 15:20, 29)
2. ukahaba (kama vile Mt. 5:32; 19:9
3. zinaa (kama vile 1 Kor. 5:1)
4. ufisadi (kama vile Rum. 1:29)

Katika Agano la Kale kulikuwa na tofauti ya wazi kati ya maneno "zinaa," ambapo sehemu moja ilikuwa na dosari, na "uzinifu" ambapo lilirejelewa kama tendo la kabla ya ndoa. Hii tofauti inapotea katika Agano Jipya la Kiyunani ambapo inarejelea tendo la kujamiiana kwa aina yoyote isiyofaa (nje ya ndoa, kabla ya ndoa, ndoa za jinsia moja, ama kuingiliana kikatili).

◙**"wala uchafu"** Hili ni neno la Kiyunani"safi" lenye kiambshi awali hasi ambacho hukanusha neno mahali lililpoambishwa. Haya maneno matatu katika Efe. 5:3, "uasherati, uchafu na tamaa,yote yanahusika na (1) yale matendo ya walimu wa uongo (kama vile 2 Tim. 3:6), na/ama (2) ule utamaduni wa watu wasiomjua Mungu ambao uko nje ya hawa waliobadili dini, ambapo tendo la uasherati mara nyingi lilihusiana na ile ibada ya sanamu.

◙**"kutamani"** Hili nenolinawasilisha lile wazo la "zaidi ya hayo kwa ajili yangu na kwa gharama yoyote." Kwa sababu hili limo ndani ya orodha ya dhambi za uzinifu bila shaka hili linahusiana na ubinafsi wa matumizi mabaya ya kingono (kama vile Kol. 3:5).

◙**"usitajwe kwenu kamwe,"** Hiki ni kauli tendewa shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo lililo katika mchakato. Hizi dhambi zilikuwa zikiendelea ndani ya kanisa.Waamini wanapaswa kujilinda na dhambi, na uvumi/tuhuma za dhambi (kama vile 1 The. 5:22). Yatupasa

kuonyesha mfano pamoja na kuihubiri injili.

◙**" kama iwastahilivyo watakatifu"** Hili linafanana na neno "isivyo wastahili" katika Efe. 5:4. Tazama Mada Maalum: Watakatifu katika Kol. 1:2.

**5:4** Waamini lazima wajihadhari na kunena kwao. Kwa hakika hili linafunua namna walivyo (kama vile Marko 7:15, 18-23; Kol. 3:18;Efe. 4:19; Yakobo 3:1-12). Tazama Mada Maalum katika Kol. 3:8. Hili ni kundi la pili la dhambi zilizotajwa katika sura ya 5. Makundi yote yana misingi mitatu. Hili linafanana na 4:17-32.

◙**"bali afadhali kushukuru"** Waamini walio wa kweli wanafunuliwa kwa moyo wao wa shukrani ambao hauhusiani na mambo mengine (kama vile Efe. 5:20; Kol. 3:17; 1 The. 5:18). Tazama Mada Maalum: Shukrani katika Kol. 4:2.

**5:5"Maana neno hili mnalijua hakika"** Hiki kifungu ni chenye msistizo sana. Hiki kina miundo miwili ya vitenzi vya Kiyunani vya neno"kufahamu": (1) kauli tendaji timilifu elekezi ama mfumo shurutishi wa neno *oida* na (2) Kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ya neno *gnōskō*. Wale manabii wa uongo walidai kuwa na ukamilifu, maarifa ya siri kumhusu Mungu, lakini yawapasa waamini kuelewa kwamba maisha ya mtu hufunua maarifa kamili na hekima (kama vile Mathayo 7).

◙**" ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa"** Maneno yoteyamerudiwa toka Efe. 5:3"uasherati" (*porneia*).Huu ni muundo wa neno wa jinsi ya kike katika Efe. 5:3, bila shaka hili ni rejea ya makahaba wa kiume, wafiraji, ama yale matendo ya kizinifu ya walimu wa uongo.

◙**"ndiye mwabudu sanamu"** Ufanano uko katika Kol. 3:5. Usemi huu huu unapatikana katika 1 Yohana 5:21. Zinaa inapokuwa kiini cha maisha yetu, inakuwa mungu wetu! Fedha inapokuwa kiini cha maisha yetu, inakuwa ibada ya sanamu (kama vile Mt. 6:24). Baadhi ya watoa maoni wanakiona kifungu hiki kama chenye kurejelea juu ya zile dhambi zote zilizotajwa katika muktadha huu (Efe. 5:3-5).

◙**"aliye na urithi"** Maisha ya waamini yanaonyesha ni nani aliye Baba yao, je ni Mungu ama yule mwovu (kama vile Mt. 7; 1 Yn 3:6, 9).

◙**"katika ufalme wa Kristo na Mungu"** Muundo wa kisarifi na kibainishi milikishi vinaunganisha Kristo na Mungu kama wamoja (kama vile Lk 22:29; Kol. 1:13). Hii ni njia ya moja ya waandishi wa Agano Jipya kuutetea Uungu wa Kristo.

Neno "ufalme" lilirudiwa rudiwa na lilikuwa kitovu cha mada ndani ya mahubiri ya Yesu. Hili linarejelea ukuu wa Mungu katika mioyo ya wanadamu wa sasa ambayo siku moja utatimizwa juu ya dunia yote (kama vile Mt. 6:10). Siku moja wanadamu wote na malaika watamkiri Kristo kama Bwana (kama vile Flp. 2:10-11), lakini wale tu waliotubu na kuiamini injili watakuwa sehemu ya ufalme Wake wa milele (Dan. 7:13; 1 Kor. 15:27-28).

**MADA MAALUM: UFALME WA MUNGU**

Katika Agano la Kale Mungu alifikiriwa kama mfalme wa Israel (kama vile 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 24:7-9; 29:10; 44:4; 89:18; 95:3; Isa. 43:15; 44:6) na Masiha akawepo kama mfalme aliyedhaniwa/kutegemewa (kama vile Zab. 2:6; Isa. 9:6-7; 11:1-5). Na kuzaliwa kwa Yesu pale Bethelehemu (mwaka wa 6-4 K.K) ufalme wa Mungu ukavunjiliwa ndani ya historia ya mwanadamu kwa nguvu mpya na ukombozi ("Agano Jipya," kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:27-36).

1. Yohana Mbatizaji akatangaza kukaribia kwa ufalme (kama vile Mt. 3:2; Mk 1:15).
2. Yesu wazi wazi akafundisha kwamba ufalme ulikuwa tayari ndani yake mwenyewe na mafundisho yake teachings (kama vile Mt. 4:17,23; 10:7; 12:28; Luke 10:9,11; 11:20; 17:21; 21:31-32). Na bado

ufalme unakuja (kama vile Mt. 16:28; 24:14; 26:29; Mark 9:1; Luk 21:31; 22:16,18).
Katika usambamba wa mihitasari kwenye Marko na Luka tunakipata kifungu, “ufalme wa Mungu.” Hii ilikuwa mada ya kawaida katika mafundisho ya Yesu yakijumisha utawala wa Mungu uliopo kiatika mioyo wa watu, ambao siku moja utakamilishwa katika ulimwengu wote. Huu unaakisishwa kwenye maombi ya Yesu katika Mat.6:10. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, alipendelea kifungu kile ambacho hakitumii jina la Mungu (yaani., Ufalme wa Mbinguni), wakati Marko na Luka, akiwaandikia watu wa mataifa, anatumia usanifu wa kawaida, akiweka jina la Uungu.

Hiki ni kile kifungu cha mfano katika mihitasari ya injili. Hotuba za kwanza na za mwisho za Yesu, na zaidi mafumbo yake, yanashughulika na mada. Zinarejerea utawala wa Mungu katika mioyo ya wanadamu sasa! Inashangaza kuona kwamba Yohana anatumia kifungu hiki mara mbili tu (na kamwe sio kwenye mafumbo ya Yesu). katika injili ya Yohana “uzima wa milele” ni sitiari muhimu.

Mvutano na kifungu hiki unasababishwa na ujio mara mbili wa Kristo, Agano la Kale linatazamisha kwenye ujio mmoja wa Masiha wa Mungu kama afisa wa kijeshi, ujio wa kitukufu-lakini Agano Jipya linaonyesha kuwa alikuja kwanza kama mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53 na mfalme mnyenyekevu katika Zak. 9:9. Enzi mbili za Kiyahudi (angalia mada maalumu: Enzi hii na Enzi inayokuja), enzi ya uovu na enzi mpya ya haki, zimeingiliana. Kwa sasa Yesu anatawala ndani ya mioyo ya waumini, lakini siku moja atatawala juu ya uumbaji wote. Atakuja kama Agano la Kale lilivyotabiri ( kama vile Ufunuo 19)!waamini wanaishi ndani ya ulimwengu wa Mungu “uliotayari” dhidi ya “ule ambao bado” (kama vile Gordon D. Fee na Douglas Stuart's *How to Read The Bible For All Its Worth*, kurasa za. 131-134).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAEFESO 5:6-14**
**[6]Mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana; kwa kuwa kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu huwajia wana wa uasi. [7] Basi msishirikiane nao.[8] Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni kama watoto wa nuru,[9] kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli;[10]mkihakiki ni nini impendezayo Bwana.[11]Wala msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza, bali myakemee;[12]kwa kuwa yanayoteneka kwao kwa siri, ni aibu hata kuyanena.[13]Lakini yote yaliyokemewa hudhihirishwa na nuru maana kila kilichodhihirika ni nuru.[14]Hivyo husema, Amka, wewe usinziaye, Ufufuke katika wafu, Na Kristo atakuangaza**.

**5:6 "Mtu asiwadanganye"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo lililo katika mchakato. Hili lilirejelea ule ujumbe na maisha ya walimu wa uongo, ambao walikuwa mchanganyiko wa wale waliodai kuwa na ujuzi wa pekee na wanasheria wa Kiyahudi (ambao unaonekana kutohusiana). Kuna mengi sisi ambao ni wa kisasa hatuyajui kuhusiana na mafundisho potofu ya karne ya kwanza.

◙**"kwa maneno yasiyo na maana"** Hili linaweza kurejelea juu ya mafundisho ya wale wenye kudai kuwa na ujuzi wa pakee ambayo kwao dhambi ya zinaa haiyaathiri maisha ya kiroho. Kwao wokovu ulipapatikana katika maarifa ya siri ya viwango vya kimalaika.Kwa ujumla hawa walitenganisha haki toka kwenye utakaso.Huu uasi bado u hai na hakika!

◙**" hasira ya Mungu huwajia"** Hii ni njeo ya wakati uliopo. Kwa vyovyote inarejelea juu ya (1) hukumu ya hapa duniani (kama vile Yohana 3:36; Rum. 1:18-32; 2:8-9; 9:22; Kol. 3:6 1 The. 2:16); na /ama (2) hukumu ya matukio yajayo ya siku za mwisho (kama vile Mt. 25:31 na kuendelea; Rum. 5:9; 1 The. 1:10; 5:9). Hasira ya Mungu ni ya kimafunuo kama lilivyo pendo la Mungu.
Ningali katika somo hili la hasira ya Mungu, hebu niweke sawa kuhusiana na ufahamu wangu wa maana zake. Kwanza ni majonzi ya kitheolojia kusistiza zaidi ama kutosistiza kweli huu.Mungu anakasirika kuona namna mwanadamu anavyolichukulia neno Lake,mapenzi Yake, na kila kitu. Huu si ulimwengu alioukusudia Mungu kuwa! Wanadamu wote watatoa hesabu kwa Mungu namna walivyoyaishi maisha yao (kama vile Gal. 6:7; 2 Kor. 5:10).

Hata hivyo, ni muhimu kutambua mtazamo wa kibiblia unaohusiana na fundisho hili. Kumbukumbu 5:9 ililinganishwa na5:10 na 7:9 inaweka mpangilio. Kadri hukumu inavyoendelea kwa kizazi cha tatu na cha nne, upendo wa Mungu na uaminifu unaendelea hadi kwa maelfu ya vizazi. Katika Isaya 28:21 hukumu inaitwa kazi ya Mungu ya "ajabu" (kama vile Kumb. 3:32-33; Zab. 103:8-14). Hukumu ni ya muhimu katika ulimwengu wa maadili, lakini haikubaliwi kwa Mungu. Kuzimu ni jeraha la wazi linalotoa damu katika moyo wa Mungu ambalo kamwe haliwezi kuponywa. Yeye huwapenda wanadamu wote waliumbwa kwa sura na mfano Wake (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 9:6). Yeye anataka kuwakomboa wanadamu wote na Yeye ameahidi kufanya hivyo kwa wote watakaotubu na kuamini kupitia Mwanae (kama vile Mwa. 3:15; Eze. 18:23,32; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9).

◙**" wana wa uasi"** Hii ni nahau ya kiebrania (kama vile Efe. 2:2; Kol. 3:6). Kulitii Agano ni sifa ya wana wa Mungu. Uasi ni sifa ya wale wafuasi wa Shetani.

**5:7"msishirikiane nao"** Kiuhalisia hii neno ni "wamiliki wenza." Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambacho mara nyingi kinamaanisha kusitisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato. Hapa Paulo anatumia uambatani wa neno *syn* kama alivyofanya katika Efe. 2:5-6na 3:6. Kifungu hiki hiki kinarudiwa katika mstari 11.Waamini hawalazimiki kuikimbia mitego iliyo katika dhambi ama mwonekano wa dhambi tu, hawa pia wachague marafiki na ushirika wao kwa umakini. Marafiki wa karibu tunaowachagua, kama maneno tuyanenayo, huifunua mioyo yetu.

**5:8-9 "giza. . . nuru"** Aya hii inafanana sana na pande mbili za Yohana (kama vile Efe. 1:4-5,7-8; 3:19; 8:12; 9:5; 12:46). Haya maneno yenye utofauti yalikuwa ishara za kiulimwengu kwa yale mema na mabaya ambayo yaliziteka fikra za Wayunani na ni ya kawaida katika fasihi ya Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi, ambayo ilikuwa ni jamii ya Kiyahudi iliyopenda mafarakano huko jangwani. Hiki kitenzi tendaji cha wakati uliopita usio timilifu katika kifungu cha kwanza kinaeleza maisha yao ya awali kama dhambi endelevu. Mwa. 6:5, 11-12: 8:21; Zab. 14:3; 58:3; Yer. 12:9).

**5:8"bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana"** Ni tofauti gani yenye nguvu namna hii (kama vile Mt. 5:19; Yohana 8:12).

◙**"enendeni kama watoto wa nuru"** Hii ni kauli nyingine tendaji shurutishi ya wakati uliopo (kama vile Yohana 3:19-21; 1 Yohana 1:7). Maneno ya waamini, maisha yao, na vipaumbele hufunua namna walivyo!

◙**"watoto wa"** Hii ni nahau ya Kiebrania ya"tabia," kama "wana wa"katka Efe. 5:6. Mazungumzo yanashuhudiwa na maisha yaliyobadishwa. Hili lilielezwa kwa kinaga ubaga katika Efe. 5:9. Hakuna tunda, hakuna mzizi (kama vile Mt. 5-7; Yakobo, na 1Yohana).

**5:9"tunda la nuru"**Toleo ya KJV lina neno "tunda la Roho,"ambalo liko katika machapisho ya kale ya Kiyunani $P^{46}$, $D^{c}$, na I. Hata hivyo, $P^{49}$,א ,A, B, D, G, P na muktadha wa papo kwa papo (Efe. 5:8), unadai "tunda la nuru." Hata lile toleo la NKJV ina neno hili. Toleo la KJV linafuata machapisho ya Kiyunani ya familia ya ki-Magharibi ambayo yalichukua maneno kutoka Gal. 5:22.

◙**"haki"** Tazama Mada Maalum katika Efe. 4:24.

**5:10**
**NASB "mkihakiki ni nini"**
**NKKV "kuchokonoa"**
**NRSV "jaribuni kujua"**
**TEV "jaribu kujifunza"**
**NJB "jaribu kugundua"**

Hili neno la Kiyunani (*dokimazō*) "hakikisha" (kama vile Rum. 12:2; 2 Kor. 8:8,22; 13:5; Gal. 6:4; 1 The. 5:21; 1 Tim.8:10; Ebr. 3:9) ama "jaribu" (kama vile 1 Kor. 3:13; 1 The. 2:4; 1 Pet. 1:7; 1 Yn 4:1) lina maana nyingine ya "kujaribu kwa mawazo hadi ukubalifu." Hili lilikuwa neno la ufuaji metali lillotumika katika kuijaribu sarafu kwa ajili ya kuangalia uhalisia yake. Tazama Mada Maalum katika Fil. 2:22.

**5:11"msishirikiane na"** Kiuhalisiahii"wanaoamini pamoja." Hii *syn* ni neno lingine ambatani. Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato.

Hii inarejelea

1. mawasiliano ya kijamii yaliyo karibu
2. mipangilio ya ibada za sanamu
3. mikutano ya walimu wa uongo (kama vile Efe 5:12)

◙**"myakemee"** Hii ni kauli nyingine tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Ni kwa namna gani waamini wanafunua uovu? Kwa sababu ya Efe. 5:12 kifungu hiki kinaonekana kumaanisha "kuyafunua maisha yetu ya kiungu" ama kwa kuitangaza injili. Nuru haiwezi kukaa pamoja na giza (kama vile Yohana 3:17-19).

**5:14"Amka, wewe usinziaye. . . Kristo atakuangaza"** Kwa huenda hii ni nukuu huru kutoka Isa. 29:19 au bila shaka 51:17; 52:1; 60:1 ama wimbo wa kale wa ki-Kristo (kama vileFlp. 2:6-11; 1 Tim. 3:16; 2 Tim. 2:11-13). Uko Katika muundo wa kimizani. Paulo alitumia vionjo vya nyimbo zenye hisia kubwa kutokana na

1. Agano la Kale (kutoka tafsiri mbalimbali)
2. Nyimbo za ki-Kristo
3. Kanuni za imani ya ki- Kristo
4. hata wandishi wa kipagani

◙**" usinziaye. . .wafu"** Hii inarejelea juu ya ule upofu wa kiroho, na kule kufa kwa kiroho kwa wale wasioamini (kama vile Efe. 2:1; 2 Kor. 4:4).

◙**"Kristo atakuangaza"** Hapa Yesu anatabiriwa kama nyota ya alfajirii iliyotukuzwa (kama vile Isa. 9:1-2; 59:8; 60:1; Luka 1:78-79), kinyume cha Lusifa, (kama vile Isa. 14:12). Nuru ni ishara ya kale ya uponyaji, afya, ukweli, maarifa, na wema (kama vile Mal. 4:2).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAEFESO 5:15-21**
***15*Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; *16*mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. *17*Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana. *18* Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho; *19*mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu; *20* na kumshukuru Mungu Baba sikuzote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo; *21*hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo**

**5:15"angalieni sana jinsi mnavyoenenda"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo, si kauli nyingine tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Ni maelezo ya ukweli, na sio amri. Neno "Kuenenda" ni sitiari ya kibiblia inayohusu maisha (kama vile Efe. 4:1,17; 5:2).

◙**"si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima"** Hekima inafunuliwa katika maisha ya ki- Ungu (kama vile Kol. 4:5), si katika yale maarifa ya walimu wa uongo ama ule uhuru usio wa ki-Mungu.

**5:16"mkiukomboa wakati"** Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo.Hili ni neno la kimatangazo ya kibiashara lenye kumaanisha "kununua kitu kwa jumla" kwa wakati ama bei muafaka. Waamini wanapaswa kuyachukua manufaa ya kila fursa ya kiroho (kama vile Kol. 4:2-6; 1 Pet. 3:15) kwa sababu tunajua kuwa siku inakuja ambapo

hakuna hata mmoja atakayeweza kufanya kazi. Dirisha liko wazi kwa wakati kwa ajili ya injili. Yatupasa kuushikilia wakati!.

**5:17"msiwe wajinga"** Hii ni kauli ya kati shurutishi (yenye ushahidi) ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi ambacho mara nyingi kinamaanisha kusitisha tendo lililo katika mchakato. Hawa walikuwa wajinga.

◙**"mapenzi ya Bwana"** Hakuna kiambata cha neno "mapenzi" Hivyo, haya ni mapenzi ya Mungu. Mapenzi ya Mungu ni pale tunapoamini katika Kristo (kama vile Yn 6:29,40), tena kuna"mapenzi" kadhaa ya waamini. Tazama Mada Maalum: Mapenzi ya Mungu katika Efe. 1:9.

**5:18 "msilewe kwa mvinyo"** Hii ni kauli tendewa shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambacho mara nyingi humaanisha kusitisha tendo ambalo liko katika mchakato (kama vile Mit. 23:30-31). Kileo na kilevi mara nyingi vinatumika kusistiza ule uzoefu wa kidini. Pia ni mfano wa kile kitu ambacho kinatawala na kueleza juu ya maisha ya mtu lakini lazima kirudiwe kwa makusudi ili kuleta matokeo (mazoea ya tabia mbaya). Kama kileo kinavyopaswa kurudiwa kwa ajili ya kuleta matokeo, hata sisi pia, "hisia" za Roho zinarudiwa kwa ajili ya kuleta matokeo. Kama waamini wanavyompokea Kristo kwa hiari kwa ajili ya wokovu, vivyo hivyo wanalazimishwa kwa hiari na kwa kurudiwa (kauli tendewa ya wakati uliopo) wajiweke wazi kwa ajili ya mwagozo na uthibiti endelevu (kila siku) wa Roho.

◙**"bali mjazwe Roho"** Hii ni kauli tendewa shurutishi ya wakati uliopo yenye maana "yawapasa kuendelea kujazwa na Roho" ama" mjazwe na Roho daima." Huu ni ushurutishi, si uchaguzi! Hii ni hali ya kawaida kwa waamini wote, si kwa watu fulani. Kifungu hiki kinamaanisha kwamba waamini lazima wawe wenye kupatikana, watu makini, na kuwa watii kwa yule Roho amuumbaye Kristo ndani ya maisha yao ya kila siku (kama vile Rum. 8:28-29; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 2:10; 4:13; Kol. 1:28). Waamini hawezi kujijaza wenyewe, bali yawapasa kumruhusu Roho kwa ajili ya kuwa na uhuru na nguvu. Utekelezaji wa mwanadamu si ufunguzi wa maisha yenye mafanikio bali yule Roho (kama vile Gal. 3:1-3). Hata hivyo, waamini wanapaswa kujiweka wazi kwa hiari kwa ajili ya uongozi na utawala wa Roho kuhusu ile misingi ya kila wakati.

Neno "kujazwa" linatumika katika Agano Jipya juu ya kile ambacho kinashawishi na kueleza sifa ya maisha ya mtu. Waamini wana uchaguzi katika kile kinachoyajaza maisha yao. Katika kitabu cha Matendo "kujazwa" na Roho kunahusiana na uinjilisti. Petro "alijazwa" mara kadhaa katika Matendo 2:4; 4:8,31. Kujazwa lilikuwa hitaji na zoezi endelevu. Ufanano wa kimuundo (Wakolosai &Waefeso zinajikita katika maelezo yanayotaka kufanana) uko ndani ya Kol. 3:16 ulibadili ile aya "mjazwe daima na yule Roho" kuwa "neno la Kristo likae kwa wingi ndani yenu."Hizi zote zinarejelea juu ya utii wa kimakusudi wa kila siku kwa yule Roho azalishaye ule ufanano na Kristo, hasa hasa kama unavyohusiana na kuhusika na watu. Yesu aliwafia watu.Watu ni fursa; watu ni wa milele.

**5:19 "mkisemezana. . . mkiimba . . . kumshangilia"** Hizi ni kauili tatu za kwanza miongoni mwa zile kauli nne tendajiza endelevu za wakati uliopo ambazo zinaeleza juu ya maisha ya kujazwa Roho. Zile tatu za kwanza ni kwa ajili ya kutendwa kwa nyimbo ama zikinukuu Zaburi. Roho ameweka wimbo ndani ya mioyo ya waamini kwa ajili ya Mungu (kama vile Kol. 3:16). Kumsifu Mungu huvunja nira!

Hiki kifungu kinasaidia katika kushughulika navipaumbele mbalimbali vya muziki ndani ya kanisa. Angalia aina mabalimbali za kimuziki zilizotajwa. Muziki katika ibada ni suala la upendeleo binafsi, si muundo wa mtu kutoa kasoro dhidi ya ule muundo usio sahihi. Huu ni hali ya moyo, sio sikio. Theolojia inayoelezwa ni ile ya hofu, lakini muundo wa muziki mara nyingi hufuatia. Tunathubutu kuvuruga kanisa la Mungu kutokana na vipaumbele binafsi! Ibada ni suala la moyo, sio midundo! Tafadhali soma Rum. 14:1-15:13 tena na tena.

◙**" mioyoni"** Tazama Mada Maalum katika Kol.2:2.

**5:20"kumshukuru Mungu Baba siku zote"** Hii ni kauli ya nne tendaji endelevu ya wakati uliopo. Kushukuru ni ushahidi mwingine wa maisha ya kujazwa na Roho (kama vile Efe. 5:4; Flp 4:6; 1 The. 5:18). Huu ni mtazamo wa ulimwengu wa biblia ambapo waamini wanaweza kutoa shukrani katika "mambo yote" (kama vile Rum. 8:29-30).

Waamini waliojazwa Roho wanafahamu kwamba Mungu yu kwa ajili yao na kwamba matukio si chanzo cha furaha na amani. Kitabu ambacho kimekuwa msaada wa maisha yangu katika eneo hili ni kile cha Hannah Whithall Smith's *The Christian's Secret of a Happy Life*! Tazama Mada Maalum: Sifa, Maombi, na Shukrani za Paulo katika Efe. 3:20.

**5:21**
**NASB, NRSV "mnanyenyekeana"**
**NKJV "mkijishusha"**
**TEV "mkinyenyekeana"**
**NJB "mkiachiana"**

Hii ni kauli ya kati ama tendaji endelevu ya wakati uliopo (tazama 5:22). Hii inaunda mabadiliko kutokana na Efe. 5:1-20 to 22-31 na muktadha unaendelea hadi 6:9. Zile kauli tano endelevu za wakati uliopo zinatoa ufafanuzi wa maana ya kujazwa Roho. Kifungu kinachofanana katika Kol.3:16 kinaonyesha kwamba hii inarejelea maisha ya kila siku yenye kumfanana Kristo.

Katika siki zetu "kutii"ni neno lililo kinyume, kwenye mahusiano.Kiuhalisia hili lilikuwa neno la kijeshi ambalo lilihusiana na kutii kulikojikita katika mlolongo wa amri. Lakini katika Agano Jipya hili mara nyingi linatumika juu ya ule mtazamo wa Yesu kuwahusu wazazi Wake wa kidunia (Luka 2:51) na Baba yake wa mbinguni (1 Kor. 15:28). Paulo alipendelea neno hili na alilitumia mara 23. Mstari wa21 ni kanuni ya kiroho kiulimwengu kwa utii wa pande mbili kati ya waamini waliounganishwa na maisha ya kujazwa Roho. Unyenyekevu unaenda kinyume na tamaduni zetu, magharibi, tazamio binafsi lililojikita akilini. Ubinafsi na utawala umejazwa utamaduni, lakini kibiblia haifai (kama vile Rum. 12:10; Gal. 5:13; Flp. 2:3;1 Yohana 4:11)!

Mstari huu unasistiza utii miongoni mwa watu kwa upande wa waamini wote. Hili halikuelekezwa kwa kundi moja. Inatakiwa kukubaliwa tena kuwa muktadha huu (Efe.5:22-31) unashughulikia mahusiano ya nyumbani kati ya waume na wanawake wa ki- Kristo, na sio waume na wake kwa ujumla wao. Katika maana yoyote wanawake si duni kiroho (kama vile Mdo 2:16-21; Gal. 3:28).

### MADA MAALUM: UNYENYEKEVU

Tafasiri hii ya mandiko ya kale yanatumia neno hili kwa maneno 10 tofauti ya Kiebrania. Maana yake halisi kufuatana na Agano la kale ilikuwa “kuamuru” “ amri iliyo sawa” neno hili limechukuliwa kutoka katika tafasiri ya maandiko ya kale ya miaka ya 70.

1. Mungu anaamuru (kama vile Law. 10:1; Yn. 2:1; 4: 6-8)
2. Musa anaamuru (kama vile Kut. 36:6; Kumb. 27:1)
3. Amri za wafalme (kama vile 2 Nya. 31: 13)

Katika Agano jipya, maana hii inaendelea hadi katika Mdo. 10:48, ambapo Mtume anaamuru. Hata hivyo, mitazamo mipya imeibuka katika Agano Jipya.

1. Suala la hiari linaibuliwa (mara nyingi IRABU YA KATI)
2. Tendo la mtu pekee kujizuia linaweza kuonekana kwa Yesu kutii kwa Baba (Luk. 2: 51)
3. Waumini wanatii katika sura ya kijadi ili kwamba injili isiathiriwe sana.
    a. Waumini wengine (kama vile Efe.5:21)
    b. Wake za wanaoamini (kama vile Kol. 3:18; Efe. 5:22- 24; Tit.2:5; 1Petr.3:1.
    c. Waumini katika serikali za kipagani (kama vile Rum. 13:1-7; 1Pet. 2: 13).

Waumini wanatenda kutokana na msukumo wa upendo, kwa Mungu, kwa Kristo, na kwa Ufalme, kwa faida ya wengine. Kama *agapaō* (upendo), kanisaliliingiza neno hili kwa maana mpya iliyohusiana na mahitaji ya Ufalme na ya wengine. Neno hili tena linachukuliwa kama uzuri wa kutokuwa mbinafsi, usiohitaji amri, bali kwa ushirika mpya wa kujitoa kwa Mungu na Masihi Wake. Waumini wanatii na kukubali kwa manufaa ya wote na Baraka za familia ya Mungu.

**MADA MAALUM: WANAWAKE NDANI YA BIBLIA**

I. Agano la Kale

A. Katika mila na desturi wanawake walichukuliwa kama ni mali kwa aliyenaye

1. Walijumuishwa katika orodha ya mali (Kutoka 20:17)
2. Walivyotendewa wanawake watumwa (Kutoka 21:7-11)
3. Nadhiri za wanawake kufutwa na waume wenye madaraka (Hesabu 30)
4. Wanawake kama mateka wa vita (kumbukumbu 20:10-14; 21:10-14)

B. Kiutendaji palikuwa na ushirikiano

1. Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27)
2. Heshima kwa baba na mama (Kutoka 20:12 [Kumb. 5:16])
3. heshima kuu kwa baba na mama (Mambo ya Walawi 19:3; 20:9)
4. mwanaume na mwanamke wangeweza kuwa Wanazareti (Hesabu 6:1-2)
5. mabinti wana haki ya urithi (Hesabu 27:1-11)
6. ni sehemu ya watu wa agano (Kumbu kumbu. 29:10-12)
7. wanapata mafundisho ya baba na mama (Mithali 1:8; 6:20)
8. wana wa kiume na mabinti wa Hemani (nyumba ya Kilawi) waliongoza muziki ndani ya Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 25:5-6).
9. Wana wa kiume na wa kike watatoa unabii katika enzi mpaya (Yoeli 2:28-29)

C. Wanawake katika dhima ya uongozi

1. Dada yake Musa, Miriamu, aliitwa nabii wa kike (Kutoka 15:20-21 vile vile nukuu Mika 6:4)
2. Wanawake walikirimiwa toka kwa Mungu kusokota nguo za aina mbalimbali kwa ajili ya Vibanda(Kutoka 35:25-26)
3. Mwanamke aliyeolewa, Debora, pia nabii (kama vileWaamuzi. 4:4), aliyaongoza makabila yote (Amu. 4:4-5; 5:7)
4. Hulda alikuwa nabii ambaye mfalme Yosia alimsihi kusoma na kutafsiri kitabu kipya kilichotolewa "*Book of the Law*" (2 Falme 22:14; 2 Nya. 34:22-27)
5. Malkia Esta, mwanamke aliyemcha Mungu, aliwaokoa Wayahudi katika Uajemi

II. Agano Jipya

A. Kwa utamaduni wa dini za Kiyahudi na ulmwengu wa kale wa Kiyunani na Rumi, wanawake walikuwa raia wa daraja la pili wenye haki na vipaumbele vichache (isipokuwa Makedonia).

B. Wanawake katika dhima ya uongozi

1. Elizabeti na Mariamu, wanawake waliomcha Mungu kwa kujihudhurisha mbele za Mungu (Luka 1-2)
2. Ana, nabii mwanamke akihudumu katika Hekalu (Luka 2:36)
3. Lidia, mwamini na kiongozi wa kanisa la nyumbani (Matendo 16:14,40)
4. Mabinti Filipo wanne waliokuwa mabikra na manabii (Matendo 21:8-9)
5. Fibii, shemasi wa kike wa kanisa katika Kenkrea (Rum. 16:1)
6. Priska (Prisila), mtendakazi pamoja na Paulo na mwalimu wa Apolo (Matendo 18:26; Rum. 16:3)
7. Maria, Trifaina, Trifosa, Persisi, Yulia, dada wa Nerea, wanawakae kadhaa watenda kazi amoja na Paulo (Rum. 16:6-16)
8. Yunia (KJV), bila shaka mwanamke mtume (Rum. 16:7)
9. Euodia na Sintike, watenda kazi pamoja na Paulo (Flp. 4:2-3)

III. Ni kwa namna gani mwamini wa sasa atailinganisha mifano hii tofauti ya kibiblia?

A. Ni kwa namna gani mtu ataupambanua kweli wa kihistoria na kiutamaduni, anaoutumia katika mazingire asilia pekee, kutoka katika ukweli wa milele ulio halali kwa makanisa yote, waamini wa rika zote?

1. Kwa umakini yatupasa kuchukuliana na kusudio la mwandishi asilia aliyevuviwa. Biblia ni neno la Mungu na njia na chanzo pekee cha imani na matendo.

2. Yatupasa kushughulika dhahiri na maandiko yenye masharti nay a kihistoria yaliyovuviwa.
    a. Utaratibu wa ibada (yaani, utaratibi na liturujia) wa Israeli (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3)
    b. dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza
    c. semi dhahiri za Paulo zenye masharti kihistoria na katika 1 Wakorintho
        1) mfumo wa kisheria wa wapagani katika Rumi (1 Wakorintho 6)
        2) kubaki katika hali ya utumwa (1 Kor. 7:20-24)
        3) ujane/useja (1 Kor. 7:1-35)
        4) mabikra (1 Kor. 7:36-38)
        5) chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor. 8; 10:23-33)
        6) matendo yasiyofaa katika Karamu ya Bwana (1 Wakorintho 11)
3. Kwa uwazi na kwa ukamilifu Mungu alijifunuaa kwa utamaduni maalumu, siku maalumu. Yatupasa kuuchukua ufunuo kwa umakini mkubwa, sio kufanya marekebisho kwa kila kipengele. Neno la Mungu liliandikwa katika maneno ya mwanadamu, likaelezwa katika utamaduni maalumu kwa wakati maalumu .

B. Tafsiri za kibiblia inapaswa kutafuta kusudi la asilia la mwandishi, nini alichokuwa akikizungumzia katika sihu zake zile? Hili ndilo jambo la kimsingi na la muhimu sana la tafsiri sahihi. Lakini basi yatupasa tulitumie hili kwa wakati wetu huu tulio nao. Tatizo kubwa la kiutafsiri linanaweza kuelezea maana ya neno. Je! Ni wapi palikuwa na huduma nyingi kuliko wachungaji ambao walionekana kama viongozi? Je! Ni wapi wahudumu au mashemasi wa kike na manabii wa kike walionekana kama viongozi? Ni dhahiri sana kuwa Paulo, katika 1 Kor. 14:34-35 na 1 Tim. 2:9-15, anadai kuwa wanawake wasishike nafasi katika ibada ya hadharani! Lakini alitumie kwa namna gani katika siku kama hizi? Nisingetaka utamaduni wa Paulo au utamaduni wangu kunyamazisha neno la Mungu na mapenzi yake. Bila shaka katika siku zile za Paulo palikuwa na mipaka sana, lakini pia katika siku zangu hizi inaweza kuwa wazi mno. Najisikia kukosa amani sana kusema kwamba kuwa maneno na na mafundisho Paulo ni ya kimasharti, karne ya kwanza, ukweli unaoendana na mazingira ya wenyeji hao. Mimi ni nani hata niweze kusababisha akili yangu au utamaduni wangu kumpinga mwandishi aliyevuviwa?!

Hata hivyo, nitafanya nini ikiwa kuna mifano ya kibiblia ya wanawake waliokuwa viongozi (hata katika maandiko ya Paulo, kama vile Warumi 16)? Mfano mzuri wa hili ni mjadala wa Paulo kuhusu ibada ya hadharani katika 1 Wakorintho 11-14. Katika 1 Kor. 11:5 anaonekana kuyaruhusu mahubiri na maombi ya wanawake katika ibada za hadharani huku vichwa vyao vikiwa vimefunikwa, lakini bado katika 14:34-35 anawahitaji wawe kimya! Kulikuwa na watoa huduma wanawake (kama vile Rum. 16:1) na manabii wa kike (kama vile Matendo 21:9). Ni utofauti huu unaonipa uhuru wa kutambua maoni ya Paulo (kama inavyohusiana na maagizo kwa mwanamke) kama ilivyozuiliwa huko Korintho na Efeso katika karne ya kwanza. Katika makanisa yote mawili palikuwa na matatizo kwa wanawake katika kutumia uhuru wao mpya uliopatikana (kama vile. Bruce Winter, *After Paul Left Corinth*), ambapo ingeweza kusababisha ugumu kwa kanisa kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo. Uhuru wao ulibidi kupunguzwa ili kwamba injili iweze kuleta matokeo mazuri.

Siku zangu ziko kinyume na siku za Paulo. Katika siku zangu injili inaweza kuwekewa mipaka ama ikiwa wanawake wenye uwezo wa kusema, waliofunzwa hawaruhusiwi kuchangia katika injili, hawaruhusiwi kuongoza! Ni nini hatima ya lengo la ibada ya hadharani? Si uinjilisti na nidhamu? Je! Mungu anaweza kuheshimiwa na kufurahishwa na viongozi wa kike? Biblia kwa ujumla wake inaonekana kusema "ndiyo"!

Nataka kukubaliana na Paulo; theolojia yangu kimsingi ni ya Kipauline. Sitaki kuathiriwa kwa kiwango kikubwa au kugeuzwa kifikra na sera za kisasa za kupigania haki za wanawake. Hata hivyo, nahisi kwamba kanisa limeenda pole pole katika kuitikia ukweli ulio wazi wa kibiblia, kama matendo yasiyo stahili kuhusu utumwa, ubaguzi, itikadi kali, na ubaguzi wa kijinsia. Hili pia limechelewa kwa kutoitikia vyema masuala ya uzalilishaji wa wanawake katika ulimwengu wa kisasa. Mungu katika Kristo amemweka huru mtumwa na mwanamke. Si thubutu kuruhusu

maandiko yenye utamaduni unaopingana na haya.

Hoja moja zaidi: kama mtafsiri ninafahamu kuwa Korintho lilikuwa ni kanisa lililoharibiwa sana. Vipawa vilivyotolewa vilikuwa vya majivuno. Wanawake wangeweza kuwa wameshikwa katika hili. Pia ningeweza kuamini kuwa Efeso ilikuwa imeaathiliwa na walimu wa uongo waliofanikiwa kutumia wanawake kama wasemaji mbadala ndani ya makanisa ya Efeso.

C. Mapendekezo kwa usomaji zaidi
1. *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart (kur. 61-77)
2. *Gospel and Spirit: Issues in New Testament Hermeneutics* by Gordon Fee
3. *Hard Sayings of the Bible by* Walter C. Kaiser, Peter H. Davids, F. F. Bruce, na Manfred T. Branch (kur. 613-616; 665-667*)*

**5:21"mnanyenyekeana"** Kunyenyekea nani kanuni ya kiulimwengu ambayo inawahusu waamini wote, lakini kwa upekee haiwezi kukamilishwa kupitia kujitoa kwa Roho (yaani, maisha ya kujitoa hadi kufa). Huu ni ushahidi wa kimageuzo ya anguko.

**NASB, NKJV "katika kicho cha Kristo"**
**NRSV "mbali na unyenyekevu kwa ajili ya Kristo"**
**TEV "kwa sababu ya unyenyekevu kwa ajili ya Kristo"**
**NJB "katika utii kwa Kristo"**

◙" **Kicho**" ni dhana ya Agano la Kale ya kumwabudu Yule Mwenye nguvu. Ule utakatifu na upekee wa YHWH, au hata uwepo wa ulimwengu wa kiroho (malaika), unasababisha athari kubwa ndani ya mwanadamu aliyeanguka! uhusiano wa waaamini wawili unaathiriwa na imani yao katika Kristo. Kumheshimu Yeye huleta heshima kwa wanadamu wote aliowatolea maisha yake (kama vile. Rum. 14:1; 15:13). Waamini wanaonyesha upendo wa Kristo kwa namna wanavyowapenda wengine (kama vile. 1 Yn 4:20).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 5: 22-24**
**22 Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. 23 Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. 24 Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.**

**5:22 "Enyi wake, watiini"** Hapana kitenzi katika andiko la Kiyunani la Efe. 5:21 (ambacho ni moja ya zile kauli tano endelevu za wakati uliopo zinazoelezea maisha ya kujazwa na roho). Katika muktadha huu sio amri, lakini ni kauli ya kati au tendwa endelevu ya wakati uliopo. Amri pekee ilielekezwa kwa waume katika Efe 5:25 (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo)! Wanaume wanapaswa kutenda katika upendo wa kujitoa kwa wake wao, ambao baadadye hujitoa ki-hiari.

hata hivyo kuna sura mbali mbali zenye kufanana ambazo hutetea wanawake kuwatii waume zao:
1. kauli tendwa shurutishi katika Kol. 3:18
2. kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo katika Tito 2:5 iliyotumika kama shurutishi
3. kauli nyingine tendwa endeelvu ya wakati uliopo katika 1 Pet. 3:5 iliyotumika kama shurutishi

sura zinazofanana zinawalazimisha watafasiri kuchukua wakati endelevu katika Efe. 5:21 kama kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo iliyotumika kama shurutishi (kama vile 1Pet. 3:1). Bado ni muhimu kuwa irabu iko kwenye hali ya kutendewa. Wanawake wanapashwa kumruhusu Roho atende kazi hii katika maisha yao. Vitabu vyote the *Analytical Greek NewTestament* by Barbara na Timothy Friberg and *An Analysis of the Greek NewTestament* by Max Zerwick and Mary Grosvenor vinakiita hiki kitenzi kama irabu tendwa, lakini *The Analytical Greek Lexicon Revised*, kilicho haririwa na Harold K. Moulton; *Word Pictures In the NewTestament* by A. T. Robertson; na "Waefeso" katika *The Anchor Bible Commentary* by Markus Barth inakiita kama irabu ya kati. Lugha ya Koine, huko Uyunani walikuwa katika mchakato ya kuzifanya hizi irabu mbili kuwa kitu kimoja. Paulo anayaelezea maisha ya ujazwaji wa roho kwa kutumia washirika watatu wa kipindi kile cha Wagiriki na Warumi

cha mandhari ya kinyumbani ambapo hapakuwepo na haki kwa wake, watoto na watumwa. Alionyesha namna gani Roho anabadilisha ushirika wa kitamaduni kwenda ushirika wa kiroho, haki kwenda uwajibikaji.

◙ kama hali ya kuendelea ni ya kati basi inasisitiza juu ya ushiriki wa hiari wa wake katika utii wa kindoa kwa faida itokanayo na amani, ndoa yenye upendo ikiwa na wanandoa wanao amini. Kama hali ya kuendelea ni tendwa basi inaonyesha hitaji la mke kumruhusu Roho kutenda kazi yake ndani ya moyo wake (kama vile Efe. 5:18) ambayo inaathiri wote mme na watoto, pia na wale watumwa wa nyumbani.

◙**"kama kwa Bwana"** Mtu anatakiwa kulinganisha Kol. 3:18, "katika Bwana." Sio kwamba mwanaume ndiye ana hatma ya mamlaka, bali hao wanawake wanapaswa kuwatii waume zao kwa sababu ya uhusiano wao na Kristo. Yesu aliweka mwongozo kwa ajili ya vyote kutii mamlaka (yaani., mara zote mapenzi ya Baba) na utekelezaji wa mamlaka (yaani., juu ya kanisa, kama vile Efe. 5:25)

**5:23 "mwanamme ni kichwa. . .kama Kristo alivyo kichwa"** Kristo anafananishwa na mwanaume na kanisa kama bibi harusi (k.v. Ufu. 19:7; 21:2,9). Wanaume wanapaswa kutenda katika uongozi wao waliopewa kama vile Kristo alivyopewa. Alijitoa mwenyewe kwa ajili ya kanisa. Sio suala la udhibiti , bali ni suala la ujitoleaji wa mtu mwenyewe. Ukuu wa mwanaume ni suala mtambuka katika jamii zetu za leo. Hili ni kwa sababu mbali mbali:

1. tunashindwa kuelewa uongozi wa kitumishi
2. hatuupendi ukuu wa familia kwenye jamii kwa sababu ya misisitizo ya leo yenye kupenda usawa juu ya thamani binafsi
3. tumechanganywa na namna ya kimafumbo ya Biblia yenye kutetea ukuu wa mwanaume katika baadhi ya sura na usawa kwa wengine

kwa mapendekezo yangu jibu lipo katika mifano ya Yesu kama mwenye ukuu wa kweli ukilinganisha na kanisa na utumishi wa kweli (utii) kwa Mungu aliye Baba. Utii huu pasipo namna yeyote unaelezea kutokuwepo na usawa, lakini ni uongozi sanifu wa kiutendaji. Ukuu wa mwanaume unaelezea aina ya uongozi ambao unatumikia hitaji la wengine kwa maana ya kujitoa kibinafsi. Jamii zetu za kisasa zinakataa mamlaka, lakini bado zinatafuta ukuu!

Kibinfasi naweza kukubali ukuu wa mwanamme kutokana na anguko(kama vile Mwa. 3:16; 1 Tim. 2:12-14). Vile vile pia inalithibitisha kama dhana ya kibiblia katika mwanga wa uongozi wa Yesu juu ya kanisa (kama vile. Efe. 5:22-33). Lakini kile ninachoona kigumu kukubali ni mamlaka ya ukuu wa familia (yaani., jamii za kiume zinazomilikiwa) kama mpango wa Mungu uliofunuliwa kwa kila lika na jamii (kama vile. Rum. 3:27; 1 Kor. 12:7, 13; Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Je mapatano ni dhahili katika Mwa. 1:27; 2:18 ambayo yalipotea kwenye kipindi cha uasi wa Adamu na Hawa (kama vile. Mwa. 3:16), je laana ya dhambi na unyenyekevu vyote vilishughulikiwa wakati wa ukombozi wa Yesu? kama enzi mpya inavyogonga ndani ya maisha ya waamini sasa, ndivyo ilivyo pia kwa urejesho wa ushirika kamili na Mungu kama ilivyokuwa Edeni ndivyo imeanza sasa?

Pia ningalipenda kutoa hoja ya kanuni za ufasiri. Kama mtafasiri wa kile ninacho amini kuwa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja wa kweli na Kristo wake, ninashangazwa kwa dhana ya kitamaduni ya maandiko. Tunaona dhahiri kuwa katika Agano la Kale (tohara, sheria za chakula, sheria za ukoma, nakadharika). Lakini ni vigumu zaidi kwetu sisi kama Wakristo wa leo kuyaona katika Agano Jipya. Nina uhakika hii (1) ni kwa sababu ya upendo wetu na heshima kwa ajili ya Biblia na (2) mwenendo wetu dhidi ya uhalisia wa mapendekezo.

Hoja hizi mbili zilizoko mbele yangu zina dhana ya wazi ya kitamaduni (1) wanaume walitawala jamii (mkuu wa kaya) na (2) utumwa. Agano Jipya kamwe halijaribu kuelezea kutolingana kwa nguzo hizi mbili za kitamaduni za ulimwengu wa kale. Yumkini kwa sababu kufanya hivyo kungalimaanisha kuangamiza Ukristo. Bado injili kwa muda wote inayaondoa yote! Ukweli wa Mungu kamwe haubadiliki lakini jamii inabdilika. Ni kosa kubwa kwetu sisi kugeuza tamaduni za karne ya kwanza kipindi cha Wagiriki na Warumi kwenda mapenzi ya Mungu kwa watu wote katika sehemu zote na vile vile ikawa kweli kwa tamaduni ya Israel. Ndani ya kila moja ya hayo Mungu anajidhihilisha mwenyewe kwa nguvu na njia za moja kwa moja. Kazi kubwa ni jinsi ya kupata umilele usio na masharti toka kwenye ganda la kitamaduni. Kitabu kizuri kinachojadili suala hili ni Fee and Stuart, *Howto Read the Bible For All Its Worth.*

Njia mojawapo ya kuamua ni kipi cha milele na, kwa hiyo, kuwalazimisha waumini wote kuyafuata kwa kipindi chote na ni kipi cha kiutamaduni au upendeleo binafsi ni kuangalia kama Biblia (Agano la Kale na Agano Jipya) inatoa ujumbe wenye kufanana au inaweka kumbu kumbu ya maoni tofauti (kama vile. Fee and Stuart's *Howto*

*read The Bible for All Its Worth*). Hofu yangu ni kuwa naweza leta mafundisho yangu ya kimadhehebu, tabia, tamaduni na upendeleo binafsi kunyamazisha ukweli uliofunuliwa! Hatma yangu ya mamlaka ni Mungu na mafunuo yake (yaani., ndani ya Mwana wake na katika kumbu kumbu zilizo andikwa, yaani Biblia). lakini natambua alijidhihilisha Yeye mwanyewe kwenye kipindi maalum cha historia, kwenye tamaduni fulani na kila kitu katika utamaduni huo ulikuwa sio mapenzi yake. Na bado, Mungu alihitaji kuongea kwa watu wa tamaduni hizo kwa namna wanavyoweza kuelewa. Kwa hiyo Biblia ni nyaraka ya kihistoria. Sipendi kutowekea maanani dhana yake ya nguvu za siri au dhana ya kitamaduni.

**MADA MAALUM: KICHWA (*KEPHALĒ*)**

Pamekuwepo na mazungumzo mapana ya kithiolojia juu ya maana ya "kichwa" (*kephalē*). Neno linaweza kutambulika kama

1. Ufanano wake katika Kiebrania kwenye Agano la Kale ni *rosh* (BDB 910, KB 1164), ambalo laweza kumaaanisha
   a. Kichwa
   b. Kiongozi
   c. Mwanzo au asili
   d. Jumla yote (kama vile *Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, juzuu. 3, kur. 1015-1020)
2. Katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani neno *rosh* linatafasiriwa na neno la Kiyunani
   a. *archē* (mwanzo, kama vile Zab. 137:6)
   b. *prōtotokos* (awali, kama vile 1 Nya. 5:12)
   c. *kephalē* (kichwa)
      1) Kichwa cha mtu
      2) Kichwa cha mnyama
      3) Kilele cha Mlima
      4) Kilele cha Mnara (kama vile Mt. 21:42)
3. Katika Agano Jipya *kephalē*
   a. Kichwa cha mtu (kama vile 1 Kor. 11:4,5,7)
   b. Kichwa cha mnyama
   c. Mwanzo au asili
   d. Jumla
   e. Kiongozi
      1) Yesu ndiye kichwa cha watawala wote na wenye mamlaka, kama vile Kol. 2:10
      2) Yesu ndiye kichwa cha kanisa (kama vile Efe. 4:15; 5:23; Col. 1:18; 2:19
   f. Mme (kama vile Efe. 5:23)

( *Dictionary of New Testament Theology*, juzuu ya. 2, kur. 156-163)

**5:24 "lakini kama ilivyo kanisa limtiivyo Kristo"** Muundo wa kitenzi hiki ama ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo au kauli ya kati elekezi ya wakati uliopo (angalia maelezo katika aya ya nne kwa Efe. 5:22). Kama mwanamke atiivyo mbele ya mmewe kwa (1) mapenzi yake mwenyewe (irabu ya kati) au (2) kwa sababu amewezeshwa na Roho wa Mungu (irabu tendwa), vile vile kwetu, kanisa lazima kujitoa kwa Kristo.
◙**"kanisa"** Angalia maelezo katika Efe. 3:10 na Mada Maalum katika Kol. 1:18.

◙**"kwa kila kitu"** Kristo, na sio mme, lazima awe hatima ya mamlaka (kama vile Mt. 10:34-39). Huu mstari haumfungi mwanamke anayeamini kuendelea kuwa na mwanaume mbovu wala aweze kuyasamehe matendo maovu au matendo yanayo lazimishwa na mwanaume mwenye kutumia mamlaka.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAEFESO 5:25-6:3**
**[25]Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; [26]ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; [27]apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. [28]Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe. [29] Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa. [30]Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. [31]Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. [32] Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa. [33] Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe; wala mke asikose kumstahi mumewe. [1] Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. [2] Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, [3] Upate heri, ukae siku nyingi katika dunia.**

**5:25 "waume, wapendeni wake zenu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ambayo ndiyo pekee yenye kushurutisha katika kifungu hiki. Mwanamume anapaswa kuweka mazingira ya kiroho nyumbani kwa kuendelea kumpenda mkewe kama Kristo alivyolipenda kanisa. Kimsingi huu ulikuwa usemi chanya katika siku zile, lakini katika siku zetu kifungu kizima kinaonekana kuwa kinyume kwa sababu kinaaksi dhana ya kitheolojia ya ukuu ndani ya nyumba (kama vile Mwa. 3:16; 1 Kor. 11:3; 2 Tim. 2:13). Hata hivyo, Wanaume wa ki-Kristo ni viongozi wa kitumishi, si wakuu.

◙**"akajitoa kwa ajili yake"** Kile kihusishi cha Kiyunani cha neno *huper* kinamaanisha "kwa ajili ya. " Hiki kinarejelea kutengwa kwa ajili ya wengine, upatanisho wa Kristo kwa ajili yetu. Hii pia ni aina ya upendo wa kujitoa unaohitajika kwa wanaume.

**5:26"ili makusudi alitakase"** Vitenzi vikuu katika Efe. 5:26,27 vyote ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu (kama vile Yn 17:17-19; Tito2:14; Ebr. 10:10,14,29; 13:12). Neno takasa linatokana na mzizi "takatifu." Sababu ya uthibitisho ni utakaso (kama vile Efe. 1:4; Rum. 8:29-20). Dhamira tegemezi inaongeza ukumbusho wa tahadhari.Kama kanisa linavyotakiwa kuwa na umoja, vivyo hivyo, mwanamke.

**NASB "alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; "**
**NKJV "alitakase na kuliosha kwa maji na neno"**
**NRSV "kwa kulitakasa na kulisafishakwa maji na neno"**
**TEV "kwa neno lake, baada ya kulisafisha katika maji"**
**NJB "Yeye alilitakasa na alilisafisha katika maji kwa muundo wa maneno."**

Bila shaka hii ni sitiari ya Agano la Kale ya kwa ajili ya kutakasa (kama vile Yohana 15:3; Tito 3:5). Hii inaweza kurejelea juu ya

1. liturujia ya ubatizo (kama vile Mt. 28:19-20; Matendo 2:38; Tito3:5
2. ukiri wa imani mbele ya umma katika ubatizo (kama vile Matendo 22:16; 1 Kor. 6:11)
3. Mwendelezo wa sura ya ndoa, taratibu za bibi harusi kufundwa kabla ya harusi, kama ishara ya utamaduni wa usafi

"Neno lenyewe" yumkini halirejelei juu ya Biblia, bali juu ya maneno ya msimamizi wa ubatizo ama weledi wa imani ya mtahiniwa.

**5:27"apate kujiletea Kanisa tukufu"** Hii ni kauli nyingine tendaji tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu, ambayo inawakilisha kiashiria cha hali ya tahadhari. Hili linaonekana kurejelea Karamu ya Harusi ya Mwanakondoo (kama vileUfu.19:6-9). Kama lilivyo pendo la Kristo liletavyo mapinduzi ndani ya kanisa, vivyo hivyo nasi, upendo wa mume kwa mke wake lazima uimarishwe na kuibariki nyumba ya Mkristo.

◙**"ila"** Kiuhalisia hili ni neno linalomaanisha "kisicho na uchafu."

◙**"kunyanzi"** Kifasihi hili linamaanisha "lisilo na dalili za nyakati."

◙**" takatifu"** Hili linatokana na mzizi huo huo kama "kutakasa" katiaka Efe. 5:26 (kama vile Efe. 1:4). Tazama Mada Maalum: Takatifu Efe. 1:4.

◙**"pasipo mawaa"**Hili ni neno la kiutakaso la Agano la Kale (kama vile 1 Pet. 1:19). Dhana hii hii inatajwa kama mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kanisa katika Efe. 1:4. Tazama Mada Maalum: Mawaa katika Kol. 1:22. Kusanyiko la uzito wa maneno haya yote ni kwamba Mungu hutamani ule utakatifu ulio kamili kwa watu Wake (Efe. 1:4). Kusudi la Ukristo ni kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; Gal. 4:14). Sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu vitarejeshwa!

**5:28"kama miili yao wenyewe"** Wanaume wa ki-Kristo wakiwapenda wake zao wa ki-Kristo, wanajipenda wao wenyewe kwa sababu ndani ya Kristo wao ni "mwili mmoja" (kama vile Mwa. 2:24). Kama kanisa lilivyo mwenezi wa Kristo, wanaume na wanawake ni waenezi wa kila mmoja.

**5:29"huulisha"**Hii ni sitiari ya ndege ambayo inamaanisha "kumlisha apate kukua." Hili linatumika juu ya kuwalea watoto katika Efe.6:4.

◙**"kuutunza"** Hii ni stiari nyingine ya watu wa aina moja, "kupasha joto." Haya maneno mawili yanapaswa kusisimua matendo ya kila mwanaume wa ki-Kristo kumhusu mkewe. Wanaume ni mawakili wa karama za wake (na watoto) wao pamoja na wao wenyewe! Kiongozi wa nyumba ya kiroho lazima atafute ukomavu wa kila mwana familia ndani ya Kristo.

**5:30"tu viungo vya mwili wake"** Kanisa kama mwili uonekanavyo ni moja ya sitiari za Paulo kuhusu ushirika ambao husistiza umoja katikati ya tofauti (kama vile 1 Kor. 12:12-27).

**5:31** Hii ni nukuu inayotoka katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani (LXX )ya Mwanzo 2:24. Kama familia ya ki- Kristo ilivyo kama chombo hai, ndivyo lilivyo kanisa la Kristo.Familia lazima iwe ni umoja usiotengana, kama kanisa na Bwana wake walivyo (kama vile Yohana 17:11,21-22) mwili mmoja (kama vile 1 Wakorintho 12). Ukweli huu unapinga kutojumuishwa kwa walimu wa uongo wa siku zile.

**5:32 "*32* Siri "** Toleo la Kilatini lina neno "sakaramenti," lakini hili ni ingizo la kimaandishi linalofuatisha utaratibu wa kanisa la Romani la utoaji wa sakaramenti. Paulo anatumia neno "siri" mara kadhaa bila shaka ni kwa sababu lilikuwa neno lililopendwa na walimu wa Uongo. Paulo analitumia katika njia nyingi. Hapa hili linahusiana na ulinganifu wa ki-sitiari kati ya wanaume na wake/Kristo na kanisa. Kwa mjadala kamaili tazama 1:9 na 3:3.

**5:33"ampende. . . kumstahi"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo na kauli ya kati (shahidi) tegemezi ya wakati uliopo. Mwanamme analazimishwa kuendelea kumpenda mkewe kama anavyojipenda (mwili mmoja, Efe. 5:31) na wake wanaitwa katika kujitoa na kuwastahi waume zao, ambapo itaongeza na kuimarisha uhusiano wa upendo kati yao. Huu ni usemi mfupi wa kifungu kizima (Efe. 5:21-33).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini ni muhimu sana kwa waamini kuishi maisha ya ki-Mungu?
2. Kwa nini dhambi za uasherati zinasistizwa katika muktadha huu?
3. Wakristo wanaweza kuanguka kutoka katika neema kutokana na maisha yao? (kama vile Efe. 5:5)

4. Je! "kujazwa Roho"kunahusisha nini?
5. Kwa nini 5:22-6:9 inaonekana kuwa kiini chanya cha msingi katika siku zake lakini ni kinyume katika siku zetu?
6. Je! 5:22-33 inafundisha kwamba wanawake wanapaswa kujitoa kwa wanaume?
7. Kwa nini Paulo anailinganisha nyumba ya Mkristo na kanisa?

# WAEFESO 6

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Watoto na Wazazi | Watoto na Wazazi | Mambo ya Nyumbani ya Mkristo (5:21-6:9) | Watoto na Mkristo | Maadili ya Nyumbani (5:21-6:9) |
| 6:1-4 | 6:1-4 | 6:1-3 | 6:1-3 | 6:1-3 |
| | | 6:4 | 6:4 | |
| Watumwa na Mabwana | Watumwa na mabwana | | Watumwa na mabwana | |
| 6:5-9 | 6:5-9 | 6:5-8 | 6:5-8 | 6:5-9 |
| | | 6:9 | 6:9 | |
| Vita dhidi ya Uovu | Silaha zote za Mungu | Silaha za Mungu na maslahi ya Mkristo | Silaha zote za Mungu | Mambo ya rohoni |
| 6:10-20 | 6:10-20 | 6:10-17 | 6:10-13 | 6:10-13 |
| | | | 6:14-20 | 6:14-17 |
| | | 6:18-20 | | 6:18-20 |
| Salamu za Mwisho | Salamu za neema | Mambo binafsi na dua | Salamu za mwisho | Babari za binafsi na salamu za Mwisho |
| 6:21-22 | 6:21-24 | 6:21-22 | 6:21-22 | 6:21-22 |
| 6:23-24 | | 6:23-24 | 6:23-24 | 6:23-24 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (**Kutoka**["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")](#))

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 6:1-9

A. Kipengele cha fasihi kinaanza katika Waefeso 5:22 kama Paulo anatumia nyumba ya Kikristo kama mfano mmojawapo wa namna gani ya maisha yaliyojaa Roho (kama vile Waefeso 5:18) yanavyoleta matokeo katika maisha ya kila siku.
B. Mifano ya kinyumbani nyumbani ya Paulo inazungumzia jozi tatu
   1. Wake na waume
   2. Watoto na wazazi
   3. Watumwa wa nyumbani na mabwana
C. Paulo kwanza anawahutubia wale wote ambao hawakuwa na haki za kiutamaduni au nguvu (wake, watoto, watumwa), lakini pia anawahutubia wale wenye nguvu (waume, wazazi na wamiliki wa watumwa).
D. Mfano huu wa nyumbani unajishughulisha na nyumba ya Mkristo. Nguvu ya heshima ya ukaribu na upendo unaweka utaratibu. Muktadha huu hauzungumzii jambo la upande mmoja tu la jozi tatu la kuwa Mkristo. Matendo ya waaminio kuelekea kwa wengine linaamriwa na mahusiano kwa Kristo na sio uthamani wa upande mwingine.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:1-3**
**[1] Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. [2] Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, [3] Upate heri, ukae siku nyingi katika dunia.**

**6:1"watoto"**Hakuna uhakika umri gani unamaanishwa hapa. Katika maisha ya Kiyahudi mvulana anakuwa mwanaume, mwajibikaji kwa sheria na ndoa akiwa katika umri wa miaka 13 (yaani, *bar mitzvah*); msichana anakuwa mwanamke katika umri wa miaka 12 (yaani, *bar mitzvah*). Katika utamaduni wa Kirumi, mvulana anakuwa mwanaume katika umri wa miaka 14, katika utamaduni wa Kiyahudi katika miaka 18.

◙ **"tiini"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo "kusikia" na "chini." Wakolosai kwa usambamba inaongeza "katika vitu vyote." Utii lazima uwe kwa kipindi kilichoamriwa (utoto). Hata amri hii lazima iwiane na Mathayo 10:34-39. Kilele cha mamlaka si uzazi bali uungu.

◙ **"katika Bwana"** Tungo hii imeondolewa katika Maandiko ya kale ya Kiyunani B, D4, F na G, lakini hii iko katika $P^{46}$, א, A, na $D^1$ kama vile katika tafsiri za Vulgate, Peshitta,Ki- Coptic na Ki-Armenian. Ujumuisho wake unafanya kuwa hakika kuwa muktadha wake ni nyumbani kwa Mkristo. Muktadha huu unamaanisha wote mtoto wa kikristo na wazazi wa mkristo..

◙ **"Maana hii ndiyo haki"** Biblia kwa uwazi zinaelezea uhusiano unaotolewa na Mungu kati ya wazazi na watoto (kama vile Kol. 3:20; Mithali 6:20; 23:27). Familia yenye nguvu inatengeneza jamii yenye nguvu.

**6:2 "heshima"** Hii ni kauli tendaji shurutishi. Ni nukuu kutoka katika Amri Kumi za Mungu (kama vile Kutoka 20:12; Kumb. 5:16). "heshima" lilikuwa ni neno la kibiashara "kutoa juu uzito." Ililiaksi dhana ya Agano la Kale ambalo ni “zito”. Wazazi wanatakiwa waheshimiwe na kupewa thamani na wazazi wa Mkristo. Hakuna wazazi wakamilifu (kama ilivyo kuwa hakuna watoto wakamilifu).

◙ **"baba na mama"** Hii inaonesha kuwa wazazi wote wanastahili heshima na adhama.

◙ **"(ambayo ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi)"** Nukuu hii katika Waefeso 6:3 inatumika katika Kumbukumbu la Torati katika muktadha kadhaa tofauti (kama vile Efe. 4:40; 5:16, 33; 30:17-18). Sio ahadi ya kibinafsi ya maisha marefu lakini ahadi ya kitamaduni ya uthabiti wa kijamii. Utaona kwamba Paulo kwa kunukuu Amri kumi anaonesha kwamba sheria (Mwanzo-Kumbukumbu la Torati) ilikuwa liko katika utendaji kazi kulingana na mwongozo wa ufunuo kwa Mkristo (kama vile Efe. 4:25, 26; Rum. 10:4; 13:9-10; Gal. 2:15-21) lakini si kwa ajili ya wokovu (kama vile Wagalatia 3)

**6:3 "duniani"** Paulo alichukua nukuu kutoka katika Agano la Kale "katika ardhi ambayo Bwana Mungu wako amekupatia" (kama vile Kutoka 20:12; Kumb. 5:16) na kuligeuza katika kanuni ya jumla. Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi walichukua ahadi za Agano la Kale kwa Israeli na kuzifanya katika kweli ya kiulimwengu.

| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:4** |
|---|
| [4] **Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana.** |

**6:4**
**NASB,NKJV**
**NRSV** **"wababa"**
**TEV, NJB** **"wazazi"**

Maandiko ya Kiyunani "wababa." Fasiri ya kisasa ya kiingereza inayofanana na hii (TEV na NJB) imepanua maana kwasababu ya Efe. 6:2, ambapo wote baba na mama wanatajwa, Hata hivyo katika muktadha kubwa ya Efe. 5:21-6:9, Paulo anaelezea makundi matatu ya watu waliokuwa hawana haki, wake, watoto, watumwa na kuwaelezea wale ambao walikuwa na haki zote-waume, wababa na mabwana. Kuna uwajibikaji wa kiroho kwa kila muumini Mkristo wa nyumbani..

◙ **"msiwachokoze"**Hii ni kauli tendaji shurutishi yenye kiambishi hasi ambacho mara nyingi inamaanisha kuzuia kitendo kilicho katika mchakato (kama vile Kol. 3:21) Luka 5:25, hii ilikuwa ni uwiano unaotakiwa katika kipindi cha ulimwengu wa kati ya Wagiriki na Warumi na yetu. Wababa sio mamlaka yenye kilele lakini mawakala wa wakristo wa familia zao. Wababa wa wakristo lazima waelewe kazi yao ya uwakala katika maisha ya watoto wao. Baba wanatakiwa wawafundishe mambo binafsi wayatakayo zaidi wao lakini yakiwa kweli za Biblia. Lengo sio mamlaka ya kimalezi, lakini kurithisha mamlaka ya Mungu kwa watoto. Siku zote kuna pengo la mtindo wa maisha kati ya kizazi kimoja na kingine lakini kamwe si pengo la kimamlaka ya kiungu. Watoto si lazima kuaksi tabia za kiuzazi, uchaguzi au mtindo wa maisha unaopendeza kwa Mungu. Lazima tuwe makini na shauku ya kuwachonga watoto wetu katika namna ya uelewa wa uzoefu wetu wa uelewa wa au kuaksi tuvitendavyo zaidi.

Kama mchungaji karibu na shule kubwa ya serikali, niligundua wengi wa vijana watukutu walitoka katika nyumba za wakristo wenye msimamo mkali ambazo hazikuwaruhusu kufanya maamuzi yao binafsi au kuwa na uhuru. Uhuru ni uzoefu wenye sumu na lazima utambulishwe katika hatua za mwanzo za uwajibikaji. Watoto wakristo lazima wajenge maisha yanayojikita katika msukumo binafi na imani, sio miongozi ya pili ya wazazi..

◙ **"kuwakuza"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ambalo linatoka katika mzizi wa neno hilohilo , "kulisha kuelekea makuzi," kama katika Efe. 5:29. Kama ilivyo majukumu ya mume kuendelea kusaidia mke wake kuendelea kumsaidia mke wake kukua makuzi ya kiroho na karama, anatakiwa pia kusaidia watoto wake kufikia makuzi yao kamili ya kiroho na karama (kama vile Efe. 4:7).

**NASB, NRSV** "**katika nidhamu na maelekezo ya Bwana"**
**NKJV** **"katika mafunzo na maonyo ya Bwana"**

| | |
|---|---|
| **TEV** | **"nidhamu ya mkristo na maelekezo"** |
| **NJB** | **"wasahishe na kuwaongoza kama Bwana afanyavyo"** |

Neno la kwanza linatoka katika mzizi wa Kiyunani kwa ajili ya "mtoto" na inarejerea kwa mafunzo ya kimalezi ya watoto (kama vile Ebr. 12:5,7,8,11) na kwa ajili ya mafunzo ya Bwana ya waaminio (kama vile 2 Tim. 3:16).

Neno la pili ni neno la kiujumla kwa maonyo, masahihisho au maonyo (kama vile 1 Kor. 10:11; Tito 3:10). Mafunzo ya watoto katika imani ilikuwa msisitizo mkubwa ya dini ya Kiyahudi (kama vile Kumb. 4:9; 6:7-9, 20-25; 11:18-21; 32:46). Mafunzo ya kizazi yanatambua umuhimu wa kurithisha imani binafsi na kweli za injili ya Mafunzo, sio upendeleo wa binafsi au maoni ya kitamaduni ya wazazi kuelekea kizazi kijacho.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:5-8**
**5 Enyi watumwa, watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo; 6 wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekezao kwa wanadamu bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo; 7 kwa nia njema kama kumtumikia Bwana wala si mwanadamu; 8 mkijua ya kuwa kila neno jema alitendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana kwamba ni mtumwa au kwamba ni huru.**

**6:5 "watumwa"** Huu ni mfano wa tatu wa kinyumbani kuonesha namna gani kujazwa na Roho Mtakatifu kunafanya tofauti kila siku (kama vile Kol. 3:22). "Watumwa" (*douloi*) inarejerea watumwa wa nyumbani.

◙ **"kuwa mtii"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Kuna usambamba mkubwa katika kifungu hiki cha habari katika 1 Petro 2:18-21. Kuna usambamba wa uwazi kati ya wake, watoto na watumwa, isipokuwa kwamba wake walikuwa hawaamriwi kutii kama watoto (kwa kipindi) na watumwa.

## MADA MAALUM: MAONYO YA PAULO KWA WATUMWA

1. utosheke, lakini kama patakuwepo na fursa kwa ajili ya kunufaika na uhuru wenyewe, chukua (1 Kor. 7:21-24).
2. Katika Kristo hapana mtumwa wala (Gal. 3:28; Kol. 3:11; kama vile 1 Kor. 12:13).
3. Tenda katika Bwana, naye atakulipa (Efe. 6:5-9; Kol. 3:22-25; kama vile 1 Pet. 2:18-20).
4. Katika Kristo watumwa huwa ndugu (1 Tim. 6:2; Filemoni 1:16-17).
5. Watumwa wa ki-Mungu huleta heshima kwa Mungu (1 Tim. 6:1; Tito 2:9).

Maonyo ya Paulo kwa wamiliki wa watumwa:

Watumwa wa Kikristo na mmiliki wa watumwa wana Bwana mmoja, kwa hiyo, kwa hiyo, wanapaswa kuwatenda wengine kwa heshima (Efe. 6:9; Kol. 4:1).

Utumwa ni moja ya iana ya kitamaduni (kama vile tamaduni za wazee wa kaya) ambao walikuwa ndio nguzo ya ulimwengu wa karne ya kwanza. Agano Jipya halileti changamoto wala mwelekeo. Hata hivyo, kweli ya injili, kwa muda iliathiri mabadiliko katika mwelekeo wa utamaduni.

◙ **"ambao ni mabwana kwa namna ya mwili"** Hapa neno la Kiyunani mwili *(sarx)* inatumika kwa namna ya mwili, sio uovu. Hii kweli ya jumla inahusiana na wote mabwana wakristo na mabwana wapagani (yaani kwa wote wakarimu na wasio karimu). Angalia tungo "katika Bwana" haipatikana hapa kama katika mifano mingine miwili iliyopita (kama vile Efe. 5:21 na 6:1). Tamaduni za Magharibi za kisasa hazina watumwa, ila bado ukweli huu wa kiroiho unatumika katika waajiri na waajiriwa wa kikristo.

◙ **"kwa kuogopa na kutetemeka"** Hii ni sitiari ya heshima (kama vile 1 Kor. 2:3; 2 Kor. 7:15; Fil. 2:12).

◙ **"kwa dhati ya moyo"** Hii ni sitiari kutoka katika neno "singleness" (umoja wa nia). Inatumika katika namna mbili

katika Agano Jipya (1) dhati (kama vile II Kol. 1:12; 11:3; Kol. 3:22) au (2) ukarimu (kama vile Rum. 12:8; 2 Kor. 8:2; 9:11,13). Katika muktadha huu ni wazi #1. Msukumo wa mwamini siku zote ni ufunguo unaopelekea vitendo sahihi, sio utazamaji (kama vile Efe. 6:6- 7). Waamini wanaishi maisha yao katika kila eneo kama vile wanamuishia Bwana (kama vile Kol. 3:22-25 na Rum. 14:7-9)! Wanasukumwa si kwa uthamani au vigezo vyao lakini kwa vile walivyo katika Kristo. Waume wakristo wanawapenda wake zao si kwasababu wake zao ni wakamilifu au wanastahili lakini kwasababu ni wakristo. Huu ni ukweli wa mahusiano yote kati ya binadamu. Waamini wanampenda Mungu kwa kuwapenda wengine waliofanywa kwa mfano wake, ambao aliwafilia (kama vile 1 Yohana 2:9, 11; 4:20). Angalia Mada Maalum katika Kol. 2:2.

◙ **"kama kwa Kristo"** Waamini hufanya kazi kuelekea wengine kwasababu ya uhusiano wao kwa Kristo, na sio kwasababu wanastahili (kama vile Efe. 5:22; Rum. 14:7-9). Hii ni kweli kwa wake na waume, wazazi na watoto, mabwana na watumwa. Waaminio wanawafanya watu wawe kipaumbele kwasababu ya sura ya Mungu na upendo kwao, sio kwasababu ya vigezo vyao binafsi.

**6:8 "mkijua kuwa kila jambo jema**a" Muktadha huu si wa mazingira ya kuabudu bali uhusiano wa kila siku wa waaminio na wengine,wakristo wenzetu na wasio amini. Mungu haangalii matendo yetu yote. Hakuna ukawaida; yote yamewekwa wakfu! Mstari wa 8a ni sentensi ya daraja la tatu yenye masharti inayomaanisha matendo yatarajiwayo ya mbeleni. Waamini wanatarajiwa kutenda kazi njema (kama vile Efe. 1:4; 2:10; 4:17-5:14). Waaminio hawahesabiwi haki na Mungu *kwa sababu wanatenda* matendo mema bali wanaokolewa ili *watende* kazi njema.

◙**"watapokea kutoka kwa Mungu"** Mungu anaangalia maisha ya Waamini na watatoa hesabu (kama vile 2 Kor. 5:10). Biblia inazungumzia zawadi (kama vile Mathayo 5:12,46; 6:1-2; 10:41-42; Luka 6:23, 35; 1 Kor. 3:8, 14; 9:17-18; 2 Yohana 8; Ufunuo 11:18; 14:13; 22:12) na mataji (kama vile 1 Kor. 9:25; 2 Tim. 4:8; Yakobo 1:23; 1 Petro 5:4; Ufunuo 2:10). Paulo alikuwa anaelezea kanuni ya jumla sawa na Gal. 6:7-9.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:9**
**9 Nanyi, akina bwana, watendeeni wao yayo hayo, mkiacha kuwaogofya, huku mkijua ya kuwa yeye aliye Bwana wao na wenu yuko mbinguni, wala kwake hakuna upendeleo.**

**6:9 "mabwana"** Huu bado ni muktadha wa kifasihi 5:22-6:9, ambao ni wa kinyumbani wa Paulo "kujazwa Roho" maisha katika matendo. Katika mstari huu mabwana wanaorejerewa wako wazi, wakati katika Efe. 6:5 wanaweza kuwa aidha waamini au wasioamini.

◙ **"watendeeni wao yayo hayo"** Hii ni kauli tendaji shurutishi. Hapa tena panaitajika uwiano kwa wamiliki wa watumwa, kama 5:29 walivyo kwa waume na 6:4 kwa wazazi. Kila mtu lazima atende kwa utauwa (Kujazwa-Roho) kanuni, sio upendeleo wa kijamii. Sheria ya dhahabu ya Yesu (Mathayo 7:12) inatumika hapa.

◙ **"mkiacha kuwaogofya"** Hii ni kauli tendaji ya wakati uliopo usio timilifu. Neno kifasihi linamaanisha "kulegeza."

◙ **"hakuna upendeleo."** Neno "upendeleo" ni ambatani kutoka "kukabiliana" na "kuinua." Inaashiria hukumu ya Agano la Kale kutoa hukumu kwa haki bila kuinua uso wake kuona kama anamtambua mtuhumiwa au la. Mungu hana upendeleo kwa watu (kama vile Kol. 10:17; Mdo. 10:34; Rum. 2:11; Gal. 2:6; Kol. 3:25; 1 Petro 1:17). Ubora wote wa duniani unapita katika Kristo (kama vile Rum. 3:22; Gal. 3:26,28; Kol. 3:11). Angalia Mada Maalum: Ubaguzi wa Rangi katika Kol. 3:11.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini kifungu hiki cha habari kilikuwa kikishtusha sana wakati wa Paulo?
2. Je hili linasisitiza haki au wajibu?
3. Je kifungu hiki cha habari kinasema nini juu ya wanawake? Kifungu hiki cha habari kinaweza kutumika kama mwongozo katika siku zetu?
4. Je Waefeso 6:21 inahusiana vipi na 5:22-6:9?
5. Je inapaswa watoto wawatii wazazi? Toa maana ya "watoto."
6. Je inawezekana uhusiano wa mtumwa/bwana kufananishwa na mwajiri/mwajiriwa?
7. Je kwa namna gani wake na watoto wanahusiana na watumwa?

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA WA 6:10-24

A. Maisha ya Mkristo ni maisha ya mapambano kiroho. Matatizo, mateso, na dhiki sio vitu vya kuogofya bali kawaida, kwa Mkristo katika ulimwengu ulioanguka (kama vile Rum. 5:3-4; 8:17-18; 1 Petro 1:6-9; 2:11; 4:12-17; 5:10).

B. Vita vya kiroho vinaweza kufananishwa kimuktadha na kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo usio mkamilifu, "mjazwe kwa Roho," ya Waefeso 5:18 na kauli tendwa ya wakati uliopo (au kati, ataangalia maelezo katika Efe. 5:22) shurutishi "mfanywe imara katika Bwana," 6:10. Kama kujazwa kunahusishwa na kufanana na Kristo kila siku (Kol. 3:16) ndivyo ilivyo pia katika vita vya kiroho. Watu ni kipaumbele kwa Mungu. Uwanja wa mapambano unadhihirishwa katika uhusiano wa kila siku wa kati ya Mungu na sisi wa kila siku. Ni watu tu ndio wa milele. Japokuwa hizi kauli tendwa zinazungumzia nguvu ya Mungu, Mkristo lazima aruhusu Roho kufanya kazi katika maisha yao. Agano linajumuisha pande mbili, maamuzi ya aina mbili.

C. Lazima tuwe makini na kupitiliza: (1) shetani anasababisha kila kitu na (2) hakuna uovu binafsi. Nadhania kwasababu ya dhana ya Mungu mmoja ya Agano la Kale kwamba Shetani aliumbwa na kuendeshwa kuwa (kama vile 1 Wafalme 22:19-23; Ayubu 1-2; Zekaria 3:1-5). Yeye hayuko mahali pote wakati wote, wala hajui kila kitu. Shetani amekuwa akitajwa mapema katika barua katika Efe. 2:2 and 4:14, 27! Yeye ni mmoja wa maadui watatu ambao Wakristo wanakabiliana nae kila siku-ulimwenguni, Shetani (na wake), na mwili (kama vile Efe. 2:2-3; Yakobo 4).

D. Mungu anatupatia nyenzo na silaha, lakini waamini lazima (1) kutambua vita vya kiroho vya kila siku na (2) kujiachilia wenyewe kwa imani katika hazina za Mungu na alafu (3) kusimama (kama vile Efe. 6:11,13,14). Makuzi ya kiroho sio jambo ambalo linatokea tu, au labda kuwa linatokana na uwezo wa akili na umri (yaani akili), au karama.

E. Mistari ya 21-22 zinataka kufanana na Kol. 4:7-8. Huu ni ushahidi wa ziada wa uhusiano wa karibu kati ya vitabu hivi viwili. Hata hivyo, inashangaza kwamba mjadala mzima wa mambo ya kiroho wameondolewa katika Wakolosai. Kila kitabu kina upekee wake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:10-17**
**[10] Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. [11] Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. [12] Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. [13] Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. [14] Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, [15] na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; [16] zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. [17] Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu;**

**6:10 "hatimaye"** Kifasihi hii ni "kwa yaliyobakia." Hii ni tabia ya tungo za Paulo zinazomaanisha anaelekea kufunga barua yake (kama vile 2 Kor. 13:11; Fil. 3:1; 4:8; 1 The. 4:1; 2 The. 3:1). Mara nyingi inaashiria mpito kuelekea suala lingine jipya.

◙ **"Mzidi kuwa hodari katika Bwana"** Hii aisha ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo usio timilifu, "mfanye imara,"au kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo usio timilifu, "muwe imara." Muundo wa Kisarufi ni huohuo ni kazi tu ndiyo yenye kufanya kazi tofauti. Thiolojia iko wazi: Waamini lazima waendelee kumruhusu Roho kuwatia nguvu kwa mapambano ya rohoni yanayoendelea (kama vile Efe. 3:20; 1 Kor. 16:13). Huu mkanganyiko baina ya irabu ya sauti tendwa (nguvu ya Mungu inayotiririka kupitia waaminio) na sauti ya kati (waaminio kwa uhai wakijishughulisha katika kumuishia Kristo) ni mvutano wa kilahaja unaopatikana katika Biblia nzima. Kimsingi ni mvutano wa uhusiano wa kiagano (kama vile Fil. 2:12-13). Mungu siku zote anachukua hatua, siku zote anaandaa ajenda, lakini pia amechagua kwamba binadamu lazima waitikie (mwanzoni katika kuanzisha na kuendelea). Wakati mwingine Biblia inasisitiza mwitikio wa mwanadamu (Ezek. 18:31, "jitengenezeeni wenyewe moyo mpya na roho mpya") na wakati mwingine kukidhiwa na Mungu (kama vile Ezek. 36:26-27, "Nitawapeni moyo mpya na roho mpya ndani yenu.").Yote ni kweli!
Maneno manne ya Kiyunani (*dunamis* = nguvu; *energeia* = energy; *kratos* = uwezo na *ischus* = uweza) yanatumika katika Efe. 1:10 kufunua nguvu ya Mungu katika Kristo. Hapa, maneno ya haya matatu yanatumika.

## MADA MAALUM: KUFANYWA IMARA

Neno hili (*krataioō*) katika SAUTI IRABU TENDWA inatumika mara kadhaa katika Agano Jipya kwa maana tofauti.

1. Maendeleo ya asili ya Yesu kama mwanadamu, Luka 1:80; 2:40
2. Waamini wanatiwa nguvu na Roho Mtakatifu, Efe. 3:16
3. Waumini kuwa imara au kuwa thabiti katika imani yao katika uso wa upambanaji wa ndani katika kanisa la Korintho 1 Kor. 16:13

◙ **"katika uweza wa nguvu zake"** YHWH mara nyingi lilitumika kufunua kama mpiganaji aliyebeba silaha katika Agano la Kale(kama vile Isaya 42:13; 49:24-25; 52:10 na haswa 59:16-17).Ni ngao Yake, sio yetu. Ushindi wetu ni katika Yeye (kama vile Fil. 2:13), lakini lazima tushirikiane (kama vile Fil. 2:12).

**6:11 "vaeni silaha zote za Mungu"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati usiotimilifu ambayo inawasilisha namna ya uharaka (kama vile Efe. 6:13). Hili ni tendo la kimaamuzi la mapenzi ya Mwamini. Mungu ametupatia vifaa vyote vya kiroho vinavyotakikana, lakini lazima tutambue hitaji na kujitoa wenyewe katika kukidhiwa na Mungu na kufanya kazi katika maisha yetu kila siku (kama vile 1 The. 5:8). Kuhesabiwa haki (Warumi 4; 6) haitoi kufunguliwa ktoka katika vita ya kiroho na majaribu (kama vile Warumi 7). Uwepo wa "mtu mpya" haiashirii kuondolewa kabisa kwa"mtu wa kale." Mara nyingi vita inapanuka. Iwapo shetani hawezi kutuzuia kuokolewa, atajaribu kiroho kutufanya kuwa watu wa kushindwa na wenye kunyamazishwa!

◙ **"ili muweze kusimama"** Hii ni kauli tendwa isiyo na kikomo ya wakati uliopo inayofuatiwa na kauli tendaji ya wakati usio timilifu isiyo na kikomo, ambayo inaashiria mashindano ya kila siku, si moja yenye maamuzi ya ushindi "vita" au majaribu (Hii ni sawa na majaribu ya Yesu katika  Luka 4:13, ambapo shetani aliondoka mpaka atakapopata fursa tena). Neno "kusimama" ni neno la kijeshi likimaanisha kuendelea kuwa katika sehemu yako bila kutoka. Linarudiwa katika Efe 6:13 na 14. Kusudi lake la msingi ni ngao ya mwamini.

**MADA MAALUM: KUSIMAMA (*HISTĒMI*)**

eno hili lililozoeleka linatumika  katika namna kadhaa ya kithiolojia katika Agano Jipya

1. kujieneza
   a. sheri ya Agano la Kale, Rum. 3:31
   b. haki yenu wenyewe, Rum. 10:3
   c. agano jipya, Ebr. 10:9
   d. mamlaka, 2 Kor. 13:1
   e. Kweli ya Mungu, 2 Tim. 2:19
2. kupinga kiroho
   a. shetani, Efe. 6:11
   b. katika siku ya hukumu, Ufunuo  6:17
3. kupinga kwa kusimama katika miguu yake mwenyewe
   a. sitiari za kijeshi, Efe. 6:14
   b. sitiari za kijamii, Rum. 14:4
4. nafasi ya kweli, Yohana 8:44
5. nafasi ya neema
   a. Rum. 5:2
   b. 1 Kor. 15:1
   c. 1 Petro 5:12
6. nafasi ya imani
   a. Rum. 11:20
   b. 1 Kor. 7:37
   c. 1 Kor. 15:1
   d. 2 Kor. 1:24
7. nafasi ya majivuno, 1 Kor. 10:12

Neno hili linaelezea vyote neema ya kiagano na rehema za Mungu mwenye nguvu na ukweli kwamba waamini wanaitaji kuitikia na kufuata kwa imani!  Vyote ni kweli za Kibiblia. Lazima  vishikiliwe kwa pamoja!  Angalia Mada Maalum: Agano na Mada Maalum: Mgongano katika Maandiko

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"dhidi ya hila zote za shetani"** |
| **NKJV, NRSV** | **"dhidi ya hila zote za ibilisi"** |
| **TEV** | **"dhidi ya mbinu zote za uovu"** |
| **NJB** | **"mbinu za shetani"** |

Wakristo wanashambuliwa ma mjaribu wa kimalaika, Shetani (kama vile Efe. 2:2; 4:14, 27; 2 Kor. 2:11; 1 Pet. 5:8 9).  Shetani anatumia mbinu nyingi (*methodia*).

1. Kukosa umoja
2. dhambi binafsi
3. walimu wa uongo
4. Kukatishwa tama
5. Hali ya kutojali
6. Mateso

Hivi ni baadhi ya vitu ambavyo wapokeaji wa barua hii walikabiliana navyo. Hata hivyo waamini hawawezi kufikiria kuwa ndiyo sababu ya dhambi zote na matatizo kwa majaribu ya kimalaika au mashambulizi mwanadamu aliyeanguaka hata mwanadamu aliyekombolewa anakabiliana (1) asili ya dhambi inayoendelea; (2) mfumo wa

ulimwengu ulioanguka; na (3) mashambulizi ya kimalaika na kipepo (kama vile Efe. 2:2-3; Yakobo 4:1,4,7). Vita vinaanza katika ufahamu lakini inatembea kwa kasi kuelekea matendo ya dhambi. Kwa Mada Maalum: Uovu binafsi angalia 2:2.
Angalia hesabu ya muda "dhidi ya" inatokea katika muktadha huu (mara moja katika mstari wa 11 na mara nne katika Efe. 6:12). Ufanyikaji wa uovu unazimwa na ufanyikaji wa ngao ya Mungu!

**6:12**
**NASB, NRSV** **"Kushindana kwetu sio"**
**NKJV** **"hatushindani"**
**TEV** **"hatupigani dhidi ya"**
**NJB** **"tunatakiwa tushindane"**

Hiki ni kitenzi cha wakati uliopo kinachoashiria mashindano yanayoendelea, sio jaribu la mara moja. Hii aidha ilikuwa ni sitiari ya kijeshi au kimichezo. Kiuhalisia ina maanisha kukabiliana kimapigano mkono kwa mkono. Maisha ya Mkristo ni magumu! Maisha ya Mkristo ni ni karama ya juu unayoiishi kwa toba na imani, kama ilivyo kwa wokovu.

▣ **"dhidi ya damu na nyama"** mpangilio wa maneno unatakiwa kiuhalisia uwe "damu na nyama." Angalia namna isiyo ya kawaida ya mpangilio wa maneno haya. Inapatikana hapa tu na katika Ebr. 2:14. Sababu haijulikani, lakini inaweza ikawa inafananishwa na hali ya kudharau mwili ya wajuzi walio walimu wa uongo (Ubinadamu wa Yesu). Waamini lazima wakumbuke kwamba tatizo la kiroho ni dhambi, uovu na shetani, sio mashindano na wanadamu wengine!

▣ **"dhidi ya watawala; dhidi ya nguvu"** Maneno haya yanaweza kuhusu mamlaka ya kibinadamu kama katika Rum. 13:1-7, lakini hapa muktadha unahitaji kiwango cha kimalaika (*aeons*) ya mamlaka (kama vile Rum. 8:38-39; 1 Kor. 2:8; Kol. 1:16; 2:10, 15; Efe 1:21; 3:10; 1 Petro 3:22). Hii ni sehemu ya maoni walimu wa uongo wajuzi. Hivi viwango vya kimalaika (*aeons*) labda
1. Uovu, yaani, malaika walioanguka chini ya utawala wa shetani, ya kipepo
2. Mamlaka ya kimamlaka yaitwayo *stoichea* ambayo sio muhimu yawe maovu (kama vile Gal. 4:3,9; Kol. 2:8). Kwa ajili ya mjadala mzuri wa somo, angalia Hendrik Berkhof, *Christ and the Powers* (Herald Press). Kwa "watawala" angalia Mada Maalum: *Archē* katika Kol. 1:16.

**MADA MAALUM: VIWANGO VYA MALAIKA KATIKA MAANDIKO YA PAULO**

Walimu walifikiria kwamba malaika walikuwa na wivu wa upendo wa malaika na umakini (utolewaji wa sheria Yake katika Mlima Sinai) kwa mwanadamu aliyeanguka na, hivyo, walikuwa maadui kwao. Wajuzi wa walimu wa uongo walieleza kwamba wokovu ulikuwa unapatikana tu kwa taratibu za siri kupitia mihimili isiyo rafiki ya tufe za kimalaika (kama vile Wakolosai na Waefeso), ambayo ilipelekea mungu mwema mkuu.

George Eldon Ladd anao muhtasari mzuri wa maneno yaliyotum,iwa na Paulo kwa ajili ya malaika katika kitabu chake cha *A Theology of the New Testament:*

> "Paulo alimaanisha sio tu malaika wazuri na wabaya, kwa shetani na mapepo; anatumia kikundi kingine cha maneno kuelezea vyeo vya roho za kimalaika. Misamiati ni kama ifuatayo:
> ‘'utawala' [*archē*], I Kor. 15:24; Efe. 1:21; Kol. 2:10
> ''Watawala' [*archai*; RSV, "falme'], Efe. 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:15; Rum. 8:38
> ''Mamlaka' [*exousia*], I Kor. 15:24; Efe. 1:21; Kol. 2:10
> ''Mamlaka' [*exousiai*; RSV, "mamlaka"], Efe. 1:21
> ''Nguvu' [*dynamis*], I Kor. 15:24; Efe. 1:21
> ''Nguvu' [*dynameis*], Rum. 8:38

''Enzi' [*thronoi*], Kol. 1:16

''U-bwana' [*kyriotē*s; RSV, "tawala"], Efe. 1:21

''watawala' [*kyriotētes*], Kol. 1:16

''Watawala wa giza wa ulimwengu,' Efe. 6:12

''majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho,' Efe. 6:12

''mamlaka ya giza,' Kol. 1:13

''kila jina litajwalo,' Efe. 1:21

''vya mbinguni, vya duniani, vya chini ya nchi,' Fil. 2:10 "(ukurasa. 401).

**MADA MAALUM:PEPO(ROHO WACHAFU)**

A. Watu wa kale waliamini kwamba viumbe vyote vina uhai. Walifikiri kwamba sifa za mwanadamu ni sawa na nguvu ya asili, wanyama, na viumbe vya asili. Maisha yalielezeka kupitia mwingiliano wa uwepo wa vitu/viumbe hivi na wanadamu.

B. Mifano hii wakati mwingine ilileta matokeo ya kuabudu miungu mingi (miungu wengi). Kwa kawaida mapepo (*genii*) ilikuwa miungu midogo au nusu miungu (mizuri au miovu) ambao ilileta matokeo kadha wa kadha katika maisha ya watu binafsi.
   1. Machufuko na migogoro huko Mesopotamia,
   2. Mpangilio na kazi huko Misri,
   3. Kanaani, tazama W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel,* Toleo la Tano, kur. 67-9

C. Agano la Kale halielezi sana au kukuza jambo la miungu wadogo, malaika, au pepo, huenda ni kwa sababu ya msistizo wake mkali unaozungumzia Imani ya Mungu mmoja (tazama Mada Maalumu : Mungu mmoja Imani ya Mungu mmoja kama vile Kut. 8:10; 9:14; 15:11; Kumb. 4:35,39; 6:4; 33:26; Zab. 35:10; 71:19; 86:8; Isa. 46:9;Yer. 10:6-7; Mik. 7:18). Haliizungumzii miungu ya uongo ya mataifa ya wapagani (*Shedim*, BDB 993, kama vile Kumb. 32:17; Zab. 106:37) na halitaji majina au kufananisha baadhi yao.
   1. *Se'im* (mazimwi au majitu yenye manyoya, BDB 972 III, KB 1341 III, kama vile Law. 17:7; 2 Nya. 11:15; Isa. 13:21; 34:14)
   2. *Lilith* (jike, pepo apotoshaye kizinifu nyakati za usiku, BDB 539, KB 528, kama vile Isa. 34:14)
   3. *Mavet* (neno la Kiebrania liliotumika kumtaja mungu mwovu wa Wakanani, Mot, BDB 560, KB560, kama vile Isa. 28:15,18; Yer. 9:21; na kwa kadri iwezekavyo Kumb. 28:22)
   4. *Resheph* ( mahali, moto, au mawe yenye kutiririsha mvua ya mawe, BDB 958, KB 958, kama vile Kumb. 32:24; Zab. 78:48; Hab. 3:5)
   5. *Dever* (uharibifu, BDB 184, cf. Zab. 91:5-6; Hab. 3:5)
   6. *Az'aze*l (jina halina uhakika, lakini huenda akawa pepo wa jangwani au jina la mahali, BDB 736, KB 736, kama vile Law. 16:8,10,26)

   (Mifano hii inachukuliwa kutoka *Encyclopedia Judaica*, juzuu l. 5, uk. 1523.).Hata hivyo, hakuna imani ya Mungu wawili au uhuru wa malaika kutoka kwa YHWH katika Agano la Kale. Ibilisi chini ya YHWH (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3), hayuko huru, ni adui anayejiongoza (kama vile A. B. Davidson, *A Theology of the Old Testament*, kr. 300-306).

D. Dini ya Kiyahudi iliendelezwa kipindi cha uhamisho wa Babeli (586-538 b.k). Kitheolojia iliathiriwa aina mbili za Kiajemi zilizochukua nafasi kwa wafuasi wa Zoroaster, mungu mkuu na mzuri aliitwa Mazda au Ormazd na mpinga uovu aitwaye Ahriman. Huyu aliruhusiwa ndani ya dini ya Kiyahudi baada ya uamisho na kuwa mfano wa aina mbili kati ya YHWH na malaika Zake na Ibilisi malaika zake au pepo.

   Theolojia ya dini ya Kiyahudi yenye kutoa mfano wa uovu inaelezwa na kunakiliwa vema katika Edersheim ya Alfred *The Life and Times of Jesus the Messiah,* juzuu. 2, kiambatisho XIII (kur. 749-863) na XVI (kur. 770-776). Dini ya Kiyahudi ilitoa mifano ya uovu katika njia tatu.
   1. Ibilisi au Malaika wa maangamizi
   2. kusudi la uovu (yetzer hara) ndani ya mwandamu
   3. Malaika wa Mauti

Edersheim anayabainisha haya kama

1. Mshitaki
2. Mjaribu
3. Mwadhibishaji (juzuu. 2, uk. 756)

Kuna tofauti zinazodhihirika kitheolojia kati ya dini ya Kiyahudi iliyokuwepo baada ya uhamisho na nanma uwaslilishaji na maelezo ya uovu inavyofanyika ndani ya Agano Jipya.

E. Agano Jipya, haswaa Injili, linadai uwepo na upinzani wa uovu wa viumbe vya kiroho kwa mwanadamu na kwa YHWH (katika dini ya Kiyahudi, Ibilisi alikuwa adui wa mwanadamu, lakini si kwa Mungu). Hawa wanayapinga mapenzi ya Mungu, amri, na ufalme.

Yesu alikabiliana na kuvifukuza hivi viumbe vya kimapepo, pia viliitwa (1) roho chafu (kama vile. Luka 4:36; 6:18) au (2) roho za uovu kama vile. Luka 7:21; 8:2), kutoka kwa wanadamu. Yesu kwa udhihilisho alitengeneza tofauti kati ya maradhi (kimwonekano na kiakili) na hali ya kimapepo. Aliithibitisha nguvu Yake na mtazamo wa ndani wa kiroho kwa kuwatambua na kuwafahamu hawa pepo wabaya. Mara nyingi walimtambua na kumwita, lakini Yesu aliukataa ushuhuda wao, alihitaji wawe kimya, na kuyafukuzia mbali. Utambuzi wa pepo hawa ni ishara ya kuvunja ufalme wa Ibilisi.

Kuna upungufu wa ajabu wa habari ndani ya barua za Kitume za Agano Jipya kuhusiana na somo hili. Utambuzi huu kamwe haukuorodhesha karama za kiroho, wala methodolojia au hatua yake iliyotolewa kwa ajili ya vizazi vijavyo vya huduma au waamini.

F. Mwovu yu dhahiri; mwovu ni mtu binafsi; mwovu yupo. Si asili yake wala kusudi lake linalofunuliwa. Biblia inatetea ukweli wake na kwa ukali inapinga ushawishi wake yule mwovu. Ndani ya ukweli hakuna hatima yenye mitazamo yenye uwili ndani yake. Mungu yu ndani ya utawala wake mwenyewe ; mwovu anaangamizwa na kuhukumiwa na ataondolewa kutoka katika uumbaji.

G. Watu wa Mungu yawapasa kumpinga mwovu (kama vile Yakobo 4:7). Hawawezi kutawaliwa na naye (kama vile 1 Yohana 5:18), bali wanaweza kujaribiwa na ushuhuda na ushawishi wake kuangamizwa (kama vile Efe. 6:10-18). Mwovu ni sehemu ya mtazamo wa ulimwengu kwa wakristo uliofunuliwa. Wakristo wa sasa hawana haki ya kueleza wazi kwa mara nyingine (kutafasiri upya maandishi ya Rudolf Baltmann); kuyaua maovu (miundo ya kijamii ya Paul Tillich), wala kujaribu kuelezea kwa ukamilifu katika namna ya kisaikolojia (Sigmund Freud). Ushawishi wake umeenea kote, lakini umeangamizwa. Waamini wanahitaji kuenenda ndani ya ushindi wa Kristo!

**NASB "dhidi ya nguzo za ulimwengu za giza"**
**NKJV "dhidi ya utawala wa giza wa kizazi hiki"**
**NRSV "dhidi ya nguvu zote za ulimwengu za giza zilizopo"**
**TEV "dhidi ya nguvu za ulimwengu wa kizazi hiki cha giza"**
**NJB "jeshi la kiroho la uovu katika mbingu"**

Hili ni neno la Kiyunani *kosmocrator* katika muundo wa wingi. Neno linatumika katika kipindi cha Kiyunani na maandiko ya walimu wa Kiyahudi kumzungumzia mtu aliyepinda madaraka ya kiulimwengu. Hii inaonekana kumzungumzia Shetani (kama vile Yohana 12:31; 14:30; 2 Kor. 4:4; Efe. 2:2) na ya kipepo (kama vile 1 Kor. 2:6,8 15:24; Efe. 3:10; 6:12; Kol. 2:15).

▣ **"dhidi ya nguvu zote za uovu"** Tungo hii ilitumika katika siku za Paulo na wasoma nyota ambao waliamini kuwa kulikuwa na malaika au miungu nyuma ya vitu vieleavyo angani (kama vile Rum. 8:39) ambayo iliathiri maisha ya binadamu (zodiaki). Yote hii ilianza na elimu ya usomaji wa nyota wa Kibabeli. Bado ipo na iko hai (usomaji nyota na bahati).

**NASB, NKJV**
**NRSV "katika maeneo ya kimbingu"**
**TEV "katika ulimwengu wa kimbingu"**
**NJB "katika mbingu"**

Kibainishi cha mahali (cha tufe) kivumishi hasi cha wingi "katika ulimwengu wa roho" inatumika tu katika Waefeso (kama vile Efe. 1:20; 2:6; 3:10; 6:12). Kutoka katika muktadha wa matumizi yake yote (haswa 3:10 na 6:12), lazima imaanishe ulimwengu wa roho ambamo waamini wanaishi sasa na baadaye, sio mbinguni na kupita na kupita.

**6:13 "vaeni silaha zote za Mungu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati usio timilifu ambao unaonesha hitaji kwa ajili ya matendo ya kimaamuzi (kama vile mstari wa 11). Hili ni neno lingine la kijeshi. Inawezekana ikawa ni maelezo ya YHWH kama mpambanaji kutoka Isaya 59:17. Silaha zinatajwa katika mpangilio ambao askari angeweza kuvalishwa (kumbuka Paulo aliandika haya kutokea gerezani alipofungwa na kusimamiwa na askari wawili wa Kirumi).Tambua silaha zote ni silaha za Mungu! Yeye anatoa, lakini Waamini lazima watambue vita na kufanyia kazi utoshelevu wa kukidhiwa mahitaji anaoutoa Mungu.

▣ **"ili muweze kumpinga"** Hii ni kauli tendwa ya wakati usiotimilifu (yenye ushahidi) tegemezi ikiwa na kauli tendaji ya wakati usiotimilifu isiyo na ukomo. Kuna vita vya kiroho kabla na baada ya kuokoka. Baadhi ya waaminio hawajui kuwa kuna vita ya kiroho inayoendelea; hawachukui silaha za Mungu na hawampingi. Neno hili ni sawa na lile la Yakobo 4:7 na 1 Petro 5:9. Wakristo wanaweza kupoteza au kuharibu amani yao, uhakika na huduma waliyokarimiwa kupitia (1) ujinga; (2) kupuuzia; na/au (3) dhambi (kama vile 1 Kor. 9:27; 15:2; Gal. 2:2; 3:4; Fil. 2:16; 1 Tim. 1:19). Hii haimanishi mbingu au kuzimu, lakini huduma za kiufanisi za ufalme!

▣ **"siku ya ouvu"** Hii ni nahau ya Agano la Kale yanayorejerea (1) siku ya majaribu; (2) kizazi chote cha uovu ambacho tunaishi; au (3) siku ya taabu (kama vile Zab 49:na kuendelea).

▣ **"mkiisha kufanya mambo yote"** Neno hili lilikuwa na kidokezo cha kuwa umefanya kila kitu kilichotakikana. Paulo anatumia neno hili zaidi ya mara 18 katika barua zake. Katika ulimwengu wa roho (1) maandalizi; (2) muendelezo; na (3) Maarifa ni muhimu!

▣ **"kusimama"** Hii ni kauli tendaji ya wakati usiotimilifu usio na kikomo "kusimama." Neno hilo hilo linatumika katika Efe. 6:11 (kitenzi jina cha kauli tendwa ya wakati uliopo) na 14 (kauli tendaji shurutishi ya wakati usio timilifu). Waamini wameamriwa na kutiwa moyo kupinga, kukabili, na kusimama dhidi ya mbinu za shetani(kama vile Efe. 4:14). Hii ilifanywa kwa namna ya

1. maarifa ya injili ya mwamini (kofia ya wokovu na upanga wa Roho, Efe. 6:17)
2. nafasi ya mwamini katika Kristo
3. kujiachia kwa Roho akaaye ndani kwa mwamini
4. utekelezaji wa kuvaa silaha iliyotolewa na Mungu kwa mwamini
5. maamuzi na matendo ya mwamini
6. maombi (kama vile Efe. 6:18)

Angalia Mada Maalum:kusimama katika Efe. 6:11.

**6:14** Tatu za kauli endelevu kati ya nne zinachukuliwa katika kifungu cha habari cha Isaya. Zote kisarufi zinahusiana na kauli tendaji shurutishi ya wakati usiotimilifu, "kusimama" in Efe. 6:13 (Huu muundo ni kama 5:18, shurutishi inayofuatiwa na kauli tano endelevu , 5:19-21).

1. **"mkisha kukaza"** kauli ya kati endelevu ya wakati usio timilifu (Efe. 6:14). Hii nukuu kutoka Isaya 11:5 ambapo ilitumika kwa Masihi.
2. **"mkisha kuvaa**" kauli ya kati endelevu ya wakati usiotimilifu (kama vile Efe. 6:14). Hii ni nukuu kutoka Isaya 59:17, ambapo inatumika kwa Mungu kama askari kwa niaba ya Israeli yenye dhambi (kama vile Efe. 59:12)
3. **"mkisha kuvaa"** kauli ya kati endelevu ya wakati usio timilifu (Efe. 6:15). Hii ni nukuu kutoka Isaya 52:7, ambapo Bwana atakuja kwa watu wake kama Mfalme akileta habari njema (kama vile Efe. 61:1)
4. **"mkishachukua"** kauli tendaji endelevu ya wakati usiotimilifu (Efe. 6:16, kama vile Efe. 6:13). Hii inarejerewa katika Isaya 59:17. Kukidhiwa kwa mahitaji ya Mungu lazima ifanyiwe kazi kila siku.

◙ **"kweli"** Hakuna kiambata katika kiyunani, kwahiyo inaweza kutafsiriwa katika namna ya Agano la Kale la "ukweli" au "uaminifu." Angalia Mada Maalumu katika Efe. 1:13.

◙ **"dirii kifuani"** Hii ni moja ya ngao zilizoorodheshwa katika Isaya 59:17, kama ilivyo kofia katika Efe. 6:17.

◙ **"ya haki"** Hii inamaanisha haki ya Kristo (kama vile 2 Kor. 5:21).Hata hivyo, kama mvutano wa kilahaja unavyohusiana na kuimarishwa Efe. 6:10, Ni vyote shutumu ya haki ya Kristo (kuhesabiwa haki na utakaso kinafasi) na kule kufanana na Kristo kunakoendelea kunakofanywa na wafuasi Wake (utakaso endelevu kunakoleta ushindi katika mashindano ya kiroho ya kila siku. Angalia Mada Maalum katika Efe. 4:24.

**6:15 "kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani "** Hii aidha ni (1) utayari (kama vile Isaya 52:7) au (2) msingi wa uhakika (kama vile fasiri za NEB). Waamini lazima wajiandae kwa mashindano ya kiroho ambayo kwa hakika yatakuja.

**6:16 "kwa nyongeza"** KJV inafasiri hii kama "kupita vyote," lakini inamaanisha nyongeza kwa kile ambacho kimekwisha tajwa katika ngao ya kijeshi kwa ajili ya vita.

◙ **"ngao"** Neno hili linahusiana na neno la Kiyunani kwa"mlango." Inaamaanisha kwa sehemu kubwa 4' x 2' ngao ya mwili mzima. Ilikuwa imetengenezwa kwa mbao ikiwa imefunikwa kwa ngozi na imezungushiwa chuma. Ilikuwa inachovywa katika maji kabla ya vita ili kuzima moto wa mishale ilichovywa. It was a symbol of full protection.

◙ **"mishale ya moto"** Hii inamaanisha mishale iliyochovywa katika mafuta na kuwashwa. Hizi zilikuwa ni sitiari za mashambulizi ya kiroho.

◙ **"yule muovu"**Kuna utata ambao aidha unaweza inamanishwa uovu kwa ujumla (hasi) au shetani kwa uhalisia (jinsi ya kiume). Utata huohuo unaweza ukawa unaonekana katika Mathayo 5:37; 6:13; 13:38; Yohana 17:15; 2 The. 3:3; 1 Yohana 2:13-14. Muundo wa neno Kiyunani ni ule ule (hivyo, jinsi inaweza ikaeleweka tu kupitia muktadha). katika Mathayo 13:19; 1 Yohana 5:18-19 ni wazi kuwa anamaanishwa shetani (atangalia mada maalum Efe. 2:2).

**6:17 "vaeni kofia za wokovu"** Hii kauli ya kati isiyo timilifu (yenye ushahidi) shurutishi. Ni kiashiria cha maarifa ya waamini ya injili na tumaini lao katika Kristo (kama vile 1 The. 5:8).

◙ **"upanga wa Roho, ambao ni neno la Mungu**" Paulo anafafanua wazi silaha za kuchukiza (yaani, ujuzi wa Biblia na sala, Efe. 6:18). Hii ilikuwa ni mfano wa mfano wa Agano la Kale kwa Mungu akizungumza na watu wake (kama vile Isaya 49: 2; Hosea 6: 5). Ufunuo wa Mungu (Neno lililo hai, Yesu Kristo, na neno lililoandikwa, Biblia) linaelezwa kwa maneno haya sawa katika Ebr. 4:12. Ingawa neno tofauti la Kiyunani kwa "neno" (rhēma dhidi ya logos) linatumika kwa Waebrania, neno kwa ajili ya "upanga" ni sawa (lugha ndogo ndogo kwa umbo la silaha ya Kirumi).
Ni hatari kuchora tofauti kali kati ya suala sambamba katika Koine Kigiriki (ilikuwa ni lugha ya biashara na tofauti za Kigiriki cha Kiyunani zilikuwa zimeharibika) kama "rhēma" na "logos." Hii inaweza kutaja matumizi ya Maandiko wakati wa majaribu, kama Yesu alivyofanya katika Mathayo 4:1 na kuendelea. Ujuzi wa Waumini wa Injili utawalinda katika vita vyao vya kiroho vya kila siku. Ndiyo sababu kumbukumbu za maandiko na kujifunza Biblia binafsi ni muhimu sana (kama vile Zaburi 19: 7-11, 119: 105; Mithali 6:23). Hii ndiyo silaha pekee ya kukataa iliyoorodheshwa kati ya silaha (ingawa nadhani sala katika Waefeso 6:18 ni nyingine). Ni kwa ajili ya ulinzi. Kama ilivyo katika Efe. 6: 18-20 inaweza kutumika kwa ajili ya Ufalme mapema!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:18-20**
**[18] kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote; [19] pia na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kwa kufumbua kinywa changu, ili niihubiri kwa ujasiri ile siri ya Injili; [20] ambayo kwa ajili yake mimi ni mjumbe katika minyororo; hata nipate ujasiri katika huyo kunena jinsi inipasavyo kunena.**

**6:18** "**kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati kati**" Angalia idadi ya mara neno linalojumuisha "yote" linatumika katika Efe. 6:18. Sala ni silaha nyingine yenye nguvu katika vita vya kiroho ambazo ni maisha ya kila siku ya Kikristo katika zama hii ulioanguka. Paulo aliomba sala kwa Efe. 6:19 (kama vile Kol 4: 3-4; 1 Wathesalonike 5:17). Hakuomba maswala ya kibinafsi lakini kwa uwazi na ujasiri katika kutangaza injili (kama vile Wakolosai 4: 3-4). Inavutia kutambua kwamba Paulo hazungumzii vita vya kiroho katika Wakolosai lakini anasisitiza haja ya maombi (kama vile Kol. 4:2).

◙ **"katika Roho"** Neno "roho" halina neno (ananthrous). Hii inaweza kueleweka kwa njia tofauti. Inaweza kutaja

1. Roho anaombea waumini (kama vile Rum. 8: 26-27)
2. Wakristo wanaomba kwa nguvu za kiroho (kama vile Yuda 1:20)
3. sambamba na Yohana 4:23 "kwa roho na kweli"
4. "roho" kama tofauti na "akili" (kama vile 1 Kor. 14: 14-15) Sala ya ufanisi, haiwezekani haiwezekani bila ushiriki wa Roho!Angalia mambo ya sala iliyoongozwa na roho:

1. wakati wote
2. katika Roho
3. kuwa macho pamoja na uvumilivu
4. Waombee watakatifu wote

◙ **"kwa watakatifu wote"** Angalia Mada Maalum: Watakatifu katika Kol. 1:2.

**6:19** "***Uombee* kwa niaba yangu**" Paulo aliomba sala, sio mwenyewe, bali kwa uwezo wa kuhubiri injili wazi kama alivyozungumza wakati wa majaribio mbele ya mamlaka ya Kirumi (kama vile Kol. 4: 3; 5:25, 2 The. 3: 1):

1. "kusema kwamba nipewe" (Efe. 6:19)
2. "kujulisha kwa ujasiri siri ya Injili" (Efe. 6:19 "uhuru wa kuzungumza," kama vile Efe. 3:12, Waebrania 4:16, 10: 19,35).
3. "Naweza kusema kwa ujasiri, kama nivyopaswa kusema" (Efe. 6:20; Kol. 4: 4).

**MADA MAALUM:MAOMBI YENYE UFANISI**

A. Kuhusiana na uhusiano wa mtu binafsi na nafsi za Mungu mmoja
   1. Inahusika kwenye mapenzi ya Baba
      a. Mathayo 6:10
      b. 1 Yohana 3:22
      c. 1 Yohana 5:14-15
   2. Kukaa ndani ya Yesu Yohana 15:7
   3. Kuomba kwa jina la Yesu
      a. Yohana 14:13,14
      b. Yohana 15:16
      c. Yohana 16:23-24
   4. Kuomba katika roho
      a. Waefeso 6:18
      b. Yuda 1:20
B. Inahusika na nia ya mtu binafsi
   1. Kutokuyumba yumba
      a. Yohana 21:22

b. Yakobo 1:6-7
2. Kuomba vibaya Yakobo 4:3
3. Kuomba kwa tama Yakobo 4:2-3

C. Inahusika na uchaguzi wa mtu binafsi
1. Ustahimilivu
a. Luka 18:1-8
b. Wakolosai 4:2
c. Yakobo
2. Ugomvi nyumbani 1 Petro 3:7
3. Dhambi
a. Zaburi 66:18
b. Isaya 59:1-2
c. Isaya 64:7

Maombi yote hujibiwa, lakini si maombi yote yanazaa matunda. Maombi ni uhusiano wa pande mbili. Jambo baya kuliko yote ambalo Mungu angalifanya ni kujibu maombi ya waaminio ambayo si sahihi.

◙ **"kwa ujasiri"** Tazama Mada Maalum: Ujasiri (*Parrhēsia)* katika Kol. 2:15.

◙**"Siri ya injili"** Paulo anatumia neno hili kwa njia mbalimbali tofauti kuelezea mpango wa ukombozi wa Mungu. Hapa inahusu Wayahudi waamini na Wayahudi kuwa mwili mmoja katika Kristo. Dhana hii inaelezewa wazi katika Efe. 2: 11-3: 13. Neno linaonekana katika Efe. 1: 9; 3: 3, 4, 9; 5:32. Angalia Mada Maalum Katika Efe. 3:3.

**6:20** "**mimi ni mjumbe katika minyororo**" Paulo alielewa utume wake kwa Wayahudi kama uongozi (1 Kor. 4: 1, 9:17, Tito 1: 7) na mjumbe (kama vile 2 Kor. 5: 20). Alikuwa jela akihubiri injili kwa mamlaka ya Kirumi huko Roma, kama alivyokuwa na mamlaka ya Yudea (kama vile Mdo 9:15)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:21-22**
**21 Basi ninyi nanyi mpate kuzijua habari zangu, ni hali gani, Tikiko, ndugu mpendwa, mhudumu mwaminifu katika Bwana, atawajulisheni mambo yote; 22 ambaye nampeleka kwenu kwa kusudi lilo hilo mpate kuzijua habari zetu, naye awafariji mioyo yenu.**

**6:21 "Tikiko, ndugu mpendwa, mhudumu mwaminifu katika Bwana"** Yeye ametajwa katika Mdo. 20: 4; Kol. 4: 7; Tito. 3:12; 2 Tim. 4:12. Alikuwa mhusika wa barua. Pia, labda alibeba barua za Wakolosai na Filemoni kwa Asia Ndogo na alikuwa akiongozana na Onesimo. Pia labda anaweza kubeba barua ya Waefeso kwa makanisa yote ya Asia Ndogo. Pia anaweza kufanya kazi kama mwandishi wa Paulo, kama Tertio wa Rum. 16:22.

**6:21-22** Aya hizi ni sawa kwa Kiyunani kama Kol. 4: 7-8, isipokuwa Wakolosai anaongeza "mtumishi mwenzako," ambayo inaonyesha kwamba Paulo aliandika vitabu viwili karibu na wakati huo huo.

**6:22** Paulo alitaka makanisa kujua hali yake ili waweze kumwombea wala wasiwe na wasiwasi juu yake. Alihisi kuwa alikuwa katika mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha na huduma yake (kama vile Mdo 9:15).

◙**"Mioyo"** Tazama Mada Maalum katika Kol. 2: 2.

◙ Mmoja anashangaa kama Paulo mwenyewe hakuwa ameandika mstari huu wa 6: 23-24

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAEFESO 6:23-24**
**23 Amani na iwe kwa ndugu, na pendo, pamoja na imani, zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Bwana Yesu Kristo.**
**24 Neema na iwe pamoja na wote wampendao Bwana wetu Yesu Kristo katika hali ya kutokuharibika.**

**6:23-24** Hizi mandhari sawa zilifungua barua! Paulo mara nyingi aliandika mawazo ya kufunga mwenyewe ili kuthibitisha barua zake.

**6:24**
**NASB "upendo usio haribika"**
**NKJV "katika ukweli"**
**NRSV "upendo usiokufa"**
**TEV "ukiwa na upendo usiokufa"**
**NJB "uzima wa milele"**

Neno hili kwa kawaida lina maana "isiyoharibika" (kama vile 1 Kor. 9:25; 15:52, 1 Tim. 1:17). Ilikuwa na kidokezo wa kitu kisichobadilika na cha milele. Hili lilikuwa faraja kutokana na machafuko na migogoro iliyosababishwa na walimu wa uongo na vita vya kiroho.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je kuna msukumo binafsi wa uovu katika ulimwengu wetu?
2. Nini wajibu wetu katika mashindano ya kiroho?
3. Kwanini Paulo anatumia vita katika kuelezea maisha ya Mkristo?
4. Je Paulo anajiombea nini kwa ajili yake yeye mwenyewe?

# UTANGULIZI WA FILEMONI

## MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Kitabu hiki ni mfano wa barua binafsi, ambazo zilikuwa za kawaida kabisa katika karne ya kwanza ya ulimwengu kati ya kipindi cha Wagiriki na Warumi. Yawezekana ilitosha katika karatasi moja ya mafunjo (kama vile 3 Yohana). Haijajulikana nani hasa kimsingi ilikusudiwa kwake.
   1. Filemoni
   2. Apia na Arkipo (kama vile Kol. 4:17)
   3. Au baadhi ya namna, nyumba yote ya kanisa la nyumbani

B. Barua inatoa mwanya kuelekea
   1. Mbinu za kichungaji za mtume Paulo
   2. Makanisa ya nyumbani ya karne ya kwanza (Rum. 16:5; 1 Kor. 10:19; Kol. 4:15)

C. Ukristo ulikuwa tayari unabadilisha mtindo wa maisha ya ulimwengu wa Mediteranian. Vikwazo vya kijamii kwa injili vilikuwa vikianguka(1 Kor. 12:13; Gal. 3:28; Kol. 3:11)

## MWANDISHI

A. Asili binafsi ya barua inashawishi wasomaji wengi (isipokuwa mmoja, F.C Baur) kwamba mwandishi alikuwa Paulo, Mtume.

B. Filemoni na Wakolosai kwa ukaribu wanafanana
   1. Asili yao ni moja
   2. Watu walewale wanaotoa salamu
   3. Hitimisho linalofanana
   4. Tikiko aliwasilisha barua kwa Wakolosai na kusafiri pamoja na Onesmo (kama vile Kol. 4:7, 9). Ikiwa Filemeoni ni mtu wa Paulo, na vivyo hivyo Wakolosai (ambacho kimekuwa kikitiliwa wasiwasi na wataalamu kadhaa wa kisasa).

C. Imeorodheshwa kati ya barua za Paulo na wote mpiga porojo Marcion (aliyekuja Rumi katika miaka ya 140 B.K) na orodha ya vitabu vya kikanoni, kisehemu cha Murato (iliyoandikwa katika Rumi ya miaka aya 180-200 B.K).

## TAREHE

A. Tarehe za barua hii iliunganishwa na moja ya vifungo vya Paulo (Efeso, Filipi, Kaisaria, au Rumi). Kifungo cha kirumi kinatosheleza kwa uzuri sana kweli za Matendo ya Mitume.

B. Mara Rumi inapodhaniwa kuwa sehemu ya vifungo, swali linainuka- wakati gani? Paulo alikuwa Jela mwanzoni mwa miaka ya 60 na hii imewekwa kumbukumbu katika Matendo ya Mitume. Hata hivyo, aliachiwa na kuandika barua za kichungaji (1 & 2 Timotheo na Tito) na baadaye alikamatwa tena na kuuawa Juni 9, mwaka wa 68 B. K. (kujiua kwa Nero). Dhanio bora kabisa la kisomi kwa uandishi wa Kolosai, Waefeso na Filemoni ni kifungo cha kwanza cha Paulo, miaka ya kwanza ya 60. Wafilipi yawezekana kiliandikwa kuelekea miaka ya kati ya 60.

C. Tikiko sambamba na Onesmo, yawezekana alichukua barua za Wakolosai, Waefeso, na Filemoni kwa Asia ndogo. Baadaye (yawezekana miaka kadhaa ya baadaye), Epafrodito,alipona kutoka katika maradhi yake ya mwili, akachukua barua ya Wafilipi kupeleka katika kanis a lake la nyumbani.

D. Yawezekana mfuatano wa maandiko ya Paulo yanayofuata F.F. Bruce na Murray Harris( kukiwa na marekebisho kidogo)

| Kitabu | Tarehe | Mahali kilipoandikwa | Uhusiano na Matendo ya Mitume |
|---|---|---|---|
| 1 Wagalatia | 48 | Antiokia | Mdo 14:28; 15:2 |
| 2 1 Wathesalonike | 50 | Korintho | Mdo 18:5 |
| 3 2 Wathesalonike | 50 | Korintho | |
| 4 1 Wakorintho | 55 | Efeso | Mdo 19:20 |
| 5 2 Wakorintho | 56 | Makedonia | Mdo 20:2 |
| 6 Warumi | 57 | Korintho | Mdo 20:3 |
| 7-10 Barua za gerezani | | | |
| Wakolosai | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Filemoni | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Waefeso | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Wafilipi | mwishoni mwa 62-63 | Rumi | Mdo 28:30-31 |
| 11-13 Safari ya 4 ya Umishionari | | Efeso(?) | |
| 1 Timotheo | 63(au baadaye, | Makedonia | |
| Tito | 63 lakini kabla | | |
| 2 Timotheo | 64 B.K 68) | Rumi | |

## MAZINGIRA YA BARUA (watu waliotajwa katika Filemoni)

A. Filemoni alikuwa Bwana wa watumwa wa Onesmo. Aliishi Kolosai. Yawezekana alikuwa muongokaji wa Paulo, yawezekana wakati Paulo alikuwa akihudumu katika Efeso.

B. Onesmo alikuwa mtumwa wa Filemoni aliyekimbia. Alikuwa pia muongokaji wa Paulo, wakati akiwa gerezani katika Rumi (miaka ya 61-63 B.K). haijulikani kwa namna gani Paulo na Onesmo walipokutana. Huenda
   1. Wote walikuwa wafungwa
   2. Onesmo alitumwa katika safari fupi kwa Paulo
   3. Onesmo alimtafuta Paulo kwa ajili ya ushauri baada ya kubadilisha mawazo yake kuhusu kuondoka.

C. Epafra alikuwa mwamini kutoka Asia ndogo na mwanzilishi wa makanisa ya bonde la mto Lycus (Kolosai, Laodikia na Hierapoli). Alileta neno kwa Paulo gerezani kuhusu porojo za uvumi katika Kolosai na kuhusu uaminifu wa Filemoni.

D. Tikiko alikuwa mpeleka barua tatu katika eneo hili: Kolosai, Waefeso, na Filemoni (kama vile Kol. 4:7-9; Efe. 6:21-22). Onesmo pia alirudi pamoja nae kumuona bwana wake (Flp 1:11). Filemoni ni moja ya barua za binafsi zilizotunzwa katika Agano JIpya (kama vile 3 Yohana).

   Na karibia miaka 50 baadaye (110 B.K) Ignatius,katika njia yake Rumi kuwa mashujaa, aliandika barua ("Kwenda kwa Waefeso" 1:3) kwa Askofu wa Efeso aliyeitwa Onesmo! Inawezekana ilikuwa mtumwa huyu aliyeongoka!

## KUSUDI LA BARUA

A. Inaoneshwa namna Paulo alivyotumia mamlaka yake ya kitume na kutiwa moyo kichungaji.

B. Inaoneshwa namna Ukristo umewafanya ndugu wa kiume na wa kike kutokana na watumwa na wamiliki wa watumwa. Utajiri na umaskini! Huu ukweli ungeweza kubadili dola ya kirumi.

C. Inaonesha imani ya Paulo kwamba angetolewa kutoka katika vifungo vya Warumi na kurudi Asia ndogo.

**MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (kutoka "A Guide To Good Reading" Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu chote cha Biblia kwa mara moja. Eleza dhamira kuu ya kitabu kizima kwa maneno yako mwenyewe (mzunguko wa usomaji #1)

3. Dhamira kuu ya kitabu kizima
4. Aina ya fasihi (aina ya fasihi aliyotumia katika kuwasilisha ujumbe wake).

**MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (kutoka "A Guide To Good Reading" ("Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu kizima cha Biblia kwa mara ya pili kwa mara moja. Weka kwa muhtasari masomo makuu (mzunguko wa Usomaji #2) na elezea somo kwa sentensi moja.

6. Somo la kipengele cha kwanza cha fasihi
7. Somo la kipengele ya pili cha fasihi
8. Somo la kipengele cha tatu cha fasihi
9. Somo la kipengele cha nne cha fasihi
10. Na nyinginezo.

# FILEMONI

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Salamu Flm 1:1-3 | Salamu | Salamu | Salamu | Anwani |
| | mst. 1a | mst. 1a | mst. 1a | mst. 1-3 |
| | mst. 1b | mst. 1b – 2 | mst. 1b – 2 | mst. 1-3 |
| | mst. 2 | | | |
| mst. 3 | mst. 3 | mst. 3 | mst. 3 | |
| Upendo wa Filemoni | Upendo wa | Shukrani | Upendo wa | Shukrani na |
| Na Imani | Filemoni na imani | mst. 4-7 | Filemoni na imani | maombi |
| mst. 4-7 | mst. 4-7 | | mst. 4-7 | mst. 4-7 |
| Paulo anasihi kwa | kusihi kwa ajili ya | Kusihi kwa Paulo | Ombi kwa ajili ya | ombi kuhusu |
| Ajili ya Onesmo | Onesmo | juu ya Onesmo | Onesmo | Onesmo |
| | | | | Flm. 1:8-21 |
| Mst.8-16 | mst. 8-16 | mst. 8-16 | mst. 8-11 | |
| | | | mst. 12-14 | |
| | Unyenyekevu wa | | mst. 15-16 | |
| | Onesmo | | | |
| | unahamasishwa | | | |
| | mst. 17-22 | mst. 17-21 | mst. 17-20 | |
| | | | mst. 21-22 | |
| | | hitimisho la matumaini | | maombi binafsi |
| | | na salamu | | kutaka heri |
| mst. 21-22 | | mst. 22 | | mst. 22 |
| Salamu ya Mwisho | kwaheri | | salamu za mwisho | |
| Mst. 23-25 | mst. 23-25 | mst. 23-24 | mst.23-24 | mst. 23-23 |
| | | mst. 25 | mst. 25 | mst. 25 |

*Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani (Bief Definitions of Greek), Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi (Textual Criticism), Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko (Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "**A Guide to Good Bible Reading" ("Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

## *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:1a**
**Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu, na Timotheo aliye ndugu yetu,**

**Filemoni 1:1"Paulo"** Jina la Kiyunani *Paulos* lilimaanisha "mdogo." Nadharia kadhaa zimekua kutokana na asili ya jina hili la Kiyahudi.

3. Jina linalojulikana likifunua umbo lake la nje, karne ya pili iliweka desturi kuwa Paulo alikuwa mfupi, mnene, mwenye kipara, mwenye matege, mwenye nyusi nyingi kama kichaka, na mwenye macho yanayotokeza njema na yawezekana ndio asili ya jina lake, akitoa katika vitabu visivyo vya kikanoni kutoka katika Thesalonika iliyoitwa *Paul and Thekla*
4. Tathmini yake binafsi ya Paulo ambapo alijiita mwenyewe "mdogo kati ya watakatifu" kwasababu aliliudhi kanisa kama ilivyo katika Matendo ya Mitume 9:1-2 (rejea 1 Wakorintho 15:9; Waefeso 3:8; 1 Tim 1:15)
5. Wengi wa Wayahudi waishio nje ya nchi yao (Wayahudi waishio nje ya Palestina) ilitolewa majina mawili wakati wa kuzaliwa; moja la Kiebrania (Sauli) na moja la Myunani wa asili (Paulo).

◙**"mtumwa"** Agano Jipya kiuhalisia linaelezea kwamba Paulo alikuwa gerezani mara tatu: (1) katika Kaisaria; (2) katika Filipi; (3) katika Rumi (kuna maelezo yanayowezekana kufungwa katika Efeso, kama vile 1 Kor. 15:32; 2 Kor.1:8). Mwandishi huyu anadhania kufungwa katika Rumi katika miaka ya mwanzo ya 60.

Kwasababu ya asili ya upendo wa kichungaji ya barua ya ufupi, wafasiri wengi wamedhani kwamba Paulo alichagua cheo hiki badala ya ukiri wa utume wake katika ufunguzi.

◙**"Kristo Yesu"** aina za cheo cha Yesu alivyotumia barua hii fupi inashangaza. Angalia; Kristo Yesu ; Flp. 1:1; Bwana Yesu, Kristo, Flp 1:3; Bwana Yesu, Flp 1:5; Kristo, Flp 1:8; Kristo Yesu, Flp 1:9; Bwana, na Kristo Flp 1:20; Kristo Yesu, Flp 1:23; na Bwana Yesu Kristo, Flp 1:25

"Kristo" ni Kiyunani ambacho sawasawa na neno la Kiebrania "Masihi," linalomaanisha "mpakwa mafuta" (angalia Mada Maalum katika Kol 1:1) ilimaanisha "aliyeitwa na kuwezeshwa na Mungu kwa ajili ya kazi fulani." Katika Agano la Kale makundi matatu ya viongozi walikuwa wamepakwa mafuta: makuhani, wafalme na manabii. Yesu alitimiza ofizi zote hizi za kupakwa mafuta (kama vile Waebrania 1:2-3).

"Yesu" ilimaanisha "YHWH anaokoa" au "wokovu una YHWH" (kama vile Mathayo 1:21). Ilikuwa ni jina la Agano la Kale "Joshua." "Yesu" linatokana na neno la Kiebrania kwa ajili ya wokovu, *"hosea,"* lenye viambishi tamati kwenye jina la agano la Mungu, "YHWH" (angalia Mada Maalum katika Kol 1:3)

◙**"Timotheo"** Jina lake lilimaanisha "aliyeheshimiwa na Mungu." Aliongoka kupitia kushuhudiwa na Paulo katika safari yao ya kwanza ya kimishionari kuelekea Derbe/Listra (kama vile Mdo. 26:1). Paulo alimualika yeye kujiunga na timu ya umishionari katika safari yake ya pili yawezekana kuchukua nafasi ya Yohana Marko (Mdo. 15:36:41). Alikuwa na mama Myahudi na baba Myunani (Mdo 16:3). Alikuwa mwakilishi mwaminifu wa Paulo, mwanafunzi na mkabilianaji wa matatizo (Mdo 16:1-17:14; 18:5-19:22; 20:4; Rum. 16:21; 1 Kor. 4:17; 16:10; 2 Kor. 1:1, 19; Fil.1:2; 2:19; Gal. 1:1; Flm. 1:4; na vitabu viwili 1 Timotheo and 2 Timotheo).

Anatajwa na Paulo katika barua kadhaa (1 Kor. 4:12; 16:10; 2 Kor. 1:1; Fil. 1:1; Kol. 1:1; 1The. 1:1; 2 The. 1:1; 1 Tim. 1:2; 2 Tim. 1:2). Hii haimaanishi uandishi mwenza, lakini UWEPO WA Timotheo na salamu. Timotheo anaweza kuwa alifanya kazi kama katibu wa Paulo, au mwandishi, kama walivyofanya wakina Sila, Tertio, Tikiko.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:1b-3**
**1b kwa Filemoni mpendwa wetu, mtenda kazi pamoja nasi, 2 na kwa Afia, ndugu yetu, na kwa Arkipo askari mwenzetu, na kwa kanisa lililo katika nyumba yako. 3 Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu, Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo.**

◙**"Filemoni"** mshirika mwaminifu wa kanisa la Kolosai. Mtu huyu anatajwa tu katika hii barua. Kwa dhahiri kanisa la nyumbani katika Kolosai likuwa likikutana katika nyumba yake. Maoni ya Paulo kumuhusu yeye yanaashiria kuwa kwa binafsi alimfahamu mtu huyu. Epafra na sio Paulo alianza kanisa katika Kolosai (kama vile Kol 1:6-7), hivyo, lazima Paulo alikuwa alishakutana nae mapema, yawezekana katika Efeso (Filemoni 1:10, 19). Hata hivyo inawezekana kwa kiasi kwamba Paulo alimfahamu kwa binafsi (kama vile Filemoni 1:5) na kwamba Epafra alimfahamisha yeye kuhusu huduma ya mtu huyu.

**Filemoni 1:2 "Afia"** Hii inawezekana akawa mke wa Filemoni kwasababu jina lake linakuwa la pili.

◙**"Arkipo"** wengine wanafikiri kwamba huyu alikuwa mtoto wa kiume wa Filemoni, lakini inawezekana alikuwa Mchungaji wa kanisa lililokuwa likikutana katika nyumba ya Filemoni (kama vile Kol 4:17) au mtu mwingine asiyejulikana kwetu. E.J. Goodspeed na J. Knox anafikiria kwamba Arkipo alikuwa mmiliki wa Onesmo na Filemoni alikuwa mchungaji wa nyumbani aliyeorodheshwa kusaidia kutia moyo Arkipo kuwa na huruma kwa mtumwa aliyetoroka.

◙**"askari mwenzetu"** Paulo aliyaona maisha ya Kikristo kama mapambano ya kijeshi (kama vile Waefeso 6:10-18). Anatumia hali hii ya kitabia mara kadhaa (kama vile Filemoni 2:25; 2 tim 3:2).

◙**"kanisa"** *Ekklesia* ilitoka katika maneno mawili ya Kiyunani, "nje ya" na "kuita." Inatumika katika Kiyunani cha Koine kufunua aina yoyote ya mkusanyiko, kama mkutano wa mjini (kama vile Mdo 19:32). Kanisa lilichagua neno hili kwasababu lilitumika katika tafsiri ya Agano la Kale (tafsiri ya Kiyunani ya vitabu vitano vya Musa iiyoandikwa mapema kama 250 K.K kutoka katika Mkataba ya Alexandria, Misri). Neno hili lilitafsiri neno la kiebrania *qahal* lililokuwa likitumika katika tungo "kusanyiko la Israel" (kama vile Hesabu 20:4). Waandishi wa Agano Jipya lilieleza kwamba walikuwa walioitwa kwa mpango wa Mungu" ambao wangekuwa watu wa Mungu katika siku zao. Hawakuona msingi wa kuvunja kati ya watu wa Mungu wa Agano la Kale na wao, watu wa Mungu wa Agano jipya.

Waamini lazima waeleze kwamba kanisa la Yesu Kristo, sio walimu wa Kiyahudi wa kisasa ndio urithi wao wa kweli wa maandiko ya Agano la Kale. Angalia Mada Maalumu katika Kol 1:18.

◙**"kwa kanisa likutanalo katika nyumba yako"** Hakukuwa na majengo ya makanisa hadi karne ya tatu (kama vile Mdo 2:40; 5:42; 20:20; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15). Haya makanisa ya nyumbani yalifuata utaratibu wa Kiyahudi wa masinagogi ya nyumbani (kusoma maandiko, maombi, nyimbo, n.k). maandiko ya Kiyunani yana utata wa kimaana kama kwa namna watu walivyotajwa katika Filemoni 1:1-2 walimiliki wa nyumba ambayo kanisa lilikutanika.

**Filemoni 1:3 "Baba"** Neno hili halitumiki katika maana ya kizazi cha tendo la kimwili la ndoa au mfululizo wa mfuatano, lakini uhusiano wa karibu wa mahusiano ya kifamilia. Mungu alichagua maneno ya familia kujifunua mwenyewe kwa wanadamu walioanguka (kama vile Hosea 2-3 kama mwenye upendo, mpenzi mwaminifu, Hosea 11 kama baba na mama). Angalia Mada Maalum: Baba katika Kol 1:2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:4-7**
**4 Namshukuru Mungu wangu sikuzote, nikikukumbuka katika maombi yangu; 5 nikisikia habari za upendo wako na imani uliyo nayo kwa Bwana Yesu na kwa watakatifu wote; 6 ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu, katika Kristo. 7 Maana nalikuwa na furaha nyingi na faraja kwa sababu ya upendo wako, kwa kuwa mioyo ya watakatifu imeburudishwa nawe, ndugu yangu.**

**Filemoni 1:4 "Namshukuru Mungu wangu"** ilikuwa ni desturi wakati wa kipindi cha ulimwengu wa kati ya Wayunani na Warumi kuanza barua kwa namna ya aina ya umadhubuti au kiwango: (1)kutoka kwa nani; (2) kwenda kwa nani; na (3) Baraka au shukrani, Paulo alifuata utaratibu huu (kushukuru kwa wasomaji, kama vile Rum. 1:8; 1 Kor. 1:4; Fil. 1:3; Kol. 1:3; 1 The. 1:2; 2 The. 1:3; Baraka za Mungu, 2 Kor. 1:3; Efe. 1:3; Shukrani kwa Mungu, kama vile 1 Tim. 1:12; 2 Tim. 1:3). Angalia Mada maalum: Sifa, Maombi, na Shukrani za Paulo kwa Mungu katika Waefeso 3:20.

◙**" nikikukumbuka katika maombi yangu"** angalia Mada Maalum: Maombi ya kusihi katika Kol 4:3.

**Filemoni 1:5"nikisikia habari za upendo wako"** Paulo hakuanza kanisa katika Kolosai. Kwa dhahiri Epafra alikuwa amemletea habari za uvumi unaoenea katika Kolosai (kama vile Kolosai 1:4) na huduma ya Filemoni kwa Watakatifu (kama vile Filemoni 1:7)

◙**"imani"** (kama vile Kol 1:4).Neno hili la Kiyunani (*pistis*) inatafsiriwa katika kiingereza kwa namna tatu: "imani," "amini," na "sadiki". Neno hili la Kiyunani lilikuwa na viashiria vya kipekee vitatu.

4. Historia yake ya nyuma ya Agano la Kale ilimaanisha "uaminifu" au "inayoaminika" kwahiyo, ilitumika na waamini kuishi maisha ya utauwa.
5. Ilitumika na waamini kukubali au kupokea karama za bure za Mungu za msamaha ndani ya Kristo.
6. Ilitumika katika namna ya jumla ya mafundisho ya Mkristo au kweli kumuhusu Yesu (yaani "imani," kama vile Mdo 6:7 na Yuda 1:3, 20).

Katika baadhi ya vifungu vya habari ni ngumu kubaini alimaanisha nini. Angalia Mada Maalumu: Imani, Amini, Sadiki katika Wakolosai 1:2. Na Imani ya Agano la Kale katika Efeso 2:8.

◙**"na kwa watakatifu wote"** Hii kiuhalisi inamaanisha "wale walio watakatifu," wale waliowekwa kando kwa ajili ya huduma ya Mungu. Hii sio rejea kwa maisha yasiyo na dhambi lakini mahakama ya waaminio (kisheria) nafasi katika Kristo. Mara nyingi ina wingi isipokuwa katika Wafilipi 4:21, lakini hata huko imetumika kwa namna ya muktadha jumuishi. Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia. Neno hili linaaksi matumizi ya Agano la Kale kwa kujumuisha Israeli kama taifa takatifu (kama vile Kutoka 13:5; 19:5-6; Kumbu kumbu la Torati 7:6; 1 Petro 2:9; na Ufunuo 1:6).

Ingawa neno “watakatifu” linafanana na msimamo walio nao waamini katika Kristo, si jambo la tukio kwamba mzizi wa neno ni “takatifu.” Waaminio wanaitwa si tu katika wokovu lakini kwenye utakaso unaoendelea (kama vile Gal. 2:15-18, 19-20). Waamini wanaamriwa kabla kuwa “watakatifu”(kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:28-29; Gal. 4:19; Efe. 1:4), na sio mbinguni; katika huduma, sio upendeleo. Angalia Mada Maalum:Watakatifu katika Kol 1:2.

**Filemoni 1:6**
**NASB** **“kwamba ushirika wa imani yenu”**
**NKJV, NRSV** **“kwamba kushirikishana kwa imani yenu”**
**TEV** **“kwamba ushirika pamoja nanyi kama waamino”**
**NJB** **“kwamba ushirika wenu katika imani”**

Mstari huu umekuwa ukifasiriwa katika namna mbalimbali.
1. Ushirika wa waaminio wao kwa wao (kama vile 2 Kor. 8:4; Filemoni 2:1-5)
2. Kushirikishana injili na wasio amini (kama vile Filemoni 1:5
3. Kushirikishana mambo mazuri na wengine

**MADA MAALUM: *KOINŌNIA***
Neno "ushirika" (*koinōnia*) unamaanisha
1. Ushirika wa karibu na mtu
    a. na Mwana (kama vile 1 Kor 1:9; 1 Yohana 1:6)
    b. na Roho (kama vile. 2 Kor. 13:14; Flp. 2:1)
    c. na Baba na Mwana (kama vile. 1 Yohana 1:3)
    d. na ndugu wa agano wa kiume/kike (kama vile. Matendo 2:42; 2 Kor. 8:23; Gal. 2:9; Philemon aya. 17; 1 Yohana 1:3,7)
    e. usio na uovu (kama vile. 2 Kor. 6:14)
2. ushirika wa karibu na vitu ama makundi
    a. na injili (kama vile Flp. 1:5; Philemon aya. 6)
    b. na damu ya Kristo (kama vile 1 Kor. 10:16)
    c. usio na giza (kama vile 2 Kor. 6:14)
    d. na mateso (kama vile. 2 Kor. 1:7; Flp. 3:10; 4:14; 1 Pet. 4:13)
3. Zawadi ama changizo zilizotolewa kwa mtindo wa ukarimu (kama vile Rum. 12:13; 15:26; 2 Kor. 8:4; 9:13; Flp. 4:15; Ebr. 13:16)
4. Kipawa cha Mungu cha neema, kupitia Kristo kinachorejesha ushirika wa mwanadamu na yeye na ndugu zake wa kiume na kike

Hii inatangaza uhusiano wa ulalo (mwanadamu kwa mwanadamu) ambao unaletwa kwa uhusiano wa kweli (mwanadamu na muumbaji). Pia unasisitiza hitaji na furaha ya jumuiya ya Kikristo (yaani, Ebr. 10:25).

**NASB** **“kupitia maarifa ya kila kitu kizuri/chema”**
**NKJV** **“kwa kutambua kwa shukrani kila kitu kizuri”**
**NRSV** **“unapoelewa mazuri/mema yote ambayo tunaweza kufanya”**
**TEV** **“utaleta uelewa wa ndani wa kila Baraka”**
**NJB** **“unaweza kuja kwa kuelezea katika maarifa kamili ya wema/uzuri wote**

Kuna baadhi ya maswali yanayohusishwa katika kufasiri tungo hii:
1. Maarifa haya yanakuwa yanamaanisha nani – Filemoni, kanisa katika nyumba yake, Onesmo au Paulo
2. Ni kwa kitu gani maarifa haya (*epignōskō,* Filemoni 1:10; Kol. 1:9; 3:10) yanarejea – msamaha, utumwa, mamlaka ya kitume, au Injili?

Katika ya maandiko ya Paulo hekima na maarifa havitenganishwi kutoka katika maisha ya maadili, lakini inatengeneza umoja wote (kama vile Filemoni 1:9; Kol 1:9-10).

**NASB** **“ambacho kimo ndani yenu kwenu kwa ajili ya kristo”**

**NKJV "ambacho kimo ndani yenu katika Kristo Yesu"**
**NRSV "kwamba tuweze kufanya kwa ajili ya Kristo"**
**TEV "ambacho tunacho katika maisha yetu katika umoja na Kristo"**
**NJB "tunaweza kufanya kwa ajili ya Kristo"**

Kuna chaguzi mbili za fasiri katika utafsiri: (1) vitu tunavyofanya kama waaminio katika Kristo au (2) vitu tulivyonavyo kama waaminio katika Kristo.

**Filemoni 1:7"Upendo"** Paulo anatumia neno hili (*agapē)* mara tatu katika kitabu chake kidogo. Alikuwa amesikia upendo wao na imani kwa Yesu na wafuasi wake (Filemoni 1:5); alikuwa na furaha tele na faraja katika upendo wao (Filemoni 1:7); na alisihi kwa Mungu huyu – upendo uliovuviwa kumuhamasisha Filemoni (Filemoni 1:9)

◙**"mioyo"** Hii kwa dhahiri ni neno "bakuli" (matumbo) *(splagchna*, kama vile Mdo 1:18). Hii inawezekana inafanana na dhabihu za Agano la Kale za sadaka za viungo hivi haswa vya mwili kwenye madhabahu (Kama vile Kutoka 29:13; Mambo ya Walawi 3:3-4,10, 15; 4:8-9; 7:3-4; 8:16, 25; 9:10,16). Watu wa kale walipata hisia katika sehemu ya chini ya kitovu (kama vile Isaya 63:15; Yeremia 4:19). Kwa Paulo inahusiana na upendo wa Mkristo (kama vile 2:1; 2 Kor. 6:12; 7:15; Filemoni 1:8, 21; Kol. 3:12; Filemon 1:7,12, 20). Kwa Mada Maalum: Watakatifu rejea uk.28

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:8-16**
**8 Kwa hiyo, nijapokuwa nina ujasiri katika Kristo kukuagiza likupasalo; 9 lakini, kwa ajili ya upendo nakusihi, kwa kuwa ni kama nilivyo, Paulo mzee, na sasa mfungwa wa Kristo Yesu pia. 10 Nakusihi kwa ajili ya mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu, yaani, Onesimo; 11 ambaye zamani alikuwa hakufai, bali sasa akufaa sana, wewe na mimi pia; 12 niliyemtuma kwako, yeye mwenyewe, maana ni moyo wangu hasa; 13 ambaye mimi nalitaka akae kwangu, apate kunitumikia badala yako katika vifungo vya Injili. 14 Lakini sikutaka kutenda neno lo lote isipokuwa kwa shauri lako, ili kwamba wema wako usiwe kama kwa lazima, bali kwa hiari. 15 Maana, labda ndiyo sababu alitengwa nawe kwa muda, ili uwe naye tena milele; 16 tokea sasa, si kama mtumwa, bali zaidi ya mtumwa, ndugu mpendwa; kwangu mimi sana, na kwako wewe zaidi sana, katika mwili na katika Bwana.**

**Filemoni 1:8**
**NASB "kuwaagizeni mfanye kile kilicho sahihi"**
**NKJV "kuwaamuru ninyi kufanya kile kinachofaa"**
**NRSV "kuwaamuru ninyi kutimiza wajibu wenu"**
**TEV "kuwaagizeni niyi kufanya kile kinachostahili kufanywa"**
**NJB "kuwaambieni ninyi nini wajibu wenu"**

Hii inaaksi mamlaka ya kitume ya Paulo. Hata hivyo, Paulo alipendelea kutumia kutia moyo na umakini wa kutumia ujuzi (Filemoni 1:9, 10, 17, 20).

**Filemoni 1:9**
**NASB, NKJV "Paulo Mzee"**
**NRSV "Mimi, Paulo, nafanya hivi kama mzee"**
**TEV "balozi"**
**NJB "Mimi, Paulo, mzee"**

Hili sio tatizo la andiko la Kiyunani kwa maana maandiko yote ya Kiyunani yana neno "mzee" (*presbutēs)*. Wana taaluma wameweka wazi kwamba maneno ya Kiyunani ya lugha ya Koine ya neno "mzee" na "balozi" (*presbutēs)* Inawezekana yalikuwa yanaandikwa kwa tarakimu zilezile au angalau mara kwa mara ukichanganya (kama vile MSS of LXX; 2 Chr. 32:31). Fasiri ya Kiingereza TEV, RSV, na NEB zina "balozi," wakati NJB na NIV zina "mzee."

Paulo ana orodhesha sababu kadhaa kwanini Filemoni anatakiwa aheshimu ombi lake.

1. Utume wa Paulo (Filemoni 1:8)
2. Umri wa Paulo (Filemoni 1:9)
3. Vifungo vya Paulo (Filemoni 1:9)
4. Huduma ya Paulo kwenye maisha ya Onesmo(Filemoni 1:10
5. Uwezekano wa huduma ya Onesmo kwa Paulo (Filemoni 1:11, 13)
6. Upendo wa Paulo kwa ajili yake( Filemoni 1:12)
7. Onesmo alikuwa amebadilishwa kutoka katika mtumwa mpaka kuwa ndugu katika Kristo (Flm. 1:15-16
8. Mtazamo wa Filemoni juu ya Paulo (Flm. 1:17)
9. Wokovu wa Filemoni wakati wa ushuhudiaji wa Paulo (Flm. 1:19)
10. Huduma ya Filemoni kwa Paulo (Filemoni 1:20)

◙**"mfungwa wa Kristo Yesu**" Angalia kidokezo katika Filemoni 1:1

**Filemoni 1:10"mwanangu"** Walimu wa sheria wanatumia tungo hii kuelezea wanafunzi wao, lakini katika muktadha huu inamaanisha wokovu wa Onesmo kupitia ushuhuda wa Paulo (kama vile1 Kor. 4:14-15; 2 Kor. 6:13; 12:14; Gal. 4:19, 1 The.2:11; 1 Tim. 1:2; 2 Tim. 1:2; 2:1; na Tito 1:4).

◙**"katika vifungo vyangu"** Hii kwa dhahiri "katika kufungwa kwangu." Haijajulikana bado namna ambavyo Onesmo alikutana na Paulo katika gereza:

1. Onesmo alikuwa amefungwa pamoja na Paulo
2. Onesmo alikuwa ametumwa kwa safari fupi kwenda kumuona Paulo gerezani
3. Alikuja kwa Paulo kwakuwa alijua Filemoni ni rafiki yake

**Filemoni 1:10 – 11 "Onesmo"** jina lilimaansha "ya kufaa" au "enye faida" (kama vile Filemoni 1:20). Paulo anatumia faida hii ya maneno kumsihi Filemoni. Huyu mtumwa aliyegeuzwa hapo mwanzo hakuwa wa faida (*achrēstos)*, lakini sasa "anafaa" (*euchrētos* kama vile 2 Tim. 4:11) kwa wote Paulo na Filemoni.

Katika Fasiri ya F.F Bruce katika kipengele hiki cha *Paul: Apostle of the Heart Set Free,* inasaidia sana kuona mchezo wa maneno:

"Jina lake ni Onesmo – mwenye kupata faida kwa jina na kwa asili. Najua kwamba katika siku zilizopita mlijua kuwa si wa faida, lakini sasa, nakuhakikishia, amejifunza kuwa mkweli kwa jina lake – mwenye faida kwenu na mwenye faida kwangu" (ukurasa wa 393).

**Filemoni 1:12 "niliyemtuma kwako"** Tungo hii ina kidokezo cha kisheria cha "kumaanisha jambo lake kwako." Hii pia inamaanisha kwamba waaminio lazima wakabiliane na matokeo ya matendo yao hata kama yalifanywa kabla ya wokovu. Pia ilikiri haki za kisheria za wamiliki wa watumwa (Filemoni 1:14, 18).

◙**"maana ni kutuma moyo wangu hasa"** Hii ni kauli kali sana! Paulo alikuwa na hisia za ndani kwa watu waliongoka kupitia yeye. Hii hakika inafunua moyo wa kichungaji wa Paulo, kama anavyofanya kumlea kwa namna thabiti ya Filemoni.

**Filemoni 1:13** Paulo kwa udhahiri alikuwa mtu anajitegemea kifedha. Mara nyingi alikataa msaada wa kifedha kutoka kwa watu alio wahubiri kwasababau walimu wa uongo walimshutumu kwa unyonyaji wa kifedha.ila kadiri miaka ilivyokwenda alikuwa na uwezo wa kupokea misaada kutoka katika baadhi ya makanisa aliyokuwa akiyahudumia kiroho. Msaada huu ulikuwa wa namna mbili.

1. Kanisa la Filipi (Wafilipi 1:5, 7; 4:15) na yawezekana kanisa la Thesalonike (kama vile 2 Wakorintho 11:9) walimtumia fedha aliweze kukidhi mahitaji yake akiwa gerezani
2. Kanisa katika Filipi lilituma wawakilishi, Epafrodito, kusaidia Paulo, (kama vile Wafilipi 2:25)

Katika namna hiyo inayofanana Paulo alimuona Onesmo kama zawadi kutoka kwa Filemoni na kanisa katika Kolosai.

**Filemoni 1:14** Mungu anaangalia katika moyo, nia kwanza (kama vile 1 Samweli 16:7; 1 Wafalme 8:39; 1 Mambo ya Nyakati 28:9; Yeremia 17:10; Luka 16:15; Mdo. 1:24). Paulo alimtaka Filemoni abarikiwe kwa ukarimu wake na upendo kwa Kristo (kama vile 2 Kor. 8-9), sio tu kwa utii wake kwa maagizo ya Paulo (kama vile Filemoni 1:8).

**Filemoni 1:15 "Maana, labda ndiyo sababu alitengwa nawe kwa muda"** Hiki ni kitenzi cha Irabu sauti tendewa. Tungo hii inaweza kueleweka kwa namna mbili: (1) katika namna ya mpango wa Mungu ulioamriwa kabla (ukingo wa NASB una mrandano wa kimaandiko wa Mwanzo 45:5, 8) au (2) kwamba Mungu alitumia tabia isiyo sahihi ya Onesmo kama fursa kwa ajili ya wokovu wake na huduma ya Filemoni kwa Kristo na urafiki na Paulo (kama vile Filemoni 1:16).

**Filemoni 1:16 "si kama mtumwa, ……………ndugu mpendwa"** Wakristo hawakukabiliana na utumwa kwa uwazi (kama vile Waefeso 6:5-9), lakini ikiharibiwa na maoni ya heshima na kustahili kwa binadamu (kama vile Gal. 3:28; Kol. 3:11). Angalia Mada Maalum: Maonyo ya Paulo kwa watumwa katika Waefeso 6:5.

**NASB, NKJV**
**NRSV "yote katika mwili na katika Bwana"**
**TEV "yote kama watumwa na ndugu katika Bwana"**
**NJB "yote katika hali ya asili na katika Bwana"**

Tungo hii inaelezea faida za kurudi kwa Onesmo katika hali mbili, moja ya asili (ya mwili) na nyingine iliyo juu ya asili (ya kiroho). Filemoni angepata faida kama mtu wa kawaida na kama mkristo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:17-20**
**17 Basi kama ukiniona mimi kuwa mshirika nawe, mpokee huyu kama mimi mwenyewe. 18 Na kama amekudhulumu, au unamwia kitu, ukiandike hicho juu yangu. 19 Mimi Paulo nimeandika kwa mkono wangu mwenyewe, mimi nitalipa. Sikuambii kwamba nakuwia hata nafsi yako. 20 Naam, ndugu yangu, nipate faida kwako katika Bwana; uniburudishe moyo wangu katika Kristo.**

**Filemoni 1:17-18 "ikiwa"** kulikuwa na madaraja mawili ya sentensi zenye masharti zinazokadiriwa kuwa kweli kutoka katika mawazo ya mwandishi au kwa makusudi yake ya kifasihi. Filemoni alikuwa rafiki wa Paulo na Onesmo alimkosea (kama vile Filemoni 1:18).
◙**"mshirika"** hii ni neno *koinōnu* lenye muundo wa neno *koinōnia "*kushirikisha pamoja na." "kuwa na ushirika nae" au "kuwa katika chama." Paulo analitumia kumaanisha michango ya kifedha (kama vile Wafilipi 4:15). Hivyo inaweza ikawa mchezo wa maneno unaohusiana na urafiki wa Paulo (Filemoni 1:19) na madai ya Onesmo (Filemoni 1:17).

◙**"mpokee huyu kama mimi mwenyewe"** kauli ya Paulo inaweza kuwa ilitokana na maneno ya Yesu katika Mathayo 25:44-45 au yaliyokwisha kuyapitia alipokutana na Yesu njiani Dameski (kama vile Mdo 9).Kwa kuwatesa Wakristo, Paulo alikuwa anamuudhi Kristo. Kwa kukubali Onesmo, Filemoni alikuwa anamkubali Paulo. Upendo wa kweli ni mzuri, sawa jumuishi na wa mabadilishano. Tunaona upendo wetu kwa Mungu ka namna tunavyopendana sisi kwa sisi (kama vile 1 Yohana 2:9, 11, 4:20).

**Filemoni 1:18** Kiashiria cha sarufi ya mstari wa 18 ni kwamba Onesmo aliiba kutoka kwaFilemoni (sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti), kwamba Onesmo alikuwa anamdai Filemoni (kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo usio timilifu) na kwamba Paulo alielewana na Filemoni kuwa kama ana madai basi ayaweke katika kumdai yeye Paulo (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo usio timilifu).

**Filemoni 1:19"Mimi Paulo nimeandika kwa mkono wangu mwenyewe"** Kwa dhahiri Paulo alitumia waandishi kuandika kwa ajili yake (kama vile Tertio katika Warumi 16:22), yawezekana kwasababu ya matatizo ya macho (kama vile Wagalatia 4:15; 6:11), yawezekana ikawa imesababisha ufahamu wa uongofu (kama vile Mdo. 9:8, 18: 22:11; 26:13). Hata hivyo kunaweza kuwa na barua za kutunga zikidaiwa kuwa zimeandikwa na Paulo zikizunguka miongoni mwa makanisa (kama vile 2 The. 3:17). Kwa hivyo Paulo alichukua kalamu na karatasi na kuandika mistari michache kwa ajili yake mwenyewe (kama vile 1 Kor. 16:21; Gal. 6:11; Kol. 4:18; 2 The. 3:17; Filemoni 1:19)

◙**"kwamba nakuwia hata nafsi yako"**Hii kwa nguvu inamaanisha kwamba Paulo aliongoza Filemoni kwa imani katika Kristo. Wakati na mahali haijajulikana kwa Paulo hakuanzisha kanisa katika Kolosai. Dhanio bora zaidi ni kwamba Filemoni kama Epafra aliokolewa wakati wa miaka miwili ya Paulo ya uamsho katika Efeso (kama vile Mdo. 19:10, 20).

**Filemoni 1:20** Mstari huu ni sawa na Warumi 1:12. Namna tunavyoishi kama Wakristo kunatia moyo na kupendezesha waumini wengine.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1: 21**
**21 Kwa kuwa nakuamini kutii kwako ndiyo maana nimekuandikia, nikijua ya kuwa utafanya zaidi ya hayo nisemayo.**

**Filemoni 1:21** "Hii ilikuwa mbinu ya ujuzi ya Paulo kuhakikisha ushirikiano wa Filemoni"

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:22**
**22Na pamoja na hayo uniwekee tayari mahali pa kukaa; maana nataraji ya kwamba kwa maombi yenu mtajaliwa kunipata.**

**Filemoni 1:22"uniwekee tayari mahali pa kukaa"** Paulo alikuwa natarajia kufunguliwa (kama vile Wafilipi 1:25; 2: 24). Barua za kichungaji (I na 2 timotheo na Tito) inaweka kumbukumbu ya safari yao ya kimishionari wakati Matendo ya Mitume inamalizika wakati Paulo bado yuko gerezani baada ya safari yake ya tatu ya kimishionari.

Inashangaza kuona Filemoni anadhaniwa kuwekwa kundi moja na Wakolosai na Waefeso,inatokea mwanzo katika vifungo vya Paulo. Katika vitabu hivi, Paulo alikuwa hajui matokeo au nini yatakuwa maamuzi ya vifungo vyake. Katika Wafilipi iliyoandikwa kuelekea mwisho wa vifungo vya Paulo, alitegemea kuachiliwa. Kwahiyo maoni haya katika Filemoni 1:22 yumkini yalikuwa (1) njia ya kumkumbusha Filemoni kwamba angekutana na Paulo ana kwa ana na yawezekana karibuni – kuhusu ombi lake la kumsamehe na kumkubali Onesmo au (2) nahau kwa ajili ya ukalimu.

◙**"kupitia maombi yenu"** Paulo aliamini katika nguvu ya mombi (kama vile Waefeso 6: 18-19). Pia alitendea kazi kile alichokihubiri (angalia maneno tofauti yaliyotumika ya Kiyunani: *deomai*, 2 Kor. 5:20; 8:4; 1 The. 3:10; *proseuchomai,* Mdo.16:25; 20:36; 21:5; 22:17; 28:8; Fil. 1:9; Kol. 1:3,9; 4:3; 1 The. 5:17,25; 2 The. 1:11; 3:1; 1 Tim. 2:8; *proseuchē,* Mdo.16:13,16; Rum. 1:9; 12:12; 15:30; 1 Kor. 7:5; Efe. 1:16; Fil. 4:6; Kol. 4:2,12; 1 The. 1:2; 1 Tim. 2:1; 5:5; Filemoni 4,22).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:23-24**
**23 Epafra, aliyefungwa pamoja nami katika Kristo Yesu, akusalimu; 24 na Marko, na Aristarko, na Dema, na Luka, watendao kazi pamoja nami.**

**Filemoni 1:23-25** hii inafanana na hitimisho la Wakolosai. Vitabu hivi (Filemoni na Wakolosai) vinatoka katika mazingira yaleyale ya kihistoria.

**Filemoni 1:23 "Epafra"** Alikuwa mwanzilishi wa makanisa matatu (Kolosai, Hierapoli, na Laodikia) katika bonde la mto Lycus, na uwakilishi wa Paulo (Wakolosai 1:7). Yawezekana aligeuzwa wakati wa Paulo alipokaa katika Efeso (kama vile 19:10). Jina lake lilikuwa ufupisho wa Epafrodito ambalo lilikuwa kwa asili likifanana na mungu mke Afrodito. Mtu mwingine kwa jina hili hili anatajwa katika Wafilipi 2:25; 4:18. Hata hivyo, alikuwa akitokea sehemu nyingine tofauti kijiografia.

**Filemoni 1:24 "Marko"** alikuwa akijulikana kama Yohana na Marko mjomba wake Barnaba" katika nyumba ya Yohana Marko palikuwa sehemu ya Meza ya Bwana na Chumba cha juu wakati Yesu alipokuwa akiwatokea wanafunzi baada ya Ufufuo (Mdo 12:12). Alikuwa mwandishi wa injili ya Marko na rafiki na mwandishi wa Petro (kama vile 1 Petro 5:13). Alikuwa ni chanzo cha kutoelewana kukubwa kati ya Barnaba na Paulo baada ya safari yao ya kwanza ya kimishionari (Mdo 12:25; 13:5; 15:36-39). Baadaye hata hivyo Paulo alimsamehe na kumthibitisha (kama vile 2 Tim 4:11).

◙**"Dema"** Dema alikuwa mmoja wa wasiri wa Paulo na mtenda kazi pamoja naye. Alitajwa pamoja na Epafra, Luka, Aristako na Marko katika Kol 4:10-12. 2 Timotheo 4:9 inaorodhesha watendakazi wale wale wawili, Luka na Marko. Maandiko yanaelezea kwamba "Dema, baada ya kuipenda dunia, akaniacha." Paulo alikuwa na wasaidizi wengi. Wengine kama Luka walikuwa waaminifu. Wengine kama Yohana Marko kwa wakati fulani hawakuwa waaminifu na kurudi katika huduma. Dema kwa dhahiri aliacha huduma ya Paulo kwasababu ya majaribu asiyoyataja au fursa zisizotajwa. Hakuna mahali panapo onekana au hii haimaanishi kuwa alimwacha Kristo.

◙**"Luka"** Alikuwa Mtenda kazi wa karibu sana wa kimishionari wa Paulo na daktari (kama vile Kol. 4:14; 2 Tim. 4:11) . Alikuwa na Paulo wakati wa mizunguko yake mingi ya kuhubiri injili katika Matendo ya Mitume. Hii inadhibitishwa na kauli ya neno"tu" katika Matendo ya Mitume (kama vile Mdo 16:11,16; 20:6,7,13; 21:1,5, 7,10,12,15,17,25; 27:1,18,26,27). Luka anaweza kuwa alikuwa "mtu wa Makedonia" katika Mdo.16:9.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): FILEMONI 1:25**
**25 Neema ya Bwana Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu.**

**Filemoni 1:25** Huu ni mfano dhahiri wa namna ya ufungaji wa Paulo wa Baraka. Angalia kwamba tungo "iwe na roho zenu" ni mfano mzuri wa utumiaji wa herufi ndogo "r" (roho) ambalo lilitumika kwa roho ya binadamu, (au binafsi, kama vile Mdo.7:59; 2 Tim. 4:22) na sio Roho Mtakatifu (kama vile Wagalatia 6:18; Wafilipi 4:23). Hata hivyo katika namna nyingi katika Agano la Kale, linamaanisha roho ya mtu ambayo inatiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Hii yawezekana ndio maana yake hapa.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kanisa la kwanza lilikutana wapi?
2. Ni kwa nani barua hii ilikuw aimekusudiwa kufika?
3. Barua hii inafunua vipi mbinu za kichungaji za Paulo?
4. Ni kwa namna gani barua hii inahusiana na jambo la utumwa?
5. Kwanini Filemoni 1:22 inashangaza?
6. Kwanini "roho" liko katika herufi ndogo?

# UTANGULIZI WA WAFILIPI

## MAELEZO YA AWALI

A. Hii ni moja ya barua za Paulo za kawaida. Akiwa pamoja na kanisa hili hakujisikia hitaji la kuelezea juu ya mamlaka yake ya Kiutume. Kujawa kwake na furaha juu yao ni dhahiri. Aliwaruhusu hata kumtumia fedha (kama vile Flp. 1:5,7; 4:15), ambapo haikuwa kawaida kwake.
B. Paulo akiwa gerezani, bado analitumia neno kwa furaha (nomino na kitenzi) mara kumi na sita. Amani na tumaini lake havikujikita juu ya mazingira.
C. Kuna dalili ya kuwepo kwa mafundisho ya uongo ndani ya kanisa (kama vile Flp. 3:2, 18-19). Hawa waasi wanaonekana kuwa sawa na wale walio katika makanisa ya Galatia, ambao waliitwa Washikiria Sheria na tamaduni za Kiyahudi sana. Hawa walisisItiza kwamba mtu anatakiwa kuwa Myahudi kabla ya kuwa Mkristo.
D. Hii barua inahusisha mfano wa nyimbo za kale za ki-Kristo za kumtukuza Mungu, kanuni za imani, ama mashairi ya kiluturujia (kama vile Flp. 2:6-11). Hii ni moja ya vifungu vizuri sana vya thiolojia kumhusu Kristo katika Agano Jipya lote (kama vile Yohana 1:1-14; Kol.1:13-20; Ebr. 1:2-3). Paulo anaitumia kama mfano wa unyenyekevu wa Kristo unaopaswa kuigwa na kila mwamini (kama vile Flp. 2:1-5), si katika mwanzo wa maana ya mafundisho.
E. Katika mistari 104 ya kitabu, Jina la Yesu ama wadhifa linatokea mara 51. Inaonekana wazi huyu ndiye mkuu ndani ya moyo wa Paulo, fikra, na theolojia.

## FILIPI NA MAKEDONIA

A. Jiji la Filipi
   1. Katika 356 k.k. jiji hili lilitekwa na kupanuliwa na Filipi II wa Makedon, baba wa Alexanda Mkuu. Mwanzoni kijiji cha Thracia kiliitwa *Krenides* (chimbuko). Hili jiji lilikuwa muhimu kwa sababu ya mawe ya dhahabu ndani yaliyokuwa ndani ya eneo hilo
   2. Katika mapigano ya Pydna katika 168 k.k. eneo hili lilikwa Jimbo la Kirumi na baadaye kuwa moja kati kwa yale manne yaliyokuwa Makedonia.
   3. Katika 42 k.k. Brutus na Cassius (walioutetea muundo wa serikali ya Kijamhuri) walipigana na Antoni na Octavian (walioutetea mfumo wa serikali ya Kifalme) karibia na Filipi, juu ya mageuzi ya kiserikali katika Rumi. Baada ya mapigano hayo, Antoni aliishi hapa na baadhi ya mashindi wake walibobea.
   4. Katika 31 k.k. baada ya mapigano ya Actium ambapo Octavian alimshinda Antoni, wafuasi wa Antoni waliokuwa Rumi waliondolewa na kuhamishiwa hapa.
   5. Katika 31 k.k. Filipi ikawa Koloni la Kirumi (kama vile Matendo 16:12). Wale watu walioishi mijini walitangazwa kuwa raia wa Rumi. Lugha ya Kilatini ilikuwa ikizungumzwa na jiji likawa kama Rumi ndogo. Hii ilikuwa karibu na Njia ya kuelekea Ignatia, njia kuu ya mashariki hadi njia kuu ya Magaharibi mwa njia kuu ya Kirumi. Upendeleo maalum walioufahidi kama raia wa Kirumi ulikuwa:
      a. kutokuwepo kwa kodi za kichwa na kodi za ardhi
      b. haki ya kununua na kuuza bidhaa
      c. ulinzi wote na haki za sheria za Kirumi
      d. viongozi maalum wa serikali za mitaa (maakimu na afisa wa mahakama)

B. Injili Iliyoingia Filipi
   1. Katika safari ya pili ya kimisheni Paulo alitaka kurudi kaskazini na kuingia kaskazini mwa Asia ya kati (Uturuki ya sasa, kibiblia Bithynia). Badala yake, katoka maono alimwona mwanamme (bila shaka ni Luka) wa Makedonia (kaskazini mwa Uyunani) akimwita na kuja kuwasaidia (Matendo 16:6-10). Kwa maono haya Roho alimwongoza Paulo hadi Ulaya.

2. Paulo alifuatana na wasaidizi wake
    a. Sila (Silvano)
        (1) Sila alikuwa kiongozi na nabii kutoka kanisa la Jerusalemu ambaye alichukua nafasi ya Barnaba kama mtendakazi wa umisheni wa Paulo (kama vile Matendo 15:15:22,32; 36-41).
        (2) Sila na Pauo wote walifungwa gerezani huko Filipi (Matendo 16:16-26).
        (3) Paulo mara nyingi alijiita Silvano (kama vile 2 Kor. 1:19; 1 The. 1:1; 2 The. 1:1).
        (4) Inawezekana kwamba baadaye Sila alikuja kuwa rafiki mwenza wa Petro, kama Yohana Marko alivyofanya (kama vile 1 Pet. 5:12).
    b. Timotheo
        (1) Huyu alibadili dini Kwenye safari ya kwanza ya kimisheni ya Paulo (kama vile Matendo 16:1-2; 2 Tim. 1:5;3:15)
        (2) Bibi na mama yake walikuwa Wayahudi, lakini baba yake alikuwa Myunani (kama vile Matendo 16:1; 2 Tim. 1:5).
        (3) Kwa kuwa alishuhudiwa vema na ndugu (kama vile Matendo 16:2) na Paulo aliziona karama za huduma ndani yake (kama vile 1 Tim. 4:14; 2 Tim. 1:6), alimchagua yeye kama msaidizi ili kuchukua nafasi ya Yohana Marko (kama vile Matendo 13:13).
        (4) Paulo alimtahiri Timotheo ili kwamba aweze kukubalika kwa Wayahudi (kama vile Matendo 16:3).
        (5) Timotheo akawa mwakilishi mwaminifu wa kitume kwa Paulo (kama vile Flp. 2:19-22; 1 Kor. 4:17; 3:2,6; 2 Kor. 1:1,19).
    c. Luka
        (1) Jina lake halikujulikana, lakini bila shaka, mwandishi wa Injili ya Luka na kitabu cha Matendo alikuwa Luka.
        (2) Kwa uwazi kabisa huyu alikuwa tabibu wa Mataifa (kama vile Kol. 4:14). Wengine wanafikiri neno "tabibu" lilimaanisha "aliyesoma sana." Bila shaka ni kweli kuwa huyu alihabarisha katika maeneo kadhaa kwa kutumia mbinu zaidi ya zile za kitabibu, kama vile mashua. Hata hivyo, Yesu alilitumia neno hili hili la Kiyunani "tabibu" (kama vile Matendo Mt. 9:12; Marko 2:17; 5:26; Luka 4:23; 5:31)
        (3) Huyu alikuwa msafiri mwenza wa Paulo (kama vile Matendo 16:10-17; 20:5-15; 21:1-18; 27:1-28:16; Kol. 4:14; 2 Tim. 4:11; Filimoni 1:24).
        (4) Inatia shauku kwamba vifungu vya neno "sisi" vya Matendo vinaanza na kumalizika katika Wafilipi. Katika *Paul, Apostle of the Heart Set Free*, (uk. 219), F. F. Bruce anatoa maoni kwamba Luka alikaa huko Filipi kwa ajili ya kuwasaidia waamini wapya na kukusanya fedha za msaada kwa Mataifa kwa ajili ya kanisa la Jerusalemu.
        (5) Luka anaweza kuwa, katika maana, tabibu pekee wa Paulo. Paulo alikuwa na matatizo kadhaa ya kimaubile kutokana na ubadilikaji wake (kama vile Matendo 9:3,9), huduma yake (kama vile 2 Kor. 4: -12; 6:4-10; 11:23-29) na udhaifu wake wa kipekee (kama vile 2 Kor 7. 12:1-10).

3. Paulo alirudi Filipi katika safari yake ya tatu ya kimisheni (kama vile Matendo 20:1-3,6). Alimtuma Sila na Timotheo mwanzoni (kama vile Matendo 19:19-24; Flp. 2:19-24).

C. Filipi kama Koloni la Kirumi (kama vile Matendo 16:12)
    1. Paulo alilitumia jina la mji kama koloni la Kirumi katika istilahi yake
        a. "askari wa hakimu," Flp. 1:13

b. "uraia," 3:20 (Matendo 16:22-34, 35-40)

c. "nyumbani mwa Kaisari," Flp. 4:22

2. Mji ulijaa askari wa Kirumi waliokuwa wastaafu na waliokuwa uhamishoni. Katika namna mbalimbali hii ilikuwa "Rumi ndogo." Vivutio vya Kirumi viliweza kuonekana katika mitaa ya Filipi (kama vile Matendo 26:21).
3. Wote Paulo (Matendo 22:25; 26:32) na Sila (Matendo 16:37) walikuwa raia wa Kirumi, ambapo waliruhusiawa kuwa na haki za kisheria na nafasi ya kijamii.

D. Jimbo la Makedonia

1. Wanawake walikuwa na uhuru zaidi na fursa za kiuchumi katika Makedonia kuliko sehemu yoyote ndani ya Dora ya Kirumi.
2. Hili linafafanuliwa kwa
    a. kuwepo kwa wanawake wengi waliokuwa wakisali kando kando ya mto nje ya Filipi (kama vile Matendo 16:13)
    b. mwanamke mfanya biashara Lidia (kama vile Matendo 16:14)
    c. wanawake waliofanya kazi kwa pamoja katika injili (kama vile Flp. 4:2-3)
    d. wanawake wenye vyeo waliotajwa huko Thesalonika (pia katika Makedonia, kama vile Matendo 17:4).

## MWANDISHI

A. Hii barua kuu ya kipekee imeongeza sifa kwa Paulo. Kiwakilishi cha cha nafsi ya kwanza "Mimi" na "yangu" kimeonekana mara 51.

B. Imenukuliwa ama kudokezwa na waandishi wa kale (kwa dondoo kamili tazama H. C. G. Moule, *Studies in Philippians*, kr. 20-21, kilichochapishwa na Kregel):

1. Clementi wa Rumi katika *I Clement*, kilichondikwa kwa kanisa la Kikorintho yapata 95 b.k
2. Ignatius, katika *Letters of Ignatius*, mnamo 110 b.k
3. Polycarp, yule rafiki mwenza wa Mtume Yohana, katika *Letter to the Philippians*, mnamo 110 b.k
4. Utangulizi wa Marcionite (mfuasi wa Marcion muasi) kwa barua ya Paulo kwa Wafilipi mnamo 170 b.k
5. Irenaeus, mnamo 180 b.k
6. Clementi wa Alexandria, yapata 190 b.k
7. Tikiko wa Carthage, yapata 210 b.k

C. Japokuwa Timotheo anatajwa pamoja na Paulo katika Flp. 1:1, yeye alikuwa mtenda kazi mwenza, si mwandishi mwenza (japo angewaza kufanya kazi kama mwandishi kwa Paulo kutoka enzi na enzi).

## TAREHE

A. Tarehe haina uhakika wapi Paulo alitiwa gerezani (kama vile 2 Kor. 11:23)

1. Filipi, Matendo 16:23-40
2. Efeso, 1 Kor. 15:32; 2 Kor. 1:8
3. Yerusalemu/Kaizaria, Matendo 21:32-33:30
4. Rumi,Matendo 28:30 (imeelezwa katika Utangulizi Marcionite kwa Wafilipi)

B. Wasomi walio wengi wanaamini kwamba kifungo cha Kiyunani kinaendana na muktadha wa maisha ya Paulo na kitabu cha Matendo ni kizuri zaidi. Kama ni hivyo,le tarehe ya mwanzoni mwa miaka ya 60 inaonekana kufaa zaidi.

C. Hiki kitabu kinajulikana kama moja ya "nyaraka za gerezani" za Paulo (Wakolosai, Waefeso, Filimoni, na Wafilipi). Kutokana na fikra za ndani inaonekana kwamba Wakorosai, Waefeso, na Filemoni viliandikwa mwanzoni wakati wa kifungo cha Kirumi kwa Paulo na kuchukuliwa kwa pamoja na Tychicus hadi Asia Ndogo (Kol. 4:7; Efe. 6:21). Wafilipi walikuwana tabia tofauti. Paulo aliona tumaini kuwa angeachiliwa kutoka kifungoni (Flp. 1:17-26) na angeweza kuwatembelea (2:24).

Muundo huu pia unatoa kipindi cha wakati kwa: (1) Uwezo wa Paulo wa kuwafikia askari wa Kifalme (kama vile Flp. 1:13; Matendo 28:16)na wahudumu (kama vile Fp. 4:22 na (2) ziara kadhaa kati ya Paulo na wajumbe katoka kanisa la Filipi.

## MADHUMUNI YA BARUA

A. Kuzitoa shukrani za Paulo kwa kanisa hili pendwa ambalo lilimsaidia kifedha mara kadhaa na hata kumtuma msaidizi, Epafrodito (kama vile Flp. 1:3-11; 2:19-30; 4:10-20). Pia barua inaweza kuwa imeandikwa kwa ajili ya kueleza kuhusu Epafrodito kurudi nyumbani mapema wakati Paulo alipokuwa gerezani.

B. Kuwatia moyo Wafilipi kuhusiana na mazingira yake. Hakika injili ilikuwa ikiendelea mle gerezani. Paulo aliwekewa mipaka, lakini injili haikuwekewa mipaka!

C. Kuwatia moyo Wafilipi dhidi ya mafundisho ya walimu wa uongo yaliyoonekana kuwa sawa na Washikiria sana Sheria, tamaduni za Kiyahudi wa Wagalatia. Hawa waasi walidai kuwa waamini wapya wawe Wayahudi kwanza na kasha wawe Wakristo (kama vile Matendo 15). Hata hivyo kwa sababu ya orodha ya dhambi katika Flp. 3:19 hii inaendana zaidi na wale walimu wa uongo wa Kiyunani (Wanamafunuo ya Uongo) kuliko wale wa Kiyahudi, ufanano wa hawa waasi si yumkini. Inawezekana kwamba baadhi ya waamini waliyarudia maisha yao ya awali ya kutomjua Mungu.

D. Kuwatia moyo Furaha ya Paulo ilitegemea 'juu ya mazingira lakini juu ya imani yake katika Kristo. Furaha hii katikati ya matatizo ilikuwa makubaliano ya Kiuvumilivu, lakini ni mtazamo wa kiulimwengu na mapambano thabiti. Paulo alizitumia sitiari kutoka katika maeneo mbalimbali ya maisha ili kueleza juu ya nguvu ya maisha ya Mkristo.
   1. riadha (kama vile Flp. 3:12,14; 4:3)
   2. askari (kama vile Flp. 1:7,12,15,16,17,22,28,30);
   3. biashara (kama vile Flp. 3:7,8; 4:15,17,18)

## MUHTASARI WA KIMUKTADHA

A. Ni vigumu kukielezea kwa muhtasari kitabu cha Wafilipi kwa sababu ni cha maelezo binafsi na kisicho rasmi. Paulo alikuwa akizungumza na marafiki zake na aliwaamini watenda kazi pamoja naye katika Kristo. Moyo wake ulijawa na fujraha kabla ya fikra zake kupanga mawazo mengine. Kwa namna ya uwazi wa ajabu hiki kitabu kinaufunua moyo wa Mtume aliye mkuu kwa Mataifa. Paulo alijisikia mwenye “furaha”katika Kristo, katika mazingira yoyote yale na katika huduma ya injili.

B. Sehemu za fasihi
   1. Utangulizi ule ule wa namna ya Paulo, Flpl. 1:1-2
      a. salamu
         (1) kutoka kwa Paulo (na Timotheo) Flp. 1:1

(2) kwa watakatifu walioko Filipi (wakiwemo maaskofu na mashemasi), Flpl. 1:1
(3) mtindo wa maombi ya Paulo , Flp. 1:2

b. maombi, Flp. 1:3-11:
(1) ushirika katika injili tangu siku ya kwanza, Flp. 1:5
(2) waunga mkono wa huduma ya Paulo, Flpl. 1:7
(3) Ombi la Paulo kwa:
(a) upendo mwingi, Flp. 1:9
(b) ufahamu tele, Flp. 1:9
(c) utambuzi tele, Flp. 1:9
(d) utakatifu tele, Flp. 1:10

2. Uhusiano wa Paulo kwao dhidi ya uhusiano wao kwake, gerezani, Flp. 1:12-26
   a. Mungu ameutumia wakati wake gerazni ili kuineza injili
      (1) kwa askari wa Kifalme, Flpl. 1:13
      (2) kwa wale walio nyumbani mwa Kaizari, Flp. 1:13; 4:22
      (3)Kifungo cha Paulo pia kutiwa moyo kwa wahubiri, Flp. 1:14-18
   b. Tumaini la Paulo la kuachiliwa huru kwa sababu ya
      (1) maombi yao, Flp. 1:19
      (2) Roho Mtakatifu, Flp. 1:19
   c. Tumaini la Paulo kwa vyovyote katika kuachiliwa huru ama katika mauti, Flp. 1:20-26
3. Msistizo wa Paulo, Flp. 1:27-2:18
   a. wito kuenenda kama Kristo katika umoja katikati ya mateso, Flp. 1:27-30
   b. kuishi katika ufanano pekee wa Kristo, Flp. 2:1-4
   c. Kristo mfano wetu, Flp. 2:5-11Flp. 2:12-18
4. Mipango ya Paulo iliyowahusu Wafilipi, Flp. 2:19-30
   a. kumtuma Timotheo Flp. 2:19-24
   b. kurudi kwa Epafrodito, Flp. 2:25-30
5. kusimama imara dhidi ya walimu wa uongo, Flp. 1:27; 4:1
   a. mbwa, watahiriwa wa uongo, wenye kushika Sheria za Kiyahudi sana (Matendo 15, Wagalatia), Flp. 3:1-4
   b. urithi wa Paulo wa Kiyahudi
      (1) katika haki ya walimu wa uongo, Flp. 3:5-6
      (2)katika haki ya Kristo, Flp. 3:7-16
   c. Huzuni ya Paulo juu yao, Flp. 3:17-21
6. Paulo anayarudia maonyo yake
   a. umoja, Flp. 4:1-3
   b. sifa za kumfanana Kristo, Flp. 4:4-9
7. Paulo anazirudia shukrani zake kwa masaada wa Wafilipi
   a. kipawa chao cha sasa,Flp. 4:10-14
   b. kipawa chao cha awali, Flp. 4:15-20 (1:5)
8. hitimisho lile lile la Pauline, Flp. 4:21-23

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka "A Guide To Good Reading" (Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu chote cha Biblia kwa mara moja. Eleza dhamira kuu ya kitabu kizima kwa maneno yako mwenyewe (mzunguko wa usomaji #1)

5. Dhamira kuu ya kitabu kizima
6. Aina ya fasihi (aina ya fasihi aliyotumia katika kuwasilisha ujumbe wake).

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (**Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" (Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu kizima cha Biblia kwa mara ya pili kwa mara moja. Weka kwa muhtasari masomo makuu (mzunguko wa Usomaji #2) na elezea somo kwa sentensi moja.

11. Somo la kipengele cha kwanza cha fasihi
12. Somo la kipengele ya pili cha fasihi
13. Somo la kipengele cha tatu cha fasihi
14. Somo la kipengele cha nne cha fasihi

# WAFILIPI 1

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Salamu | Salamu | Salamu | Salamu | Anwani |
| 1:1-2 | 1:1-2 | 1:1a | 1:1a | 1:1-2 |
| | | 1:1b | 1:1b | |
| | | 1:2 | 1:2 | |
| Maombi ya Paulo Kwa Wafilipi | Shukrani na maombi | Shukrani | Maombi ya Paulo kwa Wasomaji | Shukrani na Maombi |
| 1:3-11 | 1:3-11 | 1:3-8 | 1:3-8 | 1:3-11 |
| | | 1:9-11 | 1:9-11 | |
| Kwangu kuishi ni Kristo | Kristo anahubiriwa | Mapito ya sasa ya Paulo | Kuishi ni Kristo | Mapito yake Paulo mwenyewe |
| 1:12-14 | 1:12-18 | 1:12-14 | 1:12-14 | 1:12-26 |
| 1:15-26 | | 1:15-18a | 1:15-17 | |
| | | 1:18b-26 | 1:18-26 | |
| | Kuishi ni Kristo | | | |
| | 1:19-26 | | | |
| | Kug'ag'ana na Mateso Kwa ajili ya Kristo | | | kuvipiga vita vya imani |
| 1:27-30 | 1:27-30 | 1:27-30 | 1:27-30 | 1:27-30 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.
Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.
Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani (Brief Definitions of Greek Grammatical Structure), Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi (Textual Criticism), Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko (Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")

## *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Wafilipi 1:1-2 inaunda utangulizi wa jumla kwa barua nzima. Kiuhalisia utangulizi ni wa ki-Paulo isipokuwa ukweli kwamba hakuna msisitizo kwenye utume wake. Kanisa hili na Paulo walikuwa na uhusiano mzuri wa ajabu. Hakuhitaji kuchomekea mamlaka yake ya kitume. Kanisa hili kwa dhahiri lilituma msaada wa kifedha kwa Paulo mara kwa mara (kama vile Flp. 1:5,7; 4:15). Kanisa lingine la Paulo ambalo tunajua alipokea msaada ni la Thesalonika (kama vile 2 Wakorintho 11:9).

B. Barua za Kiyunani za karne ya kwanza kiuhalisia zilifungua kwa maombi ya shukrani. Wafilipi 1:3-8 ni maombi ya Paulo kwa kanisa la Wafilipi. Walijumuisha kweli kuu za Kikristo na jozi za ajenda kwa barua zao.

C. Kitabu hiki kina hesabu ambatani isiyo ya kawaida pamoja na *syn* (Kiyunani "*sun*" (jua)) ambayo ilimaanisha"kwa kushirikiana na":
   1. Fil. 1:7; 4:14 *syn* + usharika (*koinōnia*, mzizi uleule, Flp. 1:5; 2:1; 3:10; 4:14,16)
   2. Fil. 1:27 *syn* + kung'ang'ana (*athleō* katika Flp. 4:3 jina sahihi)
   3. Fil. 2:2 *syn* + nafsi (*psuchē*, maana ileile katika Flp. 1:27)
   4. Fil. 2:17-18 *syn* + kufurahi (*chairō*)
   5. Fil. 2:25; 4:3 *syn* + mfanyakazi (*ergon*, kama vile Rum. 16:3,9,21; 2 Kor. 1:24)
   6. Fil. 2:25 *syn* + askari (*stratiōtē*, kama vile Filemoni 1:2)
   7. Fil. 3:10 *syn* + muundo (*morphē*)
   8. Fil. 3:17 *syn* + mwanzilishi (*animeomai*, mzizi ule ule katika 1 Kor. 4:16)

D. Wafilipi 1:9-11 ni maombi ya Paulo kwa ajili ya ukuaji wa kiroho na makuzi ya kanisa. Mistari hii inalenga kwenye mtindo wa maisha ya kufanana na Kristo kwa Wafilipi wakati mistari ya 3-8 inalenga kwenye nafasi ya Kristo hivyo kuunganisha vipengele viwili vya wokovu; nafasi yetu katika Kristo (kuhesabiwa haki na kutakaswa kinafasi) na kumiliki kwa hiyo nafasi katika kufanana na Kristo (utakaso endelevu).

E. Kuna vidokezo kadhaa ambavyo Paulo alitegemea mara atakapofunguliwa kutoka geezani katika Wafilipi 1:17-26:
   1. Neno "kukombolewa" katika Wafilipi 1:19
   2. Sentensi yenye masharti daraja la kwanza ya Wafilipi 1:22
   3. Kauli ya Paulo katika Wafilipi 1:25
   4. Tungo zenye utata za Wafilipi 1:26

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 1:1-2**
**1 Paulo na Timotheo, watumwa wa Kristo Yesu, kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu, walioko Filipi, pamoja na maaskofu na mashemasi. 2 Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.**

**1:1"Paulo"** Jina la Kiyunani Paulo lilimaanisha "mdogo." Baadhi ya nadharia zimekua kutokana na asili ya jina la Kiyunani.

4. Jina lililojulikana lilielezea umbile lake la mwili, karne ya pili iliweka desturi kuwa Paulo alikuwa mfupi, mnene, mwenye kipara, mwenye mategе, mwenye nyusi nyingi kama kichaka, na mwenye macho yanayotokeza njema na yawezekana ndio asili ya jina lake, akitoa katika vitabu visivyo vya kikanoni kutoka katika Thesalonika iliyoitwa *Paul and Thekla*
5. Katika mapito yake ambapo Paulo alijiita mwenyewe "mdogo kati ya watakatifu" kwasababu aliliudhi kanisa kama ilivyo katika Matendo ya Mitume 9:1-2. Wengine wameona huu "udogo" kama wenye asili ya cheo cha kujichagulia mwenyewe. Hata hivyo, katika kitabu kama Wagalatia, ambapo anahimiza uhuru wake na hali ya kuwa sawa na kumi na wawili wa Yerusalemu, hii inaweza isiwe hivyo (rejea 2 Wakorintho 11:5; 12:11; 15:10).
6. Kwa hali ya kuwa mzazi, Wayahudi waliokuwa uhamishoni (Wayahudi waliokuwa wakiishi nje ya Palestina) walikuwa wakipewa majina mawili kipindi cha kuzaliwa. Jina la Kiebrania la Paulo aliitwa Sauli na la Kiyunani aliitwa Paulo.

◙**"Timotheo"** Jina la Timotheo lilimaanaisha "aliyeheshimiwa na Mungu" au "amuheshimuye Mungu." Aliongoka kipindi cha safari ya kwanza ya Paulo ya kimishionari ya kwenda Derbe/Listra (kama vile Mdo 16:1). Paulo alimualika yeye kujiunga na kikundi chake cha umishionari katika safari yake ya pili, yawezekana kuziba nafasi ya Yohana Marko. Alikuwa na mama Myahudi (kama vile Mdo 16:1; 2 Timotheo 1:5) na baba Myunani (Mdo 16:1). (rejea Mdo 15:36-41). Paulo alimtahiri yeye ili aweze kusaidia kazi yake kati ya Wayahudi (rejea Mdo 16:3). Alikuwa mwakilishi wa Paulo mwaminifu, mwanafunzi na mkabilianaji wa ghasia (kama vile Mdo 16:1-17:14; 18:5-19:22; 20:4; Rum. 16:21; 1 Kor. 4:17; 16:10; 2 Kor. 1:1, 19; Flp 1:2; 2:19; Gal. 1:1; Filemoni. Kol. 1:4; na vitabu viwili vya I na 2 Timotheo). Paulo alimtuma mahususu kwenda Filipi kulisaidia kanisa (kama vile 19:22; Wafilipi 2: 19-24).
◙"mtumwa mwaminifu" Hii inarejerea

1. Cheo cha heshima cha Agano la Kale likihusiana na YHWH (Kama vile Kutoka. 14:31; Yoshua, Waamuzi 2:8; manabii, Ezra 9:11; Yeremia. 7:25; manabii, Dan. 9:6; Amosi 3:7; na Daudi, Zaburi 78:70)
2. Msisitizo kwa Yesu kama Bwana (*kurio*s) na waaminio kama watumwa wake (*doulos*)

◙**"Kwa Watakatifu wote"** "watakatifu" (*hagioi*), ambayo yamewekwa kando kwa ajili ya huduma ya Mungu. Hili sio rejeo kwenye maisha yasiyo na dhambi, bali ni kwa nafasi ya waamini ya kimahakama (kisheria) katika Kristo. Mara nyingi iko katika wingi ispokuwa katika Flp. 4:21, lakini hata huko inatumika katika muktadha wa kiushirikiano. Kuokolewa ni kuwa mmoja wa familia. Neno hili linaaksi matumizi ya Agano la Kale kwa ajili ya Waisrael walioko pamoja kama watu watakatifu (kama vile. Kut. 1 3:5; 1 9:5-6; Kumb. 7:6; 1Pet. 2:9; na Uf. 1 :6). Ingawa neno "watakatifu" linahusiana na msimamo wa waamini katika Kristo, sio kwa bahati mbaya kuwa mzizi wa neno ni "takatifu" (*hagios*). Waamini hawakuitiwa tu wokovu, bali pia kwenye utakaso endelevu. Waamini wamejaliwa kwenye "utakatifu" (*hagiasmos*, kama vile. Efe. 1 :4), sio tu mbinguni; kwenye huduma, marupurupu. Angalia Mdada Maalum: Watakatifu katika Kol. 1:2

◙**"katika Kristo"** Hii ni tungo ya kisarufi iitwayo kihusishi cha mahali (ya tufe). Hii ilikuwa ni njia aipendayo zaidi Paulo ya kuwaelezea Wakristo. Inazungumzia umuhimu wa mazingira yale Mkristo ayaishiyo (kama vile Mdo 17:28)! Kithiolojia inafanana na ile ya Yohana "mkikaa ndani yake" (kama vile Yohana 15).

Muundo huu mara nyingi inahusianishwa na uhusiano wa karibu wa ushirika pamoja na Kristo. Inaashiria nafasi ya kithiolojia na mwamini, na uzoevu wa jambo fulani (kama vile Rum. 3:24; 4:17; 8:39; 15:17; 1 Kor. 1:2; Gal. 2:17; Efe. 1:4,7; Flp. 1:13; 2:1,5; 4:7,13). Katika baadhi ya vifungu "katika Kristo" ni sawa kwa ukaribiano wa kisawe "katika kanisa" (kama vile Rum. 12:5; 1 Kor. 4:15; Gal. 1:22; 3:28; Efe. 3:6; Kol. 1:2). Kuelezea matumizi ya Paulo ya neno hili angalia Efe. 1:3-14: (1) katika Kristo, Flp. 1:3,10,12; (2) ndani yake/katika yeye, Flp. 1:4,7,10,13 [mara mbili]; (3) ndani ya wapendwao, Flp. 1:6.

◙**"katika Filipi"** Hii ilikuwa ni koloni la Kirumi (angalia utangulizi).

**NASB** **"waangalizi"**
**NKJV, NRSV** **"maaskofu"**
**TEV** **"viongozi wa kanisa"**
**NJB** **"wazee walioko zamu"**

Nyadhifa (1) "mchungaji," (2) "mzee," (3) "askofu," au (4) "mwangalizi" yote vinarejerea kazi ileile katika kanisa la mahali (kama vile Mdo. 20:17, 28 na Tito 1:5,7). Neno "mwangalizi" (*episkopoi*) lilikuwa na historia ya miji ya Kiyunani wakati "wazee" (*presbuteroi*) lilikuwa na historia ya Kiyahudi. Inawezekana pia kwamba "mwangalizi" pia lilikuwa na historia ya Kiyahudi kutoka katika matumizi ya Mapambo yatokanayo na matumizi ya magombo ya Bahari ya Chumvi ya *mebaqqerim* (1QS 6:11,20) . Pia angalia wingi (kama vile Mdo. 20:17; Efe. 4:21). Filipi lilikuwa na kanisa moja lililo na viongozi wengi. Hali ya kutengeneza utawala (dola) utofauti kati ya maneno haya ulisababisha baadhi ya maandiko ya Kiyunani kutofautiana katika Flp. 1:1; MSS $B^3$, $D^c$ na K mabadiliko "pamoja na (*syn*) maaskofu (*episcopois*)" ndani ya "maaskofu wenzangu" (*synepiscopois*).

**NASB, NKJV**
**NRSV, NJB** **"mashemasi"**
**TEV** **"wasaidizi"**

Hili ni neno la Kiyunani kwa nyumba za watumwa (*diakonoi*). Asili yake halisi ilikuwa ni "kuamsha vumbi kwa kusafisha." Lilikuwa ni neno la jumla kwa ajili ya huduma lililotumiwa na Yesu katika Marko 10:43-45, kwa ajili ya Mitume katika Mdo. 1:17 na kwa ajili ya karama za rohoni katika 1 Kor. 12:5. Andiko hili linaunga mkono kazi mbili za uongozi katika kanisa la mahali pamoja, japokuwa wanawake wazee (majukumu ya wajane) yanatajwa katika 1 Tim. 3:11. Maneno haya mwanzoni ilikuwa ni kazi lakini yakaja kuwa vyeo na ofisi kwa haraka(kama vile I Clement 42 na Ignatius' *Letter to Tralles*, 3:1 na *Letter to Smyrna*, 8:1). Ignatius wa Antiokia (karne ya pili mwanzoni) alianza desturi za Kikatoliki za kutumia neno "Askofu" (mwangalizi) kaka ambaye alikuwa mkubwa wa viongozi wengine wa kanisa la mahali.
Agano Jipya linaaksi muundo wote wa aina tatu wa serikali ya kanisa:
1. Mfumo wa ki-uaskofu (mitume)
2. Mfumo wa ki Kiprotestant (wazee)
3. Mfano wa kikusanyiko

Aina zote tatu zinaweza kuonekana katika baraza la Yerusalemu Mdo. 15. Muundo sio muhimu kama ukiroho wa viongozi (kama vile 1 Tim. 3:1-13)! Kule kupata na kuendelea kushikilia nguvu huwa kunaharibu mguso wake.

**1:2 "neema"** Neno hili la Kiyunani (*charis*) ni sawa na ufunguzi wa kawaida wa Kiyunani uliozoeleka "salamu" (*charein*, kama vile Yakobo 1:1). Paulo alitengeneza desturi ya ufunguzi wa kitume wa Kiyunani kuwa wa kipekee wa Kikristo. Hali ya kukosekana rejea kwa utume wa Paulo ni muhimu. Nyingi za barua hizi zinaanza kwa kuelezea mamlaka yake ya Kitume (kama vile Rum.; I na 2 Kor.; Gal.; Efe.; Kol.; I na 2 Tim. na Tito). Paulo alikuwa ana mahusiano mazuri na kanisa lake la mahali.

◙ **"na amani"** Hii inaweza ikaaksiwa na neno la Kiebrania *Shalom*. Paulo anaweza kuwa aliunganisha Kiyunani na salamu ya Kiebrania kama njia ya kutambua makundi haya mawili yaliyoko ndani ya kanisa. Baadhi wanaeleza

kuwa umuhimu wa uwiano wa Kithiolojia kwa matumizi ya Paulo ya neema kabla ya amani. Hii hakika ni kweli, lakini hii sio kauli ya kithiolojia lakini kama salamu ya ufunguzi. Angalia mada maalumu katika kol. 1:20.

◙ **"Kutoka kwa Mungu Baba Yetu"** Yesu aliwafundisha waaminio kuita YHWH kwa cheo kinachojulikana chenye ukaribu, Baba (kama vile Mt. 6:9).Hii kwa ukamilifu wake inabadilisha namna mtu anavyoutazama Uungu (kama vile Hosea 11). Dhana ya "MUNGU" inaleta vidokezo vya mpito wakati "Baba" inaongeza maelezo ya hali ya kuwako na kuendelea kuwako, hata ukaribu wa kifamilia! Angalia Mada Maalum katika Kol.1:2.

◙ **"Bwana Yesu Kristo"** Kuadhimishwa huku kikamilifu kunasisitiza Uungu wa Yesu (Bwana, kama YHWH), ubinadamu (jina lake la kibinadamu), na cheo (Masihi, Mpakwa Mafuta). Usanifu huu kamili unaunganishwa kisarufi kwa "Mungu Baba Yetu" pamoja na pendekezo moja tu kwa wote. Hii ilikuwa ni njia waandishi wa Agano Jipya waliuelezea Uungu wa Yesu na kuulinganisha. Kuna njia moja ya uwepo wa ki-Ungu lakini udhihirisho wa nafsi tatu. Angalia maelezo kamili katika Kol. 1:1 na Efe. 1:1-2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 1:3-11**
**3 Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, 4 sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala**
**zangu kwa furaha, 5 kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi.**
**6 Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya**
**Kristo Yesu; 7 vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu na katika kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, ninyi nyote**
**mmeshirikiana nami neema hii. 8 Maana Mungu ni shahidi wangu, jinsi ninavyowaonea shauku ninyi nyote**
**katika moyo wake Kristo Yesu. 9 Na hii ndiyo dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika**
**hekima na ufahamu wote; 10 mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka**
**siku ya Kristo; 11 hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.**

**1:3 "Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo,"** Hii "kumbukumbu" inaweza kurejerea kwa (1) Zawadi zao za kifedha kwa Paulo; Kihusishi cha Kiyunani "*epi*" kinaweza kuelezea kisababishi au shukrani (kama vile fasiri ya James Moffatt na Flp. 1:5, 7) au (2) ufunguzi wa kawaida wa Paulo unasisitiza kwenye neno "kumbuka," kama katika Rum. 1:8-9; Efe. 1:16; 1 The. 3:6; Filemoni 1:4.

**1:4 "siku zote niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha"** Furaha ni msisitizo unaorudiwa katika kitabu (*chara,* kama vile Flp. 1:4, 25; 2:2, 29; 4:1); "furahini" (*chairō,* kama vile Flp. 1:18; 2:17, 18, 28; 3:1; 4:4 [mara mbili],10); "furahini pamoja" (*sunchairō,* kama vile Flp. 2:17, 18). Hii inaonekana sana zaidi wakati Paulo amefungwa au yupo wakati anakabiliwa na hali ya kufa.

◙ **"ninyi nyote"** Maneno "nyote," "siku zote," na "kila" ni tabia/sifa za Wafilipi (kama vile Flp. 1:3,4,7,8,25; 2:17; 4:4,5,6,8,13,21). Zinaweza kuhusianishwa kihistoria na kithiolojia kwenye migawanyo iliyosababishwa na walimu wa uongo wa Kiyunani au hali ya kujitenga ya Wayahudi.

**1:5**
**NASB “Ushiriki wenu katika injili”**
**NKJV “ushirika wako katika injili”**
**NRSV “kushirikiana kwenu katika injili”**
**TEV “njia ambayo mlinisaidia mimi katika kazi ya injili”**
**NJB “ushirika wenu katika injili”**

Hili neno la ufunguo (*koinōnia*) lilimaanisha

1. " ushiriki wa pamoja uliomo"
2. "ushirika uliomo" (kama vile Flp. 4:15)

nahau kwa kutoa fedha (kama vile Fil. 4:15; Rum. 12:13; 15:26; 2 Kor. 9:13; Gal. 6:6; 1 Tim. 6:18), hivyo inaweza kurejerea kwa zawadi za kifedha kwenda kwa Paulo kunakofanywa na kanisa hili (kama vile Flp. 1:7; 4:10,14-18) Angalia Mada Maaluma katika Flp. 2:1.

◙ **"tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi "** Hii inafanana na Mdo. 16:12-40. Tungo hii inataka kutoa maana ya tungo iliyopita ikirejerea ushiriki wao katika huduma ya Injili kuliko zawadi zao za kifedha.

**1:6 "najawa na ujasiri"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati timilifu kutoka katika mzizi wa neno ”kushawishi,” maana yake “nilikuwa na ninaendelea kuwa na uhakika.”

◙ **"yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu"** Hii ni njeo ya kati ya wakati uliopita usio timilifu (yenye ushahidi) endelevu. Mungu (*Theos*) haliko katika maandiko lakini linakadiriwa (kama vile Rum. 8:11; Gal. 1:6, 15 na 1 The. 5:24). Ya kati inatilia mkazo ushirika wa mtendaji katika tendo linalofunuliwa katika kitenzi. Hata hivyo, muundo ni wenye ushahidi, inamaanisha kuwa kuwa neno hili halikuwa katika muundo wa utendaji wakati wa Paulo, hivyo, ya kati inaweza kufanya kazi kama irabu sauti tendaji. Lazima kuwe na uwiano wa kithiolojia kati ya pendo la kuanzia la Mungu na pendo la kuanzia la mwanadamu na mwitikio wa imani inayoendelea. Inaweza kurejerea

1. mwanzo wa kanisa
2. mwanzo wa ushiriki wao katika injili
3. mwanzo wa wokovu wao wa kibinafsi

**NASB “ataliboresha”**
**NKJV “atalikamilisha”**
**NRSV “atalikamilisha**
**TEV “atalishughulikia mpaka alikamilishe”**
**NJB “ataendelea kulikamilisha”**

Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati ujao, ambayo inaweza ikarejerea kwa uhakika wa tukio. Waaminio wanaishi katika mvutano kati ya "ule ulio tayari" na "ule ambao bado" wa ufalme wa Mungu. Faida za ufalme kamili ni kwa baadaye, wakati uraia na hadhi upo. Waaminio wanaishi kwa kupishana kwa enzi mbili za Kiyahudi. Kizazi kipya kimefika (Betlehem-Pentekoste) lakini nyakati za zamani zinabaki (asili iliyoanguka katika vyote uumbaji wa mwili na mwanadamu aliyeanguka).

◙ **"Siku ya Yesu Kristo"** Rejea ya Kuja kwa Mara ya Pili ni sehemu ya kawaida ya maneno ya ufunguzi katika barua zake (kama vile 1 Kor. 1:7, 8; 2 Kor. 1:10; Kol. 1:5; 1 The. 1:10 na 2 The. 1:4 na kuendelea).Hili tukio la siku za mwisho linatokea katika Flp. 1:6, 10; 2:16. Msisitizo wa siku za mwisho wa siku maalum ya kuja wakati wanadamu watakapokutana na Yesu Kristo (kama Mkombozi au Mtoa hukumu) inaenda kwa uteuzi kadhaa katika maandiko ya Paulo:

1. "Siku ya Bwana wetu Yesu Kristo" (kama vile 1 Kor. 1:8)
2. "Siku ya Bwana" (kama vile 1 Kor. 5:5; 1 The. 5:2; 2 The. 2:2)
3. "Siku ya Bwana Yesu" (kama vile 1 Kor. 5:5; 2 Kor. 1:14)
4. "Siku ya Yesu Kristo" (kama vile Flp. 1:6)
5. "Siku ya Kristo" (kama vile Flp 1:10; 2:16)
6. "Siku zake (Mwana wa Mungu)" (kama vile Luka 17:24)
7. "Siku ya Mwana wa Mungu kufunuliwa" (kama vile Luka 17:30)
8. "ufunuo wa Bwana Yesu Kristo" (kama vile 1 Kor. 1:7)
9. "wakati wa Bwana Yesu atafunuliwa kupitia mbingu" (kama vile 2 The. 1:7)
10. "katika uwepo wa Bwana Yesu katika ujio wake" (kama vile 1 The. 2:19)

Katika Agano la Kale waandishi waliona nyakati mbili, za uovu na nyakati ijayo ya haki, nyakati ya (Angalia Mada Maalum katika Efe. 1:21). Mungu angeingilia katika historia kupitia Masihi kuanzisha nyakati.Tukio hili lilikuwa linajulikana kama siku ya Bwana. Angalia kwamba waandishi wa Agano Jipya waliweka sifa hii kwa Kristo. Kuja kwake mara ya Kwanza, kuzaliwa kwake, kulisimuliwa kabla katika maandiko mengi ya Agano la Kale. Wayahudi hawakutarajia mtu wa ki-Ungu, muingiliano wa ki-Ungu. Kuja kote mara mbili kwa Masihi, moja kama Mtumwa Mtesekaji na mmoja kama Mtoa hukumu na Bwana, hazikuwa wazi kwa watu wa Agano la Kale.

◙ **"Yeye aliyeanzisha. . .atakamilisha"** Maneno yote "aliyeanzisha" na "kukamilisha" yalikuwa maneno ya kiufundi kwa mwanzo na mwisho wa utoaji dhabihu (kama vile Rum. 12:1-2).

**1:7**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"nimewaweka katika moyo wangu"** |
| **NRSV** | **"mnanishikilia mioyoni mwenu"** |
| **TEV** | **"mpo moyoni mwangu siku zote"** |
| **NJB** | **"mna nafasi moyoni mwangu"** |

Tungo ya Kiyunani ni yenye utata. Inaweza kurejerea kwenye upendo wa Paulo kwao (NASB, NKJV, TEV, NKJV) au upendo wao kwa Paulo (NRSV). Angalia Mada Maalum katika: Moyo katika Kol. 2:2.

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | |
| **NRSV** | **"kulinda na kuthibitishwa kwa injili"** |
| **TEV** | **"kuilinda injili na kuieneza kwa nguvu"** |
| **NJB** | **"kulinda na kuineza injili"** |

Haya yalikuwa ni maneno ya kiufundi kwa ajili ya "utetezi wa kisheria." Neno la kwanza ni *apologia* (kama vile Mdo. 22:1; 25:16; 2 Tim. 4:16), Neno la pili ni *bebaiōsis*, (kama vile Ebr. 6:16 na James Moulton na George Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament Illustrated from the Papyri and Other Non-literary Sources*, ukurasa wa. 108, ambayo inasema ilitumika "kuhakikishia kisheria"). Hii ingemaanisha kwa kutokezea kwa Paulo kabla (1) Nero au viongozi wengine wa kiserikali au (2) mahubiri yake ya Injili.

◙ **"ninyio mnaoshiriki neema hii pamoja nami"** Hii ni neno ambatani likuwa na "*syn*" na "*koinonia.*" ilionesha hisia za Paulo za umoja pamoja na waamini. Kitabu hiki kina hesabu zisizokuwa za kawaida za ambatani pamoja na "*syn,*" ambazo zilimaanisha "kwa ushirika wa pamoja na":

1. Fil. 1:7; 4:14 *syn* + ushirika (*koinonia*)
2. Fil. 1:27 *syn* + ushirikiano
3. Fil. 2:2 syn + nafsi au ufahamu
4. Fil. 2:17-18 *syn* + furahi
5. Fil. 2:25; 4:3 *syn* + mfanyakazi
6. Fil. 2:25 *syn* + askari
7. Fil. 3:10 *syn* + muundo
8. Fil. 3:17 *syn* + mwanzilishi
9. Fil. 4:3 *syn* + mfanyakazi (au jina kamili)

Miundo tofauti ya neno "ushirika pamoja na" (*koinōnia*) inatokea mara kadhaa pia (kama vile Flp. 1:5,7; 2:1; 3:10; 4:14,16). Paulo alijisikia mmoja pamoja na kanisa katika nafsi na huduma.

**1:8 "Kwa maana Mungu ni shahidi yangu"** Paulo anakula kiapo. Hii ilikuwa mbinu ya kawaida ya kuelezea ukweli wake (kama vile Rum. 1:9; 2 Kor. 1:23; 1 The. 2:5, 10).

◙ **"namna niiwatamanivyo nivyi nyote"** Paulo anatumia neno hili kufunua shauku yake kubwa ya kuwa na rafiki zake (kama vile Flp. 4:1; Rum. 1:11; 1 The. 3:6; 2 Tim. 1:4)

◙ **"pamoja na upendo wa Kristo"** KJV inafasiri tungo hii kama "bakuri za Kristo." Hii yawezekana inahusiana kwa mfanano na dhabihu ya Agano la Kale ya viungo vya ndani vya chini (ambayo wakanaani walikula) juu ya madhabahu ya dhabihu katika Hema (kama vile Kutoka 29:13; Mambo ya Walawi 3:3-4,10, 15; 4:8-9; 7:3-4; 8:16, 25; 9:10,16). Watu wa kale waligundua hisia katika sehemu ya chini ya tumbo (kama vile Isaya 63:15; Yeremia 4:19). Kwa Paulo inahusianishwa na upendo (kama vile Flp. 2:1; 2 Kor. 6:12; 7:15; Flp. 1:8,21; Kol. 3:12; FilemonI 7,12,20).

**1:9-11** Haya ni maombi ya Paulo kwa niaba ya kanisa. Mistari hii inalenga katika mtindo wa maisha wa kufanana na Kristo kwa waamini wakati Flp. 1:3-8 inalenga katika nafasi yao katika Kristo. Hii ina inaunganisha sehemu mbili ya wokovu: nafasi yetu katika Kristo (kuhesabiwaa haki na kutakaswa kinafasi) na kumiliki kwetu kwa hiyo nafasi katika hali ya kufanana na Kristo (Utakaso unaoendelea). Flp.1:9-11 ni sentensi moja kwa Kiyunani.

**MADA MAALUM: USTAHIMILIVU**

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja (tazama Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milinganyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia. Wakristo wa Mashariki walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana au kukashifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuwanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwitikio wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

1. maandiko yahusuyo uhakika
   a. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
   b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
   c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
2. maandiko yahusuyo umuhimu wa ustahimilivu
   a. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
   b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
   c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
   d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
   e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na

uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumika, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumika kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabu cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uwanafunzi. Inaelezwa katika Agano Jipya 3:5
- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote ni vya nyakati:

- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

**1:9 "upendo wenu na uzidi zaidi na zaidi"** Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo ambayo inasisitiza katika maombi yake kwamba upendo wao uendelee kukukua (kama vile 1 The. 3:12). Upendo ni ushahidi na alama ya mwamini wa kweli (kama vile 1 Kor. 13; 1 Yohana 4:7-20). Angalia Mada Maalumu: Abound (*Perisseuō*) katika Efe. 1:8.

**NASB “maarifa ya kweli na utambuzi”**
**NKJV “maarifa na utambuzi wote”**
**NRSV “maarifa na ufahamu kamili”**
**TEV “maarifa ya kweli na hukumu kamilifu”**
**NJB “maarifa na uelewa kamilifu”**

Maombi haya mawili yanajumuisha maarifa kamili ya kiroho yanayopelekea hali ya kufanana na Kristo(kama vile Kol. 1:9). Ya kwanza, *epignōksō*, mara nyingi inatumika katika Agano Jipya kwa maarifa yanayotakikana kwa ajili ya wokovu (yote ujumbe wa kweli uaminike na mtu kukaribishwa). Ya pili (*aisthēsis*) ilikuwa utendaji wake umeegamia na kusisitiza maamuzi yake ya mtindo wa maisha (kama vile Flp. 2:15). Makuzi ya Mkristo yanajumuisha viashiria vitatu vyote:

1. mafundisho yaliyo sawa (kama vile 1 Yohana 4:1-6)
2. uhusiano wa kibinafsi (kama vile Yn. 1:12; 3:16)
3. mtindo wa maisha wa kimungu (kama vile 1 Yohana 1:7; 2:6)

Inatakiwa ustahimilivu (kama vile Mt. 10:22; 24:11-13; Gal. 6:9; Ufunuo 2:7, 11, 17, 26; 3:5, 12, 21; 21:7).

**1:10 "Hivyo kwamba muweze kuthibitisha"** Hili lilikuwa ni neno la kifua vyuma (*dokimazaō*). Ililitumika kwa kujaribu uhalisia wa sarafu au vyuma halisi. Ilikuja kuwa kisawe cha "jaribio lenye mtazamo kuelekea uthibitisho" (kama vile Rum. 2:18; 1 Kor. 16:3; 1 The. 2:4). Angalia Mada Maalum: Maneno ya Kiyunani kwa kujaribu na visawe vyake katika Flp. 2:22.

**NASB, NKJV** **"vitu ambavyo ni bora"**
**NRSV, TEV** **"vilivyo bora"**
**NJB** **"utambuzi wa kweli"**

Kiuhalisia hii tungo ni "vitu ambavyo vinahesabika." Tungo ileile iko katika Rum. 2:18.

**NASB, NKJV** **"vya dhati"**
**NRSV** **"Safi"**
**TEV** **"huru kutoka katika uchafu"**
**NJB** **"bila hatia"**

Hili ni neno ambatani kutoka "mwanga wa jua" (*eilē*) na "hukumu" (*krinō*). Kiuhalisia lilimaanisha"kujaribiwa mchana kweupe." Ilikuja kuwa upanuzi wa kisitiari usiochanganywa na, hivyo, (1) tiifu (kama vile 1 Kor. 5:8; 2 Kor. 2:17; 2 Pet. 3:1) au (2) "usafi wa kimaadili" (kama vile 2 Kor. 1:12).

**NASB, NRSV** **"isiyolaumiwa"**
**NKJV** **"bila hatia"**
**TEV** **"huru kutoka….lawama"**
**NJB** **"huru na namna yoyote ya kuhukumiwa"**

Hii kiuhalisia, "bila kosa" au "kutosababisha mwingine kujikwaa" (inayofanana na 2 Kor. 8:16). Neno linamaana ya maisha bila lawama (kama vile Mdo. 24:16; 1 Kor. 10:32). Dhana hii ya lawama inarejerea kuhukumiwa kwa Agano la Kale (kama vile Mwanzo 44:10; Yoshua 2:17; Waamuzi 15:3). Hii hali ya kutokuwa na hatia inamaanishwa mara kadhaa katika Wafilipi (kama vile Flp. 2:15; 3:6). Waamini wanawajibika kwa ndugu zao katika Kristo na apia kuwa washuhudiaji wa kweli (mtindo wa maisha na vitenzi) kwa wasioamini (kama vile 1 Tim. 3:2,7.

### MADA MAAALUM: PASIPO LAWAMA, PASIPO HATIA, PASIPO KUHUKUMIWA, WALA MAWAA

E. Maelezo ya ufunguzi
   8. Hii dhana kithiolojia inaelezea asili ya mwanadamu (yaani., Mwanzo 1, bustani ya Edeni)
   9. Dhambi na uasi umekwisha haribu mazingira haya ya ushirika kamili (yaani., Mwanzo 3)
   10. Wanadamu (wa kiume na wa kike) wanatamani urejesho wa ushirika na Mungu kwa sababu wameumbwa kwa sura na mfano wake Mungu (yaani., Mwa. 1:26-27)
   11. Mungu ameshughulika na dhambi ya mwanadamu kwa njia kadhaa kwa kutumia
      d. Watu wa Mungu (yaani., Abraham, Musa, Isaya)
      e. mtindo wa utoaji dhabihu (yaani., Walawi 1-7)
      f. Mifano ya ki-Mungu (yaani., Nuhu, Ayubu)
   12. Hatimaye Mungu anamtoa Masihi
      c. Kama ufunuo kamili wake mwenyewe (kama vile Yn 1:1-14; Kol. 1:13-17; Ebr. 1:2-3)
      d. Kama dhabihu kamili kwa ajili ya dhambi (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)
   13. Wakristo waliumbwa pasipo lawama
      d. Rasmi kupitia haki ya Kristo iliyowekwa ndani yetu (kama vile. Rum. 4:3,6,8,11,22,23,24; Yakobo 2:23)
      e. Kwa mwendelezo wa kazi ya Roho (Yn 16:8-1)
      f. Lengo la Ukristo ni kufanana kama Kristo (kama vile. Rum. 8:28-30; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4;

4:13; 1 The. 3:13; 4:3; 5:23; 2 The. 2:13; Tito 2:14; 1 Pet. 1:15), ambao katika ukweli, ni urejesho wa taswira ya Mungu iliyopotea katika anguko la Adamu na Hawa.

14. Mbinguni ndio urejesho wa ushirika kamili wa Bustani ya Edeni. Mbinguni ndiko Yerusalem Mpya inayotegemewa kuja nje ya uwepo wa Mungu (kama vile Ufu.21:2) kwenye ardhi iliyotakaswa (kama vile 2 Pet. 3:10). Biblia ilianza na kuishia kwenye maudhui yale yale ya:
    d. Ushirika binafsi wa ndani na Mungu
    e. Ndani ya muundo wa bustani (Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)
    f. Kwa maelezo ya kinabii, uwepo na urafiki wa wanyama (kama vile Isa. 11:6-9)

F. Agano la Kale
5. Kuna maneno mengi ya Kiebrania ya aina tofauti ambayo yanachukua dhana nzima ya utimilifu, pasipo lawama, pasipo hatia ambayo yangalikuwa vigumu kuyataja na kuonyesha namna yahusianavyo
6. Maneno makuu yanayochukua dhana nzima ya utimilifu, kutokuwa na kosa, au kutokuwa na hatia (kutokana na Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kur. 94-99) ni:
    d. *shalom* (BDB1022, KB 1532)
    e. *thamam* (BDB1070, KB 1743)
    f. *calah* (BDB478, KB 476)
7. Tafasiri ya maandiko ya Kiyunani (yaani., Biblia ya kanisa la mwanzo) inazitafasiri dhana hizi za Kiebrania kwa maneno ya lugha ya kawaida ya Koine yaliyotumika katika Agano Jipya (angalia hapa chini)
8. Dhana muhimu imejikita kwenye mtindo wa utoaji dhabihu
    c. *amōmos* (BDB 1071, cf. Kut. 29:1; Law. 1:3,10; 3:1,6; Hes. 6:14)
    d. *amiantos* and *aspilus* pia yana vidokezo vya kimadhehebu

G. Agano Jipya
10. Dhana ya kisheria
    c. Kidokezo cha sheria cha kimadhehebu ya Kiebrania kimetafasiriwa kwa neno *amōmos* (BDB 1071, kama vile Efe 5:27; Flp. 2:15; 1 Pet. 1:19)
    d. Vidokezo vya sheria za Kiyunani (kama vile. 1 Kor. 1:8; Kol. 1:22)
11. Kristo yule asiye na dhambi, lawama, hatia (*amōmos*, kama vile. Ebr. 9:14; 1 Pet. 1:19)
12. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kumfuata Yeye (*amōmos*, kama vile. Efe. 1:4; 5:27; Flp. 2:15; Kol. 1:22; 2 Pet. 3:14; Yuda 1:24; Ufu. 14:5)
13. Dhana hii pia inatumiwa na viongozi wa kanisa
    c. *anegklētos*, "pasipo mashitaka" (kama vile. 1 Tim. 3:10; Tit. 1:6-7)
    d. *anepilemptos*, "zaidi ya shutuma" au "hapana nafsi ya lawama" (kama vile. 1 Tim. 3:2; 5:7; 6:14; Tit 2:8)
14. Dhana ya “kutokuwa najisi” (*amiantos*) imetumika kwa
    c. Kwa Kristo mwenyewe (kama vile. Ebr. 7:26)
    d. Urithi wa Wakristo (kama vile. 1 Pet. 1:4)
15. Dhana ya “ujumla” au “kusikika” *(holoklēria*) (kama vile. Mdo. 3:16; 1 The. 5:23; Yakobo 1:4)
16. Dhana ya kuwa “pasipo kosa,” “kutokuwa na hatia” linaelezewa kwa *amemptos* (kama vile. Lk 1:6; Fil. 2:15; 3:6; 1 The. 2:10; 3:13; 5:23)
17. Dhana ya “kutokuwa kwenye lamama” linaelezewa kwa *amōmētos* (kama vile. 2 Pet. 3:14)
18. Dhana ya “kuwa safi,” “pasipo doa” mara nyingi zimetumika katika sura zenye moja ya maneno ya hapo juu (kama vile. 1 Tim. 6:14; Yakobo 1:27; 1 Pet. 1:19; 2 Pet. 3:14)

H. Idadi ya maneno katika Kiebrania na Kiyunani yanayoelezea dhana hii yanaonyesha umuhimu wake. Mungu ametupatia mahitaji yetu kupitia Kristo na sasa anatuita kuwa kama Yeye.

Waamini kihali, kihukumu wametangazwa kuwa “sawa” “wenye haki” “wasio na lawama” kwa kazi ya Kristo. Sasa waamini wanatakiwa kumiliki nafasi yao. “Tembeeni katika nuru kama Yeye alivyo nuruni” (kama vile. 1 Yn 1:7). “tembeeni kwa thamani ya mwito wenu" (kama vile. Efe. 4:1,17; 5:2,15). Yesu ameirejesha taswira ya Mungu. Ushirika wa ndani sasa ni dhahiri, lakini kumbukeni Mungu anahitaji watu wanaoaksi tabia yake, kama Mwana

wake alivyofanya, kwa ulimwengu uliopotea (yaani., mataifa). Hatukuitiwa chochote bali utakatifu (kama vile. Mt. 5:20,48; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:13-16). Utakatifu wa Mungu, sio tu kisheria, bali namna uishivyo!

◙ **"mpaka siku ya Kristo"** Angalia Mada Maalum: Maneno ya Agano Jipya kwa ajili ya Kurudi kwa Kristo katika Kol. 3:4.

**1:11 "mkisha kujazwa"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Dhana ya"kujazwa" inaunganishwa na nguvu ya Mungu, Roho (kama vile Efe. 5:18). Anazalisha hali ya kufanana na Kristo katika wote wamwaminio na kushirikiana pamoja naye, ambalo ndio kusudio la wokovu(kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"tunda la haki"** |
| **NKJV** | **"matunda ya haki"** |
| **NRSV** | **"mavuno ya haki"** |
| **TEV** | **"sifa nzuri ya kweli"** |
| **NJB** | **"matunda ya uelekevu"** |

Tazama neno "tunda" ni umoja, kama lilivyo katika Gal. 5:22, ambapo tunda la Roho ni upendo. Hapa tunda ni haki. Neno "haki" katika maandiko ya Paulo mara nyingi linalenga msimamo wa waamini wa kisheria (nafasi ya kuhesabiwa haki na kutakaswa, angalia Mada Maalum: Utakaso katika Efe. 1:1) mbele za Mungu (kama vile Warumi 4-8). Hapa, hata hivyo, inamaanisha kuufanyia kazi kivitendo wokovu wa ndani (utakaso endelevu, kama vile Fil. 1:10; Yakobo 3:18). Angalia Mada Maalum: Haki katika Efe. 4:24.

◙ **"Kwa sifa na utukufu wa Mungu"** (kama vile Mt. 5:16; Efe. 1:6, 12, 14). Maisha ya Wakristo yanahitaji kuleta heshima kwa Mungu! Kuhesabiwa haki lazima kuzalishe utakaso. Hakuna tunda, hakuna mzizi! Kristo amefanya vyote kutuokoa na kuturejesha katika sura ya Mungu katika uanadamu ulioanguka. Waaminio lazima waoneshe tabia za kifamilia za Mungu! Angalia maelezo juu ya "utukufu" katika Efe. 1:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 1:12-18**
**[12] Lakini, ndugu zangu, nataka mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuieneza Injili; [13]**
**hata vifungo vyangu vimekuwa dhahiri katika Kristo, miongoni mwa askari, na kwa wengine wote pia. [14] Na**
**wengi wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kunena neno la Mungu pasipo hofu. [15] Wengine wanahubiri habari za Kristo kwa sababu ya**
**husuda na fitina; na wengine kwa nia njema. [16] Hawa wanamhubiri kwa pendo, wakijua ya kuwa nimewekwa**
**ili niitetee Injili; [17] bali wengine wanamhubiri Kristo kwa fitina, wala si kwa moyo mweupe, wakidhani**
**kuongeza dhiki za kufungwa kwangu. [18] Yadhuru nini? Lakini kwa njia zote, ikiwa ni kwa hila, au ikiwa ni kwa**
**kweli, Kristo anahubiriwa; na kwa hiyo nafurahi, naam, nami nitafurahi.**

**1:12 "sasa nataka mjue"** Hii inamaanisha kuwa kanisa lilikuwa limeuliza maswali kadhaa (kama la Korintho, kama vile 1 Kor. 7:1, 25; 8:1; 12:1; 16:1) kupitia Epafrodito ambaye alikuwa ameleta zawadi za kifedha kwake alipokuwa gerezani (kama vile Flp. 2:25).

◙**"kwamba katika mazingira yangu"** Hii inamaanisha kukamatwa kwa Paulo na kufungwa, na hukumu(s). Nabii Agabo alikuwa ametabiri kukamatwa kwa Paulo na kufungwa kwake in Mdo. 21:10 na kuendelea. Ukweli kwamba Paulo angezungumza mbele ya wafalme wa Mataifa ulifunuliwa kwa Anania katika Mdo. 9:15. Mungu alikamilisha kusudi lake alilolitaja kwa huduma ya Paulo, ila katika namna ambao kiuhalisia kwa wakati huo Paulo hakuwahi kuifikiria kabla. Ukweli huu huu ni ushahidi katika maisha ya waaminio. Hawaongozwi na kutawaliwa na bahati, nafasi au majaliwa. Mungu anatumia hata vitu vinavyoonekana havina heshima na vilivyokataliwa katika namna ya ajabu kwa jaili ya heshima yake na utukufu (kama vile Flp. 1:20; Rum. 8:28-29).

◙ **"yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuieneza Injili"** Neno "kuendelea" linatumika tena katika Flp. 1:25 na katika 1 Tim. 4:15. Kwa kuanzia lilikuwa na asili ya historia mbili ambayo inafafanana na matumizi ya Paulo ya neno:

1. Lilikuwa ni neno la kijeshi kwa ajili ya kusogea kwa vikosi kupitia miinuko yenye mashimo mashimo
2. lilitumika na wanafalsafa wa Kiyunani (wastoiki) kama neno la kutazama kwa ugumu wa njia kwenda kwenye hakima.

Licha ya kuwa injili iliendelea, saa nyingine inakuwa ngumu. Inafurahisha kujua kwamba maendeleo yanayotajwa ni dhahiri.

1. katika Flp. 1:13 kama ambavyo injili inaenezwa kupitia mlinzi wa kifalme na jumba la kirumi lenyewe
2. katika Flp. 1:14 kwamba wahubiri wengine wa Kikristo katika Rumi walikuwa wanapata ujasiri kutokana na mtazamo na matendo ya kuihubiri injili wakati Paulo mwenyewe akiwa gerezani

**NASB** **"mlinzi wa Mfalme"**
**NKJV** **"mlinzi wa ikulu"**
**NRSV** **"mlinzi wa kifalme"**
**TEV** **"ulinzi mzima wa ikulu yote"**
**NJB** **"kifalme"**

Matoleo ya fasiri ya KJV, NKJV, na TEV yana neno "jumba la kifalme," ambalo linawezekana kwasababu neno linatumika katika njia hii katika Mdo. 23:35. Katika muktadha huu inarejerea kwa mwili wa wanajeshi, sio sehemu, kwasababu ya matumizi ya tungo, "na mapumziko yote," ambayo kiuhalisia inamaanisha mtu. Utambulisho wa watu hawa kwa uhakika haujulikani, lakini yawezekana walikuwa watumwa wa kifalme, washauri wa kisheria, au watumishi wa mahakamani ambao walikuwa wanahusishwa katika shauri la kisheria la Paulo.

## MADA MAALUM: MLINZI WA MFALME

Kwa asili yake neno, "praetoria," linahusu hema la majeshi ya Kirumi ("hakimu"), lakini baada ya kipindi cha kuangushwa kwa mtawala wa Rumi lilitumika katika dhana ya utawala kuonesha makao makuu ama maskani ya siasa (kama vile. Mt. 27:27; Yohana 18:28,33; 19:9; Matendo 23:35; Flp. 1:13).

Hata hivyo kwenye ulimwengu wa kirumi wa karne ya kwanza lilitumika kwa watumishi ambao waliunda kikosi maalumu cha ulinzi wa ufalme. Kundi hili la maaskari waliopewa heshima maalumu lilianziswha na Augustino (27 b.c.) lakini mwishowe lilitiwa mkazo katika Rumi na Tiberia.

1. Kuwa wenye cheo kimoja, kamanda wa karne
2. pokea mshahara mara mbili ya kiwango
3. kuwa na upendeleo maalumu (yaani, walistaajabu baada ya miaka 16 badala ya miaka 25)
4. kuwa wenye nguvu kiasi kwamba uchaguzi wao kwa amiri jeshi mkuu wa ufalme wa Rumi aliyeheshimiwa

Ulipofika muda wa Konstantine ndipo kikundi hiki kilichokuwa kimepewa heshima maalumu chenye nguvu kisiasa mwishowe kilivunjika

**1:14** Tungo ya Kiyunani "katika Bwana" inaweza kwenda na "ndugu" au pamoja na neno "ujasiri zaidi" kuelezea msingi wa ujasiri wa wahubiri wengine katika kumuangalia namna Paulo alivyokuwa akikabiliana na kifungo. Ni muhimu kuweka angalizo kuwa hali ya mtu binafsi ya kutojidharau na mtazamo na matendo wakati wa msongo wa mawazo na nyakati ngumu mara nyingi ni chanzo cha kutia moyo wakristo wengine (kama vile Ayubu, Yeremia, Paulo).

◙ **"kuzungumza neno la Mungu bila hofu"** Tungo "neno la Mungu" kutofautiana kwa baadhi ya maandiko ya Kiyunani. Maandiko ya kale ya Kiyunani, א, A, B, na P yana tungo milikishi"neno la Mungu." Hata hivyo, katika $P^{46}$,

D$^{C}$, na K, tungo milikishi imeondolewa. Toleo la UBS$^{4}$ linatoa ondoleo alama "B" (uhakika karibia). Kama ilivyo kweli juu ya utofautiano uliopo kwenyeMaandiko mengi, yana athiri namna ya kifungu cha habari kidogo sana.

**1:15** Utambulisho wa wahubiri hawa wa Kikristo wenye wivu (kama vile Flp. 1:15,17,18) umesababisha mjadala mkubwa katika ya wafasiri. Inaonekana wazi kutoka Flp. 1:11-18 kwamba walikuwa wakimuhubiri kweli Yesu, lakini kutokana na nia zao mbaya ambazo kimsingi zilikuwa zimeelekezwa kwa Yesu na ujumbe wa injili lakini kuelekeza Paulo kiuhalisia.Baadhi wanaelezea kwamba hawa ni viongozi walioanzishwa (Kiyahudi na Mataifa) waliofikiwa na akili na uwepo wa kiroho wakati wa kuja kwake Rumi. Yawezekana walikuwa wale wenye kushika sheria na taratibu za Kiyahudi kama kule Galatia lakini wakiwa na maumivu kidogo. Hatahivyo, kwasababu ya maneno makali ya Paulo kwa wagalatia (3:2 na kuendelea), Haielekei kuwa kweli kwamba andiko hili linamaanisha walimu wa uongo. Hapa ni wahubiri walio na nia dhaifu. Hii inaonekana kama siku zetu-wivu, uhasama na ushiriano mara nyingi inafanya tabia za kanisa la Yesu Kristo, badala ya upendo na kukubaliwa ambavyo vinatakikana katika 1 Kor. 13; Rum. 14; Gal. 5:26.

**1:16**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **“nimeteuliwa”** |
| **NRSV** | **“nimewekwa hapa kwa”** |
| **TEV** | **“Mungu amenipa kazi ya”** |
| **NJB** | **“naendelea imara”** |

Neno "kuteuliwa" (*keimai*) lilikuwa neno la kijeshi kwa ajili ya wanajeshi kuwa katika zamu yao. Linatumika kisitiari kwa anayechaguliwa kufanya jukumu (kama vile Luka 2:34). Kufungwa kwa Paulo na shauri katika Rumi hakukuwa kwa ajali, lakini haukuwa mpango ulioamriwa kabla na Mungu (kama vile Mdo. 9:15). Maisha ya Yesu pia ya "kuteuliwa" (kama vile Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28). Inasaidia kuona maisha yetu katika mtazamo ule ule wa kithiolojia!

◙ **"kuitetea injili"** Hili ni neno lile lile la Kiyunani (*apologia*) linalotumika katika Flp. 1:7. Kutokana na hili tunapata neno la Kiingereza"kukiri kosa" ambalo linamaanisha "kujitetea kisheria." Tungo hii lingemaanisha shauri la kiserikali (kama vile Mdo. 22:1) lakini lingemaanisha pia mahubiri yake ya Kiyahudi katika Sinagogi.

**1:16-17** Ni ajabu kugundua kwamba katika upokeaji wa maandiko tungo katika Flp. 1:16 na 17 inageuzwa katika juhudi yakutaka kufananisha mpangilio wa mstari wa 15. Huu utofautiano wa maandiko ya Kiyunani (kama ilivyo kwa wingi wake) haiathiri namna ya kifungu cha habari.

**1:17 "nia za ubinafsi"** Hili neno kwa asili lilimaanisha "kuzungushia sufi kwa ajili ya kukodi," lakini ilikuja kutumika katika namna ya tabaka la majivuno ya wale wenye maisha ya hadhi dhidi ya watu waliokuwa wakifanya kazi kwa ajili ya kuishi. Lilikuja kutumika kisitiari kwa ajili ya nia za ubinafsi. Ukuu wa moyo wa Paulo unaweza kuonekana (Flp. 1:18) katika ukweli kwamba alifurahia kwamba Kristo alikuwa akihubiriwa hata kama mtangaza habari hizi alikuwa ana nia mbaya. Nguvu iko katika Neno, sio kwa Muhubiri!

**1:18** Paulo alielewa kwamba ujumbe wa injili ulichukua nafasi ya uhasama. Mstari huu ulikuwa na kumaanisha kwa ajabu kwa mgawanyo wa kidhehebu ambao unapatikana katika kanisa leo na namna waamini wanavyojifananisha wao kibinafsi na kithiolojia (kama vile Warumi 14 and 1 Wakorintho 8-10).

◙ **"katika kweli"** Angalia Mada Maalum: Kweli katika maandiko ya Paulo katika Efe. 1:13.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 1: 19-26**

**19 Maana najua ya kuwa haya yatanigeukia kuwa wokovu wangu, kwa sababu ya kuomba kwenu, na kuruzukiwa Roho wa Yesu Kristo; 20 kama vile nilivyotazamia sana, na kutumaini, kwamba sitaaibika kamwe, bali kwa uthabiti wote, kama sikuzote na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa**

**kwa maisha yangu, au ikiwa kwa mauti yangu. [21] Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida. [22] Ila ikiwa kuishi katika mwili, kwangu mimi ni matunda ya kazi; basi nitakalolichagua silitambui. [23] Ninasongwa katikati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vizuri zaidi sana; [24] bali kudumu katika mwili kwahitajiwa zaidi kwa ajili yenu. [25] Nami nikitumaini hayo, najua ya kuwa nitakaa na kudumu pamoja nanyi, ili mpate kuendelea na kufurahi katika imani; [26] hata mzidi kuona fahari katika Kristo Yesu juu yangu kwa sababu ya kuwapo kwangu pamoja nanyi tena.**

**1:19 "wokovu wangu "** Kiuhalisia neno (*sōtēria*) lilimaanisha "wokovu." Paulo mara nyingi alilitumia kuzungumzia wokovu wa kiroho katika Kristo. (baadhi ya mifano: Rum. 1:16; 11:14; 1 Kor. 1:21; 7:6; 1 Tim. 4:16; 2 Tim. 2:10; 3:15; 4:18; Tito 3:5.) Hatahivyo, hapa analitumia katika namna ya ukombozi wa mwilini wa Agano la Kale (kama vile 2 Tim. 4:18; Yakobo 5:15). Lilitumika mara nyingi katika namna ya muktadha unaohusiana na shauri la mahakamani (kama vile Marko 13:11; Luka 12:11-12). Inawezekana pia kwamba ni maelezo kwa Ayubu 13:16 katika Tafsiri ya Agano la Kale (LXX), ambayo mwishowe Ayubu alilipiwa kisasi na Mungu (kama vile Ayubu 42).

Paulo alijisikia kuwa alikuwa anakwenda kufunguliwa (kama vile sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti Flp. 1:22). Inaonekana kuwa Wakolosai na Waefeso walikuwa wameandikiwa kabla wakati wa kipindi cha kufungwa kwa Paulo kuelekea mwisho. Paulo alifunguliwa na kufanya safari ya nne ya kimishionari ambayo ilifunuuliwa katika barua zake za kichungaji (1 Timotheo, Tito na 2 Timotheo) na alafu akakamatwa tena na kushikiliwa kabla ya kujiua kwa Nero mwaka 68 A. D.

Ujasiri wa Paulo uko katika namna mbili: (1) maombi ya Wakristo wa Kifilipi na (2) nguvu ya Roho wa Mungu. Inashangaza kujua mara ngapi Paulo aliomba kuombewa kutoka katika makanisa (kama vile Rum. 15:30; 2 Kor. 1:11; Efe. 6:18-19; Kol. 4:3; 1 The. 5:25). Hii ni siri kuhusiana na maombi ya kusihi; Mungu mwenyewe amejiwekea mpaka na kiwango cha maombi ya watoto wake(kama vile Mt. 7:7-11; 18:19; 21:22; Luka 11:9-13; Yohana 14:13-14; 15:7,16; 16:23-24; 1 Yohana 3:22; 5:14-15). Kwa namna fulani, kwa dhati, maombezi yenye bidii yanaachilia nguvu ya Roho katika namna isiyokuwa ya kawaida; "hata sasa hatujapata kwakuwa hatuombi" (kama vile Yakobo 4:2).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kutoshelezwa"** |
| **NKJV** | **"kusambaza"** |
| **NRSV, TEV** | **"kusaidiwa"** |
| **NJB** | **"msaada"** |

Neno hili kwa uhalisia na kwa asili linatumika juu ya mtu mwenye mali kama mlezi wa kuitegemeza kwaya. Lilikuja kutumika kisitiari kwa kutoshelezwa kuliko kamili na kukidhiwa kuliko tele.

◙ **"Ya Roho ya Yesu Kristo"** Mara kadhaa Roho Mtakatifu anaelezwa kwa namna ya uhusiano kwa Yesu (kama vile Rum. 8:9; 1 Kor. 15:45; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:6; na 1 Pet. 1:11). Cheo cha Roho kilichotolewa na G. Campbell Morgan kilikuwa ni "Yesu mwingine"! Hii kwa hakika iko sambamba katika mstari na kusudi la Roho mtakatifu linalotajwa katika Yohana 16:7- 15. Huduma ya msingi ya Roho mtakatifu ni kuwaleta wanadamu katika kuvuvia, kufunua kwao injili inayopatikana katika mtu na kazi ya Yesu Kristo, kuwabatiza katika Kristo na alafu kuwaumbia Kristo ndani yao. Kule Paulo kuunganisha kwa Yesu na Roho kulikuwa ni kutuonesha kwamba Wakati au Enzi mpya ilikuwa imekwisha kuja. Ilikuwa ni "kipindi cha Roho." Roho alileta kwetu katika enzi mpya ya haki. Lakini bado Nyakati mpya pia ilikuwa ni ya kimasihi. Yesu alikuwa chombo cha Baba cha kuanzisha enzi mpya ya Roho. Angalia Mada Maalum: Yesu na Roho katika Kol. 1:26 na Hulka ya Roho Efe. 1:14.

**1:20 "kama vile nilivyotazamia sana "** Neno hili linaweza likawa liliundwa na Paulo na pia linatumika katika Rum. 8:19. Ni sitiari ya mtu Fulani mwenye shingo ndefu iliyotokeza anayetazama kwaumakini akimuangalia mtu au kitu.

**NASB "kwamba sitaaibishwa katika chochote"**
**NKJV "kwamba katika chochote sitaaibishwa"**
**NRSV "kwamba sitaabishwa katika kwa namna yoyote"**
**TEV "kwamba sitafeli katika zamu zangu"**
**NJB "kwamba sitakuja kukiri kushindwa"**

Hii inaashiria hali ya Paulo ya uwajibikaji katika majukumu aliyopewa lakini pia kwa kutambua magumu na majaribu (kama vile 1 Kor. 4:1-29; 9:27).

**NASB, NKJV**
**NRSV "kwa ujasiri wote"**
**TEV "ukijaa ujasiri"**
**NJB "kutoogopa kikamilifu"**

Neno hili la Kiyunani lina maana ya msingi ya "ujasiri wa kunena" (1) katika uwepo wa Mkuu (Mungu, Hakimu, Mfalme, n.k.) au (2) katika hali nzito (kama vile Mdo. 4:13, 29, 31; Efe. 3:12; 1 Tim. 3:13; Ebr. 10:9; 1 Yohana 4:17). Haya yalikuwa maombi ya kujirudia rudia ya Paulo (kama vile Efe. 6:19; Kol. 4:3). Angalia Mada Maalum: Ujasiri (*Parrhēsia*) katika Kol. 2:15.

**NASB "Kristo hata sasa kama siku zote atainuliwa katika mwili wangu"**
**NKJV "kama siku zote kwa hiyo sasa pia Kristo atatukuzwa katika mwili wangu"**
**NRSV "Kristo atainuliwa hata sasa kama siku zote katika mwili wangu"**
**TEV "kwa utu wangu wote nitaleta heshima kwa Kristo"**
**NJB "hivyo kwa sasa kama siku zote Kristo atatukuzwa katika mwili wangu"**

Hiki ni kitenzi tendwa cha wakati ujao kinachoonesha kwamba Paulo hakuwa muhusika mkuu au kichocheo cha Mungu kuheshimiwa, lakini kwamba Kristo ataheshimiwa kupitia Paulo kwa namna ya maombi ya ndugu na nguvu ya Roho Mtakatifu (Fil. 1:19) Ni muhimu kwamba Paulo anafunga tungo hii kwa neno la Kiyunani kwa ajili ya "mwili." Waaminio watamheshimu Mungu kwa miili yao (kama vile 1 Kor. 6:20) au hawata muheshimu Mungu kabisa! Kwa Wayunani mwili ulikuwa muovu. Kwa Paulo kimaadili ilikuwa haijaegemea sehemu yoyote lakini ilikuwa na uwanja wa majaribu na sehemu kwa kumuheshimu na kumtukuza Kristo.

◙ **"hata iwe kwa kuishi ama kwa kufa"** Waaminio lazima wamtukuze Kristo, baadhi kwa vifo vyao na baadhi kwa maisha yao ya uaminifu (kama vile Rum. 14:8; 2 Kor. 5:1-10; 1 The. 5:20; Ufunuo 13:14).

**1:21 "kwangu kuishi ni Kristo na kufa ni faida"** "kuishi" ni kauli tendaji ya wakati uliopo usio na ukomo, wakati "kufa" ni kauli tendaji ya wakati usiotimilifu usio na kikomo. Hii ina maana kwamba kitendo cha kuendelea kuishi ni Kristo (Rum. 12:1-2). Hii ni tungo ngumu kuielewa, lakini tunapoangalia maandiko mengine ya Paulo, tunaona kwamba ilimaanisha kuwa waaminio ni wafu kwa dhambi, wafu kwao wenyewe binafsi, na wafu kwa sheria, lakini hai kwa Mungu kwa ajili ya huduma (kama vile Rum. 6:1-11; Kol. 3:4; Gal. 2:20; 5:24; 6:14). Hata hivyo, katika muktadha huu, lazima ilimaanisha kifo cha mwili. Paulo alikuwa anajaribiwa kwa maisha yake, japo maisha yake yalikuwa yalikwisha twaliwa tayari, yalitwaliwa na Kristo!

◙ **"kufa ni faida "** Kwa Paulo, kifo kilimaanisha ushirika mkamilifu pamoja na Mungu (kama vile Flp. 1:23). Hii haina maana kwamba Paulo alikuwa hakuwa na woga kabisa juu ya kifo. Alizungumza juu ya hofu yake na vitu anavyoviwaza katika 2 Kor. 5:1-10. Kuna chembechembe ya hofu kwa habari ya kifo kwetu sisi sote, lakini injili inawasaidia waaminio kukabiliana kwa ujasiri na kifo cha mwili na Mungu mtakatifu. Hata hivyo lazima tuelewe kuwa neno "faida" hapa halimaanishi faida ya kibinafsi ya mali kwa Paulo lakini faida za kiinjili (kama vile Flp. 1:12).

**1:22 "ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti.

◙ **"katika mwili"** Angalia Mada Maalum katika Kol. 1:22.

◙ **"Hii ingemaanisha kufanya kazi kwenye matunda kwa ajili yenu"** Hii imefasiriwa katika namna mbili: (1) Baadhi wanaiyona kama kuzaliwa na kuendelezwa kwa kazi ambayo ilikuwa tayari imekwisha aanza (2) wengine wanaitazama kama shauku ya kazi mpya. Kuna ushahidi wa kutosha katika kanisa ka kwanza kwamba Paulo alikuwa ameachiliwa kutoka katika gereza na alikuwa na miezi michache ya vishughuli vya kimishionari kabla hajakamatwa tena na kushikiliwa katika miaka ya 68 B.K., ambayo ni mwaka ambao Nero mwenyewe alijiua. Ushahidi unaonekana kama ifuatavyo:

1. Matumizi ya neno "ukombozi" katika Flp. 1:19
2. Sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti katika Flp. 1:22
3. Nyaraka za kichungaji hazifanani na mfuatano wa Matendo ya Mitume
4. Clement wa Rumi, katika barua yake ya kwanza kwa Wakorintho (95 B.K), hasa katika Sura ya 5, inasema kwamba Paulo aliachiliwa kutoka katika gereza na kuelekea kwenye vifungo vya magharibi
5. inaelezewa katika barua za utangulizi wa Paulo katika vipengele na visehemu vya Murato
6. inaelezewa katika toleo la Eusebius liitwalo *Ecclesiastical Histories*, 2:22
7. inaelezewa katika mahubiri ya Chrysostom, ambayo yanatajwa shughuli za mwisho mwisho alizokuwa akifanya

◙ **"hata cha kuchagua sitambui"** Hili neno siku zote linamaanisha "kutangaza." Paulo kwa hakika hakuwa na chaguzi kuhusu maisha yake au kufa kwake, lakini anaelezea kwamba Mungu ndiye aliyefanya hivyo. Hata hivyo alikuwa anashughulika kisaikolojia katika ya chaguzi mbili: (1) moja ingekuwa na faida kwake, yaani kifo cha mfiadini au (2) kuachiliwa kwake kungekuwa na faida kwa kanisa kwasababu angekuwa na muda mwingi wa kuhubiri, kufundisha na kutia moyo.

**1:23 "ninasongwa songwa sana katika kila *uelekeo*"** Neno *sunechō* linamaanisha "kusongwa au kushikiliwa pamoja" (kama vile Luka 12:50; 19:43) na inaonesha mashindano makali sana ya kibinafsi ambayo Paulo aliyasikia yakihusishwa na chaguzi za huduma yake.

◙ **"Natamani kuondoka"** Neno "shauku" ni neno la kiyunani lenye nguvu sana mara nyingi likifasiriwa kama "tamaa," lakini hapa linatumika katika namna chanya ya shauku kali. Neno "ondoka" neno la Kiyunani la uzuri wa namna yake linalomaanisha meli kuachiliwa kutoka inapokuwa imefungwa bandarini au kwa ajili ya maskani ya kijeshi kuangusha na kuhamishwa (kama vile 2 Tim. 4:6). Kwasababu ya matumizi ya Paulo ya neno hili katika 2 Kor. 5:1,11, yawezekana inamaanisha kifo cha mwili.

◙ **"na kuwa pamoja na Kristo"** Mafarisayo walikuwa siku zote wakitegemea ufufuo wa siku za mwisho, (kama vile Ayubu 14:14-15; 19:25-27; Dan. 12:2). Hii ni ushahidi kutoka katika vifungu vingi vya Agano Jipya ambavyo vinarejerea kuja kwa mara ya Pili, hukumu na maisha ya baadaye. Hata hivyo, katika kifungu hiki cha habari maarifa yaliyoongezeka yanaletwa katika dhana ya desturi ya Kiyahudi *Hades*k*:* wakati mwamini anapokufa, hawaingii katika kulala kusiko na fahamu au kushuka katika sehemu ambazo zinashikiria ufahamu nusu, lakini wanakuwa pamoja na Bwana (kama vile Marko 12:26-27; Luka 16:19-31; 23:43; 2 Kor. 5:8). Kuna utata mkubwa sana wa kibiblia katika eneo hili. Biblia inaonesha kufundisha hali ya ufahamu wa kati, hali ya kutokuwa na mwili (Kama vile 1 Kor. 15:51-52; 1 The. 4:13, 17; Ufunuo 6:9; 20:4). Katika vifo waaminio watakuwa pamoja na Bwana lakini katika ushirika ulio na kikomo na ushirika huu hautafikia kilele kwa ukamilifu mpaka Siku ya Ufufuo (kama vile 1 Yohana 3:2).

**MADA MAALUM:WAFU WAKO WAPI?**

I. Agano la Kale

A. Watu wote wanakwenda shimoni(sheol) (hakuna mizizi yenye chanzo kimoja cha neno na asili ya neno

lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)

B. Tabia za shimoni (sheol)
1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), kumb.32:22
2. Gereza lenye vizuizi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
7. panahusiana na *utelekezaj*i (maangamizo; angalia Mada Maalumu: *Kutelekezwa*. . .*Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
8. panahusiana na “shimo lefu” (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
9. waovu hushuka ndani ya shimo la sheol,Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5
11. kule watu huitwa *Repha'im* (yaani., "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11

II. Agano Jipya
A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usio onekana)
B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheo*l)
1. Anarejerea mauti, Mt. 16:18
2. imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14
3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (Gehenna), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Luk 10:15; 16:23-24
4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Luk 16:23
C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)
1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Luk 23:43
2. Sehemu ya waovu iitwayo “kwenye vifungo vya giza”,iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa “shimoni” Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3
D. Gehenna
1. inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, “bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalem). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YWHW (Kama vile Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.
3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza,kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna
a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk 9:43
b. Mahali pa milele, Mk 9:48 (Mt. 25:46)
c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28

d. panafanana na Sheol, Mt. 5:29-30; 18:9
e. Panaainisha waovu kama “wana wa Jehanamu” Mt. 23:15
f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
g. Dhana ya Gehenna inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8).Yawezekana ziwa la moto pakawa ndo mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimoni, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimoni, kama vile Luk 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).
h. ilikuwa haikusanifiwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41

E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimoni (sheol), kuzimu(hades) na Jehanamu(Gehenna) kuwa
1. kiasili watu wote walikwenda shimoni/kuzimu
2. uzoefu wao wa (mema/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezewa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawezi kutengeneza andiko juu ya mfano.

III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

F. Agano jipya halifundishi juu ya “zinaa ya nafsi,” ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa
1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili
3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla

G. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo
1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
2. Abraham angeweza tayari kuwa na mwili, Mk 12:26-27; Luk 16:23
3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mipya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
6. Paulo anadai kuwa waumini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

IV. Mbinguni

A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.
1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Heb. 4:14; 7:26
3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Heb. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)

B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).

C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msemo(mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafahamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia
   A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*
   B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

◙ **"kwakuwa hilo ndilo bora zaidi"** Huu ni mfuatano wa kauli linganifu za vitu viwili kwa mara tatu ambazo zinaonesha

**1:25** Hii ilimaanisha kluwa Paulo alitegemea kuachiliwa.

◙ **"kwa ajili ya kuendelea kwenu na furaha katika imani"** Flp. 1:25-26 inaunda sentensi moja ya kiyunani. Ikiwa ni kweli kwamba neno "maendeleo" (kama vile 1 Tim. 4:15) inamaanisha ugumu wa safari, hivyo umuhimu wa wa neno "furaha," hivyo tabia za vitabu hivyo, inaunganishwa na ugumu wa maisha ya mkristo. Kutoka katika vifungu vingine vya Agano Jipya vinakuwa wazi kwamba tabia ya kipekee ya Mkristo ni furaha katika kati ya shida nyingi katika matatizo ya mwili na dhiki (kama vile Mt. 5:10-12; Rum. 5:3; 8:18; 1 The. 5:16; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 4:12-16)
**1:26**
**NASB “ujasiri wenu mnaojivunia ndani yenu ijawe katika Kristo Yesu”**
**NKJV “furaha yenu kwangu iwe tele katika Yesu Kristo”**
**NRSV “kwamba niweze kuwashirikisha kwa wingi kujivunia kwenu katika Kristo Yesu”**
**TEV “nitakapokuwa nanyi tena, mtakuwa na sababu hata zaidi ya kujivunia mimi katika maisha yenu katika umoja katika Kristo Yesu”**
**NJB “ili kwamba kurudi kwangu kwenu muongezeke katika kufurika kwa katika Yesu Kristo katika hesabu yangu”**

Tungo hii ina vitu viwili: (1) Kristo au (2) Paulo. Je walikuwa wakifurahi katika Kristo na injili au katika kurudi kwa Paulo na huduma katikati yao? Muktadha unaunga mkono hiki cha pili. Huduma ya Paulo ingemtukuza Kristo. Angalia Mada Maalum: Kutoshelezwa (*Perisseuō*) katika Efe. 1:8.

## MASWALI YA MJADALA KWA 1:1-26

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.
Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Waangalizi na mashemasi ni watu aina gani? Walikuwa na majukumu gani?
2. Kwanini kanisa hili lilikuwa la kipekee sana kwa Paulo?
3. Kwanini mstari wa 6 ni muhimu? Unafanana vipi na mstari wa 5 na kumi?
4. Orodhesha ambavyo Paulo analiombea kanisa.
5. Je ni namna gani kufungwa kwa Paulo kungeweza kusaidia kueneza Injili?
6. Je ni vitu gani vinawatambulisha wahubiri wa Kikristo wanaohubiri wivu, ugomvi ufuasi wa kikundi ama chama?
7. Kwa nini mstari wa 18 ni muhimu sana katika namna ya kushughulikia mambo ya kidhehebu siku za leo?
8. Kwanini Roho Mtakatifu anaitwa Roho wa Yesu Kristo? Kuna umuhimu gani wa mabadilishano haya?
9. Je Paulo ana maanisha nini anaposema “kuishi ni Kristo na kufa ni faida”? je hii inafanyaje kazi katika maisha ya leo ya kila siku. Na katika mtazamo wa kiulimwengu wa Wakristo?
10. Nini kinatokea kwa Wakristo wanapokufa?
11. Kwa namna gani matatizo na furaha vinafanana na uzoefu wa Wakristo?

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 1:27-30**
**27 Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili, nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikie mambo yenu, kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili; 28 wala hamwaogopi adui zenu, katika neno lo lote; kwao hao ni ishara mathubuti ya kupotea, bali kwenu ninyi ni ishara ya wokovu, huo utokao kwa Mungu. 29 Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake; 30 mkiwa na mashindano yale yale mliyoyaona kwangu, na kusikia kwamba ninayo hata sasa.**

**1:27 "mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili "** Flp. 1:27-30 Inaunda sentensi moja iliyorefushwa katika maandiko ya Kiyunani. Hii ni kauli ya kati ya wakati uliopo (yenye ushahidi) shurutishi kutoka katika mzizi wa kiyunani kwa ajili ya mji (*polis* kama vile Flp. 3:20; Mdo. 23:1; Efe. 2:19). Ingeweza kufasiriwa "lazima muendelee kuishi kama raia" (kama vile Flp. 3:20). Hii inaaksiwa katika fasiri kadhaa za kiingereza:

1. . *The Berkeley Version of the NewTestament* (Gerrit Verkuyl)
2. . *The NewTestament: An American Translation* (Edgar J. Goodspeed)
3. *The Emphasized NewTestament: A NewTranslation* (J. B. Rotherham)

Hii ingeweza kuakisi mazingira ya kihistoria ya Filipi kama Koloni la Warumi. Pia kithiolojia inamaanisha waaminio ni raia wa ulimwengu wa aina mbili na wanawajibika kwa yote. Sitiari ya kawaida ya Paulo kwa ajili ya maisha ya Mkristo ni neno "tembea." Wakristo wa mwanzo waliitwa kabla "Njia" (kama vile Mdo. 9:2;18:25-26;19:9,23; 22:4; 24:14,22). Waamini wanapaswa kuishi maisha yanayowastahili (kama vile Efe. 4:1, 17; 5:2, 15; Kol. 1:10; 1 The.2:12).

◙ **"nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo,"** Ukweli huu huu kuhusu haja ya kuendelea bila kuacha ndani ya maisha ya Mkristo Flp. 2:12 na katika Efe. 6:6 kama Paulo navyoonya watumwa wa Wakristo kufanya kazi kwa bidii kwa vyovyote vile iwe wanaangaliwa na mabwana zao au la!

◙ **"mnasimama imara katika roho moja"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo. Paulo anatumia mara nyingi tungo "kusimama imara" katika namna moja au mbili: (1) nafasi zetu katika Kristo(kama vile Rum. 5:2; 1 Kor. 15:1) or (2) hitaji letu la kuendelea kushikilia hali ya kufanana na Kristo (kama vile Flp. 4:1; 1 Kor. 15:1; 16:13; Gal. 5:1; Efe. 6:11,13,14; 1 The. 3:8; 2 The. 2:15). Huu ni wito wa umoja kikanisa (kama vile Mdo. 4:32; Efe. 4:1-6). Dhana ya "roho moja" imefanyiwa mjadala mkubwa sana. Inaweza ikamaanisha roho ya binadamu iliyokombolewa, au kwa Roho Mtakatifu. Muktadha huu na pia umekuwa kama katika Flp. 2:1, inayo inayounganisha vipengele vyote. Angalia waaminio wanatakiwa wasimame katika roho moja na akili moja (*psuchē*). Umoja ni muhimu (kama vile Efe. 4:1-6).

◙**"kwa pamoja mkiishindania"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Hili neno ambatani *syn* ni aidha (1) neno la kimichezo kwa ajili ya ushiriki wa timu katika michezo za kiyunani (2) au neno la kijeshi. Tunapata neno "mwanamichezo" kutoka katika neno la Kiyunani (kama vile Flp. 4:3; 2 Tim. 2:5). Maisha ya Mkristo kama vita vya kiroho yanajadiliwa katika Efe. 4:14; 6:10-20. Tazama toleo la fasiri la NJB "kushindana ,"kama timu yenye lengo moja kwa ajili ya imani."

◙ **"imani ya Injili"** Kibainishi cha wazi kipo ambacho kinafanya "imani." Muktadha unaitaji kwamba hii itumike katika namna ya kweli za Kikristo (kama vile Efe. 4:5; 1 Tim. 4:20; 2 Tim. 1:14 na Yuda 3, 20). Waaminio wanauliza maswali mengi ambayo Biblia haijayabainisha kwa uwazi peupe (hatua halisi za uumbaji, asili ya shetani, asili ya malaika, hali halisi ya asili ya mbinguni na kuzimu, n.k.). Kila kitu ambacho ni muhimu kwa ajili ya wokovu na ufanisi wa Maisha ya Mkristo umefunuliwa. Shauku ya utakatifu lazima ihitaji zaidi ya kile tulichopewa (ufunuo).

**1:28 "wala hamwaogopi adui zenu "** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo ambayo imetumika kuelezea mkurupuko wa wanyama (kama vile Mdo. 18:9, 10; 1 Kor. 2:3). Wapinzani wanaweza kuwa

1. Wayahudi wa mahali, japo kuna masinagogi yaliotajwa katika Filipi
2. Wapinzani wa kiyahudi wasafirio, kama katika Mdo. 17:13, au kama watu wa dini ya kiyahudi wa makanisa ya Wagalatia (kama vile Flp. 3:2-6)
3. Wapagani wa kawaida wa mahali (kama vile Mdo. 16:16-21)
4. mamlaka za kijamii za mtaa (kama vile Mdo. 16:21-40)

◙ **"kwao hao ni ishara mathubuti ya kupotea,"** Hili neno la Kiyunani, "ishara," lilimaanisha ushahidi uliojikita katika ushahidi (kama vile Rum. 3:25,26; 2 Kor. 8:24). "Maangamizi" lilikuwa ni sitiari ya kijeshi ambalo lilimaanisha "kuachia," "kuleta kwenye si kitu," au "kuharibu." Shuhuda zisizoogopesha za Wakristo na mtindo wa maisha ulikuwa ni mashahidi kwenda katika hukumu ya wapinzani na wokovu wa waamini.

◙ **"lakini ninyi"** Hili neno "ninyi" lililoko pote katika Flp. 1:28 na 29 ni la kimsisitizo. Ni utofauti uliopo kati ya waaminio na wasio amini.

◙ **"ya wokovu kwa ajili yenu"** Neno hili kwa kiasi Fulani lina utata, kama katika Flp. 1:19. Lingaliweza kutumika (1) katika namna nzima ya kiwokovu au (2) katika namna yake ya Agano la Kale ya ukombozi wa kimwili (kama vile Yakobo 5:15). Katika muktadha wa walimu wa uongo na dhiki za nje ni ngumu kuchagua kati ya chaguzi mbili.

◙ **"huo utokao kwa Mungu"** Maneno "ishara" na "wokovu" katika Flp. 1:28 yote ni ya jinsi ya kike wakati neno "kwamba" haina jinsi. Hivyo neno "kwamba" inawezekana likarejerea ujasiri ambao Mungu anawapa waamini ili kuweza kukabiliana na mashindano haya. Hii ni sawa na tungo za namna hii katika Efe. 2:8,9 ambapo "kwamba" inamaanisha "neema" au"imani," ambayo pia yana jinsi ya kike, lakini kuelekea katika mchakato mzima wa wokovu.

**1:29 " Maana mmepewa kwa ajili ya "** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu kutoka katika mzizi wa neno *charis* (kama vile Flp. 2:9; Rum. 8:32). Karama za neema ya Mungu ni ufunguo kwa ajili ya vyote wokovu na maisha ya Mkristo (kama vile Flp. 1:28).

◙ **"si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake"** Hizi ni kauli mbili za wakati uliopo zisizo na ukomo ambazo zinaweka bayana nini ambacho Mungu amewapa waamini katika Kristo. Moja inahusianishwa na imani inayoendelea na nyingine makuzi yanayoendelea. Ni ngumu kwa waamini wenye utamaduni wa kimagharibi kufanya mjadala juu ya mateso. Katika Agano Jipya ilikuwa ni kawaida mara kwa mara katika maisha ya Mkristo (kama vile Mdo. 14:22; Rum. 8:17; 1 The. 3:3; 2 Tim. 3:12; 1 Pet. 3:14; 4:12-16). Ufafanuzi wa kimuhtasari wa baadhi ya makusudi ya mateso inaweza ikawa
1. ilikuwa kwa faida kwa ajili ya Kristo (kama vile Ebr. 2:10; 5:8), hivyo,
2. ilikuwa ni kwa ajili ya faida za waamini (kama vile Flp. 2:10; Rum. 5:3; Yokobo 1:2-4; 1 Pet. 1:6,7), na
3. inaleta uhakika wa furaha kwa sehemu ya waaminio katika Kristo(kama vile Mt. 5:10-12; Mdo. 5:41; Yakobo 1:2; 1 Pet. 3:14; na 4:12-16)

**1:30 "mkiwa na mashindano yale yale "** Wakristo wa Filipi walikuwa wanapitia mateso. Neno "kushindana," limetumika mara nyingi na Paulo, ilikuwa huenda ni sitiari ya kimichezo au kijeshi. Tunapata neno la Kiingereza"kugunia kwa maumivu" kutoka katika neno hili la Kiyunani.

◙**"ambayo mliona ndani yangu"** Tunajifunza kitu kutoka katika dhiki za Paulo katika Filipii kutoka Mdo. 16: 22-24 na 1 The. 2:2. Paulo alitengeneza mfano wa ukristo kwa ajili yao na yetu.

## MASWALI YA MJADALA KWA WAFILIPI 1:27-30

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Paulo anawaambia waamini wafanye nini katika Wafilipi 1:27?
2. Wapinzani gani wanaotajwa katika Wafilipi 1:28?
3. Je mateso na  dhiki vina umuhimu gani kwa Waamini

# WAFILIPI 2

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Unyenyekevu wa Wakristo na unyenyekevu wa Kristo | Umoja upitiao unyenyekevu | unyenyekevu na mfano wa Kristo | Unyenyekevu wa Kristo na Ukuu wake | Kuutunza umoja katika unyenyekevu |
| 2:1-11 | 2:1-4 | 2:1-11 | 2:1-11 | 2:1-11 |
| | Kristo aliyenyenyekea Na kuinuliwa | | | |
| | 2:5-11 | | | |
| Mkiangaza kama nuru ulimwenguni | Waangaza nuru | | Mkiangaza kama nuru ulimwenguni | Tendeni kwa ajili ya wokovu |
| 2:12-18 | 2:12-18 | 2:12-13 | 2:12-13 | 2:12-18 |
| | | 2:14-18 | 2:14-16 | |
| | | | 2:17-18 | |
| Timotheo na Epafrodito | Timotheo anasifiwa | Timotheo na Epafrodito | Timotheo na Epafrodito | Wito wa Timotheo na Epafrodito |
| 2:19-24 | 2:19-24 | 2:19-24 | 2:19-24 | 2:19-3:1a |
| | Epaferodito anasifiwa | | | |
| 2:25-30 | 2:25-30 | 2:25-3:1a | 2:25-30 | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka**"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii Mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu

4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 2:1-11

A. Muktadha huu dhahili unahusiana na moja ya dhamira ya kitabu “wito wa umoja kati ya Wakristo huko Ufilipi” (kama vile. Flp. 1 :27; 2:1 -4; 4:2-3,5,7,9 na Efe. 4:1 -6).

B. Pamekuwepo na mijadala mingi kati ya watoa maoni kwa namna utenzi huu wa ajabu kwa Kristo (kama vile. Flp. 2:6-1 1 ) unatenda kazi kwa ajili ya maadili au kwa ajili ya wokovu.

   1. Unatenda kazi kama mfano kwa waumini kuishi kwa pamoja, wakiyatoa maisha yao (kama vile. Flp. 2:1 -5).
   2. Pia unashughulika na fedheha na uinuliwaji uliokuwepo kabla wa Masiha aliyekuwa mwanadamu
   3. Kwa namna tofauti unatenda kazi maeneo yote

C. 2:6-1 1 unaonekana kuwa ni utenzi wa mwanzo wa Kikristo

   1. Muundo ni wa meta, kishairi, au shairi lenye kujaa hisia
   2. Ndani yake lina maneno adimu ya Kiyunani yasiyotumiwa na Paulo
   3. Unakosa baadhi ya viashiria pekee vya thiolojia ya Paulo inayohusu Kristo
   4. Paulo ananukuu tenzi nyingine za kanisa la mwanzo, ushairi, au muundo wa kiluturujia katika 1 Tim. 3:1 6 na 2 Tim.2:1 1 -1 3
   5. Kwa ajili ya maoni mengine angalia Gordon Fee, *To What End Exegesis?* pp. 1 731 -1 89

D. Muundo wa utenzi kwa Kristo umekuwa ukijadiliwa. Unaonekana kugawanywa katika misisitizo miwili iliyo sawa

   1. Nafsi ya Yesu na kazi
      a. Kabla ya kuwepo, Flp.2:6
      b. Kubadilika kuwa mwanadamu, Flp. 2:7
      c. Kifo mbadala, Flp. 2:8
   2. Mwitikio wa Mungu Baba
      a. Bwana wa wote, Flp. 2:9
      b. Ukiri wa wote, Flp. 2:10
      c. Mamlaka iliyo kuu (Bwana), Flp. 2:11

E. Maelezo fasaha ya utenzi huu mkubwa kwa Kristo

   1. Mistari ya 6-8
      a. Fedheha ya Kristo
      b. Usuli wa Agano la Kale katika Mwanzo 3 (uainishi wa Adamu/Kristo)
      c. Mitizamo ya matendo ya Yesu
   2. Mistari ya 9-11
      a. Kuinuliwa kwa Kristo
      b. Usuli wa Agano la Kale ni Isa. 52:13-53:12 (mtumwa mwenye mateso)
      c. Mitizamo juu ya matendo ya Mungu Baba
   3. Biblia zinazoutoa utenzi kwa namna tofauti na lugha ya mjazo ni za muhimu katika kuvitazama vipengere vya mita na ufanano (k.v. NRSV, TEV, NJB)

F. Kweli za msingi zinazopatikana katika utenzi wa thiolojia ya Kristo

   1. Yesu ni Mungu kamili (katika asili, *morphē*)
   2. Yesu ni mwanadamu kamili(katika muundo, *schēma*)
   3. Hakika Yesu anahitaji mazuri yetu, sio ya kwake, kwa hiyo inawalazimu Wakristo
   4. Yesu ni chombo kamili kinachotakiwa kuabudiwa kwa mapenzi ya Baba

G. Utenzi haukuwa wa Paulo

   1. Unaondoa suala la ufufuo ambao ndio ulikuwa msisistizo mkubwa wa Paulo kwa wakati huu
   2. Unaondoa msisitizo wa Paulo wa mara kwa mara juu ya uhusiano wa Yesu na kanisa
   3. Unatumia maneno mbali mbali ambayo hayakutumiwa na Paulo mahala popote
   4. Paulo anatumia nukuu zingine za utenzi wa kanisa la mwanzo, ushairi wa katekismu, au muundo wa liturujia katika 1 Tim. 3:1 6; 2 Tim. 2:1 1 -1 3 na yumkini Kol. 1 :1 5-20; 1 Tim. 1 :1 7; 6:1 5-1 6

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 2:1-11**
**[1]Basi ikiwako faraja yo yote katika Kristo, yakiwako matulizo yo yote ya mapenzi, ukiwako ushirika wo wote wa Roho, ikiwako huruma yo yote na rehema, [2] ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mkinia mamoja. [3] Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. [4] Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine. [5] Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; [6] ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; [7] bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; [8]tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. [9]Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; [10]ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; [11]na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.**

**2:1 "ikiwako"** Hii ni ya kwanza katika orodha nne ya sentensi yenye masharti daraja la kwanza inayodhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi la kifasihi. Mistari ya 1-4 ni sentensi moja katika Kiyunani.

◙ **"faraja yoyote katika Kristo"** Hili neno linaweza kutafasiriwa katika Nyanja tofauti: "kuchochea,""kusihi," "kufariji," "kutia moyo," "kushawishi." kifungu hiki kinafanana na mazungumzo ya Paulo juu ya mienendo iletayo na kuendeleza umoja ndani ya Kristo katika makanisa ya nyumbani Efe. 4:2-3. "Katika Kristo"(uhusika wa mahali) ni njia ya kawaida ya Paulo ya kuwatambua waamini. Kwa ajili ya maisha, maisha ya kweli, maisha tosherevu, waamini lazima wawe katika muungano muhimu pamoja na Kristo kwa imani (kama vile Yohana 15).

◙**"yakiwako matulizo yoyote ya mapenzi"**upendo mara zote umekuwa mzizi na tunda la maisha ya Mkristo (kama vile. Yn 1 3:34-35; 1 5:12,17; 1 Kor. 13; Gal. 5:22; 1 Yn 3:1 1 ,27; 4:7-21 ). Yesu aliyaishi, akayafundisha, na kuyaamuru kwa wafuasi wake.

◙ **"ushirika wowote wa Roho"** Hili ni neno la Kiyunani *koinōnia*, lenye kumaanisha "ushirika wa pamoja na" (kama vile. 2 Kor. 13:14). Tena, swali ni kuwa, "je hili linarejelea kwa mshirika mpya aliye kombolewa, roho ya mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu,"au "ni yule Roho Mtakatifu waliopewa"? Hapana kibainishi chenye neno "roho," huu unaweza kuwa ni utata uliokusudiwa. Yawezakuwa kithiolojia unarejelea kwa yote. Angalia Mada Maalum: *Koinōnia* katika uk.170)

◙ **"ikiwamo huruma"** Kiuhalisia hili neno ni "huruma,"ambalo pia limetumika katika Flp. 1:8. Watu wa kale waliamini kuwa sehemu ya chini ya tumbo ilikuwa ndio mahali pa mihemuko. Maneno yote haya pia yanatumika katika Kol. 3:12.

◙**"rehema"** Paulo analitumia neno hili mara nne: (1 ) kuelezea tabia ya Mungu (kama vile Rum. 12:1 ; 2 Kor.1 :3) na (2) kuelezewa jinsi gani Wakristo wanapaswa kuwatendea wengine (kama vile Flp. 2:11 ; Kol. 3:12). Mungu anatamani kuitengeneza tabia yake (taswira) ndani ya watoto wake. Urejesho wa taswira ya Mungu uliopotea kwenye anguko ndio sababu ya kurudi kwa Yesu.

**2:2 "ijalizeni furaha yangu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu na inayoonyesha ni namna gani Paulo aliwawaza waamini hata kama alikuwa mbali gerezani. Matendo yao na chaguzi vilisababisha furaha au maumivu kwa Paulo..

◙ **"ili muwe na nia moja"**Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo ambayo imeelezewa na kauli nne endelevu za wakati uliopo (yumkini zimetumika kama shurutishi) inayoanza katika Flp. 2:2 na kuendelea mpaka Flp. 2:4. Zinashughulika na maswali magumu yenye kuleta mantiki ya kuendeleza umoja kwenye ushirika wa Kikristo (kama vile. Rum. 14:1 -15:13; 1 Kor. 8:1 -13; 1 0:23-33). Miongozo ya Paulo ni ya muhimu, sio tu kwa Wafilipi katika karne ya kwanza, bali ni kanisa la kila rika. Kauli nne endelevu ni

1. Kuuendeleza upendo ule ule
2. Kuunganishwa katika roho na kujitazamisha kwenye kusudi moja
3. Kuwafikiria wengine kama wa muhimu zaidi kuliko wewe mwenyewe
4. Kuuangalia umuhimu wa wengine

Uwe makini na dini ya kiubinafsi. Ukristo ni uzoefu wa kifamilia. Mara nyingi Paulo analivyotumia neno hili "fikiri/tafakari" (*phroneō)* katika Wafilipi likajakuwa mada nyingine ( kama vile. Flp. 1 :7; 2:2[mara mbili]; 2:5; 3:15 [mara mbili]; 3:19; 4:2; na 4:10).

**2:3 "msitende neno lolote kwa kujivuna wala kwa mashindano"** Hili laweza kuwa linaelezea hali ilivyo katika kanisa la Wafilipi iliyosababishwa na walimu wa uongo au na mateso (kama vile Flp. 1 :15,17; Gal. 5:26). Hakuna kitenzi, lakini msukumo wa mstari huu ni wa kushurutisha. Urudiaji wa neno "tafakari" (*phroneō*) katika muktadha waweza kudokeza kuwa kitenzi ni cha kufikiriwa.

◙ **"bali kwa unyenyekevu"** Unyenyekevu haukuwa upendeleo wa wema katika ulimwengu wa Wagiriki na Warumi, lakini Kristo ameifanya dhana ya kipekee ya maisha yake mwenyewe na kuwaita wafuasi wake kuyaigiza katika maisha yake ya Kikristo ( kama vile Flp. 2:8; Mt. 1 1 :29; 1 Pet. 5:5,6). Ni kinyume cha kimuktadha cha "ubinafsi na mashauri yaliyo tupu."

◙ **"kila mtu na amuhesabu mwenzake kuwa ni bora kuliko nafsi yake"**Hii ni kauli ya kati (shahidi) ya wakati uliopo. Hili linaenda kinyume na tabia zote za kiasili za binadamu, lakini ni mapenzi ya Mungu (kama vile Rum. 1 2:10; 1 Kor. 10:24, 33; Gal. 6:2; Efe. 5:2). "muhimu zaidi"angalia Mada Maalum:
Matumizi ya Paulo ya neno ambatani *Huper* katika Efe. 1 :19.

**2:4 "kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe"** Hii ni kauli tendaji endelevu ikiwa na kiambata hasi (ikitumika kama shurutishi) mara zote ikimaanisha kuzuia kitendo kilicho katika mchakato. Ilimaanisha "kuangalia kitu kwa umakini" (kama vile 2 Kor. 4:18). Neno "moyo wa kupenda"linaweza kurejelea kwa (1 ) vitu; (2) karama za kiroho; au (3) matukio. Kitu muhimu hapa ni neno "pekee."sio kwamba waamini wasiwe na moyo wa kupenda mambo yao wenyewe (k.v. 1 Tim. 5:8), bali wasiyaweke kama vipaumbele wakiwatenga wengine, hasa wapendwa wenzao. Mlinganyo unaonekana katika Gal. 6:1 -2. Waamini wanapaswa kuweka uangalifu mkali ili kwamba waweze kuwaangalia wengine.

**2:5 "iweni na nia iyo hiyo ndani yenu"**Hii kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo .waamini wanaamriwa kuendelea kufikiri (*phroneō*) kama Kristo. Lengo la Ukristo ni mfanano katika mawazo na matendo (kama vile Kol. 3:1 6). Huu ni mwanzo wa Paulo wa utumiaji wa nukuu toka utenzi wa Wakristo wa mwanzo. Kuna maneno mbali mbali katika kipengere cha ushairi kisichopatikana popote kwa Paulo. Mifano mingine ya Paulo aliyo nukuu toka aina hii ya uyakinifu ni Efe. 5:14; 1 Tim. 3:16; 2 Tim. 2:11 -13 na yumkini Kol. 1 :15-20; 1 Tim. 1 :17; 6:15-16. Wakristo wanaonywa kufuatisha mifano ya Yesu kwa namna mbili: (1 ) uliuacha utukufu wake wa ki-Ungu, wa awali ili awe mwanadamu, si kwa ajili yake, bali kwa ajili ya wengine na (2) alikuwa tayari kufa, sio kwa ajili ya dhambi zake, bali kwa ajili ya wengine,Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuiga tabia hizi za kujitoa (kama vile.1 Yn 3:1 6). Sisi ni waangalizi wa ndugu zetu kwa sababu ndugu zetu wana sura na mfanano wa Mungu!

**2:6 "ambaye Yeye mwanzo alikuwako"** Kiuhalisia hii tungo inamaanisha "ambaye amekuwa katika muundo wa Mungu."Hii ni moja ya njeo mbili za wakati uliopo (hapa ni kauli endelevu) katikati ya mlolongo wa vitenzi vyenye tungo za wakati uliopita usiotimilifu na wakati endelevu. Zinasisitiza uwepo wa Yesu wa Nazareti kabla (kama vile. Yn 1 :1 ; 8:57-58; 1 7:5,24; 2 Kor. 8:9; Kol. 1 :1 7; Ebr. 1 0:5-7). Uwepo wa Yesu kabla ni mfano mwingine wa Uungu wake. Yesu hakuwa mwanadamu pale Bethelehem. Hapakuwahi kuwepo na wakati ambao Yesu hakuwahi kuuishi

na hakuwa Mungu.

◙ **"namna ya Mungu"** Hili ni neno la Kiyunani *morphē* linatumiwa kwa maana tofauti.

1. Maana ya asili ya Aristotlian
2. Maana ya asili ya kitu fulani au asili isiobadilika ya kitu fulani (hii ni namna ya makasisi wa kanisa la mwanzo waliweza kuyatafasiri)
3. Muundo wa nje wa kitu, kama ilivyo kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX). Hii haimanishi kuwa YHWH ana mwili wa nyama, lakini hilo ni chagizo na tabia-hasa asili ya Mungu Baba-ni ushahidi wa Mungu ndani ya Mwana. Hii ni njia nyingine ya kuutetea Uungu kamili wa Kristo. Angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu mmoja katika Efe. 4:6.

◙ **"hakuona kuwa sawa na Mungu"** Kiuhalisia hii ni "hakuona kule kuwa sawa na Mungu" kuwa ni kitu cha kushikamana nacho. Hii ni tungo nyingine ya wakati uliopo (hapa ni kitenzijina). Neno la Kiyunani la "usawa" linatokana na neno la Kiingereza "chenye kipimo sawa." Ni njia nyingine ya kutetea kuwa Yesu ni Mungu kamili (kama vile. Yn 1 :1 ; Tito 2:1 3).

**NASB "kitu cha kuchukuliwa"**
**NKJV "unyang'anyi"**
**NRSV "unyonyaji"**
**TEV "kuchukua kwa nguvu"**
**NJB "kitu cha kuchukuliwa"**

Hili neno adimu la Kiyunani, *harpagmos*, mwanzo lilimaanisha "kitendo cha kutaifisha kitu fulani" au "kuhitajika baada ya zawadi" *(harpagma)*. Hata hivyo, lingaliweza kutumika katika maana ya kutendewa (likimalizia na neno la Kiyunani *mos*) lenye kumaanisha "kile ambacho kimetaifishwa au kushikiliwa." Uwezekano wa tatu ni "ni kile kitu mtu anacho lakini hakitumii kwa faida binafsi."hili linaaksiwa kwenye tafasiri ya Wafilipi ya Flp. 2:7: "alipigwa kwa faida ya wengine."yesu tayari anao usawa na Mungu. Sababu ya kithiolojia kwa ajili ya utata wa kifungu hiki ni uainishi wa Adamu/Kristo, ambapo Adamu anajaribu kuleta usawa na Mungu kwa kula tunda lililokatazwa (kama vile Mwanzo 3). Yesu ambaye ni Adamu wa pili (kama vile Rum. 5:12 na kuendelea), akafuata mpango wa Mungu kwa utii kamili ambapo Maumivu yaliendeleza uinuliaji (kama vile Isaya 53).

**2:7**
**NASB, NKJV**
**NRSV "alijifanya hana utukufu"**
**TEV "pasipo kuhesabiwa uzuri"**
**NJB "kwa mapenzi yake akavitoa vyote"**

kiwakilishi nomino ni chenye msisitizo. Huu ulikuwa ni uchaguzi wa Yesu mwenyewe! Kuna nadharia mbali mbali kuhusu kile kinachomaanisha kuwa Yesu alijifanya hana utukufu (kama vile. 2 Kor. 8:9).

1. Paulo analitumia neno hili mara kadhaa (kama vile Rum. 4:14; 1 Kor. 1 :17; 9:1 5; 2 Kor. 9:3). Inawezekana Yesu aliamua kuishi kama mwanadamu. Aliuacha utukufu wake wa ki-Ungu kwa hiari na kuukubali udhaifu wa mwili. Hakika bado ana mtazamo mkubwa na nguvu za kiroho kuliko mwanadamu wa kale aliyeanguka. Yeye akawa kile ambacho mwanadamu alitarajiwa awe. Yeye ni Adamu wa pili na zaidi.
2. Yesu hakujishusha chini kuliko Mungu katika kubadilika kwake kimwili, lakini inaonekana yeye aliongeza ubinadamu/utu kwenye Uungu wake. Aliuuacha utukufu wa ki-Ungu wa nje na kuchukua umbo la nje la mtu. Hili lilionyesha kuongeza na sio kutoa. Kipindi cha huduma ya Yesu hapa duniani, alijazwa na kuwezeshwa na Roho, lakini pia alikuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili (alijaribiwa, Mathayo 4, alipatwa pale Gethseman, Marko 14:32-42). Alimfahamu na kumfunua Baba (kama vile Yn 1:18). Alikuwa ni mmoja wa uanadamu wetu (kama vile Yn 1:4)
3. Inawezekana kuwa huu uondoaji ilikuwa ni njia ya kuidokeza Isa. 53:1-3. Kama ndivyo ilivyo, haihusiani na ubinadamu wake (Flp. 2:7-8a) lakini ni kutokana na kusulubiwa kwake (Fil. 2:8b) kama mtumishi wa YHWH (kama vile Marko 10:45-15:53).

◙ **"akatwaa namna ya utumwa"** Hii ni fasihi kamili yenye kufanana na kifungu "asili ya Mungu"(k.v Flp. 2:6). Neno "utumwa" (*doulos*) hapa lingaliweza kutumika kwa maana ya mtumwa mwenye mateso katika Isa. 42:1 -9; 49:1 -7; 50:4-1 1 ; 52:1 3-53:1 2. Yesu aliuacha utukufu wake wa mbinguni kwenye hori la ng'ombe (kama vile 2 Kor. 8:9). Huu pia ni usuli wa Flp. 2:9-11. Mstari huu unasisitiza juu ya ubadilikaji wa umbo la Yesu (kauli endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu), na sio kusulubiwa kwake kuliko tajwa katika Fil. 2:8. Yesu kwa uwazi anaonyesha kuwa kiongozi wa kweli, nguvu ya kweli ndio moyo wa utumishi. Kiongozi, lazima mtu atumike (kama vile Marko 10:42-45; Mathayo 20:25-28). Unyenyekevu wake ndio alama ya nguvu ya kweli. pendo lake alilotowa ni alama ya kweli ya Uungu.

◙ **"akawa ana mfano wa wanadamu"** Toleo la RSV na NRSV yanalitafasiri hili neno kama "kuzaliwa."huu ni msisitizo mkubwa wa pili wa utenzi huu wa kanisa la mwanzo: ubinadamu kamili wa Yesu. hili lilifanyika kukanusha walimu wa uongo wenye ujuzi, walioshikilia pande mbili za umilele (asili ya neno) kati ya roho na maada. Asili ya pande mbili za Yesu ni suala kubwa la kithiolojia la Agano Jipya (kama vile 1 Yn 4:1-6). Matumizi ya Yesu ya neno la Agano la Kale "Mwana wa Adamu"yanaonyesha mwelekeo huu. Katika Zab. 8:4 na Eze. 2:1 neno lina maana ya kawaida ya Kiyahudi nafsi ya mtu. Hata hivyo, katika Dan. 7:13 linalenga juu ya tabia za ki-Uungu (yaani.,kupita mawinguni na kuupokea ufalme wa milele). Yesu alitumia kifungu hiki kwa ajili yake mwenyewe. Hakikutumiwa kwa wingi sana na walimu wa dini ya Kiyahudi na hakikuwa na vidokezo vya kijeshi, utaifa, au utenganishaji. Mwanzo wa Fil 2:8 unasisitiza juu ya ukweli wa thiolojia ile ile ikiwa na utofauti kuwa ingawa Yesu alikuwa mwanadamu kamili, hakushriki katika asili ya anguko la mwanadamu (kama vile. Rum. 8:3; 1 Kor. 5:21 ; Ebr. 4:1 5;7:26; 1 Pet. 2:22; 1 Yn 3:5).

**2:8 "alipoonekana kuwa na umbo la mwanadamu"** Kuna baadhi ya mkanganyiko kati ya tafasiri ikiwa kama hiki kifungu kiendane na mstari wa 7 au 8 . hili ni neno la Kiyunani "*schēma,*" ambalo mara nyingi lilitofautiana na neno "*morphē*." Katika falsafa ya Kiyunani neno *morphē* lilimaanisha "muundo wa ndani wa kitu ambao unaaksi kiukweli asili yake," wakati "*schēma*" lilimaanisha "badiliko la muundo wa nje wa kitu ambao hauwakilishi kikamilifu asili yake ya ndani"(kama vile. 1 Kor. 7:31 ). Yesu ni kama sisi kwa kila namna isipokuwa ile asili ya dhambi ya anguko la mwanadamu.

◙**"alijinyenyekesha akawa mtii hata mauti"** Hili laweza kuwa dokezo kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) ya Isa. 53:8. Yesu aliufuata mpango wa ukombozi wa milele wa Baba yake (kama vile. Lk22:22; Mdo 2:23; 3:1 8; 4:28) hata kufikia mateso na kifo (kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu na kauli yenye kuarifu ya wakati uliopita usio timilifu).

◙ **"naam, mauti ya msalaba"** Msalaba ulikuwa ni jiwe la kujikwaa kwa Wayahudi (kama vile. 1 Kor. 1 :23). Hawakumtegemea Masihi mwenye mateso, bali yule Masihi aliye mshindi. Pia kwa sababu ya Kumb. 21 :23, unao maanisha kuwa ikiwa mtu aliwekwa hadhalani baada ya kufa, kwao ilikuwa ni alama ya kulaaniwa na Mungu. Wayahudi wasingaliweza kuona namna Masihi wao angalilaniwa na Mungu, lakini huu ndio ukweli wa Gal. 3:1 3, kuwa akawa laana kwa ajili yetu. Dhana ya Masihi mwenye mateso (kama vile. Mwa. 3:1 5; Zaburi 22) lilikuwa ni suala ovu kwao. Bado hii ni namna YHWH anavyoshughulika na tatizo la dhambi ya Mwanadamu. Upatanisho mbadala wa kifo cha Yesu (kama vile. Isa. 52:1 3-53:1 2; Marko 1 0:45; Yn 1 :29; 1 Pet. 1 :1 9). Msalaba ni kiini cha ukweli wa Agano Jipya ambapo upendo na haki ya Mungu hukutana na kuungana

**2:9**
**NASB, NKJV**
**NRSV "kwa hiyo basi"**
**TEV "kwa sababu hiyo"**
**NJB "na kwa hili"**

Agano Jipya linamuwasilisha Yesu kwa namna mbili: (1 ) Mungu kamili aliyeishi kabla kama vile. Yn 1 :1-3,1 4; 8:57-58; Kol. 1 :17) na (2) Mungu aliye inuliwa kwa sababu ya utii wake, maisha matakatifu ya kidunia (kama vile. Rum.

1 :4; Flp. 2:9). Katika kanisa la mwanzo hili lilipelekea kuwepo na msigishano kati ya orthodox na wale wanathiolojia walio asiliwa. Hata hivyo, kama ilivyo mara nyingi wote walikuwa na mtazamo wa ukweli. Vile Yesu alikuwa limedhihilishwa na yale Yesu alitenda! Hapana thiolojia mbili kumhusu Yesu, lakini njia mbili za kuutizama ukweli ule ule. Mwitikio wetu usiwe wa kujaribu kuamua ni kipi cha kweli, bali kumshukuru Mungu kwa ajili ya Kristo kabla, kwa wakati huu, na wakati ujao!

◙ **"tene Mungu akamwadhimisha mno"** Hili ni dokezo kwenye tafasiri ya maandiko ya Kiyunani ya agano la kale (LXX) ya Isa. 52:1 3. Muundo wa uimalishaji wa neno *huperupsoō* unapatikana hapa tu katika Agano la Jipya na kwa nadra katika ulimwengu wa Kiyunani. Angalia Mada Maalum: matumizi ya Paulo ya neno ambatani *Huper* katika Efe. 1 :1 9. Huu haukuwa uasili wa thiolojia kumhusu Kristo, inayodai kuwa Yesu alizawadiwa Uungu. Yesu alirejeshwa kwenye Uungu kabla ya utukufu (kama vile Efe.4:1 0). Katika injili ya Yohana kifo cha Yesu kinarejelea juu ya kutukuzwa kwake (kama vile. Flp. 7:39; 12:1 6,23; 13:31 -32;16:1 4; 17:1 ). Mtumishi mnyenyekevu sasa ni Mfalme wa Wafalme!

◙ **"akamkirimia jina lile lipitalo majina yote"** Hili jina maalum lililo inuliwa ni “Bwana”(kama vile. Flp. 2:1 1 ). Kitenzi (*echarisato*) katika Flp. 2:9 kinamaanisha “kukirimiwa wema”kama katika Flp. 1 :29. Neno “Bwana”ni kidokezo kwenye jina la Agano la Kale la Mungu,YHWH (kama vile. Kut. 3:1 4; 6:3), pale Wayahudi waliogopa kulitaja wasije wakavunja moja ya zile amri kumi (kama vile. Kut. 20:7; Kumb. 5:1 1 ). Kwa hiyo, walitumia neno mbadala Adon, lililo maaanisha Bwana, Mmiliki, Mme. Yesu aliyekuja kwa umbo la kitumishi, aliurudia u-Bwana wake (kama vile. Yohana 17:5; Kol. 1:15-20). "Yesu ni Bwana" ulikuwa ni ukiri wa imani wa wazi, ya mtu binafsi kwa lile kanisa la mwanzo (kama vile. Rum. 10:9; 1 Kor. 8:6; 1 2:3). Yesu wa Nazareti amepewa cheo cha Uungu wa kimamlaka (kama vile. Efe. 1 :21 na Ebr. 1 :4). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Kol. 1 :3.

**2:10 "ili kwa jina la Yesu, kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi"** Ili siku moja watu wakubali kuwa Yesu ni Bwana. Swali ni kuwa ikiwa hili watalifanya ndani ya muda kwa imani, na baadaye kuwa sehemu ya familia ya Mungu, au watalifanya kwenye siku ya Bwana na kuhukumiwa nae (k.v. Mt. 25:31 -48; Ufu. 20:11 -15). kifungu mfanano katika mstari huu kinarejea malaika, wanadamu wote walio huru na waliofungwa, walio hai na walio kufa. Na viumbe vyote vyenye nafsi vitaukubali u-Bwana wa Yesu, lakini ni mwanadamu tu anaweza kombolewa. Mistari ya 10-11 inaonekana kuwa kama vidokezo kwa Isa. 45:23, ambao umenukuliwa toka Rum. 14:11. Katika mazingira haya ya asili ilikuwa ni hali ya kumwabudu YHWH ambayo sasa imehawilishwa kwa Masihi (kama vile Yn. 5:23). Ubadilishaji wa wadhifa na utendaji kazi kati ya YHWH NA Yesu ni njia nyingine waandishi wa Agano Jipya wanadai Uungu kamili wa Yesu. Angalia Mada Maalum: Malaika katika maandiko ya Paulo katika Efe 6:12

**2:11 "na kila ulimi utakiri"** Hii ni kauli ya kati tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu (ikitumika kwa wakati ujao, baadhi ya maandiko ya Mesoretic yana herufi za wakati ujao yaani., A,C,D,F,G ) ya neno *exomologeō* ambalo linakubali ukweli kuwa ukiri wa maneno, wa uwazi wa Ukuu wa Kristo utakuwa ni ukweli wa siku ya mwisho. Huu ukubalifu wa Ukuu wa Yesu ulikiwa ni ukiri wa mwanzo wa imani (yaani., liturujia ya kiubatizo). Paulo alilitumia neno hili kama alivyotumia nukuu mbali mbali za Agano la Kale toka kwenye tafasiri za maandiko ya Kiyunani ya Agano la Kale (kama vile. Flp. 2:11 na Rum. 1 4:11 toka Isa. 45:23 na Rum. 15:9 toka Zab1 8:49. Pia neno linalohusiana na *homologeō* katika Rum. 10:13 toka Yoel 2:37).

**MADA MAALUM: UKIRI**

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la pande zote mbili yaani Agano la Kale (*Nacham*, BDB 636, KB 688, mf., Kut. 13:17; 32:12,14; *Shuv*, BDB 996, KB 1427, m.f. 1 Fal. 8:47; Eze. 14:6; 18:30; tazama Mada Maalumu: Toba [Agano la Kale]) na Agano Jipya.

1. Yohana Mbatizaji (Mt. 3:2; Marko 1:4; Luka 3:3,8)
2. Yesu (Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Matendo 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Petro. 3:9)
4. Paulo (Matendo 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini Toba ni nini? Ni huzuni ya kiroho? Ni kumaanisha kuacha dhambi? Eneo zuri katika Agano la Jipya katika

kuelewa maana tofauti ya dhana hii ni 2 Wakorintho 7:8-11, ambapo hizo tatu zinanahusiana, lakini ni tofauti, maneno ya Kiyunani yanatumiika.

1. "huzuni" (*lupeō*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 9 [mara tatu], 10 [mara mbili], 11). Inamaanisha kupata maumivu au kutambua na ina maana ya kitheolojia isiyofungamana na upande wo wote.
2. "toba" (*metanoeō*, kama vile. mst. 9,10). Ni muunganiko wa neno "baada ya" na "kumbukumbu," ambayo inadokeza akili mpya, njia mpya ya kufikiri, mtazamo mpya kuhusu maisha na Mungu. Hii ni toba ya kweli.
3. "majuto" (*metamelomai*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 10). Ni muungano wa "baada ya" na "uangalifu." Linatumika juu ya Yuda katika Mt. 27:3 and Esau katika Ebr. 12:16-17. Linadokeza sikitiko juu ya matokeo, si juu ya matendo. Toba na imani ni matendo ya kimaagano yanayohitajika (kama vile. Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko ambayo yanadokeza kwamba Mungu hutoa toba (kama vile. Matendo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Lakini maandiko mengi yanalitazama hili kama mwitikio muhimu wa agano la mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu ya wokovu huru.

Maelezo ya maneno yote ya Kiebrania na Kiyunani yanahitajika ili kuielewa maana kamili ya toba. Neno la Kiebrania linadai "mabadiliko ya tendo," ambapo neno la Kiyunani linadai "mabadiliko ya akili." Mtu aliyeokolewa anapokea akili na moyo mpya (kama vile. Eze. 36:26-27). Anafikiri tofauti na kuishi tofauti. Badala ya "Kilicho ndani ni kwa ajili yangu?" sasa swali ni "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Toba si hisia ambazo hufifia au dhambi ya moja kwa moja, bali uhusiano mpya na Aliye Mtakatifu ambaye humbadilisha mwamini kwa uendelevu na kuwa ndni ya utakatifu. Si rahisi mtu akasitisha kufanya kitu au kuachana nacho, bali ni kwa mtazamo na uelekeo mpya katika maisha. Anguko linatusabisha sisi kujitazama wenyewe lakini injili inaturuhusu sisi kumtazama Mungu. Toba ni tendo la kugeuka na imani ni tendo la kugeukia kitu/kifikra!

◙ **"kwa utukufu wa Mungu Baba"** Hali ya kumwabudu Yesu ni kusudi la Mungu Baba la kumtuma Yeye. Kifungu hiki "utukufu wa Mungu"vinashabihiana na maisha ya mwamini katika Flp. 1:11 na hapa katika Flp. 2:11 kwa ajili ya wokovu wao, yaletwayo kupitia kazi ya Kristo. Kifungu hiKi muhimu kinatumika mara tatu katika maombi ya Paulo ya kumsifu Mungu wa Utatu katika Efe. 1:3-14. Hatimaye Yesu ataugeuza uwezo wote, mamlaka na sifa kwa Baba akaaye naye (kama vile. 1 Kor. 1 5:27-28). Angalia maelezo kamili juu ya "utukufu" katika Efe. 1 :6.

## TAMBUZI ZA KIMKTADHA KWA WAFILI 2:12-30

A. Flp. 2:12-18, kama Fil. 2:1-11 , zinahusiana na maisha ya Mkristo
B. Flp. 2:19-30 inahusiana na wasaidizi wa Paulo, Timotheo na Epaphrodito na ujio wao huko Filipi.
 1 . Timotheo, Flp. 2:19-24
 2. Epaphrodito, Flp. 2:25-30

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU LA MANENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 2:12-13**
**12 Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. 13 Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.**

**2:12-13** Hii ni sentensi moja katika Kiyunani.

**2:12 "basi"** Ni dhahili limeunganishwa na mazungumzo ya nyuma ya unyenyekevu na utii wa Kristo. Katika uelewa wa ndani wa mfano wa Yesu katika Fil. 2:6-11, hawa waamini waliombwa kuishi (1 ) kwa unyenyekevu na uangalizi, Flp. 2:1-5, na (2) kama Kristo, Flp. 2:14-18.

◙ **"wapendwa wangu"** Paulo alilipenda kanisa hili kwa namna ya tofauti (kama vile. Flp. 4:15-16). Paulo anatumia kifungu hiki mara nyingi kuelezea wale walioongoka katika huduma yake (kama vile Rum. 12:19; 1 6:8,9,12; 1 Kor.

4:14,17; 10:14; 1 5:58; 2 Kor. 7:1 ; 12:19; Efe. 6:21 ; Flp. 4:1 [mara mbili]; Kol. 4:7,9,1 4; 1 Tim. 6:2; 2 Tim. 1 :2; Filemon 1 :1 ,2,16).

**NASB, NKJV "kama mlivyotii siku zote"**
**NRSV, TEV "kama mlivyonitii mimi"**
**NJB "kama siku zote mlivyotii"**

Neno haliongei ni nani waliyemtii. Inagaliweza kuwa (1 ) Baba/Mwana/Roho; (2) imani ya Wakristo; au (3) Paulo. Utii wa Kristo, uliotajwa katika Fil. 2:8, ulitolewa kama mfano kwa wafilipo kuufuata (kama vile. Lk 6:46). Kifungu hiki chaweza kurejea utii wa kanisa kwa mafundisho ya Paulo (kama vile. Flp. 2:12b). Ukristo ni mchakato unaojumuisha toba, imani, utii, huduma, na ustahimilivu!

◙ **"si wakati nilipokuwa tu, bali sasa zaidi hata nisipokuwepo mimi"** Ukristo ni vile tulivyo, na sivyo vile tutendavyo! Waamini lazima kutotenda matendo ili waonekana (kama vile. Flp. 1:27; Efe. 6:6; Kol. 3:22).

◙ **"utimizeni wokovu wenu wenyewe"** Hiki kitenzi ni neno la kimahesabu lililotumika kwa ajili ya kutatuwa matatizo yaliyoletwa. Muundo wake ni kauli ya kati (shahidi) shurutishi iliyoko kwenye wingi. Mistari ya 12-13 imekuwa mitizamo ya majadiliano mengi ya kithiolojia yanayohusianishwa na ukuu wa Mungu, uliotiwa msisitizo katika Flp. 2:13 (kama vile. Flp. 1 :6), na mapenzi huru ya nafsi za wanadamu zipatikanazo katika Flp. 2:1 2. Neno “wokovu”katika Flp. 2:1 2

1. linarejelea kwenye uhusiano wa kiroho wa waamini pamoja na Kristo. Paulo ametajwa kufanyika Mkristo katika Flp. 2:9-1 0. Huu ni mfano mwingine wa mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru, vyote vya mwanzo endelevu (kama vile. Flp. 2:1 6)
2. Hairejelei kwenye wokovu wa kiroho wa milele, bali huenda kwa
    a. Agano la Kale “ukombozi wa mwili"
    b. “ukamilifu wake,”kama ilivyofanyika katika Flp. 1:19

Hii dhana ya wokovu kama “ukamilifu” pia yaweza kuonekana katika Mdo. 4:10; 14:9; 27:34. Uanzilishaji wa neema ya Mungu na hitaji la mwitikio wa imani ya mwanadamu aliyetubu kwa uwazi unaonekana katika Efe. 2:8-9. Kiuhakika, waamini hawatembei katika wokovu wao, lakini baada ya kuokolewa, wanashirikiana na Roho kuishi katika ukomavu wa Kristo (kama vile. Flp. 2:14-17; Efe. 2:10; 5:18). Wokovu ni kwa wote na bure kabisa bali unahitaji mwitikio wa imani iliyo hai, inayoghalimu, ya toba na endelevu (kama vile. Mt. 13:44-46). Muktadha unazuia utafasiri wa kibinafsi kwa sababu ya vitenzi “yako/chako” katika Flp. 2:12, “wewe”katika Flp. 2:13, na vitenzi vyote viko katika hali ya umoja, ambavyo vinalirejelea kanisa zima la Filipi, na sio wokovu wa kiroho wa mtu binafsi. Kama inafanya kurejelea kwenye wokovu wa kiroho hilo ni la ushirika (kama vile Flp. 1:28) na endelevu (kama vile. 1Kor. 1 :18;1 5:2; 2 Kor. 2:15). Msukumo wa sura hii waweza kuwa ni kuwatia moyo ili kuendelea kuamini katika uwepo wa Mungu na mwitikio kwa ajili ya kanisa la Filipi (kama vile Gal. 3:4; 1 Kor. 1 5:2).

◙ **"kwa kuogopa na kutetemeka"** Hii ilikuwa ni nahau ya Agano la Kale ya kuonyesha heshima iliyochanganyikana na hofu kumwelekea Mungu (kama vile. Zab. 2:11 ;119:120). Linatumika mara nyingi katika maandiko ya Paulo (kama vile. 1 Kor. 2:3; 2 Kor. 7:1 5; Efe. 6:5). Waamini wanapaswa kukumbuka utakatifu wenye uvuvio wa Mungu!

**2:13 "kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu"** Neno "Mungu" ndilo linalowekwa kwanza katika sentensi ili kuleta msisisitizo. Neno “kazi”ni kauli tendaji yenye hali ya kuendelea ya wakati uliopo ambayo inarejelea kwenye “kazi endelevu yenye kuleta matokeo” (kama vile. Gal. 5:6). Hili ni neno tofauti ambatani toka Flp. 2:12 lakini likitoka katika mzizi mmoja. Kifungu “ndani yako”kiko katika hali ya wingi na chaweza kumaanisha “kati yenu,”ambalo linaangazia juu ya shughuli ya Mungu katika maisha ya kanisa (kama vile. Kol. 1 :27).

**NASB "kutaka kwenu,kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema"**
**NKJV "kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake"**
**NRSV "kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema”**

**TEV "kufanya utake na kuweza kutii kusudi lake"**
**NJB "kwa kusudi lake jema, aliwapeni ninyi nia na nguvu ya kutenda"**

Mienendo na matendo ya waamini inatolewa na Roho. Kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ya Flp.2:13a inajirudia kama kauli tendaji yenye kitenzijina cha wakati uliopo katika Flp.2:13b. Hili ni fumbo la ukuu wa Mungu na Agano alililolitengeneza Mungu. Wokovu ni zawadi huru na ujitoaji usiogharimu kitu! Paulo ni moja ya mfano mzuri aliyeokolewa chini ya neema ya Mungu (kama vile. 1 Kor. 15:10). Katika muktadha huu (kama vile. Gal. 3:4; 1 Kor. 15:2) mapenzi ya Mungu ni kwa ajili ya kanisa lililoko pamoja, lenye upendo, lenye ushuhuda na lenye nguvu.

**ANDIKO LA NASB LILILOBORESHWA):WAFILIPI 2:14-18**
**[14]Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano, [15] mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu, [16] mkishika neno la uzima; nipate sababu ya kuona fahari katika siku ya Kristo, ya kuwa sikupiga mbio bure wala sikujitaabisha bure. [17]Naam, hata nikimiminwa juu ya dhabihu na ibada ya imani yenu, nafurahi; tena nafurahi pamoja nanyi nyote. [18]Nanyi vivyo hivyo furahini, tena furahini pamoja nami.**

**2:14-16** Hii mistari ni sentensi moja katika Kiyunani.

**2:14 "yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano"** Kuna matengano ya wazi katika kusanyiko la Wafilipi. Ingawa chanzo kilikuwa hakijulikani ikiwa ni
1. Viongozi wa Kikristo waliokuwa na wivu (kama vile. Flp. 1 :14-17)
2. Wanawake wawili waliokuwa katika magomvi kati yao (kama vile. Flp. 4:2-3)
3. Walimu wa uongo (kama vile. Flp. 3:2 na kuendelea)

Andiko halielezei ikiwa alikuwa Paulo, Wakristo wengine au wasioamini ndio walikuwa chanzo cha manung'uniko.
**2:15**
**NASB "kwamba mpate kuwa "**
**NKJV "kwamba muweze kuwa"**
**NRSV, TEV "ili kwamba muwe"**
**NJB "ili kwamba muweze kubaki"**

Hii ni kauli ya kati (shahidi) tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Kama waamini wanavyochagua kuokolewa, vivyo hivyo wanalazimika kuchagua kuishi kwa ajili ya Kristo! Kitabu cha Agano Jipya ni
Agano la maisha mapya. Waamini wana haki na wajibu!

◙ **"wasio na lawama"** Kiuhalisia neno hili ni "pasipo na dosari" (kama vile. Flp. 3:6). Mwanzoni katika Agano Jipya lilirejelea kwa wanyama waliokuwa wakitolewa sadaka lakini likaja kutumika ki-sitiari kwa ajili ya wanadamu (kama vile. Nuhu, Mwa. 6:9,17 na Ayubu, Ayu. 1:1 ). Linatumika kwa Yesu katika Ebr. 9:14 na 1 Pet. 1:19. Hii ilikuwa njia nyingine ya kurejelea kwenye maisha ya mfano wa Yesu. haya ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya watu wake (kama vile. Law. 1 9:2; Kumb. 1 8:1 3; Mt. 5:48; 1 Pet. 1 :16). Mungu anahitaji kujiaksi mwenyewe kwa watu wake ("wana wa Mungu," kama vile. Efe. 1 :4, 6:27; Kol. 1 :22; Yuda 24) na kwa hiyo kuuvuta ulimwengu uliopotea kuja kwake (kama vile. Flp. 2:15). Angalia Mada Maalum: Pasipo lawama katika Kol. 1:22.

◙ **"wala udanganyifu"** Hili ni neno toka kwenye kiwanda cha divai kwa maana ya "divai ambayo haijachanganywa."linatumika katika Agano Jipya ki-sitiari kwa ajili ya usafi wa kimaadili (kama vile. Mt. 10:16; Rum. 16:19).

◙ **"wasio na ila"** Hili lilitumika katika tafasiri ya maandiko ya Kale ya Kiyunani (LXX) kwa wale wanyama waliotolewa sadaka. Neno mara nyingi limetumika ki-sitiari katika Agano Jipya kuonyesha usimamaji imara katika

maadili (kama vile. Efe. 1:4; Kol. 1:22; Yuda 24; Ufu. 14:5,6). Hii haimaanishi kutokuwa na dhambi, bali ni ukomavu.

◙ **"katika kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka"** Katika Kumb. 32:5 kifungu hiki kinawarejelea Waisrael, lakini katika muktadha huu kinarejelea kwenye ulimwengu usioamini. Huu ni mfano mwingine wa mwandishi wa Agano Jipya kujumuisha sura za Agano la Kale kuendana na wanadamu wote. Mzizi wa neno " mkosaji"na "ubaya"yanahusiana na dhana ya Agano la Kale la haki ya Mungu ambao umeelezewa kama "futi kamba." Mchepuko wowote toka kwenye kiwango chake ulielezewa kama "ukosaji"au "kupinda." Maneno haya yanatafasiriwa kwa kiingereza"dhambi,""uchafu"au "makosa."Tambua kuwa katika muktadha ni kanisa lililoitwa kuwa nuru katika ulimwengu wenye giza.

NASB **"mnaonekena kuwa kama mianga katika ulimwengu"**
**NKJV "mnaonekena mianga katika ulimwengu"**
**NRSV "mnaonekena kama nyota katika ulimwengu "**
**TEV "mkaonekane kama nyota zing'aazo angani"**
**NJB "mking'aa kati yao kama nyota ulimwenguni"**

Tambua wingi huonyesha ushirika wa muktadha. Hii hairejelei kwa mtu binafsi, kama katika Daniel 12, bali kwa makanisa kwa ujumla (kama vile. Flp. 2:12). Pamekuwepo na uwelewa mara mbili wa neno hili:
1. Kama inavyohusiana na Dan. 12:3, ambapo waamini wanaelezewa kama mianga au nyota ziangazazo mawinguni
2. Wale watoao mwanga (yaani., injili ya Flp. 2:16) katika ulimwengu (*kosmos*).katika Mt. 5:1 4-16 waamini wanapaswa kuwa watoa nuru, wakiwa na Yesu kama mfano (kama vile. Yn 8:1 2; Efe. 5:1 4).

**2:16**
**NASB, NKJV**
**NRSV "mkilisha neno la uzima"**
**TEV "mkiwapa neno la uzima"**
**NJB "mkiliendeleza neno la uzima"**

Hii ni tungo endelevu ya wakati uliopo ambayo inaweza kutafasiliwa kwa namna mbili: (1 ) "mkishikiria kwa nguvu," ikiwarejelea waamini kuendeleza uaminifu wao au (2) "mkiwalisha," inawarejelea waamini kama mashuhuda. Yote yangaliweza kufaa muktadha huu (hasa. Flp. 2:12).

◙ **"katika siku ya kristo"** Hii inarejelea kwenye ujio wa Yesu wa mara ya pili. Kifungu kama hicho kinatumika katika Flp. 1:6,10. Mara nyingi katika Agano Jpya ujio wa Yesu wa mara ya pili unatumika kama chachu kwa maisha ya Wakristo wa sasa. Angalia Mada Maalum katika Flp. 1:10.

◙ **"nipate kuona fahari katika Kristo"**Maisha ya ki-Ungu ya wakristo wa Filipi (yaani., kanisa) ulikuwa ni ushahidi wa utume wa Paulo (kama vile. Flp. 4:1; 1 The. 2:19-20).

◙ **"sikupiga mbio bure wala sikujitaabisha bure"** Kiuhalisia hili neno "nisipige mbio bure wala nisijitaabishe bure"(yaani., kwa kusudi la kuimalisha makanisa ya injili yenye nguvu). Hivi ni vitenzi vya njeo za wakati uliopita usiotimilifu. Neno la kwanza "kimbia,"lilitumika huko Misri kwenye mafunjo kwa maji yaliyo tiririka pasipo mwelekeo maalum. Katika muktadha huu, neno "bure" lazima lirejee makuzi ya mfanano wa Kristo (na sio wokovu wao) kama wanavyong'aa kwa ajili ya Kristo! Mara nyingi alielezea hamu yake kuhusu makuzi ya makanisa mapya na kuimalishwa kwao kwa kutumia sitiari kama vile (kama vile. Gal. 2:2; 4:1 1 ; 1 The. 2:1 ; 3:3,5). Mara zote Paulo aliongelea juu ya huduma yake kama alivyo mwana riadha anaposhindana (kama vile. 1 Kor. 9:24-27; 1 Tim.6:1 2; 2 Tim. 4:7).

**2:17,18** Mistari hii inayo maneno manne ambayo mara nyngi yanatafasiliwa "furahini." Hii inaonyesha kuwa hata katika matarajio ya mauti (adhabu kali ya Kirumi wakati akiwa gerezani), Paulo alikuwa na furaha kumtumikia

Kristo na wao (yaani., kanisa alilolianzisha). Pia aliwaonya kufanya kile kile. Waamini wanapaswa kuyatoa maisha yao kwa niaba yaw engine kama Kristo alivyotoa maisha yake kwa ajili ya wengine(kama vile. Flp. 2:5-1 1 ; 2 Kor. 5:1 3-1 4; Gal. 2:20; 1 Yn 3:1 6).

**2:17 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza inafikiriwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kusudi lake la kifasihi. Hili halipashwi kuchukuliwa kama tarajio la Paulo la hukumu ya kifo. Katika kitabu kile kile alielezea tumaini lake na matarajio yake ya kuachiwa (kama vile. Flp. 1:25; 2:24).

**NASB,NKJV "hata nikimiminwa juu ya dhabihu na ibada ya imani yenu"**
**NRSV "nimemiminwa kama sadaka"**
**TEV "damu ya maisha yangu yamemiminwa kama dhabihu"**
**NJB "damu yangu imemiminwa kama sadaka"**

Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo. Paulo anajitazama mwenyewe kama sadaka kwa ajili ya imani ya watu wa Filipi (yaani., watu wa mataifa, kama vile. Rum. 1 5:1 6). Paulo anarejewa kwenye huduma yake kama sadaka mara nyingi tu (kama vile. Rum. 1 5:1 6; 2 Tim. 4:6). Neno la Kiyunani linaaksi neno la Agano la Kale kwa ajili ya divai kuitoa kama sadaka (kama vile. Kut. 29:38-41 ; Hes. 1 5:3-1 0).

◙ **"hata nikimiminwa juu ya dhabihu na ibada ya imani yenu"** Paulo anayatazama maisha yake na huduma kama sadaka kwa Mungu (kama vile. Rum. 1 2:1 -2). Aliwatoa watu wa mataifa kama sadaka kwa Mungu(kama vile. Rum. 1 5:1 6). Yesu alikuwa sadaka kwa ajili ya wanadamu wote(kama vile. Isaya 53; Marko 1 0:45; 2 Kor. 5:21 ; Efe. 5:2). Waamini wanamuiga Yesu na Paulo (kama vile.4:1 9). Neno la Kiyunani lililotafasiriwa kama "huduma" *(leitourgia*) linatokana na neno la Kiingereza "liturujia."lilitumika katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) kwa ajili ya kuhani aliyekuwa akitoa dhabihu. Hii inaweza kuwa kidokezo kingine cha sadaka binafsi ya Paulo kwa ajili ya injili

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 2:19-3:1**
**[19] Walakini natumaini katika Bwana Yesu kumtuma Timotheo afike kwenu karibu, nifarijiwe na mimi, nikiijua hali yenu. [20] Maana sina mtu mwingine mwenye nia moja nami, atakayeiangalia hali yenu kweli kweli. [21] Maana wote wanatafuta vyao wenyewe, sivyo vya Kristo Yesu. [22] Ila mwajua sifa yake, ya kuwa ametumika pamoja nami kwa ajili ya Injili, kama mwana na baba yake. [23]Basi, natumaini kumtuma huyo mara, hapo nitakapojua yatakayonipata. [24]Nami naamini katika Bwana ya kuwa nitakuja na mimi mwenyewe hivi karibu. [25]Lakini naliona imenilazimu kumtuma kwenu Epafrodito, ndugu yangu, mtenda kazi pamoja nami, askari pamoja nami; tena ni mtume wenu na mhudumu wa mahitaji yangu. [26]Kwa kuwa alikuwa na shauku kwenu ninyi nyote, akahuzunika sana, kwa sababu mlisikia ya kwamba alikuwa hawezi. [27]Kwa maana alikuwa hawezi kweli kweli, karibu na kufa; lakini Mungu alimhurumia; wala si yeye peke yake, ila na mimi pia; nisiwe na huzuni juu ya huzuni. [28] Kwa hiyo nimefanya bidii nyingi zaidi kumtuma, ili mtakapomwona tena mpate kufurahi, nami nipunguziwe huzuni yangu. [29]Mpokeeni, basi, katika Bwana, kwa furaha yote, mkawahesabu watu kama huyu kuwa watu wa kuheshimiwa. [30] Maana kwa ajili ya kazi ya Kristo alikaribia kufa akaponza roho yake; ili kusudi ayatimize yaliyopungua katika huduma yenu kwangu. [3-1] Hatimaye, ndugu zangu, furahini katika Bwana. Kuwaandikieni mambo yale yale hakuniudhi mimi, bali kutawafaa ninyi**

**2:19 "lakini natumaini katika Bwana kumtuma"** Paulo alitambua maisha yake na mipango yake sio ya kwake, bali ilikuwa inadhibitiwa kwa mapenzi ya Mungu (kama vile. Flp. 2:24; 1 Kor. 4:19; Yakobo 4:13-17).

◙ **"nifarijiwe na mimi"** Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo. Neno hili limetumika katika maana ya "kuagana"na"kutakiana heri"na limepata kuonekana kwenye makaburi mengi ya kale. Hili ni tumizi tu katika Agano Jipya na linaonekana kutumika kwa maana ya "hali ya furaha" (NRSV).

**2:20**
**NASB "mwenye nia moja nami"**

**NKJV "mwenye fikra kama yangu"**
**NRSV "kama yeye"**
**TEV "mwenye kushiriki fikra zangu"**
**NJB "anaye waangalia faraja yenu"**

Kiuhalisia neno "nafsi zenye kufanana" (*isopsuchos*) linamaanisha kuwa Timotheo alikuwa na upendo wenye kufanana na wa Paulo kwa kanisa la Wafilipi. Neno ambatani lenye kufanana na "mwenye fikra kama" (*sumpsuchos*) linatumika katika Flp. 2:2.

**NASB, NRSV "atakaye iangalia hali yenu kweli kweli"**
**NKJV "atakaye iangalia hali yenu kwa uaminifu"**
**TEV "atakaye waangalia kweli"**
**NJB "atakaye iangalia faraja yenu"**
Ki-asili hili neno lilimaanisha "mzaliwa halali,"lakini lilikuja tumika ki-sitiari kwa ajili ya neno "halisi."katika mstari huu lina kidokezo chanya.

**2:21** Haijulikani ni nani Paulo alikuwa akimrejelea, lakini dhahili alimaanisha ushiriki wake kwenye huduma. Yumkini hii inahusiana na wachungaji wenye wivu katika kanisa la Rumi (kama vile. Flp. 1:14-17). Wengine wanaliona kama linahusiana na walimu wa uongo wa sura ya 3. Hata hivyo, hili linaonekana kuwa si la kawaida kwa sababu Paulo asingewarejelea wao kama "wahubiri wa Kristo" (kama vile. Flp. 1 :1 5). Mfano mzuri wa aina hii ya fursa mchanganyiko ambazo Paulo anazirejelea zinaweza onekana kwa Dema (kama vile. 2 Tim. 4:10). Shauku binafsi zilikuwa, tatizo lililokuwa linaendelea (kama vile. 1 Kor. 10:24; 13:5; Flp. 2:4).

**2:22 "sifa yake"** Hili neno limetumika kwa ajili ya sarafu au chuma cha thamani kuthibitisha uhalisia wake. Timotheo amekuwa na Paulo huko Filipi kama ilivyo andikwa katika matendo 16 na 20. Alishuhudiwa vizuri na kanisa na aliwapenda mno.

**MADA MAALU: MANENO YA KIYUNANI KWA AJILI YA MAJARIBIO NA VIDOKEZO VYAKE**

Kuna manaeno mawili ya Kiyunani ambayo yana kidokezo kwa ajili ya kumjaribu mtu kwa kusudi fulani.

1. *Dokimazō, Dokimion, Dokimasia*

   Neno hili ni neno la mtu yule afuaye vyuma kwa ajili ya kujaribu uhalisia wa kitu fulani (yaani, kistiari mtu fulani) kwa moto (tazana Mada Maalumu: Moto). Moto hudhihilisha chuma halisi na huteketeza (yaani, husafisha) dongo la chuma. Kitendo hiki cha kifizikia kinakuwa nahau yenye nguvu kwa Mungu na/au Ibilisi na/au binadamu kuwajaribu wengine. Neno hili linatumika tu katika maana chanya ya kujaribu kwa kuangalia hadi kuufikia ukubalifu (tazama Mada Maalumu: Mungu Huwajaribu Watu Wake [Agano la Kale).

Linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya

a. Madume ya ng'ombe – Luka 14:19
b. sisi wenyewe – 1 Kor. 11:28
c. imani yetu – Yakobo 1:3
d. hata Mungu –Ebr. 3:9

Matokeo ya majaribu hayajafikiriwa kuwa chanya (kama vile. Rum. 2:18; 14:22; 16:10; 2 Kor. 10:18; 13:3,7; Flp. 2:27; 1 Pet. 1:7), hivyo, neno husilisha wazo la mtu aliyepimwa na kuhakikishwa

a. kuwa wa thamani
b. kuwa wazuri
c. kuwa halisi
d. kuwa wa maana
e. kuwa wa kuheshimiwa

2. Peirazō, Peirasmus

Neno hili mara nyingi lina maana nyingine ya kupimwa kwa kusudi la utafutaji au ukataaji. Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu ya Yesu nyikani.

   a. Linabeba jaribio la kumtega Yesu (kama vile Mat. 4:1; 16:1; 19:3; 22:18, 35; Marko 1:13; Luka 4:2; Ebr. 2:18).
   b. Neno hili (*peirazōn*) linatumika kama wadhifa kwa Ibilisi katika Mat. 4:3; 1 The. 3:5 (yaani, "mjaribu").
   c. Matumizi
      1) Lilitumiwa na Yesu alipokuwa akiwaonya wanadamu kutomjaribu Mungu (kama vile Mat. 4:7; Luka 4:12, [au Kristo kama vile 1 Kor 10:9]).
      2) Pia linamaanisha jaribio la kufanya kitu fulani ambacho kimeshindikana (kama vile Ebr.11:29).
      3) Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu na masumbufu ya waamini (kama vile 1 Kor. 7:5; 10:9, 13; Gal. 6:1; 1 The. 3:5; Ebr. 2:18; Yakobo. 1:2, 13, 14; 1 Pet. 4:12; 2 Pet 2:9).

◙ **"kama Mwana na Baba yake"** Hii ilikuwa ni namna ya Paulo kumrejelea msaidizi mzuri, mwema na mwaminifu (kama vile.Tito 1:4). Hata hivyo, kwa suala la Timotheo, pia lilimaanisha kuongoka (kama vile. 1 Tim. 1:2; 2 Tim. 1 :2).

**2:23 "hapo nitakapoyajua yatakayo nipata"** Paulo alitarajia kitu kingine kuhusu suala lake la kisheria mapema iwezekanavyo, lakini bado ilikuwa haijulikani ikiwa atahukumiwa kifo au ataweza kurudi tena na kuweza kuwatembelea. Mpango wa Paulo wa hiyo barua yake akiwa gerezani unaonekana kuwa kwa: (1 ) Wakolosai, Waefeso, na Filemoni mapema katika mchakato wa shitaka na (2) Wafilipi kuelekea hitimisho la shitaka lenyewe.

**2:24 "naamini"** Hii ni kauli timilifu tendaji elekezi iliyotumika kwa maana ya "kuwa na uhakika au kutokuwa na shaka" (kama vile. 2 Kor. 2:3; Ebr. 13:18). Matumaini ya Paulo yalikuwa katika Bwana (Flp. 2:24), katika Roho (1 :1 9b), na katika maombi yao (1:19a). Paulo alikuwa na matumaini zaidi katika kufunguliwa kwake toka gerezani katika kitabu hiki kuliko cha Wakolosai au Waefeso.

**2:25 "naliona"** Hizi ni nyaraka za wakati uliopita usiotimilifu. Paulo alikuwa akiandika kana kwamba alikuwa amekwisha tenda.

◙**"inanilazimu"** Hili ni neno la nguvu la Kiyunani (kama vile. Mdo. 1:24; 13:46; 2 Kor. 9:5; Ebr. 8:3). Limewekwa kuwa mwanzo wa sentensi kwa ajili ya msisitizo.

◙ **"Epafrodito"** Jina lake linahusiana na mungu wa kike, Afrodito. Halifanani na Epafrasi aliyetajwa katika Kol. 1 :7; 4:12; Filemon 23, ingawa although Epafrasi ni kifupisho cha Epafrodito.

◙ **"ndugu yangu, mtenda kazi pamoja nami"** Paulo alimwona mtu huyu kuwa mshirika wa karibu. Inavyoonekana alitumwa na Wafilipi kupeleka zawadi ya fedha kwa Paulo akiwa gerezani kwa ajili ya kumsubiri na kumsaidia. Akiwa kule,akaugua karibu kufa (Flp. 2:27). Paulo alimrudisha kwenye kanisa lake la nyumbani na kuelezea shukrani zake kwao kwa ajili ya kumtuma. Paulo alihitaji kanisa lisije likamkasirikia kwa vile amerudi mapema.

◙ **"mtume wenu na mhudumu wa mahitaji yangu"** "Mtu anayetumwa" ni "mtume" lenye maana "yeye aliyetumwa." Hapa, linatumika kwa maana isiyo ya kifundi (kama vile. Flp. 4:18; 2 Kor. 8:23). Kumbuka muktadha unapima maana ya neno, na sio msamiati/kamusi.

**2:26 "kwa kuwa alikuwa na shauku kwenu ninyi nyote"** Hili ni neno la nguvu lililotumiwa na Paulo akitamani kuliona kanisa hili kama ilivyo katika Flp. 1:8 na 4:1. Flp. 1:8 na 4:1 . Epafrodito alipatamani nyumabani vile vile pia alikuwa mdhaifu kimwili.

**NASB, NKJV**

**NRSV "akahuzunika sana"**
**TEV "alijawa huzuni"**
**NJB "alikuwa na wasiwasi"**

Hili neno laweza maanisha “kupakumbuka nyumbani”kutokana na tumizi moja lililopatikana katika lugha ya Koine iliyoandikwa kwenye mafunjo huko Misri. Hapa linaelezea maumivu ya kiakili juu ya taarifa ya udhaifu wake kimwili baada ya kulifikia kanisa la Wafilipi. Neno lile lile linatumika kwa ajili ya maumivu ya Yesu akiwa Gethsemani (kama vile. Mt. 26:37; Marko 14:33).

**2:27 "maana alikuwa hawezi kweli kweli hata kufa"** Inavyoonekana Paulo hakuweza kumponya (kama vile. Fil. 2:30). Ni vigumu kupima lini na na kwa namna gani Mtume alitumia karama ya uponyaji na kwa nini hawakuweza kufanya hivyo kwa baadhi ya matukio (kama vile. 2 Kor. 12; 2 Tim. 4:20). Uponyaji hauji wenyewe. Je wahubiri wote wa leo wanaodai kuwa shauku ya Mungu ni kuona wote wanapona kweli wanaamini kuwa Paulo Mtume hakuwa na imani thabiti kwa ajili ya tukio hili? Imani sio kitu muhimu cha uponyaji wa ki-Ungu, bali mapenzi ya Mungu na mpango kwa yule aliyeponywa. Paulo alihitaji Wafilipi wajue kuwa Epafrodito alikuwa anaumwa kikweki kweli. yawezekana baadhi katika kanisa wangalihuzunika kama angelirudi nyumbani mapema (kama. Flp. 2:28-30).

**2:30 "akiyahatarisha maisha yake"** Hii ni kauli ya kati yenye hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu ambayo kikawaida inamaanisha “kuhatarisha.” Lazima irejelee kwenye ugonjwa wake. Paulo analitumia neno la Kiyunani “nafsi” (*psychē*) kuyarejelea maisha ya Epafrodito. Biblia haifuatishi dhana ya Kiyunani kuwa wanadamu wana “nafsi isiyokufa”lakini dhana ya Kiebrania kuwa wanadamu ni “nafsi inayoishi” (kama vile. Mwa. 2:7). Mwili wa asili ni mpaka wa nje wa maisha yetu hapa duniani. Wanadamu wanahusishwa na sayari hii kama wanyama, lakini pia wanahusishwa na Mungu. Wanadamu, hata hivyo, ni wamoja, sio sehemu mbili au tatu zenye kukinzana (kama vile. 1 The. 5:23; Ebr. 4:12). Umoja huu unajadiliwa katika Agano Jipya kwa hali ya kutofautiana:
1. Mtu wa kale –mtu mpya
2. Hali ya nje –hali ya ndani
3. Enzi ya sasa na enzi ijayo
4. Mwili –roho
5. maisha ya ufufuo-siku ya ufufuo

Uwe mwangalifu na thiolojia ya kuyahakiki maandiko inayochagua mistari miwili au mitatu nje ya muktadha wa kifasihi na kudai kuwa ndio “ya muhimu”kuweza kuitafasiri mingine iliyobaki ndani ya Biblia. kama jawabu la utafasiri kwenye maandiko ni ubinadamu wa pande tatu (mwili, nafsi na roho) hivyo I wapi sura ya wazi yenye mafundisho toka kwa Yesu au Paulo? Yeyote anaweza chukua mstari uliojitenga na kudai kuwa ndio jawabu. Hili lingalimaanisha kuwa ukweli wa Mungu haukuandikwa kiusahihi kwa ajili ya mwanadamu wa kawaida, bali ni kwa kundi lile la wasomi wenye maarifa ya siri kuhusu huu mstari wenye “jawabu”au mtizamo (wa wenye ujuzi wa kipekee). Mtazamo huu wa utafasiri ni ugonjwa katika Ukristo wa leo.

**NASB "kusudi ayatimize yaliyopungua katika huduma yenu kwangu"**
**NKJV "kuyatoa yaliyopungua katika huduma yenu kwangu"**
**NRSV "kuitengeneza ile huduma ambayo hamkuweza kunipa"**
**TEV "ili kwamba mnipe msaada ule ambao hamkunipa"**
**NJB "kufanya kazi kwangu amabyo hamkuifanya ninyi"**

Katika Kiingereza hili linasikika kwa namna Fulani ya kinyume, hata hivyo, ilikuwa ni nahau ya Kiyunani ikionyesha ukosefu wa fursa ikiwa na shauku chanya (kama vile. Flp. 4:10; Rum. 1:10).

**3:1 "hatimaye"** Kiuhalisia hili neno ni “yaliyobaki” (*loipon*). Paulo mara zote analitumia neno hili kuifanya tafasiri kuwa somo jipya, mara nyingi akiwa anafunga barua yake (kama vile. 2 Kor. 13:1 1 ; Efe. 6:10; 1 The. 4:8; 2 The. 3:1 ). Kuna aina mpya ya utafasiri katika Agano Jipya iitwayo "muundo wa urudiaji wa vifungu" inayotafuta kutambua aina ya mgeuzo wa maelezo kwa mfano (mfano. A, B, C, B, A). Kipengere hiki cha mfanano kinajulikana

toka katika Agano la Kale na wengi wanadai kuwa pia kilikuwa cha kawaida katika fikra za Kiyunani. Mara zote hitimisho la Paulo linaonekana kuingiza ukweli wa kati wa muundo huu wa ufanano.

◙ **"furahini katika Bwana"** Hii ni maudhui yanayo jirudia, furahini katika mateso, furahini katika wokovu, furahini katika Yeye!

◙**"kuwaandikieni mambo yale yale hakuniumizi mimi, bali kutawafaa ninyi"** Kweli muhimu zinahitaji kurudiwa rudiwa kwa ajili ya kusisitiza, kuleta matokeo, kuwashikilia. Paulo lazima angalisema mambo haya kwa kusimulia kwa mdomo pindi akiwa Filipi na yawezekana angewaandikia kwenye barua yake ya nyuma.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Elezea maana ya Flp. 2:12-13 (kwa namna zote kimuktadha na kitheolojia)
2. Kwa nini Wakristo wa kule Filipi walikuwa wanalalamika na kugombana (Flp. 2:14)?
3. Kwa nini wahudumu wenza wa Paulo walionekana kuwa mitizamo tofauti (Flp. 2:21)?
4. Kwa nini Paulo hakumponya Epafrodito?

# WAFILIPI 3

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Haki ya Kweli | Yote kwa ajili ya Kristo | Onyo | Haki ya Kweli | Njia ya Kweli ya Wokovu wa Mkristo |
| 3:1-11 | 3:1-11 | 3:1b<br>3:2-4a<br>3:4b-6<br>3:7-11 | 3:1-11 | 3:1b-16 |
| Shinikizo Kuihusu Marko | Shinikizo Kulihusu lengo | Ukiri na Ushawisi | Kwenda moja kwa moja hadi kwenye Lengo | |
| 3:12-16 | 3:12-16 | 3:12-16 | 3:12-16<br>3:15-16 | |
| | Wenyeji wetu ni mbinguni | | | |
| 3:17-4:1 | 3:17-4:1 | 3:17-4:1 | 3:17-21 | 3:17-4:1 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka**"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii Mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAFILIPI 3: I**
**Hatimaye, ndugu zangu, furahini katika Bwana. Kuwaandikieni mambo yale yale hakuniudhi mimi, bali kutawafaa ninyi.**

**3:1"Hatimaye"** Kiuhalisia hii ni "kuhusu wengine" (*loipon*). Paulo mara nyingi alilitumia neno hili ili kufanya mabadiliko kwa jambo jipya, mara nyingi kati ukaribu wa barua (kama vile 2 Kor. 13:11; Efe. 6:10; 1 The. 4:8; 2 The. 3:1).

◙**" furahini katika Bwana"** Hii ni dhamira inayorudiwa mara kwa mara. Furahini katika mateso, furahini katika wokovu, furahini katika Yeye!

◙**" Kuwaandikieni mambo yale yale hakuniudhi mimi, bali kutawafaa ninyi"** Kweli zilizo kuu zinahitajika kurudiwa rudiwa kwa ajili ya msistizo, matokeo na zuio. Paulo lazima angeyasema mambo haya kwao kuwasimulia akiwa huko Filipi na yumkini angeliwaandikia katika ile barua ya awali.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAFILIPI 3:2-6**
**[2] Jihadharini na mbwa, jihadharini na watendao mabaya, jihadharini na wajikatao. [3] Maana sisi tu tohara, tumwabuduo Mungu kwa Roho, na kuona fahari juu ya Kristo Yesu, wala hatuutumainii mwili. [4] Walakini mimi ningeweza kuutumainia mwili. Mtu ye yote akijiona kuwa anayo sababu ya kuutumainia mwili, mimi zaidi. [5]Nalitahiriwa siku ya nane, ni mtu wa taifa la Israeli, wa kabila ya Benyamini, Mwebrania wa Waebrania, kwa habari ya kuishika torati, ni Farisayo, [6] kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi Kanisa, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia.**

**3:2"Jihadharini na mbwa"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopoya "iweni macho" (*blepō*), iliyorudiwa mara tatu kwa ajili ya msistizo. Walimu wa sheria za Kiyahudi waliwaita watu wa Mataifa "mbwa." Paulo alikijadili kifungu hiki ili kuwarejelea walimu wa uongo. Neno "mbwa" katika Agano la Kale lilirejelea (1) malaya wa kiume (kama vile Kumb. 23:18) ama (2) watu waovu (kama vile Zab. 22:16,20). Kiutamaduni nahau hii inarejelea juu ya mbwa chotara wa mitaani walio waovu. Hawa walimu wa uongo walikuwa kama mbwa wenye njaa na wale waovu wasioamini (kama vile Mt. 7:6; Gal. 5:15; Ufu. 22:15).

**NASB "tohara ya uongo"**
**NKJV "ya mateso"**
**NRSV "ile iutesao mwili"**
**TEV "wasistizao juu ya kuukata mwili"**
**NJB "mateso binafsi"**

Hii inarejelea juu ya msistizo wa wale walioshikilia sana Sheria na tamaduni za Kiyahudi kuhusu tohara (kama vile Matendo 15:1,5; Gal.5:2-3, 12). Kimsingi alifundisha kwamba mtu anapaswa kuwa Myunani kabla ya kuwa Mkristo. Kuwa Myahudi kulihusisha kutahiriwa, kujibatiza mwenyewe, na kutoa dhabihu ndani ya hekalu. Tohara ilikuja kuwa sitiari iliyogeuka kuwa "nira" ya Sheria ya Musa.

**3:3**
**NASB, NKJV**
**NRSV "tohara ya kweli"**
**TEV "tohara iliyo ya kweli"**
**NJB "watu wa kweli wa ile tohara"**

Hii tohara/imani ya tohara inabainishwa katika Rum. 2:28-29 na Gal. 3:29. Katika njia nyingine kanisa ni Israel ya kiroho (kama vile Gal. 6:16). Katika Agano la Kale, tohara ilikuwa alama ya Agano la Ki-Ibrahimu (kama vile. Mwa. 17:11,14,23-25). Hii ilihusisha mtazamo mwema, si kama utaratibu wa kimwili (kama vile Law. 26:41; Kumb. 10:16; na Yer.4:4). Tohara ya kiroho iliyo ya kweli inabainishwa kwa kauli tatu tendaji za wakati uliopo yenye hali ya kuendelea:

1. yule amwabuduye ndani ya ama kwa Roho Mtakatifu wa Mungu
2. yule amutukuzaye katika Kristo

3. yule asiyeweka tumaini lake kwake katika mwili

**NASB " kuona fahari juu ya Kristo Yesu"**
**NKJV "kufurahi katika Kristo Yesu"**
**NRSV "na kuona fahari katika Kristo Yesu"**
**TEV "kufurahi katika maisha yetu kndani ya umoja pamoja na Kristo Yesu"**
**NJB "na kumfanya Kristo Yesu kuwa afahari yetu"**

Paulo mara nyingianalitumia neno hili (kama vile Rum. 2:23; 3:27; 4:2; 5:2,3,11; 11:18; 15:17; 1 Kor. 1:31; 3:21;4:7; 5:6;7:14; 8:24; 9:2,4,11, 15,16; 10:8,13,15,16; 11:10,12; 2 Kor. 1:14; 5:12; 7:4; 10:17;11:17,18,30;12:1,5,6,9,11; Gal. 6:4,13,14; Efe. 2:9; Flp. 1:26; 2:16; 3:3; 2 The. 1:4). Hili linatafsiriwa kulingana na muktadha kama "furahi," "fahari," "fahari ya tumaini," ama "nderemo."

**NASB " hatuutumainii mwili"**
**NJJV, NRSV "hatutumaini kati mwili"**
**NJB "mambo ya nje tu hayatuthamini"**
**"si kwa sifa za mwili"**

Neno hili linamaanisha fahari ya matumaini katika kila kitu ama mtu fulani. Kifungu hiki kiko tofauti na kile kifungu cha awali. Uhusiano wa Paulo na Kristo na ufahamu wake wa injili ulimpa matumaini.Hiki kinaweza kurejerea juu ya fahari ya Kiyunani kutoka unasaba wa Abrahamu (kama vile Flp. 3:4-5; Mt. 3:9; Yohana 8:33,37,39). Yumkini hili linarejelea juu ya taratibu za Kiyahudi kama tohara (kama vile Matendo 15 na Wagalatia).

**3:4"ningeweza"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza ambayo inadhahaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi ama sababu za kiuandishi.

◙**"Walakini mimi "** Paulo pasipo matakwa yake anazitofautisha sifa zake za Kiyahudi na zile za wale washika sheria na tamaduni za Kiyahudi. Hawa hawakuwa na ubaguzi ama ubora wa kidini juu yake (kama vile Flp. 3:5-6; 2 Kor. 11:22). Paulo anajitetea kwa sababu kwa kumshambulia, walikuwa wakijaribu kuifedhehesha injili.

**3:5"Nalitahiriwa siku ya nane"** Wayahudi walitahiri siku ya 8 baada ya kuzaliwa (kama vile Mwa. 17:9-14; Law. 12:3). Flavius Josephus anatwambia kwamba Waarabu walitahiri yapata umri wa miaka 13, kwa kufuata Mwa. 17:23-27.

◙**"wa taifa la Israeli"** Kwa orodha ya upendeleo wa watu wa Kiyahudi, tazama Rum. 9:4-5, 11:1.

◙**"kabila ya Benyamini "** Huyu alikuwa mfalme wa kwanza wa kabila la Israeli, Sauli. Hii pia ilikuwa sehemu ya ufalme wa kusini, Yuda, baada ya kugawanyika kwa makabila mnamo 922 k.k.

◙**" Mwebrania wa Waebrania"** Kwa vyovyote hii nahau inarejelea juu ya (1) ubaguzi halisi wa unasaba ama (2) kuzungumza kwake lugha ya Kiebrania (Kiaramu).

**3:6"kwa habari ya kuishika torati, ni Farisayo"** Hili lilikuwa dhehebu lisilobadilika na lilifahamika sana ndani ya Dini ya Kiyahudi ambayo iliokua wakati wa kipindi cha Wamakabayo (kama vile Yohana 3:1). Hawa walitamani kuishikiria Sheria ya Musa katika kila kipengele (kama vile Matendo 26:4-5). Walipewa maagizo kwa kila eneo la maisha ambayo yamekuwa siku zote katika mjadala kati ya shule mbili za Walimu wa Sheria (Shammai na Hillel). Baadaye masimulizi yao yaliungnishwa kwa pamoja katika kitabu cha sheria za Kibabeli na Kipalestina. Nikodemo na Yusufu wa Arimathea walikuwa mfano dhahiri ya utiifu wao na kujitolea kwa dhati.

**MADA MAALUM : MAFARISAYO**

I. Neno lilikuwa na uwezekana wa kuwa na asili moja kati ya hizi zifuatazo:

A. “Kujitenga.” Kundi hili lilianza wakati wa ufuasi wa kiongozi wa Kiyahudi Yuda wa karne ya pili ( huu ni mtizamo mpana sana unaokubalika), na kujitenga wao wenyewe toka kwenye umma wa watu ili kutunza tamaduni simulizi za sheria ya Musa (yaani., mienendo ya kichini chini ya Kiyahudi iliyopatikana karne ya 18).

B. “Kugawa” Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiebrania (BDB 827, BDB 831 I, KB 976); yoye yakimaanisha “kugawanya.” Baadhi ya wasomi wanasema linamaanisha mfasili (kama vile Neh. 8:8; 2 Tim. 2:15).

C. “Uajemi.” Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiarama (BDB 828, KB 970). Baadhi ya mafundisho ya mafarisayo yanaingiliana na wafuasi wa dini za Kiislamu za awali toka Uajemi zilizoanzishwa na Zoroaster (angalia maada maalumu Uovu).

II. Pamekuwepo na nadharia nyingi nani alianzisha Ufarisayo.

A. Kikundi cha kithiolojia cha dini ya mwanzo ya Kiyahudi (angali., Yusufu)

B. Kikundi cha kisiasa toka kipindi kile cha Herode

C. Kikundi cha kisomi cha wafasiri wa sheria za musa ambao walitaka kuwasaidia watu wa kawaida kuelewa Agano la Musa na tamaduni simulizi zilizowazunguka.

D. Mienendo ya chini kwa chini ya waandishi, kama vile Ezra na Sinagogi kuu, wakigombea uongozi wa ukuhani mkuu katika hekalu.

Yaliundwa nje ya misigishano na

1. Makabaila wasiokuwa Wayahudi (hasa Antiokia IV).
2. jamii ya watu wakuu dhidi ya watu wa kawaida
3. wale waliojifungamanisha kwenye maisha ya agano dhidi ya Wayahudi wa kawaida toka Palestina

III. Habari zetu kuwahusu wao zinatoka

A. Yusufu, aliyekuwa mfarisayo
   1. Vitu vya kale vya Kiyahudi
   2. Vita vya Wayahudi

B. Agano Jipya

C. Asili ya awali ya Kiyahudi

IV. Mafundisho yao makuu

A. Imani ya kuja kwa Masiha, iliyoshawishiwa na waandishi wa Kibiblia wa Kiyahudi wenye fasihi ya kimaono kama vile Enock.

B. Imani ya kwamba Mungu yu hai katika maisha yetu ya kila siku. Hii moja kwa moja ilikuwa kinyume na Masadukayo (kama vile Mdo 23:8). Mafundisho mengi ya Kifarisayo yalikuwa ni kijazilizo cha yale ya Masadukayo.

C. Imani katika maelekezo ya kimwili baada ya maisha yaliyolenga maisha ya duniani, yaliyojumuisha zawadi na adhabu (kama vile Dan.12:2)

D. Imani katika mamlaka ya Agano la Kale vile vile simulizi za kitamaduni (Talmud). Walitambua kuwa watiifu kwa amri za Mungu za Agano la Kale kama zilivyo tafasiliwa na shule za wasomi wa sheria za Kiyahudi (Shammai, asiyependa mabadiliko na Hillel, anayependa mabadiliko). Watafasiri wa sheria za Kiyahudi walisimamia juu ya mazungumzo kati ya wanasheria/walimu wa falsafa mbili zinazokinzana, mmoja asiyependa mabadiliko na mwingine anayependa mabadiliko. Mazungumzo haya ya kisimulizi juu ya maana ya andiko hatimaye likaandikwa kwa miundo miwili.: sheria za kiibada za Wababel na sheria za

kiibada zisizo kamili za Wapalestina. Waliamini kuwa Musa alipokea hizi sheria za mdomo kwenye Mlima Sinai. Mwanzo wa haya mazungumzo ya kihistoria yalianzishwa na Ezra na watu wa "Sinagogi kuu" (baadaye wakaitwa Sanhedrin)

E. Imani ilioanzishwa juu ya mafundisho ya kithiolojia ya kimalaika. Haya yalijumuisha viumbe wazuri na wabaya. Hili lilianzia huko Uajemi yenye pande mbili na fasihi za Kiyahudi zenye mwingiliano na Biblia.
F. Imani juu ya mamlaka ya kifalme ya Mungu, lakini pia mazoezi ya utashi huru wa binadamu(yetzer).

V. Nguvu ya mabadilko ya Kifarisayo.

A. Walipenda , waliheshimu, kuamini mafunuo ya Mungu (yaani., yote, yakijumuisha sheria, Manabii, Maandiko, na simulizi za kitamaduni)
B. Walijitolea kuwa wafuasi wenye haki (yaani., maisha ya kila siku na imani) wa mafunuo ya Mungu. Walitaka "Israel yenye haki" kutimiza ahadi ya kinabii ya siku mpya yenye mafanikio.
C. Walitetea kuwepo usawa na jamii za Kiyuda, ambao unajuisha ngazi zote za watu, kwa maana kuwa, walikataa uongozi wa kikuhani (yaani., masadukayo) na thiolojia(kama vile Mdo 23:8).
D. Walipigania kitu halisi cha mtu kwenye agano la sheria za Musa. Walitetea au kudai mamlaka ya Mungu, lakini pia wakashikilia kwenye hitaji la utendaji huru wa mwanadamu
E. Agano Jipya linataja mafarisayo mbali mbali walioheshimika (yaani., Nikodemu, Mtawala tajili kijana, Yusufu wa Alimataya).

Walikuwa ni kundi hilo tu la dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza kuhimili uharibifu wa Yerusalem na hekalu toka kwa Warumi mwaka wa 70 B.k. wakawa ni dini ya Kiyahudi ya kisasa

◙**"juhudi"** Shauku haitoki kwa Mungu moja kwa moja (kama vile Rum. 10:2).

◙**"mwenye kuliudhi Kanisa"** Sauli kwa udhihirisho alifungwa na huenda hata kuua waamini (Matendo 8:3; 9:1,13,21; 1 Kor. 15:9; Gal. 1:13-14,23; 1 Tim. 1:13). Hili rejeo linaonekana wazi kwa Kanisa la wote (kama vile Mt. 16:18; Efe. 1:22; 3:10,21; 5:23-32). Tazma Mada Maalum: Kanisa (*Ekklesia*) katika Kol. 1:18.

◙**"kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia"** Paulo alikuwa akinena na uelewa wake wa Sheria ya Musa kabla ya Ukristo wake (kama vile Marko 10:20) na fasiri yake (Buku la Sheria na maadili ya Kiyahudi). Ikiwa hawa manabii wa uongo walitaka kufurahi ndani ya Uyahudi wao, Paulo pia anaweza kuwa (kama vile 2 Kor. 11:16-23). Tazama Mada Maalum katika Efe. 4:24. Neno "kutokuwa na hatia" kiuhalisia lilitumika katika kitabu cha Agano la Kale kwa ajili ya dhabihu ya wanyama (kama vikle Flp. 2:15). Hili halimaanishi "kutokuwa na dhambi" (kama vile Mwa. 6:9,17; Ayubu 1:1), bali yule aliyekamilisha kile ambacho ni kuyakamilisha mapenzi ya Mungu.

Tazama Mada Maalum: Kutokuwa na Lawama katika Kol. 1:22.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAFILIPI 3:7-11**
**7 Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo.**
**8 Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo;**
**9 tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani;**
**10 ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake;**
**11 ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya wafu.**

**3:7"naliyahesabu kuwa hasara"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu (yenye ushahidi) . Paulo alikuja kuona namna taratibu na kanuni zilizokuwa hazitumiki zilivyokuwa kama njia kuu ya kupata na kuishikilia

haki ya kweli (kama vile Kol. 2:16-23). Huu ulikuwa uhamisho mkuu kitheolojia wa kimsistizo kutoka mafunzo ya awali ya kidini ya Paulo na badiliko la maisha lililotokea akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo.9:1-22; 23:3-16, 26:9-18).

**3:8-11** Mistari hii ni sentensi moja katika Kiyunani.

**3:8"naliyahesabu"** Hii ni kauli ya kati elekezi (yenye ushahidi) ya wakati uliopo. Neno hili linatumika mara tatu katika Flp. 3:7, 8. Hili neno la kibiashara "kupoteza" Kipindi chote cha mwanzo Paulo aliamini katika haki (ubora wa asili yake na ule wa kidini) sasa alikuwa akiyahesabu kuwa "hasara."

**NASB , NRSV "kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu"**
**NKJV "kwa ufahamu mzuri sana wa Kristo Yesu Bwana wangu"**
**TEV "kwa ajili ya kile kilicho kizuri zaidi, ule ufahamu wa Kristo Bwana wangu"**
**NJB "kwa ajili ya faida iliyo kuu ya kumfahamu Kristo Yesu Bwana wangu"**

Jawabu la Ukristo ni kuwa na uhusiano binafsi pamoja na Kristo. Katika Kiebrania "kujua" kunamaanisha uhusianao na mtu wa karibu sana, si jambo linalohusu kitu Fulani ama mtu fulani (kama vile Mwa. 4:1; Yer. 1:5). Injili ni (1) mtu wa kumkaribisha; (2) kiini cha kuamini; na (3) maisha yapasayo kuishi! Kwa aya ya "uzuri usio na kiasi" (*huperechō*) tazama Mada Maalum: Matumizi Ambatani ya neno *Huper* katika Efe. 1:19. Neno hili hili linatumiaka katika Flp. 2:3; 3:8; na 4:7.

◙**"nimepata hasara ya mambo yote"**Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Hii ingeweza kurejelea juu ya familia yake, urithi wake, faida yake ya kidini na /ama mafunzo ya sheria za Kiyahudi. Kila kitu alichokifikiria kama chenye faida hapo mwanzo ghafla kilipoteza uzuri wake! Kila kitu kilibadilikia njiani kwenda Dameski (kama vile Matendo 9; 22:3-16; 26:9-18).

**NASB, NKJV "nikiyahesabu kuwa kama mavi"**
**NRSV "nimeyaona hayo yote kuwa ni takataka"**
**TEV "nimeyafikiri yote kama uchafu"**
**NJB "tena nayaona haya kama kinyaa"**

Kiuhalisia hii ni neno hili limamaanisha "kinyesi" ama bila shaka kifupi kinachojulikana sana cha kifungu "kuwatupia mbwa" (kama vile Flp. 3:2). Ki-sitiari kilimaanisha "kisicho na uzuri."

◙**"ili nipate Kristo"**Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu. Paulo analitumia neno hili la kibiashara kisitiari, "kupata" ama "kushinda" kwa Kristo ama injili kama katika Flp. 1:21; 3:7,8; na 1 Kor. 9:19-22 [ mara tano]. Katika Tito 1:11 alilitumia katika maana halisi.

**3:9 "nionekane katika yeye"** Hii ni kauli tendewa tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Hii inaelezea maombi ya ndani ya Paulo. "Katika Yeye" ama "katika Kristo" ulikuwa ni muundo wa kisarufi uliopendelewa na Paulo kwa waamini (kwa mfano mzuri agalia Efe. 1:3, 4, 6, 7, 9, 10 [mara tatu], 12, 13 [mara mbili]).

◙**" nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria"** Hili ni jambo la kiufunguzi (kama vile Rum. 3:9-18,21-31). Ni kwa jinsi gani mwanadamu awe na haki kwa Mungu? Ubora ama haki? Haya kwa ujumla wake yalijibiwa na Paulo akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Matendo 9; 22:3-16; 26:9-18). Tazama Mada Maalum katika Efe. 4:24.

◙**"bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo "** Imani ni namna mtu anavyoipokea zawadi ya neema ya Mungu katika Kristo (kama vile Rum. 3:24; 6:23; Efe. 2:8-9). Imani na toba ni vipengele viwili muhimu kwa mwitikio wa mwanadamu kwa lile agano jipya (kama vikle Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21).

◙**"haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani" Haki ni zawadi toka kwa Mungu** (kama vile *dōrea*, Rum. 5:15; 2 Kor. 9:15; Efe. 3:7; *dōrēma*, Rum. 5:16; *dōron*, Efe. 2:8; *charisma*, Rum. 6:23). Mara nyingi Yeye huangalia mwanzo (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu hutamani wanadamu wote waokolewe (kama vile Eze. 18:23,32; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9); Yeye amefanya njia kwa wanadamu wote ili waokolewe! Hawa wanawapaswa kuitikia na kuendelea kuitikia juu ya lile jitoleo la Mungu kwa

1. toba
2. imani
3. Utii
4. Huduma
5. Ustahimilivu

Tazama Mada Maalum katika Efe. 4:24.

**3:10"uweza wa kufufuka kwake"** Hii aya lazima irejelee juu ya maisha ya waamini wapya ndani ya Kristo. Huu mtiririko wa vifungu katika Flp. 3:10 unaweza kuaksi mateso ya Paulo kwa ajili ya injili (kama vile 2 Kor. 4:7-12,16; 6:4-10; 11:23-28) ambayo yalihusisha kifungo chake kilichokuwepo kwa wakati huo. Wengine wanaviona vifungu hivi vyote vilivyo katika Flp. 3:10 kama kipengele cha umoja wa siri wa mwamini pamoja na Kristo ama ukomavuwa kumfanana Kristo (kama vile Ebr. 5:8) hivyo waamini wanakomazwa na mateso (kama vile Rum. 5:1-5).

◙**"t ushirika wa mateso yake "** Mateso ni jambo la kawaida la uzoefu wa Mkristo wa Pet. 3:14; 4:12-19). Kama waamini waushirikivyo ushindi wa Kristo, pia wanaishiriki huduma Yake (kama vile Mt. 10:24; Luka 6:40; Yohana 13:14-16; 15:20; 17:18; 20:21; 2 Tim. 3:12). Tazama Mada Maalum: *Koinōnia* katika Flp. 2:1.

◙**"nikifananishwa na kufa kwake"** Hii ni kauli tendewa endelevu ya wakati uliopo. Waamini wanapaswa kuifia dhambi na waishi wenyewe kwa Mungu (kama vile Mt. 16:24-26; Rum. 6:1-11; Gal. 2:20; Kol. 3:3). Maisha ya kweli yanatanguliwa na kifo kwa maisha ya zamani!

**3:11** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la tatu ambayo ilimaanisha tendo la baadaye lenye uhakika.Mstari 11 lazima ufasiriwe katika mwangaza wa mstari wa 10. Kifungu hiki hakidhihirishi shaka kuhusu wokovu, bali Unyenyekevu!

◙ **"ili nipate"** Hapa tena kuna mtindo wa kiupembuzi ama wa kimafumbo wa theolojia ya Paulo. Paulo alifahamu kuwa alikuwa Kristo na kwamba kama Kristo alivyopalizwa na Roho nasi pia yatupaswa kupalizwa (kama vile Rum. 8:9-11). Hata hivyo, Paulo aliona kuwa wokovu si kama tukio pekee lililokamilishwa (kama vile Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito 3:5), bali pia ni tendo endelevu (kama vile 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15) na hatima katika kilele cha baadaye (kama vile Rum. 5:9,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28). Ukristo una sifa ya pumziko na thawabu ya Mungu na maisha yenye nguvu yenye huduma ya kupendeza kwa Mungu (kama vile Efe 2:8-9 na 10). George E. Ladd's *A Theology of the NewTestament*, kur. 521-522, kina mjadala mzuri juu ya suala hili.

◙**"kiyama"** Hili ni neno ambatani lisilo la kawaida**.** Hili linapatikana hapa tu katika Agano Jipya. Kiuhalisia hii ni "mbali na walio *kufa* katika maisha ya *ufufuo*." Paulo amekuwa akijadili kuhusu uhusiano binafsi wa karibu sana kati yake mwenyewe na Kristo mfufuliwa. Aliisubiri siku ile ya mwisho itakapomjia, vilevile, angeuelewa ufufuo wa kimwili kama alivyokwisha kuuelewa ufufuo wa kiroho (kama vile Rum. 6:4-11; 2 Kor. 5:17; 1 Yohana 3:2).

Hii ni sehemu ya ule mvutano wa "utayari ambao haujatimia" wa ufalme wa Mungu, kupishana kwa zama mbili za Kiyahudi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAFILIPI 3:12-16**
**12 Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. 13 Ndugu, ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu.; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; 14 nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. 15 Basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo; na hata mkiwaza mengine katika jambo lo lote, Mungu atawafunulia hilo nalo. 16 Lakini, hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo.**

**3:12 "Si kwamba nimekwisha kufika"** Paulo aliishi katika wasi wasi wa ule wakati uliokuwepo lakini aliukamilisha Ufalme wa Mungu. Alimjua Kristo, alijijua yeye ni nani ndani ya Kristo, alijuia kuwa alikuwa amekubaliwa na Kristo lakini alipambana kuishi kama Kristo (kama vile Warumi 7). Paulo aliifikia hatima yake lakini si kwa ukamilifu; alikuwa mkamilifu lakini si mkailfu kabisa. Baadhi ya machapisho ya kale ya Kiyunani, $P^{46}$, D*, na G, yanaongeza neno "ama amekuwa mwenye haki." Hili ongezeko pia linapatikana ndani ya maandishi ya Kiyunani yaliyotumiwa na Irenaeus na Ambrosiaster. Hata hivyo, andiko fupi zaidi linaungwa mkono na MSS $P^{61}$, א, A, B, $D^{c}$, K, na P pamioja na tafsiri za kale, Toleo la Kilatini, ki-Ashuru, na Coptic.

**NASB, TEV " nimekwisha kuwa mkamilifu"**
**NKJV "au nimeshakamilika"**
**NRSV "au nimekwisha kufikia kusudi"**
**NJB "ama sijalifikia kusudi langu"**

Hii ni kauli timilifu tendewa ya hali inayoendelea yenye kudokeza kitu fulani kilichotokea katika wakati uliopita lakini ukafikia hali ya utulifu na hili lilikamilishwa na Mungu. Neno lenyewe lilimaanisha

1. kudhihirika kwa ukamilifu
2. kuandaliwa kwa ukamilifu
3. kamilifu
4. komavu
5. utosherevu

Hili halina maana mbadala ya Kiingreza ya ukamilifu au kutokuwa na dhambi.

◙**" nakaza mwendo"** Hii ni kauli tendaji elekezi yawakati uliopo. Kwa asili hili lilikuwa neno la kiuwindaji lililomaanisha "kufuatilia mnyama." Hili lilikuja kutumika ki-sitiari juu ya mashindano ya mbio za miguu. Paulo hakufatilia wokovu (kama vile Rum. 9:30) bali ukomavu, Ufanano na Kristo (kama vile Rum. 6:4-9).

**NASB " ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu"**
**NKJV "kwamba niweze kukichchumalia kile kilichochumaliwa na Kristo Yesu kwangu"**
**NRSV " kilifanya liwe langu, Kwa sababu ya Kristo Yesu alivyolifanya kuwa langu"**
**TEV "kishinda taji ambalo Kristo Yesu amekwisha kulishinda kwa ajili yangu"**
**NJB "katika bdii ya kulishikiria lie taji ambalo Kristo Yesu amelitwaa kwa**

**Kwa ajili yangu"**

Kipengele hiki kinaanza na sentensi yenye masharti dalaja la tatu (yenye kutumia *ei* badala ya *ean*) yenye kumaanisha tendo lenye uhakika (kama vile Filp. 3:11). Hili linaweza kurejelea juu ya (1) wokovu (Flp. 3:9); (2) Ufanano na Kristo (Flp. 3:10); au (3) ufufuo (Flp. 3:11). Hili ni neno la Kiyunani lenye nguvu. Paulo "alitwaliwa"na Kristo akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Matendo 9:1-22; 22:3-16; 26:9-18). Mmoja wa wale wafuasi wake aliteswa na sasa anafarijiwa kama Bwana aliyefufuliwa. Theolojia na uzoefu binafsi viliunganishwa! Paulo sasa alihitaji kuwa kama wale na Yeye aliowashambulia.

**3:13"ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu"** Hii ni kauli tendaji ya wakati uliopo yenye kitenzijina. Neno hili limetumika mara tatu katika Flp. 3:12-13. Paulo anajitahidi kuwa mkomavu ndani ya Kristo lakini alijua kuwa alishindwa kwa sababu ya kupungukiwa na ukomavu wa ufanano wa Kristo (kama vile  Warumi 7). Bado ile kweli kuu ya injili iliyomo ndani ya Kristo (na waamini wote) tayari imekwisha kukamilishwa (kuhesabiwa haki na kutakaswa, kama vile Rum. 8:29-30). Maneno "angalia," "fikiria," ama "dhahania" (kama vile Rum 4:3; 6:11; 1 Kor. 13:5) yote yanarejelea juu ya uthibitisho wa kiakili ambapo mwanadamu aliyeanguka anaielewa injili na kuchagua kuishi katika nuru ya kweli mpya na mtazamo wa kiulimwengu ndani ya Kristo!

Kuna tofauti ya machapisho katika sentensi hii pamoja na neno "bado" dhidi ya "hapana" Maandishi ya kale yanagawanyika katika sehemu hizi mbili. Maelezo mazuri zaidi ni ya wale waandishi waliobadilisha "hapana" ya Paulo "ningali bado" kwa sababu huenda walifikiri kwamba huyu alikuwa mnyeyekevu sana. Kama zilivyo tofauti nyingi za machapisho hili linaiathiri fasiri ya kwa kiasi kidogo.

◙**" nikiyasahau yaliyo nyuma"** Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) ya wakati uliopo unaoendelea. Paulo alianza kwa ukiroho zaidi. Aliusahahu Uyahudi wake uliokuwa umepita. Hata hivyo, kwa sababu ni njeo ya wakati uliopita kifungu hiki kinaweza kuhusisha kazi yake ya Kiutume au kifungo chake cha wakati uliokuwepo. Msimamo wake mbele za Mungu haukujikuta juu ya utendakazi wa mwanadamu, wakati uliopita au uliopo!

◙**"nikiyachuchumilia yaliyo mbele"** Hii ni kauli nyingine ya kati (yenye ushahidi) ya wakati uliopo yenye hali ya kuendelea. Hii ni ya kwanza katika mpangilio wa maneno ya riadha. Hii inamaanisha "mkimbiaji anayejiandaa kwa ajili ya kushinda mbio." Huu ni uambatani uliozidishwa wenye vihisishi viwili, *epi* na *ek*. Paulo kwa uthabiti aliishi maisha ya shukrani. Baada ya kuwa ameokolewa kiwango cha nguvu zake kilibaki juu lakini kwa ujumla shauku yake ilibadilika kutokana na juhudi zake mwenyewe hadi huduma ya injili.

**3:14** Huu ni mpangilio wa sitiari za kiriadha. Hizi zinaonyesha bidii nyingi zinazohitajika kwa maisha ya Mkristo (kama vile 1 Kor. 9:24,27; Ebr. 12:1).

◙**"mwito mkuu wa Mungu"**  Tazama Mada Maalum: Wito katikaEfe. 4:1.

**3:15"tulio wakamilifu" Hili ni neno sawa** "timilifu" kama vile Flp. 3:12 lakini Paulo analitumia katika maana mbili tofauti. Wakristo wanaweza kuwa wakomavu pasipokuwa na dhambi (kama vile 1 Kor. 2:6; 14:20; Efe. 4:13; Ebr. 5:14; 6:1).

◙ **" tuwaze . . . na tuwaze hayo"** Paulo mara nyingi anarejelea juu ya  matendo ya kiakili. Paulo anatumia maneno kadhaa ya kIyunani kwa ajili ya kufikiri kwa mantiki ama kuwaza. Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo ya neno "*phroneō*" (kama vile Flp. 1:7; 3:15,19); "*ginosko*" (kama vile Flp. 1:12); "*psuchē*" (kama vile Flp. 1:27); "*noēma*" (kama vile Flp. 4:7); "*logizomai*" (kama vile Flp. 4:9); "*manthano*" (kama vile Flp. 4:9, 11). Waamini

nawamwabudu Mungu kwa akili zao (kama vile Kumb. 6:23, iliyonukuliwa katika Mat. 22:36-38; Marko 12:29-34; Luka 10:27-28). Ukristo wa kweli hauwezi kuwa kinyume na akili. Hata hivyo, hatupaswi kuamini katika fikra zetu zilizoanguka, bali katika kujifunua kwa Mungu mwenyewe (Andiko).

◙**"mkiwaza"** Hii ni sentensi yenye masharti dalaja la kwanza, ambayo inadhahaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi ama kwa sababu zake za kiuandishi. Kulikuwa na wale waliokuwa ndani ya ushirika " waliowaza mengine."

◙**"Mungu atawafunulia hilo nalo"** Kulikuwa na hali ya kutokubaliana miongoni mwa waamini kuhusiana na mitazamo mingi ya imani. Paulo alijipa matumaini kwamba agano lililomhusisha Roho akaaye ndani, moyo mpya, na akili mpya hatimaye huwahabarisha na kuwaumba upya waamini wote (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:26-27; Yohana 6:45; Efe. 1:17; 1 The. 4:9; 1 Yohana 2:27).
Katika muktadha hiki kifungu kinayafunua mawazo ya Paulo kuhusu mamlaka ya ujumbe wake. Yeye alijisikia kuongozwa na Roho (kama vile 1 Kor. 2:10; 7:10-12; 11:23; 14:37-38; 2 Kor. 10:8; 12:1; Gal. 1:12,16; 2:2; 2 The.3:14). Hii ilikuwa njia nyingine ya kuirejelea maana yake ya mamlaka ya kiutume. Hili linaweza kufasiriwa katika njia mbili: (1) Mungu ataifunua kweli yake kwa waamini walio waovu au (2) Mungu atawafunua wale walio waovu kwa waamini kupitia mafundisho au matendo yao. Katika muktadha #2 inaonekana kuwa nzuri zaidi.

**3:16**
**NASB " hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo"**
**NKJV "hata hivyo, kwa kiwango tulichofikia, na tuenende kwa agizo hilo hilo,**
**Na tuwe na fikra zile zile"**
**NRSV "na tulifikirie tu lile tulilolifikia"**
**TEV "Kwa vyovyote, tusonge mbele katika njia hiyohiyo ambayo tumeifuata**
**mpaka sasa hivi"**
**NJB "sasa, twendelee mbele kutokana kutoka hatua ile tuliyoifikia"**

Mstari huu ni onyo la Paulo la kuendelea kuishi kama Mkristo (kama vile Efe. 4:1, 17; 5:2,15). Waamini wanathibitishwa na kutakaswa kwa neema ya Mungu kupitia inami katika Kristo, lakini wanapaswa kupambana hadi kuufikia ukomavu wa kumfanana Kristo (kama vile 2 Kor. 3:18). Kuna mtiririko wa maongezeko katika mstari katika machapisho ya kale ya Kiyunani. Andiko fupi sana (NASB na NRSV) linapatikana katika machapisho ya Kiyunani $P^{16}$, $P^{46}$, א*, A, B. Lile Toleo la $UBS^4$ linatupa andiko hili fupi sana lenye dalaja "A"(yumkini). Upokeaji wa maandiko unaongeza neno "na tuwe na fikra zile zile" (NKJV) ambalo linapatikana katika MSS $א^c$,K, na P. Kuna maongezeko kadhaa ambayo yanaonekana kuonyesha uelekeo wa kiuandishi kwa ajili ya kubadilisha na kuongeza

katika mstari huu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : WAFILIPI 3:17-41**
**17 Ndugu zangu, mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi. 18 Maana wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; 19 mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani. 20 Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; 21 atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake. 1 Basi, ndugu zangu, wapendwa wangu, ninaowaonea shauku, furaha yangu, na taji yangu, hivyo simameni imara katika Bwana, wapenzi wangu.**

**3:17"mnifuate mimi"** Mstari huu una kauli shurutishi mbili. Paulo anawasistiza kumfuatia yeye alivyomfuata Kristo (kama vile Flp. 4:9; 1 Kor. 4:16; 11:1; 1 The. 1:6; 2 The. 3:7,9). Kifungu hiki kimantiki kimeunganiswa na Flp. 3:15-16. Tazama namna mfano wa Paulo unavyopanuliwa ili kulijumuisha kundi la huduma yake na bila shaka Epaphrodito ("-angu"-"sisi").

◙**"mfano "** Tazama Mfano ufuatao.

**MADA MAALUM: MUUNDO**

Neno *tupos* lina elimu-maana pana.

1. Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek New Testament*, uk. 645
   a. Sampuli
   b. mpango
   c. Mtindo au namna ya kuandika
   d. Amri ya serikali ama agizo litolewalo na mtawala
   e. Sentensi ama uamuzi
   f. Mfano wa mwili wa binadamu kama sadaka ya kuondoa nadhiri kwa Mungu anayeponya
   g. Kitenzi kilichotumika kwa maana ya kuongeza agizo au mwongozo wa sheria
2. Louw and Nida, *Greek-English Lexicon*, juzuu. 2, uk. 249
   a. Kovu (kama vile Yohana 20:25)
   b. Sura (kama vile Matendo 7:43)
   c. Fanya kwa mfano (kama vile Ebr. 8:5)
   d. Mfano (kama vile 1 Kor. 10:6; Flp. 3:17)
   e. Umboasili (kama vile Rum. 5:14)
   f. Aina (kama vile Matendo 23:25)
   g. Maudhui (kama vile Matendo 23:25)
3. Harold K. Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised,* p. 411
   a. Kipigo, chapa, alama (kama vile Yohana 20:25)
   b. Eleza kinaganaga
   c. Sanamu (kama vile Matendo 7:43)
   d. Kanuni, mpango (kama vile Rum. 6:17)
   e. Muundo, kusudi (kama vile Matendo 23:25)
   f. Umbo, enye kufanana na kitu kingine (kama vile 1 Kor. 10:6)
   g. Umbo tarajiwa, aina (kama vile Rum. 5:14; 1 Kor. 10:11)
   h. Sampuli mfano (kama vile Matendo 7:44; Ebr. 8:5)
   i. Mfano adilifu(kama vile. Flp. 3:17; 1 The. 1:7; 2 The. 3:9; 1 Tim. 4:12; 1 Pet. 5:3)

Kumbuka, msamiati hauweki maana; ni matumizi tu ya maneno kwenye sentensi/aya ndiyo yanaweka maana (yaani, muktadha). Kuwa mwangalifu kugawanya rasmi kundi la fafanuzi kwa neno na kulitumia kila mahali neno hilo linapotumika katika Biblia, muktadha huamua maana!

**3:18"wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao"** Kulikuwako na, bado wapo, waalimu wa uongo ndani ya kanisa. Katika kitabu hiki kwa vyovyote hawa wanaweza kuwa wale washika sana Sheria na Desturi za Kiyahudi (kama vile Flp. 3:2-16), kama katika kitabu cha Wagalatia na Matendo 15, au Mafunuo ya Uongo (kama vile 1 Yohana 2:18,22; 4:1-6). Njia pekee ya mtu kujilindana makosa ni kujua, kushikilia, na kuishi katika kweli! Walimu wa uongo ni watu wepesi, wenye mantiki, wenye mvuto, wenye kujieleza kwa ufasaha, na ni watu wenye ushawishi. Mwamini Mwana; kifuatie kitabu; jitolee kwa huyo Roho!

◙**"hata kwa machozi"** Neno hili linatia mkazo wa uchungu (kama vile Mt. 2:18; 26:75; Marko 5:38-39; Yohana 11:31; Yakobo 4:9; 5:1). Paulo hakupata furaha katika wengine waliokuwa katika ukosefu wa maadili au theolojia.

◙ **"adui za msalaba wa Kristo"** Hakuna uhakika kuhusu upekee wa haya "maadui wa msalaba." Vifungu vilivyotumiwa na Paulo vina nguvu sana, hivi vinaonekana kurejelea juu ya walimu wa uongo wasioamini wa Flp. 3:2-16. Dhambi zilizoorodheshwa katka Flpl. 3:19 haziendani na wanasheria wa Kiyahudi, bali wale wasio penda sheria na kutaka kuishi kwa neema au Wakristo walioongoka kwa uhakika wakarudi katika maisha yao ya awali ya upagani (kama vile Kol. 2:16-23; 2 Pet. 2:20-22). Muktadha unaunga mkono ile hoja ya mwisho. Lakini, ikiwa ni hivyo, tofauti ya Flp. 3:20 inamaanisha kwamba Paulo aliwaza kuwa hawa walikuwa hawajaokolewa kiukweli (kama vile Mt. 7:13; 1 Yohana 2:19; 2 Pet. 2:1-22; Ufu. 2:4-5; 10-11; 16-17; 25-26; 3:2,5,11,21).

Jihadhari na mifumo yenu (kimadhehebu, kiuzoefu, kiutamaduni) theolojia hailifasiri hili andiko. Kiuhalisia muktadha na kusudi asilia la mwandishi lazima kiwe kigezo kikuu. Kitabu cha Agano Jipya si wasilisho la kimfumo wa ukweli bali ni cha kimashariki, aina ya kimafumbo. Kitabu cha Agano Jipya kwa ukawaida kinawasilisha kweli katika mwonekano wa jozi zenye mkanganyiko (fumbo). Maisha ya Mkristo si maisha ya kuhisi wasiwasi wa lile hakikisho na tumaini pamoja na jukumu na onyo! Wokovu si matokeo bali maisha mapya!

**3:19**
**NASB**

**NASB,NKJV " mwisho wao ni uharibifu"**
**NRSV "wanaoelekea kuishia jehanamu"**
**NJB "mwisho wao ni kuangamia"**

Hawa walikuwa waaminifu, waliopashwa habari, watu wa dini. Paulo analitumia neno hili *apōleia* kuelezea juu ya hukumu kuu ya Mungu (kama vile Flp. 1:28; Rum. 9:22; 2 The. 2:3; 1 Tim. 6:9). Hata hivyo, katika Injili hili linapaswa kukubalika kuwa neno hili lilitumika katika maana ya "upotevu" (kama vile Mt. 26:8; Marko 14:4).Hivyo, haiwezekani kumjua yule anayerejelewa na Paulo (waamini au wasioamini).

**NASB "mungu wao ni tumbo"**
**NKJV, NRSV "ambao mungu waonitumbo lao"**
**TEV "kwa sababu mungu wao ni wa shauku za kimwili"**
**NJB "mungu wao ni tumbo lao"**

Hili linaonyesha kwamba uelekeo wao kufikia (1) utaratibu wa kutozitenda sheria au (2) uchoyo na kupenda vitu vya anasa. Haya maoni yanapendwa sana na walimu wa uongo wa Kiyunani (kama vile Rum. 16:17-18) kuliko wanasheria wa Kiyahudi (kama vile Flp. 3:2-6). Toleo la TEV linaweza kuwa limeshika maana ya ki-sitiari,"kwa sababu mungu wao ni wa hamu za kimwili."

◙**"utukufu wao u katika fedheha yao"** Hili linaweza kurejelea juu ya
1. msistizo wa wale washika Sheria sana na Maadili ya Kiyahudi kuhusiana na tohara au majivuno ya Kiyahudi
2. msistizo wa wana-Mafunuo ya uongo kuhusu maarifa
3. maisha ya uovu wa kupenda ngono (ukware)

Hawa walimu wa uongo walijivunia kila kitu ambacho wangefedheheshwa nacho! Walimu wa uongo wa Agano Jipya mara nyingi wanabainishwa na tabia ya kupenda fedha /ama unyanyasaji wa kingono.
◙ **" waniao mambo ya duniania"** Hiki kifungu kinaonyesha asili nyingi za udini wa mwanadamu (kama vile Isa. 29:13; Kol. 2:16-23; 3:1-2).

**3:20**
**NASB, NKJV "Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni"**
**NRSV "Lakini wenyeji wetu uko mbinguni"**
**TEV "Sisi, kwa vyovyot, ni wenyeji wa mbinguni"**

**NJB "Lakini makao yetu yako mbinguni"**
Huu mstari ni tofauti na ule wa Flp. 3:18-19. Kiwakilishi "yetu" ni cha kimsistizo. Neno "Mbinguni" ni wingi (kama vile 2 Kor.12:2; Efe. 4:10; Ebr. 4:14; 7:26) linayafuata matumizi ya Kiebrania (*shamayim*). Bila shaka Paulo alikuwa akitumia cheo cha koloni la Kirumi la mji kama kielelezo (kama vile Flp. 1:27).

◙**"tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo"** Paulo mara nyingi analitumia neno hili "tunamtazamia" katika uhusianao wa Ujio wa mara ya Pili (kama vile Rum. 8:19,23,25; 1 Kor. 1:7; Gal. 5:5; Ebr. 9:28). Shauku ya waamini kwa ajili ya Ujio wa mara ya Pili ni moja ya ushahidi wa uhusiano wao na nguvu ya kuishi katika ufanano na Kristo (kama vile Rum. 8:19, 23; 1 Kor. 1:7). Msistizo wa Paulo juu ya kurudi kwa Bwana ni wa mara kwa mara, lakini uelewa wa suala la muda ni wa kiutata. Kuna vifungu kadhaa ambamo Paulo amejijumuisha mwenyewe katika kikundi cha wale watakaokuwa hai katika Ujio wa mara ya Pili (kama vile 1 Kor. 15:51-52; 2 Wakorintho 5; Flp. 3:20; 1 The. 4:15,17).
Hata hivyo, kuna vifungu vingine vinavyoeleza kurudi kwake baadaye nje ya wakati wa maisha yake (kama vile 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14 na hasa 2 Wathesalonike). Inawezekana kwamba neno "sisi" la kundi la kwanza la kimaandishi ni la kiuhalisia, au kwamba mawazo ya Paulo kuhusu jambo hili yalikuzwa. Ni vigumu kudhani kwamba mwandishi aliyevuviwa "alikuziwa" theolojia yake. Mtazamo bora ni kusisitiza mfano wa lugha. Paulo, kama waandishi wa Agano Jipya, alielezea uyumkini na "ukaribu" wa Ujio wa mara ya Pili. Waamini wanapaswa kuishi katika nuru ya kurudi kwake Bwana wakati wowote! Hata hivyo, Yesu (Mathayo 24) na Paulo (2 Wathesalonike 2) alinena juu ya matukio ya kihistoria ambayo yanapaswa kutokea kabala ya Ujio wa mara ya Pili. Yote kwa kiasi fulani ni ya kweli!
Kurudi kwa Yesu ni tumaini linalotia hamasa ya kila kizazi cha waaminio lakini ukweli wa kizazi kimoja pekee! Hii ni moja kati ya idadi tatu za Paulo kumuita Yesu "Mwokozi" (kama vile Efe. 5:23) kabla ya Barua za Kichungaji (1 Timotheo,2 Timotheo, Tito), ambamo amelitumia si chini ya mara kumi. Neno hili lilikuja kuwa haba kipindi cha Mfalme wa Kirumi. Katika Tito kuna ufanano katika matumizi ya hili neno kati ya Mungu Baba na Yesu Mwana (kama vile Flp. 1:3 dhidi ya1:4; 2:10 dhidi ya 2:13; 3:4 dhidi ya 3:6). Wakristo wa kale walikuwa tayari kukikabili kifo kuliko kumwachia jina hili Mfalme wa Kirumi. Maneno yoye "Mwokozir" na "Bwana" yalikuwa majina ya Mfalme wa Kirumi yaliyotumiwa na Wakristo pasipo kumtaja Yesu.

**3:21"atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu"** Paulo anaweka msistizo wa uhakika juu ya waanini kuishi kimwili (kama vile 2 Kor. 5:1-10), sehemu zote hapa na mbinguni. Kitheolojia hili linarejelewa kama adhama (kama vile Rum. 8:30; 1 Yohana 3:2), wakati wokovu utakapokamilishwa na kutambuliwa kwa utimilifu. Mwili wetu wa mavumbi (kama vile Zab. 103:14) utabadilishwa na kuumbwa upya (1 The.4:13-18) katika mwili wa Kiroho kama ule wa Kristo (kama vile 1 Kor. 15:45; 1 Yohana 3:2).

◙**"vitu vyote viwe chini yake"** Kristo aliyefufuka ni Bwana wa vyote (kama vile 1 Kor. 15:24-28; Kol. 1:20).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.
Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! katika Flp. 3:2 Paulo anamrejelea nani.?
2. Kwa nini Paulo anajipa sifa za Kiyahudi?
3. Kwa vitebdo, ni kwa namana Flp. 3:10 inahusiana na waamini?
4. Je! hawa manabii wa uongo wameokolewa?

# WAFILIPI 4

**MGAWANYO ZA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA**

| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
|---|---|---|---|---|
| Maonyo | Mkiwa pamoja, wenye Furaha na maombi | Nasaha za mwisho | Maelekezo | Ushauri wa mwisho |
| (3:17-4:1) | (3:17-4:1) | (3:17-4:1) | 4:1 | (3:17-4:1) |
| 4:2-7 | 4:2-7 | 4:2-3 | 4:2-3 | 4:2-3 |
| | | 4:4-7 | 4:4 | 4:4-9 |
| | | | 4:5-7 | |
| 4:8-9 | 4:8-9 | 4:8-9 | 4:8-9 | |
| Kushukuru kwa Zawadi za Wafilipi | ukarimu wa Wafilipi | | asante kwa ajili ya zawadi | asante kwa msaada tuliopokea |
| 4:10-14 | 4:10-20 | 4:10-14 | 4:10-13 | 4:10-20 |
| | | | 4:14-20 | |
| | | 4:15-20 | | |
| 4:15-20 | | 4:15-20 | | |
| Salamu za mwisho | salamu na Baraka | | salamu za mwisho | salamu na heri za mwisho |
| 4:21-23 | 4:21-23 | 4:21-22 | 4:21-22 | 4:21-22 |
| | | 4:23 | 4:23 | 4:23 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka **"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 4:1**
[1] **Basi, ndugu zangu, wapendwa wangu, ninaowaonea shauku, furaha yangu, na taji yangu, hivyo simameni imara katika Bwana, wapenzi wangu.**

**4:1 "ndugu zangu mpendwao"** Paulo aliunganisha maneno mawili ya Agano Jipya kwa Waamini: "wapendwao" [mara mbili] na "ndugu." Huu muunganiko wa upendo ulionesha upendo mkubwa kwa kanisa hili kama linavyoonekana katika tungo inayofuata na katika usambamba wa FlP. 1:8.

◙ **"ambao ninatamani kuwaona"** Ni neno lilelile lenye nguvu (epipotheō) linatumika pia katika FlP. 1:8; 2:26; 2 Kor. 9:14.

◙ "**furaha yangu, na taji yangu**" Neno "taji" (stephanos) lilimaanisha taji apewayo mshindi katika mchezo wa mashindano. Shauku hii hii inaweza kuonekana katika maoni ya Paulo kwa kanisa lingine la Makedonia (kama vile 1 The. 2:19-20; 3:9). Kanisa hili lilikuwa uthibitishao wa wa ufanisi wa utume wa Paulo (kama vile 1 Kor. 9:2; 1 The. 2:19).

◙ "**kusimama imara"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hii ni sitiari ya kijeshi inayomaanisha hali ya uwezo wa Mkristo kubaki mwaminifu katikati ya matatizo (kama vile Flp. 1:27; 1 Kor. 16:13; Efe. 6:11-14). Pia inahusiana na ustahimilivu (angalia Mada Maalum katika Flp. 1:9-11), ambayo inawezekana tu "katika bwana" (kama vile Gal. 6:9; Ufunuo 2:7,11,17,26; 3:5,12,21).

Hili ni fumbo lingine la kibiblia katika mahusiano kati ya ukuu wa Mungu na utashi huru wa kibinadamu *(linganisha Ezekieli 18:31 na Ezekieli 36:26-27).* Katika mstari huu waamini wanaamuriwa "kusimama imara," wakati katika Yuda 1:24 ni Mungu anayewawezesha kusimama imara. Angalau zote mbili ni kweli.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 4:2-3**
**[2] Namsihi Euodia, namsihi na Sintike, wawe na nia moja katika Bwana. [3] Naam, nataka na wewe pia, mjoli wa kweli, uwasaidie wanawake hao; kwa maana waliishindania Injili pamoja nami, na Klementi naye, na wale wengine waliotenda kazi pamoja nami, ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima.**

**4:2 "Euodia...Sintike"** Kwa dhahiri, hata katika kanisa hili lenye upendo bado kuna mvutano wa ndani. Hii haimaanishi mvutano wa kimadhehebu ambao unatajwa katika sura ya 3, lakini ni kama kamvutano ka ushirika. Hii ya kwanza jina lake halisi "safari ya mafanikio au ushindi." Jina la pili linamaanisha "mahusiano ya kupendeza" au "bahati nzuri." Majina yao hayakufanana na matendo yao ya sasa. Katika Makedonia wanawake walikuwa na uhuru zaidi kulikomsehemu nyingine yoyote katika ulimwengu wa kale wa Kirumi (kama vile Mdo. 16:12-15). Wakati mwingine uhuru unageuka kuwa upendeleo wa kibinafsi au hata kibali.

◙ **"Kuishi katika amani ya Bwana"** Ufunguo kuelekea katika amani uko katika uhusiano wa waaminio kwa Kristo ambao kimsingi unabadilisha mahusiano yao na ndugu zao wa kiagano. Upendo wa waamini kwa Mungu ni unaonekana wazi katika upendo wao kwa wengine wanapopendana (kama vile Efe. 4:1-6; 2:1-5; 1 Yn. 4:20-21).

**4:3**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"mtumwa mwaminifu"** |
| **NRSV** | **"mtendakazi mwaminifu"** |
| **TEV** | **"mwenza mwaminifu"** |
| **NJB** | **"mtendakazi"** |

Hii mara kwa mara inafasiriwa kama "nira-nyenza" (kama vile Arndt na Gingrich, *A Greek-English Lexicon of the NewTestament,* ukurasa 783). Hata hivyo, ni nomino ya kiume ya umoja, katika orodha ya majina mengine mengi, yawezekana lilikuwa jina sahihi lenyewe, Syzygus (kama vile NJB na Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament,* ukurasa 607), ambayo ingekuwa ni tamthiliya katika maana ya jina. Inawezekana kuwa hii ilikuwa ni njia ya Paulo ya kumrejerea Luka. Hii "sisi" sehemu za Matendo ya Mitume inaanza na kuishia katika Filipi. Luka inawezekana alianza kukaa pale na kusaidia waongofu wapya na kukusanya matoleo kwa ajili ya Kanisa katika Yerusalemu.

◙ "kuwasaidia wamama hawa" Hii ni kauli shurutishi ya kati ya wakati uliopo inayomaanisha "kupatana na". Paulo alikuwa anatoa maonyo kwa mmoja wa washirika wa kanisa la Wafilipi kuwasaidi hawa wanawake kukabiliana na tofauti zao katika Bwana (kama vile Gal. 6:1-4)

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“walioshirikiana nami katika shauri la injili”** |
| **NKJV** | **“waliofanya kazi pamoja nami”** |
| **NRSV** | **“waliofanya kazi nami”** |
| **TEV** | **“waliofanya kazi kwa bidii pamoja nami”** |
| **NJB** | **“walisumbuka sana”** |

Neno hili lilitumika hapa tu katika Flp. 1:27. Ni neno la kijeshi au kimichezo kwa ajili ya "mapigano makali." Ni la kisitiari kwa ajili ya uenezaji wa injili. Wanawake hawa walimsaidia Paulo katika kazi ya injili. Wasaidizi wengi wa Paulo waonatajwa katika Warumi 16 na walikuwa ni wanawake. Hata Wamishionari walikuwa na hali ya kutofautiana (kama vile Mdo. 15:36-41). Namna wanavyotatua kama wakristo ndio jambo kubwa na ushuhuda!

◙ **"Klement"** Hili ni jina la kawaida katika ulimwengu wa Kirumi. Mtu huyu hajatajwa mahali pengine popote kwenye Agano Jipya. Hata hivyo, Origen wa Aleksandria, Eusebius na Jerome waliamini kwamba linamaanisha Clement wa Rumi aliyeandika barua kwa kanisa la Korintho wakati Fulani kuelekea mwishoni mwa karne ya kwanza (95 B.K). hata hivyo utambulisho huu unaonekana kuwa ni wa kufikirika sana tu.

◙ **"na watenda kazi wenzangu waliosalia"** Paulo alikuwa amekusudia kutumia wasaidizi wengi katika kazi yake ya injili. Hakuwa mpendelea wanawake; kwa dhahiri alikasimisha majukumu yake kwa wanaume wengine na wanawake. Ni ajabu kutazama katika Warumi 16 kwa namna majina ya wanawake wengi yanavyojitokeza kama wasaidizi wa Paulo.

◙ **"ambao majina yao yapo katika kitabu cha uzima"** Hili laweza kuwa uandikishaji wa watu wa agano katika Agano la Kale (kama vile Dan. 7:10; 12:1) ambao ulikuwa sitiari ya kumbukumbu ya Mungu. Kuna vitabu viwili vilivyotajwa katika Dan. 7:10 na Ufunuo. 20:12-15: (1) kitabu cha kumbukumbu na (2) kitabu cha uzima. Kitabu cha kumbukumbu kinajumuisha majina ya matendo ya waliokombolewa pamoja na waliopotea kama vile Zaburi 58:6; 139:16; Isaya 65:6; Malaki 3:16). kitabu cha uzima kinajumuisha majina ya waliokombolewa na kinaweza kuonekana katika Kutoka Kutoka 32:32; Zaburi 69:28; Isaya 4:3; Dan. 12:1; Luka 10:20; Flp. 4:3; Ebr. 12:23; Ufu. 3:5; 13:8; 17:8; 20:12,15; 21:27. Mungu anafahamu walio wake. Atawapatia thawabu wafuasi wake na kuwahukumu waovu (kama vile Mt. 25:31-46; Ufunuo 20:11-15). Kati ya ulimwengu wa Wayubnani na warumi msemo huu ulikuwa usajili rasmi wa Jiji; kama ndiyo huenda ulikuwa mchezo mwingine juu ya heshima rasmi ya mkoloni wa kirumi na jiji ukoloni wa; ikiwa hivyo ndivyo, inawezekana ikawa ni tamthiliya ingine katika wadhifa rasmi wa jiji kama koloni la Kirumi (kama vile Flp. 1:27; 3:20)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 4:4-7**
**4 Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini. 5 Upole wenu na ujulikane na watu wote. Bwana yu karibu. 6 Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. 7 Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.**

4:4 Kuna miundo miwili tendaji shurutishi ya wakati uliopo ya neno “furahini” *katika* Flp. 4:4. Neno linaweza kufasiriwa kama kwaheri, lakini kwa muktadha huu lazima lifasiriwe "furahini" (kama vile 1 The. 5:16). Hii ni dhamira kuu katika Wafilipi. Tazama mara ngapi maneno "yote" na "kila" yanatumika katika Flp. 4:4-13 kama katika Flp. 1:1-8. Furaha haitakiwi kuunganishwa na mazingira. Suala la msingi ni uhusiano wa Waaminio na Kristo ("katika Bwana").

**4:5**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“roho ya *upole*”** |
| **NKJV, NRSV** | **“upole”** |
| **TEV** | **“mtazamo wa kipole”** |
| **NJB** | **“namna njema”** |

Mwito huu katika mwenendo wa maisha ya Mkristo ulianza katika Fil. 3:1, lakini mjadala wa walimu wa uongo ulikua na kupotosha fikra za Paulo mpaka mahali hapa ambapo anarejerea upya msisitizo. Neno lenyewe lilifasiriwa vizuri zaidi "mpole," au "anayezaa matunda." (kama vile 1 Tim. 3:3; Tito 3:2; Yakobo 3:17; 1 Pet. 2:18)

.

◙ **"ijulikane kwa watu wote"** Mstari huu umefasiriwa katika namna mbili:

1. waaminio wanapaswa kuwa na wema huu kwa waaminio wengine ili wale walio nje ya kanisa watambue na kuvutiwa na Kristo (kama vile Mt. 5:16)
2. upole huu utumike kwa watu wote bila kujali uhusiano walio nao kwa Bwana kama ushuhuda kwa uweza wake kwenye maisha ya wale wapagani waliomini na kama kinga kwa upinzani usio haki kwa wasioamini (kama vile Rum. 12:17; 14:18; 2 Kor. 8:21; 1 Pet. 2:12,15; 3:16)

**NASB, NRSV**
**NJB** **"Bwana yu karibu"**
**NKJV** **"Bwana yu karibu kuja"**
**TEV** **"Bwana anakuja hivi karibuni"**

Neno karibu latumika kwa wakati (kama vile Mt. 24:32, 33). Kuja kwa Mara ya Pili ni dhamira inayorudiwa rudiwa katika Wafilipi. Hii ina maana inayofanana na neno la kiaramu *maranatha* (kama vile 1 Kor. 16:22; Ufunuo 22:10). tazamio la kuja kwa mara ya pili wakati wowote kulikuwa ni kutia moyo wakristo kuisha maisha ya kikristo (kama vile Rum. 13:12; Yakobo 5:8-9). Yawezekana pia hii ingeweza kuhusu ule uwepo wa Bwana wa wakati wa kwa wakati kwa Waaminio (kama vile Mt. 28:20; Rum. 10:8 na F. F. Bruce's *Answers to Questions*, ukurasa 201).

## MADA MAALUM: *MARANATHA*

Hiki ni kifungu cha lugha ya Kiarama ambacho kinaaksi uthibitisho wa liturujia ya kithiolojia ya ya kanisa la mwanzo la Kipalestina ya (1) Uungu wa Yesu (Zaburi 110) au (2) ujio wa Yesu mara ya pili (Mdo 3:19-21). Maana yake inategemea kwa namna mtu anavyoligawa neno:

1. "Bwana wetu, njoo" (yaani.,., *marana-tha*) ni maana ya kifungu mfanano chenye kushurutisha Ufu. 22:20. Kwa hiyo, tafasiri nyingi zinadai kuwa maana hiyo katika 1 Kor. 16:22. Kama ndivyo, kwa hiyo ingekuwa maombi ya kurudi kwa Yesu.
2. "Bwana wetu amerudi" (yaani., *maran-atha)* ingalikuwa ni utimilifu wa lugha ya Kiarama. Hii ni tafasiri ambayo Chrysostom mwaka (345-407 B.K) anaipendelea , ambayo inazungumzia juu ya badiliko la Yesu kuwa mwanadamu.
3. "Bwana wetu anakuja" ingaliaksi UTIMILIFU WA KINABII wa Kiebrania, ambao unatumiwa na wengi kudhani kuwa sababu kwa ajili ya huduma ya Mkristo. Ujio wa mara ya pili mara zote umekuwa ni utiaji moyo kwa ajili ya waumini wa kila rika.
4. Kitabu The Didache[mafundisho ya Mitume kumi na wawili] ( kilicho andikwa mwanzoni mwa karne ya kwanza au ya pili) 10:6, kinatumia kifungu kile kile katika muktadha wa karamu ya mwisho ambapo uwepo wa Yesu sasa na matukio ya siku ya mwisho yajayo yote yamesisitizwa katika maombi.

**4:6 "Msijisumbue kwa neno lo lote"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Kanisa la Filipi lilikuwa katika hali ya wasiwasi mkubwa kutoka nje na ndani. Wasiwasi si tabia inayostahili katika maisha ya Kikristo (kama vile Mt. 6:25-34 na 1 Pet. 5:7). Hakuna lolote lililopaswa kuwapa wasiwasi waaminio ila labda kusimama kwao imara katika Bwana katika kumtumikia Yeye. Adui mkuu wa amani ni wasiwasi.

◙ **"bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru"** Haya ni majibu ya msingi kwa maombi ya woga na wasiwasi, kwa wengine na sisis wenyewe yaliyochanganywa na shukurani. Inafurahisha kwa mara ngapi na kwa namna Paulo anavyoyatumia neno "shukrani" kwa kuunganisha na maombi (kama vile Efe. 5:20; Kol. 4:2; 1 The. 5:17-18; 1 Tim. 2:1). Kuna mvutano wa kweli kati ya "bila kitu"na "katika kila kitu." Angalia mada Maalum: Sifa za Paulo, Maombi na Shukrani katika Efe. 3:20.

◙ **"haja zenu na zijulikane na Mungu"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo. Katika vifungu vya habari kadhaa katika Agano jipya ambayo zinasisitiza waamini wakazanie maombi (kama vile Mt. 7:7-11; Luka 18:2-8). Yawezekana, shukrani na ustahimilivu ni vitu viwili vinavyokosa katika usahihi wa thiolojia ya maombi. Mungu anajua kinachohitajika lakini ana shauku ya kuwa na ushirika na uaminifu katika maombi. Mungu amejipambanua mwenyewe katika maeneo yote katika kutenda kazi kwa kutegemea maombi ya watoto wake; "Hatujapata kwa kuwa hatuombi" (kama vile Yakobo 4:2).

**4:7 "amani ya Mungu"** Ni jambo la kushangaza kwamba katika muktadha huu amani ya Mungu imetajwa katika Flp. 4:7 na Mungu anayeitoa anatajwa katika Flp. 4:9. Ya kwanza inasisitiza kitu gani Mungu hutoa na ya pili tabia Yake. Amani imetumika katika namna mbalimbali kadhaa katika Agano Jipya:

1. inawezekana ikawa wadhifa (kama vile Isa. 9:6; Rum. 15:33; 16:20; 2 Kor. 13:11; Flp. 4:9; 1 The. 5:23; 2 The. 3:16)
2. inaweza kurejerea amani ya injili katika namna ya kufikia lengo (kama vile Yohana 14:27; 16:33; Kol. 1:20)
3. Inawezekana ikamaanisha amani ya Mungu kwa kumaanisha namna ya watu fulani (kama vile Efe. 2:14-17; Kol. 3:15)

Wakati mwingine 2 na 3 zinaunganishwa katika Rum. 5:1. atangalia Mada Maalumu katika Kol. 1:20.

◙ **"ipitayo akili na ufahamu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Imefasiriwa katika namna mbili: (1) Amani ya Mungu ni bora zaidi kuliko mawazo ya wanadamu au (2) Amani ya Mungu iko juu sana ya mawazo ya mwanadamu. Usambamba wa kifungu katika Efe. 3:20 ni msaada. Njia za Mungu ziko juu sana ya mawazo yetu (kama vile Isaya 55:8-9). Mfano wa amani ipitayo akili na uelewa wa mwanadamu inapatikana katika maisha ya Paulo katika sura hii (kama vile Flp. 4:11-13). Amani ya Mungu lazima iachanishwa na mazingira na kufungwa salama kwa mtu na kazi ya Kristo. Kwa "kupita" (*huperechō*) angalia Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya *Huper* ambatani katika Efe. 1:19.

◙ **"itahifadhi mioyo yenu"** Amani ya Mungu inakuwa kama askari wanaolinda waamini. Kweli hii hii nzuri ya majeshi ya Mungu kwa watoto wake inaweza kuonekana katika 1 Petro 1:4, 5. Maneno mawili ya Kiyunani "moyo" (*kardia*) na "akili" (*nous*) ni visawe katika kuzungumzia mtu mzima (kuhisi na kufikiri). Paulo anasisitiza kufikiria kikristo katika barua yake hii. Angalia dokezo katika Flp. 3:15. Angalia Mada Maalum: Moyo katika Kol. 2:2.

◙ **"katika Kristo Yesu"** Yeye ni msingi katika Thiolojia ya Paulo. Faida zote za Mungu na Baraka zinatiririka kwa mwanadamu aliyeanguka kupitia maisha, mafundisho, mauti, ufufuo, Kuja kwa Mara ya Pili na ushirikiano wa pamoja na Kristo Yesu. Waaminio kwa kwa namna ya faida kabisa wanaunganisha pamoja naye. Hii kithiolojia ni sawa na visawe vya Yohana "kukaa ndani yangu" ya Yohana 15.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 4:8-9**
**[8] Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo. [9] Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.**

**4:8-9** Huu ni mwendelezo wa msisitizo wa maisha ya kufikiria ya waamini. Waalimu walio na akili/ufahamu kama kitanda cha mbegu cha nafsi. Jinsi tunavyofikiri ndio tunavyokuwa. Mistari hii inatakikana sana katika maisha ya makanisa ya kisasa ya magharibi katika siku kama hiyo inayokubalika katika jamii ya uovu. Hii ni orodha inayofanana na ya orodha ya vitu vyema ya Stoiki. Paulo aliifahamu Thiolojia ya Kiyahudi kama raia wa Tarso. Anajaribu hata kunukuu baadhi ya waandishi wa Kiyunani (kama vile Mdo 17:28; 1 Kor. 15:37 na Tito 1:12). Angalia Mada Maalum: Maadili na kinyume chake katika Agano Jipya katika Kol. 3:5.

**4:8 "hatimaye"** Angalia angalizo katika Flp. 3:1.

◙ **"Kweli"** Hii ni kweli inayovutana na uongo, Hatahivyo, sio ukweli wa kitaaluma, lakini mtindo wa maisha wa kiungu. Neno hili linatumika na Mungu Rum. 3:4.

◙ **"ya heshima"** Hii kinadharia ilimaanisha "kupewa hadhi." Neno hili mara kwa mara lilifasiriwa "kaburi" na ina linatumika kwa viongozi wa makanisa ya nyumbani katika 1 Tim. 3:8, 11 na Tito 2:2. Inaonekana kutumika kwa maana ya "hadhi" pamoja na "mvuto" kuelekea vyote waliookolewa na wanaopotea.

◙ **"haki/sawa"** Hii inaashiria kubaki katika viwango vya tabia ya Mungu, hivyo kuwa mtu mwelekevu mwenye maadili. Katika Agano la Kale neno la Kiebrania kwa "haki" linatoka katika neno kwa futi ya kupimia" na kumaanisha asili ya Mungu kama kiwango ambacho wanadamu wanapimwa. Hii haimaanishi kwamba wanadamu wanaweza wakawa wenye haki kiukamilifu na Mungu wao kwa nguvu zao wenyewe, lakini kwamba Mungu kwa uhuru amewaachilia haki ya Kristo kwa wale waaminio ndani yake mara ilipotolewa, tabia ya Mungu inageuza mpokeaji!

◙ **"safi"** Hii inatumika kwa namna ya usafi wa kimaadili(kama vile 1 Yohana 3:3).

◙ **"ya kupendeza"** Neno hili linatumika hapa tu katika Agano Jipya. Inaonekana linamaanisha "yenye kupendeza," "yenye upole," "enye kuchukuliana," au "enye kupendeza." Huu ni wito mwingine wa waaminio kuishi maisha yenye mvuto.

**NASB** **"isimwayo vyema"**
**NKJV** **"ya kusifiwa"**
**NRSV** **"ya kusifiwa"**
**TEV** **"inayostahili sifa"**
**NJB** **"ya kutamaniwa"**

Neno linatumika hapa tu katika Agano Jipya. Linamaanisha lile ambalo "enye kustahili sifa" au "enye mvuto."

◙ **"kama upo ubora wowote"** Muudo wa kisarufi wa maneno haya nane unatumika katika Fil. 4:8 linabadilika baada ya la sita na kuwa sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli. Neno "bora" linatumika hapa tu katika maandiko ya Paulo na mara tatu tu katika Petro (kama vile 1 Pet. 2:9; 2 Pet. 1:3, 5). Linamaanisha kufanya jambo fulani vizuri ikifuatiwa na fahari yake inayofuatana nayo. Lilikuwa ni neno lililozoeleka katika maadili ya kifalsafa (Stoiki). Lilitumika kuelezea wema katika maelezo ya vitendo ya ukamilifu wake.
◙ **"enye kustahili sifa"** Hii ilimaanisha "kwamba iliyothibitishwa na wote yaani Mungu na mwanadamu" (kama vile Fil. 1:11). Inamaanisha kijamii kukubalika kwa desturi kwa kusudi la kuwavuta watu wa Mungu (kama vile 1 Tim. 3:2,7,10; 5:7; 6:14)

**NASB** **"kukaa katika mambo haya"**
**NKJV** **"kutafakari mambo haya"**
**NRSV** **"kufikiria kuhusu mambo haya"**
**TEV** **"kujaza fahamu zenu na mambo haya"**
**NJB** **"fahamu zenu zijazwe na"**

Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo. Hili neno la kibiashara (*logizomai*) linamaanisha mchakato wa kupiga hesabu au kuwaza kwamba lilikuwa endelevu na kipaumbele. Kukaa katika mambo haya ili kwamba viweze kutengeneza mawazo yako na maisha yako (angalia dokezo Fil. 3:15). Mungu atafanya sehemu yake katika maisha ya waamini kupitia neema, lakini lazima washiriki kwa kuondoa vitu vile ambavyo wanavifahamu kwamba vitavuta mioyo yao mbali na Mungu (kama vile 1 The. 5:21-22).

**4:9 "mambo mliyojifunza na kupokean kusikia na kuona"** Vitenzi hivi vyote vinne tendaji elekezi vya wakati uliopita usiotimilifu. Hivi vinafanana na shughuli za Paulo huko Filipi. Vyote maudhui ya thiolojia ya waaminio na

mtindo wa maisha yao (kama vile Ezra 7:10) ni muhimu ikiwa waamini wanataka kuakisi namna Bwana alivyo na kuwavuta wengine kumuelekea Yeye.
Ni jambo la kushangaza sana kwamba jina la pili "kupokea" (*paralambanō*) lilikuwa jina rasmi kwa "kupokea desturi" na lilitumika katika namna hiyo na Paulo 1 Kor. 11:23; 15:3.

◙ **"kuona"** Msisitizo huu ulianza katika Flp. 3:17. Kama Paulo alivyomfuata Kristo, waaminio nao wanapaswa kumfuata yeye.

◙ **"yatendeni mambo haya"** Hii ni kauli tendaji shuritishi ya wakati uliopo, "endeleeni kuyatenda mambo haya!" Msiwe wasikilizaji, lakini watendaji (kama vile Luka 11:28; Yakobo 1:22). Ni sawa na dhana ya Kiebrania, *Shema* (kama vile Kumbukumbu la Torati. 5:1; 6:4; 9:1; 20:3; 27:9-10), ambalo lilimaanisha "kusikia ili kuweza kutenda." Ukristo hautakiwa kugeuzwa kweye imani inayotenganishwa tofauti na maisha ya kiungu ya kila siku.

◙ **"Mungu wa amani"** Kama vile mstari wa 7 unavosisistiza amani ambayo Mungu hutoa. Msisitizo huu juu ya Mungu atoaye amani waweza kuonekana katika Rum. 15:33; 16:20; 2 Kor. 13:11; 1 The. 5:23; Ebr. 13:20. Yesu anaitwa Bwana wa Amani katika 2 The. 3:16.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 4:10-14**
**10 Nalifurahi sana katika Bwana, kwa kuwa sasa mwisho mmehuisha tena fikira zenu kwa ajili yangu, kama vile mlivyokuwa mkinifikiri hali yangu lakini hamkupata nafasi. 11 Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo. 12 Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. 13 Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. 14 Lakini mlifanya vema, mliposhiriki nami katika dhiki yangu.**

**4:10 "Nalifurahia"** Paulo ana shukrani sana kwa msaada huu wa kanisa (fedha, kujali, maombi, Epafrodito).

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"kwamba sasa mmefufua fikra zenu kwa ajili yangu"** |
| **NKJV** | **"kwamba sasa hatimaye kunijali kwenu kumehuishwa tena** |
| **TEV** | **"baada ya muda mrefu, kwa mara nyingine mmepata nafasi ya kunionesha kuwa mnanijali"** |
| **NJB** | **"sasa hatimaye kujali kwenu juu yangu kumehuishwa tena"** |

Kwa mtazamo wa haraka tamko hili laonekana kama hasi katika kiingereza. Linafanana sana na mstari upatikanao katika Warumi 1:10 Neno "lihuishwa" lamaanisha "kuchipua tena". Paulo anasema tu kwamba walikuwa na shauku ya kumsaidia lakini hawakuwa wamepata fursa (njeo isiyotimilifu katika kitenzi na kitenzi jina cha Flp. 4:10b). Hii yamkini inamaanisha zawadi ya kifedha (kama vile Flp. 4:14). Kwa chapisho zuri angalia Gordon Fee, *To What End Exegesis?* Ukurasa wa 282-289.

**4:11 "Nimejifunza kuridhika na kila hali niliyonayo"** Hii ni njeo ya wakati uliopita usiotimilifu ikitumia neno la kistilahi (*autarkēs*). Wanafalsafa wa kistoiki walitumia neno hili "kuridhika" kama lengo la falsafa yao, ambayo haikuwa ya tamaa ikiwaweka mbali na mambo ya dunia, "ya kujitosheleza." Paulo hakuwa anamaanisha kuwa yeye anajitosheleza, lakini kwamba mwenye kutoshelezwa na Yesu ("katika Bwana," Flp. 4:10). Amani ya Mungu haijaunganishwa a mazingira, lakini kwa mtu na kazi ya Kristo. Kuridhika ni vyote mtazamo wa Kikristo na urafiki na Mkombozi. Dhana ya kithiolojia ya kuridhika kwa mkristo pia inapatikana katika 2 Kor. 9:8; 1 Tim. 6:6,8; Ebr. 13:5.

**4:12** Mstari huu una vitenzi vitatu vya njeo timilifu pamoja na vitenzi jina sita vya wakati uliopo usio na kikomo. Ni ukiri mzuri wa kisanii wa imani ya Paulo wa upaji wa Mungu katika Kristo atoao wakati kwa wakati unaostahili "ndani ya Kristo." Angalia Mada Maalum: Utajiri katika Efe. 4:28.

◙ **"Najua jinsi ya kuchukuliana na njia ya unyenyekevu, pia najua jinsi ya kuishi katika mafanikio"** Hizi "najua"

mbili ni kauli tendaji elekezi za wakati uliotimilifu. Paulo alijua kuwa na vingi! Neno la kwanza linafasiriwa "kujinyenyekeza" katika Flp. 2:8, ambapo linatumika na Yesu. Hapa linamaanisha "chini ya inavyotakikana katika maisha ya kila siku." Neno la pili inamaanisha "zaidi ya vinavyotakikana katika maisha ya kila siku." Kuna hatari mbili zinazowakabili waamini katika mtindo wao wa maisha ya ukristo: umaskini na utajiri (kama vile Mithali 30:7-9). Hatari ni kwamba mtu akiwa maskini anakatishwa tama kwa Mungu na akiwa na utajiri anakuwa anajitosheleza kwa kujitenga mbali na Mungu.

◙ **"mafanikio. . .uhakika"** Angalia Mada Maalum: Utoshelevu katika Efe. 1:8.

**NASB, NRSV**
**TEV** **"nimejifunza siri"**
**NKJV** **"nimejifunza"**
**NJB** **"nimeweza kupata siri"**

Hii kwa dhahiri inamaanisha "nimeanzishiwa." Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati usiotimilifu. Neno hili linatumika hapa tu katika Agano Jipya. Lilitumika katika siri za injili za kidini kwa mtu kuingizwa katika imani zisizofaa za kiganga. Paulo alikuwa anajaribu kuelezea kwa uzoefu na kwa kithiolojia kwamba siri ya furaha inapatikana katika Kristo, na sio katika mazingira (kama vile *The Christian's Secret of a Happy Life* kilichoandikwa na Hannah Whithall Smith).

**4:13** Neno "Kristo" linapatikana katika toleo la King James ambalo halionekani katika mstari wa maandiko ya zamani ya Kiyunani (א*, A, B, au D*). Hata hivyo kiwakilishi "yeye" kwa hakika kinarejerea kwa Yesu. Huku ni kufunuliwa kwa upande wa pili wa kweli inayopatikana katika Yohana 15:5. Kweli ya Kibiblia mara kwa mara inawasilisha jozi zilizojaa mvutano. Siku zote upande mmoja unasisitiza kuhusishwa kwa Mungu na kwingine Mwanadamu. Hii mbinu ya Mashariki ya uwasilishaji wa kweli ni ngumu sana kwa watu wa magharibi kuielewa. Mivutano mingi kati ya madhehebu ni kutoelewana kwa aina hii ya uwasilishaji wa kilahaja wa uwasilishaji wa kweli. Kuangalia upande mmoja pekee ni kukosa lengo lililokusudiwa! Huu ushahidi wa kimaandiko uliotengwa umetengeneza taratibu za thiolojia ambazo ni kweli tu"kweli nusu"!

◙ **"kutiwa nguvu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo, "ambaye anaendelea kutia nguvu" (kama vile Efe. 3:16; Kol. 1:11; 1 Tim. 1:12; 2 Tim. 4:17). Waamini wanatakiwa waendelee kutiwa nguvu na Kristo. Wanatakikana pia wawe wenye nguvu (kama vile 1 Kor. 16:13 Efe. 6:10; 2 Tim. 2:1). Huu ni mvutano wa kimafumbo unaopatikana mara kwa mara katika maandiko. Ukristo ni agano; Mungu analianzisha na kuweka vigezo na upendeleo, lakini lazima binadamu waitikie na kutii na kuendelea! Waamini hawa walikuwa katika msongo wa ndani na nje kutoka kwa walimu wa uongo na washitaki! Kama vile Paulo alivyoridhika na mazingira yote, hivyo lazima wafanye hivyo pia (na sisi, pia).

**4:14** Waamini hawa walishirikiana na Paulo katika kueneza injili (kama vile Flp. 1:5) na mateso ambayo yaliletwa nayo. Angalia Mada Maalum: Dhiki katika Efe. 3:13.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 4:15-20**
**15 Nanyi pia, ninyi wenyewe mnajua, enyi Wafilipi, ya kuwa katika mwanzo wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna kanisa lingine lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi peke yenu.**
**16 Kwa kuwa hata huko Thesalonike mliniletea msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja.**
**17 Si kwamba nakitamani kile kipawa, bali nayatamani mazao yanayozidi kuwa mengi, katika hesabu yenu.**
**18 Lakini ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena nimejaa tele; nimepokea kwa mkono wa Epafrodito vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu.**
**19 Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.**
**20 Sasa atukuzwe Mungu, Baba yetu, milele na milele. Amina.**

**4:15,16** Hii ilikuwa ikieleweka kuwa kinzani kwa 2 Kor. 11:8-9, ambayo inamaanisha kwamba makanisa mengine ya Makedonia pia yalisaidia. Hatahivyo, kipengele cha muda ni muhimu. Paulo anasema kwamba kwa wakati huu hakuna kanisa lingine kuacha kanisa hili la Filipi waliokuwa wamemsaidia. Paulo alikuwa mwenye kusitasita kupokea msaada au michango ya kifedha (kama vile 1 Kor. 9:4-18; 2 Kor. 11:7-10; 12:13-18; 1 The. 2:5-9; na 2 The. 3:7-9).

**4:15 "Nyie wenyewe mnajua"** Hii ni ile ya kihuruma "ninyi" na kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu. Paulo alijishirikisha mwenyewe na kanisa hili na wazidi kuongezeka.

**MADA MAALUM: KANISA (*EKKLESIA)***

Neno hili la Kiyunana, *ekklesia*, linatokana na maneno mawili, "nje ya"na "kuitwa." Neno hili linatumika kidunia (yaani., jamii iliyoitwa kwenye kikao, k.v Mdo. 19:32,39,41) na kwa sababu ya utumiaji wa maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno hili kwa ajili ya "kusanyiko" la Israel (*Qahal,* BDB 874, KB 1078, k.v. Hes. 16:3; 20:4; Kumb. 31:30),na matumizi ya kidini. kanisa la mwanzo walijiona wao kama mwendelezo wa Agano la Kale la watu wa Mungu. Walikuwa Waisrael wapya (k.v. Rum. 2:28-29; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), utimilizo wa kusudi la Mungu kidunia (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH
Neno lililotumika kwa maana nyingi katika injili na matendo.

1. Mikusanyiko ya kidunia , Mdo. 19:32,39,41
2. Watu wa Mungu ulimwenguni katika Kristo, Mt. 16:18 na Waefeso
3. Kusanyiko la waumini wa mahali katika Kristo, Mt. 18:17; Mdo. 5:11 (katika aya hii, ni kanisa huko Yerusalem); Mdo. 13:1; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; Filemoni uk. 2
4. Watu wa Israel kwa ujumla, Mdo. 7:38, katika hotuba ya Stephano
5. Watu wa Mungu kwenye Miji, Mdo. 8:3; Gal. 1:2 (Yuda au Palestina)

Kanisa ni watu waliokusanyika, na sio jengo. Hapakuwepo na majengo ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Katika Yakobo (moja ya kitabu cha mwanzoni kabisa cha Wakristo) kanisa lilitajwa kwa neno "*synagōgē*" (kusanyiko). Neno kanisa limetokea tu kwa Yakobo (k.v. Yakobo 2:2; 5:14).

**NASB, NKJV,**
**NRSV** **"mliyonishirikisha katika maswala ya utoaji na upokeaji"**
**TEV** **"aliyewashirikisha faida na hasara zangu"**
**NJB** **"mlijihusisha pamoja nami katika suala la utoaji na upokeaji"**
`

Huu ni mfululizo wa maneno ya kibiashara Flp. 4:15-18 ambayo yanaweza kuthibitishwa na kutatolea maana kutoka katika nyaraka za koine ya Kiyunani ipatikanayo Misri na ostaraca (chungu kilichovunjika kutumika kama zana za kuandikia). Hili lilikuwa ni neno la Kibenki kwa akaunti ya wazi. Paulo alikuwa na ufahamu kamili juu ya matatizo yaletwayo na fedha. Kama alikuwa harusiwi kuchukua pesa kama malipo ya mafundisho yako. Mashitaka ya uongo yaliyotolewa katika Korintho yaliimarisha hitaji lake la kutopokea fedha. Paulo lazima alikuwa na kutulia na kusanyiko lake.

**4:17 "Natafuta. . .tafuta"** Hili ni neno lenye nguvu lilitumika mara mbili linaoneshwa hisia tata za Paulo kuhusu shukrani kwa zawadi na bado wala hatafuti msaada wao. Aligundua kwamba wangepokea baraka kutoka kwa Mungu kwa ajili ya uwakili na ukarimu katika injili. Kwa hili alikuwa na furaha.

◙**"faida iongezekayo katika hesabu yangu"** Hii ni sitiari ingine ya kibiashara ambayo ilimaanishariba inayoongezeka na ilitunzwa katika akaunti nyingine. Kutoa katika injili kunasababisha matokeo ya Baraka za injili (kama vile Flp. 4:19).

**4:18 "nimepokea kila kitu katika ukamilifu,"** Hili ni neno lingine la kibiashara kwa risiti ya malipo kamilifu. Paulo alikuwa anahisi kanisa hili lilikuwa limefanya kila kitu kilichotegemewa na zaidi. (Matumizi ya neno "kutosheleza" au "kuwa na vitu tele" na kauli tendwa elekezi ya wakati ulio timilifu "kusambaziwa kwa wingi au utele").

◙ **"Epafrodito"** Alikuwa ni mwakilishi wa kanisa la Filipi aliyetumwa kuwasilisha zawadi za kifedha na kukaa kusaidia Paulo (kama vile Flp. 2:25-30).

◙ **"zawadi ya kukubalika, inayopendeza kwa Mungu"** Hii ilitoka katika sitiari ya Agano la Kale ya dhabihu ya kuubalika katika madhabahu ya sadaka za kuteketezwa (kama vile Mwanzo 8:21; Mwanzo 29:18,25,41; Mambo ya walawi 1:9,13; Ezekieli 20:41). Sitiari hii hii imetumika na Paulo 2 Kor. 2:15 na Efe. 5:2. Msaada aliopewa Paulo kama mtumishi wa injili ni uhalisia unaotolewa kwa Mungu utalipwa na kubarikiwa na Yeye!

**4:19 "Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji"** Hii sio hundi iliyowazi kutoka kwa Mungu! "Mahitaji" lazima yajulikane. Hii lazima itazamwe kwa msingi wa kanuni ya kutoa ya kiroho inayopatikana katika 2 Wakorintho 8 na 9, hasa 9:6-15. Hii si ahadi inaweza kuchukuliwa nje ya muktadha wake na kufanyiwa kazi kwa kila shauku ya kibinadamu. Katika muktadha huu inahusiana na kutoshelezwa kwa huduma. Mungu siku zote atawajazeni watoaji wote wanaootoa kwa ukarimu ili wawe na vingi zaidi vya kutoa. Hii haimaanishi kuwa watakuwa na vingi zaidi kwa ajili ya kwao wenyewe, bali watakuwa na zaidi kwa ajili ya kutoa kwa injili!

◙ **"Kulingana na utajiri wa utukufu wake katika Kristo Yesu"** Lazima ikumbukwe kuwa sura yote hii nzima inachochewa na kazi ya Kristo na kwamba vyote katika maisha ya Mristo, "katika Bwana," (kama vile Flp. 4:1, 2, na 4). Baraka zote za Bwana zinakuja kupitia Kristo.

**4:20 "Kwa Mungu wetu na Baba utukufu wa milele na milele"** Hii inafanana sana. Neno "milele na milele" kiuhalisia ni "kwa vizazi na vizazi," ambayo ni nahau ya Kiyunani "milele." Angalia Mada Maalum: Sifa za Paulo, maombi na Shukrani katika Efe. 3:20.
Maelezo ya Mungu baba ni moja ya kweli kuu ya Biblia (kama vile Hosea 11). Sitiari za familia zinatumiwa na Mungu (Baba, Mwana) kusaidia wanadamu asili Yake na tabia. Mungu amejiachilia mwenyewe kwa uelewa wa kibinadamu kwa kutumia nyadhifa za kibinadamu, analojia za kibinadamu na hasi. Kwa kidokezo kamili kwenye "utukufu" angalia Waefeso Efe. 1:6.

◙ **"Amina"** Ni neno la Kiebrania "imani" au "uaminifu" (kama vile Habakuki 2:4). Kwa asili neno hili lilitumika kufunua hatua madhubuti, kukanyaga kwa ukamilifu. Ilikuja kutumika kisitiari ya mtu aliyekuwa mwaminifu, thabiti, mkakamavu, anayetegemewa, mwaminifu. Baadae ilikuja kuwa kawaida kwa namna ya ukiri wa kauli ya uaminifu. Angalia Mada Maalum katika Efe. 3:20.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): WAFILIPI 4:21-23**
**21 Mnisalimie kila mtakatifu katika Kristo Yesu. Ndugu walio pamoja nami wawasalimu. 22 Watakatifu wote wawasalimu, hasa wao walio wa nyumbani mwa Kaisari. 23 Neema ya Bwana Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu.**

**4:21-23** Inawezekana iliandikwa na mkono wa Paulo wake yeye mwenyewe ambayo ilikuwa ni mbinu ya kawaida kuthibitisha uhalali wa barua zake (kama vile 1 Kor. 16:21; Gal. 6:11; Kol. 4:18; 2 The. 3:17; Filemoni 1:19). Hii ilikuwa ni jambo la kawaida katika mafunjo ya Koine ya Kiyunani inayopatikana Misri. Nyingi za barua za Paulo ziliandikwa na mwandishi (kama vile Rum. 16:22).

**4:21 "wasalimie kila mtakatifu"** Haya ni matumizi pekee ya neno "mtakatifu" katika Agano Jipya na katika umoja. Linafuatiwa na Fil. 4:22 kwa muundo wa wingi. Hata katika Fil. 4:21 inatumika katika namna ya pamoja. Kuokolewa kunasababisha kuwa sehemu ya familia, mwili, shamba, jengo, watu! Haiwezekani kuwa kiroho "mpiganaji binafsi." Injili inapokelewa kwa binafsi lakini inapelekea katika ushirika wa pamoja. Kuwa mwangalifu

ya  kusisitiziwa kwa kupita kawaida kwa magharibi ya kisasa juu ya haki na uhuru. Ukristo ni uzoefu wa pamoja. Hata Mageuzi yanayojulikana (Luther) kauli mbiu kama "ukuhani wa Waamini" kibiblia sio sawa. Watu wa Mungu wa Agano Jipya wanaelezewa kwa tungo za kikuhani za Agano la Kale (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:60. lakini angalia kwamba zote ziko katika wingi, "ufalme wa makuhani."
Kumbuka, waaminio wanakarama za mtu binafsi  kwenye wokovu kwa ajili ya ustawi wa pamoja (kama vile 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili tuhudumie. Taratibu zetu za desturi za kisasa zimebadili "Nini kilichopo kwa ajili yangu?" kwahiyo kugeuza wokovu kuelekea tiketi ya mbinguni badala ya maisha ya huduma. Waamini hawaokolewi ili kwamba waweze kufanyia kazi uhuru wala kudhihirisha uwezo wao, wanaokolewa kutoka katika dhambi kumtumikia Mungu (kama vile Romanswarumi 6 6). Angalia Mada Maalum: Watakatifu katika Kol. 1:2.

**4:22 "Hasa watu wa nyumba ya Kaisari"** Hii kwa dhahiri inafanana na watumwa, watumishi na viongozi wadogo wadogo katika Rumi ndani ya huduma za kiserikali (kama vile Fil. 1:13). Injili ya Paulo ilikuwa mpaka imevamia watumishi wa Mfalme na siku moja kusababisha mfumo wa kipagani kuanguka.

**4:23**
**NASB, NRSV,**
**NJB** **"iwe na roho zenu"**
**NKJV, TEV** **"iwe nanyi nyote"**

Hii ina maanisha mtu. Katika Agano Jipya mara kwa mara ni ngumu kujua kama mwandishi anamaanisha Roho Roho Mtakatifu (likiwa "R" herufi kubwa ) au roho ya mwanadamu (yenye"r" herufi ndogo). Katika muktadha huu ni wazi kidogo "r." Kuna kutofautiana kwa maandiko katika kufunga kwa maandiko ya Paulo (kama vile Gal. 6:18 na Filemoni 25). Baadhi ya Maandiko ya Kiyunani, א[c], K, na Textus Receptus (NKJV), yana "pamoja nanyi nyote," ambayo ilikuwa ufungaji wa Paulo 1 Kor. 16:24; 2 Kor. 13:13; 2 The. 3:18 na Tito 3:15. Mengi ya maandiko ya Mafunjo ya kiyunani ya Kale yana "pamoja na roho zenu"

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Tungo gani yenye ufunguo wa  surah ii
2. Je "kusimama imara" kunamaanisha nini?
3. Ni kanuni gani zinazotumika kutatua mafarakano/hali ya kutokuwa na umoja katika kanisa la mahali?
4. Toa vipengele vya maombi ya Paulo ambavyo Paulo anavitaja katika mstari 4-7
5. Elezea kwa maneno yako mwenyewe umuhimu wa mstari wa 8 na 9 katika siku zetu za leo
6. Je mstari wa 10 ni kauli hasi ya Paulo kuwakandia Wafilipi kwa kukataa kumsaidia?
7. Je ni siri gani ya furaha inayoelezewa katika mstari wa 11-13?
8. Orodhesha na elezea maneno matatu ya kibiashara yanayopatikana katika mistari ya 15, 17 na 18.
9. Elezea kwa namna gani muktadha unaathiri ufasiri sahihi wa mstari wa 19a.

# Maelezo Mafupi ya Muundo wa Kisarufi Cha Kiyunani

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Meditarania ilianzishwa na Alexanda mkuu (336-323 B.C) na ikadumu mpaka miaka ya (300 B.C-A.D 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

## I. NJEO

A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
   1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukueiezwa.
   2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.

B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
   1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
   2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA
   3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU
   4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
   5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
   6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- "okolewa" (Rum 8:24)
2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA- "ameokolewa na matokeo yake yanaendelea" (Efe 2:5,8)
3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- "anaokolewa" (cf. 1Kor 1:18; 15:2)
4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- "ataokolewa" (cf. Rum 5:9,10; 10:9)

C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO "hakuna madoido" lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida "kisichoainishwa" "kisichotambulika" "kisichochoka." Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
   1. NJEO YA WAKATI ULIOPITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, "umekuwa na unaendelea kuokolewa."
   2. NJEO YA WAKATI ULIOPITA AINISHI. Hii ilikuwa kama njeo ya WAKATI ULIOPITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: "Petro alikuwa akisimama nje mlangoni" (Yoh 18:16)
   3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: "kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi", "kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi" (1Yoh 3:6 & 9).
   4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njeo hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPITA na WAKATI ULIOPITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: "kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha" au " Yerusalemu yote wakaanza kumwacha"(Mt3:5)
   5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: "Heri wale….wata..."(Mt 5:4-9).

## II IRABU

A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA

B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.

C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
   1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
   2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
   3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
   4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.

D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitizia KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika

Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” ( 2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

## III. DHAMIRA (au “NAMNA”)

A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI Y A UCHAGUZI).

B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna <u>pekee</u> ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.

C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno “ingalikuwa”, “ingaliweza”, “yawezekana” au “yenye uwezo”.

D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. “yawezekana isiwe” (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano ( cf. Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo 8:20 na 1Thes 3:11

E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.

F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezewa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.

G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au “kisichotambulika” cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993

D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950
E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

## V. NOMINO

A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
   1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI "kuwa" au "kufaa"
   2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, "aina gani?" mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza "ya/za"
   3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza "kutoka".
   4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ya".
   5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na"
   6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno "kwa" au "enye"
   7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali "kwa umbali gani" au "kwa namna gani"
   8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

## VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.
B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament
   1. Viunganishi vya wakati
      (a)*epei, epedē,hopote, hōs, hote, hotan (*TEGEMEZI)- "lini"
      (b) *heōs- "*wakati"
      (c)*hotan, epan (*TEGEMEZI)- "kila, wakati wowote"
      (d) *heōs, achri, mechri (*Tegemezi)- "mpaka"
         a. *priv (*kitenzijina)- "kabla"

b. *hōs*- “tangu”, “lini”, “kama”.

2. Viunganishi venye mantiki
   a. Kusudi/dhumuni
      1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs (*TEGEMEZI) *hōs*- “ya kwamba”, “kuwa”
      2) *hōste(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
      3) *pros(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
   b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
      (1) *hōste(*ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
      (2) *hiva(*TEGEMEZI)- “ya kwamba”
      (3) *ara*- “kwa kiasi hicho”
   c. Chanzo au sababu
      1) *gar(*chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
      2) *dioti, hotiy*- *“*kwa sababu ya”
      3) *epei, epeidē, hōs*- “tangu”
      4) *dia(*ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”
   d. Maamuzi
      (1) *ara, poinun, hōste*- “kwa hiyo”
      (2) *dio(*KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”
      (3) *oun*- *“*kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”
      (4) *tinoun*- “kufuatana na”
   e. –a kinyume au tofauti
      (1) *alla(* yenye KINYUME thabiti)-“lakini”, “isipokuwa”
      (2) *de*- *“*lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwingine”
      (3) *kai- “lakini”*
      (4) *mentoi, oun- “ingawa”*
      (5) *plēn*- “hata hivyo” (haswa katika Luka)
      (6) *oun- “ingawa”*
   f. Ulinganifu
      (1) *hōs,kathōs (*ingiza vishazi linganifu)
      (2) *kata(*kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper)*
      (3) *hasos(*katika Kiebrania)
      (4) *ē- “kuliko”*
   g. Enye mlolongo au mtiririko
      (1) *de*- *“*na”, “sasa”
      (2) *kai*- *“*na”
      (3) *tei*- “na”
      (4) *hina, oun*- *“*kile”
      (5) *oun*- *“*kasha”(katika Yohana)

3. Matumizi yenye mkazo
   a. *alla*- *“*kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”
   b. *ara*- *“*hakika”, agharabu”, “kweli”
   c. *gar*- *“*lakini kweli”, “agharabu”, “hakika”
   d. *de*- *“*hakika”
   e. *ean*- *“*hata”

f. *kai*- “hata”, “hakika”, “kweli”
g. *mentoi*- “hakika”
h. *oun*- “kweli”, “kwa hali zote”

VII.

A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.
B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno “kama.” Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa “tangu”(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)
C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
    1. “kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
    2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
    3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)
D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16
E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

## VIII. VIZUIZI

A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani…………”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu……….” ( Mt 6:25); “wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi…….”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo…………………”(Ef 5:18)
B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa……..”(Mt 5:17); “msisumbuke………”(Mt 6:31); “msiuonee haya………..”(2Tim 1:8)
C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali yeyote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti………”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe………..”(1Kor 8:13)

XI

A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno "wale, Yule,ile" kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya "muonyeshwaji", ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda
   1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
   2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
   3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: "Mungu ni Roho" Yoh 4:24, "Mungu ni nuru" 1Yoh 1:5; "Mungu ni upendo" 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno "a" herufi ya kwanza ya alfabeti au "an" mbadala wa "a" kwenye irabu zinazoanza na herufi kama "e", "h". Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;
   1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
   2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

## X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
   1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.
      a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
      b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
      c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
   2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
      a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) SIFA
      b. VITENZI elekezi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) KISHAMILISHI
         (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
         (5) KIRAI HUSISHI
      c. Virai vya NOMINO
         (1) NOMINO

(2) KIVUMISHI

(3) KIRAI HUSISHI

3. Mpanglio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:
   a. "walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika" (Gal 2:9) kirai "mkono wa kuume wa shirika" imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
   b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
   c. "ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi" (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.

D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na

1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: "mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe……."(Mt 28:20)
2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
   a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
   b. Yohana 14:1 (maada mpya)
   c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
   d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: "usifiwe utukufu wa neema yake" (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
   a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama "lala" kwa kifo (Yoh 11:11-14) au "nyayo" kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
   b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama "ufalme wa mbingu" (Mt 3:21) au "sauti toka mbinguni" (Mt 3:17)
   c. Maumbo ya hotuba

      (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)

      (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)

      (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)

      (4) Kejeli (Gal 5:12)

      (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)

      (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno

         (a) "kanisa"

            i. "kanisa" (Efe 3:21)

            ii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)

            iii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)

         (b) "huru "

            i. "Mwanamke huru" (Gal 4:31)

            ii. "uhuru" (Gal 5:1)

            iii. "huru" (Gal 5:1)

   d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana

      (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno "chakula" (Yoh 4:31-34)

      (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno "hekalu" (Yoh 2:19; Mt 26:61)

      (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno "chukia" (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)

(4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.

5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.
6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*
   a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”
   b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”

E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
   1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.
   2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neno kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)

      Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
   3. Utumiaji wa *The Ephasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
   4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
      a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
      b. Young’s Lateral Translation of the Bible cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.
Mhutasari ufuatao utahusika

I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
   A. Agano la Kale
   B. Agano Jipya
II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya "maoni dhaifu" pia yanaitwa "uhakiki wa maandiko"
III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye

I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale
1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na "Herufi Aristeas." Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao " Esene". Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
   a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, "Kama vile wengi watakavyo shangazwa <u>Naye</u>."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, "Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa <u>Nawe</u>."
      (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
         (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, "hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye"
         (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, "hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi"
   b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
      (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, "ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, "ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana……"
   c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), "Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.''

(2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), "Ataona —ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki."

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuzwa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaiita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili A.D., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania א (*aleph*) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya"Maandishi ya Kialekzandria."
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alexandrianus, kijulikanacho kama "A" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alexandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama "B" au (03), iliyopatika katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya "Maandishi ya Kialekzandria."
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama "C" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama "D" au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya karnre ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama "Maandishi ya Magharibi." Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
   a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
      (1) $P^{75}$,$P^{76}$ ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
      (2) $P^{46}$ (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
      (3) $P^{72}$(yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
      (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
      (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
      (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni א,C, L, W, 33
   b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
      (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
      (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
      (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsri za kale za Kisiria
      (4) Andiko D la Machapisho ya kale "Bezae" ilifuata aina ya maandishi haya
   c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
      (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

(2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
(3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
(4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya
d. aina ya nne iwezekanayo ni ya "Kikaizari" kutoka Palestina
(1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
(2) baadhi ya shuhuda zake ni $P^{45}$ na W

II. Matatizo na nadharia ya "ukosoaji dhaifu."

A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea
1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
(1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
(2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
2. makusudi
a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

B. Mafundisho muhumu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)
1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
*a.* kitabu cha J. Harold Greenless, *Inroduction to New Testament Textual Criticism*, "Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning'inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa

Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia” (uk. 68).

*b.* W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* ( Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo “angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri.” Criswell alisema “Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa…Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza…” Mababa wa uzao wa SBC wasio wakosaji walidai kuwa “kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu” pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda ( Mt. 27 na Matendo 1): “Ni maoni tofauti ya kujinyonga,” Criswell alisema “Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia.”Criswell aliongeza, “Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu…”

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Critcism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

# FAHARASA

**Uasilishaji.** Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (cf. Rum.1:4).Yesu aliyaishi maisha haya kama mfano ambao Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama "mwana" Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresha hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!
Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyozawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

**Shule ya Alexandria.**Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nyingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebisho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

**Ufuasi wa Alexandria.**Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lililothibitishwa, pamoja na Agano Jipya. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipya zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama "A, na machapisho ya alama "B" (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiriwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

**Istiari.** Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikua katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

**Uchanganuzi wa misamiati.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipya. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

**Ushabihiano wa Maandiko.** Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

**Utata.**Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwezekanazo au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

**Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu.** Inamaanisha kuwa na "tabia zinazohusiana na wanadamu." neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekanalo, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo yanahusiana na wanadamu (cf. Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

**Shule ya Antiokia.**Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianzia huko Antiokia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiari wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Ilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Ilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu walioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

**Kutabaini.** Hii ni moja miongoni mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waebrania. Unahusiana na misitari ya ushairi yenye kukinzana kimaana (cf. Mit. 10:1; 15:1).

**Fasihi ya mafunuo.** Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inahaidi ushindi mkuu na kupitia juhudi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenye maneno ya mafumbo. Mara nyingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nyingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1)katika Agano la Kale, Ezekieli (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

**Mtetezi.**Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi "ulinzi wa kisheria." Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kifikra kwa imani za Kikristo.

**Haki ya kutangulia.**Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno "dhanio." Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyosadikika kuwa kweli paspo uchambuzi au uchunguzi.

**Ufuasi wa Arius.**Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (B.K. 318) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K.walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

**Jamii ya watu wakuu.** Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia uchunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

**Miandiko binafsi.** Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebrania na Kiyunani.

**Maandiko ya asili ya karne ya sita.** Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama "D." Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nyingi za maandishi yenye ueledi. Inaunda msingi wa "uundaji wa maandiko"ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

**Upendeleo.** Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

**Mamlaka ya Kibiblia.** Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenyewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafsiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

**Orodha ya vitabu vya Agano Jipya.**Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

**Kristo kama kitovu.**Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

**Fasiri.**Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafsiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

**Itifaki.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza: (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika: (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza: (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi: (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (cf. Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

**Magombo ya Bahari ya Chumvi.** Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossoretes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu B.C.

**Mambo yaliyofasiliwa.** Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

**Mbinu pembuzi.**Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-mapenzi huru, ulinzi-ustahimilivu, imani-kazi; uwamuzi-ufuasi; uhuru wa Mkristo-uwajibikaji wa Mkristo

**Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine.**Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

**Mlinganyo wa nguvu.** Hii ni nadhalia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali. Katika nadharia hizi mbili ndipo pana "mlinganyo wa nguvu" unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi vya kisasa na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi

nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth,* uk. 35 na katika Robert Bratcher's utangulizi katika Biblia ya TEV.

**Kutofuata mfumo.** Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

**Kupotosha maana.** Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni "kuondoa" kulingana na kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha "kuingiza" wazo la kigeni.

**Elimu ya asili na historia ya neno.** Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

**Fasili ya maandiko.** Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha "uondoaji nje" (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

**Namna ya Uwasilishaji.** Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

**Maarifa ya utambuzi/mafunuo.** Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafunuo ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawezi kuhusishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika*)* kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (cf. 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (cf. 1Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihiiitajika kupitia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*eons)*; au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

**Kanuni za ufasili.** Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

**Uhakiki juu ya maandiko.** Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

**Nahau.** Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenye maana maalumu na sio vilivyohusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: "ilikuwa ni vizuri sana" au "umeniua". Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

**Nuru.**Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Kudukiza.** Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majaribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenye hadhi ya juu.

**Unasaba.** Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweka tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na "misamiati ya kiuchunguzi" ambayi inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

**Uvuvio.**Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Lugha ya maelezo.** Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hata yakamaanisha kuwepo.

**Ushikiliaji sana wa sheria.** Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

**Tafasili sisisi.** Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiokia. Ina maana kwamba utafasili unahusika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

**Fasihi tanzu.** Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

**Sehemu ya fasihi.** Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

**Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.**

**Maandiko ya asili.** Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno "MS" (umoja) au "MSS" (wingi).

**Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi.** Hii inarejerea karne ya nane A.D. maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

**Mshabihiano wa neno.** Huu ni namna ya msemo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano " birika linachemka" ki uhalisia inamaanisha "maji yaliyeko kwenye birika yanachemka".

**Orodha ya vitabu vya Agano jipya.** Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 A.D. Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa "kiutendaji" pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

**Ufunuo wa asili.** Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum 2:14-15). Umeongelewa katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Unatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolijia unasisitizwa tena na mwenendo wa "dunia ya zamani" kati ya wanasayansi wa Kikristo (cf. maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kiasili. Kwa maoni yangu , hii ni fursa mpya ya ajabu kushuhudiwa juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

**Ufuasi wa Nestory.** Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antiokia ya Syria na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyingine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtizamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha "mama wa Mungu" alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cycil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antiokia. Antiokia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

**Mwandishi wa awali.** Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

**Mafunjo/Magombo.** Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

**Vifungu Mlinganyo**. Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahsusi na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapojaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

**Ufafanuzi/fasili.** Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa "neon kwa neon" ambapo neon la Kiingreza laweza kuweka kwa kila neon la Kiebrania au Kiyunani kwenye "fasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtizamo wa kawaida wa neon au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi "mlinganyo wa nguvu" ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth, Uk. 35.*

**Aya.** Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhalia. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

**Uparokia.** Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

**Fumbo.** Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, nab ado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

**Pilato.** Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohoni. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha "mtizamo/mawazo" ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

**Dhanio.** Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenyewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

**Uhakiki wa maandishi.** Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

**Ualimu wa dini ya Kiyahudi.** Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 B.C). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii "dini ya wandishi" ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 A.D muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kiutendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoelezwa katika tamaduni za Talmud.

**Ufunuo.** Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemezana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uvuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3)Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

**Elimu-maana.** Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

**Maandiko ya kale ya Kiyunani.** hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 B.C (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili nay a tatu B.C (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni "LXX".

**Machapisho ya asili.** Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne A.D. Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa "*eleph*" (א). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja.

**Kujitakasa.** Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

**Visawe.** Hii inarejerea maana yenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejesha mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (cf. Zab 103:3).

**Sintaksi.** Hili ni neno la Kiyunani linalirejeresha muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

**Usanisi.** Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. Neon hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwingine katika maana moja, wakati mwingine huitwa "taaluma ya mabadiliko ya hali" (k.v. Zab 19:7-9).

**Thiolojia mpangilio.** Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna ( Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

**Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi.** Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ulitolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

**Uhakiki wa tofauti za kiuwandishi.** Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa "uhakiki wa asili ya neno".

**Upokeaji wa Maandiko.** Usanifishaji huu ulianzia kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633 A.D. Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament uk. 27 cha A.T Robertson* anasema "andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkono. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 A.D.

**Sheria za Musa.** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya "ufundishaji". Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

**Uanishaji.** Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analojia. Namna hii ya kanuni za ufasili ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusi ulioandikwa katika Agano jipya.

**Maandiko ya Vatican.** Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne A.D . Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu zingine zilipotea( Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa "B".

**Tafasili ya Biblia ya Kilatini.** Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa "kawaida"wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 A.D.

**Hekima ya Fasihi.** Hii ni fasihi tanzu iliyozoeleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi lilikuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipya juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezewa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyoungana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

**Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia.** Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno "picha ya ulimwengu" inarejerea "kwa namna gani" juu ya uumbaji wakati "mtizamo wa kidunia" unahusiana na "nani." Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

**YAHWE/YEHOVA.** Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linaelezewa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania "kuwa" ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani "Adonai" likimaanisha "Bwana". Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

# MAELEZO YA KIMAFUNDISHO YA BOB

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ufuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neon la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu (Angalia MADA MAALUM: UVUVIO[SPECIAL TOPIC: INSPIRATION). Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake (Angalia Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi (Special Topic: YHWH's Eternal Redemptive Plan). Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, uumbaji na ukombozi (Angalia MADA MAALUM: UWEPO WA MUNGU MMOJA (SPECIAL TOPIC: MONOTHEISM). Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendelea. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja (Angalia MADA MAALUM: UTATU(SPECIAL TOPIC: TRINITY).
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa ndani wa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo (Angalia Majaaliwa (Calvinism) Dhidi Ya Mapenzi Huru Ya Kibinadamu (Arminianism) Predestination (Calvinism) vs Human Free Will (Arminianism)
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada (Angalia MADA MAALUM: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL). Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana Tazama Mada Maalum:Ina Maana Gani "Kupokea" "Kusadiki" "Kukiri/Kutubu" na "Kusihi"? (Special Topic: What Does It Mean to "Receive," "Believe," "Confess/Profess," and "Call Upon"?)
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini(Mada Maalum: "Kuamini" Katika Agano Jipya(Special Topic: "Believe" in the NT)katika Kristo na toba toka dhambini (MADA MAALUM: TOBA[AGANO JIPYA] SPECIAL TOPIC: REPENTANCE (NT) Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.

8. Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine"(Mada Maalum: Yesu na Roho(Special Topic: Jesus and the Spirit) Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake. Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

"Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.